Historia ya kushushwa Qur'an 96: 1 - 5, inatukumbusha na kutufunza kuwa Mtume (s.a.w) alianza kushushiwa wahyi kwa kupewa amri ya Kusoma. Hivyo, hapana shaka kabisa kuwa Elimu ndiyo Faradhi ya kwanza inayopaswa kutekelezwa na kila Muislamu tangu zama za Mtume (s.a.w) hadi sasa.

Kusoma au kutafuta Elimu kumefanywa kuwa Faradhi ya kwanza ili kumuwezeshe mja kumjua Mola wake na kumpatia ujuzi wa kutosha juu ya kanuni na sheria za Allah (s.w), ambazo zikifuatwa katika kila kipengele cha maisha ya kila siku, hupatikana uadilifu na amani ya kweli katika jamii.

Hii ni Juzuu ya Pili ya Maarifa ya Uislamu katika mfululizo wa juzuu 7 za masomo kwa Darasa la Watu Wazima unao kusudia kumuwezesha mja na jamii kufikia kilele hicho.

Mfululizo huu wa masomo katika juzuu 7 ni:

1. Lengo la Maisha ya Mwanadamu
2. Nguzo za Uislamu
3. Qur'an na Sunnah
4. Familia ya Kiislamu
5. Jamii ya Kiislamu
6. Historia ya Kuhuisha Uislamu
7. Kuhuisha Uislamu katika Jamii

2

Nguzo za Uislamu - IPC

Toleo 2

Maarifa ya Uislamu

## Darasa la Watu Wazima

## Juzuu 2

(Toleo la Pili)

# Nguzo za Uislamu



Islamic Propagation Centre

**Maarifa ya Uislamu**

## Darasa la Watu Wazima

**Juzuu 2**

(Toleo la Pili)

# Nguzo za Uislamu

**Islamic Propagation Centre**

Maarifa ya Uislamu

**Darasa la Watu Wazima**
Juzuu ya Pili,
(Toleo la 2)

© Islamic Propagation Centre

Toleo la Kwanza, Septemba 10, 2003
Nakala 2000

Toleo la Pili, November 5, 2006, Shawwal 14, 1427
Nakala 1000

Kimetayarishwa na Kusambazwa na :-
**Islamic Propagation Center** (**IPC**),
P.O.BOX 55105, Simu 022-2450069,
**Dar es Salaam, TANZANIA.**

Kimechapwa na:
Afroplus Industries (LTD)
P.O.Box 32427, Tel: 022 2773751,
Dar es Salaam,
Tanzania.

بسم الله الرحمن الرحيم

# NENO LA AWALI KWA TOLEO LA PILI

Shukurani zote na sifa zote njema anastahiki Allah (s.w), Bwana Mlezi wa Walimwengu wote. Rehema na amani zimwendee Mtume Muhammad (s.a.w), ahili zake, Swahaba zake na wale wote waliofuata na wanaofuata mwenendo wake (Sunnah yake) katika kuhuisha na kusimamisha Uislamu katika jamii.

Tunamshukuru Allah (s.w) kwa kutuwafikisha kutoa **Toleo hili la Pili** la juzuu ya pili ya "Maarifa ya Uislamu" katika mfululizo wa Mafunzo haya yanayotolewa katika **Juzuu Saba** kwa lengo la kuwawezesha watu kuufahamu Uislamu katika usahihi wake na kuwapa ari na hamasa ya kuufuata katika maisha yao ya kila siku na hatimaye kuusimamisha katika jamii.

Juzuu hii ya pili ya "Darasa la Watu Wazima", pamoja na kuainisha **nguzo tano za Uislamu** na lengo kuu la nguzo hizo, imechukua pia jukumu la kuainisha lengo la kila nguzo na namna linavyofikiwa. Aidha juzuu hii ya pili imezingatia hali halisi ya mazingira ya jamii ya Waislamu na imejaribu kutathmini utekelezaji na ufikiaji wa lengo la kila nguzo ya Uislamu. Ili kufikia lengo kwa ufanisi , juzuu hii imegawanywa katika sura tano zifuatazo:-

1. Shahada
2. Kusimamisha Swala
3. Zakat na Sadaqat
4. Swaumu
5. Hija na Umra.

Katika **Toleo hili la Pili,** sura hizi zimeboreshwa zaidi, hasa katika eneo la kuonesha namna linavyofikiwa lengo la kila nguzo ya Uislamu. Uboreshaji huu umefanyika ili kuzidi kuwapa Waislamu uwezo wa kutekeleza nguzo za Uislamu kwa usahihi na kupata maandalizi stahiki yatakayo wawezesha kuusimamisha Uislamu katika jamii.

Kwa kuzingatia kuwa kazi ya binadamu haikosi mapungufu, kwani ukamilifu haupo ila kwa Allah (s.w) tu, tunawaomba wasomaji wetu wa juzuu hizi za "Darasa la Watu Wazima" mvumilie mapungufu yote yale yanyovumilika na mtoe masahihisho, maoni na mapendekezo yenu kwa ajili ya kuboresha mafunzo haya ili lengo tarajiwa lifikiwe kwa ufanisi.

Tunachukua fursa hii kuwashukuru na kuwaombea dua, Allah (s.w) awalipe kheri nyingi hapa duniani na akhera wale wote waliochangia na wanoendelea kuchangia utoaji na uboreshaji wa mafunzo haya.

رَبَّنَآ ءَاتِنَا مِن لَّدُنكَ رَحْمَةً وَهَيِّئْ لَنَا مِنْ أَمْرِنَا رَشَدًا ﴿١٠﴾

*"Mola wetu! Tupe uongofu utakao kwako na Tutengenezee uongofu katika (kila) jambo letu" (18:10)*

**Aaamiin**

# Yaliyomo

**Neno la Awali Kwa Toleo la Pili.......................................................... i**
**Utangulizi...................................................................................... Viii**

## Sura ya Kwanza: SHAHADA

**Kutoa Shahada Mbili ............................................................... 1**
Maana ya Shahada ya Kwanza.......................................................1
Maana ya Shahada ya Pili ............................................................2
**Mwenendo wa Mtu aliyetoa Shahada.......................................... 4**
Kujielimisha kwa Ajili ya Allah (s.w)..........................................5
Kuwa na Hekima ..........................................................................6
Ikhlas ...........................................................................................6
Kujiepusha na Ria na Kujiona ......................................................8
Kuepuka Unafiki ..........................................................................9
Kuwa Mkweli ...............................................................................11
Kujiepusha na Uwongo ................................................................12
Uwongo na Ulaghai katika Biashara ...........................................13
Ni wapi uwongo unaporuhusiwa? ...............................................14
Kuwa Muaminifu (Kuchunga Amana) ........................................15
Madaraka ni Amana .....................................................................17
Uchaguzi ni Amana ......................................................................17
Kazi ni Amana .............................................................................18
Mali ya Umma ni Amana .............................................................19
Siri ni Amana ...............................................................................20
Kuwa Muadilifu ...........................................................................21
Kuchunga Ahadi ...........................................................................22
Deni ni Ahadi ...............................................................................25
Nadhiri ni ahadi............................................................................27
Mikataba ni Ahadi .......................................................................28
Kuepuka Usengenyaji .................................................................31
Kujiepusha na Dharau .................................................................33
Kujiepusha na Matusi ..................................................................34
Kuepuka Mabishano .....................................................................35
Kuepuka kujisifu na kujitukuza ...................................................36
Kuepukana na Kibri na Majivuno ................................................37
Kuepukana na Kulaani Ovyo .......................................................39
Kujiepusha na Viapo ....................................................................40
Kujiheshimu na kuwaheshimu wengine ......................................40
Kuwa Mpole na Mnyenyekevu ....................................................42
Kuwa mwenye Huruma ...............................................................43
Kuwa na Haya ..............................................................................45
Kuwa na Upendo ..........................................................................46
Kujiepusha na Chuki na Uadui .....................................................48

Kuwa Mwenye Kusamehe ........ 50
Kudhibiti Hasira ........ 52
Kuwa mwenye Subira na Uvumilivu ........ 53
Kuwa Mkarimu ........ 59
Kuepuka Uchoyo na Ubahili ........ 62
Kuwa Mwenye Kutosheka ........ 63
Kuepuka Tamaa na Kuombaomba ........ 64
Kuepuka Husuda ........ 66
Kumtegemea Mwenyezi Mungu (s.w) ........ 67
Kuepukana na Woga ........ 69
Kuepukana na Kukata Tamaa ........ 70
Kuwa na Istiqama (Msimamo Thabiti) ........ 71
**Zoezi la kwanza ........ 73**

## Sura ya Pili: KUSIMAMISHA SWALA

**Umuhimu wa Kusimamisha Swala ........ 75**
Lengo la Kusimamisha Swala ........ 76
Maana ya Swala ........ 77
**Sharti za Swala ........ 78**
Twahara ........ 78
Sitara ........ 91
Kuchunga Wakati ........ 95
Kuelekea Qibla ........ 102
**Nguzo za Swala ........ 103**
**Sunnah za Swala ........ 106**
**Namna ya kuswali kama alivyoswali Mtume (s.a.w) ........ 107**
Lugha ya Swala ........ 119
Mambo yanayobatilisha Swala ........ 119
Dua na Dhikri Baada ya Swala ........ 120
Khushui (Unyenyekevu) Katika Swala ........ 122
Namna ya Kufikia Lengo la Swala ........ 124
**Swala tano za Faradh katika Nyakati za Dharura ........ 126**
Swala ya Mgonjwa ........ 127
Swala ya Msafiri ........ 129
Kusimamisha Swala Vitani ........ 134
**Kusimamisha Swala ya Jamaa ........ 136**
Ruhusa kwa Wanawake Kuswali Jamaa Msikitini ........ 138
Udhuru wa Kutoswali Jamaa Msikitini ........ 138
Inaruhusiwa kuswali swala moja mara mbili ........ 139
Namna ya Kuswali Katika Jamaa ........ 139
**Swala ya Ijumaa ........ 148**
**Kusimamisha Swala za Sunnah ........ 152**
Swala ya Maamkizi ya Msikiti ........ 153
Sunnah za Qabliyyah na Ba'adiyah ........ 153
Swala ya Witri ........ 154

Swala ya Tahajjud .................................................... 156
Swala ya Tarawehe .................................................... 157
Swala ya Idil-Fitri na Idil-Hajj .................................................... 159
Swalatudh-Dhuhaa .................................................... 160
Swalatul-Istikharah .................................................... 160
Swala ya Kukidhi Haja .................................................... 161
Swalatut-Tawbah .................................................... 162
Swala ya Kupatwa kwa Jua na Mwezi .................................................... 163
Swala ya Kuomba Mvua - (Swalatul Istisqaa) .................................................... 164

**Tathmini ya Swala Zetu .................................................... 165**

**Swala ya maiti .................................................... 169**

Namna ya Kumkafini Maiti .................................................... 175
Namna ya kumswalia Maiti .................................................... 178
Masharti ya Swala ya Maiti .................................................... 178
Nguzo za Swala ya Maiti .................................................... 179
Sunnah za Swala ya Maiti .................................................... 179
Namna ya Kutekeleza Swala ya Maiti .................................................... 179
Kusindikiza Jeneza .................................................... 182
Kuzika .................................................... 183

**Zoezi la Pili .................................................... 187**

## Sura ya Tatu: ZAKAT NA SWADAQAT

Maana ya Zakat .................................................... 189
Maana ya Swadaqa .................................................... 189

**Msisitizo wa Utoaji wa Zakat na Swadaqat katika Uislamu ......... 190**

**Masharti ya Utoaji wa Zakat na Swadaqat .................................................... 194**

Kutoa vilivyo halali .................................................... 194
Kutoa vilivyo vizuri .................................................... 195
Kutoa kwa kati na kati .................................................... 196
Kujiepusha na ria na kufuatilia kwa masimbulizi .................................................... 196
Kuwapa wanaostahiki .................................................... 198

**Mali inayojuzu kutolewa Zakat, nisaab na kiwango cha Zakat ..... 205**

Mazao ya Shambani .................................................... 206
Wanyama wafugwao kwa ajili ya chakula .................................................... 208
Dhahabu (gold), fedha (silver) na fedha taslimu (cash) .................................................... 210
Vito (mapambo )vya Dhahabu na Fedha .................................................... 211
Mali ya kuchimbuliwa ardhini au mali ya kuokota .................................................... 211
Mali ya Biashara .................................................... 211

**Zakat hutakasa Nafsi .................................................... 213**

**Ukusanyaji na Ugawaji wa Zakat .................................................... 218**

**Zoezi la tatu .................................................... 221**

## Sura ya Nne: SWAUMU

Maana ya Swaumu (Funga) .................................................... 222

**Umuhimu wa Funga ya Ramadhani katika Uislamu .................................................... 223**

Kwa nini Funga imefaradhishwa Mwezi wa Ramadhani .......... 225
**Kuonekana kwa mwezi wa Ramadhani ........................................ 226**
Kwanini kufuata mwandamo wa mwezi?.................................. 226
Ni lazima kila mfungaji aone mwezi? .................................... 227
Mwezi ukionekana sehemu moja, Waislamu wote ulimwenguni watalazimika kufunga? ...................................................... 228
**Nguzo za Funga ............................................................... 230**
**Yanayobatilisha Funga ........................................................ 230**
Kula na Kunywa kwa kusudi ................................................ 231
Kujitapisha Makusudi.......................................................... 231
Kupatwa na Hedhi au Nifasi ................................................ 231
Kujitoa Manii Makusudi....................................................... 231
Kunuia Kula na hali umefunga ............................................. 232
**Yanayoharibu au Kupunguza Thamani ya Funga........................... 232**
**Yasiyobatilisha funga ......................................................... 233**
Kula au Kunywa kwa Kusahau ............................................. 233
Kuoga wakati umefunga ...................................................... 233
Kutokwa na Manii .............................................................. 234
Kuamka na Janaba.............................................................. 234
Kubusiana na kukumbatiana Mume na Mke .......................... 234
Kusukutua na kupandisha Maji Puani.................................... 235
Kupaka Wanja na Dawa ya Machoni ...................................... 235
Kumeza usichoweza kujizuia nacho....................................... 235
Kujipaka mafuta au manukato ............................................. 235
Kuumika au kutoa Damu ..................................................... 235
Kupiga Sindano .................................................................. 236
**Waislamu Wanaolazimika Kufunga Ramadhani............................ 236**
Wenye akili timamu ............................................................ 236
Waliofikia Baleghe ............................................................. 236
Wenye afya ........................................................................ 237
Wakazi wa Mji .................................................................... 238
Kwa Mwanamke, asiwe katika Hedhi wala Nifasi.................... 240
**Hukumu ya Muislamu Aliyeacha Kufunga kwa Makusudi ............ 240**
Kulipia Ramadhani ............................................................. 241
**Sunnah zinazoambatana na funga ya Ramadhani ........................ 241**
Kula na kuchelewesha Daku.................................................. 241
Kufuturu Mapema ............................................................... 242
Kuzidisha Ukarimu ............................................................. 243
Kuzidisha kusoma Qur'an..................................................... 243
Kusimamisha Swala ya Usiku ya Tarawehe ............................ 244
Kuutafuta usiku wa Lailatul-Qadr ........................................ 244
**Umuhimu wa usiku wa Lailatul Qadr........................................ 245**
Kukaa Itiqaf ....................................................................... 247
**Zakatul-Fitri ..................................................................... 249**
Umuhimu wa Zakatul Fitri ................................................... 249
Nisaab ya Zakatul-Fitri ........................................................ 249
Kiwango cha Zakatul-Fitri .................................................... 249

Muda unaofaa kutolewa Zakatul-Fitri ..... 250
Watu wanaostahiki kupewa Zakatul-Fitri ..... 250
**Iddil -Fitri ..... 251**
Swala ya Iddil-Fitri ..... 251
Yaliyo Sunnah kuyafanya Siku ya Idd ..... 253
Tahadhari Katika Siku ya Idd ..... 254
**Funga za Kafara ..... 254**
**Funga za Sunnah ..... 259**
Kufunga siku tatu katika kila mwezi mwandamo ..... 259
Funga za Jumatatu na Al-khamisi ..... 261
Kufunga siku sita katika Mwezi wa Shawwal ..... 261
Funga ya Arafa ..... 262
Funga ya Ashura ..... 262
Funga katika mwezi wa Sha'aban ..... 263
Uhuru wa kuvunja Funga ya Sunnah ..... 264
**Siku Zilizoharamishwa Kufunga Sunnah ..... 265**
Siku kuu za Iddil-Fitri na Iddil-Hajj ..... 265
Siku za Tashriq ..... 265
Siku ya Shaka ..... 265
Siku ya Ijumaa ..... 266
**Lengo la Funga ..... 266**
Funga inavyomuandaa mtu kuwa mcha-Mungu. ..... 268
Kwa nini Lengo la Funga halifikiwi na Wafungaji Wengi? ..... 277
**Zoezi la Nne ..... 280**

## Sura ya Tano: Hija na 'Umra

Maana ya Hija na 'Umra ..... 281
**Umuhimu na nafasi ya Ibada ya Hija katika Uislamu ..... 281**
**Wanaowajibika kuhiji ..... 283**
**Muda wa Hijja ..... 287**
**Mwenendo wa mwenye kunuia Hija au 'Umra ..... 287**
**Vituo vya kunuia Hija ..... 288**
**Ihram ..... 290**
Yaliyoharamishwa kwa Mwenye kuwa katika Ihram ..... 290
Kafara kwa mwenye kuvunja masharti ya Ihram ..... 291
**Aina za Hija ..... 293**
**Matendo ya Hija na 'Umra' ..... 294**
Ihram na Nia ya Hija au 'Umra ..... 294
Talbiya ..... 295
Tawaf ..... 297
Kusa'i ..... 301
Siku ya Tarwiyya ..... 303
Siku ya Arafa (mwezi 9, Dhul-Haji) ..... 303
Kulala Muzdalifa ..... 305
Siku ya Kuchinja (10 Dhul-Hija) ..... 306
Siku za Tashriq (Ayyamut Tashriq) ..... 306

Tawaful Widaa (Tawaf ya Kuaga) .... 307
**Kubatilika kwa Hija .... 307**
**Lengo la Hija .... 308**
**Namna Hija inavyomuandaa Muumini kuwa Khalifa wa Allah katika jamii .... 308**
Maandalizi ya Safari ya Hija .... 308
Safari ya Hija .... 310
Ihram: .... 312
Talbiya .... 313
Tawaf .... 315
Sai' .... 316
Kupiga kambi Mina, Mwezi 8 Dhul-Hija .... 319
Kusimama Arafa, Mwezi 9 Dhul-Hajj .... 319
Kupiga Kambi Muzdalifa .... 319
Kutupa Mawe Mina .... 320
Kuchinja Mnyama .... 320
Kupiga kambi Mina mwezi 11 - 13 Dhul-Hijja .... 322
Kuaga Ka'aba .... 322
**Yanayopelekea Lengo la Hijja Kutofikiwa .... 323**
Kuhiji kwa Chumo la Haramu .... 324
Kutochunga Miiko ya Hijja .... 325
Kutotekeleza Nguzo za Hija Vilivyo .... 326
Kutojulikana kwa Lengo la Hijja .... 326
**Zoezi la Tano .... 326**

# UTANGULIZI

## Nguzo za Uislamu

Tunajifunza kuwa Uislamu hauwezi kusimama katika kila kipengele cha maisha ya jamii bila ya kusimamisha kwanza kwa ukamilifu nguzo tano za Uislamu. Kwa maana nyingine, nguzo tano za Uislamu ndio nyenzo kuu za kuuwezesha Uislamu kusimama katika jamii. Nguzo za Uislamu tunazifahamu kwa kurejea Hadithi ifuatayo:

> *Ibn Umar (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: Uislamu umejengwa juu ya (nguzo) tano, kushuhudia kuwa hapana mola ila Allah na kwamba Muhammad ni Mtume wa Allah, kusimamisha Swala, kutoa Zakat, kufunga Ramadhani na kuhiji nyumba Takatifu (al-Ka'abah) kwa mwenye uwezo." (Bukhari na Muslimu)*

## Kueleweka Vibaya kwa Hadith Hii

Kuna baadhi ya "Waislamu" wameielewa vibaya Hadithi hii kuwa: "Uislamu ni nguzo tano" au kuwa Uislamu unakamilishwa na nguzo tano tu. Kwa maana nyingine wameelewa kuwa nguzo tano zikitekelezwa Uislamu utakuwa umeshakamilika na Waislamu hawana wajibu wa lolote lingine. Kutokana na mtizamo huu potofu, utamkuta Muislamu anaswali, anafunga na ni Al-haj, lakini anakula riba, anazini na anachanganyika na kushirikiana na makafiri katika shughuli mbali mbali zilizo nje ya mipaka ya Allah (s.w).

## Lengo la Nguzo tano za Uislamu

Ifahamike wazi kuwa Allah (s.w) ni muweza wa kila kitu na ni mwenye kujitosheleza kwa kila kitu. Yeye ndiye chanzo cha Utajiri, Heshima, Furaha na yale yote anayoyatamani na kuyathamini mwanaadamu. Hivyo, ni wazi kwamba Allah (s.w) hahitajii chochote kutoka kwa mwanaadamu bali mwanaadamu ndiye anayehitajia kutoka kwake. Kwa hiyo ni dhahiri kuwa Allah (s.w) hakutuamrisha kusimamisha Nguzo tano za Uislamu ili tumuongezee furaha, utukufu au hadhi katika Uungu wake; kwani hata watu wote wakiamua kumtii, hawamuongezei hata chembe ya daraja katika Utukufu wake, vivyo hivyo watu wote wakiamua kumuasi, hawampunguzii hata chembe ya Utukufu wake. Kwanini sasa, Allah (s.w) ametuamrisha tusimamishe hizi nguzo tano?

Allah (s.w) ametuwekea hizi nguzo tano ili ziwe nyenzo pekee za kutufikisha kwenye lengo la kuumbwa kwetu.Lengo la kuumbwa binaadamu ni kumuabudu Allah (s.w) kama tunavyokumbushwa katika Qur-an:

وَمَا خَلَقْتُ ٱلْجِنَّ وَٱلْإِنسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ ﴿٥٦﴾

*"Sikuwaumba majini na watu ila wapate kuniabudu" (51:56)*

Kumuabudu Allah (s.w), kama lengo la maisha yetu ni kumtii Allah (s.w) katika kila kipengele cha maisha kwa kuchunga mipaka aliyotuwekea katika kila kitendo tunachokifanya. Hivyo, Allah (s.w) ametuamrisha kusimamisha nguzo tano ili ziwe nyenzo kuu za kutuweka katika nidhamu ambayo itatuwezesha kuendesha maisha ya kumtii Allah (s.w) katika kila kipengele cha maisha yetu. Kama mtu atatekeleza hizi nguzo tano zote kwa pamoja na bado akawa hajawa katika nidhamu iliyokusudiwa na badala yake akawa anaendelea kuishi kinyume na lengo la maisha yake, ni kipimo tosha kuwa Shahada yake, Swala zake, Zakat zake, Swaumu zake na Hija yake, havijakubaliwa na Mola wake. Amefanya mazoezi yasiyotoa matunda tarajiwa.

Ukipitia Qur-an, utaona kuwa kila nguzo katika hizi tano ina lengo lake maalumu. Yaani, kila nguzo imekusudiwa kumtayarisha mtu katika uwanja maalumu ili hatimaye afikie lengo kuu la maisha yake. Hii ndiyo hekima ya kuamrishwa kutekeleza kwa ukamilifu nguzo zote tano za Uislamu. Mtu akiacha angalau nguzo moja kwa kusudi hawezi kwa vyovyote vile kufikia lengo la maisha yake kwa sababu kwa vyovyote vile patatokea mapungufu katika kumuandaa na kumuweka katika nidhamu itakayomuwezesha kuyafanya maisha yake yote kuwa ibada. Katika juzuu hii tunafahamishwa lengo la kila nguzo na namna lengo hilo linavyofikiwa. Pia kwa kuzingatia hali halisi tumejaribu kutathmini ufikiwaji wa lengo la kila nguzo.

## Sura ya Kwanza
# SHAHADA

### Kutoa Shahada Mbili

Kwa mujibu wa Hadith, tuliyoirejea katika utangulizi, nguzo ya kwanza ya Uislamu ni kutoa shahada mbili kwa kusema:

أَشْهَدُ أَنْ لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللهُ وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا رَسُولُ اللهِ

***Ash hadu an laailaha illa llaahu wa ash hadu anna Muhammadar Rasuulu llahi***

**Tafsiri:**
*Nashuhudia kuwa hapana mungu ila Allah na ninashuhudia kuwa Muhammad ni Mtume wa Allah.*

Shahada ndio kiingilio cha Uislamu. Yaani wasiokuwa Waislamu, wakiamua kuingia katika Uislamu, hukaribishwa na Waislamu kwa kutamkishwa hizi shahada mbili. Ukweli ni kwamba mtu hatakuwa Muislamu kwa kutamka tu haya maneno ya shahada bila ya kufahamu maana ya ndani.

### Maana ya Shahada ya Kwanza:

*"Nashuhudia kuwa hapana mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila Allah"*

Maana yake ni kwamba, huyu mja baada ya uchunguzi wa kina kwa kuzingatia dalili mbali mbali zinazodhihiri katika umbile la mbingu na ardhi na vyote vilivyomo, katika nafsi ya mwanaadamu, katika historia ya mwanaadamu, katika maisha ya Mitume na mafundisho yao, anayakinisha moyoni mwake kuwa yuko Mungu Muumba, Mpweke, Mwenye Uwezo juu ya kila kitu na Mmiliki wa kila kitu. Baada ya kuwa na yakini hii, huyu mja sasa anatoa ahadi kwa Allah(s.w) na kwa walimwengu wote kuwa, hatakuwa na mwingine yeyote atakaye muabudu au atakayemtii katika kukiendea kila kipengele cha maisha yake kinyume na Allah (s.w).Kwa maana nyingine mja anayetoa shahada hii, anaahidi kuwa ataendesha maisha yake yote ndani ya mipaka aliyowekewa na Allah (s.w) katika kukiendea kila kipengele cha maisha yake ya kibinafsi na kijamii. Yaani wenye kumshuhudia Allah kikweli ni wale wanaofuata Uislamu katika kila kipengele cha maisha yao kama Allah (s.w) anavyowaamrisha katika aya zifuatazo:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ ٱدْخُلُوا۟ فِى ٱلسِّلْمِ كَآفَّةً وَلَا تَتَّبِعُوا۟
خُطُوَٰتِ ٱلشَّيْطَٰنِ ۚ إِنَّهُۥ لَكُمْ عَدُوٌّ مُّبِينٌ ﴿٢٠٨﴾

*"Enyi Mlioamini! Ingieni katika Uislamu wote (katika hukumu zote za Uislamu) wala msifuate nyayo za Shetani, kwa hakika yeye kwenu ni adui aliye dhahiri". (2:208).*

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ ٱتَّقُوا۟ ٱللَّهَ حَقَّ تُقَاتِهِۦ وَلَا تَمُوتُنَّ إِلَّا وَأَنتُم
مُّسْلِمُونَ ﴿١٠٢﴾

*"Enyi mlioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu kama ipasavyo kumcha; wala msife isipokuwa mmekwishakuwa Waislamu kamili". (3:102).*

## Maana ya Shahada ya Pili

*"Na ninashuhudia kuwa Muhammad ni Mtume wa Allah"*

Hii ndio sehemu ya pili ya shahada ambayo huikamilisha shahada ya kwanza. Labda swali litaulizwa: "Kumshuhudia Mtume Muhammad (s.a.w) kunakamilishaje shahada ya kwanza?" Tumeona kuwa maana halisi ya kumshuhudia Allah (s.w) ni kumuabudu Allah pekee katika kila kipengele cha maisha yetu.Tutamuabudu vipi Allah (s.w) katika kila kipengele cha maisha yetu? Tutajuaje ni yepi aliyoyaharamisha Allah na yepi aliyoyahalalisha? Ni njia ipi tuifuate ili tupate radhi zake na ipi tuiepuke ili tuepukane na ghadhabu zake? Tutajuaje ipi njia sahihi na ipi potofu? Yote haya hatuwezi kuyajua mpaka tupate muongozo kutoka kwa Allah (s.w) mwenyewe.

Utaratibu aliouweka Allah (s.w) katika kuwaongoza wanaadamu ni kuwaleta Mitume miongoni mwa wanaadamu wanaume ambao huwaletea mwongozo na kuwafanya Waalimu wajuzi wenye hekima ili wawafundishe wanaadamu wenzao kinadharia na kimatendo juu ya Allah (s.w) na namna ya kumuabudu. Hivyo ili mja aweze kumjua Allah (s.w) na kumuamini ipasavyo na kisha aweze kumuabudu inavyostahiki katika kila kipengele cha maisha yake, hanabudi kwanza kumuamini Mtume na kufuata mafundisho yake. Kwahiyo, sisi watu wa Umma huu wa Mtume wa mwisho, hatuwezi kuwa Waumini wa kweli wa Allah (s.w) bila ya kumshuhudia Mtume Muhammad (s.a.w) kuwa ni Mtume wa Allah (s.w).

Kumshuhudia Muhammad (s.a.w) kuwa ni Mtume wa Allah (s.w), ni kutoa ahadi kuwa utafuata mafundisho ya Mtume (s.a.w) vilivyo kwa kutekeleza yale yote aliyoyaamrisha na kuacha yale yote aliyoyakataza na kumuigiza mwenendo na tabia yake kama inavyosisitizwa katika Qur'an:

قُلْ إِن كُنتُمْ تُحِبُّونَ ٱللَّهَ فَٱتَّبِعُونِى يُحْبِبْكُمُ ٱللَّهُ وَيَغْفِرْ لَكُمْ
ذُنُوبَكُمْ ۗ وَٱللَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٣١﴾

*"Sema ( Muhammad kuwaambia watu): 'Ikiwa nyinyi mnampenda Mwenyezi Mungu, basi nifuateni; (hapo)Mwenyezi Mungu atakupendeni na atakughufirieni madhambi yenu.Na Mwenyezi Mungu ni mwenye Maghufira na Mwenye Rehema". (3:31)*

وَمَآ ءَاتَىٰكُمُ ٱلرَّسُولُ فَخُذُوهُ وَمَا نَهَىٰكُمْ عَنْهُ فَٱنتَهُوا۟ ۚ وَٱتَّقُوا۟
ٱللَّهَ ۖ إِنَّ ٱللَّهَ شَدِيدُ ٱلْعِقَابِ ﴿٧﴾

*"...Na anachokupeni Mtume basi pokeeni na anachokukatazeni jiepusheni nacho. Na muogopeni Mwenyezi Mungu; kwa yakini Mwenyezi Mungu ni mkali wa kuadhibu". (59:7)*

لَّقَدْ كَانَ لَكُمْ فِى رَسُولِ ٱللَّهِ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ لِّمَن كَانَ يَرْجُوا۟
ٱللَّهَ وَٱلْيَوْمَ ٱلْـَٔاخِرَ وَذَكَرَ ٱللَّهَ كَثِيرًا ﴿٢١﴾

*"Bila shaka mnao mfano mwema kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa mwenye kumuogopa Mwenyezi Mungu na siku ya Mwisho, na kumtaja Mwenyezi Mungu sana". (33:21)*

Kwahiyo, Muumini anapotoa shahada mbili anaahidi kwa dhati ya moyo wake kuwa atamtii Allah(s.w) na Mtume Muhammad (s.a.w) kwa unyenyekevu kwa kukiendea kila kipengele cha maisha ya kibinafsi na ya kijamii kwa mujibu wa mwongozo wa Qur-an na Sunnah ya Mtume (s.a.w). Mtu hatakuwa Muumini pale atakapoendesha maisha yake ya kibinafsi au ya kijamii kinyume na shahada kama tunavyokumbushwa katika aya ifuatayo:

وَمَا كَانَ لِمُؤْمِنٍ وَلَا مُؤْمِنَةٍ إِذَا قَضَى ٱللَّهُ وَرَسُولُهُۥٓ أَمْرًا أَن
يَكُونَ لَهُمُ ٱلْخِيَرَةُ مِنْ أَمْرِهِمْ ۗ وَمَن يَعْصِ ٱللَّهَ وَرَسُولَهُۥ فَقَدْ

*"Haiwi kwa mwanamume aliyeamini wala kwa mwanamke aliyeamini, Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanapokata shauri, wawe na hiari katika shauri lao. Na Mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake, hakika amepotea upotofu uliowazi." (33:36).*

ضَلَّ ضَلَـٰلًا مُّبِينًا ﴿٣٦﴾

## Mwenendo wa Mtu aliyetoa Shahada

Muislamu aliyetoa shahada ya kweli hanabudi kumfanya Mtume (s.a.w) kuwa kiigizo chake kimwenendo na kitabia. Mtume (s.a.w) alikuwa na tabia njema kabisa kama tunavyofahamishwa katika Qur'an:

*"Na bila shaka (Wewe Muhammad) una tabia njema kabisa." (68:4)*

وَإِنَّكَ لَعَلَىٰ خُلُقٍ عَظِيمٍ ﴿٤﴾

Mtume (s.a.w) mwenyewe amewahimiza waumini kujipamba na tabia njema kama tunavyojifunza katika Hadithi zifuatazo:

*Abdullah bin Amr (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: "Aliye kipenzi changu kuliko wote katika nyinyi (Waislamu) ni yule aliyewazidi kwa tabia njema". (Bukhari)*

*Harithat bin Wahab (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: "Yule ambaye tabia yake ni mbaya na katili, hataingia Peponi". (Abu Daud)*

*Abu Hurairah (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: "Mwenye imani iliyopea katika Waislamu ni yule mwenye tabia njema, na aliye mbora katika nyinyi ni yule anayemtendea wema mkewe". (Tirmidh)*

*Abu Darda (r.a) amesimulia kuwa Mtume (s.a.w) amesema: "Hapana kitu kitakachotia uzito katika mizani ya Muumini katika siku ya hukumu kuliko tabia njema..." (Tirmidh)*

*Abu Hurairah (r.a) amesimulia kuwa Mtume (s.a.w) aliulizwa juu ya mambo yatakayopelekea watu wengi kuingia Peponi. Alijibu Mtume: "Uchaji - Mungu na tabia njema". Kisha akaulizwa tena: "Ni mambo yepi yatakayompelekea mtu kuingizwa Motoni?" Alijibu Mtume, "Mdomo na tupu (viungo vya siri)". (Tirmidh)*

Hivyo, muumini wa kweli hanabudi kujipamba na vipengele vya tabia njema vilivyoainishwa katika Qur-an na Sunnah. Katika juzuu hii

tumerejea vipengele vya tabia njema vifuatavyo:

### 1. Kujielimisha kwa Ajili ya Allah (s.w).

Elimu ndiyo zana aliyotunukiwa mwanadamu ili aitumie kutekeleza majukumu yake kama Khalifa wa Allah (s.w) hapa ulimwenguni. Mara tu baada ya Nabii Adam (a.s) kuumbwa na kabla hajaruzukiwa chochote na hata kabla ya kukaribishwa kwenye neema za bustanini (Peponi) alifunzwa mambo yote ya msingi yatakayomuwezesha kuwa Khalifa hapa Ulimwenguni:

وَعَلَّمَ ءَادَمَ ٱلۡأَسۡمَآءَ كُلَّهَا

*"Na (Allah (s.w)) akamfundisha Adam majina ya vitu vyote..." (2:31).*

Naye Mtume Muhammad (s.a.w) Wahyi na amri ya kwanza aliyoipokea kutoka kwa Mola wake ni kusoma kwa ajili ya Allah (s.w). Hivyo kila Muislamu analazimika kuitekeleza kwa hima amri hii ya kwanza ili aweze kumuabudu Mola wake inavyostahiki na aweze kuwa Khalifa wake hapa ulimwenguni.Aidha kila Muislamu analazimika kujielimisha mambo ya msingi yatakayomuwezesha kuwa Muumini wa kweli na kumuwezesha kuendesha maisha yake yote ya kibinafsi na kijamii kwa mujibu wa Qur-an na Sunnah.

Ni wazi kuwa Muislamu mwenye kujipamba na tabia ya kujielimisha katika mambo muhimu ya maisha kwa lengo la kupata ufanisi katika kumuabudu Allah (s.w) na kusimamisha Ukhalifa katika jamii; atakuwa tofauti kiutendaji na kiuchaji na yule aliye mvivu wa kujielimisha kama tunavyojifunza katika Qur-an:

هَلۡ يَسۡتَوِي ٱلَّذِينَ يَعۡلَمُونَ وَٱلَّذِينَ لَا يَعۡلَمُونَۗ . . .

*"Je, wanaweza kuwa sawa wale wanaojua na wale wasiojua?" Wanaotanabahi ni wale wenye akili tu." (39:9).*

يَرۡفَعِ ٱللَّهُ ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ مِنكُمۡ وَٱلَّذِينَ أُوتُواْ ٱلۡعِلۡمَ دَرَجَٰتٖۚ

*"Allah atawainua daraja wale walioamini miongoni mwenu;na waliopewa elimu watapata daraja zaidi..." (58:11)*

Ukizingatia kuwa kutafuta elimu ni faradh kwa kila Muislamu mwanamume na mwanamke, mkubwa na mdogo, aya hizi zatosha kuwa

kichocheo kwa kila Muumini kujibidiisha kwa kujielimisha kwa ajili ya Allah(s.w) kwa kadri ya uwezo wake na kila wakati awe anaomba dua ifuatayo:

*"... Mola wangu! Nizidishie elimu."* (20:114) رَّبِّ زِدْنِي عِلْمًا ﴿١١٤﴾

## 2. Kuwa na Hekima

Elimu, pamoja na ubora wake, hainufaishi bila ya kutumiwa kwa hekima. Kufanya jambo kwa hekima ni kufanya jambo kwa kutumia ujuzi unaostahiki na kwa kufuata utaratibu unaostahiki kulingana na mahali na wakati kwa kuzingatia mwongozo na mipaka ya Allah (s.w) na Sunnah ya Mtume wake.

Kila Muumini anawajibika kufanya mambo yake yote kwa ujuzi wa kutosha. Kabla Muislamu hajafanya jambo lolote anatakiwa afahamu lengo la hilo analolifanya na je, hilo lengo linampelekea kumuabudu Mola wake na kuwa Khalifa wake au la. Baada ya kulifahamu lengo hanabudi kuwa na ujuzi na mbinu zinazostahiki kumfikisha kwenye lengo kwa wepesi na kwa ufanisi. Asichague njia ndefu na ngumu akaacha njia fupi na nyepesi inayowafikiana na mwongozo wa Allah (s.w) na Sunnah za Mitume wake.

Hekima ni katika vipengele vya tabia njema vilivyo azizi anavyotakiwa avipiganie Muumini ili awe na hadhi inayostahiki, hadhi ya Ukhalifa wa Allah (s.w) hapa ulimwenguni. Waumini hatuna budi kufanya mambo yetu kwa hekima na daima tumuombe Allah atuzidishie Hekima.

يُؤْتِي ٱلْحِكْمَةَ مَن يَشَآءُ ۚ وَمَن يُؤْتَ ٱلْحِكْمَةَ فَقَدْ أُوتِيَ خَيْرًا
كَثِيرًا ۗ وَمَا يَذَّكَّرُ إِلَّآ أُو۟لُوا۟ ٱلْأَلْبَٰبِ ﴿٢٦٩﴾

*"(Allah) Humpa hikma amtakaye, na aliyepewa hikma bila shaka amepewa heri nyingi. Na hawakumbuki ila wenye akili."* (2:269).

## 3. Ikhlas

Ikhlas ni kufanya kila jambo jema kwa ajili ya Allah (s.w) tu. Yaani kutoa huduma na mali kwa watu wanaohitajia msaada bila ya kutaraji malipo yoyote kutoka kwao ila kutoka kwa Allah (s.w) tu. Kwa mfano kumlisha na kumvisha fukara, maskini au yatima bila ya kutarajia hata kupata shukurani (ahsante) kutoka kwake ila tu kwa kutegemea malipo kutoka kwa Allah (s.w) ni kitendo cha Ikhlas. Wale wanaotoa misaada

kwa wanaohitajia kwa Ikhlas, wamesifiwa na Allah (s.w) katika Qur-an:

وَيُطْعِمُونَ ٱلطَّعَامَ عَلَىٰ حُبِّهِۦ مِسْكِينًا وَيَتِيمًا وَأَسِيرًا ﴿٨﴾
إِنَّمَا نُطْعِمُكُمْ لِوَجْهِ ٱللَّهِ لَا نُرِيدُ مِنكُمْ جَزَآءً وَلَا
شُكُورًا ﴿٩﴾ إِنَّا نَخَافُ مِن رَّبِّنَا يَوْمًا عَبُوسًا قَمْطَرِ
يرًا ﴿١٠﴾

*"Na huwalisha chakula maskini na yatima na wafungwa na hali yakuwa wenyewe wanakipenda (chakula hicho. Husema nyoyoni mwao wanapowapa chakula hicho): Tunakulisheni kwa ajili ya kutaka radhi ya Mwenyezi Mungu (tu). Hatutaki kwenu malipo wala shukurani. Hakika sisi tunamuogopa Mola wetu hiyo siku yenye shida na taabu." (76:8-10).*

وَسَيُجَنَّبُهَا ٱلْأَتْقَى ﴿١٧﴾ ٱلَّذِى يُؤْتِى مَالَهُۥ يَتَزَكَّىٰ ﴿١٨﴾ وَمَا
لِأَحَدٍ عِندَهُۥ مِن نِّعْمَةٍ تُجْزَىٰٓ ﴿١٩﴾ إِلَّا ٱبْتِغَآءَ وَجْهِ رَبِّهِ ٱلْأَعْلَىٰ
﴿٢٠﴾ وَلَسَوْفَ يَرْضَىٰ ﴿٢١﴾

*"Na amchaye (Mwenyezi Mungu) ataepushwa nao (huo moto uwakao kwa nguvu). Ambaye hutoa mali yake kwa ajili ya kujitakasa na hali ya kuwa hakuna yeyote anayemfanyia ihsani ili awe anamlipa. Isipokuwa (anafanya haya) kwa kutaka radhi ya Mola wake Mtukufu. Basi atapata la kumridhisha." (92:17-21).*

Si katika kutoa tu mali, bali lolote lile analolifanya Muislamu wa kweli hana budi kulifanya kwa nia ya kupata radhi ya Allah (s.w). Utendaji wa Mwanaadamu uliofanywa kwa Ikhlas ndio tu utakaomuwezesha kuwajibika vilivyo kwa wanaadamu wenzake na kwa Mola wake Mtukufu.

Ili kujikumbusha mara kwa mara kufanya mambo yetu kwa Ikhlas, ni Sunnah kila tunapoanza swala kabla ya kusoma Suratul-Fatiha tuseme:

إِنِّى وَجَّهْتُ وَجْهِىَ لِلَّذِى فَطَرَ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضَ حَنِيفًا ۖ وَمَآ
أَنَا۠ مِنَ ٱلْمُشْرِكِينَ ﴿٧٩﴾

*“Ninauelekeza uso wangu kwa yule aliyeziumba mbingu na ardhi, hali ya kuwa nimewacha dini za upotofu mimi (nimejisalimisha ni Muislamu na ) si miongoni mwa washirikina. (6:79)*

إِنَّ صَلَاتِي وَنُسُكِي وَمَحْيَايَ وَمَمَاتِي لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ
﴿١٦٢﴾ لَا شَرِيكَ لَهُ ۖ وَبِذَٰلِكَ أُمِرْتُ وَأَنَا أَوَّلُ الْمُسْلِمِينَ ﴿١٦٣﴾

*Hakika swala yangu, na ibada zangu (zote nyingine) na uzima wangu na kufa kwangu ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, Bwana wa walimwengu wote. Hana mshirika wake na kwa haya ndiyo niliyoamrishwa,na mimi ni wa kwanza wa waliojisalimisha. (6:162-163)*

### 4. Kujiepusha na Ria na Kujiona

Ria ni kinyume cha Ikhlas. Kufanya ria ni kufanya jambo jema ili watu wakuone, wakusifu, wakupe shukurani, n.k. Mtu anayefanya ria hafanyi wema kwa kutarajia malipo kutoka kwa Allah (s.w) bali hufanya kwa kutarajia malipo ya hapa duniani tu, iwe ni mali au sifa au shukurani.

Mwenye kufanya ria hata akijiita Muislamu hana malipo yoyote mbele ya Alllah(s.w) katika siku ya Hukumu isipokuwa adhabu kali Motoni kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:-

مَن كَانَ يُرِيدُ الْحَيَاةَ الدُّنْيَا وَزِينَتَهَا نُوَفِّ إِلَيْهِمْ أَعْمَالَهُمْ
فِيهَا وَهُمْ فِيهَا لَا يُبْخَسُونَ ﴿١٥﴾ أُولَٰئِكَ الَّذِينَ لَيْسَ لَهُمْ
فِي الْآخِرَةِ إِلَّا النَّارُ ۖ وَحَبِطَ مَا صَنَعُوا فِيهَا وَبَاطِلٌ مَّا
كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٦﴾

*“Wanaotaka maisha ya dunia na mapambo yake, tutawapa huku duniani (ujira wa) vitendo vyao kamili, humu wao hawatapunjwa. Hao ndio ambao hawatakuwa na kitu katika akhera ila moto na wataruka patupu waliyoyafanya katika dunia hii na yatakuwa bure waliyokuwa wakiyatenda.” (11:15-16)*

Katika aya nyingine Allah (s.w) anatukamia:

فَوَيْلٌ لِّلْمُصَلِّينَ ﴿٤﴾ الَّذِينَ هُمْ عَن صَلَاتِهِمْ سَاهُونَ ﴿٥﴾
الَّذِينَ هُمْ يُرَاءُونَ ﴿٦﴾

*"Basi adhabu (kali) itawathubutikia wanaoswali; ambao wanapuuza swala zao. Ambao hufanya riyaa". (107:4)*

Katika Hadith tunafahamishwa kuwa Mtume (s.a.w) amesema:

*"Katika siku ya hukumu, vitendo vyote vilivyofanywa hapa duniani vitahudhurishwa mbele ya Allah (s.w). Vitendo vilivyofanywa kwa ajili ya Allah (s.w) vitatengwa. Na vitendo vingine vilivyofanywa kwa nia nyingine mbali mbali vitatupwa motoni". (Baihaqi).*

## 5. Kuepuka Unafiki

Mnafiki ni yule anayeukubali Uislamu mdomoni (kwa kauli tu) lakini moyoni mwake na katika matendo yake anaukanusha. Wanafiki wanaainishwa vema katika aya zifuatayo:-

وَمِنَ ٱلنَّاسِ مَن يَقُولُ ءَامَنَّا بِٱللَّهِ وَبِٱلْيَوْمِ ٱلْءَاخِرِ وَمَا هُم بِمُؤْمِنِينَ ﴿٨﴾ يُخَـٰدِعُونَ ٱللَّهَ وَٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ وَمَا يَخْدَعُونَ إِلَّآ أَنفُسَهُمْ وَمَا يَشْعُرُونَ ﴿٩﴾

*"Na katika watu wako wasemao: Tumemuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho; na hali ya kuwa wao si wenye kuamini. Wanataka kumdanganya Allah na wale walioamini, lakini hawadanganyi ila nafsi zao, nao hawatambui." (2:8-9)*

Wanafiki pamoja na kuonyesha imani ya uwongo, ni maadui wakubwa wa Allah (s.w) na Mtume wake. Hushirikiana na Makafiri na Washirikina katika kuupiga vita Uislamu. Wao ni maadui wabaya zaidi kuliko makafiri na washirikina kwa sababu wao hutoa siri za ndani za Waislamu na kuwapelekea maadui wa Uislamu ili wapate kuuhilikisha Uislamu. Hivyo Allah (s.w) amewaahidi wanafiki kuwa watapata adhabu kali kama tunavyojifunza katika aya ifuatayo:

إِنَّ ٱلْمُنَـٰفِقِينَ فِى ٱلدَّرْكِ ٱلْأَسْفَلِ مِنَ ٱلنَّارِ وَلَن تَجِدَ لَهُمْ نَصِيرًا

*Bila shaka wanafiki watakuwa katika tabaka la chini kabisa katika moto. Hutamkuta kwa ajili yao msaidizi'. (4:145)*

Hakuna alama au nembo maalum zinazoonekana katika sura au viwili wili vya wanafiki, bali wanafiki wanatambulika kwa matendo

yao au mienendo yao. Mwenendo wa kinafiki au sifa za wanafiki zimebainishwa kwa uwazi katika Qur-an na Hadith Sahihi. Katika Qur'an Allah (s.w) amewaelelezea wanafiki katika aya zifuatazo:

*(2:8-20), (3:167-168), (4:60-63), (4:138-145), (9:43-68), (33:12-20), (57:13), (59:11-17), (63:1-8).*

Katika aya hizi tunajifunza kuwa wanafiki wamesifika kwa sifa zifuatazo:

1. Maneno ya wanafiki siku zote ni kinyume na matendo yao.
2. Wanafiki hujaribu kumdanganya Allah pamoja na Waislamu wakidhani kuwa yaliyo vifuani mwao hayajulikani.
3. Siku zote wanafiki hufanya ufisadi huku wakidai kuwa wanatenda wema (wanatengeneza).
4. Huwaona waumini wa kweli kuwa ni wajinga kwa kufuata kwao Uislamu inavyotakikana.
5. Huwacheza shere Waislamu.
6. Wanafiki huyapenda zaidi maisha ya dunia kuliko ya akhera.
7. Hawapendi kuhukumiwa na sheria ya Allah (s.w).
8. Hutumia viapo kama kifuniko cha maovu yao.
9. Huwafanya makafiri na washirikina kuwa ndio marafiki zao wa ndani badala ya Allah na Mtume wake na waislamu.
10. Hujaribu kushika njia ya katikati baina ya Uislamu na Ukafiri, hivyo huyumba yumba baina ya Uislamu na Ukafiri.
11. Huenda kuswali kwa uvivu.
12. Hawamkumbuki Allah(s.w) ila kwa kidogo sana.
13. Huwafitinisha Waislamu.
14. Huchukia Waislamu wanapofikwa na kheri na hufurahi wanapofikwa na msiba.
15. Hawako tayari kutoa mali zao katika njia ya Allah na wakitoa chochote hutoa kwa ria.
16. Mara nyingi huzifanyia shere aya za Qur-an.
17. Huamrisha maovu na kukataza mema.
18. Ni wenye kutapatapa wakati wa matatizo na humdhania vibaya Allah na Mtume wake.
19. Husema uongo na hawatekelezi ahadi.
20. Hujitahidi kuwavunja moyo Waislamu wa kweli ili wabakie katika ukafiri sawa na wao.

21. Hufanya hiyana katika mambo ya kheri na huchagua mambo mepesi mepesi yenye kuwafurahisha.
22. Wanawaogopa na hukaa upande mmoja na maadui wa Uislamu na Waislamu.
23. Hupenda kusifiwa kwa kazi nzuri zilizofanywa na wengine.
24. Huchochea fitna baina ya Waislamu, n.k.

Hizi ndizo sifa za wanafiki kama zilivyobainishwa katika Qur-an. Kwa muhtasari, Mtume (s.a.w) anatufahamisha sifa za wanafiki kama tunavyojifunza katika Hadith ifuatazo:

*Mtume (s.a.w) amesema: Mambo manne akiwanayo mtu humfanya awe mnafiki wa wazi hata kama anaswali, anafunga na anadai kuwa ni Muumini,. Anayesema uwongo kila anapoongea, anayevunja ahadi kila anapo ahidi, anayehini amana kila anapoaminiwa, na anayechupa mipaka kila unapotokea ugomvi. (Bukhari)*

Muislamu wa kweli hana budi kujiepusha na unafiki kwa kujinasua na tabia za wanafiki.

## 6. Kuwa Mkweli

Ukweli ni uhakika wa jambo. Muislamu wa kweli hana budi kuwa mkweli na kusimamia ukweli. Allah (s.w) anatuamrisha tuwe wakweli katika kuendesha shughuli zetu zote.

يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ ٱتَّقُوا۟ ٱللَّهَ وَكُونُوا۟ مَعَ ٱلصَّـٰدِقِينَ ﴿١١٩﴾

*"Enyi mlioamini Mcheni Mwenyezi Mungu na kuweni pamoja na wakweli." (9:119).*

Msema kweli ni mpenzi wa Allah (s.w) . Naye Allah (s.w) amewaandalia wakweli ujira mzuri kabisa kwa hapa duniani na huko akhera kama tunavyobainishiwa katika Qur-an" kuwa Allah (s.w) atasema katika hiyo siku ya hisabu:-

هَـٰذَا يَوْمُ يَنفَعُ ٱلصَّـٰدِقِينَ صِدْقُهُمْ ۚ لَهُمْ جَنَّـٰتٌ تَجْرِى
مِن تَحْتِهَا ٱلْأَنْهَـٰرُ خَـٰلِدِينَ فِيهَآ أَبَدًا ۚ رَّضِىَ ٱللَّهُ عَنْهُمْ وَرَ
ضُوا۟ عَنْهُ ۚ ذَٰلِكَ ٱلْفَوْزُ ٱلْعَظِيمُ ﴿١١٩﴾

*"Hii ndiyo siku ambayo wakweli utawafaa ukweli wao.Wao watapata bustani zipitazo mbele yake mito. Humo watakaa milele. Allah amewawia radhi nao wanaradhi naye. Huku ndiko kufaulu kukubwa. (5:119)*

وَٱلصَّـٰدِقِينَ وَٱلصَّـٰدِقَـٰتِ • • أَعَدَّ ٱللَّهُ لَهُم مَّغْفِرَةً وَأَجْرًا عَظِيمًا ﴿٣٥﴾

*"... Na wanaume wasemao kweli na wanawake wasemao kweli... Allah amewaandalia msamaha na ujira mkubwa". (33:35).*

Msisitizo wa Muislamu kujipamba na tabia ya kuwa mkweli pia tunaupata katika Hadith ifuatayo:

*'Abdullah bin Mas'ud (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: Utaongea ukweli kwa sababu ukweli unaongoza kwenye Ucha-Mungu na Ucha-Mungu unaongoza kwenye Pepo. Mja ataendelea kusema kweli na kubakia katika ukweli mpaka aorodheshwe mbele ya Allah kuwa ni miongoni mwa wakweli wakubwa.Tahadharini na uwongo! Uwongo unaongoza kwenye uasi na uasi unaongoza kwenye Moto.Mja ataendelea kusema uwongo na kubakia katika uwongo mpaka aorodheshwe mbele ya Allah kuwa ni miongoni mwa waongo wakubwa".*
*(Bukhari na Muslim).*

## 7. Kujiepusha na Uwongo

Uwongo ni kinyume cha ukweli. Uwongo ni giza na ukweli ni nuru. Uwongo ni upotofu na ukweli ni uongofu. Ambapo ukweli ni uhakika wa asili wenye kudumu, uwongo ni uzushi ambao hutoweka mara tu ukweli unaposimama.

وَقُلْ جَآءَ ٱلْحَقُّ وَزَهَقَ ٱلْبَـٰطِلُ ۚ إِنَّ ٱلْبَـٰطِلَ كَانَ زَهُوقًا ﴿٨١﴾

*"Na sema: Ukweli umefika na uwongo (batwili) umetoweka. Hakika uwongo ndio wenye kutoweka." (17:81)*

Uongo ni uovu wenye kumuangamiza mja hapa duniani na huko akhera. Aidha uwongo ni miongoni mwa maovu makubwa mbele ya Allah (s.w) kama inavyobainika katika Hadith zifuatazo:

*Abubakar (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: Nikufahamisheni juu ya madhambi makubwa katika madhambi*

*makubwa? Sikia! Ni kumshirikisha Allah (s.w), kutotii wazazi na kusema uwongo". (Bukhari na Muslim).*

Katika Hadithi nyingine tunafahamishwa:
*Abubakar (r.a) anasimulia kuwa Mtume wa Allah aliuliza: "Je, nikufahamisheni madhambi makubwa?" Aliuliza swali hilo mara tatu. Tukamjibu: "Kwa nini usitufahamishe, Ee Mtume wa Allah?" Akaeleza "Ni kumshirikisha yeyote na Allah (s.w)."Na kusema uwongo na kutoa ushahidi wa uwongo. "Aliendelea kurudia hili mpaka tukaanza kujishauri, kuwa ingelikuwa vyema kama tusingelimuuliza." (Bukhari)*

Mtume (s.a.w) ametukataza kusema uwongo hata katika mazungumzo ya utani. Mtume (s.a.w) alitoa makemeo makali kama ifuatavyo:

*Kuna Kifo kwa mtu anayejihusisha na simulizi za uwongo ili kuchekesha watu na kuna kifo kwake, kuna kuangamia kwake. (Tirmidh).*

Katika Hadith nyingine Mtume (s.a.w) amesema:
*Muumini hataweza kuikamilisha imani yake mpaka aache kusema uwongo katika utani na katika midahalo hata kama ni mkweli katika mambo yote mengine. (Ahmad)*

Pia katika Hadith nyingine Mtume (saw) aliulizwa;
*Kuwa Muislamu anaweza kuwa mwoga. Akajibu "Ndiyo". Akauliza tena, " Je, Muislamu anaweza kuwa bakhili?" akajibu, "Ndiyo, anaweza kuwa bakhili." Aliuliza tena, "Je, Muumini anaweza kuwa mwongo?" Alijibu, "Hapana". (Malik)*

Ieleweke kuwa si kwamba maovu mengine yaliyotajwa katika Hadith hii yanaruhusika, bali maovu hayo baada ya kuyafanya muislamu anaweza kutanabahi na kurejea kwa mola wake kwa kuleta toba ya kweli na toba ya kweli haipatikani mpaka awe mkweli katika kukiri makosa yake. Kwa mujibu wa Hadith, *Mwongo* si **Muumin**i bali **Mnafiki.**

Mtume (saw) pia anatutahadharisha tujiepushe na kuwabembeleza watoto kwa kuwadanganya kuwa tutawapa zawadi fulani. Mtume(saw) anasisitiza kuwa ukimwahidi mtoto zawadi hunabudi kumletea zawadi hiyo. Tukiwadanganya watoto hao kwamba tutawapa kitu na tusiwape, tutakuwa tunawafundisha uwongo.

### Uwongo na Ulaghai katika Biashara

Waislamu wa kweli hawanabudi kuwa wakweli katika kila kipengele

cha maisha yao. Imekuwa kawaida kwa wafanyabiashara waliowengi kutumia udanganyifu na ulaghai katika biashara ili kujipatia faida kubwa. Wafanyabiashara wasio waadilifu mara nyingi huwapunja watu kutokana na kutojua kwao bei halisi za vitu, hasa wanunuzi wanapokuwa wageni wa sehemu ile. Pia baadhi ya wafanyabiashara huchanganya bidhaa mbovu na nzuri au kuficha dosari (upogo) ya bidhaa na kuiuza kwa bei ya bidhaa nzima. Na baadhi ya wafanyabiashara hutumia viapo vya uwongo ili kuwahadaa watu wanunue bidhaa zao. Huu wote ni udanganyifu katika biashara. Biashara ya namna hii ni biashara haramu kama Mtume (saw) anavyotufahamisha :

*" Si halali kwa Muislamu kuuza bidhaa yenye dosari, mpaka azioneshe dosari hiyo kwa mnunuzi." (Bukhari)*

*"…Kiapo cha uwongo kitasaidia biashara inunuliwe , lakini inapunguza mapato".(Ahmad)*

## Ni wapi uwongo unaporuhusiwa?

Katika maisha ya kila siku kuna sehemu **tatu** tu ambapo uwongo unaruhusiwa. Ni katika vita, katika kuleta suluhu na katika maongezi ya kusuluhishana kati ya mume na mkewe au mke na mumewe kama tunavyojifunza katika hadith zifuatazo:-

*Asma bint Yazid (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah (saw) amesema: Uwongo si halali ila katika mambo matatu; uwongo wa mume kwa mkewe (au wa mke kwa mumewe) ili kumfurahisha; uwongo katika vita na uwongo katika kusuluhisha au kuleta amani kati ya watu". (Ahmad, Tirmidh).*

*Ummu Kulthumu bint U'qubah (r.a) amesema, Sikumsikia Mtume wa Allah (saw) akitoa ruhusa ya kusema uwongo juu ya chochote watu wanachosema ila katika mambo matatu:- vita, kurudisha amani kati ya watu (kusuluhisha) na mazungumzo ya mume kwa mkewe au ya mke kwa mumewe". (Muslim)*

Hivyo, Muislamu wa kweli analazimika kuwa mkweli katika mazungumzo, katika mahusiano yake ya wengine na katika utendaji wake wa kila siku katika kila kipengele cha maisha yake. Atakuwa mkweli katika mazungumzo ya kawaida, katika uchumi, siasa , familia,

n.k. Pia ukweli kwa muumini ni lazima upatikane katika dhamira, msimamo na utii.

### 8. Kuwa Muaminifu (Kuchunga Amana)

Uaminifu ni uchungaji wa amana. Amana ni kitu chochote halali mtu alichokabidhiwa ili akihifadhi na kukirudisha kwa mwenyewe atakapokihitaji au ili akitumie inavyostahiki au akifikishe mahali palipokusudiwa. Mali uliyokabidhiwa na mtu au umma ni amana; uongozi au cheo ulichopewa na jamii ni amana.

Amana kuu aliyotunukiwa Binadamu na Mola wake Ni roho, vipaji au vipawa vyote alivyonavyo na neema zote za Allah(sw) zilizomzunguka. Binadamu ametunukiwa vitu hivi ili aweze kumuabudu Mola wake inavyostahiki na kuwa **Khalifa** wetu katika ardhi. Amana hii kuu anaibainisha Allah (sw) katika aya ifuatayo:

إِنَّا عَرَضْنَا ٱلْأَمَانَةَ عَلَى ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ وَٱلْجِبَالِ فَأَبَيْنَ أَن يَحْمِلْنَهَا
وَأَشْفَقْنَ مِنْهَا وَحَمَلَهَا ٱلْإِنسَٰنُ ۖ إِنَّهُۥ كَانَ ظَلُومًا جَهُولًا ﴿٧٢﴾

*"Kwa yakini sisi tulidhihirisha **amana** juu ya **mbigu** na **ardhi** na **milima** (majabali) vikakataa kuichukua na vikaiogopa lakini mwanadamu akaichukua. Bila shaka yeye ni dhalimu mkubwa, mjinga sana." (33:72)*

Amana iliyokataliwa na kuogopewa na **mbingu, ardhi** na **milima** (ya majabali) si nyingine bali amana ya kuwa **Khalifa** wa Allah(sw) kuongoza ulimwengu kwa kufuata kanuni na sheria zake.

Hivyo kila mwenye akili hanabudi kuwa na yakini kuwa chochote alicho nacho ni amana kutoka kwa mola wake Muumba ili aitumie katika kumuabudu ipasavyo na kusimamisha ukhalifa katika jamii. Allah (sw) anatukumbusha mara kwa mara juu ya amana hii na kutuamuru:

قُلْ إِنَّ صَلَاتِى وَنُسُكِى وَمَحْيَاىَ وَمَمَاتِى لِلَّهِ رَبِّ ٱلْعَٰلَمِينَ ﴿١٦٢﴾
لَا شَرِيكَ لَهُۥ ۖ وَبِذَٰلِكَ أُمِرْتُ وَأَنَا۠ أَوَّلُ ٱلْمُسْلِمِينَ ﴿١٦٣﴾

*"Sema: Hakika swala yangu, na matendo yangu (ibada zangu) na uzima*

*wangu na kufa kwangu ni kwa ajili ya Allah. Hana mshirika wake. Na haya andiyo niliyoamrishwa, na mimi ni wa kwanza wa waliojisalimisha". (6:162-163).*

Muislamu wakweli anatakiwa awe na msimamo huu. Awe na yakini kuwa kila alichonacho ni cha Allah (s.w)na analazimika kukitumia kwa ajili yake tu. Kinyume cha hivyo ni kumfanyia khiana Allah (s.w) na Mtume wake. Tunaonywa katika Qur-an:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ لَا تَخُونُواْ ٱللَّهَ وَٱلرَّسُولَ وَتَخُونُوٓاْ
أَمَٰنَٰتِكُمۡ وَأَنتُمۡ تَعۡلَمُونَ ﴿٢٧﴾ وَٱعۡلَمُوٓاْ أَنَّمَآ أَمۡوَٰلُكُمۡ وَأَوۡ
لَٰدُكُمۡ فِتۡنَةٞ وَأَنَّ ٱللَّهَ عِندَهُۥٓ أَجۡرٌ عَظِيمٞ ﴿٢٨﴾

*"Enyi mlioamini! Msimfanyie khiana Allah na Mtume wala msikhini amana zenu na hali mnajua. Na jueni ya kwamba mali zenu na watoto ni mtihani na jueni ya kwamba kwa Mwenyezi Mungu yapo malipo makubwa. (8:27-28).*

قَدۡ أَفۡلَحَ ٱلۡمُؤۡمِنُونَ ﴿١﴾ وَٱلَّذِينَ هُمۡ لِأَمَٰنَٰتِهِمۡ وَعَهۡدِهِمۡ
رَٰعُونَ ﴿٨﴾

*"Hakika wamefuzu waumini.... Ambao amana zao na ahadi zao wanaziangalia" (23:1, 8)*

Kutokana na uzito wake hebu tuangalie amana katika upeo mpana katika utendaji wetu wa kila siku .

**Uongozi wa aina yoyote ni amana** na Muislam anahimizwa achunge amana hiyo ndio Uislam wake ukamilike. Mtume (saw) amesema:

*"Kila mmoja wenu ni mchunga na ataulizwa juu ya wale au vile alivyokuwa akivichunga. Imamu (kiongozi) ni mchunga. Ataulizwa juu ya wale aliokuwa akiwaongoza . mwanamume ni mwangalizi wa watu wa nyumbani kwake. Ataulizwa juu yao. Mke ni mwangalizi wa nyumba ya mumewe. Ataulizwa juu ya jukumu hili. Mtumishi (mfanyakazi) ni mwangalizi wa vitu au mali ya mwajiri wake . Ataulizwa juu ya jukumu hili".*

### Madaraka ni Amana

Pamoja na amana hii ya uongozi aliyonayo kila mtu kutokana na nafasi yake ya asili katika jamii kuna amana nyingine ambazo hukabidhiwa na jamii kwa watu kulingana na uwezo wao. Kazi na majukumu ni lazima vigawanywe kulingana na uwezo wa kila mtu ili kila mtu achunge amana yake. Kumpa mtu kazi au madaraka asiyo na uwezo nayo ni kumuingiza kwenye mtihani na wenye kumchagua watakuwa ni wenye kuulizwa juu ya kushindwa kwake. Halikadhalika mtu kujipachika mwenyewe madaraka au kuomba madaraka au kazi asiyo na uwezo nayo ni kujiingiza katika kujifelisha mtihani kwa ushahidi wa hadith ifuatayo;

*Abu-Dhar (r.a) amesimulia kuwa alimuomba Mtume (saw) amchague kuwa Gavana wa nchi fulani. Mtume (saw) kusikia ombi hili alitingisha bega lake na akasema:Ee Abu-Dhar! Wewe ni dhaifu na madaraka haya ni amana. Siku ya kiyama hili litakuwa ndio chanzo cha aibu na fedheha. Lakini watasalimika wale watakao chukua madaraka hayo (kazi hiyo) na wakayaendesha kama inavyostahiki. (Muslim)*

Katika Uislamu, si ujuzi na uzoefu wa kazi tu vinavyoangaliwa katika kumvisha mtu amana ya kazi au madaraka Fulani, bali hapana budi viambatane na tabia nzuri na uaminifu. Halikadhalika tabia nzuri na ucha-mungu havitatosha kumfanya mtu achaguliwe kufanya kazi fulani, bila ya kuwa na ujuzi na uzoefu unaostahiki. Mfano mzuri tunaupata kwa Nabii Yusuf (a.s) yeye alikuwa Mtume wa Allah(sw) na kwa hiyo alikuwa mfano bora wa tabia njema na ucha-mungu. Lakini hakujitolea kuchukua dhima ya kuendesha nchi kwa misingi ya tabia njema na utume wake tu bali pia kwa msingi wa ujuzi juu ya wadhifa huo kama tunavyofahamishwa katika aya ifuatayo:

قَالَ ٱجْعَلْنِى عَلَىٰ خَزَآئِنِ ٱلْأَرْضِ ۖ إِنِّى حَفِيظٌ عَلِيمٌ ﴿٥٥﴾

*Akasema(Yusuf):"Nifanye mtazamaji wa khazina za nchi (yote) hakika mimi ni mlinzi mzuri na mjuzi hodari". (12:55)*

### Uchaguzi ni Amana

Tunatakiwa tuwe waaminifu katika kuwachagua watu kuchukuwa nafasi za kazi katika nyadhifa mbali mbali. Tuwachague kutokana na ujuzi wao, uzoefu wao, tabia yao, na uaminifu wao. Kama kutokana na hongo , udugu, unafiki, ukabila au upendeleo wa namna

yoyote, tutaacha kufuata utaratibu wa kumchagua mtu kulingana na sifa zinazostahiki kwa kazi fulani na badala yake tukawachagua wasiostahiki, tutakuwa moja kwa moja tumekhini(tumefanya khiyana). Mtume (saw) amesema kuwa:

*Atakaye mchagua kiongozi kwa upendeleo ambapo palikuwa na mtu mwingine ambaye alistahiki zaidi mbele ya Allah kuliko yule aliyemchagua, basi atakuwa amemfanyia khiana Allah, Mtume wake na waislamu wote. (Hakim)*

**Kazi ni Amana**

Pamoja na kuwa waaminifu katika kuwachagua watu kwa nyadhifa na kazi mbalimbali, waliochaguliwa nao wanatakiwa wawe waaminifu katika kutekeleza kazi. Muislamu analazimika kuifanya kila kazi yake kwa ufanisi na kila mara ajitahidi kuifanya vizuri zaidi.

Inafahamika wazi kuwa uzembe katika kazi huleta madhara mengi katika jamii. Kutokana na kukosekana uaminifu katika kutekeleza majukumu mbali mbali katika jamii huzaa magonjwa mengi ambayo hudhoofisha jamii. Magonjwa haya ni wizi, hongo, upendeleo, n.k. Uzembe na ulaghai katika kazi vimeshutumiwa vikali katika Uislamu kama inavyobainishwa na hadith zifuatazo:

*Mtume wa Allah amesema: "katika siku ya Hukumu wakati Allah (sw) atakapokusanya watu wote, waliopita na wasasa, bendera itakitwa kwa kila Mlaghai (mdanganyifu) ambayo itamtambulisha. Kisha itanadiwa kuwa hili ni kundi la wadanganyifu". (Bukhari)*

Katika hadith nyingine Mtume (saw) amesema:
*Patakuwa na bendera katika kila kichwa cha mdanganyifu itakayoinuliwa kulingana na udanganyifu wake . Sikilizeni! Hapana ulaghai au udanganyifu mkubwa kuliko ule wa Amir (Kiongozi) anayedanganya watu (ummah). (Muslim)*

Kwa maana nyingine hapatakuwa na mdanganyifu mkubwa zaidi anayestahiki kupata adhabu kali zaidi mbele ya Allah (sw) kuliko yule alipewa madaraka kuangalia mambo ya watu katika jamii halafu akawa amelala usingizi wa kukoroma (anastarehe) bila ya kujali matatizo yaliyowaelemea.

## Mali ya Umma ni Amana

Uaminifu ni pamoja na kutochukua kitu cha mtu binafsi au kitu cha ummah pasina idhini ya wenyewe. Kuchukua mali ya mtu au mali ya umma na kuwapa wengine pasi na idhini au kuifanyia shughuli isiyopendelewa na mwenye mali ni hiana au ukosefu wa uaminifu. Hata kuchukua malipo zaidi kuliko mahitaji ya mtu ya lazima ni kufanya khiana. Kuhusu jambo hili Mtume (saw) amesema:

*Yeyote yule tutakaye mpa shughuli, upatikanaji wa mahitaji yake itakuwa ni jukumu letu pia, kama utachukuwa zaidi kuliko mahitaji yake basi atakuwa anakhini.* (Abu Daud)

Hapa tunapata fundisho kuwa katika Uislam watu watakao ajiriwa na umma kutoa huduma mbali mbali watastahiki kulipwa mishahara itakayowawezesha kutosheleza mahitaji yao. Atakayepokea mshahara zaidi ya mahitaji yake bila ya kujali wadhifa wake na cheo chake atakuwa amekhini mali ya Ummah. Atakuwa amekhini kwa sababu atakuwa ametumia mali ya ummah ambayo ilitakiwa wapewe wanaohitajia zaidi, kama vile maskini,mafakiri, mayatima, wasafiri walioharibikiwa katika njia ya Allah, n.k. tunaonywa katika Qur'an:

وَمَا كَانَ لِنَبِيٍّ أَن يَغُلَّ ۚ وَمَن يَغْلُلْ يَأْتِ بِمَا غَلَّ يَوْمَ الْقِيَامَةِ ۚ ثُمَّ تُوَفَّىٰ كُلُّ
نَفْسٍ مَّا كَسَبَتْ وَهُمْ لَا يُظْلَمُونَ ١٦١

*"Na hiana kwa nabii kufanya khiyana atakayefanya khiana, atavileta siku ya kiyama alivyovifanyia khiana, kisha kila mtu atalipwa kwa aliyoyachuma, wala hawatadhulumiwa".* (3: 161)

Ni kawaida kuwa watu wengi hudharau au hulichukulia kwa wepesi suala la uaminifu katika mali ya ummah. Kinyume chake Uislamu umelipa uzito sana suala hili. Uislamu umeharamisha unyonyaji wa mali ya ummah hata kwa mali iliyo ndogo kiasi gani. Msisitizo wa ubaya wa kuhini (mis-appropriate) mali ya ummah, ambao hufunga njia zote za kujipatia mali kwa njia za haramu, uko wazi katika Hadith zifuatazo:

*Adi bin Umaira (r.a) amesimulia kuwa amemsikia Mtume (saw) akisema: "Yeyote yule tutakayempa madaraka na akawa ameficha sindano au kitu kidogo kuliko hiki, basi atakuwa amekikhini na atatokea nacho siku ya Kiyama"*

*Pale pale aliinuka Ansar mweusi akasema:"Ee Mtume wa Allah! Nivue madaraka (nijiuzulu) ya Ugavana." Mtume alimuuliza kuwa kuna nini? Akajibu (Ansar): " Nimesikia yote uliyozungumza sasa hivi". Mtume(saw) akasema; "Bado ninasema kuwa yeyote yule tutakayemfanya gavana hana budi kutuonyesha kila kitu (katika mali ya ummah). Achukuwe chochote kile kilicho haki yake na akiweke pembeni chochote kile alichoambiwa akitunze". (Muslim).*

Katika hadith nyingine, mtu mmoja aliyeitwa Ibn Labtih kutoka kabila la Uzd alitumwa na Mtume (saw) kama kiongozi wa kukusanya zakat na sadaqa. Aliporudi na alivyokusanya alisema; "Hivi ndivyo vitu vyenu na hivi nimepewa zawadi ". Msimulizi wa Hadith hii anasema aliposikia habari hii Mtume (saw) alisimama na kumhimidi Allah kisha akasema;

*...Ninamchagua miongoni mwenu kiongozi wa mambo haya ambayo Allah (sw) amenipa majukumu nayo. Wakati mtu huyo anaporudi, anasema hiki ni chetu na hiki nimepewa zawadi. Kama anasema kweli kwa nini asingelibakia nyumbani kwa wazazi wake. Hebu tuangalie hasa niwapi zawadi hii imetoka? Kwa jina la Allah, kama yeyote miongoni mwenu anapokea kitu chochote kisichomstahiki, siku ya Kiyama atatokea mbele ya Allah(s.w) akiwa amebeba kitu hicho. Sitaki kumwona yeyote yule miongoni mwenu, akutane na Allah (sw) akiwa amebeba ngamia kichwani mwake au ngombe au mbuzi wakilia kichwani mwake na akasema;*

*"Ee Allah! Nimefikisha ujumbe wako". (Muslim).*

**Siri ni Amana**

Kutoa siri za watu, kikundi au nchi ni ukosefu wa uaminifu wa hali ya juu. Ufujaji wa siri huharibu mipango yote ya kheri iliyokusudiwa kufanywa. Ufujaji wa siri huvunja ushirikiano, uhusiano na urafiki kati ya watu. Mtume (saw)amesema;

*Wakati mtu anapomwambia mwingine jambo kisha akamgeukia (akamwambia kuwa ni siri), basi hiyo ni amana.*

Uislamu unasisitiza sana kuwa mambo yote ya siri yaliyoongelewa kwenye mkutano wowote usioenda kinyume na maadili ya Uislamu ni lazima yachungwe. Hapana siri kwa mikutano inayojadiliana kutenda maovu. Muislamu akitokea kuhudhuria

mikutano ya kujadili mambo ya uovu huo. Kuhusu siri za mikutano Mtume (saw) amesema:

*Siri ya mikutano ni amana, lakini mikutano ya aina tatu haitajuzu kutunziwa siri; ule ambao damu inamwagwa bila haki; ule ambao unahusiana na uzinifu; au ule ambao mali inaporwa. (Abu Daud).*

Siri za ndani ya nyumba haziruhusiwi kabisa kutolewa nje, hata jirani au rafiki wa karibu sana hatakiwi akafahamu. Na siri za mke na mume zinatakiwa ziishie chumbani. Mtume (saw) amesema:

*Katika siku ya Hukumu, jambo litakalo kuwa la uhaini mkubwa kuliko yote mbele ya Allah (sw) ni mume kutoa siri ya mkewe kwa wengine, hata kama mume atakuwa anampenda mkewe na mkewe akawa anampenda mumewe. (Muslim).*

Muislamu wa kweli ni lazima awe ni mwenye kuaminika pindi anapoaminiwa kwa kupewa amana yeyote ile iwe ni *mali, madaraka, heshima, siri, n.k.* Kama anavyotuhakikishia Mtume (saw) katika hadith;

Mfano mzuri wa uchungaji wa amana ni ule aliouonesha Mtume (saw) katika kipindi kigumu cha mabadiliko muhimu ya historia ya ulimwengu. Tunafahamu kuwa Mtume(saw) alikuwa mwaminifu mno mpaka akapewa jina la Al-Amiin (mwaminifu) kwa kiasi ambacho hata wale waliokuwa wakimpiga vita walikuwa wakiweka amana zao kwake. Safari ya kuhamia Madina ilipowadia na wakati maisha yake yalipokuwa hatarini (kwani njama za kumuua zilishatimia), Mtume (saw) hakusahau amana za watu alizokuwa nazo pamoja na kwamba watu hao hao ndio maadui zake. Akambakiza Ali(r.a) ili kuwarudishia wenyewe amana zao ndipo afunge safari kumfuata Mtume na masahaba wengine Madina. Leo hii Muislamu akikhini amana ya mtu atakuwa na kisingizio gani? Madhambi yote husameheka mbele ya Allah isipokuwa kufa na dhambi ya shirk na kukhini amana ya mtu. Siku ya Kiama ni lazima amana hiyo irejeshwe kwa mwenyewe. Kila Muislamu wa kweli hana budi Kumuiga Mtume (saw) na kuwa Amiin (mwaminifu) katika maisha yake yote.

### 9. Kuwa Muadilifu

Uadilifu ni usimamizi wa ukweli na kutoa haki kwa kila anayestahiki kulingana na ukweli. Allah (s.w) ametuamrisha kuwa waadilifu kama ifuatavyo:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ كُونُوا۟ قَوَّٰمِينَ بِٱلْقِسْطِ شُهَدَآءَ لِلَّهِ وَلَوْ
عَلَىٰٓ أَنفُسِكُمْ أَوِ ٱلْوَٰلِدَيْنِ وَٱلْأَقْرَبِينَ ۚ إِن يَكُنْ غَنِيًّا أَوْ فَقِيرًا
فَٱللَّهُ أَوْلَىٰ بِهِمَا ۖ فَلَا تَتَّبِعُوا۟ ٱلْهَوَىٰٓ أَن تَعْدِلُوا۟ ۚ

*Enyi mlioamini! Kuweni wenye kusimamia uadilifu, mtoao ushahidi kwa ajili ya Allah ijapokuwa ni juu ya nafsi zenu au wazazi au jamaa, akiwa tajiri au maskini, Mwenyezi Mungu anawastahiki zaidi. Basi msifuate matamanio mkaacha kufanya uadilifu. (4:135).*

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ كُونُوا۟ قَوَّٰمِينَ لِلَّهِ شُهَدَآءَ بِٱلْقِسْطِ ۖ وَلَا
يَجْرِمَنَّكُمْ شَنَـَٔانُ قَوْمٍ عَلَىٰٓ أَلَّا تَعْدِلُوا۟ ۚ ٱعْدِلُوا۟ هُوَ أَقْرَبُ
لِلتَّقْوَىٰ ۖ وَٱتَّقُوا۟ ٱللَّهَ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ خَبِيرٌۢ بِمَا تَعْمَلُونَ ﴿٨﴾

*Enyi mlioamini! Kuweni wasimamizi kwa ajili ya Allah, muwe mkitoa ushahida kwa uadilifu. Wala kuchukiana na watu kusikupelekeeni kutowafanyia uadilifu. Fanyeni uadilifu, kufanya hivyo huwafanya kuwa wacha mungu. Na Mcheni Allah. Hakika Allah anajua mnayoyatenda (5:8)*

## 10. Kuchunga Ahadi

Kuchunga au kutekeleza ahadi ni miongoni mwa vipengele muhimu vya tabia ya muumini wa kweli. Utekelezaji wa ahadi pia ni matunda ya ukweli na uaminifu. Mtu mkweli na mwaminifu ni lazima awe ni mwenye kutekeleza ahadi. Tumeona katika hadith kuwa ukosefu wa uaminifu, uwongo na uvunjaji wa ahadi ni alama kuu tatu za unafiki.

Muislam hana budi kujizatiti katika kutekeleza ahadi zote alizozitoa katika kutekeleza mambo mema. Muislamu akiahidi kutekeleza jambo jema au akiapa kufanya jambo fulani jema analazimika kutekeleza ahadi hiyo au kiapo hicho. Ama kiapo au ahadi ya kufanya mambo maovu si jambo lililosahihi mbele ya Allah(sw). Kwa hiyo ahadi au kiapo cha kufanya mambo yaliyokinyume na sharia ya Allah (sw) si ahadi au kiapo kinacho tambulika mbele ya Allah na atakapodhihirika kuwa ahadi yake au kiapo chake kilikuwa nicha kutenda maovu akivunje

mara moja. Vinginevyo kila ahadi njema ni lazima itekelezwe na kuna adhabu kali mbele ya Allah kwa wavunjao ahadi. Hebu tuone msisitizo wa Allah (s.w) juu ya utekelezaji wa ahadi:

.... وَأَوْفُوا۟ بِٱلْعَهْدِ ۖ إِنَّ ٱلْعَهْدَ كَانَ مَسْـُٔولًا ﴿٣٤﴾

*"...Na timizeni ahadi. Kwa hakika ahadi itaulizwa (siku ya Kiyama). (17:34)*

وَأَوْفُوا۟ بِعَهْدِ ٱللَّهِ إِذَا عَـٰهَدتُّمْ وَلَا تَنقُضُوا۟ ٱلْأَيْمَـٰنَ بَعْدَ تَوْكِيدِهَا
وَقَدْ جَعَلْتُمُ ٱللَّهَ عَلَيْكُمْ كَفِيلًا ۚ إِنَّ ٱللَّهَ يَعْلَمُ مَا تَفْعَلُونَ ﴿٩١﴾

*"Na timizeni ahadi mnazozitoa kwa jina la Mwenyezi Mungu mnapoahidi, wala msivunje hizo ahadi baada ya kuzithubutisha , hali mume kweisha mfanya Mwenyezi Mungu kuwa shahidi kwenu. Hakika Mwenyezi Mungu anayajua yote mnayoyafanya. (16:91)*

فَبِمَا نَقْضِهِم مِّيثَـٰقَهُمْ لَعَنَّـٰهُمْ وَجَعَلْنَا قُلُوبَهُمْ قَـٰسِيَةً ۖ

*"Basi kwa sababu ya kuvunja kwao ahadi yao, tuliwalaani na tukazifanya nyoyo zao kuwa ngumu. (5:13)*

Aya hizi zinatosha kutuonesha umuhimu wa kuchunga ahadi katika Uislamu. Aya zinabainisha kuwa utekelezaji wa ahadi ni amri kama amri nyingine za Allah (sw) ambazo mja akizitekeleza hupata mafanikio mema hapa duniani na malipo makubwa humngojea huko akhera na akizivunja huhasirika katika maisha yake hapa duniani na huko akhera. Tunafahamishwa pia katika Qur'an kuwa miongoni mwa watu wema watakaofuzu mbele ya Allah ni wale watekelezao ahadi zao kama tunavyohamiswa katika aya zifuatazo:

قَدْ أَفْلَحَ ٱلْمُؤْمِنُونَ ﴿١﴾ ... وَٱلَّذِينَ هُمْ لِأَمَـٰنَـٰتِهِمْ وَعَهْدِهِمْ
رَٰعُونَ ﴿٨﴾

*"Hakika wamefuzu Waislamu...ambao amana zao na ahadi zao wanaziangalia (wanazitekeleza). (23:1,8)*

.... وَٱلْمُوفُونَ بِعَهْدِهِمْ إِذَا عَـٰهَدُوا۟ ۖ

*Wema ni (wale)… watekelezao ahadi zao wanapo ahidi. (2:177)*

Pia Uislamu unaitazama ahadi kwa upeo mpana zaidi kuliko ahadi za kawaida tunazotoa kwa wanaadamu wenzetu.

**Ahadi kuu** tunayoitoa mbele ya Allah (s.w) ni kuwa tutamuabudu na kumtegemea yeye pekee. Ahadi hii ameitoa kila mtu hata kabla ya kuja hapa duniani kama tunavyojifunza katika Qur-an:

وَإِذْ أَخَذَ رَبُّكَ مِنۢ بَنِىٓ ءَادَمَ مِن ظُهُورِهِمْ ذُرِّيَّتَهُمْ وَأَشْهَدَهُمْ عَلَىٰٓ أَنفُسِهِمْ أَلَسْتُ بِرَبِّكُمْ ۖ قَالُوا۟ بَلَىٰ ۛ شَهِدْنَآ ۛ أَن تَقُولُوا۟ يَوْمَ ٱلْقِيَٰمَةِ إِنَّا كُنَّا عَنْ هَٰذَا غَٰفِلِينَ ﴿١٧٢﴾

*"Na kumbuka Mola wako alipowaleta katika wanaadamu miongoni mwao kizazi chao na kuwashuhudisha juu ya nafsi zao (akawaambia): Je, mimi siye Mola wenu? Wakasema: Ndiye, tunashuhudia.(Akawaambia) "Msije mkasema siku ya Kiyama kuwa sisi tulikuwa tumeghafilika na hayo. (7:172).*

Aya hii inatupa mwanga kuwa kumuamini Allah (sw) na kumuabubu inavyostahiki katika maisha ya kila siku ni ahadi ya asili iliyofungamana na umbile la binaadamu. Hivyo ni wazi kuwa kumuamini Allah (sw) na kumuabudu inavyostahiki ni jambo jepesi linalolandana na asili ya umbile la mwanadamu mwenyewe. Hata hivyo kwa kuwa binaadamu ameumbwa na udhaifu mwingi; Allah (sw) hakumuacha binadamu hivyo hivyo na ahadi yake ya asili, bali ameweka utaratibu madhubuti wa kumkumbusha binaadamu ahadi yake hii mara kwa mara katika maisha yake yote. Allah (sw) ameleta mitume pamoja na vitabu ili kuwakumbusha wanaadamu wa kila ummah na kila zama juu ya ahadi hii kuu. Waislamu wanajikumbusha mara kwa mara juu ya ahadi hii katika swala kila wanaposoma Suratul-Fatiha.

إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ ﴿٥﴾

*"Ni Wewe tu tunayekuabudu na ni wewe tu tunayekuomba msaada". (1:5).*

Pia tunapotoa shahada:

أَشْهَدُ أَنْ لَآ إِلَٰهَ إِلَّا ٱللَّهُ وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا رَسُولُ ٱللَّهِ

*"Nashuhudia kuwa hapana mola ila Allah na ninashuhudia kuwa Muhammad ni Mtume wa Allah".*

Katika shahada tunatoa ahadi kuwa katika kuendesha maisha yetu ya kila siku tutamtii na kumnyenyekea Allah (s.w). Pekee na tutafuata mwenendo wa Mtume wake. Hivyo, yule mwenye kumuasi Allah (s.w) na Mtume wake ni mwenye kuvunja ahadi.

Aidha, katika Qur-an tunaamrishwa kuchunga ahadi yoyote ya halali tuliyoitoa kwa mtu au kwa jamii:

*"Na timizeni ahadi. Kwa hakika ahadi itaulizwa". (17:34).* وَأَوْفُوا۟ بِٱلْعَهْدِ ۖ إِنَّ ٱلْعَهْدَ كَانَ مَسْـُٔولًا ﴿٣٤﴾

Kuvunja ahadi ya halali pasina dharura ni tabia ya unafiki.Katika mchakato wa maisha ya kila siku tuna weka ahadi za aina nyingi na hapa tutarejea baadhi ya aya za kuomba ahadi hizo:

## Deni ni Ahadi

Ahadi nyingine inayochukua nafasi ya juu ni ahadi ya kulipa deni. Kukopa katika Uislam pasina riba ni jambo la halali kwa mtu aliyetingwa na shida ya msingi. Kukopa kwa ajili tu ya kujistarehesha au kufanya mambo ambayo si ya lazima wakati huo ni jambo lisilopendelewa na Uislamu kwani kushindwa kulipa deni hilo itakuwa ni miongoni mwa mambo yatakayomhasirisha mja mbele ya Allah (sw) katika siku ya Hukumu. Mtume (saw) amesema:

*Mkopaji akifa (na deni) atalazimishwa kulipa deni hilo siku ya Kiyama. Bali deni linaruhusiwa katika hali tatu;kwanza, wakati mja atakapo kuwa hana cha kumuwezesha kupigania katika njia ya Allah na akakopa ili ajitayarishe kupigana na adui yake na adui wa Allah(sw); Pili, wakati mtu atakapofiwa na Muislamu wa karibu yake na akakopa ili agharimie mazishi, na tatu, kwa manamume ambaye kwa kuhofia hatari za kuendelea kukaa bila kuoa kwa kusindwa kuchunga mipaka ya Dini, akakopa ili kugharimikia ndoa, Allah (sw) atawasamehe katika siku ya Hukumu(iwapo watakufa na madeni). (Ibn Majah).*

Katika hadith nyingine tunafahamishwa kuwa Mtume wa Allah amesema

*Siku ya Kiyama Allah (sw) atamwita mkopaji na kumsimamisha mbele yake. Kisha ataulizwa; Ee mwana wa Adamu! Ni kwa shida gani ulijiingiza katika deni hili? Na kwa nini umechukua (umeharibu) haki za wengine? Atajibu: "Ee Bwana wetu! Yu wafahamu vema kile nilichokopa, siku (kila wala kukinywa wala kukifuja, lakini wakati fulani ajali ya moto ilitokea, wakati mwingine palitokea wizi (mali hiyo) ilipotea au hasara ilitokea (juu yake). Allah (s.w.) atasema:"Ee mja wangu! Umesema kweli. Nina haki zaidi kulipa deni hili. Allah ataamuru ichukuliwe amali njema na ataipima katika mizani, na amali yake njema itakuwa nzito kuliko amali mbovu, ataingia peponi kwa Rehema ya Bwana wake". (Ahmad).*

Hadith zinatufahamisha kuwa Allah (sw) atawalipia madeni wale tu ambao walilazimishwa na hali ikabidi wakope na kwa bahati mbaya wakakosa cha kulipa mpaka wakafa na madeni. Katika hali hii Allah (sw) atawalipia madeni hayo siku ya kiyama kwani ni lazima kila mwenye haki alipwe haki yake siku hiyo ya Kiyama kwani ni lazima kila mwenye haki alipwe haki yake siku hiyo. Lakini atakayekopa bila ya sababu ya msingi, halafu itokee asilipe deni lake mpaka akafa, ni lazima atalilipa mwenyewe deni hilo mbele ya Allah (sw). Pia Mtume (saw) amesema:

*Mali ya wengine (kama mkopo) kwa nia ya kulipa (kisha asiweze kulipa) Allah (sw) atamlipia deni lake. Na mwenye kuchukua mkopo kwa nia ya kutolipa, basi Allah atamuangamiza na kumhilikisha. (Bukhari)*

Katika Hadith nyingine tunafahamishwa kuwa:

*Abu Qatawa ameeleza kuwa mtu mmoja aliuliza: Ee Mtume wa Allah kama nitauawa katika njia ya Allah, dhambi zangu zote zitasamehewa? Alijibu (Mtume): "Ndio, kama utaumwa, na kama ni mwenye subira na shukurani na mwenye kutafuta Radhi za Allah, kama umebakia katika mstari wa mbele na kuwashambulia maadui bila ya kurejea nyuma. "Kisha Mtume akamuuliza kuwa amesemaje. Muulizaji alirudia tena swali lake na kisha Mtume (saw) akasema: Dhambi zako zitasamehewa lakini deni lako halitasamehewa. Sasa hivi Jibril amenifahamisha juu ya hili. (Muslim).*

Huu ndio uzito wa deni na Muislam wa kweli atajitahidi kujiepusha na madeni na ikibidi akope ajitahidi kulilipa katika muda aliouahidi au mapema zaidi pale atakapopata uwezo. Utashangaa leo hii waislamu wamefanya kukopa ndio mtindo wa maisha!

**Nadhiri ni ahadi**

Mara nyingi mwanaadam anapokuwa na hali ngumu , humwomba Mola wake kuwa akimuondoa kwenye hali ile ya shida atamuabudu inavyostahiki na atatenda wema kwa waja wake. Lakini wanafiki huvunja ahadi hiyo na kusahau kabisa yale aliyoahidi baada ya kupata hali nzuri aliyoitamani. Katika historia tunafahamishwa mfano wa watu wa namna hii. Mtume (saw) alipokuwa Madina, mtu mmoja jina lake Sa'laba alihudhuria mkutano wa Ansar na mbele ya mkutano aliahidi kuwa kama Allah (sw) atamtajirisha, atatoa sadaqa na atawafanyia wema jamaa zake. Punde alitajirika kwa mali ya urithi. Lakini, kwa bahati mbaya hakutekeleza ahadi yake wala hakukumbuka yale aliyoyatamka mbele ya Allah (sw). kutokana na kisa hiki Allah anatukumbusha katika aya zifuatazo:

۞وَمِنْهُم مَّنْ عَٰهَدَ ٱللَّهَ لَئِنْ ءَاتَىٰنَا مِن فَضْلِهِۦ لَنَصَّدَّقَنَّ وَلَنَكُونَنَّ مِنَ
ٱلصَّٰلِحِينَ ﴿٧٥﴾ فَلَمَّآ ءَاتَىٰهُم مِّن فَضْلِهِۦ بَخِلُوا۟ بِهِۦ وَتَوَلَّوا۟ وَّهُم
مُّعْرِضُونَ ﴿٧٦﴾ فَأَعْقَبَهُمْ نِفَاقًا فِى قُلُوبِهِمْ إِلَىٰ يَوْمِ يَلْقَوْنَهُۥ بِمَآ أَخْلَفُوا۟
ٱللَّهَ مَا وَعَدُوهُ وَبِمَا كَانُوا۟ يَكْذِبُونَ ﴿٧٧﴾ أَلَمْ يَعْلَمُوٓا۟ أَنَّ ٱللَّهَ يَعْلَمُ سِرَّهُمْ
وَنَجْوَىٰهُمْ وَأَنَّ ٱللَّهَ عَلَّٰمُ ٱلْغُيُوبِ ﴿٧٨﴾

*"Na miongoni mwao wako waliomuahidi Mwenyezi Mungu kuwa:"akitupa katika fadhila zake tutatoa sadaqa na tutakuwa miongoni mwa watendao mema. Lakini alipowapa hizo fadhila zake walizifanyia ubakhili na wakakengeuka, nao (mpaka hivi sasa) wanakengeuka. Kwa hiyo atawalipa unafiki nyoyoni mwao mpaka siku ya kukutana Naye, kwa sababu ya kukhalifu kwao waliyomuahidi Mwenyezi Mungu na kwa sababu ya kusema kwao uwongo". Je hawajui kwamba Mwenyezi Mungu anajua siri zao na minong'ono yao, na kwamba Mwenyezi Mungu ndiye ajuaye mambo ya ghaibu" (9:75-78).*

Muislamu wa kweli anatakiwa kila mara akumbuke hali yake duni aliyonayo hapo awali kutokana na uchanga wake , ugonjwa, uhaba wa mali au kutokana na mazingira fulani ya dhiki na alinganishe hali nzuri na wasaa alionao hivi sasa kisha amshukuru Allah (sw) kwa kuzidisha

unyenyekevu kwake na kutenda mema.

### Mikataba ni Ahadi

Waislamu wa kweli hawana budi kufuata masharti ya mikataba waliofunga na wengine kipindi ambapo haiendi kinyume na sharia ya Allah (sw). Katika historia tunaona jinsi Mtume (saw) alivyofuata masharti ya mikataba ya amani waliyowekeana na makabila au mataifa ya makafikiri. Kwa mfano, kutokana na mkataba wa amani wa Hudaybiyya, Mtume (saw) alimkatalia Muislamu kutoka mikononi mwa Makurayshi kujiunga na kundi la waislamu wenzake kwa vile ingalikuwa ni kinyume na makubaliano ya mkataba pamoja na kwamba mkataba kulikuwa haujawekwa sahihi. Uislam unatutaka tuwe wakweli katika mikataba yetu hata kama tumefunga mikataba hiyo na maadui zetu na maadui wa Mwenyezi Mungu. Tunatanabahishwa katika Qur'an:

...وَلَا يَجْرِمَنَّكُمْ شَنَـَٔانُ قَوْمٍ أَن صَدُّوكُمْ عَنِ ٱلْمَسْجِدِ ٱلْحَرَامِ أَن تَعْتَدُوا۟ ۘ وَتَعَاوَنُوا۟ عَلَى ٱلْبِرِّ وَٱلتَّقْوَىٰ ۖ وَلَا تَعَاوَنُوا۟ عَلَى ٱلْإِثْمِ وَٱلْعُدْوَٰنِ ۚ وَٱتَّقُوا۟ ٱللَّهَ ۖ إِنَّ ٱللَّهَ شَدِيدُ ٱلْعِقَابِ ﴿٢﴾

*"...wala kule kuwachukia watu kwa kuwa walikuzuilieni kufika katika msikiti uliotukuzwa (Makka) kusikuopelekeeni kutowafanyia uadilifu, Na saidianeni katika wema na ucha-Mungu, wala msisaidiane katika maovu na uadui. Na Mcheni Mwenyezi Mungu ; hakika Mwenyezi Mungu ni mkali wa kuadhibu". (5:2)*

Maelezo haya yanatosha kutupa mwanga wa uzito wa ahadi mbele ya Allah(sw). Muislamu wa kweli hana budi kujizatiti kuwa mkweli katika ahadi zake zote alizozitoa kwa Allah (s.w) na kwa wanaadaml wenziwe. Zote hizi zitakuwa ni zenye kuulizwa mbele ya Allah (sw) katika siku ya Hukumu.

## 11. Kuwa na Kauli Njema

Muislamu anatakiwa kila mara azungumze mambo ya maana na ya kheri. Ulimi utumike kusema ukweli, kuamrisha mema, kukataza maovu, kuwashauri wengine juu ya mambo ya kheri, kupatanisha waliogombana, kumsabihi Allah, kutoa elimu yenye kunufaisha watu na katika mazungumzo mengine ya kheri.

وَمَنْ أَحْسَنُ قَوْلًا مِّمَّن دَعَآ إِلَى ٱللَّهِ وَعَمِلَ صَـٰلِحًا وَقَالَ إِنَّنِى مِنَ ٱلْمُسْلِمِينَ ﴿٣٣﴾

*"Na ni nani asemaye kauli bora kuliko (yule) aitaye (watu) kwa Allah na (mwenyewe) akafanya vitendo vizuri na kusema (kwa maneno yake na vitendo vyake): "Hakika mimi ni miongoni mwa Waislamu". (41:33).*

Allah (s.w) anatuamrisha kusema maneno mazuri katika aya ifuatayo:

وَقُل لِّعِبَادِي يَقُولُوا الَّتِي هِيَ أَحْسَنُ ۚ إِنَّ الشَّيْطَانَ يَنزَغُ بَيْنَهُمْ ۚ إِنَّ الشَّيْطَانَ كَانَ لِلْإِنسَانِ عَدُوًّا مُّبِينًا ﴿٥٣﴾

*"Na waambie waja wangu waseme daima maneno yaliyo mazuri. Maana Shetani huchochea ugomvi baina yao. Hakika shetani kwa wanaadamu ni adui aliye dhahiri". (17:53)*

Hivyo Muislamu hana budi kuzungumza na watu kwa maneno mazuri ya heshima. Maneno mazuri ya heshima yanajenga na kuzidisha upendo kati ya watu. Maneno mazuri ya heshima ni ngao ya kumzuilia shetani asiingilie kati na kuleta migongano na kutoelewana. Ni katika msingi huu tunaamrishwa tuulinganie Uislamu kwa hekima na kwa mawaidha mazuri:

ادْعُ إِلَىٰ سَبِيلِ رَبِّكَ بِالْحِكْمَةِ وَالْمَوْعِظَةِ الْحَسَنَةِ ۖ وَجَادِلْهُم بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ ۚ إِنَّ رَبَّكَ هُوَ أَعْلَمُ بِمَن ضَلَّ عَن سَبِيلِهِ ۖ وَهُوَ أَعْلَمُ بِالْمُهْتَدِينَ ﴿١٢٥﴾

*"Walinganie (watu) katika njia ya Mola wako kwa hekima na mawaidha mema, na ujadiliane nao kwa namna iliyo bora. Hakika Mola wako ndiye anayemjua aliyepotea katika njia yake naye ndiye anayewajua walioongoka". (16:125).*

Kauli njema ni yenye kumuongoza mja kwenda Peponi na kauli mbaya humuongoza mja kwenda Motoni kama tunavyojifunza katika Hadithi zifuatazo:

*Sahl bin Sa'd(r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: "Atakayeweza kuchunga kilichopo kati kati ya taya zake (ulimi) na kilichopo katikati ya miguu yake miwili (utupu) ninaweza kumhakikishia Pepo." (Bukhari).*

*Abu Hurairah(r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: "Mja atatamka neno lenye kumfurahisha Allah bila ya kuona uzito wake, bado Allah (s.w) humlipa malipo makubwa kutokana na neno hilo. Na mja atatamka neno lenye kumuudhi Allah bila ya kuona uzito wake, na bado linakuwa ndio mwanzo wa kumuingiza Motoni. (Bukhari).*

## 12. Kuepuka Maongezi yasiyo na Maana

Maongezi au mazungumzo yasiyo na maana ni yale yasiyoleta manufaa au kheri yoyote ila hasara tu. Mazungumzo haya yapo katika kupiga soga, kupiga porojo, kupiga hadithi za pauka pakawa, kutaniana, kubishana, na mengine ya namna hiyo. Mara zote mazungumzo ya aina hii huwapelekea watu kusengenya, kusema uwongo, kufitinisha, kugombana na kupoteza muda. Aidha mazungumzo ya aina hii huwasahaulisha watu kumkumbuka Allah (s.w).

Muumini hana budi kujiepusha na tabia hii ya kujiingiza kwenye mazungumzo ya upuuzi. Miongoni mwa sifa za waumini ni pamoja na kujiepusha na mambo ya upuuzi kama tunavyojifunza katika Quran:

قَدْ أَفْلَحَ ٱلْمُؤْمِنُونَ ﴿١﴾ ٱلَّذِينَ هُمْ فِى صَلَاتِهِمْ خَٰشِعُونَ ﴿٢﴾

وَٱلَّذِينَ هُمْ عَنِ ٱللَّغْوِ مُعْرِضُونَ ﴿٣﴾

*"Hakika wamefuzu Waumini. Ambao katika Swala zao ni wanyenyekevu. Na ambao hujiepusha na mambo ya upuuzi". (23:1-3).*

Waja wema mbele ya Allah ni pamoja:

وَٱلَّذِينَ لَا يَشْهَدُونَ ٱلزُّورَ وَإِذَا مَرُّوا۟ بِٱللَّغْوِ مَرُّوا۟ كِرَامًا ﴿٧٢﴾

*"Na wale ambao hawashuhudii uwongo na wanapopita penye upuuzi hupita kwa heshima (zao). (25:72).*

Muislamu anashauriwa daima abaki kimya kama hana la maana la kuzungumza. Mtume (s.a.w) ametuusia:

*"Kuwa kimya. Hii ni njia ya kumfukuza shetani na kuimarisha dini yako" (Ahmad).*

*“Anayekuwa kimya (anayenyamaza wakati hana la maana la kuzungumza) atakuwa salama”. (Ahmad, tirmidh).*

*“Ni jambo bora mno kwa Muumini kuacha yasiyomhusu” (Malik, Ahmad, Tirmidh).*

*“Ni katika ubora wa Imani ya mtu kwa kuacha kujihusisha na mambo ya upuuzi”. (Tirmidh).*

### 13. Kuepuka Usengenyaji

Kusengenya ni kumzungumza vibaya mtu asiyekuwapo hata kama hayo yanayozungumzwa juu yake ni kweli. Maana ya kusengenya imebainishwa vema katika Hadithi ifuatayo:

*Abu Hurairah (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: “Wote mnajua kusengenya ni nini?” Walijibu, “Allah na Mtume wake ndio wajuzi zaidi”. Alisema Mtume: “Maongezi juu ya ndugu yako ambayo hayapendi” Aliulizwa Mtume, “Je, kama kile kinachozungumzwa ni kweli juu ya ndugu yangu?” Akasema (Mtume): “Kama hilo unalomsengenya kwalo analo, bado utakuwa umemsengenya na kama hilo unalomsengenya kwalo hanalo, utakuwa umemzulia”. (Muslim)*

Kama Muislamu anataka kuongea mabaya ya mtu angoje mwenyewe awepo na iwe kwa nia ya kumrekebisha na sio kwa nia ya kumuaibisha na kumfedhehesha. Ilipokuwa hapanabudi Mtume(s.a.w) aongee juu ya tabia mbaya ya mtu, alikuwa hamtaji muhusika moja kwa moja bali alikuwa akisema: “*Wakoje watu hawa wanaofanya kadha wa kadha*”.

Kusengenya hakuishii tu kwenye ulimi bali mtu aweza kusengenya kwa ishara ya macho, ulimi, midomo, mikono, miondoko na maandishi. Hata mwenye kusikiliza habari za kusengenya naye anahesabiwa kuwa amesengenya kama tunavyojifunza katika Hadithi:

*Ibn ‘Umar(r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: “Msikilizaji (wa maneno ya usengenyi) naye ni mmoja wa wasengenyaji”. (Tabrani).*

Kusengenya ni miongoni mwa madhambi makubwa kwa mujibu wa Qur-an na Sunnah. Katika Qur-an Allah (s.w) anatutahadharisha juu ya tabia ya usengenyi kama ifuatavyo:

وَيْلٌ لِّكُلِّ هُمَزَةٍ لُّمَزَةٍ ﴿١﴾

*“Adhabu kali itamthubutikia kila mlamba kisogo, msengenyaji. (104:1)*

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ ٱجۡتَنِبُواْ كَثِيرٗا مِّنَ ٱلظَّنِّ إِنَّ بَعۡضَ ٱلظَّنِّ إِثۡمٞۖ
وَلَا تَجَسَّسُواْ وَلَا يَغۡتَب بَّعۡضُكُم بَعۡضًاۚ أَيُحِبُّ أَحَدُكُمۡ أَن يَأۡكُلَ لَحۡمَ
أَخِيهِ مَيۡتٗا فَكَرِهۡتُمُوهُۚ وَٱتَّقُواْ ٱللَّهَۚ إِنَّ ٱللَّهَ تَوَّابٞ رَّحِيمٞ ١٢

*“Enyi mlioamini! Jiepusheni sana na dhana, kwani dhana ni dhambi. Wala msipeleleze (msipekue habari za watu). Wala baadhi yenu wasiwasengenye wengine. Je, mmoja wenu anapenda kula nyama ya nduguye aliyekufa? La! Hapendi. Na mcheni Allah. Bila shaka Allah ni mwenye kupokea toba na mwingi wa Kurehemu”.. (49:12).*

Katika Hadithi kinabainishwa kina cha uovu wa kusengenya kama ifuatavyo:

*Abdullah bin Mas’ud amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: Kumsengenya Muislamu ni uovu na uasi na kumpiga ni ukafiri”. (Bukhari na Muslim).*

*Abdur-Rahmaani bin Ghanna(r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: “Miongoni mwa waja wema mbele ya Allah ni yule au wale wanaomkumbuka Allah (kila wakati wanapokuwa macho) na miongoni mwa waja waovu mbele ya Allah ni wale wanaopita huku na huko wakiwateta (wakiwasengenya) watu ambao wanasababisha kutoelewana kati ya wacha-Mungu”. (Ahmad, Baihaqui).*

Dhambi ya kusengenya ni miongoni mwa madhambi makubwa mbele ya Allah (s.w) yasiyosameheka mpaka kwanza asamehe yule aliyesengenywa kama tunavyojifunza katika Hadithi zifuatazo:

*Abu Sayeed na Jabir(r.a) wamesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: “Kusengenya ni kubaya kuliko kuzini”. Wakauliza, “Ee Mtume wa Allah! Inakuwaje kusengenya kuwe kubaya kuliko kuzini? Alijibu Mtume, “Mtu mwenye kuzini akitubia kwa Allah (s.w) anaweza kusamehewa, lakini msengenyaji hasamehewi mpaka kwanza asamehewe na yule aliyemsengenya”. (Baihaqi).*

*Anas(r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: "Msamaha kwa dhambi ya kusengenya hupatikana kwa kutakwa msamaha. kwa yule aliyesengenywa kwa kusema: "Ee Allah! Tusamehe pamoja naye". (Baihaqi).*

Kinachoruhusiwa katika Uislamu ni mtu kushitakia dhulma aliyofanyiwa na mtu kama inavyobainishwa katika Qur-an:

۞لَّا يُحِبُّ ٱللَّهُ ٱلْجَهْرَ بِٱلسُّوٓءِ مِنَ ٱلْقَوْلِ إِلَّا مَن ظُلِمَ ۚ وَكَانَ ٱللَّهُ سَمِيعًا عَلِيمًا ﴿١٤٨﴾

*"Allah hapendi (watu) kutoa maneno ya kutangaza ubaya (kwa watu wengine) ila kwa yule mwenye kudhulumiwa, na Allah ndiye asikiaye ajuaye(4:148)*

Pia tunaruhusiwa kueleza ubaya wa mtu kwa anayemuhusu ili amrekebishe. Tunaruhusiwa pia kumsema mtu kwa ubaya kwa lengo la kuwatahadharisha wengine na tabia mbaya ya mtu ili wasiathirike.

## 14. Kujiepusha na Dharau

Kudharau wengine ni tabia mbaya na ni kitendo kiovu mbele ya Allah (s.w). Katazo la kuwadharau watu liko bayana katika Qur-an:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ لَا يَسْخَرْ قَوْمٌ مِّن قَوْمٍ عَسَىٰٓ أَن يَكُونُواْ خَيْرًا مِّنْهُمْ وَلَا نِسَآءٌ مِّن نِّسَآءٍ عَسَىٰٓ أَن يَكُنَّ خَيْرًا مِّنْهُنَّ ۖ

*"Enyi mlioamini! Wanaume wasiwadharau wanaume wenzao, huwenda wakawa bora kuliko wao; wala wanawake wasiwadharau wanawake wenzao; huwenda wakawa bora kuliko wao..." (49:11)*

Mwenye kuwadharau wengine hujihisi kuwa yeye ni bora kuliko hao anaowadharau. Hili ni kosa kubwa kwani anaye mjua aliye mbora ni Allah (s.w) Pekee kama tunavyojifunza katika Qur-an:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلنَّاسُ إِنَّا خَلَقْنَٰكُم مِّن ذَكَرٍ وَأُنثَىٰ وَجَعَلْنَٰكُمْ شُعُوبًا وَقَبَآئِلَ لِتَعَارَفُوٓاْ ۚ إِنَّ أَكْرَمَكُمْ عِندَ ٱللَّهِ أَتْقَىٰكُمْ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ عَلِيمٌ خَبِيرٌ ﴿١٣﴾

*"Enyi Watu! Kwa hakika tumekuumbeni(nyote) kutoka kwa (yule) mwanaume(mmoja; Adamu) na (yule yule) mwanamke (mmoja; Hawwa). Na tumekufanyeni mataifa na makabila (mbalimbali) ili mjuane. Hakika ahishimiwaye sana miongoni mwenu mbele ya Mwenyezi Mungu ni yule amchaye Mungu zaidi katika ninyi. Kwa yakini Mwenyezi Mungu ni Mjuzi, Mwenye habari (49:13).*

Aya hii kwa ujumla inatuwekea msingi wa usawa. Inatukumbusha kuwa watu wote asili yao ni moja; ni watoto wa Adam ambaye ameumbwa kutokana na udongo.

وَلَقَدْ خَلَقْنَا ٱلْإِنسَـٰنَ مِن صَلْصَـٰلٍ مِّنْ حَمَإٍ مَّسْنُونٍ ﴿٢٦﴾

*"Na tulimuumba mtu kwa udongo mkavu unaotoa sauti, wenye kutokana na matope meusi yaliyovunda." (15:26).*

Tofauti za rangi, kabila, taifa n.k. ziko pale kwa ajili ya anuani tu na kamwe zisiwe msingi wa kubaguana na kudharauliana. Pia tofauti za vipawa zilizopo kati ya watu kama vile elimu, utajiri, ufalme, n.k. isiwe sababu ya kubaguana. Vipawa hivyo ametunukiwa mwanaadamu kama mtihani kwake.Ama atamshukuru Mola wake kwa kutumia vipawa hivyo kwa ajili yake kama inavyostahiki awe mwenye kufaulu au atatakabari kwa kutumia vipawa hivyo apendavyo kinyume na maagizo ya Mola wake awe ni mwenye kufeli.

## 15. Kujiepusha na Matusi

Mtu anayetukana ana lengo la kumdhalilisha mwingine. Waislamu tumekatazwa kutukanana na hata kuitana majina tusiyoyapenda kwa kejeli.

وَلَا تَنَابَزُوا۟ بِٱلْأَلْقَـٰبِ ۖ بِئْسَ ٱلِٱسْمُ ٱلْفُسُوقُ بَعْدَ ٱلْإِيمَـٰنِ ۚ وَمَن لَّمْ
يَتُبْ فَأُو۟لَـٰٓئِكَ هُمُ ٱلظَّـٰلِمُونَ ﴿١١﴾

*".... Wala msitukanane kwa kabila wala msiitane majina mabaya (ya kejeli). Jina baya kabisa kuitwa mtu ni "Fasiqi" baada ya kuwa yeye ni Muislamu. Na wasiotubu basi hao ndio madhalimu". (49:11)*

Fasiq ni yule aliyebobea katika uasi. Yaani mtu anayejizatiti kumuasi Allah (s.w) kwa namna mbali mbali kama vile mwizi, mlevi,

mzinzi na kadhalika. Ni vibaya mno mbele ya Allah (s.w) kumsingizia au kumwita Muislamu "*mwizi*" na huku si mwizi au kumwita "*mnafiki*" au "*kafir*" na huku ni Muislamu kamili. Tabia hii imekemewa vikali katika Qur-an:

إِنَّ ٱلَّذِينَ يُحِبُّونَ أَن تَشِيعَ ٱلْفَٰحِشَةُ فِى ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ لَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ

فِى ٱلدُّنْيَا وَٱلْءَاخِرَةِ ۚ وَٱللَّهُ يَعْلَمُ وَأَنتُمْ لَا تَعْلَمُونَ ﴿١٩﴾

*"Kwa yakini wale wanaopenda uenee uovu kwa wale walioamini watapata adhabu iumizayo katika dunia na katika akhera, na Allah ndiye ajuaye, na nyinyi hamjui". (24:19).*

Kutokana na makemeo haya, Muumini wa kweli hana budi kujiepusha na tabia ya kuwaita watu kwa majina mabaya kwani kufanya hivyo mtu hujilaani mwenyewe kiasi kwamba hayo majina mabaya yatamgeukia, kama tunavyojifunza katika Hadithi zifuatazo:

*Abu Dh-dhari(r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: Hapana mtu atakayemsingizia mwingine uasi kwa Allah au akamwita "kafiri", ila hayo yatamgeukia yeye mwenyewe iwapo huyo aliyemsingizia hayuko hivyo". (Bukhari)*

## 16. Kuepuka Mabishano

Mabishano husababisha ugomvi, maudhi au kudharauliana. Mabishano yaweza kutibua mahusiano mzuri kati ya watu. Hivyo Uislamu unatukataza kubishana. Tunatakiwa tuzungumze na watu na kufahamishana mambo kwa hoja na sio kwa mabishano. Tunafundishwa katika Qur-an kuwa tukizungumza na watu ambao hawataki kuelewa bali wanafurahia ubishi tu, basi tusiendelee kuzungumza nao. Bali tuagane nao kwa salama.

وَعِبَادُ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلَّذِينَ يَمْشُونَ عَلَى ٱلْأَرْضِ هَوْنًا وَإِذَا خَاطَبَهُمُ

ٱلْجَٰهِلُونَ قَالُوا۟ سَلَٰمًا ﴿٦٣﴾

*"Na waja (wema) wa Rahman ni wale wanaotembea katika ardhi kwa unyenyekevu na wajinga wakisema nao, huwajibu "Salama". (25:63)*

## 17. Kuepuka kujisifu na kujitukuza

Waislamu tumekatazwa kujisifu sisi wenyewe na pia tumekatazwa kuwasifu wengine kupita kiasi.Mtume (saw) amekataza jambo hili katika Hadith zifuatazo:

*Abu Hurairah (r.a) ameeleza kuwa Mtume (saw) amependekeza kwetu kuwa tumtupie mchanga (vumbi) usoni yule anayejihusisha na kuwasifusifu watu kupita kiwango kinachostahili.(Tirimidh).*

*Abu Bakar (ra) amesimulia kuwa mtu mmoja alimsifu mtu mwingine mbele ya Mtume (saw). Mtume (saw) alisema mara tatu. "Ole wako umekata kichwa cha ndugu yako!" (Kisha anasema Mtume); Yeyote miongoni mwenu ambaye ataona hapana budi kumsifu mwingine na aseme; Nafikiri fulani yuko hivi na hivi ( ana sifa hizi na hizi) na Allah (sw) atamuhesabu hivyo kama kweli mbele yake anastahiki sifa hizo. Lakini asithubutu mtu kumpachika yeyote sifa ya Ucha-Mungu(wema) juu ya Allah." (Bukhari na Muslim)*

Aidha Allah (sw) ametukataza kujisifu sifu katika aya ifuatayo:

...إِنَّ رَبَّكَ وَاسِعُ الْمَغْفِرَةِ ۚ هُوَ أَعْلَمُ بِكُمْ إِذْ أَنشَأَكُم مِّنَ الْأَرْضِ وَإِذْ أَنتُمْ أَجِنَّةٌ فِي بُطُونِ أُمَّهَاتِكُمْ ۖ فَلَا تُزَكُّوا أَنفُسَكُمْ ۖ هُوَ أَعْلَمُ بِمَنِ اتَّقَىٰ ﴿٣٢﴾

*"...Yeye (Allah) ndiye anayekujueni sana tangu alipokuumbeni katika ardhi na mlipokuwa mimba matumboni mwa mama zenu. Basi msizitakase nafsi zenu; Yeye (Allah) anamjua sana aliyetakasika". (53:32)*

Kuwasifu sana watu kupita kiasi huwapelekea wale wenye kusifiwa kuvimba vichwa na kujihisi kuwa wao ni watukufu na bora zaidi kuliko wengine katika jamii. Tunayaona madhara makubwa yaliyojitokeza katika jamii ya waislamu kutokana na sifa za kupita kiasi tulizowapachika masheikhe zetu na watu wengine tuliowapachika usharifu, uwalii, ucha-mungu,n.k. Mgawanyiko wa waislamu tunaoushuhudia hivi leo kwenye madh-habu, twarika na matapo mengine mbali mbali, unatokana na dhambi hii ya kuwasifu viongozi wa hayo makundi kupita kiasi.

Pia tunajifunza katika historia kuwa chanzo cha Mitume wa Allah (sw) na watu wema kushirikishwa na Allah (s.w) ni kuwasifu kupita

kiasi. Katika Qur'an (9:30) tunafahamishwa kuwa kuwaiga washirikina waliowatangulia katika kuwasifu kupita kiasi viongozi wao, Mayahudi walimfaya Uzair (Mtu mwema) mwana wa Mungu na wakristo wakamfanya Isa Bin Maryam mwana wa Mungu. Kwa kuchelea watu wa Ummah nao wasijetumbukia kwenye shirki hii ya sifa, Mtume (saw) anatuasa katika Hadith ifuatayo:

> *" Imepokelewa kutoka kwa Umar(r.a) kuwa amesema Mtume wa Allah (saw) Msizidishe kwenye kunisifu kama walivyozidisha wakristo ( manasara) katika kumsifu mwana wa Maryam. Mimi ni mja wa Allah tu; kwa hiyo niiteni ;"Mja wa Allah na Mtume wake". (Bukhari)*

Hivyo muumini wa mkweli hanabudi kujiepusha na kujisifu sifu au kuwasifusifu watu. Na ikiwa hapana budi kumsifu mtu tuzingatie mipaka na tuseme kama alivyotuelekeza Mtume (saw) katika Hadith tuliyoirejea hapa juu. Tabia ya kujisifusifu au kuwasifusifu watu ni tabia ya uwongo, unafiki na ushirikina.

### 18. Kuepukana na Kibri na Majivuno

Kibri, majivuno na majigambo ni katika tabia mbaya iliyokemewa vikali katika Qur-an kama ifuatavyo:

وَلَا تَمْشِ فِي ٱلْأَرْضِ مَرَحًا ۖ إِنَّكَ لَن تَخْرِقَ ٱلْأَرْضَ وَلَن تَبْلُغَ ٱلْجِبَالَ

طُولًا ﴿٣٧﴾ كُلُّ ذَٰلِكَ كَانَ سَيِّئُهُۥ عِندَ رَبِّكَ مَكْرُوهًا ﴿٣٨﴾

> *"Wala usitembee (usiende) katika ardhi kwa maringo. Hakika wewe huwezi kuzipasua ardhi wala huwezi kufikia urefu wa mlima. Haya yote ubaya wake ni wenye kuchukiza mbele ya Mola wako". (17:37-38)*

وَلَا تُصَعِّرْ خَدَّكَ لِلنَّاسِ وَلَا تَمْشِ فِي ٱلْأَرْضِ مَرَحًا ۖ إِنَّ ٱللَّهَ لَا يُحِبُّ كُلَّ

مُخْتَالٍ فَخُورٍ ﴿١٨﴾

> *"Wala usiwatazame (watu) kwa upande mmoja wa uso, wala usiende katika ardhi kwa maringo, hakika Allah hampendi kila ajivunae ajifaharishaye". (31:18).*

Mtu mwenye kiburi hujiona kuwa ni bora, wa juu na wa maana zaidi kuliko wengine. Kibri na kujiona husababishwa na neema mja

alizotunukiwa na Mola wake kama vile utajiri, madaraka, umaarufu, elimu, nguvu nyingi, uzuri wa sura, n.k. Mwenye kibri na kujiona anasahau kuwa kama alivyozipata neema hizi bila ya kupeleka barua yoyote ya maombi kwa Allah (s.w) ndivyo anavyoweza kukatikiwa na neema hizi na asiweze kufanya chochote. Katika Qur-an tunapigiwa mfano wa Qaaruni aliyetakabari kutokana na hiyo neema ya mali aliyokuwa nayo.Lakini Allah(s.w) alipomuondolea neema hiyo hakuweza kufanya lolote. Rejea Qur-an: (28:76-83).

Kibri na majivuno huzaa maovu yafuatayo: *dharau, ukatili, uonevu, udhalimu* na *kutoshaurika*. Waislamu tunaaswa tujiepushe mbali na tabia hii mbaya ambayo malipo yake ni moto wa Jahannam kama tunavyojifunza katika aya ifuatayo:

قِيلَ ٱدْخُلُوٓا۟ أَبْوَٰبَ جَهَنَّمَ خَٰلِدِينَ فِيهَا ۖ فَبِئْسَ مَثْوَى ٱلْمُتَكَبِّرِينَ ٧٢

*"Itasemwa: "Ingieni milango ya Jahannam mkae humo" Basi ni ubaya ulioje wa makazi ya wanaotakabari! (39:72).*

Pia Hadithi zifuatazo zinatubainishia kina cha uovu wa kibri:

*Abu Hurairah (r.a) Amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: Allah (s.w) amesema, "Utukufu ni nguo yangu na kibri ni kilemba changu. Yeyote atakayeshindania kimojawapo katika hivi ataangamia. (Muslim).*

*Abu Hurairah (r.a) amesimulia kuwa, Mtume wa Allah amesema: "Yule ambaye moyoni mwake mna chembe (punje) ya kibri hataingia peponi" Sahaba mmoja akauliza: "Je, kama mtu anapenda nguo nzuri na viatu?" Mtume (s.a.w) akasema, "Allah (s.w) ni mzuri na anapenda vizuri. Kibri ni kukataa ukweli na kupuuza watu". (Muslim)*

*Abu Hurairah (r.a) amesema kuwa Mtume wa Allah amesema: "Siku ya Kiyama, Allah (s.w) hatamwangalia yule anayevaa vazi lake kwa kibri" (Bukahri na Muslim).*

Msingi mkuu wa kibri ni ukafiri - kumkadhibisha Allah (s.w) na ujumbe wake:

سَأَصْرِفُ عَنْ ءَايَٰتِىَ ٱلَّذِينَ يَتَكَبَّرُونَ فِى ٱلْأَرْضِ بِغَيْرِ ٱلْحَقِّ وَإِن

يَرَوْا۟ كُلَّ ءَايَةٍ لَّا يُؤْمِنُوا۟ بِهَا وَإِن يَرَوْا۟ سَبِيلَ ٱلرُّشْدِ لَا يَتَّخِذُوهُ

سَبِيلًا وَإِن يَرَوْا۟ سَبِيلَ ٱلْغَىِّ يَتَّخِذُوهُ سَبِيلًا ۚ ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ كَذَّبُوا۟

بِـَٔايَـٰتِنَا وَكَانُوا۟ عَنْهَا غَـٰفِلِينَ ﴿١٤٦﴾

*"Nitawaepusha na (kuzingatia) aya zangu wale wanaotakabari katika nchi pasipo haki; na ambao kila hoja wanayoiona hawaiamini; na kama wakiiona njia ya uwongofu hawaishiki kuwa ndiyo njia, lakini wakiiona njia ya upotofu (upotevu) wanaishika kuwa ndiyo njia. Hayo ni kwa sababu ya kuzikadhibisha Aya zetu na kuzipuuza". (7:146)*

وَٱلَّذِينَ كَذَّبُوا۟ بِـَٔايَـٰتِنَا وَٱسْتَكْبَرُوا۟ عَنْهَآ أُو۟لَـٰٓئِكَ أَصْحَـٰبُ ٱلنَّارِ ۖ

هُمْ فِيهَا خَـٰلِدُونَ ﴿٣٦﴾

*"Na wale watakaokadhibisha aya zetu na kuzifanyia kiburi hao watakuwa watu wa Motoni, watakaa humo daima. (7:36).*

## 20. Kuepukana na Kulaani Ovyo

Kulaani ovyo kumekatazwa katika Uislamu. Mtu anapolaani wengine anakuwa amejisahau kuwa naye ni mkosaji. Mtume (s.a.w) ametukataza kulaani ovyo katika Hadithi zifuatazo:

*Ibn 'Umar (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: "Si sawa kwa Muumini kuwa mkubwa wa kulaani". Na katika upokezi mwingine, Mtume amesema, "Si stahiki ya Muumini kuwa mkubwa wa kulaani".* (Tirmidh).

*Abu Dard (r.a) amesimulia kuwa amemsikia Mtume wa Allah akisema: "Watu wenye mazoea ya kulaani hawatakuwa mashahidi wala wenye kushufaia katika siku ya Kiyama". (Muslim).*

*Ibn Abbas (ra) ameeleza kuwa upepo ulipeperusha nguo ya mtu. Kwa hiyo aliulaani (upepo). Mtume wa Allah (saw) alisema ; "Usiulaani kwa sababu umeamrishwa ufanye hivyo na kwa sababu laana inakurudia mwenye kulaani kitu kisichostahiki kulaaniwa (kisicho na hatia). (Tirmidh na Abu-Daud).*

Muislamu anatakiwa ajiepushe na tabia ya kulaani na badala yake awe mwingi wa kuwasamehe wenye kumkosea na kuwatakia msamaha kwa Allah (s.w) ili naye asamehewe dhambi zake.

## 20. Kujiepusha na Viapo

Waislamu tumekatazwa kuapa apa ovyo ovyo. Kiapo kinakubalika tu pale inapobidi kutolewa mbele ya Kadhi kama ushahidi. Mara nyingi mtu anayeapa apa ovyo ovyo ni muongo. Anaapa ili ahalalishe uwongo. Anahisi kuwa akisema bila kuapa watu hawatamuamini. Kuapa apa ovyo ni tabia ya kinafiki. Tunafahamishwa katika Qur-an kuwa wanafiki wakati wa Mtume (s.a.w) walikuwa wakificha ubaya wao dhidi ya Uislamu na Waislamu kwa kutoa viapo mbele ya Mtume (s.a.w). Lakini Allah (s.w) alimfahamisha Mtume wake kuwa asiamini viapo vyao kwani wao ni waongo.

## 21. Kujiheshimu na kuwaheshimu wengine

Katika Uislamu kila mtu anayo haki ya kuheshimiwa. Heshima ni haki ya mwanaadamu aliyozaliwa nayo. Miongoni mwa mambo ya msingi aliyousia Mtume (s.a.w) katika khutuba yake ya kuaga aliyoitoa katika uwanja wa Arafa 9 Dhul-Hijjah 10A.H, ni kulinda heshima ya kila mtu. Aliusia:

> *"Enyi watu hakika damu yenu (yaani uhai wenu), mali zetu na heshima yenu ni vitu vitakatifu kamwe visiharibiwe hadi mtakaposimamishwa mbele ya Mola wenu, kwa utukufu wa vitu hivyo ni kama ulivyo Utukufu wa siku hii, na mwezi huu na mji huu. Kwa hakika mtakutana na Mola wenu na atakuulizeni juu ya vitendo vyema. Je, nimefikisha ujumbe? Ee! Allah shuhudia".*

Kutokanana usia huu kila Muumini analazimika kuwaheshimu wanaadamu wenzake wakubwa na wadogo. Aseme nao kwa uzuri, asiwadharau, asiwadhalilishe, asiwafedheheshe na asiwavunjie heshima kwa namna yoyote ile. Awatii wazazi, wenye mamlaka juu yake na walio wakubwa kwake katika mambo yote yanayowafikiana na Qur-an na Sunnah, awahurumie na kuwasikiliza walio chini yake au wadogo zake. Kwani Mtume (s.a.w) amesema:

> *"Si katika sisi yule ambaye hamheshimu mkubwa wetu na kumhurumia mdogo wetu".*

Kuwaheshimu watu kama ilivyosisitizwa katika Qur-an ni pamoja na:

(i) Kuzungumza na watu kwa kauli nzuri, kwa upole na huruma. Qur-an inatuamrisha:
*"... Na semeni na watu kwa wema..." (2:83).* وَقُولُوا۟ لِلنَّاسِ حُسْنًا

(ii) Kuwatii wazazi, kuwahurumia na kusema nao kwa vizuri:

...وَقُل لَّهُمَا قَوْلًا كَرِيمًا ﴿٢٣﴾

*"... Na sema nao (wazazi) kwa msemo wa heshima (kabisa)". (17:23).*

(iii) Kuanza kutoa salaam kwa Waumini:

وَإِذَا جَاءَكَ الَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِآيَاتِنَا فَقُلْ سَلَامٌ عَلَيْكُمْ... ﴿٥٤﴾

*"Na wanapofika wale wanaoamini aya zetu wambie "Assalaam alaykum" (yaani amani iwe juu yenu)..." (6:54)*

(iv) Kurudishia saalam kwa ucheshi baada ya kusalimiwa:

وَإِذَا حُيِّيتُم بِتَحِيَّةٍ فَحَيُّوا بِأَحْسَنَ مِنْهَا أَوْ رُدُّوهَا... ﴿٨٦﴾

*"Na mnapoamkiwa kwa maamkio yoyote yale; basi itikieni kwa yaliyo bora kuliko hayo, au rejesheni hayo hayo. (4:86)*

(v) Kuwaheshimu watu wa dini nyingine kwa kutowabughudhi, kutowadharau au kutowadhalilisha kwa namna yoyote ile:

وَلَا تَسُبُّوا الَّذِينَ يَدْعُونَ مِن دُونِ اللَّهِ فَيَسُبُّوا اللَّهَ عَدْوًا بِغَيْرِ عِلْمٍ

*"Wala msiwatukane ambao wanaabudu kinyume cha Allah, wasije wakamtukana Allah kwa jeuri zao bila kujua...." (6:108).*

ادْعُ إِلَىٰ سَبِيلِ رَبِّكَ بِالْحِكْمَةِ وَالْمَوْعِظَةِ الْحَسَنَةِ وَجَادِلْهُم بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ إِنَّ رَبَّكَ هُوَ أَعْلَمُ بِمَن ضَلَّ عَن سَبِيلِهِ... ﴿١٢٥﴾

*"Waite (watu) katika njia ya Mola wako kwa hekima na mawaidha mema, na ujadiliane nao kwa namna iliyo bora. Hakika Mola wako ndiye anayemjua aliyepotea katika njia yake.. (16:125).*

(vi) Kuwakaribisha wageni na kuwapisha kwenye viti au nafasi ya kukaa:

يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓا۟ إِذَا قِيلَ لَكُمْ تَفَسَّحُوا۟ فِى ٱلْمَجَـٰلِسِ فَٱفْسَحُوا۟
يَفْسَحِ ٱللَّهُ لَكُمْ ۖ وَإِذَا قِيلَ ٱنشُزُوا۟ فَٱنشُزُوا۟ يَرْفَعِ ٱللَّهُ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟
مِنكُمْ وَٱلَّذِينَ أُوتُوا۟ ٱلْعِلْمَ دَرَجَـٰتٍ ۚ وَٱللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرٌ ﴿١١﴾

*"Enyi mlioamini mnapoambiwa (katika mikutano): "Wafanyieni wasaa wenzenu katika (nafasi za) kukaa", wafanyieni nafasi. Na Mwenyezi Mungu atakufanyieni nafasi (Duniani na Akhera). Na (hata) ikisemwa, "Simameni", (ondokeni muwapishe wenzenu), basi ondekeni. Mwenyezi Mungu atawainua wale walioamini miongoni mwenu, waliopewa elimu watapata daraja zaidi. Na Mwenyezi Mungu anazo habari za mnayoyatenda". (58:11)*

Ili mtu aheshimiwe hana budi kujiheshimu yeye mwenyewe na kuwaheshimu wengine.Mtu asiyejiheshimu hujidharaulisha yeye mwenyewe kwa wanaadamu wenzake. Muheshimiwa zaidi mbele ya Allah ni yule anayemheshimu na kumtii Allah (s.w) na Mtume wake.

... إِنَّ أَكْرَمَكُمْ عِندَ ٱللَّهِ أَتْقَىٰكُمْ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ عَلِيمٌ خَبِيرٌ ﴿١٣﴾

*"... Hakika aheshimiwaye sana miongoni mwenu mbele ya Allah ni yule amchaye Allah zaidi katika nyinyi. Kwa yakini Allah ni Mjuzi Mwenye habari(za mambo yote)." (49:13)*

## 22. Kuwa Mpole na Mnyenyekevu

Mtu mpole ni yule aliyetulia, asiyelipuka kwa hamaki. Huzungumza na watu kwa sauti ya chini. Akiudhiwa halipuki kwa hasira na kupaza sauti bali husubiri kwa utulivu. Huwa ni mwepesi wa kuwasamehe waliomkosea. Muumini hana budi kujipamba na sifa hii ya upole kwani ni miongoni mwa sifa za waja wema wa Allah (s.w)

وَعِبَادُ ٱلرَّحْمَـٰنِ ٱلَّذِينَ يَمْشُونَ عَلَى ٱلْأَرْضِ هَوْنًا وَإِذَا خَاطَبَهُمُ
ٱلْجَـٰهِلُونَ قَالُوا۟ سَلَـٰمًا ﴿٦٣﴾

*"Na waja wa Rahman ni wale wanokwenda (na kurejea) katika ardhi kwa unyenyekevu; na wajinga wakisema nao (maneno mabaya) huwajibu (maneno ya) salama". (25:63)*

Pamoja na kujipamba na tabia ya upole, Waislamu hawaruhusiwi kuyaachia maovu yakafanyika katika jamii bila ya kuyakemea. Ni juu ya Waumini kuamrisha mema na kukataza maovu na kuwa wagumu kwa maadui wa Uislamu na wenye kuhurumiana wao kwa wao. Hii ndiyo tabia ya Mtume na Maswahaba wake kama tunavyojifunza katika Qur'an:

مُّحَمَّدٌ رَّسُولُ ٱللَّهِ ۚ وَٱلَّذِينَ مَعَهُۥٓ أَشِدَّآءُ عَلَى ٱلْكُفَّارِ رُحَمَآءُ بَيْنَهُمْ ۖ

*"Muhammad ni Mtume wa Allah na walio pamoja naye ni wenye nyoyo thabiti (ngumu) dhidi ya makafiri na wenye kuhurumiana wao kwa wao..." (48:29).*

Pindi maadui wakiacha uadui wao dhidi ya Uislamu, waislamu watawaelekea kwa upole:

۞ وَإِن جَنَحُوا۟ لِلسَّلْمِ فَٱجْنَحْ لَهَا وَتَوَكَّلْ عَلَى ٱللَّهِ ۚ إِنَّهُۥ
هُوَ ٱلسَّمِيعُ ٱلْعَلِيمُ ﴿٦١﴾ وَإِن يُرِيدُوٓا۟ أَن يَخْدَعُوكَ فَإِنَّ حَسْبَكَ ٱللَّهُ ۚ
هُوَ ٱلَّذِىٓ أَيَّدَكَ بِنَصْرِهِۦ وَبِٱلْمُؤْمِنِينَ ﴿٦٢﴾

*"Na kama (hao maadui) wakielelekea katika amani, wewe pia ielekee (amani) na mtegemee Allah. Hakika yeye ndiye asikiaye na ajuaye.Na kama wakitaka kukuhadaa basi Allah atakutosheleza. Yeye ndiye aliyekusaidia kwa nusura yake na kwa walioamini". (8:61-62).*

## 23. Kuwa mwenye Huruma

Muumini hana budi kujipamba na tabia ya kuwahurumia viumbe wenzake. Amuoonee huruma kila mwenye shida na ajitahidi kumsaidia iwezekanavyo. Katika kuonesha umuhimu wa kipengele hiki cha tabia njema Mtume (s.a.w) amesema:

*"Ambaye hahurumii watu, pia Allah (s.w) hatamuhurumia". (Bukhari).*

Huruma hudhihiri katika kuwasaidia wenye shida na matatizo kwa mali na kauli njema kama tunavyojifunza katika Qur-an:

لَن تَنَالُوا۟ ٱلْبِرَّ حَتَّىٰ تُنفِقُوا۟ مِمَّا تُحِبُّونَ ۚ وَمَا تُنفِقُوا۟ مِن شَىْءٍ
فَإِنَّ ٱللَّهَ بِهِۦ عَلِيمٌ ﴿٩٢﴾

*"Hamtaweza kuufikia wema mpaka mtoe katika vitu mnavyovipenda, na chochote mnachokitoa, basi hakika Allah anakijua". (3:92).*

۞ لَّيْسَ ٱلْبِرَّ أَن تُوَلُّوا۟ وُجُوهَكُمْ قِبَلَ ٱلْمَشْرِقِ وَٱلْمَغْرِبِ
وَلَـٰكِنَّ ٱلْبِرَّ مَنْ ءَامَنَ بِٱللَّهِ وَٱلْيَوْمِ ٱلْـَٔاخِرِ وَٱلْمَلَـٰٓئِكَةِ وَٱلْكِتَـٰبِ
وَٱلنَّبِيِّـۧنَ وَءَاتَى ٱلْمَالَ عَلَىٰ حُبِّهِۦ ذَوِى ٱلْقُرْبَىٰ وَٱلْيَتَـٰمَىٰ وَٱلْمَسَـٰكِينَ
وَٱبْنَ ٱلسَّبِيلِ وَٱلسَّآئِلِينَ وَفِى ٱلرِّقَابِ

*"Sio wema (tu) kuwa mnaelekeza nyuso zenu upande wa Mashariki na Magharibi. Bali wema (hasa) ni (wale) wanaomwamini Allah na Siku ya Mwisho na Malaika na Kitabu na Manabii, wanawapa mali, juu ya kuwa wanayapenda, jamaa na mayatima na maskini na wasafiri (walioharibikiwa) na waombao na katika kuwakomboa watumwa..." (2:177*

• وَبِٱلْوَٰلِدَيْنِ إِحْسَانًا وَذِى ٱلْقُرْبَىٰ وَٱلْيَتَـٰمَىٰ وَٱلْمَسَـٰكِينِ
وَقُولُوا۟ لِلنَّاسِ حُسْنًا • • • ﴿٨٣﴾

*"… Na wafanyie wema wazazi na jamaa na yatima na maskini na semeni na watu kwa wema…" (2:83).*

Pamoja na kuonyesha huruma kwa wanaadam wenzetu, Uislamu pia umetutaka tuwe na huruma kwa wanyama. Tunafahishwa katika hadith kuwa mtu mmoja alimuambia Mtume:

*Ee Mtume wa Allah! Ninapochinja mbuzi ninajaribu kumuonea huruma. Mtume (saw) akasema: "Kama utamuonea huruma , Huruma ya Allah itakuwa juu yako". (Hakim)*

Pia katika hadith nyingine Mtume (saw) amesema:

*"Mwanamke mkosefu alimuona mbwa akiwa anachungulia kisima, siku ya joto kali na ulimi wake ukiwa umening'inia kuonyesha kiu kali aliyokuwa nayo. Alimuonea huruma na akamtekea maji na chombo chake. Kutokana na kitendo chake hiki (cha kumuhurumia mbwa), alipata uokovu". (Muslim)*

Pia Hadith ifuatayo inatuonyesha kuwa waislam wanatakiwa

wanyooshe mkono wa huruma kwa viumbe vyote vilivyo hai. Mtume (saw) amesema:

> *"Wahurumie waliomo ardhini, na yule aliyopo mbinguni atawamiminia huruma yake"*

Kinyume chake kuwa katili kwa wanyama ni kitendo cha dhambi kinachoweza kumuingiza mtu motoni. Mtume (saw) amesema:

> *Mwanamke alitiwa motoni kwa sababu alimfunga paka bila ya kumlisha au kumwachia huru, ambapo angaliweza kwenda huku na huku na kujilisha kutokana na wadudu , n.k. (Bukhari)*

Kutokana na Hadith hizi tujue kuwa Allah (sw) hata turehemu iwapo tutakuwa wakatili kwa wanaadamu wenzetu na viumbe wengine.

## 24. Kuwa na Haya

Kuwa na haya ni miongoni mwa tabia njema. Mtu mwenye haya ni yule anayejichunga na maovu na mambo ya aibu. Kuhusu umuhimu wa kuwa na haya, tunajifunza katika Hadithi zifuatazo:

> *Abu Hurairah amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: Haya ni sehemu ya imani na imani mahali pake ni Peponi; na uchafu (uovu) ni sehemu ya ugumu wa moyo na ugumu wa moyo mahali pake ni Motoni. (Ahmad, Tirmidh).*

> *Ibn Mas'ud amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: Miongoni mwa ujumbe watu waliopokea kutokana na mafundisho ya mwanzo ya Utume ni: Wakati unapokuwa huna haya, fanya ulitakalo. (Bukhari).*

Hapa ina maana kuwa mtu asiye na haya hachagui la kufanya au la kusema. Pia Mtume (s.a.w) amesema katika Hadithi iliyosimuliwa na Imran bin Husain kuwa:

> *Haya haileti kitu kingine ila uzuri na katika maelelezo mengine; Haya ni nzuri katika kila hali. (Bukhari na Muslim).*

Mtume (s.a.w) ambaye ndiye kiigizo chetu alikuwa ni mwenye haya sana kama Hadithi ifuatayo inavyobainisha:

*Abu Said al-Khudri (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah alikuwa na haya zaidi kuliko wasichana vigori ndani ya mitandio yao. Alipoona kitu kisichopendeza kwake tulikuwa tunakigundua kutokana na uso wake. (Bukhari na Muslim).*

Muislamu anatakiwa awe na haya katika maongezi, katika kuangalia na katika kujisitiri uchi na katika kufanya kila jambo. Haya ni ngao ya kumuepusha mja na mambo maovu na machafu. Wa kwanza anayestahiki kuonewa haya ni Allah (s.w) kwani mwanaadamu hana kificho chochote cha kumsitiri asionekane kwake. Hivyo mja anayemuamini Allah (s.w) atamuonea haya na kujiepusha na maovu na machafu katika maisha yake yote popote atakapokuwa.

## 25. Kuwa na Upendo

Upendo ni matunda ya vipengele vingi vya tabia njema vikiunganishwa pamoja. Kwa mfano kuongea na watu vizuri, kuwahurumia wakati wanamatatizo au kuwafanyia wema wa aina yoyote kama kuwasaidia kazi, kuwakirimu kitu n.k. ni miongoni mwa maadili mema yanayoleta upendo na mahusiano mema kati ya wanaadamu. Kinyume chake, kauli mbaya, ukatili, usengenyi, fitina, uchochezi, husuda, na matendo mengine mabaya kama haya yakitendwa kwa wanadam hujenga chuki na uadui.

Uislamu unatutaka tudumishe upendo kati yetu kwa kuwafanyia wenzetu mema tunayoyapenda na ambayo tungeliwataka wengine watufanyie. Pamoja na kusisitizwa na Uislamu kuwafanyia wengine mema na kujiepusha na kuwaudhi, tunashauriwa pia tuwe na tabia ya kupeana zawadi ili kukaza imara zaidi kifungo cha uhusianao mwema na upendo. Muislamu anashuriwa ajitahidi kutoa zawadi kuwapa wengine kila anapopata fursa ya kufanya hivyo na pia anashauriwa kupokea zawadi kwa moyo mkunjufu kila anapo pewa hata kama yeye ni tajiri na huyo anayempa ni maskini. Hebu turejee Hadith zifuatazo tuone jinsi Mtume (saw) anavyotuelekeza katika kupeana na kupokea zawadi:

*Aysha(ra) amesimulai kuwa Mtume wa Allah amesema: Peaneni zawadi, kwani zawadi inaondoa chuki. (Tirmidh)*

*Aysha (ra) ameeleza kuwa Mtume wa Allah alikuwa akipokea zawadi akirudisha kitu kingine badala yake kama badilisho kumpa yule aliyetoa. (Bukhari).*

*Jabir amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: Yeyote yule aliyepewa zawadi na akawa na uwezo, na airudishie kwa zawadi nyingine , na yule ambaye hana kitu cha kurejesha , na atoe shukurani na yule asiyetoa ahsante, ni mkosefu wa shukurani, na yule anayejifanya amepewa kitu na huku hakupewa, anakuwa kama yule aliyevaa magwanda(nguo) mawili ya uwongo ( ni mwongo mkubwa-mnafiki). (Tirmidh, Abu-Daud).*

Hadith hizi mbili zinatufahamisha kuwa zawadi isielekee upande mmoja tu bali kila anayepokea zawadi naye ajitahidi, kutoa zawadi ya namna nyingine kwa yule aliyempa kama ana uwezo na kama hana cha kutoa atoe ahsante na kumuombea dua aliye mzawadia.

Si tabia ya kiislamu kukataa zawadi- ya aina yoyote iliyohalali. Tunajifunza hili kutokana na hadith zifuatazo:

*Abu Hurairah ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: Ningalikaribishwa unyayo wa mguu wa mbuzi (uliopikwa) hakika ningalikaribia na ningalipewa zawadi ya mguu wa mbuzi, hakika ningali pokea. (Bukhari).*

*Anas amesimulia kuwa Mtume wa Allah alikuwa harudishi manukato yoyote (aliyopewa kama zawadi). (Bukhari)*

*Ibn Sayid amesimulia: "Omar aliniteua kukusanya Zakat. Nilipo maliza na kuwasilisha zakat yote kwake, aliamuru nipwe ujira wangu. Nilisema: Nilifanya kwa ajili ya Allah na ujira wangu uko kwa Allah. Alisema: chukua kile ulichopewa kwa sababu niliteuliwa kufanya kazi kama hiyo wakati wa Mtume wa Allah. Aliniteua nikasema namna unavyosema. Mtume wa Allah akaniambia: unapopewa kitu ambacho hukukiomba, basi kula na toa sadaqa. (Abu Daud).*

Hadith zote hizi zinatufundisha kuwa Muislamu akipewa kitu chochote cha halali asikatae hata kikiwa kidogo namna gani. Na kama hakihitajii sana, basi akipokee kisha atoe sadaqa. Pia tunapata fundisho kuwa Muislamu akikaribishwa na mwenziwe kula kitu chochote kilicho halali asikatae. Alimradi madhumuni ya kutoa na kupokea zawadi siku zote yawe ni kuzidisha upendo, udugu na mahusiano mema kati ya Waislamu na wanaadamu wote kwa ujumla.

Pia kutoleana salamu ni miongoni mwa nyenzo za kujenga upendo baina ya watu kama tunavyojifunza katika Hadith ifuatayo:

*Abu Hurairah (ra) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema; "Hamtaingia Peponi mpaka mwamini na hamtaamini mpaka mpendane. Je, nisikufahamisheni juu ya jambo ambalo mkilifanya mtapendana? Toleaneni salamu baina yenu" (Muslim)*

## 26. Kujiepusha na Chuki na Uadui

Muislamu anatakiwa kwa kadiri ya uwezo wake ajitahidi kujiepusha na matendo yote yale yatakayosababisha kutoelewana baina yake na watu wengine. Ajiepushe na kujenga chuki na uadui moyoni mwake dhidi ya mtu yeyote na ajitahidi kujiepusha na kuwafanyia wengine yale yote yatakayowafanya wajenge chuki na uadui dhidi yake au dhidi ya watu wengine. Mtume (s.a.w) anatuusia:

*"Msikate uhusiano, msijiingize katika uadui, msikaribishe chuki na husuda dhidi ya wengine na msiwadharau wengine. Kuweni ndugu kati yenu na kuweni watumwa wa Allah. Hapana ruhusa kwa mtu kukata uhusiano na ndugu yake zaidi ya siku tatu". (Bukhari).*

Katika Hadithi nyingine imeelezwa kuwa Mtume (s.a.w) amesema: *Hairuhusiwi kwa Muislamu kuvunja uhusiano na Muislamu mwenzake zaidi ya siku tatu. Baada ya siku tatu kupita na ikatokea akakutana na ndugu yake, ni lazima amsalimu. Kama ataitikia salamu basi wote watapata thawabu (ujira) na kama hataitikia salaam, dhambi zitakuwa juu yake (yule asiyeitikia) na yule aliyeanza kutoa salaam atakuwa hana hatia na dhambi ya kukata uhusiano. (Abu Daud).*

Kama Waislamu, kwa bahati mbaya, imetokea wamegombana, waislamu wengine wanawajibika kuwasuluhisha. Kuwapatanisha waliogombana ni amri ya Allah (s.w) kama ilivyo katika aya ifuatayo:

إِنَّمَا ٱلْمُؤْمِنُونَ إِخْوَةٌ فَأَصْلِحُوا۟ بَيْنَ أَخَوَيْكُمْ ۚ وَٱتَّقُوا۟ ٱللَّهَ

لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ ﴿١٠﴾

*"Kwa hakika Waislamu wote ni ndugu, basi patanisheni baina ya ndugu zenu na mcheni Allah ili mrehemewe". (49:10)*

Katika kusuluhishwa, yule aliyemkosea mwenzake hana budi kukiri makosa yake na kisha kumtaka samahani yule aliyemkosea. Mtume (s.a.w) ametuusia:

*Yule ambaye amehujumu haki au heshima ya ndugu yake hana budi kumtaka samahani leo kabla ya siku hiyo kuja ambayo hatakuwa na dirham wala dinar (za kulipa); kama atakuwa na amali njema, basi zitachukuliwa kiasi kile kinacholingana na hujuma aliyomfanyia ndugu yake. Kama hatakuwa na amali yoyote njema, basi madhambi ya yule aliyedhulumiwa yatachukuliwa na kuwekwa katika hesabu yake." (Bukhari).*

Chuki na uadui ni kazi ya shetani. Penye chuki na uadui hapana jema lolote linalofanyika na ni furaha kwa shetani. Chuki inayoruhusiwa kwa waislamu ni ile ya kuchukia uovu na maadui wa Allah (s.w) - maadui wa Uislamu na Waislamu. Waislamu wanakatazwa kuwa na urafiki na maadui wa Allah (s.w):

يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ لَا تَتَّخِذُوا۟ عَدُوِّى وَعَدُوَّكُمْ أَوْلِيَآءَ
تُلْقُونَ إِلَيْهِم بِٱلْمَوَدَّةِ وَقَدْ كَفَرُوا۟ بِمَا جَآءَكُم مِّنَ ٱلْحَقِّ . . . ﴿١﴾

*"Enyi mlioamini! Msiwafanye adui zangu na adui zenu kuwa marafiki, mnawapelekea (habari zenu) kwa ajili ya urafiki hali ya kuwa wameshaikanusha haki iliyokujieni..." (60:1)*

يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ لَا تَتَوَلَّوْا۟ قَوْمًا غَضِبَ ٱللَّهُ عَلَيْهِمْ قَدْ يَئِسُوا۟ مِنَ
ٱلْـَٔاخِرَةِ كَمَا يَئِسَ ٱلْكُفَّارُ مِنْ أَصْحَـٰبِ ٱلْقُبُورِ ﴿١٣﴾

*"Enyi mlioamini! Msifanye urafiki na watu ambao Mwenyezi Mungu amewakasirikia; na wamekata tamaa ya kupata malipo ya Akhera kama walivyokata tamaa makafiri walio makaburini" (60:13)*

يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ لَا تَتَّخِذُوا۟ ٱلَّذِينَ ٱتَّخَذُوا۟ دِينَكُمْ هُزُوًا وَلَعِبًا
مِّنَ ٱلَّذِينَ أُوتُوا۟ ٱلْكِتَـٰبَ مِن قَبْلِكُمْ وَٱلْكُفَّارَ أَوْلِيَآءَ ۚ وَٱتَّقُوا۟ ٱللَّهَ
إِن كُنتُم مُّؤْمِنِينَ ﴿٥٧﴾

*"Enyi mlioamini! Msiwafanye marafiki wale walioifanyia mzaha na mchezo dini yenu miongoni mwa wale waliopewa kitabu kabla yenu na miongoni mwa makafiri.Na mcheni Mwenyezi Mungu kama nyinyi ni wenye*

*kuamini. (5:57)*

Pamoja na hivyo haina maana Waislamu wasiwafanyie uadilifu hawa maadui wa Allah na maadui wa Uislamu, bali Waislamu wataendelea kuwatendea wema na kuishi nao kwa wema iwapo watataka amani.

## 27. Kuwa Mwenye Kusamehe

Muislamu anatakiwa ajenge tabia ya kuwavumilia wengine. Awe na tabia ya kujihesabu. Ajione kuwa naye kama binaadamu wenzake ni mkosaji na angependa asamehewe na wale aliowakosea kwa makusudi au kwa bahati mbaya. Kitendo cha kuwasamehe wale waliokukosea ni kitendo cha ucha Mungu chenye malipo makubwa mbele ya Allah (s.w) kama inavyobainishwa katika aya zifuatazo:

۞وَسَارِعُوٓاْ إِلَىٰ مَغۡفِرَةٖ مِّن رَّبِّكُمۡ وَجَنَّةٍ عَرۡضُهَا ٱلسَّمَٰوَٰتُ وَٱلۡأَرۡضُ
أُعِدَّتۡ لِلۡمُتَّقِينَ ﴿١٣٣﴾ ٱلَّذِينَ يُنفِقُونَ فِي ٱلسَّرَّآءِ وَٱلضَّرَّآءِ وَٱلۡكَٰظِمِينَ
ٱلۡغَيۡظَ وَٱلۡعَافِينَ عَنِ ٱلنَّاسِۗ وَٱللَّهُ يُحِبُّ ٱلۡمُحۡسِنِينَ ﴿١٣٤﴾

*"Na yaendeeni upesi upesi maghufira ya Mola wenu na Pepo (yake) ambayo upana wake (tu) ni (sawa na) mbingu na ardhi. (Pepo) iliyowekewa wamchao Mungu. Ambao hutoa katika (hali ya) wasaa na katika (hali ya) dhiki, na wazuiyao ghadhabu na wanasamehe watu na Mwenyezi Mungu anawapenda wafanyao ihsani." (3:133-134)*

فَمَآ أُوتِيتُم مِّن شَيۡءٖ فَمَتَٰعُ ٱلۡحَيَوٰةِ ٱلدُّنۡيَاۖ وَمَا عِندَ ٱللَّهِ خَيۡرٞ وَأَبۡقَىٰ
لِلَّذِينَ ءَامَنُواْ وَعَلَىٰ رَبِّهِمۡ يَتَوَكَّلُونَ ﴿٣٦﴾

*"Basi vyote hivi mlivyopewa ni starehe ya maisha ya dunia tu, lakini kilichoko kwa Mwenyezi Mungu ni bora na cha kudumu (milele). Watakistahiki wale walioamini na wakawa wanamtegemea Mola wao.(42:36)*

وَٱلَّذِينَ يَجۡتَنِبُونَ كَبَٰٓئِرَ ٱلۡإِثۡمِ وَٱلۡفَوَٰحِشَ وَإِذَا مَا غَضِبُواْ
هُمۡ يَغۡفِرُونَ ﴿٣٧﴾

*"Na wale wanaojiepusha na madhambi makubwa na mambo*

*mabaya, na wale ambao wanapokasirika husamehe. (42:37)*

Mwenye kuwasamehe wengine husamehewa makosa yake na Allah (s.w).

وَلَا يَأْتَلِ أُولُوا الْفَضْلِ مِنكُمْ وَالسَّعَةِ أَن يُؤْتُوا أُولِي الْقُرْبَىٰ وَالْمَسَاكِينَ
وَالْمُهَاجِرِينَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ ۖ وَلْيَعْفُوا وَلْيَصْفَحُوا ۗ أَلَا تُحِبُّونَ أَن يَغْفِرَ
اللَّهُ لَكُمْ ۗ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٢٢﴾

*"Na wasiape wale wenye mwendo mzuri (waumini) na wenye wasaa (katika maisha yao) miongoni mwenu (wasiape kujizuia) kuwapa walio jamaa na maskini na waliohama kwa njia ya Mwenyezi Mungu; na waachilie mbali, (wapuuze yaliyopita). Je, nyinyi hampendi Mwenyezi Mungu akusameheni? Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa msamaha (na) Mwingi wa Rehema. (24:22).*

Naye Mtume (s.a.w) anatufahamisha ubora wa kusamehe katika Hadithi zifuatazo:

*'Uqbah bin Amir (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: "Ee 'Uqbah! Je, nikufahamishe juu ya watu wema kuliko wote katika dunia hii na akhera?" Alijibu Ndio, akasema (Mtume): "Utaendeleza uhusiano mwema na mtu aliyevunja uhusiano kati yako na yeye; utampa yule aliyekunyima; na utamsamehe yule aliyekudhulumu". (Baihaqi).*

*Abu Hurairah (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema kuwa Mussa (a.s), mwana wa Imran, aliuliza: Ee Mola wangu! Nani, katika waja wako anayeheshimika (mwenye hadhi) zaidi mbele yako? (Allah) alimjibu: Yule anayesamehe ambapo ana nguvu au uwezo (wa kutosamehe). (Baihaqi).*

Hivyo Allah (s.w) anatuusia:

خُذِ الْعَفْوَ وَأْمُرْ بِالْعُرْفِ وَأَعْرِضْ عَنِ الْجَاهِلِينَ ﴿١٩٩﴾

*"Shikamana na kusamehe na amrisha mema na wapuuze majahili..." (7:199)*

Kukataa kusamehe baada ya kuombwa msamaha na yule aliyekukosea ni jambo ovu. Allah (s.w) hamsamehi yule asiyesamehe wanaadamu wenzake. Ukweli ni kwamba wanayotukosea wanaadamu wenzetu hata tuyaone ni makubwa vipi, ni madogo sana ukilinganisha na makosa yetu kwa Allah (s.w). Inakuwaje sasa tushindwe kusamehe haya makosa madogo madogo na wakati huo tunatamani kusamehewa milima na milima ya makosa yetu?

Hivyo, yule anayetaka kusamehewa na Allah(s.w), basi awe mwepesi wa kuwasamehe wanaadamu wenzake. Kuhusu uovu wa kukataa kuwasamehe wale waliokiri makosa yao na kuomba msamaha, anasema Mtume (s.a.w):

*Kama mtu, anakiri makosa yake kwa mwingine na kutaka msamaha, na yule akakataa kutoa msamaha, basi hatanyweshwa maji ya kawthar (huyo aliyekataa, kusamehe). (Tabrani).*

## 28. Kudhibiti Hasira

Kujizuia na hasira ni tabia njema inayoambatana na tabia ya kusamehe. Hasira humpata mtu anapoudhiwa. Wakati mwingine huja ghafla na kumnyima mtu wakati wa kufikiri. Hasira zinaongozwa na shetani, hivyo humnyima mtu nafasi ya kutumia akili, hekima na busara. Hivyo humpelekea mtu kufanya matendo ambayo hugeuka kuwa majuto baadaye. Hasira hasara. Kujizuilia na hasira ni kitendo cha ucha Mungu chenye malipo makubwa mbele ya Allah (s.w). Rejea Qur-an (3:133-134) na (42:36-37). Pia ubora wa kujizuilia na hasira unadhihirika katika Hadithi zifuatazo:

*Abu Hurairah(r.a) amesimulia kuwa mtu mmoja alimuomba Mtume (s.a.w): "Niwaidhi'. Mtume akasema: "Usighadhibike". Kisha akarudia mara nyingi akisema: Usighadhibike. (Bukhari)*

*Abu Hurairah(r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema "Mtu mwenye nguvu si bingwa wa mieleka bali mtu mwenye nguvu ni yule anayejizuilia na hasira". (Bukhari na Muslim).*

*Ibn Umar amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: "Hapana mja aliyemeza kidonge kichungu mbele ya Allah (s.w) kuliko kidonge cha hasira alichokimeza, huku akitaraji radhi ya Allah (s.w)". (Ahmad).*

Mbinu za kujizuia na hasira zimebainishwa katika Qur-an kama ifuatavyo:

خُذِ ٱلْعَفْوَ وَأْمُرْ بِٱلْعُرْفِ وَأَعْرِضْ عَنِ ٱلْجَٰهِلِينَ ﴿١٩٩﴾ وَإِمَّا

يَنزَغَنَّكَ مِنَ ٱلشَّيْطَٰنِ نَزْغٌ فَٱسْتَعِذْ بِٱللَّهِ ۚ إِنَّهُۥ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿٢٠٠﴾

"*Shikamana na kusamehe na amrisha mema na wapuuze majahili (wajinga). Na kama wasi wasi wa shetani ukikusumbua basi (sema: Audhubillah) jikinge kwa Mwenyezi Mungu. Bila shaka yeye ndiye asikiaye na ajuaye." (7:199-200).*

Kutokana na aya hizi tunajifunza kuwa mbinu za kujizuilia na hasira ni hizi zifuatazo:

(i) Kushikamana na kusamehe.
(ii) Kushikamana na kuamrisha mema.
(iii) Kuwapuuza majahili.
(iv) Kujikinga kwa Allah (s.w) na uovu wa shetani.

Pia Mtume (s.a.w) anatupa mbinu nyingine za kupambana na hasira katika Hadithi zifuatazo:

*Atiyyah bin Urwah Ba'id(r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: "Hakika hasira zinatoka kwa Shetani, na Shetani ameumbwa kutokana na moto na hakika moto huzimishwa na maji. Kwa hiyo yoyote miongoni mwenu atakayepandwa na hasira, na atawadhe". (Abu Daud).*

*Abu Dharr (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: "Wakati wowote mmoja wenu atakapopandwa na hasira akiwa amesimama, na akae chini. Kama (kwa kufanya hivyo) hasira itamtoka ni vyema; lakini kama haitatoka, na alale chini". (Ahmad, Tirmidh).*

Kutokana na Hadithi hizi Mtume (s.a.w) anatuelekeza tupunguze hasira zetu kwa:

(i) Kutia udhu.
(ii) Kukaa chini iwapo tumesimama.
(iii) Kulala chini.

### 29. Kuwa mwenye Subira na Uvumilivu

Subira ni kitendo cha kuwa na uvumilivu na utulivu baada ya kupatwa na matatizo au misuko suko mbali mbali katika maisha ya kila siku. Muislamu anatakiwa awe ni mwenye kusubiri baada ya kupata shida au matatizo kama tunavyoamrishwa katika Qur-an:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ ٱسْتَعِينُوا۟ بِٱلصَّبْرِ وَٱلصَّلَوٰةِ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ مَعَ ٱلصَّٰبِرِينَ

*“Enyi mlioamini! Jisaidieni (katika mambo yenu) kwa kusubiri na kuswali. Bila shaka Allah yupo pamoja na wanaosubiri” (2:153)*

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ ٱصْبِرُواْ وَصَابِرُواْ وَرَابِطُواْ وَٱتَّقُواْ ٱللَّهَ لَعَلَّكُمْ
تُفْلِحُونَ ٢٠٠

*“Enyi mlioamini! Subirini na washindeni wengine wote kwa kusubiri na kuweni imara na mcheni Allah mpate kufaulu”. (3:200)*

Suala la kupatwa na matatizo, misiba na misukosuko mbali mbali ni jambo la kawaida katika maisha ya hapa duniani. Hatuna budi kufahamu kuwa ulimwengu huu haukukusudiwa na Mola Muumba uwe Pepo. Bali umekusudiwa uwe uwanja wa kumtahini mwanaadamu. Hivyo viumbe vyote vilivyomzingira pamoja na matukio na miondoko yote ya maisha viko pale kama vifaa vya kumtahini mwanaadamu. Suala la kutahiniwa mwanaadamu limewekwa bayana katika Qur-an:

إِنَّا خَلَقْنَا ٱلْإِنسَٰنَ مِن نُّطْفَةٍ أَمْشَاجٍ نَّبْتَلِيهِ فَجَعَلْنَٰهُ سَمِيعًۢا بَصِيرًا
٢ إِنَّا هَدَيْنَٰهُ ٱلسَّبِيلَ إِمَّا شَاكِرًا وَإِمَّا كَفُورًا ٣

*Kwa hakika tumemuumba mtu kutokana na mbegu ya uhai iliyochanganyika, ili tumfanyie mtihani ( kwa amri zetu na makatazo yetu) kwa hivyo tukamfanya ni Mwenye kusikia (na) mwenye kuona. Hakika Sisi tumembainishia njia . Basi (mwenyewe tena) atakuwa mwenye shukurani au awe mwenye kukufuru (76:2-3)*

تَبَٰرَكَ ٱلَّذِى بِيَدِهِ ٱلْمُلْكُ وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَىْءٍ قَدِيرٌ ١ ٱلَّذِى
خَلَقَ ٱلْمَوْتَ وَٱلْحَيَوٰةَ لِيَبْلُوَكُمْ أَيُّكُمْ أَحْسَنُ عَمَلًا ۚ وَهُوَ ٱلْعَزِيزُ
ٱلْغَفُورُ ٢

*Ametukuka yule ambaye mkononi mwake umo Ufalme (wote); naye ni mwenye uwezo juu ya kila kitu. Ambaye ameumba mauti na uhai ili kukujaribuni (kukufanyieni mtihani); ni nani miongoni mwenu mwenye vitendo vizuri zaidi. Naye ni Mwenye Nguvu na Mwenye Msamaha. (67:1-2)*

وَلَنَبْلُوَنَّكُمْ حَتَّىٰ نَعْلَمَ ٱلْمُجَٰهِدِينَ مِنكُمْ وَٱلصَّٰبِرِينَ وَنَبْلُوَا۟
أَخْبَارَكُمْ ﴿٣١﴾

*"Na tutakufanyieni mitihani mpaka tuwadhihirishe (wajulikane) wale wanaopigania dini miongoni mwenu na wanaosubiri; nasi tutadhihirisha habari zenu. (47:31)*

أَمْ حَسِبْتُمْ أَن تَدْخُلُوا۟ ٱلْجَنَّةَ وَلَمَّا يَأْتِكُم مَّثَلُ ٱلَّذِينَ خَلَوْا۟ مِن قَبْلِكُم ۖ
مَّسَّتْهُمُ ٱلْبَأْسَآءُ وَٱلضَّرَّآءُ وَزُلْزِلُوا۟ حَتَّىٰ يَقُولَ ٱلرَّسُولُ وَٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟
مَعَهُۥ مَتَىٰ نَصْرُ ٱللَّهِ ۗ أَلَآ إِنَّ نَصْرَ ٱللَّهِ قَرِيبٌ ﴿٢١٤﴾

*"Mnadhani kuwa mtaingia Peponi, na hali hamjajiwa na mfano wa (yale yaliyowajia) wale waliopita kabla yenu? Yaliwapata mashaka na madhara na wakatetemeshwa sana hata Mitume na walioamini pamoja nao wakasema: :Nusura ya Mwenyezi Mungu itafika lini?" Jueni kuwa nusura ya Mwenyezi Mungu iko karibu. (2:214).*

أَحَسِبَ ٱلنَّاسُ أَن يُتْرَكُوٓا۟ أَن يَقُولُوٓا۟ ءَامَنَّا وَهُمْ لَا يُفْتَنُونَ ﴿٢﴾ وَلَقَدْ فَتَنَّا
ٱلَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ ۖ فَلَيَعْلَمَنَّ ٱللَّهُ ٱلَّذِينَ صَدَقُوا۟ وَلَيَعْلَمَنَّ ٱلْكَٰذِبِينَ ﴿٣﴾

*Je, watu wanadhani wataachwa (wasitiwe katika misukosuko) kwa kuwa wanasema, "Tumeamini?" Basi ndio wasijaribiwe (wasipate mitihani)? Hapana; bila shaka tuliwatia katika taabu wale waliokuwa kabla yao, na kwa yakini Mwenyezi Mungu atawatambulisha wale walio wa kweli na kuwatambulisha (wale walio) waongo. (29:2-3).*

أَمْ حَسِبْتُمْ أَن تَدْخُلُوا۟ ٱلْجَنَّةَ وَلَمَّا يَعْلَمِ ٱللَّهُ ٱلَّذِينَ جَٰهَدُوا۟ مِنكُمْ
وَيَعْلَمَ ٱلصَّٰبِرِينَ ﴿١٤٢﴾

*"Je! Mnadhani mtaingia Peponi, hali Mwenyezi Mungu hajawapambanua wale waliopigania dini ya Mwenyezi Mungu miongoni mwenu, na kuwapambanua waliofanya subira?"(3:142)*

Ili kukamilisha kusudio hili la kumjaribu (kumtahini) Mwanaadamu Mwenyezi Mungu (s.w) ameupamba huu ulimwengu kwa machungu na matamu yaliyochanganyika. Uzuri au mazuri hayapatikani kwa urahisi ila mpaka kuvuka vikwazo vingi vya matatizo na misukosuko ya namna kadha wa kadhaa. Na uzuri au mazuri yanapopatikana hayabakii milele bali huwa ni ya muda mfupi kwani nayo yamezingirwa na matatizo na mikasa elfu moja na moja. Hii ndio sura halisi ya maisha ya huu ulimwengu. Kwa hiyo wale wanaodhania ulimwengu huu ni mahali pa starehe - kufurahia maisha tu bila ya kuonja machungu yake watakuwa wamejidanganya mno na badala yake wataishi maisha ya huzuni, wasiwasi na kukata tamaa. Kinyume chake, Waislamu wanatakiwa wawe na uhakika juu ya maisha ya huu ulimwengu kuwa ni ya majaribio na mafanikio yatapatikana kwa kutenda wema kwa ajili ya Allah (s.w) na kusubiri au kustahamili mazito, matatizo na misukosuko yote ya maisha itakayowakabili.

Kufanya subira si jambo jepesi bali ni jambo linalohitaji jitihada na azma kubwa. Hebu turejee usia wa Mzee Luqman kwa Mwanae:

يَٰبُنَيَّ أَقِمِ ٱلصَّلَوٰةَ وَأۡمُرۡ بِٱلۡمَعۡرُوفِ وَٱنۡهَ عَنِ ٱلۡمُنكَرِ
وَٱصۡبِرۡ عَلَىٰ مَآ أَصَابَكَۖ إِنَّ ذَٰلِكَ مِنۡ عَزۡمِ ٱلۡأُمُورِ ١٧

*"Ewe Mwanangu! Simamisha swala, na uamrishe mema, na ukataze mabaya, na usubiri juu ya yale yatakayokusibu (kwani mwenye kuamrisha mema na kukataza mabaya lazima zitamfika tu taabu); Hakika hayo ni katika mambo yanayostahiki kuazimiwa (na kila mtu). (31:17)*

وَلَمَن صَبَرَ وَغَفَرَ إِنَّ ذَٰلِكَ لَمِنۡ عَزۡمِ ٱلۡأُمُورِ ٤٣

*Na anayesubiri na kusamehe (atalipwa wema wake). Bila shaka hilo ni katika mambo makubwa ya kuazimiwa kufanywa (na kila Muislamu). (42:43).*

Kufanya subira ni kitendo cha hali ya juu cha Ucha Mungu na Mwenyezi Mungu (s.w) Ameahidi malipo makubwa kwa yule atakayejitahidi kusubiri kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

قُلۡ يَٰعِبَادِ ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ ٱتَّقُواْ رَبَّكُمۡۚ لِلَّذِينَ أَحۡسَنُواْ فِي هَٰذِهِ ٱلدُّنۡيَا
حَسَنَةٞۗ وَأَرۡضُ ٱللَّهِ وَٰسِعَةٌۗ إِنَّمَا يُوَفَّى ٱلصَّٰبِرُونَ أَجۡرَهُم بِغَيۡرِ حِسَابٖ

*Sema: "Enyi waja wangu mlioamini! Mcheni Mola wenu. Wale wafanyao wema katika dunia hii watapata wema; na ardhi ya Allah ina wasaa. Na bila shaka wafanyao subira watapewa ujira wao pasipo hisabu". (39:10)*

وَلَنَبْلُوَنَّكُم بِشَيْءٍ مِّنَ ٱلْخَوْفِ وَٱلْجُوعِ وَنَقْصٍ مِّنَ ٱلْأَمْوَٰلِ
وَٱلْأَنفُسِ وَٱلثَّمَرَٰتِ ۗ وَبَشِّرِ ٱلصَّٰبِرِينَ ﴿١٥٥﴾ ٱلَّذِينَ إِذَآ
أَصَٰبَتْهُم مُّصِيبَةٌ قَالُوٓا۟ إِنَّا لِلَّهِ وَإِنَّآ إِلَيْهِ رَٰجِعُونَ ﴿١٥٦﴾ أُو۟لَٰٓئِكَ
عَلَيْهِمْ صَلَوَٰتٌ مِّن رَّبِّهِمْ وَرَحْمَةٌ ۖ وَأُو۟لَٰٓئِكَ هُمُ ٱلْمُهْتَدُونَ ﴿١٥٧﴾

*"Na tutakutieni katika msukosuko wa (baadhi ya mambo haya); hofu na njaa na upungufu wa mali na wa watu na wa matunda. Na wapashe habari njema wanaosubiri. Ambao uwapatapo msiba husema: "Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu, na kwake Yeye tutarejea (atatupa jaza yake)" Hao juu yao zitakuwa baraka zitokazo kwa Mola wao na rehema; na ndio wenye kuongoka. (2:155-157)*

Pia Mtume (s.a.w) anatufahamisha kuwa malipo ya subira ni Pepo na kusamehewa madhambi kama tunavyojifunza katika Hadithi zifuatazo:

*Abu Hurairah (r.a) amehadithia kuwa Mtume wa Allah amesema, Mwenyezi Mungu (s.w) amesema, "Sina malipo mengine ila Pepo kwa mja wangu aliyeamini ambaye anasubiri wakati ninapomchukulia kipenzi chake kutoka miongoni mwa wakazi wa ulimwengu". (Bukhari).*

*Anas (r.a) amesimulia kuwa amemsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu akisema kuwa Allah (s.w) amesema, "Ninapomtia msuko suko mja wangu katika vitu vyake viwili vipenzi (macho yake) na akatulia kwa subira, nitamlipa macho yake kwa Pepo" (Bukhari).*

*Abu Said na Abu Hurairah(r.a) wameeleza kuwa wamemsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu akisema: Aslani Muumini hafikwi na makero (matatizo), magumu au ugonjwa, huzuni au hata wasi wasi moyoni, iwe hakusamehewa dhambi zake. (Bukhari na Muslim).*

*Imesimuliwa katika mamlaka ya Abu Hurairah kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema Muislamu mwanamume au Muislamu mwanamke ataendelea kuwa katika majaribu juu ya maisha yake, mali yake na watoto wake mpaka amkabili Mwenyezi Mungu (s.w) katika hali ambayo dhambi zake zote zimesamehewa. (Tirmidh).*

Hivyo kila Muislamu wa kweli hana budi kujitahidi kusubiri kwa lolote zito litakalomfika na ajiliwaze kwa maliwazo aliyotufunza Mwenyezi Mungu (s.w) kwa kusema:

*"...Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu na kwake yeye tutarejea".(2:156)*

... إِنَّا لِلَّهِ وَإِنَّآ إِلَيْهِ رَٰجِعُونَ ﴿١٥٦﴾

Muislamu hatakiwi achoke kusubiri wala asitamani kufa au kuomba kifo kutokana na mazito yaliyomfika:

*Anas (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema: "Pasiwe na yoyote miongoni mwenu anayetamani kufa (au anayeomba kifo) kwa sababu ya tatizo lolote lililomfika. Kama amefika mwisho wa kuvumilia naaseme: "Ee Allah nibakishe hai iwapo kuishi ni bora zaidi kwangu na nifishe kama kufa ndio bora kwangu". (Bukhari na Muslim).*

**Maeneo ya subira**

Katika Uislamu subira inatakiwa ihudhurishwe katika maeneo makuu yafuatayo:

**Kwanza:** kusubiri unapofikwa na misukosuko au matatizo mbali mbali ya kimaisha miongoni mwa khofu, kufiwa, kuugua, kuuguliwa, kukosa maslahi ya kimaisha na matatizo mengine mbali mbali yanayowafika wanaadamu katika maisha ya kila siku.

**Pili:** kusubiri au kuwa wastahimilivu katika kutekeleza maamrisho ya Allah (s.w) katika maisha yetu yote. Maamrisho kama kusimamisha swala, kufunga Ramadhan, kuwatendea wema wazazi, mayatima, maskini, majirani na wanaadam wengine, kuchunga haki za wengine, (n.k) ni matendo mja anayotakiwa aendelee kuyafanya mpaka mwisho wa maisha yake. Juu ya kusimamisha swala, tunaamrishwa katika Qur-an:

*"Na waamrishe watu wako kuswali, na uendelee mwenyewe kufanya hivyo..." (20:132).*

وَأْمُرْ أَهْلَكَ بِٱلصَّلَوٰةِ وَٱصْطَبِرْ عَلَيْهَا ۖ

**Tatu:** kusubiri au kuwa wavumilivu katika kumtii Allah (s.w) kwa kuacha yale aliyotuharamishia. Maovu mengi yaliyoharamishwa na Allah (s.w), machoni mwa mwanaadamu yanaonekana kuwa mazuri na starehe yenye mvuto mkubwa. Kwa mfano nani asiyeona jinsi ulevi, uzinifu, muziki, kamari, riba, hongo, nyama ya nguruwe, n.k. vinavyowavutia walimwengu na kuwazamisha humo mamilioni.

Mtume (s.a.w) amesema:
*Pepo imezungukwa na yasiyopendeka (vikwazo) na Moto umezungukwa na vitu vya anasa (carnal desires). (Muslim)*

**Nne:** ni kusubiri au kustahimili maudhi kutoka kwa wanadamu wenzetu. Misukosuko na matatizo mengi yanayomkabili mwanaadamu ni yale yanayosababishwa na wanaadamu wenzake. Muislamu wa kweli hatalipiza kisasi kwa maovu aliyofanyiwa na mwingine, wala hatamuapiza na kumlaani aliyemfanyia maovu hayo bali atastahimili kwa matarajio ya kupata malipo makubwa kutoka kwa Allah (s.w).

Waislamu tunatakiwa mara kwa mara tumuombe Allah (s.w) atumiminie subira kama Yeye mwenyewe anavyotuelekeza kuomba:

...رَبَّنَآ أَفۡرِغۡ عَلَيۡنَا صَبۡرًا وَتَوَفَّنَا مُسۡلِمِينَ ﴿١٢٦﴾

*"... Mola wetu! Tumiminie subira na tufishe hali ya kuwa Waislamu". (7:126)*

...رَبَّنَآ أَفۡرِغۡ عَلَيۡنَا صَبۡرًا وَثَبِّتۡ أَقۡدَامَنَا وَٱنصُرۡنَا عَلَى ٱلۡقَوۡمِ ٱلۡكَٰفِرِينَ ﴿٢٥٠﴾

*"Mola wetu! Tumiminie subira na uithibitishe miguu yetu, na utusaidie juu ya watu hawa makafiri". (2:250).*

## 30. Kuwa Mkarimu

Ukarimu ni miongoni mwa tabia njema anayotakiwa ajipambe nayo Muislamu.Muislamu anatakiwa awe mwepesi wa kuwakirimu wengine kwa kuwasaidia wakati wanapokuwa katika hali ya kuhitajia msaada bila ya kutarajia malipo yoyote kutoka kwao. Sifa ya wakarimu inabainishwa katika aya zifuatazo:

وَيُطۡعِمُونَ ٱلطَّعَامَ عَلَىٰ حُبِّهِۦ مِسۡكِينًا وَيَتِيمًا وَأَسِيرًا ﴿٨﴾

إِنَّمَا نُطْعِمُكُمْ لِوَجْهِ ٱللَّهِ لَا نُرِيدُ مِنكُمْ جَزَآءً وَلَا شُكُورًا ﴿٩﴾

*Na huwalisha chakula maskini na mayatima na wafungwa, na hali yakuwa wenyewe wanakipenda (chakula hicho). (Husema wenyewe katika nyoyo zao wanapowapa chakula hicho): "Tunakulisheni kwa ajili ya kutaka radhi ya Mwenyezi Mungu (tu) hatutaki kwenu malipo wala shukurani". (76:8-9)*

Pia kumfanyia mgeni takrima ni jambo lililowajibishwa kwa Waislamu, kama tunavyojifunza katika Hadithi zifuatazo:

*Abu Hurairah (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema, "Yule anayemuamini Allah(s.w) na siku ya mwisho hatamdhuru jirani yake, na yule anayemuamini Allah(s.w) na siku ya mwisho atamkirimu mgeni wake na yule anayemuamini Allah na siku ya mwisho ataongea mazuri au atakaa kimya". (Bukhari na Muslim).*

*Abu Shuraikh Ka'ab (r.a) amesimulia kuwa Mtume (s.a.w) amesema,"Yeyote anayemuamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho hanabudi kumkirimu mgeni wake, na jukumu lake (la kumhangaikia sana) ni mchana mmoja na usiku.Ukarimu (kwa mgeni) ni siku tatu na zaidi ya hapo ni sadaqa. Si vyema kwa mgeni kuendelea kubakia baada ya siku tatu na kuendelea kumuweka mwenyeji wake katika hali ya uzito." (Bukhari na Muslim).*

Kiigizo chetu cha ukarimu ni Mitume wa Allah. Tunafahamishwa katika Qur-an juu ya ukarimu wa Nabii Ibrahim:

هَلْ أَتَىٰكَ حَدِيثُ ضَيْفِ إِبْرَٰهِيمَ ٱلْمُكْرَمِينَ ﴿٢٤﴾ إِذْ دَخَلُوا۟ عَلَيْهِ فَقَالُوا۟ سَلَـٰمًا ۖ قَالَ سَلَـٰمٌ قَوْمٌ مُّنكَرُونَ ﴿٢٥﴾ فَرَاغَ إِلَىٰٓ أَهْلِهِۦ فَجَآءَ بِعِجْلٍ سَمِينٍ ﴿٢٦﴾ فَقَرَّبَهُۥٓ إِلَيْهِمْ قَالَ أَلَا تَأْكُلُونَ ﴿٢٧﴾

*Je! Imekujia hadithi ya wageni wahishimiwao wa (Nabii) Ibrahimu? Walipoingia kwake wakasema: "Salaam (alaykum)". Na (yeye Ibrahimu) akasema: ("Alaykumus) Salaam" (Na katika moyo wake anasema): "Ninyi watu nisiokujueni". Mara akaenda kwa ahali yake na akaleta ndama aliyenona. Akampeleka karibu yao. (Walipokuwa hawajanyosha mikono kula) alisema: "Mbona hamuli!" (51:24-27)*

*Katika hadithi, amesimulia Ibn Abbas (r.a) kuwa: Mtume (s.a.w) alikuwa mkarimu sana kuliko watu wote na alikuwa akizidisha ukarimu katika mwezi wa Ramadhan...” (Bukhari).*

Malipo ya kuwakirimu watu ni kupata takrima ya Allah (s.w) huko Peponi kama inavyobainishwa katika aya zifuatazo:

فَوَقَىٰهُمُ ٱللَّهُ شَرَّ ذَٰلِكَ ٱلْيَوْمِ وَلَقَّىٰهُمْ نَضْرَةً وَسُرُورًا ﴿١١﴾

*“Basi Mwenyezi Mungu atawalinda (wakarimu) na shari ya siku hiyo na kuwakutanisha na neema na furaha.(76:11)*

وَجَزَىٰهُم بِمَا صَبَرُوا۟ جَنَّةً وَحَرِيرًا ﴿١٢﴾ مُّتَّكِـِٔينَ فِيهَا عَلَى ٱلْأَرَآئِكِ ۖ لَا

يَرَوْنَ فِيهَا شَمْسًا وَلَا زَمْهَرِيرًا ﴿١٣﴾

*Na atawajaza mabustani (ya Peponi) na maguo ya hariri, kwa sababu ya kusubiri (kwao). Humo wataegemea viti vya enzi, hawataona humo jua (kali) wala baridi (kali).(76:12-13)*

وَدَانِيَةً عَلَيْهِمْ ظِلَـٰلُهَا وَذُلِّلَتْ قُطُوفُهَا تَذْلِيلًا ﴿١٤﴾ وَيُطَافُ

عَلَيْهِم بِـَٔانِيَةٍ مِّن فِضَّةٍ وَأَكْوَابٍ كَانَتْ قَوَارِيرَا۟

*Na vivuli vyake vitakuwa karibu yao, na mashada ya matunda yake yataning’inia mpaka chini. Na watapitishiwa vyombo vya fedha na vikombe vya vigae.(76:14-15)*

قَوَارِيرَا۟ مِن فِضَّةٍ قَدَّرُوهَا تَقْدِيرًا ﴿١٦﴾ وَيُسْقَوْنَ فِيهَا كَأْسًا كَانَ

مِزَاجُهَا زَنجَبِيلًا ﴿١٧﴾ عَيْنًا فِيهَا تُسَمَّىٰ سَلْسَبِيلًا ﴿١٨﴾ ۞ وَيَطُوفُ

عَلَيْهِمْ وِلْدَٰنٌ مُّخَلَّدُونَ إِذَا رَأَيْتَهُمْ حَسِبْتَهُمْ لُؤْلُؤًا مَّنثُورًا ﴿١٩﴾

*Vigae vya fedha; wamevijaza kwa vipimo. Na humo watanyweshwa kinywaji kilichochanganyika na tangawizi. Huo ni mto ulio humo (Peponi) unaitwa Salsabili. Na watawazungukia (kuwatumikia), wavulana wasiochakaa, ukiwaona utawafikiri ni lulu zilizotawanywa. (76: 16-19)*

وَإِذَا رَأَيْتَ ثَمَّ رَأَيْتَ نَعِيمًا وَمُلْكًا كَبِيرًا ﴿٢٠﴾ عَالِيَهُمْ ثِيَابُ
سُندُسٍ خُضْرٌ وَإِسْتَبْرَقٌ ۖ وَحُلُّوا أَسَاوِرَ مِن فِضَّةٍ وَسَقَاهُمْ رَبُّهُمْ شَرَابًا
طَهُورًا ﴿٢١﴾

*Na utakapoyaona (yaliyoko) huko utaona neema (zisizo kuwa na mfano) na ufalme mkubwa. Juu yao wana nguo za hariri laini, za kijani kibichi na za hariri nzito. Na watavikwa vikuku vya fedha, na Mola wao atawanywesha kinywaji safi kabisa (76:20-21)*

إِنَّ هَٰذَا كَانَ لَكُمْ جَزَاءً وَكَانَ سَعْيُكُم مَّشْكُورًا ﴿٢٢﴾

*"Hakika haya ni malipo yenu; na amali zenu zimekubaliwa". (76:22)*

## 31. Kuepuka Uchoyo na Ubahili

Uchoyo na ubahili ni kinyume cha ukarimu. Mtu mchoyo ana kasoro katika imani yake. Anaona kuwa chochote alichonacho amekipata kwa jitihada na akili yake tu. Pia anahofu kuwa akitoa kumpa mwingine atapungukiwa au atafilisika. Mtume (s.a.w) anatutanabahisha katika Hadithi zifuatazo:

*Abu Hurairah (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: Mtu anasema: "Hiki changu! Hiki changu! Lakini ukweli ulivyo ni kwamba, vilivyo vyake katika mali yake ni vitu vitatu: "Kile alichokula au nguo aliyoivaa ikachakaa au kile alichokitoa sadaqa (hakika) amekiweka akiba, na kingine chochote zaidi ya hivi, hakika si vyake (si vyenye kumfaa) na ataondoka awaachie watu". (Muslim)*

*Abu Hurairah (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: "Chakula cha watu wawili kina watosha watu watatu, na chakula cha watu watatu kinawatosha watu wanne".(Bukhari na Muslim)*

*Jabir bin Abdullah (r.a) ameeleza: Mtume wa Allah amesema: "Chakula cha mtu mmoja kinawatosha watu wawili na chakula cha watu wawili*

*kinawatosha watu wanne na chakula cha watu wanne kinawashibisha watu wanane". (Muslim).*

Hivyo ukizingatia Hadithi hizi, utaona kuwa hapana sababu ya Muislamu kuwa mchoyo au bahili. Uchoyo na ubahili ni tabia mbaya na malipo yake ni kwenda Motoni kama inavyobainishwa katika Qur-an:

فَأَمَّا مَنْ أَعْطَىٰ وَٱتَّقَىٰ ﴿٥﴾ وَصَدَّقَ بِٱلْحُسْنَىٰ ﴿٦﴾ فَسَنُيَسِّرُهُۥ لِلْيُسْرَىٰ
﴿٧﴾ وَأَمَّا مَنۢ بَخِلَ وَٱسْتَغْنَىٰ ﴿٨﴾ وَكَذَّبَ بِٱلْحُسْنَىٰ ﴿٩﴾ فَسَنُيَسِّرُهُۥ
لِلْعُسْرَىٰ ﴿١٠﴾ وَمَا يُغْنِى عَنْهُ مَالُهُۥٓ إِذَا تَرَدَّىٰٓ ﴿١١﴾

*Yule anayetoa (zaka na sadaka) na kumcha Mwenyezi Mungu. Na kusadiki jambo jema (akalifuata). Tutamsahilishia njia ya kwenda Peponi. Na afanyae ubakhili, asiwe na haja ya viumbe wenzake, na akakadhibisha mambo mema (asiyafanye). Tutamsahilishia njia ya kwendea Motoni. Na mali yake haitamfaa atakapokuwa anadidimia (Motoni humo). (92:5-11).*

## 32. Kuwa Mwenye Kutosheka

Kutosheka ni kuridhika na neema uliyonayo. Kutosheka ni utajiri kuliko utajiri wote uliopo ulimwenguni.

*Abu Hurairah (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema, utajiri si kuwa na mali nyingi lakini utajiri ni kutosheka". (Bukhari na Muslim)*

Muislamu anatakiwa awe ni mwenye kutosheka na kile alichoruzukiwa na Mola wake. Kila mtu amekadiriwa riziki yake na Allah (s.w). Hakuna mwenye uwezo wa kumpunguzia au kumzidishia mtu riziki. Hili linabainishwa katika Qur-an katika usia wa Mzee Luqman kwa mwanawe:

يَٰبُنَىَّ إِنَّهَآ إِن تَكُ مِثْقَالَ حَبَّةٍ مِّنْ خَرْدَلٍ فَتَكُن فِى صَخْرَةٍ أَوْ فِى
ٱلسَّمَٰوَٰتِ أَوْ فِى ٱلْأَرْضِ يَأْتِ بِهَا ٱللَّهُ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ لَطِيفٌ خَبِيرٌ ﴿١٦﴾

*Ewe mwanangu! Kwa hakika jambo lolote lijapokuwa na uzito wa chembe ya hardali, likawa ndani ya jabali au mbinguni au katika ardhi, Mwenyezi Mungu atalileta (amlipe mstahiki); bila shaka Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa mambo yaliyofichikana, (na) Mjuzi wa mambo yaliyo dhahiri. (31:16)*

Pia Allah (s.w) anatuhakikishia:

﴿وَمَا مِن دَآبَّةٍ فِى ٱلْأَرْضِ إِلَّا عَلَى ٱللَّهِ رِزْقُهَا ... ﴿٦﴾

*"Na hakuna mnyama yoyote katika ardhi ila riziki yake iko juu ya Allah..." (11:6)*

Juu ya moyo wa kutosheka Mtume (s.a.w) anatuwaidhi katika Hadithi ifuatayo:

*Imesimuliwa katika mamlaka ya Abdullah Bin Amr bin al-'As (r.a) kuwa Mtume wa Allah amesema: "Yule aliyeingia Uislamu na akajaaliwa kupata riziki inayotosheleza mahitaji yake muhimu na Mwenyezi Mungu akamfanya kuwa mwenye kutosheka na kila alichotunukiwa, hakika amefuzu kikweli". (Muslim)*

## 33. Kuepuka Tamaa na Kuombaomba

Kinyume cha kutosheka ni kuwa na tamaa au kutototosheka. Kutototosheka ni ufakiri wa moyo. Moyo wa kutototosheka huzaa tabia nyingi mbaya ikiwa ni pamoja na upupiaji mali, husuda, uchoyo, na kuomba omba. Muislamu anatakiwa ajitahidi kutosheka na alichonacho na hata kama anahisi yuko katika dhiki ajitahidi kujizuilia kunyoosha mkono wa kuomba chochote kwa yeyote kwa kadiri iwezekanavyo.

Tumekatazwa katika Qur-an kutamani vitu vya watu:

وَلَا تَتَمَنَّوْا۟ مَا فَضَّلَ ٱللَّهُ بِهِۦ بَعْضَكُمْ عَلَىٰ بَعْضٍ ۚ لِّلرِّجَالِ
نَصِيبٌ مِّمَّا ٱكْتَسَبُوا۟ ۖ وَلِلنِّسَآءِ نَصِيبٌ مِّمَّا ٱكْتَسَبْنَ ۚ وَسْـَٔلُوا۟ ٱللَّهَ مِن
فَضْلِهِۦٓ ۗ إِنَّ ٱللَّهَ كَانَ بِكُلِّ شَىْءٍ عَلِيمًا ﴿٣٢﴾

*"Wala msitamani vile ambavyo Mwenyezi Mungu amewafadhilisha baadhi yenu kuliko wengine. Wanaume wanayo sehemu (kamili) ya vile walivyovichuma; na wanawake nao wanayo sehemu (kamili) ya vile*

*walivyovichuma;. Na mwombeni Mwenyezi Mungu fadhila zake.Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.” (4:32).*

Kuhusu suala la omba omba Mtume (s.a.w) ametuusia katika Hadithi zifuatazo:

*Abu Hurairah (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: “Yule aombaye ili aongezee mali yake, haombi lingine ila moto wa maisha. (Muslim).*

*Ibn Umar (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema: “Kama mmoja wenu ataomba bila ya sababu ya msingi atakutana na Allah na uso usiokuwa na nyama”. (Bukhari na Muslim)*

*Ibn Umar (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah alipokuwa Mimbarini akitoa khutba juu ya kutoa sadaqa na kujizuia na kuomba omba alisema: “Mkono wa juu ni bora kuliko mkono wa chini. Mkono wa juu ni ule unaotoa na wa chini ni ule unaoomba”. (Bukhari na Muslim).*

Kuomba kunaruhusiwa kwa dharura zifuatazo:

(i) Mtu aliyesimama kumdhamini mtu mwingine ili kuleta suluhu kati ya wagomvi wawili huyu anaruhusiwa kuomba hata akiwa tajiri. Kwa mnasaba huu, wadhamini wa Misikiti, madrasa, na shughuli mbali mbali za Kiislamu wanaruhusiwa kuomba michango ya Waislamu ili kufanikisha shughuli hizo.

(ii) Mtu aliyepata ajali na kuharibikiwa kabisa vitu vyote kama vile ajali ya moto, mafuriko, n.k.

(iii) Mtu ambaye amepigwa na ufukara na amekosa kabisa mahitaji muhimu ya maisha kama chakula, malazi na makazi. Lakini mtu akiwa kama na angalau chakula cha siku moja na malazi na akawa na dirham 50 mkononi mwake haruhusiwi kuomba kama tunavyofahamishwa katika Hadithi zifuatazo:

*Abdullah bin Mas’ud (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema: Anayeomba omba watu na ilhali ana mahitaji muhimu ya maisha atakuja siku ya Kiyama na kuomba omba kwake kama mikwaruzo, vidonda au majeraha usoni mwake. Iliulizwa: Ee Mtume wa Mwenyezi Mungu! Ni kiasi gani kinachomtosha mtu? Akajibu: Dirham 50 au thamani yake ya dhahabu (Abu Daud, Tirmidh, Nasai na Ibn Majah)*

*Sahl (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: Yeyote yule anayeomba na ilihali anajitosheleza kwa mahitaji muhimu, anaomba*

*moto (Jahannam). Nufali (r.a) ambaye ni miongoni mwa wasimulizi wa hadithi hii katika sehemu nyingine aliuliza: Ni yupi mwenye uwezo ambaye kuomba ni haram? Akajibu Mtume (s.a.w): Yule mwenye uwezo wa kupata chakula cha asubuhi na usiku. Mahali pengine amesema: Yule mwenye chakula cha siku moja (Usiku na mchana). (Abu Daud).*

### 34. Kuepuka Husuda

Husuda ni miongoni mwa magonjwa makubwa ya moyo. Mtu mwenye husuda anadonda la chuki moyoni mwake juu ya neema alizoneemeshwa mwingine na Mwenyezi Mungu (s.w). Kwa maana nyingine anachukia utaratibu wa Mwenyezi Mungu (s.w) aliouweka katika kugawanya neema zake kwa waja wake. Hasidi kutokana na chuki yake dhidi ya mja aliyeneemeshwa na Mwenyezi Mungu (s.w), huwa tayari kwa hali na mali kumdhuru mja huyo asiye na hatia yoyote. Ni kwa msingi huu Mwenyezi Mungu (s.w) anatufundisha kujikinga kwake na shari za viumbe vyake, akiwemo hasidi kama tunavyosoma katika Suratul-Falaq:

قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ ٱلْفَلَقِ ﴿١﴾ مِن شَرِّ مَا خَلَقَ ﴿٢﴾ وَمِن شَرِّ غَاسِقٍ إِذَا وَقَبَ ﴿٣﴾ وَمِن شَرِّ ٱلنَّفَّـٰثَـٰتِ فِى ٱلْعُقَدِ ﴿٤﴾ وَمِن شَرِّ حَاسِدٍ إِذَا حَسَدَ ﴿٥﴾

*Sema: Ninajikinga na Mola wa Ulimwengu wote. Na shari ya alivyoviumba. Na shari ya giza la usiku liingiapo na shari ya wale wanaopulizia mafundoni na shari ya hasidi anapohusudu(113:1-5)*

Husuda husababishwa na kutotosheka na kutoridhika na neema za Mwenyezi Mungu (s.w). Hasidi anataka kila neema aliyotunukiwa mwingine awe nayo yeye au mwingine abakie bila neema hiyo. Anataka awe juu ya mwingine na aonekane wa maana pekee katika jamii. Akihisi kuwa kuna yeyote aliyemzidi kwa cheo, utajiri, elimu, watoto,umaarufu, hupandwa na moto wa chuki moyoni mwake ambao humsukuma kufanya visa mbali mbali dhidi ya huyo anayemhisi kuwa amemzidi au yuko sawa naye.

Muislamu anatakiwa ajitakase na uovu huu wa husuda kwa kutosheka na kile alichonacho akijua kuwa kila neema aliyopewa mwanaadamu imekadiriwa na Mwenyezi Mungu (s.w). Na hapana yeyote mwenye uwezo wa kupunguza neema ya mtu aliyokadiriwa na Mola wake hata kwa kiasi cha chembe ndogo iliyoje na hakuna yeyote awezaye kumuongezea mtu neema kuliko vile alivyokadiriwa na Mwenyezi Mungu

(s.w).

Pia Muislamu wa kweli anajitahidi kujiepusha na husuda ili asije akaziunguza amali zake njema alizozitanguliza na akawa miongoni mwa watakaohasirika katika maisha ya akhera.

*Abu Hurairah (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: "Kuweni waangalifu juu ya husuda, kwani husuda inaunguza amali njema za mtu kama moto unavyounguza kuni. (Abu Daud).*

Husuda au wivu unaoruhusiwa ni ule unaofanywa kwa ajili ya kushindana katika kufanya mema. Wivu wa namna hii sio ule wa kuchukia kuwa kwa nini fulani ameneemeshwa bali ni ule unaomfanya mja ajitahidi zaidi kufanya mema kama anavyofanya au kumzidi mwingine. Mtume (s.a.w) ametufahamisha ni husuda ya namna gani inayoruhusiwa kwa Muislamu katika Hadithi ifuatayo:

*Ibn Mas'ud (r.a) amehadithia kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema: Hapana husuda (inayoruhusiwa katika Uislamu) ila kwa watu wawili: "Mtu ambaye Mwenyezi Mungu (s.w) amempa mali na akampa uwezo wa kuitumia katika njia ya Mwenyezi Mungu na mtu ambaye Mwenyezi Mungu amempa elimu na hekima akawa anafundisha wengine pamoja na yeye mwenyewe kuingiza elimu hiyo katika vitendo". (Bukhari na Muslim).*

## 35. Kumtegemea Mwenyezi Mungu (s.w)

Muislamu wa kweli daima huwa jasiri kwa kumtegemea Mwenyezi Mungu katika kila hali. Ana yakini kuwa hapana lolote litakalomfika, baya au zuri, ila litakuwa linatoka kwa Mwenyezi Mungu (s.w) na ana yakini kuwa ulinzi wa maisha yake na mahitajio yake yote ya kimaisha yako mikononi mwa Mwenyezi Mungu (s.w). Mwenyezi Mungu (s.w) anatuamrisha tumtegemee Yeye tu katika aya zifuatazo:

وَتَوَكَّلْ عَلَى ٱلْحَيِّ ٱلَّذِى لَا يَمُوتُ ... ﴿٥٨﴾

*Na tegemea kwa Yule aliye na uhai wa milele ambaye hatakufa". (25:58)*

وَعَلَى ٱللَّهِ فَلْيَتَوَكَّلِ ٱلْمُؤْمِنُونَ ﴿١١﴾ وَمَا لَنَآ أَلَّا نَتَوَكَّلَ عَلَى ٱللَّهِ وَقَدْ
هَدَىٰنَا سُبُلَنَا ۚ وَلَنَصْبِرَنَّ عَلَىٰ مَآ ءَاذَيْتُمُونَا ۚ وَعَلَى ٱللَّهِ فَلْيَتَوَكَّلِ
ٱلْمُتَوَكِّلُونَ ﴿١٢﴾

*"... Na kwa Mwenyezi Mungu wategemee Waislamu. Na tuna nini tusimtegemee Mwenyezi Mungu, na hali Ametuonyesha njia zetu. Na tutayavumilia maudhi yenu. Basi kwa Mwenyezi Mungu wategemee wategemeao". (14:11-12)*

... وَمَن يَتَّقِ ٱللَّهَ يَجۡعَل لَّهُۥ مَخۡرَجٗا ﴿٢﴾ وَيَرۡزُقۡهُ مِنۡ
حَيۡثُ لَا يَحۡتَسِبُۚ وَمَن يَتَوَكَّلۡ عَلَى ٱللَّهِ فَهُوَ حَسۡبُهُۥٓۚ إِنَّ ٱللَّهَ بَٰلِغُ أَمۡرِهِۦۚ
قَدۡ جَعَلَ ٱللَّهُ لِكُلِّ شَيۡءٖ قَدۡرٗا ﴿٣﴾

*"...Na anayemuogopa Mwenyezi Mungu, (Allah) humtengenezea njia ya kuokoka (na kila balaa); na humpa riziki kwa namna asiyoitazamia. Na anayemtegemea Mwenyezi Mungu yeye humtoshea. Kwa yakini Mwenyezi Mungu anatimiza kusudio lake. Hakika Mwenyezi Mungu amekwisha kiwekea kila kitu kipimo chake". (65:2-3).*

Kumtegemea Mwenyezi Mungu kwa kila jambo na hasa wakati wa dhiki na kuhitajia msaada, huzidisha imani na ujasiri kwa waumini. Hebu turejee aya zifuatazo:

ٱلَّذِينَ قَالَ لَهُمُ ٱلنَّاسُ إِنَّ ٱلنَّاسَ قَدۡ جَمَعُواْ لَكُمۡ
فَٱخۡشَوۡهُمۡ فَزَادَهُمۡ إِيمَٰنٗا وَقَالُواْ حَسۡبُنَا ٱللَّهُ وَنِعۡمَ ٱلۡوَكِيلُ ﴿١٧٣﴾
فَٱنقَلَبُواْ بِنِعۡمَةٖ مِّنَ ٱللَّهِ وَفَضۡلٖ لَّمۡ يَمۡسَسۡهُمۡ سُوٓءٞ وَٱتَّبَعُواْ رِضۡوَٰنَ ٱللَّهِۗ
وَٱللَّهُ ذُو فَضۡلٍ عَظِيمٍ ﴿١٧٤﴾

*"Wale ambao watu waliwaambia: "Watu wamekukusanyikieni. Kwa hiyo waogopeni". Lakini (maneno hayo) yakawazidishia imani wakasema Mwenyezi Mungu anatutosha. Naye ni Mlinzi bora kabisa. Basi wakarudi (vitani na neema za Mwenyezi Mungu na fadhila zake), hakuna ubaya uliowagusa; na wakafuata yanayomridhisha Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu ni mwenye fadhila kuu". (3:173-174)*

وَلَمَّا رَءَا ٱلۡمُؤۡمِنُونَ ٱلۡأَحۡزَابَ قَالُواْ هَٰذَا مَا وَعَدَنَا ٱللَّهُ وَرَسُولُهُۥ وَصَدَقَ
ٱللَّهُ وَرَسُولُهُۥۚ وَمَا زَادَهُمۡ إِلَّآ إِيمَٰنٗا وَتَسۡلِيمٗا ﴿٢٢﴾

*“Na Waislamu walipoyaona majeshi (ya makafiri) walisema, “Haya ndiyo aliyotuahidi Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Mwenyezi Mungu na Mtume wake wamesema kweli,na (jambo hili) halikuwazidishia ila imani na utii. (33:22).*

إِنَّمَا ٱلۡمُؤۡمِنُونَ ٱلَّذِينَ إِذَا ذُكِرَ ٱللَّهُ وَجِلَتۡ قُلُوبُهُمۡ وَإِذَا تُلِيَتۡ عَلَيۡهِمۡ ءَايَٰتُهُۥ زَادَتۡهُمۡ إِيمَٰنٗا وَعَلَىٰ رَبِّهِمۡ يَتَوَكَّلُونَ ﴿٢﴾

*“Hakika waumini wa kweli ni wale ambao anapotajwa Mwenyezi Mungu nyoyo zao hujaa hofu; na wanaposomewa Aya Zake huwazidishia imani na wakamtegema Mola wao tu basi”. (8 : 2)*

Hivyo Waislamu hatuna budi kumtegemea Mwenyezi Mungu (s.w) kwa kila hali. Tukifanya hivyo imani yetu itazidi na tutakuwa na moyo wa ujasiri wa kutuwezesha kupambana na hali yoyote ngumu itakayotukabili kwa sababu tunayakini kuwa halitufikii lolote, baya au zuri, ila liko katika makadirio ya Mwenyezi Mungu (s.w). Ni vyema hapa tukumbushe kuwa kumtegemea Mwenyezi Mungu (s.w) ni kutekeleza wajibu wetu kwa juhudi na maarifa katika jambo lolote tunalolifanya kisha matokeo ya jitihada zetu tumuachie Mwenyezi Mungu (s.w). Hii hasa ndio maana ya kumtegemea Allah (s.w) kama tunavyojifunza.katika aya zifuatazo:

بَلَىٰ مَنۡ أَسۡلَمَ وَجۡهَهُۥ لِلَّهِ وَهُوَ مُحۡسِنٞ فَلَهُۥٓ أَجۡرُهُۥ عِندَ رَبِّهِۦ وَلَا خَوۡفٌ عَلَيۡهِمۡ وَلَا هُمۡ يَحۡزَنُونَ ﴿١١٢﴾

*“Naam, wanaoelekeza nyuso zao kwa Mwenyezi Mungu na wakawa ni watendaji mema, basi wao watapata malipo yao kwa Mola wao, wala haitakuwa hofu juu yao wala hawatahuzunika. (2:112).*

وَأَن لَّيۡسَ لِلۡإِنسَٰنِ إِلَّا مَا سَعَىٰ ﴿٣٩﴾

*Na kwamba, mtu hatapata ila kwa yale anayoyafanya. (53:39).*

## 36. Kuepukana na Woga

Kinapokosekana kipengele hiki cha “kumtegemea Mwenyezi Mungu katika kila hali” katika tabia au mwendo wa mja nafasi yake inajazwa na kipengele cha “woga”. Woga na khofu juu ya matukio mbali mbali ya maisha ya hapa ulimwenguni husababishwa na uhaba wa imani

juu ya Allah (s.w) na sifa zake. Mtu asiyemtegemea Mwenyezi Mungu hudhania kuwa mafanikio yote ya maisha hupatikana kwa uwezo wa mwanaadamu na kuwa ni mwanaadamu pekee mwenye uwezo wa kujikinga na shari zote zinazomkabili.Dhana hii humtia mtu katika wasi wasi na woga atakapohisi kuwa tatizo au dhara fulani linalomkabili litamshinda nguvu kwa kuwa hana uwezo au msaada wa mwanaadamu wa kumuwezesha kupambana nalo.

Muislamu wa kweli hapaswi kuwa mwoga wa chochote kwa sababu hapana chochote kinachoweza kumdhuru, ila awe amekadiria hivyo Mwenyezi Mungu (s.w) na hapana mja awezaye kuepa ajali yake aliyoandikiwa na Mwenyezi Mungu. Muislamu anatakiwa awe imara katika kusimamisha Dini ya Allah katika kila kipengele cha maisha yake, bila ya kuhofu chochote kwani yeye daima yuko chini ya ulinzi na uangalizi wa Mwenyezi Mungu (s.w), na halitamsibu ila lile alilomuandikia Mwenyezi Mungu (s.w).

قُل لَّن يُصِيبَنَآ إِلَّا مَا كَتَبَ ٱللَّهُ لَنَا هُوَ مَوْلَىٰنَا ۚ وَعَلَى ٱللَّهِ فَلْيَتَوَكَّلِ ٱلْمُؤْمِنُونَ ﴿٥١﴾

*"Sema; halitatusibu ila alilotuandikia Mwenyezi Mungu, yeye ni Mola wetu. Basi Waislamu na wamtegemee Mwenyezi Mungu tu"(9:51).*

Pia Allah (s.w) ametukataza kuwaogopa makafiri:

ـ ٱلْيَوْمَ يَئِسَ ٱلَّذِينَ كَفَرُوا۟ مِن دِينِكُمْ فَلَا تَخْشَوْهُمْ وَٱخْشَوْنِ ۚ ..

*"......Leo makafiri wamekata tamaa na dini yenu basi msiwaogope, bali niogopeni mimi........."(5:3).*

## 37. Kuepukana na Kukata Tamaa

Pia Muislamu hatakiwi kukata tamaa na Rehema za Mwenyezi Mungu (s.w). Hakuna kinachoshindikana kwa Mwenyezi Mungu. Muislamu hana budi kufanya jitihada katika kufanikisha jambo muhimu la maisha kwa kufuata njia za halali anazoziridhia Mwenyezi Mungu (s.w). Kama jambo hilo lina kheri na yeye, basi Mwenyezi Mungu (s.w) atalifanikisha. Mzee Yaquub (a.s) akiwausia wanawe wasichoke kumtafuta Yusuf na ndugu yake aliwaambia:

يَـٰبَنِىَّ ٱذْهَبُوا۟ فَتَحَسَّسُوا۟ مِن يُوسُفَ وَأَخِيهِ وَلَا تَا۟يْـَٔسُوا۟ مِن رَّوْحِ

ٱللَّهِۖ إِنَّهُۥ لَا يَاْيۡـَٔسُ مِن رَّوۡحِ ٱللَّهِ إِلَّا ٱلۡقَوۡمُ ٱلۡكَٰفِرُونَ ﴿٨٧﴾

*"Enyi wanangu! Nendeni mkamtafute Yusuf na nduguye, wala msikate tamaa na Rehema ya Mwenyezi Mungu. Hawakati tamaa na Rehema ya Mwenyezi Mungu isipokuwa watu makafiri". (12:87).*

Pia iwapo baada ya Muislamu kufanya juhudi na kutumia uwezo wake wote, hakupata mafanikio aliyotarajia, asikate tamaa bali aridhike kuwa matokeo hayo ndiyo yenye kheri kwake kwa kuzingatia Qur-an:

وَعَسَىٰٓ أَن تَكۡرَهُواْ شَيۡـٔٗا وَهُوَ خَيۡرٞ لَّكُمۡۖ وَعَسَىٰٓ أَن تُحِبُّواْ شَيۡـٔٗا
وَهُوَ شَرّٞ لَّكُمۡۗ وَٱللَّهُ يَعۡلَمُ وَأَنتُمۡ لَا تَعۡلَمُونَ ﴿٢١٦﴾

*"... Lakini huenda mkachukia kitu nacho ni kheri kwenu. Na huenda mkapenda kitu nacho ni shari kwenu. Na Mwenyezi Mugu ndiye anayejua, (lakini) nyinyi hamjui". (2:216).*

## 38. Kuwa na Istiqama (Msimamo Thabiti)

Muumini wa kweli anayemtegemea Mwenyezi Mungu (s.w) kwa kila hali hana budi kuwa na msimamo thabiti katika kuusimamisha na kuufuata Uislamu. Si muumini wa kweli yule anayeyumba yumba (mudhabidhabina) kwa kuchanganya haki na batili au utii na uasi katika kuendesha maisha yake ya kila siku. Mwenyezi Mungu (s.w) ametuamrisha wale tutoao shahada ya kweli tuuingie Uislamu wote au tuwe Waislamu katika kila kipengele na kila hatua ya maisha yetu na wala tusiuingie nusu nusu. Anatuamrisha:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ ٱدۡخُلُواْ فِي ٱلسِّلۡمِ كَآفَّةٗ وَلَا تَتَّبِعُواْ
خُطُوَٰتِ ٱلشَّيۡطَٰنِۚ إِنَّهُۥ لَكُمۡ عَدُوّٞ مُّبِينٞ ﴿٢٠٨﴾

*Enyi mlioamini! ingieni katika Uislamu wote, wala msifuate nyayo za shetani, kwa hakika yeye kwenu ni adui dhahiri. (2:208)*

Hivyo, kutamka tu shahada au kusema: "*Tunakiri kuwa hapana Mola ila Mwenyezi Mungu na Muhammad (s.a.w) ni Mtume wake*" haitoshi kutufanya kuwa Waislamu wale walioahidiwa malipo makubwa huko akhera; bali tutakuwa wa kweli katika shahada zetu iwapo tutaendesha

maisha yetu yote kama alivyotutaka tuishi Mwenyezi Mungu (s.w) na kama alivyotuelekeza Mtume wake (s.a.w). Waislamu watakaokuwa imara katika kuutekeleza Uislamu katika maisha yao ya kila siku, ndio walioahidiwa malipo makubwa ya Peponi katika maisha ya Akhera. Hebu turejee aya chache zifuatazo:

إِنَّ ٱلَّذِينَ قَالُوا۟ رَبُّنَا ٱللَّهُ ثُمَّ ٱسْتَقَـٰمُوا۟ تَتَنَزَّلُ
عَلَيْهِمُ ٱلْمَلَـٰٓئِكَةُ أَلَّا تَخَافُوا۟ وَلَا تَحْزَنُوا۟ وَأَبْشِرُوا۟ بِٱلْجَنَّةِ ٱلَّتِى
كُنتُمْ تُوعَدُونَ ﴿٣٠﴾ نَحْنُ أَوْلِيَآؤُكُمْ فِى ٱلْحَيَوٰةِ ٱلدُّنْيَا وَفِى ٱلْـَٔاخِرَةِ ۖ
وَلَكُمْ فِيهَا مَا تَشْتَهِىٓ أَنفُسُكُمْ وَلَكُمْ فِيهَا مَا تَدَّعُونَ ﴿٣١﴾

*"Wale waliosema: Mola wetu ni Mwenyezi Mungu kisha wakabakia imara (wakawa na msimamo), hao huwateremkia Malaika (wakawaambia),"Msiogope wala msihuzunike, na furahini kwa Pepo mliyokuwa mkiahidiwa. Sisi ni vipenzi vyenu katika maisha ya dunia na katika Akhera, na humo mtapata vitu vinavyopendwa na nafsi zenu, na humo mtapata mtakavyovitaka". (41:30-31).*

إِنَّ ٱلَّذِينَ قَالُوا۟ رَبُّنَا ٱللَّهُ ثُمَّ ٱسْتَقَـٰمُوا۟ فَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ
وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿١٣﴾ أُو۟لَـٰٓئِكَ أَصْحَـٰبُ ٱلْجَنَّةِ خَـٰلِدِينَ فِيهَا
جَزَآءًۢ بِمَا كَانُوا۟ يَعْمَلُونَ ﴿١٤﴾

*Hakika wale waliosema: "Mola wetu ni Mwenyezi Mungu', kisha wakatengenea (wakawa na msimamo) hawatakuwa na khofu (siku ya kufa kwao wala baadaye) wala hawatahuzunika. Hao ndio watu wa Peponi, watakaa humo (milele); ni malipo ya yale waliyokuwa wakiyatenda. (46:13-14).*

Hebu pia tuone jinsi Mtume (s.a.w) alivyotuwaidhi juu ya kuwa na msimamo katika Uislamu wetu:

*Sufyaan bin Abdullah (r.a) amesimulia kuwa alisema: Ee! Mtume wa Allah niambie neno juu ya Uislamu ambalo sitakuwa tena na haja ya*

*kumuuliza mtu mwingine baada ya hapa. Alisema Mtume(s.a.w); 'Sema: Ninamuamini Mwenyezi Mungu kisha ubakie katika msimamo huo". (Muslim)*

*Abu Hurairah (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema: Fuata barabara njia sahihi ya imani na kuwa na msimamo huo, na ujue kwamba hapana yeyote atakayeokoka kutokana na amali yake (nzuri). Mmoja akauliza: Hata wewe Mtume wa Allah? Akajibu (Mtume) hata mimi, ila mpaka Allah anikunjulie Rehema zake na Fadhila zake. (Muslim)*

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ لِمَ تَقُولُونَ مَا لَا تَفْعَلُونَ ﴿٢﴾ كَبُرَ مَقْتًا عِندَ ٱللَّهِ
أَن تَقُولُوا۟ مَا لَا تَفْعَلُونَ ﴿٣﴾

*Enyi mlioamini! Kwanini mnasema msiyoyatenda. Ni chukizo kubwa mbele ya Allah kusema msiyoyatenda.*
*(61:2-3)*

**************************

## Zoezi la kwanza

1. Ibn Umar (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: "*Uislamu umejengwa juu ya (nguzo) tano...*". Orodhesha mafunzo makubwa matatu yanayopatikana katika hadithi hii.

2. *"Sikuwaumba majini na watu ila wapate kuniabudu. Sitaki kwao riziki wala Sitaki wanilishe. Kwa yakini Mwenyezi Mungu ndiye Mtoaji wa riziki, Mwenye Nguvu, Madhubuti (51:56-58).*
   Kwa kuzingatia ujumbe wa aya hizi, bainisha mambo wanayopaswa kufanya Waislamu ili waweze kumuabudu Allah(s.w) katika kila kipengele cha maisha yao, pasina kumshirikisha na viumbe vyake.

3. Eleza kwa muhtasari maana ya
   (a) *Nashuhudia kuwa hapana Mungu ila Allah*
   *(b) Na ninashuhudia kuwa Muhammad ni Mtume wa Allah.*

4. *Hakika Wale waliosema: Mola wetu ni Mwenyezi Mungu kisha wakabakia imara (wakawa na msimamo), hao huwateremkia Malaika (wakawaambia),"Msiogope wala msihuzunike, na furahini kwa Pepo mliyokuwa mkiahidiwa. Sisi ni vipenzi vyenu katika maisha ya dunia na katika Akhera, na humo mtapata vitu vinavyopendwa na nafsi zenu, na humo mtapata mtakavyovitaka". (41:30-31).*

Ni sifa zipi walizokuwa wameshikamana nazo watu hawa baada ya kutamka shahada katika maisha ya duniani?

5. *"Enyi Mlioamini! Ingieni katika Uislamu wote (katika hukumu zote za Uislamu) wala msifuate nyayo za Shetani, kwa hakika yeye kwenu ni adui aliye dhahiri". (2:208).*

*Chukua aya hii kuwa kigezo cha kufanya mjadala na wenzako juu ya namna Waislamu walivyoshindwa au kuweza kuitikia wito huu wa Allah(SW).*

6. Allah(s.w) anasema kuwa: *"Walinganie (watu) katika njia ya Mola wako kwa hekima na mawaidha mema, na ujadiliane nao kwa namna iliyo bora. Hakika Mola wako ndiye anayemjua aliyepotea katika njia yake naye ndiye Anayewajua walioongoka". (16:125).*

Kwa kuzingatia jukumu la kila muumini wa kweli lililotajwa kwenye aya hii, orodhesha malengo na njia utakazozitumia ili kuifanya(kuiwezesha) jamii ya watu waliokuzunguka waweze kuishi maisha ya shahada.

**************************

## Sura ya Pili

# KUSIMAMISHA SWALA

### Umuhimu wa Kusimamisha Swala

Kwa mujibu wa Hadith ya Ibn Umar (r.a) tuliyoirejea mwanzoni, kusimamisha swala ni nguzo ya pili ya nguzo za Uislamu. Katika kuonyesha umuhimu wa kusimamisha nguzo hii Mtume (s.a.w) amesema:

*"Swala ndio nguzo kubwa ya Dini (Uislamu) mwenye kusimamisha swala amesimamisha dini (Uislamu) na mwenye kuiacha swala amevunja Dini ." (Uislamu)"*

Katika Hadithi nyingine, amesimulia Jabir (r.a) kuwa Mtume wa Allah amesema:

*"Tofauti yetu sisi (Waislamu) na ukafiri ni kuacha swala". (Muslim)*

Pia Mtume (s.a.w) amesema:

*"Tofauti iliyopo kati yetu (Waislamu) na wengine (wasiokuwa Waislamu) ni swala". (Ahmad, Abu Daud, An-Nasai, Tirmidh)*

Kutokana na hadithi hizi, tunajifunza kuwa mtu ambaye hasimamishi swala, hatakama anajiita Muislamu si Muislamu bali ni kafiri kama makafiri wengine. Anakuwa kafiri kwa sababu amekanusha amri ya Allah iliyowazi kama inavyobainika katika aya zifuatazo:

قُل لِّعِبَادِيَ ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ يُقِيمُواْ ٱلصَّلَوٰةَ ... ﴿٣١﴾

*"Waambie waja wangu walioamini, wasimamishe swala."(14:31)*

... فَأَقِيمُواْ ٱلصَّلَوٰةَۚ إِنَّ ٱلصَّلَوٰةَ كَانَتۡ عَلَى ٱلۡمُؤۡمِنِينَ كِتَٰبٗا مَّوۡقُوتٗا

*"... Basi simamisheni swala, kwa hakika swala kwa waumini ni faradhi iliyowekewa nyakati makhsusi." (4:103)*

وَأۡمُرۡ أَهۡلَكَ بِٱلصَّلَوٰةِ وَٱصۡطَبِرۡ عَلَيۡهَاۖ ... ﴿١٣٢﴾

*"Na waamrishe watu wako kuswali (kusimamisha swala) na uendelee mwenyewe kwa hayo..." (20:132).*

Tukumbuke kuwa hawi Muumini yule anayekuwa na hiari katika kutekeleza amri ya Allah na Mtume wake kama tunavyokumbushwa katika aya ifuatayo:

وَمَا كَانَ لِمُؤْمِنٍ وَلَا مُؤْمِنَةٍ إِذَا قَضَى ٱللَّهُ وَرَسُولُهُۥٓ أَمْرًا أَن يَكُونَ لَهُمُ
ٱلْخِيَرَةُ مِنْ أَمْرِهِمْ ۗ وَمَن يَعْصِ ٱللَّهَ وَرَسُولَهُۥ فَقَدْ ضَلَّ ضَلَٰلًا مُّبِينًا ﴿٣٦﴾

*"Haiwi kwa mwanamume aliyeamini wala kwa mwanamke aliyeamini, Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanapokata shauri, wawe na hiari katika shauri lao. Na mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake, hakika amepotea upotofu ulio wazi". (33:36)*

## Lengo la Kusimamisha Swala

Bila shaka swala imepewa umuhimu mkubwa kiasi cha kufanywa nguzo kubwa ya Uislamu kutokana na lengo lake. Lengo la swala limebainishwa katika Qur-an kama ifuatavyo

ٱتْلُ مَآ أُوحِىَ إِلَيْكَ مِنَ ٱلْكِتَٰبِ وَأَقِمِ ٱلصَّلَوٰةَ ۖ إِنَّ ٱلصَّلَوٰةَ تَنْهَىٰ
عَنِ ٱلْفَحْشَآءِ وَٱلْمُنكَرِ ۗ وَلَذِكْرُ ٱللَّهِ أَكْبَرُ ۗ وَٱللَّهُ يَعْلَمُ مَا تَصْنَعُونَ ﴿٤٥﴾

*"Soma uliyoletewa wahyi katika kitabu (Qur-an) na usimamishe swala. Bila shaka swala (ikiswaliwa vilivyo) humzuilia (mwenye kuswali na) mambo machafu na maovu, na kwa yakini kumbuko la Mwenyezi Mungu (lililomo ndani ya swala ni jambo) kubwa kabisa (la kumzuilia mtu na mabaya). Na Mwenyezi Mungu anayajua mnayoyatenda." (29:45).*

Kutokana na aya hii tunajifunza kuwa lengo la kusimamisha swala ni kumtakasa mja na mambo machafu na maovu. Kwa maana nyingine, tunajifunza kuwa swala ikisimamishwa vilivyo, humfanya msimamishaji awe mtu mwema mwenye kutakasika na mambo machafu na maovu na mwenye kuendea kila kipengele chake cha maisha kwa kumtii Allah (s.w). Labda tujiulize swali: *"Ni nguvu gani au ni msukumo gani uliomo katika swala unaomfanya mwenye kuswali atakasike na maovu na awe na tabia njema anayoridhia Allah (s.w)"* Linaloleta mabadiliko haya makubwa katika tabia na utendaji wa Muumini, ni lile kumbuko la Allah (s.w) lililomo ndani ya swala. Kwa hiyo lengo hili la swala litapatikana tu pale mwenye kuswali atakapokuwa na mazingatio na kumkumbuka Allah (s.w) katika kila hatua ya swala.

## Maana ya Swala

### (a) Kilugha

Katika lugha ya Kiarabu neno "*Swalaat*" lina maana ya "*ombi*" au "dua". Katika Qur-an tunaamrishwa kumswalia Mtume, yaani kumuombea dua Mtume (s.a.w) katika aya ifuatayo:

إِنَّ ٱللَّهَ وَمَلَٰٓئِكَتَهُۥ يُصَلُّونَ عَلَى ٱلنَّبِيِّۚ يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ صَلُّواْ عَلَيْهِ وَسَلِّمُواْ تَسْلِيمًا ﴿٥٦﴾

*"Hakika Mwenyezi Mungu na Malaika wake wanamswalia Mtume (wanamtakia Rehema). Basi, enyi mlioamini mswalieni (muombeeni au mtakieni Mtume) Rehema na muombeeni amani". (33:56)*

Vile vile katika Hadith, Mtume (s.a.w) anatuambia:

*"Yule atakayealikwa kwenye karamu ya harusi aitikie wito huo, kama hataweza kuitika amswalie (amuombee dua) aliyemkaribisha." (Muslimu)*

### (b) Kisheria

Katika sheria ya Kiislamu, "swalaat" ni maombi maalumu kwa Allah (s.w) yanayofanywa kwa kufuata utaratibu maalumu uliowekwa na Allah (s.w) na kufundishwa kwa matendo na Mtume wake. Katika maombi haya maalumu mwili mzima huhusika katika maombi haya kwa kusimama, kurukuu, kuitidali, kusujudu, kukaa na kuzingatia yale yote anayosema katika kuleta maombi haya.

## Maana ya Kusimamisha Swala

Kusimamisha swala ni tofauti na kuswali. Kuswali ni kufanya vitendo vya swala kama vile kusimama, kurukuu, kuitidali, kusujudu, n.k. Kusimamisha swala ni kuitekeleza swala kwa kuchunga na kutekeleza kwa ukamilifu yafuatayo:

(i) Sharti zote za swala.
(ii) Nguzo zote za swala.
(iii) Kuwa na khushui (unyenyekevu) wakati wote wa kutekeleza sharti na nguzo za swala.

Mtu akiswali bila ya kuzingatia na kutekeleza kwa ukamilifu mambo haya matatu, ataonekana kuwa kaswali, lakini atakuwa hajasimamisha swala na atastahiki kuadhibiwa vikali na Mola wake kama tunavyojifunza katika aya ifuatayo:

فَوَيْلٌ لِّلْمُصَلِّينَ ﴿٤﴾ ٱلَّذِينَ هُمْ عَن صَلَاتِهِمْ سَاهُونَ ﴿٥﴾ ٱلَّذِينَ هُمْ يُرَآءُونَ ﴿٦﴾

*"Basi adhabu kali itawathibitikia wanaoswali, ambao wanapuuza swala zao (kwa kutozisimamisha), ambao hufanya ria". (107:4-6)*

Kupuuza swala ni pamoja na kutotekeleza ipasavyo sharti za swala, nguzo za swala, na kutokuwa na unyenyekevu wakati wa kutekeleza sharti na nguzo za swala.

Hivyo, swala inayokubalika mbele ya Allah (s.w) ni ile iliyosimamishwa kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

قَدْ أَفْلَحَ ٱلْمُؤْمِنُونَ ﴿١﴾ ٱلَّذِينَ هُمْ فِى صَلَاتِهِمْ خَٰشِعُونَ ﴿٢﴾

*"Hakika wamefuzu waumini ambao katika swala zao ni wanyenyekevu". (23:1-2)*

وَٱلَّذِينَ هُمْ عَلَىٰ صَلَوَٰتِهِمْ يُحَافِظُونَ ﴿٩﴾

*"Na ambao swala zao wanazihifadhi". (23:9)*

Kuhifadhi swala ni kutekeleza kwa ukamilifu sharti na nguzo zote za swala.

## Sharti za Swala

Sharti za swala ni yale mambo ya lazima anayotakiwa Muislamu ayachunge na kuyatekeleza kabla hajaanza kuswali. Mambo haya ni:

1. Twahara.
2. Sitara.
3. Kuchunga wakati.
4. Kuelekea Qibla.

### 1. Twahara

**Maana ya Twahara:**

"Twahara" ni neno la Kiarabu lenye maana ya usafi wa nje ulioambatana na usafi wa ndani ya mtu. Usafi wa nje unahusiana na usafi wa mwili na nguo na usafi wa ndani unahusiana na utakaso wa nafsi. Mwili na nguo hutwaharika kwa kusafisha kwa kufuata maelekezo

ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Ama nafsi hutwaharika kwa kumtii Allah na Mtume wake kwa kufuata maamrisho yao na kuacha maovu na machafu waliyotukataza. Watu waliotwaharika kwa mtazamo huu hupendeza mbele ya Allah (s.w) kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

...إِنَّ ٱللَّهَ يُحِبُّ ٱلتَّوَّٰبِينَ وَيُحِبُّ ٱلْمُتَطَهِّرِينَ ﴿٢٢٢﴾

*"...Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wanaotubu na huwapenda wanaojitakasa (wanaojitwaharisha)" (2:222)*

..فِيهِ رِجَالٌ يُحِبُّونَ أَن يَتَطَهَّرُوا۟ ۚ وَٱللَّهُ يُحِبُّ ٱلْمُطَّهِّرِينَ ﴿١٠٨﴾

*"...Humo wamo watu wanaopenda kujitakasa. Na Mwenyezi Mungu anawapenda wajitakasao". (9:108)*

Kwa ujumla tunaweza kusema twahara kwa mtazamo wa Qur-an ni usafi wa nguo zetu, miili yetu, hisia zetu, mawazo yetu na mwenendo na tabia zetu kwa mujibu wa maelekezo ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake.

Pamoja na maana hii ya ujumla, Muislamu aliyetwaharika na kuwa tayari kusimama kwenye swala ni yule aliyeepukana na Najisi na Hadathi. Hivyo tunapojitwaharisha kwa ajili ya swala tunajishughulisha na kuondoa Najisi na Hadath.

## Najisi

Katika Uislamu najisi ni uchafu unaohusiana na vitu vifuatavyo:



(1) Damu.
(2) Usaha.
(3) Matapishi.
(4) Udenda.
(5) Haja ndogo na kubwa ya binaadamu au mnyama.
(6) Pombe za aina zote.
(7) Mzoga wowote isipokuwa wa binaadamu, samaki na nzige (au jamii ya nzige).
(8) Kiungo cha mnyama kilichokatwa naye yu ngali hai.



(9) Maziwa ya mnyama asiye halali kuliwa kama vile paka, punda wa nyumbani, farasi, n.k.

(10) Mbwa na Nguruwe na kila kinachotokana nao.

## Hadathi

Hadathi ni hali ambayo ikimpata Muislamu, hawezi kuswali mpaka imuondokee. Kuna aina tatu za hadath:

(i) Hadathi ndogo - kutokuwa na udhu. Mtu asiye na udhu ana hadathi ndogo na huondoka kwa kutia udhu.

(ii) Hadathi ya kati na kati - humpata mtu aliyefanya tendo la ndoa (jimai) au aliyetokwa na manii kwa kuota au kwa njia nyingineyo. Hadath hii huondoka kwa kukoga mwili mzima.

(iii) Hadathi kubwa - huwapata wanawake wanapokuwa katika Hedhi (damu ya mwezi) au katika Nifasi (damu ya uzazi). Huondoka kwa kuoga mwili mzima baada ya hedhi au nifasi kwisha.

## Chakujitwaharishia

Nafsi ya mtu hutwaharika kwa mtu huyo kumuamini Allah (s.w) ipasavyo na kufuata mwongozo wake katika kukiendea kila kipengele cha maisha yake ya kibinafsi na kijamii.

Muislamu atatwaharika kutokana na Najisi na Hadath kwa kutumia maji safi au udongo safi kwa kufuata masharti na maelekezo ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake.

### Sifa za Maji Safi

Maji safi kwa mtazamo wa twahara ni yale yanayofaa kujitwaharishia yaliyogawanyika katika makundi yafuatayo:

**(a) Maji Mutlak (maji asili)**

Maji yoyote katika hali yake ya asili ni maji safi yanayofaa kujitwaharishia. Maji asili (natural water) ni maji ya mvua, chem chem, visima, mito, maziwa na maji ya bahari.

**(b) Maji mengi:**

Maji mengi ni maji yaliyokusanywa au yaliyokusanyika pamoja na kuwa na ujazo wa mabirika (*qullatain*) au ujazo usiopungua madebe 12. Mfano wa maji mengi yaliyokusanywa ni maji ya mapipa yenye ujazo wa

lita 240, maji ya mabirika (*matangi)* maalum yaliyojengwa kuhifadhia maji msikitini na nyumbani. Mfano wa maji mengi yaliyojikusanya ni yale ya madimbwi makubwa yanayojikusanya wakati wa mvua.

Maji mengi hayahabiriki upesi. Hayaharibiki kwa kujitwaharishia ndani ya chombo kilichoyakusanya au ndani ya mkusanyiko huo wa maji. Pia maji mengi hayaharibiki kwa kuingiwa na najisi. Bali maji mengi yatakuwa hayafai kujitwaharishia iwapo yatabadilika asili yake katika rangi au utamu (ladha) au harufu.

**(c) Maji machache:**

Maji machache ni yale yaliyokusanywa katika chombo au yaliyojikusanya katika ardhi yakiwa na ujazo chini ya Qullatain* au chini ya ujazo wa pipa lenye ujazo wa madebe 12 au chini ya ujazo wa lita 224. Mfano wa maji machache ni ya ndoo, maji ya mtungi na maji yaliyojikusanya kwenye vidimbwi vidogo vidogo wakati wa mvua.

Maji machache hayatafaa kujitwaharishia iwapo

(i) yataingiwa na najisi japo kidogo sana.
(ii) Iwapo yatakuwa yametumika katika kujitwaharishia humo humo kwa kuondoa najisi au Hadath.
(iii) Iwapo yatakuwa yametumika kwa kufulia au kuoshea vyombo au kuogea humo humo.
(iv) Iwapo yataingiwa na kitu kikayabadilisha asili yake katika rangi, harufu au tamu(ladha).

Kutokana na haya tunajifunza kuwa, tunapokuwa na maji machache hatuna budi kuwa waangalifu wakati wa kuyatumia ili tusiyaharibu. Tusijitwaharishe ndani ya vyombo vilivyohifadhia maji hayo, bali tuyateke na kujitwaharisha mbali nayo. Kwa mfano tunakoga kwa kutumia kata na tunatawadha kwa kutumia kopo au birika.

**(d) Maji makombo**

Maji makombo ni maji yaliyonywewa na binaadamu au mnyama yakabakishwa.Maji makombo yanafaa kujitwaharishia ila yale yaliyonywewa na kubakishwa na mbwa au nguruwe.

### Udongo safi

Udongo safi ni ule ulioepukana na najisi na ukabakia katika asili yake na kutochanganyika na kitu kama vile unga, majivu au vumbi la mkaa, vumbi la mbao (saw dust) n.k. kwa kawaida udongo wote katika ardhi ni safi.

### Kujitwaharisha Kutokana na Najisi

Kutokana na uzito wa kujitwaharisha tutazigawanya najisi katika makundi matatu

(a) Najisi ndogo.
(b) Najisi kubwa na
(c) Najisi hafifu

### (a) Najisi Ndogo.

Inahusu najisi zote isipokuwa najisi ya mbwa na nguruwe. Namna ya kujitwaharisha kutokana na najisi ndogo ni kuosha paliponajisika kwa maji safi mpaka iondoke rangi na harufu ya najisi.

Kama tunatumia maji machache ambayo huharibika mara tu yatakapoingiwa na japo najisi ndogo, hatuna budi kutumia kata au chombo kingine cha kuchotea maji na kujitwaharisha pembeni kwa kujimiminia maji kupitia sehemu ile yenye najisi mpaka najisi hiyo iondoke.

Katika hali ya kawaida, maji safi hutumika kwa kustanjia. Tunazitwaharisha sehemu zetu za siri kwa mkono wa kushoto mpaka tuhakikishe kuwa najisi imeondoka. Katika hali ya dharura ya kukosa maji au ugonjwa usioruhusu kutumia maji, tunaruhusiwa kustanji kwa kutumia vitu vikavu kama vile karatasi laini (toilet paper), mawe, n.k. Tukistanji kwa vitu vikavu, kama vile mawe makavu tutapangusa sehemu zetu za siri kwa mawe matatu. Kama najisi ingalipo, tutaongeza mawe mawili mawili mpaka turidhike kuwa najisi imeondoka.

### (b) Najisi Kubwa:

Najisi hii imeitwa kubwa kutokana na uzito unaochukuliwa katika kujitwaharisha.

Namna ya kujitwaharisha kutokana na najisi ya mbwa na nguruwe ni kuikosha sehemu hiyo mara saba na mojawapo katika hayo makosho saba iwe kwa kusugua kwa udongo safi. Hivi ndivyo Mtume (s.a.w) alivyotufundisha kama inavyobainika katika Hadithi zifuatazo:

*Abu Hurairah amesimulia kuwa Mtume (s.a.w) amesema: Kutwaharisha chombo cha yeyote kati yenu, baada ya kulambwa na mbwa ni kukikosha mara saba, ukitumia udongo katika safari ya kwanza. (Muslim)*

*Ibn Mughaffal amesimulia kuwa Mtume (s.a.w) aliamuru kuuawa mbwa (wenye ugonjwa au wasio na waangalizi) kisha akaulizwa: "Vipi juu ya mbwa wengine?" Kisha akaruhusu kufuga mbwa kwa ajili ya kuwindia, kuchungia (na ulinzi kwa ujumla) na akasema: Mbwa atakapolamba*

*chombo, kioshe mara saba na kisugue na udongo kwa mara ya nane". (Muslim)*

Hadithi hizi zinatupa msimamo wa Uislamu juu ya mbwa, ufugaji wake na namna ya kujitwaharisha kutokana na naye. Tumejifunza kuwa japo mbwa ni mnyama najisi tunaruhusiwa kumfuga kwa ajili ya kuwindia, na ulinzi wa nyumbani. Kama itabidi tufuge mbwa kwa ajili ya madhumuni haya, tutalazimika kuwafunza na kuwatayarishia makao yao yasiyohusiana na watu kwa malazi, chakula au ukaribu wowote.

Katika utafiti uliofanywa na Daktari mmoja huko Marekani (1978) iligundulika kuwa mbwa (na nguruwe) ni wachukuzi wa vijidudu vya magonjwa mbali mbali. Baadhi ya vijidudu hivyo havifi kwa dawa yoyote isipokuwa udongo.

### (c) Najisi Hafifu:

Najisi hafifu ni mkojo wa mtoto mdogo wa kiume chini ya miaka miwili ambaye hajaanza kula chakula ila maziwa tu. Uhafifu wa najisi hii hupatikana katika kutwaharisha. Tofauti na najisi ndogo, najisi hafifu hutwaharishwa kwa kumwagia maji tu ile sehemu iliyonajisika bila ya kusugua. Hivi ndivyo alivyofanya Mtume (s.a.w) kama tunavyojifunza katika hadith ifuatayo:

*Aysha (r.a) amesimulia kuwa mtoto mchanga wa kiume aliyekuwa angali ananyonya aliletwa kwa Mtume (s.a.w) aliagiza maji na kuyamiminia juu ya pale palipo kojolewa". (Muslim)*

### Hadathi Ndogo

Kuwa katika hadathi ndogo ni kuwa katika hali ya kutokuwa na udhu na huondolewa hadathi hiyo kwa kutia udhu baada ya kuzingatia na kutekeleza kwa ukamilifu masharti na nguzo za udhu.

### Masharti ya udhu

Ili udhu wa mtu ukamilike hapana budi kuchunga na kutekeleza masharti yafuatayo kabla ya kuanza kutawadha:

(i) Kuwa na "*maji safi*" ya kutosha kuweza kutitirika (yasiwe ya kupakaza tu) katika viungo vya udhu vinavyooshwa.

(ii) Kutokuwa na kitu kilichogandamana (kama vile *lami, rangi, ulimbo, n.k*) kitakachoweza kuzuia maji kufika kwenye ngozi ya viungo vya udhu. Ni lazima mtu aondoe hicho kilichogandamana ndio aanze kutawadha.

(iii) Kutokuwa na uchafu mwingineo au vumbi,la aina yoyote au kitu chochote juu ya viungo vya kutawadhia kitakachobadilisha rangi, harufu au tamu ya maji yatakayotiririka humo. Ni sharti mtu awe msafi kwanza ndipo aanze kutawadha.

(iv) Kuondoa najisi juu ya viungo vya udhu kabla ya kuanza kutawadha.

(v) Kukata kucha ndefu zinazozuia maji kufikia kona za vidole, kabla ya kuanza kutawadha.

Masharti haya haya ndiyo masharti ya kuoga katika kuondoa hadathi ya kati na kati na hadathi kubwa, bali pamoja na hayo,kwa wanawake wenye kusuka, hawana budi kufumua misuko yao isiyoruhusu maji kupenya.

## Nguzo za Udhu

Allah (s.w) anatufunza kutia udhu katika aya ifuatayo:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓاْ إِذَا قُمۡتُمۡ إِلَى ٱلصَّلَوٰةِ فَٱغۡسِلُواْ وُجُوهَكُمۡ وَأَيۡدِيَكُمۡ

إِلَى ٱلۡمَرَافِقِ وَٱمۡسَحُواْ بِرُءُوسِكُمۡ وَأَرۡجُلَكُمۡ إِلَى ٱلۡكَعۡبَيۡنِۚ

*Enyi mlioamini! Mnaposimama ili mkaswali, basi osheni nyuso zenu, na mikono yenu mpaka vifundoni, na mpake vichwa vyenu, na (osheni) miguu yenu mpaka vifundoni...” (5:6)*

Kutokana na aya hii na kutokana na mafundisho ya Mtume (s.a.w) nguzo au faradhi za udhu ni hizi zifuatazo

1. Kutia nia moyoni kuwa unatawadha.
2. Kuosha uso kwa ukamilifu kwa kufikisha maji mpaka kwenye mipaka yote ya uso.
3. Kuosha mikono miwili mpaka vifundoni.
4. Kupaka maji kichwani.
5. Kuosha miguu, mpaka vifundoni.
6. Kufuata utaratibu huu kwa kuanza (1) hadi (5) katika mfuatano huu.

## Sunnah za Udhu

Mtume Muhammad (s.a.w) pamoja na kutekeleza nguzo za udhu alikuwa akiongezea yafuatayo wakati wa kutawadha;

1. Kupiga mswaki kabla ya kuanza kutawadha.

2. Kuanza kutawadha kwa kuosha viganja vya mikono na kuanza kitendo hicho kwa ***"Bismillahi"***.
3. Kusukutua na kupandisha maji puani.
4. Kupaka maji shingoni wakati wa kupaka maji kichwani.
5. Kuosha masikio mara tu baada ya kupaka maji kichwani.
6. Kuosha kila kiungo cha udhu mara tatu.
7. Kuanza kuosha viungo vya kulia (kuanza na mkono na mguu wa kulia).
8. Kuelekea Qibla na kuleta dua baada ya kutawadha ifuatayo:

أَشْهَدُ أَنْ لاَ إِلَـهَ إِلاَّ اللَّـهُ وَحْـدَهُ لاَشَرِيكَ لَهُ وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّداً عَبْـدُهُ وَرَسُولُهُ.

اللَّهُمَّ اجْعَلْنِي مِـنَ التَّوَّابِيـنَ وَاجْعَلْنِي مِنَ الْمُتَطَهِّرِينَ. وَاجْعَلْنِي مِنْ عِبَادِكَ الصَّالِحِينَ

سُبْحَانَكَ اللَّهُمَّ وَبِحَمْدِكَ أَشْهَدُ أَنْ لاَ إِلَهَ إِلاَّ أَنْـتَ أَسْتَغْفِرُكَ وَأَتُـوبُ إِلَيْكَ.

***Ash-hadu an-laailaha illallahu wah-dahu laa shariikalahu wa-ash-hadu anna Muhammadan a'bduhu warasuuluhu.***

***Allahuma j-'alniy minattawwabiina, waj-'alniy minal-mutatwâhhiriina, waj-'alniy min ibaadika sw-swaalihiina.***

***Sub-haanaka llahumma wabihamdika, Ash-hadu an-laailaha illaa anta astaghfiruka wa-atuubu ilayka.***

**Tafsiri**

*"Nashuhudia kuwa hapana Mola ila Allah aliye mmoja tu, Asiye na mshirika wake. Na ninashuhudia kuwa Muhammad ni mja wake na Mtume wake. Ee! Allah nijaalie niwe miongoni mwa wenye kutubia na unijaalie niwe miongoni mwa wenye kutwahirika (kutakasika) na unijaalie niwe miongoni mwa waja wako wema. Utukufu ni wako, Ee, Allah umetukuka; Ninashuhudia kuwa hakuna Mola ila Wewe. Naomba msamaha wako na natubia kwako".*

**Namna ya Kutia Udhu Kama alivyofanya Mtume (s.a.w):-**

1. kupiga msaki

2. kusema Bismillaah na kuanza kuosha viganja vya mikono (*mara tatu*) -**hatua 1**
3. Kusukutua na kupandisha maji puani (*mara tatu)* - **hatua 2 na 3**
4. Kuosha uso kwa ukamilifu (*mara tatu*) - **hatua 4**
5. Kuosha mkono wa kulia mpaka kwenye fundo (*mara tatu*) -**hatua 5**
6. Kuosha mkono wa kushoto mpaka kwenye fundo (*mara tatu*) - **hatua 6**
7. Kupaka maji kichwani- **hatua 7**
8. Kuosha masikio (*mara tatu*)- **hatua 8**
9. Kuosha mguu wa kulia halafu wa kushoto mpaka kwenye fundo (*mara tatu*)- **hatua 9**.




***Kielelezo*: Hatua za kuchukua udhu**

Baada ya kumaliza utasimama na kuelekea kibla kisha kuleta dua kamal ilibyoelezwa hapo juu.

**Yaliyoharamishwa kwa asiye na udhu**

Mtu asiye na udhu haruhusiwi kufanya yafuatayo:

1. Kuswali.
2. Kutufu.

Mtu asiye na udhu anaruhusiwa kuchukua msahafu (Qur-an) na kusoma. Kama tunavyojifunza katika hadith ifuatayo:

*Ally (r.a) amesimulia: Mtume (s.a.w) alikuwa akitoka chooni kisha akatusomea Qur-an na hakuna chochote kilichomzuia kusoma Qur-an ila alipokuwa na janaba". (Abuu Daud, Nisai, Ibn Majah)*

### Yanayotengua Udhu

Mtu aliyetawadha hutokwa na udhu wake kwa kupatwa au kutokewa na mojawapo kati ya haya yafuatayo:

1. Kutokwa na kitu chochote kwenye sehemu za siri. Ni pamoja na kwenda haja ndogo au kubwa. Kutokwa na upepo, maji maji yatokayo katika utupu wa mbele kutokana na matamanio au sababu nyinginezo.

2. Kutokwa na fahamu kwa kulala usingizi kwa kuegemea mahali bila ya kumakinisha makalio yake ardhini. Tunajifunza katika hadithi ifuatayo:
   *Amesimulia Basrah (r.a) kuwa Mtume (s.a.w) kasema:Kutawadha kuna kuwa lazima kwa mwenye kulala usingizi kitandani, kwa sababu anapolala kitandani maungo yake hulegea".(Tirmidh, Abuu Daud).*

3. Kushika sehemu za siri kwa viganja vya mikono kama tunavyojifunza katika hadithi ifuatayo:
   *Amesimulia Basrah (r.a) kuwa Mtume (s.a.w) kasema: "Mmoja wenu atakapogusa tupu yake, na aende kutawadha tena".(Malik, Ahmad, Abuu Daud, Tirmidh, Nasai, Ibn Majah)*

Haya matatu ndio yanayotengua udhu bila ya khitilafu yoyote kati ya Waislamu.

### Hadathi ya kati na kati (Janaba).

Mtu hupatwa na hadathi ya kati na kati kwa kupatwa na Janaba. Janaba ni hali inayompata mtu baada ya kufanya kitendo cha jimai (kitendo cha ndoa) au kutokwa na manii kwa kuota au kwa namna nyingineyo. Mtu mwenye janaba yuko katika hali chafu kulingana na sharia ya Allah (s.w) na ameharamishiwa kufanya ibada hizi:

(i) Kuswali (rejea Qur-an 4:43, 5:6)
(ii) Kutufu.
(iii) Kukaa Msikitini.

*"Aysha (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: Msielekeze milango ya nyumba hizi msikitini kwa sababu si halali msikiti kwa mwanamke mwenye hedhi au kwa mtu mwenye janaba". (Abu Daud)*

(iv) Kuisoma Qur-an hata kwa moyo.

*Ibn Umar ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: "Wenye hedhi na wenye janaba hawatasoma chochote kutoka kwenye Qur-an" (Tirmidh)*

Si vibaya kwa mtu mwenye janaba kula, kuongea au kugusana na watu. Pia kutokana na mafundisho ya Mtume (s.a.w) si lazima mtu kukoga mara tu baada ya kufanya kitendo cha jimai na mkewe, hasa ikiwa usiku bali anatakiwa aoshe sehemu za siri na atawadhe alale, kisha akiamka ndipo akoge kwa kujitwaharisha kwa ajili ya swala ya Alfajiri. Mafundisho haya tunayapata katika hadithi ifuatayo:

*Aysha (r.a) ameeleza kuwa: Mtume (s.a.w) alipotaka kula au kulala akiwa na janaba, alikuwa kwanza akitawadha kama anavyotawadha kwa ajili ya swala. (Bukhari na Muslim).*

### Hadathi Kubwa:

Hadath kubwa huwapata wanawake tu wanapokuwa na Hedhi (damu ya mwezi) au Nifasi (damu ya uzazi).

Yafuatayo yameharamishwa kwa wenye hadath kubwa:

(i) Kusali na Kutufu.
(ii) Kukaa Msikitini.
(iii) Kusoma Qur'an, kugusa na kuchukua msahafu (Qur-an)
(iv) Kufunga.
(v) Kufanya kitendo cha ndoa.
(vi) Kutalikiwa (kupewa talaka).

Namna ya kujitwaharisha na hadath ya kati na kati na hadath kubwa ni kukoga kwa maji safi kwa kutekeleza masharti na nguzo za kukoga josho la wajibu.

### Masharti ya Kuoga

Masharti ya kuoga ni sawa tu na yale masharti ya udhu ila hapa yanahusu mwili mzima.

### Nguzo za Kuoga

**Kwanza**, kutia nia moyoni kuwa unaoga kwa madhumuni ya kujitwaharisha, kutokana na janaba, hedhi, au nifasi. Mahali pa nia ni moyoni na wakati wa kunuiwa ni pale unapoanza kuosha kiungo cha kwanza.

**Pili**, kueneza maji mwili mzima. Ili kuhakikisha kuwa umeeneza maji mwili mzima ni vyema ufuate mafundisho ya Mtume (s.a.w). Mtume

katika kuoga alikuwa akianza kwa kuosha sehemu za siri, kisha alikuwa akitia udhu, kisha alikuwa akijimiminia maji kichwani mara tatu, kisha alikuwa akieneza maji mwili mzima kwa kuanzia upande wa kulia na kumalizia upande wa kushoto, pote mara tatu tatu.

### Kutayammamu

Kutayammamu ni kujitwaharisha kwa kutumia udongo safi. Waislamu huruhusiwa kujitwaharisha kwa kutayammamu katika hali ya dharura ya:

- (i) Ugonjwa usioruhusu kutumia maji.
- (ii) Kuwa safarini na kukosa maji ya kutumia au kuwa katika mazingira ya safari yasiyoruhusu kutumia maji.
- (iii) Kukosa maji.

Tunajifunza haya katika aya ifuatayo:

وَإِن كُنتُمْ جُنُبًا فَاطَّهَّرُوا ۚ وَإِن كُنتُم مَّرْضَىٰٓ أَوْ عَلَىٰ سَفَرٍ أَوْ
جَآءَ أَحَدٌ مِّنكُم مِّنَ ٱلْغَآئِطِ أَوْ لَٰمَسْتُمُ ٱلنِّسَآءَ فَلَمْ تَجِدُوا۟
مَآءً فَتَيَمَّمُوا۟ صَعِيدًا طَيِّبًا فَٱمْسَحُوا۟ بِوُجُوهِكُمْ وَأَيْدِيكُم
مِّنْهُ ۚ مَا يُرِيدُ ٱللَّهُ لِيَجْعَلَ عَلَيْكُم مِّنْ حَرَجٍ وَلَٰكِن يُرِيدُ لِيُطَهِّرَكُمْ
وَلِيُتِمَّ نِعْمَتَهُۥ عَلَيْكُمْ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿٦﴾

*"Na mkiwa wagonjwa au mumo safarini au mmoja wenu ametoka chooni au mmeingiliana na wanawake, na hamkupata maji, basi, kusudieni udongo ulio safi (tayammamuni) kwa kuzipaka nyuso zenu na mikono yenu. Hapendi Mwenyezi Mungu kukutieni katika taabu; bali anataka kukutakaseni na kutimiza neema Yake juu yenu ili mpate kushukuru". (5:6)*

Katika aya hii tunajifunza kuwa kutayammamu kumeruhusiwa kwa wakati wa dharura tu. Funzo hili tunalipata katika maneno ya Allah kuwa, "*Hapendi Allah kukutieni katika taabu*"

### Masharti ya Kutayammamu

Tayammamu haitaswihi mpaka yatakapozingatiwa masharti

yafuatayo:

(i) Ipatikane dharura inayompelekea mtu kuruhusiwa kutayammamu.

(ii) Pawe na hitajio la tayammamu kama vile kuswali, kutufu n.k.

(iii) Kama kusudio la kutayammamu ni kutekeleza swala ya faradh, tayammamu hiyo ifanyike baada ya kuingia wakati wa swala hiyo.

(iv) Pawe na udongo safi (ulio twahara na ulio katika asili yake) ulio mkavu na wenye vumbi vumbi.

**Nguzo za Tayammam**

Nguzo za tayammam zinabainishwa na aya ifuatayo:

• • فَتَيَمَّمُواْ صَعِيدًا طَيِّبًا فَٱمْسَحُواْ بِوُجُوهِكُمْ وَأَيْدِيكُمْ

*"... Basi kusudieni udongo ulio safi na kupaka nyuso zenu na mikono yenu..." (4:43)*

Aya hii inabainisha kuwa nguzo za tayammam ni:

(i) Nia (kukusudia udongo).

(ii) Kupaka uso.

(iii) Kupaka mikono.

(iv) Kufuata utaratibu huu.

**Namna ya Kutayammamu**

(i) Kutia nia. Nia huwekwa pale Muislamu anapokusudia udongo na kuutayarisha kwa ajili ya tayammamu.

(ii) Kupaka uso. Piga udongo uliokusudia kwa viganja vyote viwili vya mikono, kisha puliza viganja ili takataka na vijiwe jiwe vilivyo juu yake vitoke. Kisha paka uso wako kwa kutumia viganja viwili kwa pamoja.



(iii) Kupaka mikono. Anza kupaka mkono wa kulia kwa kiganja cha kushoto. Weka kiganja cha kushoto nyuma ya kiganja cha kulia. Paka mkono wa kulia kuanzia hapo kwa kurudisha kiganja cha kushoto kinyume nyume mpaka kwenye fundo kisha kupaka sehemu ya juu ya mkono wa kulia na kuishia kwenye kidole gumba bila ya kuugusa kiganja mkono wa kulia. Utarudia zoezi hilo kupaka mkono wa kushoto.

### Kutumia Ukuta kwa Ajili ya Tayammamu

Mtume (s.a.w) aliwahi kutayammamu kwa kutumia ukuta wa nyumba kama inavyobainika katika hadith ifuatayo:

*"Abu Juhaim Al-Ansary (r.a) amehadithia kuwa Mtume wa Allah (Rehema na amani ziwe juu yake) alikuja kutoka upande wa Bir-al-Jamal. Mtu mmoja alimuona akamsalimia. Lakini Mtume hakumjibu, bali alienda kwenye ukuta wa nyumba akapakaza viganja vyake vumbi la ukuta kisha akapaka uso wake wote, kisha mkono wa kulia na wa kushoto, ndipo akamrudishia salamu". (Bukhari na Muslim).*

Kutokana na hadithi hii tunajifunza kuwa vumbi kwa ajili ya tayammamu si lazima liwe la ardhini tu bali ukuta au jiwe au sehemu yoyote yenye vumbi vumbi iliyotwahara inafaa kutumika kwa ajili ya tayammamu. Kwa mfano wakati wa mvua ambapo udongo umelowana ukuta wa nyumba au ukuta wa chombo cha usafiri au sehemu yoyote yenye vumbi vumbi au iliyokavu na twahara, itakuwa aula kuitumia kwa tayammamu.

## 2. Sitara

Sitara ni sharti la pili ya kusimamisha swala. Ili Muislamu swala yake isimame analazimika kusitiri uchi wake kulingana na mipaka iliyowekwa na Mwenyezi Mungu (s.w). Sio kujisitiri kwa kufuata matashi ya jamii ya Kitwaghuti.

### Sitara ya Mwanamume

Utupu wa mwanamume ni sehemu yote iliyo kati ya kitovu na magoti. Hivyo, Muislamu mwanamume akiwa na nguo ya kutosha kufunika kitovu na magoti na sehemu yote iliyo baina ya hivyo anaweza kuswali.

Lakini kwa ukamilifu mtu anapoweza kuwa katika hali ya kawaida avae kama kawaida ya kuvaa. Tukumbuke kuwa Allah (s.w) anatutaka tujipambe wakati wa kwenda kwenye swala. Anatuagiza:

۞يَٰبَنِيٓ ءَادَمَ خُذُواْ زِينَتَكُمۡ عِندَ كُلِّ مَسۡجِدٖ

*“Enyi wanaadamu, chukueni, mapambo yenu katika kila swala...” (7:31)*

Kujipamba hapa ni pamoja na kuvaa vizuri na kujipaka manukato ambayo kwa wanaume ni Sunnah.Wanawake wanaruhusiwa kupaka manukato yasiyo na harufu kali.

**Sitara ya Mwanamke**

Kutokana na umbile lake, *aurah* (uchi) ya mwanamke ni mwili mzima isipokuwa uso na viganja vya mikono. Muislamu mwanamke swala yake haitaswihi iwapo sehemu nyingine yoyote ya mwili itakuwa wazi bila kufunikwa wakati wa swala. Kuhusu vazi la mwanamke wa Kiislamu, tunafahamishwa kwa uwazi katika aya ifuatayo;

وَقُل لِّلۡمُؤۡمِنَٰتِ يَغۡضُضۡنَ مِنۡ أَبۡصَٰرِهِنَّ وَيَحۡفَظۡنَ فُرُوجَهُنَّ وَلَا
يُبۡدِينَ زِينَتَهُنَّ إِلَّا مَا ظَهَرَ مِنۡهَاۖ وَلۡيَضۡرِبۡنَ بِخُمُرِهِنَّ عَلَىٰ
جُيُوبِهِنَّۖ وَلَا يُبۡدِينَ زِينَتَهُنَّ إِلَّا لِبُعُولَتِهِنَّ أَوۡ ءَابَآئِهِنَّ أَوۡ ءَابَآءِ
بُعُولَتِهِنَّ أَوۡ أَبۡنَآئِهِنَّ أَوۡ أَبۡنَآءِ بُعُولَتِهِنَّ أَوۡ إِخۡوَٰنِهِنَّ أَوۡ بَنِيٓ إِخۡوَٰنِهِنَّ
أَوۡ بَنِيٓ أَخَوَٰتِهِنَّ أَوۡ نِسَآئِهِنَّ أَوۡ مَا مَلَكَتۡ أَيۡمَٰنُهُنَّ أَوِ ٱلتَّٰبِعِينَ
غَيۡرِ أُوْلِي ٱلۡإِرۡبَةِ مِنَ ٱلرِّجَالِ أَوِ ٱلطِّفۡلِ ٱلَّذِينَ لَمۡ يَظۡهَرُواْ عَلَىٰ
عَوۡرَٰتِ ٱلنِّسَآءِۖ وَلَا يَضۡرِبۡنَ بِأَرۡجُلِهِنَّ لِيُعۡلَمَ مَا يُخۡفِينَ مِن
زِينَتِهِنَّۚ وَتُوبُوٓاْ إِلَى ٱللَّهِ جَمِيعًا أَيُّهَ ٱلۡمُؤۡمِنُونَ لَعَلَّكُمۡ تُفۡلِحُونَ ٣١

*Na waambie Waislamu wanawake wainamishe macho yao, na wazilinde tupu zao, wala wasidhihirishe viungo vyao isipokuwa vinavyodhihirika (na ni uso na vitanga vya mikono). Na waangushe shungi zao mpaka vifuani mwao, na wasioneshe mapambo yao ila kwa waume zao, au baba zao, au baba za waume zao.... au wanawake wenzao, au wale iliyowamiliki mikono yao ya kuume (watumwa zao), au wafuasi wanaume wasio na matamanio (kwa wanawake) au watoto ambao hawajajua mambo yanayohusu uke. Wala wasipige miguu yao ili yajulikane yaliyofichwa katika mapambo yao. Na tubieni nyote kwa Mwenyezi Mungu, enyi Waislamu ili mpate kufaulu. (24:31)*

Neno "*ziinah*" lililotumika katika aya hii lina maana mbili; Uzuri wa kuumbika kiwiliwili (na) uzuri wa kujipamba kama vile pete, vidani na nguo.

Aya hii inatupa fundisho kuwa, sitara ya mwanamke ni mwili mzima, kwa vile kila sehemu ya mwili wa mwanamke ni pambo lenye kuwavutia wanaume jambo ambalo huweza kuleta vishawishi na kuruka mipaka ya utu. Hivyo Allah (s.w) ametoa tahadhari kuwa wanawake wasidhihirishe miili yao na mapambo yao na wala wasionyeshe dalili ya kuwa na mapambo waliyoyavaa kwa mitingisho ya mwili isipokuwa kwa wale wasioweza kuwatamani wakiwa ni miongoni mwa Maharimu zao, wanawake wenzao na watoto.

Pia pamoja na kujifunika mwili mzima wanawake wanaamrishwa wateremshe shungi zao ili pamoja na kufunika nywele zifunike pia shingo na kifua.

*Aisha (a.s) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: Swala ya mwanamke baleghe haikubaliki bila ya shungi.*

Katika Hadith tunafahamishwa kuwa, pamoja na kuteremsha sharti la kufunika mwili mzima na kuteremsha shungi, **sharti la pili** la vazi la mwanamke wa Kiislamu ni kuwa vazi hilo lisibane mwili kiasi cha kuonyesha ramani ya mwili. **Sharti la tatu** la vazi la Kiislamu ni kuwa liwe zito kiasi cha kutoweza kuonyesha rangi ya ngozi au umbo la mwili. Kama tuonavyo umezuka mtindo wa wanawake kuvaa nguo zinazofunika mwili bila ya kuficha. Juu ya mtindo huu Mtume (s.a.w) amesema:

*Katika vizazi vijavyo vya umma wangu watakuwepo wanawake ambao watavaa lakini watabaki uchi. Hao hawataingia Peponi wala kupata harufu yake.*

Pia Hadithi ifuatayo inafafanua zaidi:
*Aisha (r.a) amesimulia kuwa siku moja Asma'a bint Abubakar alikuja kwa Mjumbe wa Allah wakati akiwa amevalia nguo nyepesi, Mtume (s.a.w) alimwendea na kumwambia: "Ewe Asmaa msichana anapofikia balegh (anapovunja ungo) si sawa sehemu yoyote ya mwili wake kuachwa wazi isipokuwa hii na hii. Alionyesha uso na viganja. (Abu Daud).*

**Sharti la nne**. Pia vazi la mwanamke lisiwe lenye kuvutia sana kiasi cha kuwa sababu ya kuvuta macho ya watu. Wake wa Mtume (s.a.w) na wanawake wa Kiislamu wanaamrishwa katika Qur-an:

يَـٰٓأَيُّهَا ٱلنَّبِىُّ قُل لِّأَزْوَٰجِكَ وَبَنَاتِكَ وَنِسَآءِ ٱلْمُؤْمِنِينَ يُدْنِينَ عَلَيْهِنَّ
مِن جَلَـٰبِيبِهِنَّ ۚ ذَٰلِكَ أَدْنَىٰٓ أَن يُعْرَفْنَ فَلَا يُؤْذَيْنَ ۗ وَكَانَ ٱللَّهُ غَفُورًا
رَّحِيمًا ﴿٥٩﴾

*Ewe Mtume! Waambie wake zako, na binti zako, na wanawake wa kiislamu, wajiteremshie vizuri shungi (nguo) zao. Kufanya hivyo kutawapelekea wajulikane upesi (kuwa ni watu wa heshima), wasiudhiwe. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe na Mwingi wa kurehemu(33:59)*



Katika aya hii imebainishwa kwa uwazi kuwa lengo kubwa la kujisitiri ni kuchunga heshima ya mwanamke wa Kiislamu na kuwatakasa na mambo maovu.

Masharti mengine ya mavazi ya Kiislamu ni kwamba vazi la mwanamke Muislamu lisiwe sawa na lile vazi linalojulikana kuwa ni la wanaume:

*Imepokewa kutoka kwa Ibn 'Abbas (r.a) kuwa Mtume (s.a.w) amewalaani wanaume wanaojifananisha na wanawake na wanawake wanaojifananisha na wanaume.*

Pia vazi lisiwe la fahari, majivuno na kibri. Hii yote ni kumtakasa mwanaadamu na uchafu wa nafsi na kumvisha joho la usafi na utu.

Hivyo ni dhahiri kwamba Muislamu akitekeleza kwa ukamilifu sharti hili la sitara kwa kuzingatia masharti haya ya kujisitiri na akawa anafanya hivyo kwa swala zote tano za siku, na akawa anavaa nguo nzuri katika swala, atakuwa msafi wa mwili na mwenye kuheshimika katika jamii.

Swala hutoa fundisho na mazoezi makubwa mno ya kujisitiri na kujiheshimu hasa kwa wanawake.Kwa mfano mwanamke Muislamu anayejisitiri vilivyo kwenye swala, humzoesha kubakia katika hali ya sitara anapokuwa nje ya swala katika maisha yake ya kila siku. Kwani Mungu yule yule aliyemuamrisha kujisitiri wakati wa swala ndio huyo huyo aliyemuamrisha kujisitiri anapokuwa mbele ya wasio maharimu wake.

Je, si jambo la kushangaza kumuona mwanamke anayejisitiri vizuri wakati wa swala, na kutembea uchi barabarani mara tu baada ya swala? Je, anaweza kusema swala yake imemsaidia kumtakasa na mambo maovu na machafu? Swala inayomtakasa mja na mambo maovu na machafu ni ile inayomfanya mja afuate kwa kila hali mwenendo wa maisha anaouridhia Allah (s.w) katika kila kipengele cha maisha yake.

Pamoja na kutekeleza masharti ya mavazi, mavazi hayo pia hayana budi kuwa twahara.

### 3. Kuchunga Wakati

... إِنَّ ٱلصَّلَوٰةَ كَانَتۡ عَلَى ٱلۡمُؤۡمِنِينَ كِتَٰبًا مَّوۡقُوتًا ﴿١٠٣﴾

*"... Kwa hakika swala kwa waumini ni faradhi iliyowekewa nyakati makhususi" (4:103).*

Swala tano zilizofaradhishwa kwa Umma huu wa Mtume Muhammad (s.a.w) ni:- Adhuhuri, Alasiri. Magharibi, Ishai na Alfajiri. Wakati wa kuswali kila swala unabainishwa katika hadith ifuatayo:

*"Abdullah Ibn 'Amir amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema, Wakati wa swala ya adhuhuri ni kuanzia jua linapopinduka hadi kivuli cha mtu kinapokuwa sawa na kimo (urefu) chake. Na unamalizika kwa kuingia*

*Alasiri. Na muda wa swala ya Alasiri (ni kuanzia inapomalizika Adhuhuri) hadi jua linapopiga umanjano. Muda wa swala Magharibi (ni mara baada ya kuzama jua na) utabakia mpaka wingu jekundu litoweke. Muda wa swala ya Isha (ni baada ya kutoka Mgharibi) na kubakia hadi katikati ya usiku. Na wakati wa swala ya Alfajiri unaanza kwa kudhihirika kwa ukanda mweupe mpaka kabla ya kuchomoza jua. Jua linapochomoza jizuilie kuswali kwani huchomoza kati ya pembe za shetani. (Muslim)*

Kutokana na hadithi hii, nyakati za swala tano ni:

**Adhuhuri**: Inayopasa kuswaliwa mara tu jua linapogeuka kuelekea Magharibi mpaka kuingia swala ya al'asiri.

**Al'asiri**: Huanza pale urefu wa kivuli unapokuwa sawa na kitu chenyewe mpaka kivuli kinapokuwa mara dufu ya urefu wa kitu chenyewe.

**Magharibi**: Huanza mara tu jua linapozama na kuingia pale mawingu mekundu yanapobadilika kuwa ya kimanjano wakati inapoingia swala ya Isha.

**Isha**: Kuanzia mara tu yanapobadilika mawingu kuwa ya kimanjano mpaka usiku wa manane.

**Alfajir**: Huingia kwa kutokea alama ya mstari mweupe unaotokea Mashariki ambao ni alama ya kwisha kwa usiku na kuanza kwa mchana. Kuingia kwa Alfajiri kwa alama hii ya uzi mweupe ndio mwisho wa kula daku kwa mwenye kufunga kama isemavyo Qur-an:

...وَكُلُوا۟ وَٱشْرَبُوا۟ حَتَّىٰ يَتَبَيَّنَ لَكُمُ ٱلْخَيْطُ ٱلْأَبْيَضُ مِنَ
ٱلْخَيْطِ ٱلْأَسْوَدِ مِنَ ٱلْفَجْرِ ۖ ... ﴿١٨٧﴾

*"... Na kuleni na kunyweni mpaka ubainike kwenu weupe wa Alfajiri katika weusi wa usiku ..." (2:187)*

Hizi ndizo swala tano na nyakati zake kama alivyotufundisha Mtume (s.a.w) ambazo hutegemea uchunguzi wa mwendo wa jua katika saa ishirini na nne za siku. Utaalamu wa karne hii umerahisisha kuzijua nyakati za mwanzo na mwisho wa kila, swala kwa kutengeneza ratiba ya nyakati za swala kwa kutumia takwimu za mwendo wa jua

katika nyakati zilizonukuliwa kwa muda mrefu na wachunguzi wa hali ya hewa.

Kuswali swala katika wakati wa mwanzo ni bora zaidi kama tunavyojifunza katika hadith ifuatayo:-

*"Ummi Farawata(r.a) amesimulia kuwa Mtume (s.a.w) aliulizwa, ni kitendo gani kilicho bora kuliko vyote? Akajibu: "Swala wakati wake wa mwanzo".(Ahmad, tirmidh, Abu Daud).*

**Swala hukubaliwa kwa Kuwahi rakaa moja ndani ya wakati**

Iwapo Muislamu kwa dharura atachelewa kuiswali swala ya faradh kiasi cha kupata rakaa moja tu ndani ya wakati,swala yake itakubaliwa kwa mujibu wa Hadith ifuatayo:

*Abu Hurairah(r.a) ameeleza kuwa Mtume (s.a.w) amesema: "Mwenye kupata rakaa moja ya swala ameipata swala".(Maimamu sahihi sita tu).*

Si vizuri kabisa kwa Muislamu, kwa makusudi kuchelewesha swala kiasi hicho.

**Nyakati zilizoharamishwa kuswali**

Kwa mujibu wa Hadith mbali mbali kuna nyakati tano zilizoharamishwa kuswali na Mtume (s.a.w):-

1. Kuswali sunnah baada ya swala ya Alfajiri mpaka jua litakapochomoza.
2. Wakati wa kuchomoza jua mpaka litakapopanda juu kabisa kiasi cha urefu wa mkuki.
3. Jua linapokuwa katikati wakati wa mchana mpaka litakaposogea kidogo upande wa Magharibi.
4. Kuswali sunnah baada ya swala ya alasiri mpaka jua litakapozama kabisa.
5. Wakati wa kuzama jua.

## Adhana

Katika kutekeleza amali ya kusimamisha swala kwa nyakati zake na hasa za mwanzo, kumewekwa mwito maalum wa kuwakumbusha na kuwafahamisha waumini kuingia kwa kila swala. Mwito huu ni Adhana. Adhana ni miongoni mwa sunnah kubwa kabla ya swala.

## Historia ya Adhana

Waislamu walipohamia Madinah walipata hali ya utulivu na amani pamoja na uhuru kamili wa kuabudu. Walipata fursa ya kukutana pamoja kwa swala za jamaa na mashauri mengine yaliyohitajia mkusanyiko wa Waislamu. Hivyo katika hali hii tatizo lililowakabili kwa siku za mwanzo za maisha ya Madinah ni namna ya kuitana kwa mkusanyiko wa swala na mikusanyiko mbali mbali ya Kiislamu. Waliwakuta Mayahudi wakiitana kwa mikusanyiko yao kwa tarumbeta (sauti ya upembe) na Wakristo wakiitana kwa kengele. Namna zote hizi mbili hazikumpendeza Mtume (s.a.w) na Waislamu kwa ujumla. Mtume (s.a.w) aliona kuwa si vyema kuitana kwa mikusanyiko mitakatifu kwa njia hizo za kitwaghuti, bali alipendelea kuwa sauti ya binaadamu ingelitumiwa kufanya kazi hiyo ambayo itaamsha hamasa za waumini na kuleta mwamko mpya wa imani zao na matendo yao. Hali ya mahangaiko ya kutafuta namna ya kuitana inaelezwa vyema katika Hadithi ifuatayo:

*Ibn Umar amesimulia kuwa: "Waislamu walipokuja Madina, walikusanyika pamoja kwa swala, na walipendelea kufanya hivyo kwa wakati mmoja, lakini hapakuwa na yeyote wa kuwaita. Siku moja ilibidi wajadili jambo hili na baadhi yao wakasema: "Tutumie kitu kama kengele wanayotumia Wakristo na wengine wakasema: Tutumie tarumbeta kama mayahudi. Umar akasema: Kwa nini asichaguliwe mtu akawa anawaita watu kwa ajili ya swala? Mtume (s.a.w) akasema: Oh! Bilali, nenda ukawaite watu kwa Swala". (Muslim)*

Hadithi hii pamoja na maelezo juu ya historia ya Adhana kwa ujumla hufafanuliwa na hadithi nyingi. Katika Hadithi nyingine tunafahamishwa kuwa maoni waliyoyatoa maswahaba kwenye mkutano wao yalifikishwa kwa Mtume (s.a.w) lakini hayakumvutia. Aliona kwamba si sahihi kutumia njia ya kitwaghuti katika miito mitakatifu, bali alikubaliana na Umar (r.a) kuwa sauti ya binaadamu katika wito huu ni bora kuliko chochote kingine. Pia imesimuliwa katika hadithi iliyopokelewa na Imamu Abu Daud kuwa wakati tatizo hili lilipokuwa bado halijapatiwa ufumbuzi, siku moja, swahaba mmoja, Abdullah bin Zayd alikuja kwa Mtume (s.a.w) na kumsimulia:

*"Usiku uliopita amenijia ndotoni mtu akishikilia mkononi mwake kengele na nikamuomba aniuzie; Aliponiuliza, kuwa nataka kufanyia nini chombo kile, nilijibu kuwa, ni cha kuwaitia watu kwenye swala, baada ya kumjibu hivyo alisema: "Siwezi kukufahamisha njia iliyo bora kuliko hiyo? Nilijibu kuwa nilikuwa tayari kumsikiliza aniambie. Hivyo alinifahamisha*

*maneno ya Adhana (kama yalivyo). Mtume (s.a.w) akasema: Ndoto yako, kwa uwezo na huruma ya Allah ni kweli. Nenda kwa Bilali umfahamishe maneno haya ili awaite watu kwa ajili ya swala kwa maneno hayo (adhana) Umar aliposikia suati hiyo nyumbani kwake alikuja mbio kwa Mtume (as.a.w) huku akiburuza nguo yake ya kiunoni chini na akisema: "Naapa kwa yule aliyekutuma kwa ukweli, nimepata ufunuo (ndoto) huo, kama ilivyofunuliwa kwa Abdullah bin Zayd. Mtume (s.a.w) akasema: Allah ashukuriwe kwa hilo". (Abu Daud).*

Maneno ya Adhana yalivyofunuliwa kwa njia ya ndoto kupitia kwa swahaba Abdullah bin Zayd na Swahaba Umar bin Khattab na kuthibitiahwa na Mtume (s.a.w) ni haya yafuatayo

اللهُ أَكْبَرُ اللهُ أَكْبَرُ اللهُ أَكْبَرُ اللهُ أَكْبَرُ

أَشْهَدُ أَنْ لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللهُ أَشْهَدُ أَنْ لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللهُ

أَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا رَسُوْلُ اللهِ أَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا رَسُوْلُ اللهِ

***Allahu Akbaru-Allaahu Akbaru-Allahu Akbaru-Allah Akbaru.***
*(Allah ni mkubwa kabisa- mara 4)*

***Ash-hadu an-laailaha illa-llaah (mara 2)***
*Ninashuhudia kuwa hapana mola ila Allah.*

***Ash-hadu anna Muhammadar Rasulullah (mara 2)***
*Ninashuhudia kuwa Muhammad ni Mtume wa Allah*

***Hayya-'alal Swalaat. (mara 2)***
*Njooni kwenye Swala.*

حَيَّ عَلَى الصَّلاَةِ حَيَّ عَلَى الصَّلاَةِ

***Hayya-'alal-falaah. (mara 2)***
*Njooni kwenye kheri.*

حَيَّ عَلَى الْفَلاَحِ حَيَّ عَلَى الْفَلاَحِ

***Allahu-Akbaru. (mara 2)***
*Allah ni mkubwa kabisa.*

اللهُ أَكْبَرُ اللهُ أَكْبَرُ

***Laailaha illallahu. (mara 1)***
*Hapana mola ila Allah.*

لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللهُ

Wakati wa Adhana ya swala ya Asubuhi - Muadhini baada ya kusema Hayya'allal falaah aongeze:

الصَّلاَةُ خَيْرٌ مِنَ النَّوْمِ   الصَّلاَةُ خَيْرٌ مِنَ النَّوْمِ

***Asswalaatu khairum minan-naumi. (mara 2)***

*"Swala ni bora kuliko usingizi".*

Kisha aendelee *Allahu Akbaru* hadi mwisho.

**Kuitikia Adhana**

Ni sunnah kuitikia adhana kama alivyotufundisha Mtume (s.a.w) katika Hadithi ifuatayo:-

Umar (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: *"Muadhini anaposema "**Allaahu Akbaru x 2**". Mtu aitikie: **Allahu Akbar x 2**. Kisha anaposema: "**Ashhadu anllailaha illallah**", aitikie: "**Ash-hadu anllailaha illallah**". Kisha anaposema: "**Ash-hadu anna Muhammadar-Rasuullullaah**" aitikie: "**Ashahadu annna Muhammadar-Rasuullullaah**" Anaposema "**Hayya 'alas-swalaat- Hayya 'alasswalaat**", aseme: "**Lahaula walaa Quwwata illa billah**" (Hapana hila wala nguvu zinazomkiuka Allah). Kisha akisema: **Hayya 'alal-fallah. Hayya 'alalfallah**" asema: "**Lahaula walaa Quwwata illa billah"**. Kisha akisema: "**Allahu Akbaru, allaahu Akbaar**, aitikie: "**Allaahu akbar Allahu Akbaar**". Kisha anaposema: "**Laaillaha illaallah**", aitikie: "**Laailla illaallah**", akifanya hivyo kwa unyenyekevu na mazingatio ataingia Peponi. (Muslim).*

**Dua baada ya Adhana**

Baada ya adhana kwisha Muislamu anatakiwa amswalie Mtume (s.a.w) kisha aombe dua. Kutokana na hadithi iliyosimuliwa na "Abdullah ibn, Umar (Mtume (s.a.w)) alisema kuwa:-

*Ukisikia adhana rudia kama asemavyo muadhini, kisha niswalie mimi mara moja Allah humuongezea rehema (humswalia yeye) mara kumi. Kisha niombee sehemu ya wasillah. Hii ni sehemu huko Peponi iliyohifadhiwa kwa ajili ya mmoja katika waja wa Allah: nategemea huenda nikawa mimi, na yeyote atakayeniombea Allah anipe afya hiyo ya wasilah basi uombezi wangu utaruhusiwa kwake (siku ya Kiyama). (Muslim).*

اللّهُمَّ رَبَّ هَذِهِ الدَّعْوَةِ التَّامَّةِ، وَالصَّلاَةِ القَائِمَةِ، آتِ مُحَمَّداً الوَسِيلَةَ وَالفَضِيْلَةَ،

وَابْعَثْهُ مَقَاماً مَحْمُوداً الَّذِي وَعَدتَهُ إنَّكَ لاَ تُخْلِفُ المِيْعَادَ

***Allaahuma rabba haadhihid-daawatit-taamma. Wasswalaatil-qaaimah. Ati Muhammadal-wasiilata walfadhiilat Wab-'ath-hu maqaaman mahmuudanil-ladhii wa'ad-tahu.Innaka laa tukhliful miiaad.***

**Tafsiri:**

*"Ewe Allah, Mola wa mlingano huu uliokamilika na swala iliyosimama,Mpe Muhammad (s.a.w) daraja kubwa na enzi na mpe hicho cheo ulichomuahidi, Hakika yako wewe si mwenye kuvunja miadi". (Bukhari).*

Ni vyema kipindi kati ya adhana na Iqama kiwe kirefu kidogo, kiasi cha kumuwezesha mtu kujitayarisha na kuwahi swala ya jamaa. Hivyo, hapana budi pawe na kipindi cha kuwangojea watu. Kipindi hiki ni kiasi cha kuswali rakaa mbili.

*Amesimulia Abdullah bin Mughaffal al-Muzani (r.a): "Kuna swala (sunnah) kati ya Adhana mbili (adhana na iqama) na kaongeza: kwa mtu anayetaka kuswali".*

Pia katika hadithi tunafahamishwa kuwa kipindi kati ya adhana na Iqama ni wakati mzuri wakuomba dua. Anas bin Malik (r.a) amesimulia kuwa Mtume (s.a.w) amesema:-

*Hairudishwi (haikataliwi) dua, baina ya Adhana na Iqama.*
*(Abu Daud, An-Nisani, tirmidh).*

**Iqama**

Ni wito au amri yakusimama tayari kuanza swala. Utakuta maneno ya Iqamat ni yale yale ya Adhana lakini hutamkwa nusu yake tu isipokuwa neno la mwisho (Laailaaha illa-llahu) ambalo huwa hutamkwa mara moja kuongezea maneno:

***Qad qaamat sw-swalat - qad-qaamat sw-swalat***

*(Swala ipo tayari).*

Haya husemwa baada ya maneno (Njooni katika kheri). Ndivyo tunavyofahamishwa katika Hadithi ifuatayo:

*Ibn Umar (r.a) amesimulia kuwa palikuwa na adhana wakati wa Mtume (s.a.w) kila tamko mara mbili na Iqamat mara moja isipokuwa aliongezea kusema: Swala iko tayari. Swala iko tayari. (Abuu Daud, Nisai).*

**Swala ya Sunnah baada ya Iqamat**

Ikisha kimiwa kwa ajili ya swala ya jamaa, hairuhusiwi kuendelea na swala ya sunnah kama tunavyojifunza kutokana na hadith ifuatayo:

*"Abu Hurairah ameeleza kuwa Mtume (s.a.w) amesema: Swala ya faradh ikianza,hapana swala nyingine (kuswaliwa" Na katika riwaya nyingine Mtume (s.a.w) amesema: Swala ni ile ambayo imetolewa Iqama". (Ahmad, Abu Daud, At-tirmidh, an-Nisai na Ibn Majah).*

## 4. Kuelekea Qibla

Kuelekea Qibla ni sharti la nne la kusimamisha swala. Katika hali ya kawaida Muumini ni lazima aelekee "Qibla wakati akiswali.Qibla ni neno la Kiarabu linatokana na neno "Qabala" lenye maana ya kuelekea sehemu au upande ambao watu huelekeza nyuso zao. Kwa mtazamo wa Qur-an, Qibla ni sehemu wanapoelekea waislamu wakati wa kuswali. Katika Qur-an tunafahamishwa kuwa Qibla ni sehemu ya katikati inayowaunganisha waumini kuwa mwili mmoja (kitu kimoja).

وَمِنْ حَيْثُ خَرَجْتَ فَوَلِّ وَجْهَكَ شَطْرَ ٱلْمَسْجِدِ ٱلْحَرَامِ ۖ وَإِنَّهُۥ لَلْحَقُّ مِن رَّبِّكَ ۗ وَمَا ٱللَّهُ بِغَـٰفِلٍ عَمَّا تَعْمَلُونَ ﴿١٤٩﴾

*"Na po pote wendako geuza uso wako kwenye Msikiti Mtakatifu . Na hiyo ndiyo haki itokayo kwa Mola wako. Na Mwenyezi Mungu si Mwenye kughafilika na yale mnayoyatenda. (2:149)*

Ummati wa Muhammad (s.a.w) Qibla chake ni Ka'aba, nyumba tukufu ya Allah iliyoko mjini Makkah, Saudi Arabia. Waislamu wote ulimwenguni huielekea Ka'aba wakati wa kuswali. Swala yoyote itakayoswaliwa bila ya kuelekea upande ilipo Ka'aba, pasipo na dharura inayokubalika kisheria kama vile kuwa mgonjwa, au kuwa safarini, haiswihi.

**Namna ya Kutafuta Qibla**

Kukisia ulipo mji wa Makka, Saudi Arabia, ambao ndani yake iko Ka'aba ni jambo rahisi kwa kutumia utaalamu wa Jiografia. Chombo

kizuri cha kumuwezesha mtu kukisia ilipo Ka'aba ni ramani ya dunia. Utakapojua ulipo katika sehemu yoyote ya dunia utaweza kujua Ka'aba iko upande gani wa dira kutokea pale ulipo kwa kutumia jua au chombo cha dira (Magnetic Compass). Kwa mfano ukiwa Tanzania, utaelekea Kaskazini kamili, ukiwa Pwani kama vile Dar es Salaam na ukiwa bara kama vile Kigoma, utaelekea Kaskazini ya Kaskazini Mashariki.

Kabla ya Muislamu hajaanza kuswali, hasa anapokuwa mgeni wa mahali hana budi kufanya jitihada ya kutafuta Qibla kwanza. Ni vyema mtu asafiripo awe na dira (Magnetic Compass) na ramani ili vifaa hivi vimsaidie kutafuta Qibla, vinginevyo itabidi awaulize wenyeji wa sehemu hiyo.

Mtu akishindwa kabisa kukibaini Qibla baada ya kujitahidi mwisho wa jitihada zake, popote atakapoelekea patafaa, kwani hii sasa imekuwa ni dharura, huku tukizingatia kuwa "Mashariki na Magharibi ni ya Mwenyezi Mungu".

وَلِلَّهِ ٱلْمَشْرِقُ وَٱلْمَغْرِبُ ۚ فَأَيْنَمَا تُوَلُّوا۟ فَثَمَّ وَجْهُ ٱللَّهِ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ وَٰسِعٌ عَلِيمٌ ﴿١١٥﴾

*Na Mashariki na Magharibi ni ya Mwenyezi Mungu. Basi mahala popote mgeukiapo (alikokuamrisheni Mwenyezi Mungu mtazikuta) huko radhi za Mwenyezi Mungu. Bila shaka Mwenyezi Mungu ni Mwenye wasaa (mkubwa kabisa) na Mwenye kujua (kukubwa kabisa vile vile). (2:115)*

### Nguzo za Swala

Utekelezaji wa nguzo za swala ni hatua ya pili katika harakati za kusimamisha Swala. Baada ya kutekeleza kwa ukamilifu sharti za swala, Muislamu huwa tayari kumkabili Mola wake na kuzungumza naye katika swala.Vipi tuzungumze na Mola wetu katika swala, tumeonyeshwa kinadharia na matendo na Mtume Muhammad (s.a.w) ambaye ametuusia: "*Swalini kama mlivyoniona mimi nikiswali*". Tunafahamu Mtume (s.a.w) aliswali vipi kwa kurejea Hadith zifuatazo:

*Aysha (r.a) amesimulia kuwa Mtume (s.a.w) alikuwa akianza swala kwa takbira na kusoma Qur-an - Alhamdullilaahi Rabil-alamiina (Suratul Fatiha). Alipoinama (kurukuu) hakuwa anaweka kichwa chake juu wala hakuwa anakiinamisha sana bali alikuwa akikiweka katikati ya hali hizo mbili, na alipoinuka kutoka kwenye rukuu hakuwa anakwenda*

*kwenye sijda mpaka asimame kwanza wima na alipoinua kichwa chake kutoka kwenye sijda, hakusujudu mpaka baada ya kukaa wima; na alikuwa akisoma tahiyyatu kila baada ya rakaa mbili, na (katika hiyo tahiyyatu) alikuwa anakaa kwa kuulaza mguu wa kushoto na kuusimamisha wima mguu wa kulia. Alikataza kukaa mkao wa shetani (kunyoosha miguu) na kunyoosha mikono kama mnyama, na alikuwa akifunga (akimaliza) Swala kwa Salaam". (Muslim)*

*Abu Humid Sayid(r.a) aliwaambia Maswahaba wa Mtume (s.a.w) alitaka kuwakumbusha jinsi Mtume wa Mwenyezi alivyokuwa akiswali. Alisema (Abu Humaid) kwamba wakati alipokuwa akisoma takbira Mtume alikuwa akiweka mikono yake mkabala na mabega yake na alipokuwa akirukuu, aliweka viganja vya mikono yake juu ya magoti na kuupinda mgongo wake; wakati alipoinua kichwa (alipoinuka) alijinyoosha (alinyoosha shingo yake) wima mpaka kila kiungo kinarudia nafasi yake; wakati alipokwenda Sijda (aliposujudu) mikono yake ilikuwa kati na kati (haikuwa mbali sana wala haikuwa pamoja), na vidole vyake (ncha za vidole vyake) vya miguu vilielekea (alivielekeza) Ka'aba, alipokaa baada ya rakaa mbili alikuwa akiukalia mguu wake wa kushoto na kusimamisha mguu wa kulia. Wakati alipokaa katika rakaa ya mwisho aliutanguliza (hakuukalia) mguu wa kushoto na kuusimamisha wa kulia, alikaa kwa makalio. (Bukhari).*

*Abu Hamaid Sayid aliwaambia Maswahaba kumi wa Mtume(s.a.w), kwamba yeye anajua vizuri zaidi jinsi Mtume (s.a.w) alivyokuwa akiswali. Alisema (Abu Hamid) kwamba: Wakati Mtume (s.a.w) aliposimama kuswali, aliinua mikono yake juu mpaka ilipokuwa mkabala na mabega yake. Halafu alisoma takbira na baadaye alisoma Qur-an. Halafu alisoma takbira na kuinua tena mikono yake hadi kufikia mkabala na mabega yake.Halafu aliinama (alirukuu) akiweka viganja vya mikono yake juu ya magoti na kujiweka mwenyewe sawa sawa (bila ya kuinamisha kichwa wala kukiinua juu). Baadaye aliinua kichwa chake (aliinuka kutoka rukuu) na kusema: "Mwenyezi Mungu anamsikia (humsikia) yule anayemsifu". Halafu aliinua tena mikono yake hadi kufikia mkabala na mabega yake akiwa wima sawa sawa na kusema:"Mwenyezi Mungu ni mkubwa". Baadaye alikwenda (chini alikwenda sijda) akiweka mikono yake mbali na usawa wake na mwili na kupinda vidole vyake vya miguu. Aliinua kichwa chake na aliukunja mguu wake wa kushoto na kuukalia. Alikaa sawasawa (wima) mpaka kila kiungo cha mwili kimerudia mahali pake, na alikwenda tena sijda na kusema:"Mwenyezi Mungu ni mkubwa". Aliinuka (alijiinua) kutoka Sijda na kukalia mguu wake wa kushoto. Alikaa sawa sawa mpaka kila kiungo cha mwili kikarudia nafasi yake (mahali pake). Baadaye alisimama juu (wima) na kufanya yote kama alivyofanya*

*katika rakaa ya kwanza. Mwisho wa rakaa hizi mbili alisimama na kusoma takbira.ya kwanza na aliinua mikono yake hadi ikawa mkabala na mabega yake kama alivyosoma takbira ya kufungulia swala na baadaye alifanya hivyo hivyo katika sehemu ya swala iliyobakia mpaka kufikia Sijda ambamo mlikuwa na (Taslimu). Aliondoa mguu wake wa kushoto (hakuukalia). Alikaa kwa makalio zaidi upande wa kushoto (alikalia mfupa wa kalio la upande wa kushoto) baadaye alitoa Salaam (Taslim). Maswahaba wote `walikubali kuwa Abu Hamid amesema ukweli. (Abu Daud).*

Hadithi hizi zinatufahamisha kuwa swala ya Mtume(s.a.w) ambaye ametuamrisha tumuigize ina vipengele vilivyogawanyika katika mafungu makubwa mawili. Nguzo za Swala na Sunnah za Swala.

## Nguzo za Swala

Nguzo za swala ni vile vipengele vya swala ambavyo lazima mtu avitekeleze ndio swala yake iweze kukamilika. Nguzo moja tu ikikosekana swala haisihi (haikamiliki). Hivyo ili mwenye kuswali awe na matarajio ya kupata matunda ya Swala hana budi kutekeleza nguzo zake zote kwa ukamilifu. Zifuatazo ni nguzo za Swala:

1. Nia - dhamira moyoni.
2. Takbira ya kuhirimia (au Takbira ya kufungulia Swala).
3. Kusoma suratul-Fatiha.
4. Kurukuu.
5. Kujituliza katika rukuu.
6. Kuitidali (kusimama kutoka katika rukuu).
7. Kujituliza katika itidali.
8. Kusujudu.
9. Kujituliza katika sijda.
10. Kukaa kati ya sijda mbili.
11. Kujituliza katika kikao cha kati ya sijda mbili.
12. Kusujudu mara ya pili.
13. Kujituliza katika sijda ya pili.
14. Kukaa Tahiyyatu.
15. Kusoma Tahiyyatu.
16. Kumswalia na kumtakia rehema Mtume (s.a.w) na Waislamu.
17. Kutoa Salaam.
18. Kuswali kwa kufuata utaratibu huu (1 - 17).

Nguzo hizi za swala tunaweza kuzigawanya kwenye makundi manne:

(a) Nia.

(b) Nguzo za matamshi (visomo)
(c) Nguzo za vitendo.
(d) Kufuata utaratibu.

Katika nguzo 18, nguzo za matamshi ni hizi tano zifuatazo:
(i) Takbira ya kuhirimia swala.
(ii) Kusoma suratul-Fatiha (Al-hamdu).
(iii) Kusoma Tahiyyatu.
(iv) Kumswalia Mtume.
(v) Kutoa Salaam.

Nguzo zote zilizobakia, ukiacha nia na kufuata utaratibu ni nguzo za vitendo.

## Sunnah za Swala

Vipengele vya sunnah katika swala ni vile ambavyo mwenye kuswali akivitenda husaidia sana kukuza daraja ya swala yake na kuipa nguvu na msukumo mkubwa wa kuiwezesha kufikia lengo lililokusudiwa kwa urahisi zaidi. Ama mwenye kuswali akiacha kipengele chochote katika vipengele vya sunnah, swala yake itakamilika iwapo atatekeleza vipengele vyote vya nguzo. Katika Hadith tumeona kuwa Mtume (s.a.w) katika swala yake pana vipengele vya ziada ya nguzo kama ifuatavyo:

1. Kuinua viganja vya mikono mkabala na mabega, usawa wa vigingi vya masikio wakati wa kuhirimia swala, kwenda kwenye rukuu, baada ya rukuu na baada ya kutoka kwenye Tahiyyatu ya kwanza.
2. Kusoma dua baada ya takbira ya kuhirimia.
3. Kuanza na ***a'udhubillaah*** (kumlaani Shetani) kabla ya kuanza kusoma suratul-Fatiha.
4. Kuitikia "Aamin"baada ya kumaliza Suratul Fatiha.
5. Kusoma aya za Qur-an baada ya Suratul-Fatiha katika rakaa mbili za mwanzo.
6. Kuleta Tasbih, Tahmid na dua katika rukuu, itidali na sijda.
7. Kutoa takbira katika kubadilisha kitendo kimoja kuendea kingine isipokuwa tu kutoka kwenye rukuu kwenda kwenye itidali ndipo tunaposema: ***"Sami'Allahu liman hamidah - Rabbanaa lakal-hamdu".***
8. Kukaa na kusoma Tahiyyatu kila baada ya rakaa mbili, kwa swala zenye rakaa zaidi ya mbili.
9. Kusoma dua baada ya kumswalia Mtume na kabla ya kutoa Salaam.

## Namna ya kuswali kama alivyoswali Mtume (s.a.w)

Mtume (s.a.w) ametuagiza katika Hadith maarufu kuwa tuswali kama alivyokuwa akiswali. Hivyo katika sehemu hii tutajitahidi kuonesha utekelezaji wa swala hatua kwa hatua kwa kurejea Hadith Sahihi za Mtume (s.a.w):

## 1. Nia na Takbira ya kuhirimia

Nia ni kudhamiria moyoni kuwa unaswali, swala unayoikusudia kisha unaanza swala kwa kusema:



اللهُ أَكْبَرُ

***"Allaahu Akbar"***

*Allah ni Mkubwa kwa kila hali".*



Wakati wa kuhirimia swala ni sunnah kuinua viganja vya mikono,mkabala na mabega. Kuhusu unyanyuaji wa mikono mkabala na mabega imeripotiwa kuwa Mtume (s.a.w) alikuwa akifanya hivyo katika sehemu nne tofauti:

1. Wakati wa kuhirimia swala (kuanza swala).
2. Wakati anaposema Allaahu Akbar kwa ajili ya rukui.
3. Wakati anaposimama kutoka kwenye rukuu.
4. Wakati anaposimama kutoka kwenye tahiyyatu ya kwanza ili kuendelea na rakaa ya tatu.

Hii tunaipata katika Hadith aliyosimulia Abdullah bin 'Umar kuwa:

*"Mtume (s.a.w) aliposimama kwa ajili ya swala alinyanyua mikono yake mkabala na mabega yake na kisha kuhirimia (kusema Allahu Akbar). Alipotaka kurukuu alinyanyua mikono kama alivyofanya kwanza na aliposimama kwa ajili ya itidali alifanya hivyo hivyo na alisema Allah anamsikia yule anayemsifu. (Bukhari, Muslim na Bayhaqi).*

*Nafa'a(r.a) ameeleza kwamba Ibn 'Umar (Abdullah)(r.a) aliposimama kwa ajili ya rakaa ya tatu alikuwa akinyanyua mikono; jambo ambalo alilihusisha na Mtume (s.a.w). (Bukhari, Abu Dawud, Nasai).*

Baada ya kuhirimia swala mwenye kuswali hushusha mikono yake na kuiweka kifuani, mkono wa kulia ukiwa juu ya mkono wa kushoto kwa mujibu wa Hadith zifuatazo:

*Hulab At-Tai(r.a) amesimulia: "Nilimuona Mtume (s.a.w) akiswali hali ameweka mkono wake wa kulia juu ya mkono wa kushoto juu ya kifua chake." (Ahmad na At-Tirmidh)*

*Naye Wail bin Hijr (r.a) ameripoti: "Niliswali pamoja na Mtume (s.a.w) na aliweka mkono wake wa kulia juu ya mkono wa kushoto juu ya kifua chake". (Ahmad na At-Tirmidh).*

*Imamu Abu Dawud na Nasai wamepokea kutoka kwa Ibn Khuzaimah kuwa Mtume (s.a.w) alipokuwa akiswali alikuwa akiweka mkono wake wa kulia juu ya kiwiko (wrist) cha mkono wa kushoto na sehemu ya mkono inayofuatia kiganja .*

## 2. Kusoma Dua ya Kufungulia Swala

Kusoma dua ya kufungulia swala ni sunnah. Katika Hadithi ya Bukhari na Muslim iliyosimuliwa na Abu Hurairah (r.a), baada ya kuhirimia swala Mtume (s.a.w) alikuwa akileta dua ifuatayo:

وَجَّهْتُ وَجْهِيَ لِلَّذِي فَطَرَ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضَ حَنِيفًا ۖ وَمَآ أَنَا۠ مِنَ
ٱلْمُشْرِكِينَ إِنَّ صَلَاتِي وَنُسُكِي وَمَحْيَايَ وَمَمَاتِي لِلَّهِ رَبِّ ٱلْعَٰلَمِينَ
لَا شَرِيكَ لَهُۥ ۖ وَبِذَٰلِكَ أُمِرْتُ وَأَنَا۠ أَوَّلُ ٱلْمُسْلِمِينَ

*"Nimeuelekeza uso wangu kwa yule aliyeziumba mbingu na ardhi. Nimeacha dini za upotovu. Mimi si miongoni mwa washirikina. Hakika swala yangu (na ibada zangu zote) na uzima wangu na kufa kwangu (yote) ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, bwana (Rabbi) wa walimwengu wote. Hana mshirika wake. Na haya ndio niliyoamrishwa na mimi ni wa kwanza walio jisalimisha kikamilifu kwa Mwenyezi Mungu.*
*(6:79, 162-163)*

## 3. Kupiga Audhu Billah

Kabla ya kuanza kusoma Qur-an ni amri ya Allah (s.w) kujikinga na sheitwani kama inavyodhihirika katika aya ifuatayo:

فَإِذَا قَرَأْتَ ٱلْقُرْءَانَ فَٱسْتَعِذْ بِٱللَّهِ مِنَ ٱلشَّيْطَٰنِ ٱلرَّجِيمِ ﴿٩٨﴾

*"Na ukitaka kusoma Qur-an piga Audhu billah (jikinge) kwa Allah (akulinde) na Sheitwani aliyefukuzwa (kwenye Rehema). (16:98)*

Hivyo tuanze kusoma Qur-an kwa kusema

أَعُوذُ بِٱللَّهِ مِنَ ٱلشَّيْطَٰنِ ٱلرَّجِيمِ

***"A'udhu-billahi minash-shaytwanir- Rajiim"***

*Najikinga kwa Allah na sheitwan aliyefukuzwa-kwenye Rehma yako*

## 4. Kusoma Suratul-Fatiha

Kusoma Suratul-Fatihah ni nguzo ya tatu ya swala na ndio nguzo kubwa ya swala. Tunasoma suratul-Fatiha kama ifuatavyo:-

بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ ﴿١﴾ ٱلْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ ٱلْعَٰلَمِينَ ﴿٢﴾

***Bismillahir Rahmaanir Rahiim (1)***
***Alhamdu liLLahi rabbil-'Aalamiin (2).***

ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ ﴿٣﴾ مَٰلِكِ يَوْمِ ٱلدِّينِ ﴿٤﴾

***Rrahmaanir Rahiim (3) Maaliki yaumiddiin (4)***

إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ ﴿٥﴾ ٱهْدِنَا ٱلصِّرَٰطَ ٱلْمُسْتَقِيمَ ﴿٦﴾

***Iyyaakana 'abudu waiyyaaka nasta'iin (5)***
***Ih dinasw-swiraatwal mustaqiim (6)***

صِرَٰطَ ٱلَّذِينَ أَنْعَمْتَ عَلَيْهِمْ غَيْرِ ٱلْمَغْضُوبِ عَلَيْهِمْ وَلَا ٱلضَّآلِّينَ ﴿٧﴾

***Swiraatwa lladhiina an 'amta 'alaihim; ghairil maghdhuubi 'alaihim wala dhw-dhwaaliin (7)***

**Tafsri:**

(1) *Kwa jina la Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na mwenye kurehemu:*
(2) *Shukrani zote anastahiki Mwenyezi Mungu, Mola wa Walimwengu wote:*
(3) *Mwingi wa Rehema mwenye kurehemu*
(4) *Mwenye kumiliki siku ya malipo:*
(5) *Wewe tu ndiye tunayekuabudu, na wewe tu ndiye tunaye kuomba msaada:*
(6) *Tuongoze njia iliyonyooka:*
(7) *Njia ya wale uliowaneemesha; siyo (ya wale ) waliokasirikiwa, wala ya wale waliopotea*

## 5. Kusoma Qur-an baada ya Suratul-Fatiha

Katika rakaa ya kwanza na ya pili ni Sunnah baada ya kusoma Suratul-Fatiha kuleta Surah au aya nyingine za Qur-an:

إِنَّآ أَعْطَيْنَٰكَ ٱلْكَوْثَرَ ﴿١﴾ فَصَلِّ لِرَبِّكَ وَٱنْحَرْ ﴿٢﴾ إِنَّ شَانِئَكَ هُوَ ٱلْأَبْتَرُ

## 6. Kurukuu

Baada ya kusoma Suratul-Fatiha na Surah nyingine, au baadhi ya aya katika sura nyingine unasema ***Allahu-akbar*** kisha unarukuu (kuinama).

Rukuu ni nguzo ya swala pamoja na kujituliza humo. Katika rukuu ni sunnah kumsabihi Allah (s.w) kwa kusema kimya kimya mara tatu




***"Subhana Rabbiyal'Adhiim"***

*"Utukufu ni wako Ee Bwana (Mlezi) wangu Uliye mkuu"*

Pia ni sunnah katika rukuu kuleta tasbihi ifuatayo:

سُبْحَانَ ذِي الْجَبَرُوتِ وَالْمَلَكُوتِ وَالْكِبْرِيَاءِ وَالْعَظَمَةِ

***"Subhana Dhiljabaruut, Walmalakuut Wal-kibriyaai Wal'adhamat"***
***"Utukufu ni wako Ee Bwana mlezi mwenye nguvu, Mtawala Mwenye Enzi, Muweza wa kila kitu, Uliye mkuu".***

## 7. Kuitidali

Kuitidali ni kitendo cha kusimama wima kutoka kwenye Rukuu. Itidali ni nguzo ya swala pamoja na kujituliza humo. Tunasimama wima kutoka kwenye rukuu kwa kusema:

***"Sami'allahu liman Hamidah"***
***"Allah anamsikia kila anayemhimidi (anayemsifu)".***

سَمِعَ اللهُ لِمَنْ حَمِدَهُ

Ni sunnah kunyanyua viganja vya mikono kama tulivyofanya wakati wa kuhirimia Swala. Kisha tunapokuwa wima tunasema:

***"Rabbana Walakal-hamdu"***
***Ee Mola wetu, sifa zote za ukamilifu ni zako".***

رَبَّنَا وَلَكَ الْحَمْدُ

Pia katika Hadith iliyosimuliwa na Ally (r.a) katika Sahihi Muslimu, Mtume (s.a.w) katika itidali alikuwa akileta dua/dhikri ifuatayo:

***"Allahumma Rabbanaalakal-hamdu mil-asse-maawati wamil-al-ardi wamaabainahumaa wa mil-amaashi-ita min-shay-in ba-'adu.***

***Ee Mola wetu, sifa zote za ukamilifu ni zako kutoka mbinguni na ardhini na katika vitu vyote vilivyobaina yao (mbingu na ardhi) na kutoka katika vinginevyo unavyoviridhia."***

## 8. Kusujudu

Kusujudu ni nguzo ya swala pamoja na kujituliza humo. Kusujudu ni kitendo cha kuvituliza chini viungo saba: bapa la uso, viganja vya mikono, magoti mawili na matumbo ya vidole vya miguu (vidole vilale kwa kuelekea Qibla). Tunapokuwa katika sijda tunamtasbihi Allah (s.w)

kwa kusema:



سُبْحَانَ رَبِّيَ الأَعْلَى

*"Subhaana Rabbiyal-A'ala"*



*"Utukufu ni wako. Mola uliotukuka".*

Pia kwenye sijda ambapo mja huwa karibu zaidi na Mola wake, ni vizuri kuomba msamaha kwa Allah (s.w) kama alivyotufunza Mtume (s.a.w) katika Hadithi iliyosimuliwa na Abuu Hurairat (r.a) katika sahihi Muslimu:

اللَّهُمَّ اغْفِرْلِي ذَنْبِي
كُلَّهُ دِقَّهُ وَجِلَّهُ
وَأَوَّلَهُ وَآخِرَهُ
وَعَلانِيَتَهُ وَسِرَّهُ

*"Allahummagh-firly Dhambi, Kullahu, Diqqahu, Wajillahu wa-awwalahu, Wa-aakhirahu, Wa'alaaniyatahu, Wasirrahu".*

*"Ee Allah,Nisamehe dhambi zangu zote, ndogo na kubwa, za mwanzo na za sasa, za Dhahiri na za Siri".*

**9. Kukaa Baina ya Sijda Mbili.**

Kukaa baina ya sijda mbili na kujituliza ni katika nguzo za swala. Tukiwa katika kikao hiki tunakalia unyayo wa kushoto na tunaweka mikono yetu mapajani. Katika kikao hiki ni sunnah kuleta dua ifuatayo:

رَبِّ اغْفِرْلِي وَارْحَمْنِي وَعَافِنِي وَارْزُقْنِي

***Rabbigh-firly warhamniy Wa-'aafiniy War-zuquniy.***

*"Ee Allah! Nisamehe, na unirehemu, na Unipe afya na Uniruzuku".*

Tukisha maliza dhikri hii tunasema ***"Allahu Akbar"*** na kusujudu mara ya pili kama tulivyofanya Sijda ya kwanza. Baada ya Sijda hii tunasema ***"Allahu Akbar"*** kuendelea na rakaa ya pili au kukaa tahiyyatu

baada ya kumaliza rakaa ya pili au ya mwisho ya Swala.

**Sijdatut-Tilawat (Sijda ya kisomo)**

Sijdatut tilawat ni sijdah ya sunnah ailetayo mwenye kusoma Qur-an au mwenye kusikiliza Qur-an ikisomwa pale inapotajwa sijdah. Katika Qur-an kuna aya kumi na tano zenye kutaja sijdah ambapo msomaji na msikilizaji wanatakiwa wasujudu ili kudhihirisha unyenyekevu wao kwa Allah (s.w); aya hizi ni: (7:206); (13:15); (16:50); (17:109); (19:58): (2218): (22:77); (25:60); (27:26); (32:15); (38:24); (41:38); (53:62); (54:21); (96:19).

Ukiwa katika swala. utakaposoma moja wapo ya aya hizi ni Sunnah baada ya kumaliza aya hiyo, useme *"Allahu Akbar"* na kwenda moja kwa moja kwenye sijda kisha kujituliza humo na kusoma (*Subhaana Rabbiyal A'laa* - mara tatu kama kawaida). Kisha kusema tena *"Allahu Akbaru"* na kurejea tena kwenye kisimamo na kuendelea na utaratibu wa swala kama kawaida. Sijda hii ni moja tu. Katika sijidatut-tilawat ni sunnah kuleta dhikri ifuatayo:

سَجَدَ وَجْهِيَ لِلَّذِي خَلَقَهُ وَشَقَّ سَمْعَهُ وَبَصَرَهُ بِحَوْلِهِ وَقُوَّتِهِ وَتَبَارَكَ اللهُ أَحْسَنُ الْخَالِقِينَ



***Sajada waj-hiya lilladhiy khalaqahu, washaqqa sam-'ahu wabaswarahu bihaulihi, waquwwatihi, watabaarakallaahu ahsanul-khaaliqiina.***

*"Nauelekeza uso wangu kwa sijda kwa yule aliyeuumba na akanipa vipaji vya kusikia na kuona kwa uwezo na nguvu Zake, Ametukuka Allah, aliye Mbora wa kuumba. (Tirmidh)*

**10. Kukaa Tahiyyatu**

Baada ya sijdah ya pili ya rakaa ya pili au rakaa ya mwisho ya swala tunakaa kitako ambapo tunasoma. "Tahiyyatu" (maamkizi kwa Allah). Kukaa na kusoma Tahiyyatu baada ya rakaa ya mwisho ya swala ni miongoni mwa nguzo za swala, ama kukaa na kusoma tahiyyatu baada ya rakaa mbili za mwanzo kwa swala yenye rakaa tatu au nne ni sunnah iliyokokotezwa. Namna ya kukaa tahiyyatu inaelezwa katika hadithi kuwa katika tahiyyatu ya kwanza Mtume (s.a.w) alikuwa akikalia futi la

mguu wa kushoto na kusimamisha futi la mguu wa kulia na katika tahiyyatu ya mwisho alikaa chini na kuulaza mguu wa kushoto katika uvungu wa mguu wa kulia na alisimamisha futi la mguu wa kulia, katika vikao vyote hivyo viwili, Mtume (s.a.w) alivilaza viganja vyake juu ya mapaja karibu na magoti kama tunavyoelezwa katika hadith ifuatayo:



*Abdullah bin Jubair(r.a) ameeleza kuwa wakati Mtume (s.a.w) alipokaa tahiyyatu, alikuwa akiweka kiganja chake cha mkono wa kulia juu ya paja lake la kulia na kiganja cha mkono wa kushoto juu ya paja la mguu wa kushoto na alikuwa akinyoosha kidole chake cha shahada (wakati wa kusema, "**Ash-hadu anllaaillaha illallah**) na kukiegemeza juu ya kidole gumba na alikuwa akiweka kiganja chake cha mkono wa kushoto juu ya goti lake (la mguu wa kushoto). (Muslim).*



## 11. Kusoma Tahiyyatu

Kusoma tahiyyatu ni nguzo ya swala. "Tahiyyatu" ina maana ya "Maamkizi", ukiwa umekaa kikao cha tahiyyatu unaleta maamkizi kama ifuatavyo:

«التَّحِيَّاتُ لِلَّهِ وَالصَّلَوَاتُ وَالطَّيِّبَاتُ ، السَّلامُ عَلَيْكَ أَيُّهَا النَّبِيُّ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ ، السَّلامُ عَلَيْنَا وَعَلَى عِبَادِ اللَّهِ الصَّالِحِينَ ، أَشْهَدُ أَنْ لا إِلَهَ إِلا اللَّهُ وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ»

***"Attahiyyaatu lillaah, wasw-swalawaatu, watwa-yyibaatu, assalaamu 'alaika ayyuhannabiyyu, warahmatullaahi wabarakaatuhu, assalaamu 'alay-naa wa-'alaa 'ibaadillaahi sw-swaalihiina. Ash-hadu an-llaailaaha illallaahu wa-ash-hadu anna Muhammadan 'abduhuu warasuuluhu".***

*“Maamkizi yote ni ya Allah, na swala zote na yote mazuri, Amani iwe juu yako, ewe Mtume na Rehma na Baraka za Allah. Na amani iwe juu yetu na juu ya waja wema wa Allah. Ninashuhudia kuwa hapana Mola ila Allah. Na ninashuhudia kuwa Muhammad ni Mja na, ni Mtume wake”. (Muslim).*



## 12. Kumswalia Mtume (s.a.w)

Kumswalia Mtume (s.a.w) ni nguzo ya swala inayofuatia baada ya kusoma Tahiyyatu. Kumswalia Mtume si faradhi katika swala tu bali pia ni faradhi kumswalia kila anapotajwa kwa jina lake. Msisitizo wa amri ya kumswalia Mtume unaonekana katika aya ifuatayo:

إِنَّ ٱللَّهَ وَمَلَـٰٓئِكَتَهُۥ يُصَلُّونَ عَلَى ٱلنَّبِيِّ ۚ يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ صَلُّوا۟ عَلَيْهِ وَسَلِّمُوا۟ تَسْلِيمًا ﴿٥٦﴾

*“Hakika Mwenyezi Mungu anamteremshia Rehema Mtume; na Malaika wake (wanamuombea dua). Basi; enyi Mlioamini msalieni (Mtume, muombeeni Rehema) na amani”. (33:56)*

Pia hadithi zifuatazo zinasisitiza umuhimu wa kumswalia Mtume (s.a.w) kila atajwapo na kila mtu apatapo wasaa.

*Ali (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: Bakhili ni yule anayesikia nikitajwa, lakini haniswalii. (hanitakii rehma). (Tirmidh).*

*Abu Hurairah amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: “Anayenitakia Rehma (anayeniswalia) mara moja, Allah humrehemu mara kumi”. (Muslim).*

*“Ibn Mas’ud amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: Atakayekuwa kipenzi changu katika watu, katika siku ya Kiama atakuwa ni yule aliye mbele kuliko wote katika kunitakia Rehma (kuniswalia). (Tirmidh).*

Namna ya kumswalia Mtume (s.a.w) imeelezwa katika Hadithi nyingi lakini iliyomashuhuri katika hizo ni ile iliyosimuliwa na Abdur-Rahman bin Ubaidillah(r.a) na kupokelewa na Maimamu wote wa Hadithi kuwa Mtume (s,.a.w) ametufundisha tumswalie (tumtakie Rehma) kama ifuatavyo;

اللّٰهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ مُحَمَّدٍ كَمَا صَلَّيْتَ عَلَى إِبْرَاهِيْمَ وَعَلَى آلِ ابْرَاهِيْمَ انَّكَ حَمِيْدٌ مَجِيْدٌ وَبَارِكْ عَلَى مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ مُحَمَّدٍ كَمَا بَارَكْتَ عَلَى ابْرَاهِيْمَ وَعَلَى آلِ ابْرَاهِيْمَ إِنَّكَ حَمِيْدٌ مَجِيْدٌ

***Allahumma Swallii 'alaa Muhammad, wa-'alaa aali Muhammad, kamaa swallaita 'alaa Ibraahiima wa-'alaa aali Ibraahiima innaka hamiidun-majiid, wabaariki 'alaa Muhammad, wa-'alaa aali Muhammad kamaabaarakta 'alaa Ibraahiima wa-'alaa aali Ibraahiima innaka hamiidun-majiid.***

*Ee Allah! Mrehemu Muhammad na wafuasi wa Muhammad kama ulivyomrehemu Ibrahim na wafuasi wa Ibrahim. Hakika wewe Umtukufu na Msifiwa wa haki. Ee Allah! mbariki Muhammad na wafuasi wa Muhammad kama ulivyombariki Ibrahim na wafuasi wa Ibrahim.Hakika wewe Umtukufu na Msifiwa wa haki".*

**13. Dua kabla ya Kutoa Salaam**

Ni sunnah baada ya kumswalia Mtume (s.a.w) na kabla ya kutoa Salaam kuleta dua mojawapo kati ya dua nyingi alizotufunza Mtume (s.a.w). Miongoni mwa dua alizotufundisha Mtume, kama ilivyo hadithiwa na Abu bakar Swiddiq (r.a) ni

اللّٰهُمَّ إِنِّيْ ظَلَمْتُ نَفْسِيْ ظُلْمًا كَثِيْرًا وَلاَ يَغْفِرُ ذُنُوبَ إِلاَّ أَنْتَ فَاغْفِرْلِيْ مَغْفِرَةً مِنْ عِنْدِكَ وَارْحَمْنِيْ إِنَّكَ أَنْتَ الْغَفُوْرُ الرَّحِيْمُ

***"Allahumma inniy dhwalamtu nafsiy dhulman kathiira-walaa yaghfirudh-dhunuuba illaa anta, faghfirliy maghfiratan min' indika warhamniy innaka antalghafuurur-Rahiim.***

*"Ee Mola wangu, hakika mimi nimedhulumu nafsi yangu dhuluma kubwa wala hakuna anaye samehe madhambi isipokuwa wewe, basi nisamehe na unirehemu hakika wewe umrehemevu na msamehevu".*

Dua nyingine aliyotufundisha Mtume (s.a.w) kwa msisitizo mkubwa kama tunavyofahamishwa katika Hadithi ya Muslim, iliyosimuliwa na Ibn Abbas, ni hii ifuatayo:

لَلّهُمَّ إِنِّيْ أَعُوْذُ بِكَ مِنْ عَذَابِ الْقَبْرِ وَ أَعُوْذُ بِكَ مِنْ فِتْنَةِ الْمَسِيْحِ الدَّجَّالِ وَ أَعُوْذُ بِكَ مِنْ فِتْنَةِ الْمَحْيَا وَالْمَمَاةِ

***Allahumma Inni-audhubika min-'adhaabi-lqabri,Wa-auudhubika min fitnatil masiihi-ddajjaal, Wa-auudhubika min fitnatil-mahyaa wal-mamaati,***

*"Ee Allah najikinga kwako kutokana na adhabu ya kabr, na najikinga kwako kutokana na fitina za masiihi Ddajjaal na najikinga kwako kutokana na matatizo ya maisha na mauti.*

## Sijidat-Sah-wi (Sijda ya kusahau)

Sijdat Sah-wi ni sijidah anayoileta mtu kabla ya kutoa salaam ili kufidia kitendo cha sunnah alicho kisahau kwa mfano kusahau kukaa tahiyaatu ya kwanza.Vile vile mtu akisahau au akikosea jambo lolote ambalo halibatilishi swala kwa mfano akaswali rakaa tano badala ya rakaa nne kwa swala ya Adhuhuri. Kabla hajamaliza swala alete sijidat Sahau. Hivi ndivyo tunavyojifunza kutokana na Hadithi zifuatazo:

*Abdullah bin Mas'ud (r.a) amesimulia: Mtume wa Allah alituswalisha Adhuhuri rakaa tano.Tukamuuliza kama pameamrishwa na Mwenyezi Mungu kurefushwa swala akajibu, La! Tukamuambia: "Umetuswalisha rakaa tano. Akasema (Mtume): Mimi ni binaadamu kama nyinyi, nakumbuka kama mnavyokumbuka na nasahau kama mnavyosahau. Kisha akasujudu sijdah mbili zikawa ni fidia kwa kusahau. (Bukhari na Muslim).*

**Muhimu:** Kumbuka kuwa sijda hii Mtume (s.a.w) aliileta baada ya kutoa salaamu na baada ya kukumbushwa.

*Abdullah bin Buhaymah (r.a) amesimulia kuwa Mtume (s.a.w) aliswalisha swala ya adhuhuri, akasimama baada ya rakaa mbili, alipomaliza swala akasujudu mara mbili huku akisema: "Allah Akbar" katika kusujudu na katika kuinuka, wakati amekaa kabla ya kutoa salaam, na watu wakasujudu pamoja naye. Hii ilikuwa ni kufidia ile tahiyyatu ya mwanzo aliyoisahau". (Muslim)*

*Abu Said al-Khudry (r.a) amesimulia kuwa Mtume (s.a.w) amesema yeyote miongoni mwenu akiwa hana hakika ya swala yake na hakumbuki ameswali rakaa ngapi, tatu au nne, inabidi ajiondoe katika wasi wasi na ajiweke katika upande wa hakika (ajaalie kuwa ameswali rakaa tatu), kisha asujudu mara mbili kabla ya kutoa Salaam.Kama atakuwa ameswali rakaa tano, basi sijda hizo zitamfanyia swala yake iwe shufwa (even) na kama atakuwa ameswali rakaa nne kama kawaida, basi sijda hizo zitakuwa ni dhila kwa shetani.*

Kutokana na hadithi hizi ukisahau jambo lolote katika swala ambalo si nguzo ya swala, kabla hujatoa salaam inabidi ulete sijdat-sahau kwa kusujudu mara mbili kisha ndipo utoe salaam. Kama utakumbuka baada ya kutoa salaamu, bado utaleta sijda mbili kama alivyofanya Mtume (s.a.w) katika Hadithi ya Abdallah bin Mas'ud.

## 14. Kutoa salaam

Kutoa salaam ni nguzo ya mwisho ya swala. Tunatoa salaam kwa kusema:

أَلسَّلَامُ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَتُ اللهِ وَبَرَكَاتُهُ

*Assalaam alaykum warahmatullah Wabarakaatuh*
*"Amani na Rehma za Allah na baraka zetu ziwe juu yenu"*

Huku tunageukia kulia mpaka mashavu yetu yaonekane kwa walionyuma yetu kama alivyokuwa akifanya Mtume (s.a.w):



*Abdullah bin Mas'ud (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah alikuwa akitoa salaam kulia kwa Assalaam alaikum Warahmatullah (Amani iwe juu yenu na Rehma za Allah), mpaka weupe wa shavu lake la kulia ulikuwa ukionekana na alikuwa akitoa salaam kushoto Assalaam Alaykum warahmatullah mpaka weupe wa shavu lake la kushoto ulikuwa ukionekana. (Abu Daud, Tirmidh, Nisai).*



## Lugha ya Swala

Lugha ya swala, kuanzia kwenye Takbira ya kuhirimia Swala mpaka kumalizia swala kwa Salaam, ni Kiarabu. Hekima yake iko wazi. Kiarabu ndio lugha ya Qur-an tukufu na kwa hiyo ndio lugha rasmi ya Kiislamu inayowaunganisha Waislamu wote ulimwenguni. Waislamu ni umma mmoja tu na Waislamu wote ni ndugu moja wasio baguana kwa lugha, rangi, taifa wala ubaguzi mwingine wa aina yoyote ile.Muislamu yeyote anaweza kuwa Imamu mahali popote ilimradi tu awe anatekeleza masharti ya Uimamu. Muislamu hana msikiti maalum. Misikiti yote ni yake na anaweza kuswali kwenye msikiti wowote ulimwenguni bila ya kupata tatizo lolote la lugha. Kwa sababu hii kila Muislamu inabidi ajifunze kiasi cha uwezo wake kutamka, kwa Kiarabu yale yote tuyasemayo katika swala.

## Mambo yanayobatilisha Swala

Mtu akiwa katika swala yuko katika hali maalum na haruhusiwi kufanya kitu kingine nje ya swala hata vile vitendo vya kawaida alivyovizoea. Hivyo ukiwa ndani ya swala ukifanya au kukitokea moja ya mambo yafuatayo, swala yako itakuwa imebatilika na itabidi uanze upya.

(a) Kutoelekea Qibla kwa kifua pasi na dharura yoyote ya kisheria.
(b) Kupatikana na hadathi kubwa, ndogo au ya kati na kati.
(c) Kufikwa na najisi mwilini, nguoni au mahali pa kuswalia.
(d) Kuvukwa na nguo ukawa uchi. Wanaume wanaovaa shati fupi wajihadhari sana hapa kwani,hasa wakati wa kurukuu na kusujudu, migongo yao (viuno vyao) chini ya usawa wa kitovu (panda za makalio) huwa wazi na hivi huhesabiwa kuwa wako uchi.
(e) Kusema au kutamka makusudi lau herufi moja yenye kuleta maana nje ya maneno ya swala.Mtume (s.a.w) amesema:

> *“Hakika ya hii swala, haifai ndani yake maneno ya watu kwani swala yenyewe ni Tasbih, Takbir na kusoma Qur-an. (Muslim)*

(f) Kula au kunywa japo kwa kusahau.
(g) Kufanya jambo lisilowiana na swala mfululizo mara tatu.
(h) Kuiacha nguzo yoyote ya swala
(i) Ukizidisha nguzo yoyote ya swala makusudi.
(j) Kumtangulia Imam au kuchelewa kwa nguzo mbili za kimatendo kwa makusudi.

(k) Kutia nia ya kuikata swala au kujishauri moyoni kuwa uikate au usiikate swala.
(l) Kuwa na shaka kuwa umetimiza au hujatimiza sharti au nguzo yoyote ya swala.
(m) Kupotewa na akili au kulala ndani ya swala.
(n) Kutoa Salaam kwa makusudi kabla ya kwisha swala.
(o) Kuswalishwa na asiyekuwa Muislamu.
(p) Kukhalifu utaratibu wa nguzo za swala, yaani kutangulia kutekeleza nguzo ya swala kabla ya kutekeleza nguzo inayostahiki kutangulia katika utaratibu wa swala.
(q) Kuleta dua ya kuomba kitu haramu au muhali.
(r) Kumshirikisha Allah (s.w) katika kuleta dua yaani kuleta dua ya kuomba kitu cha halali lakini humuombi Allah (s.w) peke yake.

**Dua na Dhikri Baada ya Swala**

Ni vizuri mara Muislamu anapomaliza kuswali kama hana dharura yoyote asiondoke bila ya kuleta Dhikri na dua kama alivyofundisha Mtume (s.a.w), kwani zina umuhimu mno katika kumsaidia mja kufikia lengo la swala na lengo la kuumbwa kwake kwa ujumla iwapo atayafahamu na kuyazingatia yale anayoyatamka.

Kutokana na Hadithi iliyosimuliwa na Samura bin Jandab(r.a) na kupokelewa na Bukhari(r.a), baada ya swala Mtume (s.a.w) aliwageukia Waislamu aliokuwa akiwaswalisha. Kisha aliomba maghfira (msamaha) mara tatu na kuongezea maneno yaliyoelezwa katika Hadithi zifuatazo:

Thawban (r.a) amesimulia kuwa Mtume (s.a.w) alipomaliza swala aliomba maghfira (msamaha) mara tatu kwa kusema:

***Astagh-firullah (Mara tatu)*** أَسْتَغْفِرُ اللهَ

*"Ninaomba msamaha kwa Allah" na kusema*

اللَّهُمَّ أَنْتَ السَّلاَمُ وَمِنْكَ السَّلاَمُ تَبَارَكْتَ يَاذَا الْجَلاَلِ وَالإِكْرَامِ

***Allahumma Antassalam waminkas-salaam Tabaarakta YaaDhal jallaali Wal-ikraam.***

*"Ewe Allah, wewe ni Amani, na kwako ndiko iliko Amani. Wewe ndiye Mbariki Ewe Mwenye Utukufu na Heshima". (Muslim)*

*Mughira bin Shu'bah (r.a) amesimulia kuwa Mtume (s.a.w) alikuwa akisema katika kila baada ya sala ya faradh:*

لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللهُ وَحْدَهُ لاَ شَرِيْكَ لَهُ لَهُ الْمُلْكُ وَ لَهُ الْحَمْدُ وَهُوَ

***Laa ilaha illallaahu wah-dahulaasharilikalahu, lahul-mulku walahul hamdu wahuwa 'alaa kulli shaiy-in qadiiru.*** عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيْرٌ

*"Hapana Mola ila Allah. Ni Mmoja tu, hana Mshirika wake Ufalme ni wake, ni mwenye kusifika kwa sifa zote zilizokamilika. Ni muweza wa kila kitu. (Muslim)*

*Mu'adh bin Jabali(r.a) amesimulia kuwa: Mtume wa Allah alimshika mkono na akasema "Oh Mu'adh (r.a), hakika ninakupenda. Nikajibu nami ninakupenda, Ewe Mtume wa Allah! Akasema (Mtume): Basi usiache kusema katika mwisho wa kila swala:*

للَّهُمَّ أَعِنِّيْ عَلَى ذِكْرِكَ وَ شُكْرِكَ وَحُسْنِ عِبَادَتِكَ

***Allahumma a'inniy 'alaa dhikrika, washukrika, wahus-ni 'ibaadatika***

*Ee Allah niwezeshe niwe mwenye kukumbuka na mwenye kukushukuru na niwe miongoni mwa waja wako wema" (Ahmad, Abu Daud, Nisai)*

*Ka'b ibn Ujrah (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: "Kuna Mu-aqqibaat (vifuatilizio), atakaye visoma hivyo kila baada ya swala ya faradh, hatahuzunika. Vifuatilizio hivi ni Tasbihi (kumtukuza Allah) mara 33. Tahmid (kumsifu Allah) mara 33 na Takbir (kumtaja Allah kwa ukubwa wake) mara 34.' (Sahihi Muslim).*

Vifuatilizo hivi ni kusema:

***Subhana llahi - (Mara 33)*** سُبْحَانَ اللهِ
*"Utukufu ni wake Allah"*

***Alhamdullillahi - (Mara 33)*** الْحَمْدُ لِلّهِ
*"Sifa zote Anastahiki Allah"*

***Allahu Akbar (mara 34)*** اللهُ أَكْبَرُ
*"Allah ni mkubwa kabisa"*

Baada ya nyiradi hizi, ni vizuri pia kuomba dua yoyote kulingana na haja zako kwa lugha yoyote. Jambo hili la kuomba dua baada ya swala, umuhimu wake unadhihirika katika hadithi ifuatayo:

*Abu Umamah amesimulia kuwa: Iliulizwa: "Ee Mtume wa Allah. ni dua gani ambayo hukubaliwa zaidi?" (Mtume) alijibu: (moja) ni ile ya katikati ya nusu ya pili ya usiku na (pili) kila baada ya swala ya faradhi". (Tirmidh)*

Hivyo ni jambo la msingi mno kuomba dua yoyote kila baada ya swala na dua zilizo nzito zaidi ni zile zilizomo kwenye Qur-an na hadithi za Mtume (s.a.w).

Kwa mfano ni vizuri kila baada ya swala, au baada ya dhikri zilizotajwa tuombe dua ifuatayo:

رَبِّ ٱجْعَلْنِى مُقِيمَ ٱلصَّلَوٰةِ وَمِن ذُرِّيَّتِى ۚ رَبَّنَا وَتَقَبَّلْ دُعَآءِ ﴿٤٠﴾

***Rabii J'alnii muqiimas-swalaati wamindhurriyyatii Rabbana Wataqabbal du'aaai.***

*Mola wangu! Nijaalie niwe msimamishaji swala, na kizazi changu! (Pia kiwe hivi). Mola wetu! Na upokee maombi yangu mengine... " (14:40-41).*

Jambo muhimu la kusisitiza ni kwamba dhikri na dua zitaletwa kimya kimya bila ya kupiga makelele na kila mmoja ataleta dhikri na dua kwa uhuru wake bila ya kuongozwa na mtu. Allah (s.w) ametukataza kumdhukuru kwa makelele kama anavyotuamrisha katika aya ifuatayo:

وَٱذْكُر رَّبَّكَ فِى نَفْسِكَ تَضَرُّعًا وَخِيفَةً وَدُونَ ٱلْجَهْرِ مِنَ ٱلْقَوْلِ بِٱلْغُدُوِّ

وَٱلْءَاصَالِ وَلَا تَكُن مِّنَ ٱلْغَٰفِلِينَ ﴿٢٠٥﴾

*"Na mtaje Mola wako moyoni mwako kwa unyenyekevu na khofu na bila ya kupiga kelele katika kauli (kumkumbuka Mola wako na umtaje) asubuhi na jioni wala usiwe miongoni mwa walioghafilika". (7:205)*

Pia rejea Qur'an (7:55) na (17:110).

## Khushui (Unyenyekevu) Katika Swala

Kuwa wanyenyekevu katika swala ni jambo la tatu la msingi linaloiwezesha swala kusimama. Ili swala imfikishe mja kwenye lengo,

haina budi kuswaliwa kwa khushui (unyenyekevu).

قَدْ أَفْلَحَ ٱلْمُؤْمِنُونَ ﴿١﴾ ٱلَّذِينَ هُمْ فِى صَلَاتِهِمْ خَٰشِعُونَ ﴿٢﴾

*"Hakika wamefuzu waumini ambao katika swala zao huwa ni wanyenyekevu" (23:1-2)*

Katika aya hii tunajifunza kuwa swala itakayompelekea mja kufaulu au kupata matunda yatokanayo na swala ni ile itakayoswaliwa kwa "Khushui".

## Maana ya "Khushui"

Neno "Khushui" ambalo limepewa tafsiri ya unyenyekevu hupatikana kwa kutuliza mwili na fikra na kuzingatia yale mja anayosema na kutenda katika swala.

## Namna ya Kupata Khushui Katika Swala

### 1. Kuutuliza Mwili

Kwa kujua kuwa mara tu unapohirimia swala na kusema "Allah Akbar", tayari uko katika hadhara ya Allah (s.w), na unazungumza naye, hunabudi kuutuliza mwili wako kwa heshima na taadhima kubwa kuliko anavyojituliza askari mbele ya mfalme wa dola. Utulivu wa mwili hupatikana kwa kutojipapasapapasa, kutochezesha viungo na kuangalia tu pale unaposujudia.

*"Abu Azarr(r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: Allah (s.w) aliyemuweza wa kila kitu haachi kuwa karibu na mja wakati anapokuwa kwenye swala pindi haangalii angalii pembeni. Anapoangalia pembeni Allah anakuwa mbali naye". (Ahmad, Abuu Daud, Nisai na Darimi).*

Ni wazi kuwa kuangalia angalia vitu wakati wa swala huyatoa mawazo ya mwenye kuswali nje ya mazingatio ya Allah (s.w). Halikadhalika mtikisiko au miondoko mingine yoyote ya mwili humtoa mwenye kuswali katika mazingatio ya yale anayotenda katika swala.

### 2. Kuzituliza fikra (moyo)

Fikra hutulia kwa kuzingatia kwa makini yale unayosoma katika swala. Bila shaka mazingatio yatapatikana kwa kujua maana ya yale uyasemayo mbele ya Mola wako. Kwa mfano ukisema kwa mazingatio: ***"Iyyaakana-a'budu Waiyyaakanasta'iinu"*** huku ukijua kuwa unatoa

ahadi mbele ya Allah (s.w) kuwa "*Utamuabudu na Kumtegemea yeye pekee*", huwezi tena baada ya swala katika kuendesha maisha yako, ukawa unamnyenyekea na kumtii mwingine. Vile vile mwenye kuswali ili abakie katika khushui hanabudi kujitahidi kutofikiria mambo mengine nje ya swala. Kila wakati ajitahidi kurejesha mawazo yake katika swala. Ili utulivu wa fikra upatikane, pia yahitajika mazingira matulivu yaliyoepukana na aina zote za vishawishi vya kelele na mazungumzo. Katika Qur-an Allah (s.w) anatufahamisha kuwa:

ادْعُوا رَبَّكُمْ تَضَرُّعًا وَخُفْيَةً ۚ إِنَّهُ لَا يُحِبُّ الْمُعْتَدِينَ ﴿٥٥﴾

*Mwombeni Mola wenu kwa unyenyekevu na kwa siri kwa sauti ndogo bila ya kufanya kelele. Yeye Mwenyezi Mungu hawapendi wapitao mipaka.(7:55)*

وَاذْكُر رَّبَّكَ فِي نَفْسِكَ تَضَرُّعًا وَخِيفَةً وَدُونَ الْجَهْرِ مِنَ الْقَوْلِ بِالْغُدُوِّ

وَالْآصَالِ وَلَا تَكُن مِّنَ الْغَافِلِينَ ﴿٢٠٥﴾

*"Na mtaje Mola wako moyoni mwako kwa unyenyekevu na khofu na bila ya kupiga kelele katika kauli (yako hiyo; mkumbuke Mola wako umtaje) asubuhi na jioni, wala usiwe miongoni mwa walioghafilika".(7:205)*

**Namna ya Kufikia Lengo la Swala**

Njia ya kufikia lengo la swala imeoneshwa katika aya iliyoainisha lengo la swala:

... إِنَّ الصَّلَاةَ تَنْهَىٰ عَنِ الْفَحْشَاءِ وَالْمُنكَرِ ۗ وَلَذِكْرُ اللَّهِ

أَكْبَرُ ۗ وَاللَّهُ يَعْلَمُ مَا تَصْنَعُونَ ﴿٤٥﴾

*"... Bila shaka swala (ikiswaliwa vilivyo) humzuilia (mwenye kuisimamisha) na mambo machafu na maovu, na kwa yakini kumbuko la Mwenyezi Mungu (lililomo ndani ya swala ni jambo) kubwa kabisa (la kumzuilia msimamishaji swala na mambo machafu na maovu). Na Mwenyezi Mungu anajua mnayoyatenda". (29:45)*

Katika aya hii tunajifunza kuwa kinachompelekea mwenye

kusimamisha swala aepukane na mambo machafu na maovu ni ile **dhikri** (kumbuko) juu ya Allah (s.w) iliyomo ndani ya swala. Dhikri hii pia inasisitizwa katika suratut Twaahaa:

إِنَّنِيٓ أَنَا ٱللَّهُ لَآ إِلَٰهَ إِلَّآ أَنَا۠ فَٱعۡبُدۡنِي وَأَقِمِ ٱلصَّلَوٰةَ لِذِكۡرِيٓ ﴿١٤﴾

*"Kwa yakini mimi ndiye Mwenyezi Mungu, hakuna astahiliye kuabudiwa kwa haki ila mimi; basi niabudu na usimamishe swala kwa kunidhikiri (kunikumbuka)". (20:14)*

Kihalisia ukiirejea swala kuanzia pale kwenye kuchunga sharti zake kisha ukaja kwenye kutekeleza nguzo zake kuanzia kwenye **nia** na **takbira** ya kuhirimia mpaka kutoa **salamu**, kunakumkumbuka Allah (s.w) kwa wingi. Kwa mfano katika kutekeleza sharti za swala katika kujitwaharisha, kujisitiri, kuchunga wakati na kuelekea Qibla, msimamishaji swala anakuwa hadhiri katika kutekeleza hayo, akiwa na yakini kuwa swala yake haitaswihi iwapo atakiuka kipengele chochote katika kutekeleza sharti hizo. Na kwa msingi huu Mtume (s.a.w) anatuasa:

*"Hakutawadha yule ambaye wakati wa kutawadha hamzingatii (hamdhikiri) Mwenyezi Mungu".*

Tunachojifunza hapa ni kwamba wakati tunapotekeleza sharti za swala hatunabudi kuzingatia kwamba tunatekeleza utaratibu aliotuwekea Allah (s.w) ili tuweze kufikia lengo la kusimamisha swala. Kwa maana hii mtu aliyejitwaharisha vilivyo kwa kujiepusha na **Hadath** na **Najisi** kwa ajili ya kutafuta radhi za Allah (s.w), hawezi kuwa mchafu wa tabia katika maisha yake ya kila siku. Mtu aliyejisitiri vilivyo wakati wa swala kwa ajili ya kutafuta radhi za Allah (s.w), hawezi kutembea nje ya mipaka ya sitara aliyomuwekea Allah (s.w). Mtu anayechunga muda wa swala, kwa ajili ya kutafuta radhi za Allah (s.w) hawezi tena kupoteza muda wake ambao ndio rasilimali kuu ya maisha yake katika mambo ya upuuzi. Halikadhalika mtu anayeelekea Qibla (Al-Kaabah) wakati wa swala kwa ajili ya kutafuta radhi za Allah (s.w), hawezi kuelekea asikotaka Allah (s.w) katika kuendesha maisha yake ya kila siku. Hivyo utekelezaji wa shuruti zote za swala kwa **khushui**, humfikisha msimamishaji swala kwenye kutakasika na mambo machafu na maovu.

Ukija kwenye utekelezaji wa nguzo za swala kuanzia kwenye **nia** na **takbira** ya kuhirimia swala mpaka kwenye kutoa **salamu**, utakuta kunadhikiri mbalimbali juu ya Allah (s.w) ikiwa ni pamoja na takbir

(kumtukuza Allah), tahmid (kumsifu Allah) tasbih (kumtakasa Allah), tahiyyat (maamkizi rasmi kwa Allah), kutoa ahadi ya utii kwa Allah na kumuomba Allah maombi mbalimbali kama tulivyoona tulipopitia nguzo na Sunnah za swala. Vipengele vyote hivi vya nguzo na Sunnah za swala vikitekelezwa kwa **khushui** humuwezesha mwenye kusimamisha swala kumtii Allah (s.w) ipasavyo katika kuendesha maisha yake ya kila siku. Utakuwa ni unafiki mkubwa usio na kifani kwa mtu kumtukuza, kumsifu, kumtakasa na kumpa Allah (s.w) maamkizi ya heshima ya hali ya juu kiasi hicho, ikifuatiwa na ahadi kubwa kubwa za utii kwake pekee, kisha baada ya swala akaendesha maisha yake ya kila siku kama wanavyoendesha maisha yao makafiri na washirikina. Hii ndio maana ya Allah (s.w) kuwakamia adhabu kali wale wanaoswali kwa mtindo huu.

فَوَيْلٌ لِّلْمُصَلِّينَ ﴿٤﴾ ٱلَّذِينَ هُمْ عَن صَلَاتِهِمْ سَاهُونَ ﴿٥﴾ ٱلَّذِينَ هُمْ يُرَآءُونَ ﴿٦﴾

*"Basi adhabu kali itawathubutikia wanaoswali. Ambao wanapuuza swala zao. Ambao hufanya riyaa." (107:4-6)*

## Swala tano za Faradh katika Nyakati za Dharura

Amri ya kusimamisha swala tano imeambatana na nyakati makhususi kama tunavyojifunza katika aya ifuatayo:

فَأَقِيمُوا۟ ٱلصَّلَوٰةَ ۚ إِنَّ ٱلصَّلَوٰةَ كَانَتْ عَلَى ٱلْمُؤْمِنِينَ كِتَـٰبًا مَّوْقُوتًا

*"Basi simamisheni swala Kwa hakika swala kwa waislamu ni faradhi iliyowekewa nyakati makhsusi" (4:103)*

Hivyo swala ya mja haitakubaliwa iwapo ataiswali nje ya wakati wake makhsusi. Hapana "**kadha**" katika swala.

Pamoja na amri ya kuiswali kila swala ya faradhi katika wakati wake makhsusi, Allah (s.w) aliye Mwingi wa Rehma haikalifishi nafsi yoyote katika kuipa amri zake ila huitaraji kila nafsi itekeleze amri hizo kwa kadiri ya uwezo aliyoijaalia kuwa nao. Mara kwa mara katika kutufahamisha huruma zake juu yetu, Allah(s.w.) anakariri:

لَا يُكَلِّفُ ٱللَّهُ نَفْسًا إِلَّا وُسْعَهَا ۚ . . . ﴿٢٨٦﴾

*"Mwenyezi Mungu haikalifishi nafsi yoyote ila yaliyosawa na uwezo wake..." (2:286)*

Baada ya kutoa ruhusa ya kutofunga wagonjwa na wasafiri, wakati wa mwezi wa Ramadhani na badala yake walipe "kadha" siku walizokula anatudhihirishia Rehma zake kwa kutufahamisha:

يُرِيدُ ٱللَّهُ بِكُمُ ٱلْيُسْرَ وَلَا يُرِيدُ بِكُمُ ٱلْعُسْرَ ... ﴿١٨٥﴾

*"... Mwenyezi Mungu anakutakieni yaliyo mepesi, wala hakutakieni yaliyo mazito..." (2:185)*

Pia baada ya kutoa ruhusa ya kutayammam, baada ya kukosa maji, au kwa ajili ya maradhi au mtu anapokuwa safarini, katika Sura ya 5 aya ya 6, Allah (s.w) anamalizia kwa kusema:-

مَا يُرِيدُ ٱللَّهُ لِيَجْعَلَ عَلَيْكُم مِّنْ حَرَجٍ وَلَٰكِن يُرِيدُ لِيُطَهِّرَكُمْ
وَلِيُتِمَّ نِعْمَتَهُۥ عَلَيْكُمْ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿٦﴾

*"... Hapendi Mwenyezi Mungu kukutieni katika taabu, bali anataka kukutakaseni na kutimiza neema yake juu yenu ili mpate kushukuru". (5:6)*

## Swala ya Mgonjwa

(1) Mgonjwa ameruhusiwa kutayammam iwapo hawezi kutumia maji kutokana na ugonjwa wake:

وَإِن كُنتُم مَّرْضَىٰٓ أَوْ عَلَىٰ سَفَرٍ أَوْ جَآءَ أَحَدٌ مِّنكُم مِّنَ ٱلْغَآئِطِ
أَوْ لَٰمَسْتُمُ ٱلنِّسَآءَ فَلَمْ تَجِدُوا۟ مَآءً فَتَيَمَّمُوا۟ صَعِيدًا طَيِّبًا فَٱ
مْسَحُوا۟ بِوُجُوهِكُمْ وَأَيْدِيكُمْ ۗ إِنَّ ٱللَّهَ كَانَ عَفُوًّا غَفُورًا ﴿٤٣﴾

*"...Na kama mkiwa wagonjwa (mmekatazwa kutumia maji) au mmo safarini au mmoja wenu ametoka msalani (chooni) au mmewagusa(mmewajamii), wanawake - na msipate maji basi ukusudieni (tayamamuni) udongo safi, mpake nyuso zenu na mikono yenu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe (na) Mwenye kughufiria". (4:43)*

وَإِن كُنتُم مَّرْضَىٰٓ أَوْ عَلَىٰ سَفَرٍ أَوْ جَآءَ أَحَدٌ مِّنكُم مِّنَ
ٱلْغَآئِطِ أَوْ لَـٰمَسْتُمُ ٱلنِّسَآءَ فَلَمْ تَجِدُوا۟ مَآءً فَتَيَمَّمُوا۟
صَعِيدًا طَيِّبًا فَٱمْسَحُوا۟ بِوُجُوهِكُمْ وَأَيْدِيكُم مِّنْهُ ۚ مَا يُرِيدُ
ٱللَّهُ لِيَجْعَلَ عَلَيْكُم مِّنْ حَرَجٍ وَلَـٰكِن يُرِيدُ لِيُطَهِّرَكُمْ وَلِيُتِمَّ
نِعْمَتَهُۥ عَلَيْكُمْ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿٦﴾

*"... Na mkiwa wagonjwa au mmo safarini, au mmoja wenu ametoka chooni au mmeingiliana na wanawake, na hamkupata maji, basi kusudieni (tayammamuni) udongo ulio safi na kuupaka nyuso zenu na mikono yenu. Hapendi Mwenyezi Mungu kukutieni katika taabu, bali anataka kukutakaseni na kutimiza neema Yake juu yenu ili mpate kushukuru". (5:6)*

(2) Iwapo mgonjwa hajimudu na hana wa kumtwaharisha kwa maji au kwa udongo itabidi atayammamu kifikra na kuswali hivyo hivyo. Hili ni sahali kwa kauli ya Allah (s.w):

مَا يُرِيدُ ٱللَّهُ لِيَجْعَلَ عَلَيْكُم مِّنْ حَرَجٍ وَلَـٰكِن يُرِيدُ لِيُطَهِّرَ
كُمْ وَلِيُتِمَّ نِعْمَتَهُۥ عَلَيْكُمْ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿٦﴾

*"Hapendi Allah kukutieni katika taabu, bali anataka kukutakaseni na kutimiza neema Yake juu yenu". (5:6)*

(3) Mgonjwa anaruhusiwa kuswali akiwa amekaa na kuelekea Qibla iwapo ana uwezo huo, vinginevyo ataelekea popote pale kwa kadiri ya uwezo wake. Atarukuu na kusujudu katika hali hiyo ya kukaa iwapo anaweza, vinginevyo atarukuu na kusujudu kwa ishara tu.

(4) Iwapo mgonjwa hawezi hata kukaa ataswali akiwa amelala kwa ubavu huku akiwa ameelekea Qibla kama ana uwezo wa kufanya hivyo, vinginevyo ataelekea popote pale. Pia kama hawezi kulala kwa ubavu atalala chali. Kama hawezi kulala chali ataswali kwa ishara akiwa amelala vyovyote vile awezavyo.

(5) Pia mgonjwa anaruhusiwa kuchanganya swala kama msafiri (rejea swala ya msafiri) kama hivyo ndivyo hali ya mazingira ya ugonjwa inavyotaka.

Kutokana na tahfifu hizi, ugonjwa si udhuru wa kumruhusu mtu asiswali swala ya faradh kwa wakati wake hata kama mgonjwa huyo atakuwa mahututi kitandani akiwa nyumbani au hospitalini maadamu bado ana akili timamu.

## Swala ya Msafiri

Kutokana na umuhimu wa kusimamisha swala hata mtu akiwa safarini analazimika kusimamisha swala. Lakini Allah (s.w) kwa Rehma yake ametuhafifishia swala tukiwa safarini kama ifuatavyo:-

**Kwanza**, tunaruhusiwa ***kutayammamu*** tukiwa safarini ili tuweze kusimamisha swala kama hatutapata maji au hatutaweza kutumia maji ndani ya chombo tunachosafiria. Ruhusa hii tunaipata katika aya ifuatayo:-

وَإِن كُنتُم مَّرْضَىٰٓ أَوْ عَلَىٰ سَفَرٍ أَوْ جَآءَ أَحَدٌ مِّنكُم مِّنَ
ٱلْغَآئِطِ أَوْ لَٰمَسْتُمُ ٱلنِّسَآءَ فَلَمْ تَجِدُوا۟ مَآءً فَتَيَمَّمُوا۟
صَعِيدًا طَيِّبًا فَٱمْسَحُوا۟ بِوُجُوهِكُمْ وَأَيْدِيكُم مِّنْهُ ۚ مَا يُرِيدُ
ٱللَّهُ لِيَجْعَلَ عَلَيْكُم مِّنْ حَرَجٍ وَلَٰكِن يُرِيدُ لِيُطَهِّرَكُمْ وَلِيُتِمَّ
نِعْمَتَهُۥ عَلَيْكُمْ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿٦﴾

*".. Na mkiwa wagonjwa au mmo safarini, au mmoja wenu ametoka chooni au mmeingiliana na wanawake, na hamkupata maji, basi kusudieni (tayammamu) udongo safi na kupaka nyuso zenu na mikono yenu. Hapendi Mwenyezi Mungu kukutieni katika taabu, bali anataka kukutakaseni na kutimiza neema yake juu yenu ili mpate kushukuru" (5:6)*

Pia inawezekana udongo usipatikane ndani ya chombo tunachosafiria. Ikiwa ni hivyo tunaruhusiwa kutumia kuta au dari ya chombo. Kwa maana nyingine tunaruhusiwa kupiga viganja vyetu juu ya ukuta au dari ya chombo au juu ya kitu chochote ndani ya chombo chenye vumbi vumbi na kupaka uso kwa pigo la kwanza kisha kupaka

mikono kwa pigo la pili kama kawaida ya kutayammamu. Mtume (s.a.w) alitumia ukuta kutayammamu kama tunavyofahamishwa katika Hadithi:

*Amesimulia Abu Juhaim Al-Ansaari, Mtume (s.a.w) alitokea upande wa Bir Jamal. Mtu mmoja alikutana naye na akamsalimu. Lakini (Mtume) hakuitikia salaam hii mpaka alipokwenda kwenye ukuta na kupaka vumbi lake mikononi na usoni mwake (alipotayammamu) ndipo akarudishia salaam ile. (Bukhari).*

**Pili**, msafiri anaruhusiwa ***kupunguza*** swala kama ilivyo katika aya ifuatayo:

وَإِذَا ضَرَبْتُمْ فِى ٱلْأَرْضِ فَلَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ أَن تَقْصُرُوا۟ مِنَ ٱلصَّلَوٰةِ إِنْ

خِفْتُمْ أَن يَفْتِنَكُمُ ٱلَّذِينَ كَفَرُوٓا۟ ۚ إِنَّ ٱلْكَٰفِرِينَ كَانُوا۟ لَكُمْ عَدُوًّا مُّبِينًا

*":Na mnaposafiri katika ardhi, si vibaya kwenu kama mkifupisha swala, iwapo mnaogopa ya kwamba wale waliokufuru watakutaabisheni. Bila shaka makafiri ni maadui zenu dhahiri" (4:101)*

Swala zinazofupishwa ni swala za rakaa 4 - Adhuhuri, Al-'asr na Al-Ishaai. Magharibi yenye rakaa 3 na subhi yenye rakaa 2 zinaswaliwa kwa ukamilifu. Ifahamike wazi kuwa kufupisha swala katika safari si lazima bali ni tahfifu tu iliyotolewa kwa wasafiri. Lakini ukiwa msafiri ni bora kutumia tahfifu hii kwani ni neema kutoka kwa Allah (s.w).

*Ya-'Al bin Umayyah (r.a) amesimulia. "Nilisema kwa Umar bin Al-Khattab (r.a), Allah (s.w) amesema, "Mnaweza kufupisha swala iwapo mnahofia kuwa makafiri watawabughudhi". Watu sasa wako katika amani. Umar akasema:"Nami pia ninashangaa kama wewe". Kisha nilimuuliza Mtume wa Allah alisema (Mtume): "Hii ni zawadi (neema) aliyokupeni Allah. Kwa hiyo pokeeni zawadi yake" (Muslim)*

Ilikuwa ni kawaida ya Mtume (s.a.w) kufupisha swala kila alipokuwa safarini kama tunavyojifuna katika Hadithi zifuatazo:

*Abdullah bin Umar (r.a) amehadithia kuwa alisafiri na Mtume (s.a.w), Abu Bakr (r.a), Umar (r.a) na Uthman (r.a) na kamwe hakuwaona kabisa kuswali zaidi ya rakaa mbili katika swala za rakaa nne ndani ya safari. (Muslim)*

*Anas (r.a)ametuhadithia kuwa Mtume wa Allah aliswali dhuhuri akiwa Madina kwa rakaa nne na aliswali Asr akiwa Zul-Hulaifah kwa rakaa mbili (Bukhari na Muslim)*

Kuhusiana na masafa ambayo mtu anaruhusiwa kupunguza swala ni vyema tunukuu maelezo yaliyoandikwa na Sheikh Sayyid Sabiq katika Kitabu chake Fiqhus-Sunnah yaliyo chini ya mlango aliouita swala ya Msafiri:

*"Hitimisho tunalolipata kutokana na aya ya Qur-an ni kuwa safari yoyote ile, iwe ndefu au fupi maadamu inakubalika katika maana ya kilugha ya safari basi inatosha kwa mtu kupunguza sala, kuchanganya sala au kutokufunga.Katika Sunnah (hadith) hakuna chochote kilichoripotiwa kuhusisha maana hii ya jumla na maana maalum".*

Ibn Al-Mundhir na wanazuoni wengine wametaja zaidi ya wapokezi ishirini kuhusiana na jambo hili.

Vile vile kuna suala la muda gani mtu anaruhusiwa kupunguza swala akiwapo safarini. Katika hadithi zifuatazo tunajifunza kuwa msafiri atafupisha swala kwa muda wote atakaokuwa safarini hadi atakaporejea kwao.

*Anas (r.a) amehadithia; Tulisafiri na Mtume (s.a.w) kutoka Madinah kwenda Makka. Alikuwa akiswali kila swala kwa rakaa mbili, mpaka aliporejea Madina. Waliulizwa, mlikaa Makka kwa muda kidogo? Alijibu. Tulikaa pale kwa siku kumi" (Bukhari).*

*Ibn Abbas(r.a) amesimulia kuwa Mtume (s.a.w) alisafiri na alikaa humo safarini (ugenini) kwa muda wa siku kumi na tisa akiswali rakaa mbili mbili. Ibn Abbas amesema, kwa hiyo tuliswali rakaa mbili kila wakati tukiwa tunaelekea Makka kwa siku 19. Tulipokaa zaidi ya muda huo tuliswali rakaa nne.(Bukhari)*

*Imraan bin Husain (r.a) ameeleza: Nilikuwa pamoja na mtume (s.a.w) katika vita vya Jihad na kushuhudia ushindi tukiwa pamoja naye. Alikaa Makka siku 18 akiswali kila swala kwa rakaa mbili, akisema "Nyinyi wenyeji swalini rakaa nne. Sisi tu wasafiri". (Abu Daud).*

Kutokana na hadithi hizi tunajifunza kuwa hapana muda maalum uliowekwa kwa msafiri kupunguza swala. Pia tunajifunza kuwa mtu anaye swali swala ya safari anaweza kuwa Imamu ila ni vyema awafahamishe wale wanaomfuata ili yeye akitoa salaam baada ya rakaa mbili wale wakazi wa mji waendelee na kuikamilisha swala kwa rakaa nne. Lakini msafiri akiamua kumfuata Imamu mkazi itabidi akamilishe swala kwa

rakaa nne kama Imamu.

**Tatu,** msafiri pia amepewa tahfifu katika swala kwa kupewa ruhusa ya ***kukusanya*** swala mbili za faradhi na kuziswali kwa wakati mmoja kama tunavyojifunza kutokana na Hadithi zifuatazo:

> *Ibn Abbas(r.a) amehadithia kuwa Mtume wa Allah alikuwa akichanganya Dhuhur na Asr wakati akitoka safarini, pia alichanganya Magharibi na Isha. (Bukhari).*
>
> *Mua'dhi bin Jabal (r.a) amesimulia kuwa Mtume (s.a.w) alikuwa katika vita vya Tabuk. Jua lilipopinduka kidogo aliswali Dhuhuri pamoja na Asr. Kama alianza safari kabla ya jua kupinduka (kabla ya wakati wa dhuhur) aliakhirisha Dhuhur mpaka wakati wa Asr. Hali kadhalika kwa swala ya Magharibi, jua lilipotua kabla hajaanza safari, aliswali magharibi pamoja na isha, na kama alianza kusafiri kabla ya jua kutua; aliakhirisha Magharibi mpaka wakati wa isha na kuziswali pamoja. (Abu Daud, Tirmidh).*

Kutokana na Hadithi hizi msafiri anaruhusiwa kuchanganya Adhuhuri na Asr kuziswali wakati mmoja, pia anaruhusiwa kuswali Magharibi na Isha kwa wakati mmoja, ila swala ya Alfajiri haichanganyiki na swala yoyote na wakati wake ni ule ule wa kawaida.

Kuna aina mbili za mkusanyo na zote zinajuzu. Aina ya kwanza huitwa ***Jam-'u Taqdym***. Katika aina hii unazikusanya swala mbili katika wakati wa swala ya mwanzo. Yaani kwa kuswali Adhuhuri na 'Asr pamoja katika wakati wa Adhuhuri kwa adhana moja na Iqama mbili. Hivyo hivyo utaswali magharibi na isha katika wakati wa Magharibi.

Aina ya pili huitwa ***Jam'u Ta-akhir***. Katika aina hii unazikusanya swala mbili katika wakati wa swala inayofuatia. Yaani msafiri ataswali Adhuhuri na Asr pamoja katika wakati wa Al-'Asr kwa adhana moja na Iqama mbili. Hali kadhalika ataswali Magharibi na Ishaa kwa pamoja katika wakati wa Ishaa.

Namna ya kuswali swala za mkusanyo wa Adhuhuri na al-'Asr, ukisha-adhini na kukimu utaanza kuswali rakaa mbili za Adhuhuri. Baada ya kutoa Salaam utasimama na kukimu tena kisha utaswali rakaa mbili za Al-'Asr.

Kama unaswali ***Jam-'u Ta-akhir*** ya mkusanyo wa Magharibi na Ishaa, baada ya kuadhini na kukimu, utaanza kuswali rakaa tatu za Magharibi kama kawaida. Baada ya kutoa salaam utasimama na kukimu tena na kisha utaswali rakaa mbili za Isha.

Kama tunavyojifunza katika Hadithi uamuzi wa kukusanya swala katika wakati wa swala ya mwanzo (Jam-’u Taqdym) au katika wakati wa swala inayofuatia (Jam’uta-Akhr) utategemeana na hali ya safari kama tunavyojifunza katika Hadithi ifuatayo:-

*Abdullah ibn Abbas(r.a) amesema: “Mwenendo wa Mtume (s.a.w) ulikuwa kabla hajaanza safari akiona kuwa jua limepindukia (wakati wa Adhuhuri umeingia) alikuwa akiswali Adhuhuri na al-Asr na kisha huanza safari yake vinginevyo akiona, kuwa bado jua halijapinduka, basi huianza safari yake na mbele ya safari akiswali Adhuhuri na al-’Asr katika wakati wa Al-’Asr. Hivyo hivyo akiona jua limeshazama alikuwa akiswali Magharibi na Ishaa wakati huo wa Magharibi kabla ya kuanza safari, na kama jua bado halijazama basi huanza safari yake kisha huswali Magharibi na Ishaa wakati wa Isha. (Ahmad)*

**Nne**, msafiri pia amefanyiwa wepesi wa kusimamisha swala, kwa kuruhusiwa ***kuswali huku anatembea*** au anaendelea na safari juu ya kipando au chombo anachosafiria. Ruhusa hii tunaipata katika aya zifuatazo:-

حَٰفِظُواْ عَلَى ٱلصَّلَوَٰتِ وَٱلصَّلَوٰةِ ٱلۡوُسۡطَىٰ وَقُومُواْ لِلَّهِ قَٰنِتِينَ ﴿٢٣٨﴾ فَإِنۡ
خِفۡتُمۡ فَرِجَالًا أَوۡ رُكۡبَانٗاۖ فَإِذَآ أَمِنتُمۡ فَٱذۡكُرُواْ ٱللَّهَ كَمَا عَلَّمَكُم مَّا لَمۡ
تَكُونُواْ تَعۡلَمُونَ ﴿٢٣٩﴾

*Hifadhini swala na swala ya kati na kati. Na simameni kwa unyenyekevu katika kumuabudu Mwenyezi Mungu. Na kama mkiwa na khofu (basi swalini) na hali ya kuwa mnakwenda kwa miguu au mmepanda vipando. Na mtakapokuwa katika amani, basi mkumbukeni Mwenyezi Mungu (swalini) kama alivyokufunzeni yale mliyokuwa hamyajui”. (2:238-239)*

Pia Hadithi ifuatayo inatufahamisha juu ya swala ya Mtume (s.a.w) juu ya kipando:

*Ibn Umar (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah alipokuwa safarini alikuwa akiswali Ishaa juu ya ngamia katika upande wowote ule atakapoelekea, akiswali kwa ishara wakati wa usiku ila kwa swala za faradhi na alikuwa akiswali witri juu ya ngamia anayetembea. (Bukhari, Muslim)*

Ilivyo ni kwamba msafiri anaruhusiwa kuswali juu ya kipando huku anaendelea na safari. Namna ya kutekeleza swala hii ni kwamba, baada ya msafiri kutawadha au kutayammamu, ikiwa anasafiri kwa mguu au

kwa mnyama na anaona hofu ya kuvamiwa na maadui au wanyama, atafunga swala akiwa ameelekea Qibla, kisha ataendelea na swala huku anatembea akiwa ameelekea kule anakokwenda. Ataswali kwa ishara tu. Ikiwa msafiri anasafiri, kwa chombo kama vile gari, meli, ndege n.k atatawadha au atatayammamu, kisha atakaa na kuelekea popote pale kiti chake kinavyomruhusu, kisha ataadhini na kukimu na kuswali kwa ishara kama vile kuinamisha kichwa na kuinua katika kuashiria visimamo, rukuu, itidali, sijda na vikao. Inapendekezwa kuwa mtu ainamishe kichwa zaidi kwa sijda kuliko vile anavyoinamisha katika kuashiria rukuu.

### Kusimamisha Swala Vitani

Muislamu haruhusiwi kuswali swala ya faradhi nje ya wakati wake hata akiwa katika vita vya kupigania Dini ya Allah(s.w). Bali Allah (s.w) ametuhafifishia swala, tukiwa vitani na kutuelekeza tuswali ifuatavyo:

وَإِذَا كُنتَ فِيهِمْ فَأَقَمْتَ لَهُمُ ٱلصَّلَوٰةَ فَلْتَقُمْ طَآئِفَةٌ مِّنْهُم مَّعَكَ وَلْيَأْخُذُوٓا۟
أَسْلِحَتَهُمْ فَإِذَا سَجَدُوا۟ فَلْيَكُونُوا۟ مِن وَرَآئِكُمْ وَلْتَأْتِ طَآئِفَةٌ أُخْرَىٰ لَمْ
يُصَلُّوا۟ فَلْيُصَلُّوا۟ مَعَكَ وَلْيَأْخُذُوا۟ حِذْرَهُمْ وَأَسْلِحَتَهُمْ ۗ وَدَّ ٱلَّذِينَ كَفَرُوا۟
لَوْ تَغْفُلُونَ عَنْ أَسْلِحَتِكُمْ وَأَمْتِعَتِكُمْ فَيَمِيلُونَ عَلَيْكُم مَّيْلَةً وَٰحِدَةً ۚ وَلَا
جُنَاحَ عَلَيْكُمْ إِن كَانَ بِكُمْ أَذًى مِّن مَّطَرٍ أَوْ كُنتُم مَّرْضَىٰٓ أَن تَضَعُوٓا۟
أَسْلِحَتَكُمْ ۖ وَخُذُوا۟ حِذْرَكُمْ ۗ إِنَّ ٱللَّهَ أَعَدَّ لِلْكَٰفِرِينَ عَذَابًا مُّهِينًا ﴿١٠٢﴾

"*Na unapokuwa pamoja nao (Waislamu katika vita) ukawaswalisha, basi kundi moja miongoni mwao wasimame pamoja nawe (waswali) na washike silaha zao. Na watakapomaliza sijda zao basi na wende nyuma yenu (kulinda); na lile kundi jingine ambalo halijaswali liswali pamoja nawe, nao washike hadhari yao na silaha zao (humo ndani ya swala, maana) wale waliokufuru wanataka mghafilike na silaha zenu na vitu vyenu ili wakuvamieni mvamio wa mara moja. Wala si vibaya kwenu ikiwa mnaona udhia kwa sababu ya mvua au mnaona ugonjwa, kuondoa silaha zenu,.*

*Na mshike hadhari yenu. Hakika Mwenyezi Mungu amewaandalia makafiri adhabu itakayowadhalilisha". (4:102)*

Namna ya kusimamisha swala katika uwanja wa vita kutokana na maelekezo ya aya hii ni kwamba, askari wagawanyike katika makundi mawili ambayo yataswalishwa na Imamu mmoja na swala itafupishwa kama ilivyo katika swala ya safari. Kundi moja litaanza kuswali na Imamu wakiwa na silaha zao na kundi lingine litabaki katika ulinzi. Imamu ataswali rakaa moja na hili kundi la kwanza na watakaponyanyuka kuswali rakaa ya pili Imamu atabakia pale akiendelea kusoma Qur-an na kila mtu katika wale wanaomfuata, atamaliza upesi upesi rakaa ya pili na baada ya kutoa Salaam atarudi nyuma upesi kuchukua nafasi ya ulinzi. Baada ya kundi la pili kupokelewa nafasi zao, watakwenda kujiunga na Imamu ambaye bado anaendelea na rakaa yake ya pili. Wote watakapojiunga na swala, Imamu atamalizia swala yake ya rakaa mbili. Baada ya Imamu kutoa salaam kila mmoja katika wale wanaomfuata atasimama na kumalizia rakaa yake ya pili.

Aya hii ya (4:102) inayotuelekeza namna ya kuswali tukiwa katika vita vya kupigania Dini ya Allah (s.w) inafuatiwa na aya inayotoa amri ya kusimamisha swala kwa nyakati zake kama tunavyosoma:

فَإِذَا قَضَيْتُمُ ٱلصَّلَوٰةَ فَٱذْكُرُوا۟ ٱللَّهَ قِيَٰمًا وَقُعُودًا وَعَلَىٰ جُنُوبِكُمْ ۚ فَإِذَا
ٱطْمَأْنَنتُمْ فَأَقِيمُوا۟ ٱلصَّلَوٰةَ ۚ إِنَّ ٱلصَّلَوٰةَ كَانَتْ عَلَى ٱلْمُؤْمِنِينَ كِتَٰبًا مَّوْقُوتًا

*Mwishapo kuswali kuweni mnamkumbuka Mwenyezi Mungu - msimamapo na mkaapo na (mlalapo) ubavu. Na mtakapopata amani, basi simamisheni swala (kama kawaida). Kwa hakika swala kwa Waislamu ni faradhi iliyowekewa nyakati maalumu. (4:103)*

Hebu fikiri: Kama askari wa Allah (s.w) aliyejitoa muhanga kwa mali yake, ahli zake na nafsi yake kwa ajili ya kupigania dini ya Allah (s.w) hakuruhusiwa kuiacha swala au kuiswali nje ya wakati wake, je wewe uliyezama kwenye shughuli nyingine ndio utegemee kusamehewa kwa kupitisha wakati wa swala ukaswali wakati unapojiona kuwa huna shughuli. Aya hii inatufahamisha kwa uwazi kuwa swala tano zimefaradhishwa kwetu pamoja na nyakati zake makhsusi.

Tukiondoa ruhusa tulizopewa kuziswali swala kidharura tunapokuwa vitani, na tukiondoa udhuru wa kusahau na kupitiwa na

usingizi hapana ruhusa yoyote iliyotolewa katika Qur-an au Hadithi inayokubalika kuswali kadha kama wengi wafanyavyo. Je, mtindo huu wa kuswali kadha tunauiga kwa nani? Je, huku sio kupuuza swala? Kama tunapuuza swala kwa nini tusitarajie kupata ghadhabu za Allah (s.w) badala ya kujidanganya na kujipa matumaini ya kupata malipo mema kutoka kwake kutokana na kadha zetu hizo. Ujira wa wapuuzaji wa swala unabainishwa katika Qur-an:

فَوَيْلٌ لِّلْمُصَلِّينَ ﴿٤﴾ الَّذِينَ هُمْ عَن صَلَاتِهِمْ سَاهُونَ ﴿٥﴾

*Basi, adhabu itawathibitikia wanao swali. Ambao wanapuuza swala zao. (107:4-5).*

## Kusimamisha Swala ya Jamaa

Ni wajibu na imekokotezwa sana kwa Waislamu wanaume kusimamisha swala za faradh katika jamaa. Swala ya Vita kama ilivyobainishwa katika Qur-an (4:102) ni kielelezo cha umuhimu wa kusimamisha swala za faradhi katika jamaa. Kama katika vita waislamu wamesisitizwa kuswali pamoja katika jamaa, itakuwaje tena katika hali ya kawaida Muislamu ajiamulie kuswali peke yake nyumbani kwake?

Mtume (s.a.w) ametuagiza kwa msisitizo mkubwa kusimamisha swala katika jamaa kama tunavyojifunza katika Hadithi zifuatazo:

*Ibn Abbas (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: Atakaye msikia muadhini (kwa ajili ya swala), pasina udhuru wa kumzuia, hana budi kumuitikia. Wakauliza: Ni dharura gani (itakayomruhusu Muislamu kutomuitikia muadhini)? Alijibu (Mtume). Hofu ya kudhuriwa njiani na ugonjwa. Hana swala atakayeswali mwenyewe bila ya jamaa (baada ya kusikia adhana),(Abu Daud)*

*Abu Darda (r.a) ameeeleza kuwa Mtume wa Allah amesema, hapatakuwa na watu watatu katika kijiji au jangwani, wakaamua kuswali kila mmoja peke yake, ila Shetani huwemo katika swala zao. Hapana budi kuswali jamaa kwa sababu mbwa mwitu humkamata kondoo aliyejitenga na kundi. (Ahmad, Abu Daud, Nisai).*

Hadithi hizi mbili zinasisitiza umuhimu wa kuswali swala ya jamaa. Imesisitizwa kwamba, kila mwenye kusikia adhana, kwa sauti ya kawaida (bila ya kipaza sauti) au kila aliyeko karibu na msikiti inamlazimu atoke kuitikia mwito wa adhana kwa swala ya jamaa. Hata wale walio mbali na msikiti, (vijijini au shambani) hawana budi

kukusanyika pamoja na kuswali jamaa. Hekima ya kusisitizwa kuswali jamaa imeelezwa katika Hadithi ya pili kuwa ni silaha ya kuunganisha nyoyo na kuziwezesha kumshinda Shetani. Hii ina maana kuwa vishawishi vingi vinavyomjia mtu kwenye swala hupungua au hutoweka wakati mtu anaposwali katika jamaa.

Pia Hadithi zifuatazo zinaonesha umuhimu wa swala ya jamaa:
*Abu Hurairah (r.a) amesimulia kuwa Mtume (s.a.w) amesema, "Naapa kwa yule ambaye maisha yangu yako mikononi (mwake), hakika nataka kutoa amri zikusanywe kuni, kisha itolewe adhana kwa ajili ya swala, kisha nitoe amri mtu mmoja awe Imamu wetu, kisha (wakati huo wa swala) nitoke nikatie moto majumba ya wale wasiotoka kwa swala ya jamaa..." (Bukhari).*

Pia katika Hadithi nyingine,
*Abu Hurairah (r.a) amesimulia kuwa Mtume (s.a.w) kasema, "Kama si kwa sababu ya kuwepo watoto na wanawake katika nyumba, ningetaka nianze kuswalisha jamaa ya swala ya Isha na papo hapo kuwaamrisha vijana wachome moto nyumba zile watakazokuta humo watu" (Ahmad)*

*Abdullah bin Ummi Makhtuumi (r.a) aliuliza: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu Madina imejawa na wanyama wenye sumu na wanyama mwitu na mimi sioni (kipofu). Je, unanipa ruhusa ya (kuswali nyumbani)?" (Mtume) alimuuliza: Je, unasikia - Njoo kwenye swala, njoo kwenye kheri (yaani unasikia adhana)?" Ndio, alijibu (yule kipofu). Akasema (Mtume): Sasa kwanini usije (msikitini)? Kwa hiyo Mtume (s.a.w) hakumruhusu kuswali nyumbani. (Abu Daud, Nisai)*

Swala ya faradhi iliyoswaliwa katika jamaa ni bora zaidi mara 27 kuliko ile ya mtu peke yake kama tunavyojifunza katika Hadithi ifuatayo:

*Ibn Umar amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: Swala moja iliyoswaliwa katika jamaa malipo yake ni bora zaidi mara ishirini na saba (27) kwako kuliko malipo ya swala (hiyo hiyo) iliyoswaliwa bila ya jamaa". (Bukhari na Muslim).*

Swala ya jamaa huanza na watu wawili - Imamu (Mwenye kuswalisha) na Maamuma (Mwenye kuswalishwa), kama tunavyofahamishwa katika Hadithi ifuatayo:

*Abu Musa al-Ash-ariyyi amesimulia kuwa Mtume wa Allah*

*amesema: Wawili au zaidi ya hapo hufanya jamaa". (Ibn Majah).*

## Ruhusa kwa Wanawake Kuswali Jamaa Msikitini

Msisitizo wa kuswali swala za faradhi katika jamaa ya msikitini umewekwa kwa Waislamu wanaume. Kwa wanawake si lazima kwao kuswali jamaa msikitini lakini wakitaka kwenda msikitini wapewe ruhusa na waume zao au mawalii wao kutokana na kauli ya Mtume (s.a.w) ifuatayo:

*Ibn Umar (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah kasema: "Mke wa mmoja wenu atakapotaka ruhusa ya kwenda mskitini, hana budi kumruhusu" (Bukhari na Muslim).*

Lakini pamoja na ruhusa hii, Wanawake wa Kiislamu wanapotoka nje ya njumba zao kwenda msikitini au kwingineko hawana budi kujiheshimu kwa kujistiri ipasavyo na wasijipake manukato.

## Udhuru wa Kutoswali Jamaa Msikitini

Tumeona kuwa katika hali ya kawaida Muislamu mwanamume aliye karibu na msikiti kiasi cha kusikia adhana ni lazima mara tu asikiapo adhana aitikie wito na kwenda kujiunga na jamaa msikitini. Lakini kama tujuavyo, Uislamu ni dini ya wastani, yaani ni dini pekee inayozingatia hali halisi ya maisha ya kawaida ya mwanadamu na mazingira yake. Uwastani wa Dini ya Kiislamu, unaonekana katika kauli mbali mbali za Mtume (s.a.w) juu ya nyudhuru za kusamehewa kusali jamaa na kuruhusiwa kuswali nyumbani.

*Ibn Umar (r.a) amesimulia kuwa: Katika siku ya baridi kali na upepo aliadhini akasema, "Sikilizeni Swalini nyumbani mwenu". Baadaye alisema,"Mtume wa Allah alikuwa akimuelekeza muadhini katika usiku wa baridi na mvua kuwa aseme: Sikieni swalini nyumbani kwenu". (Bukhari na Muslim).*

*Ibn Umar (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah (s.a.w) amesema mmoja wenu atakapotengewa chakula (mezani) na wakati huo huo swala(ya jamaa) Ikaanza, naanze kula kwanza na asifanye haraka mpaka amalize kula. Na Ibn Umar alipotengewa chakula wakati swala inaanza, hakuja kwa swala (ya jamaa) mpaka alipomaliza kula, japo alikuwa akisikia Qur-an inasomwa na Imamu. (Bukhari na Muslim)*

*Aysha (r.a) ameeleza: Nimemsikia Mtume wa Allah (s.a.w) akisema: Hakuna swala wakati chakula kimetengwa (mezani) wala hapana swala wakati mtu amebanwa na haja ndogo (au kubwa). (Muslim)*

*Abdullah bin Arqama (r.a) amesimulia: Nimemsikia Mtume wa Allah (s.a.w) akisema: Iqama ikitolewa kwa kuanza swala, na kisha mmoja wenu akajisikia kubanwa na choo kikubwa au kidogo na akajisaidie kwanza. (Tirmidh)*

Kutokana na mafunzo ya Qur-an na Hadithi tunajifunza kuwa nyudhuru za kutoswali swala katika jamaa iliyowadia ni hizi zifuatazo:

(1) Machafuko ya hali ya hewa; mvua, baridi kali sana au jua kali sana.
(2) Wakati ukiwa na njaa na chakula kimeshatengwa mezani.
(3) Kushikwa na haja ndogo au kubwa.
(4) Kuwa mgonjwa au muuguzi.
(5) Kuwa na khofu ya kudhuriwa njiani.

## Inaruhusiwa kuswali swala moja mara mbili

Kwa sababu mbali mbali, mtu akiona haja ya kurudia swala ya faradhi anaweza kuswali tena. Kwa mfano, mtu akiwakuta watu wanaswali swala ya jamaa anashauriwa aifuate jamaa ile hata kama atakuwa amesha swali swala hiyo. Swala yake hii ya pili itakuwa ni Sunnah kwake na atapata ujira wake kamili. Tunafahamishwa katika hadithi ifuatayo:

*Yazid bin Amir (r.a) amesimulia: Nilikuja kwa Mtume (s.a.w) akiwa katika swala. Nilikaa bila ya kujiunga katika swala na wao. Mtume wa Allah alipomaliza kuswali aliniona nikiwa nimekaa pale akaniuliza: Ewe Yazid! Hujaukubali (hujaingia) Uislamu? 'Ndio Ewe, Mtume wa Allah, nimeukubali Uislamu. Akasema (Mtume (s.a.w)): Ni kitu gani kilichokuzuia kujiunga na watu katika swala yao? Alijibu: Nimeswali nyumbani kwangu, nafikiri swala hiyo hiyo mliyoiswali. Alisema (Mtume): "Unapokuja kwenye swala na ukawakuta watu wanaswali, swali nao japo utakuwa umeshaswali. Itakuwa ni Sunnah kwako na malipo yake yatadhibitiwa. (Abu Daud).*

## Namna ya Kuswali Katika Jamaa

Swala ya jamaa itakamilika iwapo masharti ya kuswali jamaa yatafuatwa ipasavyo. Ya muhimu katika swala ya jamaa ni kusimama inavyostahiki na kumfuata Imamu.

### 1. Jamaa ya watu wawili

Kama jamaa itakuwa ni ya watu wawili tu, Imamu na Maamuma basi Imamu atakuwa mbele na Maamuma atakuwa nyuma kidogo upande

wa kulia.





**Kielelezo:**

*Namna ambavyo inatakikana miguu ikutane katika jamaa ya watu wawili*

Pia Imamu anatakiwa asiwe mbali zaidi na Maamuma bali wawe katika usawa mmoja.



## 2. Jamaa ya Watu Watatu

Maamuma wakiwa wawili watasimama dhiraa moja nyuma ya Imamu katika mstari ulionyooka . Mmoja atakuwa sawa na imamu na mwingine atakuwa upande wa kulia.

### 3. Jamaa ya Watu Zaidi ya Watatu

Maamuma wakiwa watatu na kuendelea watasimama dhiraa moja nyuma ya Imamu katika mstari ulionyooka na kumfanya Imamu awe katikati. Wanaokuja baadaye kuunga jamaa watajaza mstari kulia na kushoto. Mstari mpya utajazwa kulia na kushoto kuanzia katikati usawa wa Imamu, dhiraa moja nyuma ya mstari wa kwanza.




**Kielelezo:**

*Jamaa ya watu zaidi ya watatu wakiwa nyuma ya Imam- dhiraa moja.*
*- Dhiraa ni kipimo cha mkono ulionyooshwa*

## Kusimama Katika Mistari

Mwenye kukimu anaposema, "*Qad-qaamatis-swalaa*" - swala iko tayari kusimamishwa: yawapasa Waislamu wasimame haraka haraka na kujiweka sawa na kunyoosha mistari huku wakiwa wamekaribiana kiasi cha kugusanisha mabega yao na vidole vyao vya miguu. Mtume (s.a.w) amesisitiza sana utaratibu huo kama tunavyojifunza katika Hadithi ifuatayo:-

*Anas (r.a) amesema: Iqama ilitolewa kwa ajili ya swala kisha Mtume wa Allah alitusogelea huku akiwa ametugeukia akasema: Nyoosheni mistari yenu na simameni bega kwa bega, kwa sababu ninawaona kwa nyuma (kama ninavyowaona kwa mbele).(Bukhari)*



***Kielelezo:*** *Namna ambavyo safu hunyoshwa kuzingatia mabega na vidole vya miguu kushikamana*



Pia katika simulizi nyingine iliyopokelewa na Imamu Bukhari na Muslim, Mtume (s.a.w) alisema:

> *"Nyoosheni mistari yenu, kwa sababu kunyoosha mistari ni sehemu ya kusimamisha swala". (Bukhari na Muslim)*

> *Anas (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah alikuwa akigeukia kulia na kusema: Kaeni sawa na nyoosheni mistari yenu kisha alikuwa akigeukia kushoto na kusema: Kaeni sawa na nyoosheni mistari yenu".*

Pia Mtume (s.a.w) pamoja na kusisitiza kunyoosha mistari, kukaribiana na kujaza nafasi, amefundisha na kusisitiza vile vile utaratibu wa ujazaji nafasi. Hebu tuangalie hadithi zifuatazo:

> *Abu Masud Ansari (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah (s.a.w) alikuwa akishika mabega yetu katika swala na kusema nyookeni (kaeni sawa) na msifarikiane, nyoyo zenu zisije zikafarikiana.Wale walio wazee na wenye hekima (elimu) na wasimame karibu yangu, kisha wafuate wanao wafuatia (kwa umri na elimu), kisha wafuatie wanaowafuatia hawa, Abu Mas'sud akasema leo utaratibu huu hamuufuati vilivyo. (Muslim).*

> *Abu Hurairah (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: Mstari ulio bora kwa Wanaume ni mstari wao wa mbele (karibu na Imamu), na mstari ulio mbaya (duni) kuliko yote ni mstari wao wa nyuma, na mstari ulio bora kuliko yote kwa Wanawake ni mstari wa nyuma na mstari ulio mbaya kwao kuliko yote ni mstari wao wa mbele (karibu na wanaume). (Muslim).*

*Abu Sa'd Al-Khudriyyi (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah aliona tabia ya baadhi ya Maswahaba wake kujirudisha nyuma, kwa hiyo aliwaambia njooni mbele na nifuateni na wale walio nyuma yenu wawafuate. Watu hawataacha kujiweka nyuma mpaka Allah awabakishe nyuma kabisa (Allah atawaweka nyuma wanaojiweka nyuma) (Muslim).*

Hadithi hizi zinatufahamisha kuwa mstari ulio bora kabisa unaostahiki ukimbiliwe kwa juhudi kubwa, kwa wanaume ni mstari wa mbele na kwa wanawake ni mstari wa nyuma. Mwenye kuwahi ndiye atakayestahiki kukaa mstari wa mbele. Pamoja na sifa hii ya kuwahi, sifa nyingine mbili za ukaaji katika mstari zimezingatiwa. Hizi ni sifa za elimu na umri. Watu wenye elimu na wazee watakaa mistari ya mbele karibu na Imamu na watoto watakaa mistari ya nyuma kwa upande wa wanaume. Utaratibu huu utakuwa kinyume chake kwa upande wa Wanawake.

### Kuswali na Wanawake Nyumbani katika Jamaa

Tunaposwali na familia zetu nyumbani, wanawake watakaa mstari wa nyuma. Hawatasimama mstari mmoja na Wanaume hata kama ni maharimu kama tunavyojifunza katika Hadithi zifuatazo:

*Anas(r.a) amesimulia, Mimi na Yati'in tuliswali katika nyumba ya Mtume (s.a.w) na Ummu Salaam aliswali nyuma yetu". (Muslim)*

*Pia Anas (r.a) amesimulia kuwa Mtume (s.a.w) aliswali pamoja naye na pamoja na Mama yake mdogo na amesema: (Mtume) alinisimamisha kuliani kwake na akamfanya yule mwanamke asimame nyuma yao". (Muslim).*

### Jamaa ya Wanawake Wenyewe

Wanawake wanalazimika kuswali kama wanaume maadam hawakuwepo katika hedhi au nifasi. Wanapokuwa katika hedhi au nifasi hawalazimiki kulipa swala walizoacha kuswali kwa sababu ya hedhi au nifasi.

Wanawake hawalazimiki kuadhini au kukimu lakini si vibaya iwapo wataadhini na kukimu. Wakiwa wengi, wawili au zaidi, watalazimika kuswali jamaa. Mmoja wao atakuwa Imamu lakini hatajitokeza mbele kama tunavyofahamishwa katika hadithi ifuatayo:

*Amesema Aisha (r.a) kuwa yeye (Aisha) alikuwa akiadhini na kuqimu na kuwaswalisha wanawake wenzake, lakini alikuwa akisimama nao katika safu ya mbele. (Baihaqi)*

**Kielelezo:**
*Namna ambayo Imam mwanamke anavyoongoza jamaa ya wanawake, huzidi mbele kidogo huku akiwa ndani ya safu moja.*



## Sifa za Imamu

Imamu ni kiongozi. Mtu yeyote mwenye sifa zifuatazo anaweza kuongoza swala:

1. Mwenye kuweza kuisoma Qur-an vizuri na mwenye kuielewa vizuri.
2. Anayefahamu na kuelewa vizuri hadithi na Sunnah.
3. Mwenye tabia njema na siha nzuri.
4. Mwenye umri mkubwa (sifa hizi zizingatiwe kwa mfuatano wake).

Kama itatokea kwenye msikiti mmoja kuna watu wengi wenye sifa hizi, itabidi ipigwe kura. Pia kiongozi au mtu mwenye mamlaka katika jamii atakuwa ndiye mwenye haki ya kuwa Imamu. Hali kadhalika mtu akiwa nyumbani kwake, atakuwa ndiye mwenye haki ya kuwa Imamu. Sifa hizi zinabainishwa katika Hadithi ifuatayo:

*Abu Mas'ud amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: Yule aliye na uwezo mkubwa zaidi wa kusoma Kitabu cha Allah (Qur-an) atakuwa Imamu wao. Kama watakuwa sawa kwa kusoma Qur-an basi atakuwa Imamu yule aliye na ujuzi mkubwa wa Hadithi, na kama wako sawa basi yule aliyetangulia kuhajiri (kuhama kutoka Makka kwenda Madina) na kama wako sawa katika kuhajiri, basi yule aliye na umri mkubwa kuliko wote ndiye atakayekuwa Imamu. Hakuna mtu atakaye kuwa Imamu wa yule aliyemzidi madaraka (au yule aliye na mamlaka juu yake) na wala hatakaa katika nyumba yake kwa kumpa heshima mpaka apate ridhaa yake. Na hakuna mtu atakayekuwa Imamu katika nyumba au familia ya mwingine. (Muslim).*

Imamu wa msikiti atakapochaguliwa hapatakuwa na mwingine

kuswalisha bila ruhusa yake. Ni vibaya mno kujipachika Uimamu mahali bila ya ridhaa ya watu unaowaongoza. Aliyejipachika Uimamu swala yake haitasihi.

*Ibn Umar amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema kuwa watu watatu ambao swala zao hazitakubaliwa ni: "Yule anayeswalisha watu na huku hawamtaki, anayekuja kwenye swala nyuma (kuja kwenye swala baada ya wakati kupita, pia kuswali mwenyewe nyuma ya mstari), na yule anayemfanya mwanamke huru kuwa mtumwa".(Abu Daud, Ibn Majah).*

Kumfuata Imamu baada ya kuwekwa ni jambo la lazima. Hata kama Imamu huyo atafanya makosa au dhambi kubwa kiasi gani kabla Waislamu hawajamtoa na kumweka mwingine itabidi lazima wamfuate kutokana na Hadithi ifuatayo:-

*Abu Hurairah (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah (s.a.w) amesema,"Jihadi ni wajibu chini ya Amir yeyote akiwa mcha-Mungu, au si mcha-Mungu na hata kama atakuwa amefanya madhambi makubwa, na swala ni wajibu nyuma ya kila Imamu akiwa mcha-Mungu au si mcha-Mungu na hata akiwa amefanya madhambi makubwa". (Abu Daudi)*

Inavyotakiwa, kama Imamu ataonekana kuwa anakiuka miiko ya Kiislamu kwa kutenda yale yaliyokatazwa katika Uislamu, kama vile zinaa, ulevi, wizi, n.k. itabidi Waislamu wamtoe kwenye Uimamu na kuweka Imamu mwingine mwenye sifa zilizotajwa. Kabla ya kuchagua mwingine watawajibika kumfuata Imamu huyo huyo muovu.Hekima yake ni kuepusha ugomvi, mifarakano baina ya waislamu.

### Kumfuata Imamu

Wanaoswalishwa (Maamuma) ni lazima wafuate amri ya Imamu na wasimtangulie Imamu kwa hali yoyote itakayokuwa. Msisitizo wa kumfuata Imamu vilivyo umewekwa bayana katika Hadithi zifuatazo:

*Anas (r.a) amesimulia. Mtume wa Allah siku moja aliwaongoza katika swala. Alipomaliza swala yake alitugeukia na kusema: "Enyi watu"Mimi ni Imamu wenu. Kwa hiyo msinitangulie katika kuinama (rukuu), wala katika kusujudu, wala katika kusimama wala katika kutoa salaam, kwa sababu ninakuoneni kwa mbele yangu na nyuma yangu" (Muslim).*

*Abu Hurairah (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: Usijaribu kumtangulia Imamu. Soma takbira (Allahu Akbar) baada yake, na sema, "Amiin" baada ya yeye kusema "Ghairil-magh'dhuubi a'layhim waladhwaaliin" na anaporukuu nawe rukuu na anaposema: "Sami'allaahu limanhamidah" sema: "Allahuma Rabbana lakal-hamdu".*

*(Bukhari na Muslim).*

*Anas (r.a) amesimulia: Mtume wa Allah alipanda farasi akaanguka na kuumia upande wake wa kulia. Aliswali swala mojawapo ya swala (tano) akiwa amekaa, nasi pia tuliswali tukiwa tumekaa nyuma yake. Alipomaliza kuswali alisema: Imamu amechaguliwa ili afuatwe. Akiswali akiwa amesimama, nanyi swalini mkiwa mmesimama, anaporukuu nanyi mrukuu anapoinuka (kuitidali) nanyi inukeni, anaposema,"Samia Llaahu limanhamidah", semeni "Rabbana lakal hamdu". (Bukhari)*

*Abu Hurairah (r.a) amehadithia kuwa Mtume wa Allah amesema, Je, haogopi yule anayetanguliza (anayeinua) kichwa chake mbele ya (kwa kumtangulia) Imamu.Haogopi kwamba, Allah atageuza kichwa chake kuwa kichwa cha punda? (Kwa maana nyingine kuwa na kichwa cha punda ni kuwa na kichwa kisicho na uwezo wa kufikiri kama kile cha punda). (Bukhari na Muslim).*

Hadithi zote hizi zinaonesha umuhimu wa kumfuata Imamu vilivyo katika swala za Jamaa. Funzo la ujumla tunalolipata hapa, ni kuwa kiongozi wa Kiislamu ni lazima atiiwe endapo atakuwa anatekeleza wajibu wake kulingana na mipaka ya Qur-an na Sunnah. Kuvunja amri ya kiongozi iliyo katika mipaka ya Qur-an na Sunnah ni kuvunja amri ya Allah na Mtume wake. Msisitizo huu wa kuwatii viongozi kwa mnasaba huu tunaupata katika Qur-an:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓا۟ أَطِيعُوا۟ ٱللَّهَ وَأَطِيعُوا۟ ٱلرَّسُولَ وَأُو۟لِى
ٱلْأَمْرِ مِنكُمْ ۖ فَإِن تَنَٰزَعْتُمْ فِى شَىْءٍ فَرُدُّوهُ إِلَى ٱللَّهِ وَٱلرَّسُولِ إِن
كُنتُمْ تُؤْمِنُونَ بِٱللَّهِ وَٱلْيَوْمِ ٱلْءَاخِرِ ۚ ذَٰلِكَ خَيْرٌ وَأَحْسَنُ تَأْوِيلًا ﴿٥٩﴾

*Enyi mlioamini, Mtiini Mwenyezi Mungu na mtiini Mtume na wenye mamlaka juu yenu, walio katika nyie (Waislamu wenzenu). Na kama mkikhitalifiana juu ya jambo lolote basi lirudisheni kwa Mwenyezi Mungu na Mtume, ikiwa mnamwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho. Hiyo ndiyo kheri, nayo ina matokeo bora kabisa. (4:59).*

**Je, Ni lazima Maamuma kurudia kusoma suratul Faatiha baada ya Imamu?**

Pamekuwa na kutofautiana watu juu ya maamuma kurudia kusoma suratul-Faatiha baada ya Imamu kusoma katika swala za kusoma kwa sauti. Baadhi ya watu wanasema ni lazima kurudia kusoma suratul-Fatiha kwa sababu ya Hadith ya Mtume (s.a.w) iliyosisitiza kuwa "*Hapana swala bila ya suratul-Faatiha*".

Kwa mujibu wa Qur-an na Sunnah hapana haja kwa maamuma kurudia tena kusoma suratul-Faatiha baada ya Imamu kusoma na wote wakaitikia "*aamin*" kwa hoja zifuatazo:

**Kwanza**, kitendo cha kuitikia "aamin" inaashiria kuwa Maamuma alishiriki kuisikiliza suratul-Faatiha wakati Imamu anasoma. Kama ilivyo katika kusoma dua za pamoja, mmoja kati yetu huongoza katika kusoma dua na wengine tuliobakia tunaitikia "aamin". Hivyo, kwa namna hii suratul-Faatiha itakuwa imepatikana kwa Imamu aliyesoma na kwa maamumah waliomsikiliza na kumfuatilia wakati anasoma, na kisha wote kwa pamoja wakaitikia "aamin".

**Pili**, ni amri ya Allah (s.w) kunyamaza na kuzingatia wakati Qur-an inasomwa:

وَإِذَا قُرِئَ ٱلْقُرْءَانُ فَٱسْتَمِعُوا۟ لَهُۥ وَأَنصِتُوا۟ لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ ﴿٢٠٤﴾

*"Na isomwapo Qur-an isikilizeni na nyamazeni ili mpate kurehemewa" (7:204).*

Kwa mujibu wa aya hii tunajifunza mambo mawili:

(1) Tunalazimika kuwa watulivu na kumfuatilia Imamu kwa makini wakati anasoma suratul-Faatiha.

(2) Ulazima wa kutulizana na kumsikiliza Imamu uko pale pale atakapokuwa anasoma sura au aya baada ya suratul-Faatiha. Hivyo kusoma suratul-Faatiha wakati Imamu anaendelea kusoma Qur-an baada ya suratul Faatiha ni kukhalifu amri ya Allah (s.w).

**Tatu**, kunyamaza kwa baadhi ya Maimamu ili kuwapa maamuma wasaa wa kusoma suratul-Faatiha, si utaratibu uliofuatwa na Mtume (s.a.w). Ni kweli kuwa, ni sunnah kutulia kidogo baada ya kusema "aamin" kabla ya kuanza kusoma sura au aya nyingine za Qur-an katika rakaa ya kwanza na ya pili kwa swala za kusoma kwa sauti, lakini si kimya kirefu kiasi cha kumaliza kusoma suratul-Faatiha kwa utulivu

na unyenyekevu.

**Nne**, kama suala ni maamuma kurudia kusoma suratul-Faatiha kwa kuwa Mtume (s.a.w) kasema *"Hapana swala bila suratul-Faatiha"*, mbona tunajua kutokana na hadithi sahihi kuwa rakaa hupatikana kwa kumkuta Imamu katika rukuu na kujituliza naye pale bila hata ya kuisikia hiyo suratul-Faatiha ikisomwa na imamu.

Hivyo kwa mujibu wa hoja hizi zilizojengwa juu ya msingi wa Qur-an na Sunnah, maamuma hahitaji kurudia suratul-Faatiha bali analazimika kunyamaza na kumsikiliza imamu kwa makini na kwa unyenyekevu wakati anaposoma surah hiyo na kisha kuitikia "aamin" baada ya kumaliza. Kisha maamuma ataendelea kumsikiliza imamu kwa makini na kwa unyenyekevu wakati akisoma sura au aya nyingine baada ya suratul-Faatiha.

Ama kwa swala au rakaa zile ambazo imamu anasoma kimyakimya, maamuma atalazimika kusoma suratul-Faatiha na sura au aya nyingine baada yake kwa kimya kimya kama anavyofanya katika kuleta visomo mbalimbali katika swala.

### Swala ya Ijumaa

Swala ya Ijumaa ni faradh inayosimamishwa siku ya Ijumaa badala ya swala ya Adhuhuri. Swala ya Ijumaa imefaradhishwa kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓا۟ إِذَا نُودِىَ لِلصَّلَوٰةِ مِن يَوْمِ ٱلْجُمُعَةِ فَٱسْعَوْا۟ إِلَىٰ ذِكْرِ ٱللَّهِ وَذَرُوا۟ ٱلْبَيْعَ ۚ ذَٰلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ إِن كُنتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٩﴾ فَإِذَا قُضِيَتِ ٱلصَّلَوٰةُ فَٱنتَشِرُوا۟ فِى ٱلْأَرْضِ وَٱبْتَغُوا۟ مِن فَضْلِ ٱللَّهِ وَٱذْكُرُوا۟ ٱللَّهَ كَثِيرًا لَّعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ﴿١٠﴾

*Enyi mlioamini! Kukiadhiniwa kwa ajili ya swala siku ya Ijumaa nendeni upesi kumtaja Mwenyezi Mungu na acheni biashara. Kufanya hivi ni bora kwenu ikiwa mnajua. Na itakapokwisha swala tawanyikeni katika ardhi mtafute fadhila za Mwenyezi Mungu na mkumbukeni Mwenyezi Mungu kwa wingi ili mpate kufaulu.(62:9-10)*

Pia faradhi ya Ijumaa inasisitizwa katika hadithi ifuatayo:

*Ibn Umar, (r.a) na Abu Hurairah (r.a) wamesikiwa wakisema: "Tumemsikia Mtume wa Allah akisema akiwa ulingoni (jukwaani): Watu wajiepushe na kutohudhuria swala ya Ijumaa, la sivyo Allah (s.w) atawapiga muhuri nyoyo zao, na kisha wakawa miongoni mwa wasioonyeka na wasiomkumbuka tena Allah (s.w). (Muslim).*

## Wanaolazimika Kuswali Swala ya Ijumaa

Wanaolazimika kuswali swala ya Ijumaa ni Waislamu wanaume waliomukalafu kama tunavyojifunza katika Hadithi ifuatayo:

*Twaariqi bin Shihaabi (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: "Ijumaa ni faradhi kwa kila Muislamu kwa kuiswali jamaa ila si faradhi kwa watu wanne" Watumwa (wafungwa), wanawake, watoto na wagonjwa".(Abu Daud).*

Kutokana na Hadithi hii tunajifunza kuwa swala ya Ijumaa ambayo ni lazima iswaliwe kwa jamaa ni faradhi kwa kila Muislamu mwanamume aliye balegh, muungwana na aliye mzima wa afya. Pia tunajifunza kuwa wanaoruhusiwa kuto swali swala ya Ijumaa ni hawa wafuatayo:

1. Wanawake.
2. Watoto wadogo.
3. Vikongwe na vilema.
4. Wagonjwa na wenye kuuguza wagonjwa.
5. Msafiri.
6. Kwa kuzuiliwa na hali ya hewa kama vile mvua, joto kali sana
7. Kuwa na khofu ya kudhuriwa njiani.

## Idadi ya Watu katika Jamaa ya Ijumaa

Kuhusu idadi ya watu inayokamilisha au inayotosheleza jamaa ya swala ya Ijumaa haikutajwa kabisa katika Qur-an wala katika Hadithi, ila tunaona katika Hadithi kuwa Mtume (s.a.w) alibakiwa na watu kumi na mbili tu wakati Maswahaba wake walipokimbilia msafara na kumuacha akiendelea kuhutubu. Hivyo, si jambo la busara kwetu kung'ang'ania kuwa ni lazima idadi maalum ya watu ifikiwe ndio swala ya Ijumaa iswihi. Kutokana na Hadithi ya Mtume (s.a.w) jamaa huanza na watu wawili - Imamu na Maamuma.

*Abu Mussa al-Ash'ariyyi ameeleza kuwa Mtume wa Allah (s.a.w) amesema: "Wawili au zaidi ya wawili hufanya jamaa". (Ibn Majah).*

Maimamu wa 'Fiqhi' wametofautiana juu ya idadi ya watu wanaotosheleza jamaa ya swala ya Ijumaa. Imamu Abu Hanifa na Ahmad bin Hambal wametoa rai kuwa jamaa inakamilishwa na watu watatu na Imamu wa nne. Imamu Abuu Yusufu yeye amesema jamaa ya Ijumaa inatoshelezwa na watu wawili na Imamu wa tatu. Ambapo Imamu Shafii anasema kuwa Jamaa ya swala ya Ijumaa inatoshelezwa na watu arubaini (40) wakazi wa mji. Kwa ujumla utaona kuwa maoni ya Maimamu watatu - Abu Hanifa, Ahmad na Abuu Yusuf, yanakaribiana sana, na kiwango cha chini cha jamaa alichokitaja Mtume (s.a.w) katika hadithi iliyotangulia. Imamu Shafii yuko mbali sana na kiwango hicho. Jambo muhimu la kuzingatia ni kwamba, kinachotakiwa tukifuate moja kwa moja ni Qur-an na Sunnah ya Mtume, na mawazo ya yeyote yule mwingine hatulazimiki, kwa namna yoyote ile iwayo, kuyafuata mpaka kwanza tuyaingize kwenye kipimo (kigezo) cha Qur-an na Sunnah.

### Namna ya kutekeleza swala ya Ijumaa

Swala ya Ijumaa ina tanguliwa na adhana mbili. Adhana ya kwanza ni wito wa kuwatanabahisha watu wafunge shughuli zote za kawaida kwa ajili ya swala ya Ijumaa. Adhana hii kwa kawaida inakuwa kabla ya wakati wa swala kuingia. Adhana ya pili ya Ijumaa inatolewa wakati inapoingia swala ya adhuhuri. Baada ya adhana ya pili khatibu husimama mimbarini au ulingoni na kuanza kutoa khutuba huku akiwa amewaelekea watu. Wakati wa Mtume (s.a.w) na Ukhalifa wa Abubakr na 'Umar adhana ya Ijumaa ilikuwa moja tu, ya wakati wa kwanza khutuba. Adhana ya nyongeza ambayo ndiyo adhana ya kwanza ilianzishwa wakati wa ukhalifa wa 'Uthman bin Affan.

Swala ya Ijumaa inatanguliwa na khutuba mbili zinazotolewa na khatibu wenigne wote wakiwa wasikilizaji. Baada ya khutuba, swala ya ijumaa hukamilika kwa kuswali rakaa mbili kwa jamaa.

### Khutuba ya Ijumaa

Khutuba ni jambo lililosisitizwa sana siku ya Ijumaa. Khutuba hii imegawanyika katika sehemu mbili zinazotenganishwa na kikao cha muda mfupi. Hivi ndivyo alivyokuwa akifanya Mtume (s.a.w) kama inavyodhihiri katika hadithi ifuatayo:

> *Jabir bin Samurat (r.a) amesimulia kuwa Mtume (s.a.w) alikuwa akitoa khutuba mbili, na katika khutuba hizo alikuwa akisoma Qur-an na kuwaonya na kuwausia watu. Swala yake ilikuwa fupi kiasi na khutuba yake pia ilikuwa fupi kiasi." (Muslim).*

Lengo la khutuba ni kuwausia, kuwatanabahisha na kuwakumbusha, Waislamu juu ya wajibu wao kwa Allah (s.w) na viumbe vyake na juu ya lengo lao la maisha kwa ujumla na namna ya kulifikia. Hivyo ili khutuba ifikie lengo lake, hapana budi itolewe kwa lugha ya wale wanaohutubiwa. Lengo la khutuba na lengo kuu la swala ya Ijumaa kwa ujumla halitapatikana iwapo khutuba itatolewa katika lugha isiyoeleweka kwa wasikilizaji.

Khutuba ya Ijumaa inatimia kwa kutimiza nguzo tano zifuatazo:

1. Kumshukuru au kumhimidi Allah kwa kusema: Al-hamdulillaah...
2. Kumtakia Rehma Mtume (s.a.w).
3. Kuwausia Waislamu kumcha Mungu au kuwapa mawaidha juu ya Uislamu.
4. Kusoma Qur-an angalau aya moja.
5. Kuwaombea Waislamu dua.

Khatibu ni sharti awe na udhu na akhutubu akiwa amesimama na kuwaelekea anao wakhutubia. Pia kulingana na Sunnah ya Mtume (s.a.w) ni vyema khutuba isiwe ndefu sana kama Mtume (s.a.w) alivyoshauri katika kauli yake ifuatayo:

*Ammar (a.r) amesimulia kuwa alimsikia Mtume (s.a.w) akisema: Urefu wa swala ya mtu na ufupi wa khutuba yake ni alama ya kuwa na hekima. Kwa hiyo refusha swala na fupisha khutuba kwani kuna dawa katika kukhutubu. (Muslim).*

## Swala ya Ijumaa

Baada ya khutuba mbili, swala hukimiwa kama kawaida na Imamu kuswalisha rakaa mbili za swala ya Ijumaa kwa sauti. Baada ya kusoma suratul Fatiha, Imamu anaweza kusoma sura yoyote lakini kutokana na hadithi nyingi za Mtume (s.a.w), ni sunnah katika rakaa ya kwanza kusoma Suratul Jumua (sura ya 62) na katika rakaa ya pili kusoma sura ya 63 Al-Munafiquun kama tunavyofahamishwa katika hadithi ifuatayo:

*Ibn Abbas (r.a)amesimulia kuwa Mtume wa Allah (s.a.w) alikuwa akisoma katika swala ya Al-fajir ya siku ya Ijumaa sura ya 32 - As-sajda na sura ya 76 - Ad-dahr na alikuwa akisoma suratul Jumua na Suratul-Munaafiquuna. (Muslim).*

*Nuuman bin Bashir (r.a) amehadithia kuwa Mtume (s.a.w) alikuwa*

*akisoma katika swala za Iddi mbili na swala ya Ijumaa suratul A'ala (87) na suratul Ghashiyah (88). Na kama imesadifu kuwa siku ya Idi ndio siku ya Ijumaa, basi alikuwa akisoma sura mbili hizi katika swala zote, yaani ya Idi naya Ijumaa. (Muslim).*

Baada ya swala ya Ijumaa na swala nyingine yoyote ya jamaa Waislamu wanashauriwa wasambae katika ardhi kutafuta fadhila za Allah huku wakimkumbuka kwa kuchunga barabara mipaka aliyoiweka ambayo iko wazi. Rejea Qur'an (62:10)

## Kusimamisha Swala za Sunnah

Baada ya Swala tano za faradhi, kuna swala nyingine za nyongeza alizozisimamisha Mtume (s.a.w) na akatuagiza nasi tumuigize. Swala hizi za ziada tunaziita Swala za Sunnah (Nawafil).

Lengo la Swala za sunnah ni lile lile la swala za faradhi la kututakasa na mambo maovu na machafu. Ni muhimu kwa kila Muislamu kudumisha hizi swala za Sunnah kwa sababu zifuatazo:

1. Kusimamisha Swala za Sunnah ni katika kumtii na kumuigiza Mtume (s.a.w), jambo ambalo ametuamrisha Allah (s.w) katika Qur-an:

لَّقَدْ كَانَ لَكُمْ فِى رَسُولِ ٱللَّهِ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ لِّمَن كَانَ يَرْجُوا۟ ٱللَّهَ وَٱلْيَوْمَ ٱلْءَاخِرَ وَذَكَرَ ٱللَّهَ كَثِيرًا ﴿٢١﴾

*"Hakika mna kiigizo chema kwa Mtume wa Allah kwa mwenye kumuogopa Allah na siku ya malipo na mwenye kumkumbuka sana Allah". (33:21)*

قُلْ إِن كُنتُمْ تُحِبُّونَ ٱللَّهَ فَٱتَّبِعُونِى يُحْبِبْكُمُ ٱللَّهُ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ وَٱللَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٣١﴾

*"Sema: Ikiwa nyinyi mnampenda Allah basi nifuateni (hapo) Allah atakupendeni na atakughufirieni madhambi yenu. Na Allah ni Mwenye maghfira Mwenye Rahma". (3:31)*

2. Kusimamisha swala za sunnah kutatupelekea kufikia ucha Mungu kwa wepesi.

3. Swala za Sunnah pia zina kazi ya kujaziliza swala za faradhi ambazo kwa sababu ya udhaifu wa kibinaadamu hazikuswaliwa kwa ukamilifu unaostahiki.Kama tunavyojifunza katika Hadithi zifuatazo.

*Imesimuliwa na Abu Hurairah (r.a) kuwa Mtume wa Allah amesema: Amali ya kwanza atakayoulizwa mtu siku ya Kiyama (siku ya Hukumu) ni Swala. Swala zake zikiwa zimekamilika atafuzu. Swala zake zikiwa pungufu atafeli na kuhasirika. Kama swala zake za faradhi zitakuwa zimepungua, Allah (s.w) atasema angalia kwa mja wangu kama anaswala za ziada (Swala za Sunnah) ili zichukuliwe kujazia sehemu iliyopungua katika swala za faradhi. Kisha ndio vitendo vyake vingine vitaangaliwa kwa namna hiyo hiyo". (Tirmidh, Abu Daud, An-Nasai, Ibn Majah na Ahmad).*

Swala za Sunnah ni nyingi. Muislamu anatakiwa, kila atakapohisi kuhitajia msaada wa Allah (s.w) atatawadha na kuswali kwani Allah (s.w) anatuagiza:

وَٱسْتَعِينُوا۟ بِٱلصَّبْرِ وَٱلصَّلَوٰةِ ۚ وَإِنَّهَا لَكَبِيرَةٌ إِلَّا عَلَى ٱلْخَٰشِعِينَ

﴿٤٥﴾ ٱلَّذِينَ يَظُنُّونَ أَنَّهُم مُّلَٰقُوا۟ رَبِّهِمْ وَأَنَّهُمْ إِلَيْهِ رَٰجِعُونَ ﴿٤٦﴾

*"Jisaidieni (katika mambo yenu) kwa kusubiri na kuswali, na kwa hakika jambo hilo ni gumu isipokuwa kwa wanyenyekevu. Ambao wana yakini ya kwamba watakutana na Mola wao na watarejea kwake". (2:45-46)*

Hata hivyo katika kitabu hiki tutajihusisha na Swala maalum za Sunnah zifuatazo:

**1. Swala ya Maamkizi ya Msikiti**

Muislamu anapoingia Msikitini kabla hajakaa anatakiwa aswali rakaa mbili za maamkizi ya msikiti, Tahiyyatul-Masjid.

**2. Swala za Qabliyyah na Ba'adiyah**

Swala hizi za Sunnah huswaliwa kabla na baada ya swala za faradhi. Swala hizi zimegawanyika katika mafungu mawili, zile zilizokokotezwa sana, Mu'akkadah na zile ambazo hazikukokotezwa sana, Ghairu Mu'akkadah.

Sunnah ambazo ni Mu'akkadah ni zile ambazo Mtume (s.a.w)

hakuacha kuzitekeleza hata mara moja katika hali ya kawaida. Ghairu Mu'akkdah ni zile sunnah ambazo wakati mwingine Mtume (s.a.w) aliacha kuzitekeleza. Swala za Sunnah za Qabliyyah na Baadiyah zilikokotezwa (zilizo Mu'akkadah) na zisizo kokotezwa (zilizo Ghairu-Mu'akkadah) zimebainishwa katika jedwali ifuatayo ikiwa ni pamoja na idadi ya rakaa ya swala hizo:-

| SWALA ZA FARADHI | RAKAA ZA SUNNA YA QABLIYYA | | RAKAA ZA SUNNA YA BAADIYYA | |
|---|---|---|---|---|
| | MK | GMK | MK | GMK |
| Al-fajiri | 2 | hamna | hamna | hamna |
| Adhuhuri na Ijumaa | 4 | 2 | 2 | 2 |
| Al-'asiri | hamna | 4 | hamna | hamna |
| Magharibi | hamna | 2 | 2 | hamna |
| Al-ishaa | hamna | 2 | 2 | hamna |

**Ufungo: MK= Muakkadah, GMK= Ghairu Muakkadah**

### 3. Swala ya Witri

Witri maana yake ni namba isiyogawanyika kwa mbili kama vile 1, 3, 5, 7, 9, 11 n.k. Sunnah ya witri huswaliwa katika kipindi cha usiku baada ya swala ya Al-Isha na kabla ya kuingia swala ya Al-Fajiri. Lakini ni bora kuicheleweshа Witri na kuiswali katika theluthi ya mwisho ya usiku, baada ya swala ya kisimamo (tahajjud).

Mtume (s.a.w) alikuwa akiswali Witri pamoja na swala ya Tahajjud (Swala ya Usiku) na wakati mwingine alikuwa akiswali Witri mara tu baada ya Al-Ishaai. Ni vema kuswali witri baada ya al-Isha kama hakuna uhakika wa kuamka Usiku. Mtume (s.a.w) ameikokoteza sana swala ya Witri kama tunavyojifunza katika hadithi ifuatayo:

*Buraydah (r.a) amesimulia, Nimemsikia Mtume (s.a.w) akisema; Witri ni haq (wajibu). Asiyeswali si miongoni mwetu. Witri ni wajibu". (Abu Daudi)*

Witri ina swaliwa kwa rakaa tatu. Huswaliwa kwa rakaa mbili na kutoa Salaam, kisha hukamilishwa na rakaa moja.

## Namna ya Kuswali Swala ya Witri

1. Katika rakaa ya kwanza utasoma Sura ya Al-A'alaa (Sabbihisma) baada ya Suratul-Faatiha.

2. Katika rakaa ya pili utasoma Suratul-Qaafiruuna baada ya suratul-faatiha..
3. Katika rakaa moja ya mwisho, baada ya kusoma Suratul-Faatiha, utasoma Suratul-Ikhlas, Al-Falaq na An-naas.
4. Kuleta Qunut (dua) katika rakaa ya mwisho katika Itidali. Dua tunayoileta katika Qunut ni hii ifuatayo:



***Allahumma ihdnii fiiman-hadaita***
*Ewe Mola niongoze kama wale uliowaongoza*



***Wa 'aafinii fiiman 'aafaita***
*Na uninusuru kama hao uliowanusuru*

وَتَوَلَّنِي فِيمَنْ تَوَلَّيْتَ

***Watawallanii fiiman tawallaita***
*Na unilinde pamoja na wale uliowalinda*



***Wabaarik lii*** وَبَارِكْ لِي فِيمَا أَعْطَيْتَ
*Unitilie baraka katika haya uliyonipa*

***Waqinii sharra maa qadhwaita***
*Unikinge na shari ulizonikadiria*

***Fainnaka taq-dhwii walaa yuq-dhwaa 'alaika***
*Kwa hakika wewe ndiwe Mwenye kunusuru, wala hakuna anayenusuru isipokuwa Wewe*



***Innahu laa yadhillu man waalaita***
*Hakika hadhaliliki uliyemtukuza*

***Tabaarakta rabbanaa wata'aalaita***
*Ni nyingi kabisa juu yetu baraka zako na umetukuka kweli kweli,*

Ni muafaka kuleta dua nyinginezo vile vile kulingana na haja ya mwenye kuswali.

## 4. Swala ya Tahajjud

Swala ya Tahajjud ni miongoni mwa swala zilizokokotezwa sana katika Qur-an na Hadithi. Neno "*Tahajjud*" lina maana ya kuamka kutoka usingizini. Swala hii huswaliwa usiku wa manane, hasa katika theluthi ya mwisho wa usiku karibu na al-Fajiri.

Swala hii vile vile hujulikana kwa jina la "*Qiyaamul-layl*". Yaani kisimamo cha usiku kwa sababu inakuwa na visimamo virefu ambapo Qur-an husomwa kwa urefu. Mkokotezo wa swala ya Tahajjud unadhihirika katika aya za Qur-an zifuatazo:

وَمِنَ ٱلَّيْلِ فَتَهَجَّدْ بِهِۦ نَافِلَةً لَّكَ عَسَىٰٓ أَن يَبْعَثَكَ رَبُّكَ مَقَامًا مَّحْمُودًا

*Na katika usiku jiondoshee usingizi (kidogo) kwa (kusoma) hiyo (Qur-an ndani ya Swala).Hiyo ni (Ibada) zaidi kwako. Huwenda Mola wako akakuinua cheo kinachosifika. (17:79).*

Miongoni mwa sifa za waja wema wa Allah (s.w) ni pamoja:

وَٱلَّذِينَ يَبِيتُونَ لِرَبِّهِمْ سُجَّدًا وَقِيَٰمًا ﴿٦٤﴾

*"Na wale wanaopitisha baadhi ya saa za usiku kwa ajili ya Mola wao kwa kusujudu na kusimama". (25:64).*

*Je,*

أَمَّنْ هُوَ قَٰنِتٌ ءَانَآءَ ٱلَّيْلِ سَاجِدًا وَقَآئِمًا يَحْذَرُ ٱلْءَاخِرَةَ وَيَرْجُوا۟
رَحْمَةَ رَبِّهِۦ ۗ قُلْ هَلْ يَسْتَوِى ٱلَّذِينَ يَعْلَمُونَ وَٱلَّذِينَ لَا يَعْلَمُونَ ۗ
إِنَّمَا يَتَذَكَّرُ أُو۟لُوا۟ ٱلْأَلْبَٰبِ ﴿٩﴾

*afanyaye ibada nyakati za usiku kwa kusujudu na kusimama na kuogopa Akhera na kutarajia rehema ya Mola wake (ni sawa na asiyefanya hayo)? Sema: "Je, wanaweza kuwa sawa wale wanaojua na wale wasiojua?" Wanaotanabahi ni wale wenye akili tu. (39:9)*

Pia Mtume (s.a.w) amekokoteza Swala za Usiku kama tunavyojifunza katika Hadith ifuatayo.

> *Abu Umamah (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: Jizoesheni kusimama Usiku (kwa swala) kwa sababu ilikuwa ndio tabia ya Wacha-Mungu waliokutangulieni na ni njia ya kukukurubisheni karibu na Mola wenu na ni njia ya kufutiwa dhambi na ni kizuizi cha kutenda maovu (dhambi)". (Tirmidh).*

Idadi ya rakaa alizoswali Mtume (s.a.w) katika hii swala ya Tahajjudi ni nane (8) na kisha akamalizia na rakaa tatu za Witri. Katika hizi rakaa nane alitoa salam kila baada ya rakaa mbili. Mtume (s.a.w) alikuwa akisoma Qur-an kwa kitambo kirefu kwa kila rakaa kiasi kwamba miguu yake ilikuwa inavimba kama tunavyojifunza katika Hadithi ifuatayo:-

> *"Mughirah (r.a) ameeleza kuwa Mtume (s.a.w) alikuwa akisimama katika (swala ya usiku) kwa kitambo kirefu kiasi kwamba miguu yake ilivimba, akaulizwa: Kwanini unafanya hivi ambapo umesamehewa dhambi zako zilizotangulia na zitakazokuja? Akauliza: "Nisiwe mja mwenye Shukrani?" (Bukhari na Muslim).*

### 5. Swala ya Tarawehe

Swala ya Tarawehe ni miongoni mwa Sunnah zilizokokotezwa. Swala hii huswaliwa katika mwezi wa Ramadhan tu wakati wowote kati ya kipindi baada ya swala ya Isha na kuingia kwa swala ya Alfajiri. Umuhimu wa swala hii umedhihiri katika Hadithi ifuatayo:

> *Abu Hurairah (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah alikuwa akisisitiza swala ya usiku katika mwezi wa kufunga (Ramadhani), bila ya kuifaradhisha kwao. Alikuwa akisema: Atakaye swali katika usiku wa mwezi wa kufunga, akiwa na imani na akitarajia malipo (kutoka kwa Allah (s.w), dhambi zake zilizotangulia husamehewa. (Muslim)*

Mtume (s.a.w) alikuwa akiswali Tarawehe katika sehemu ya pili ya usiku (katika wakati ule ule wa Tahajjud). Mtume (s.a.w) aliswali Tarawehe pamoja na masahaba katika jamaa siku tatu, kisha akaacha na akawa anaswalia nyumbani kwake kama tunavyofahamishwa katika Hadithi ifuatayo:

> *'Aysha (r.a) amesimulia kuwa Mtume (s.a.w) alikwenda msikitini usiku na akaswalisha Tarawehe na watu wakaswali naye. Asubuhi watu wakasimuliana habari hiyo. Mtume (s.a.w) siku ya pili alikwenda kuswalisha watu wakajaa msikitini. Alifanya hivyo hivyo siku ya tatu. Asubuhi siku ya nne watu wakapeana habari na wakajazana zaidi msikitini kwa ajili ya swala ya Tarawehe lakini Mtume (s.a.w) hakwenda*

*kuswalisha. Baadhi ya watu walisema kwa sauti "swalah", lakini Mtume (s.a.w) hakwenda msikitini mpaka Alfajir. Alipomaliza swala ya Alfajir aliwakabili watu na kuwaeleza: "Jambo lenu halikuwa limefichikana kwangu, lakini nilichelea kuwa kama ningaliendelea mfululizo na swala hiyo ya Tarawehe huenda ingalifanywa kuwa ni faradhi kwenu na huenda mungalishindwa kuitekeleza". (Muslim)*

Pamoja na Hadithi hii, pia Mtume (s.a.w) aliwasisitiza Waislamu kuswali swala za Sunnah majumbani mwao na kuwahakikishia kuwa kufanya hivyo kuna malipo makubwa zaidi. Swala ya Tarawehe iliendelea kuswaliwa na kila mtu nyumbani kwake katika kipindi chote cha Mtume (s.a.w) na kipindi cha Khalifa wake wa kwanza (Abu Bakar). Khalifa wa pili, Umar bin Khattab, alianzisha tena kuswali swala ya Tarawehe kwa jamaa msikitini kama inavyoendelea mpaka hivi leo.

**Idadi ya Rakaa za Swala ya Tarawehe**

Kumekuwepo na maelezo tofauti kuhusiana na idadi ya rakaa za Swala ya tarawehe kutoka kwa wanazuoni tofauti. Lakini kutokana na Hadithi iliyosimuliwa na Mama Aysha (r.a) na kupokelewa na Maimamu wa Hadithi, Mtume (s.a.w) hakupata kuswali zaidi ya rakaa 11 katika mwezi wowote ule. Hadithi ya Jabir (r.a) iliyopokelewa na Ibnu Khuzaimah na Ib n Hibban, Mtume ameripotiwa kuswali rakaa nane za tarawehe na rakaa tatu za witri pamoja na Masahaba wake na kisha siku iliyofuatia akawa hakutoka kwenda kusalisha.

Ama kuhusiana na kuswali rakaa ishirini, ni kweli kuwa Khalifa Umar, Uthman na Ali (r.a) waliswali kwa rakaa hizo. Imamu Ibnu Hibban amesema kuwa mwanzoni ilikuwa ni rakaa kumi na moja isipokuwa kisomo (kisimamo) kilikuwa kirefu kiasi cha watu kuchoka. Hivyo baadaye ikaamuliwa kuwa idadi ya rakaa iongezwe na kisomo kipunguzwe na kuwa cha wastani ingawaje jambo hili halikuingiza Swala ya Witri, kutoka hapo kwenye rakaa 20 ilifika kwa badhi ya wengine akiwemo Imamu Malik hadi rakaa 36 ikiwa kisomo kimezidi kufupishwa. Iliyo sunnah ni kuswali tarawehe kwa rakaa 11-8 za kisimamo cha usiku cha kawaida na rakaa 3 za witri. Kwa kuwa mwezi wa Ramadhani ni mwezi wa Qur-an inahimizwa sana kuwa Waislamu wahitimishe Qur-an yote alau kwa kusoma juzuu moja kila siku. Tarawehe ni swala sawa na swala nyingine hivyo kusihi kwake kunafungamana na kupatikana khushui, masharti na nguzo zote za swala. Ama hizi tarawehe zinazoswaliwa katika misikiti mingi mbazo Imamu hupata sifa kwa kuswali mbio mbio pasipo na mazingatio wala utulivu ni kinyume kabisa

na utaratibu wa swala. Watu wengi ambao huharakisha kumaliza swala ya tarawehe kwa kiasi cha kutokamilisha nguzo za swala hawapati malipo yoyote kutokana na swala zao. Bali kwa kuwa watu hawa wanaifanyia swala mchezo hapana cha kutarajia zaidi ya adhabu kali waliyoahidiwa na Allah (s.w):

فَوَيْلٌ لِّلْمُصَلِّينَ ﴿٤﴾ الَّذِينَ هُمْ عَن صَلَاتِهِمْ سَاهُونَ ﴿٥﴾

*"Basi adhabu itawathibitikia wanao swali, ambao wanapuuza swala zao". (107:4-5)*

## 6. Swala ya Idil-Fitri na Idil-Hajj

Iddil-Fitri na Iddil-Hajj ni swala za Sunnah zilizokokotezwa. Iddi hizi mbili zinazofahamika vyema kwa Waislamu kuwa ni vilele vya siku mbili baada ya kukamilisha nguzo ya Funga na Hajj. Kielelezo cha kilele cha sherehe katika Uislamu si ngoma wala tarumbeta, wala si kula na kunywa sana, bali ni kumkumbuka Allah (s.w) na kumtaja kwa wingi.

Swala ya Idd inaswaliwa baada ya jua kuchomoza na kabla ya jua kufika katikati. Ina rakaa mbili na khutuba kama swala ya Ijumaa lakini tofauti na Ijumaa, khutuba hufuatia baada ya swala. Kama ilivyo swala ya Ijumaa, swala za Idd mbili ni swala za jamaa. Ni sunnah kuswalia Idd uwanjani ili kukusanya jamaa kubwa zaidi.

## Swala ya Idd ikiangukia Ijumaa

Mtume (s.a.w) ametoa ruhusa ya kutoswali swala ya Ijumaa iwapo itakuwa imeswaliwa swala ya Idd iliyoangukia siku ya Ijumaa kwa mujibu wa Hadithi zifuatazo:-

*Zaid bin Arqam (r.a) ameeleza kuwa Mtume (s.a.w) aliswalisha Idd kisha akatoa ruhusa kwa swala ya Ijumaa, akasema: "Anayetaka kuswali na aswali". (Vitabu Vitano vya Hadith).*

*Abu Hurairah (r.a) amesimulia kuwa Mtume (s.a.w) amesema: Katika siku yenu hii ya leo zimekutana Idd mbili (yaani Idd na Ijumaa)basi anayetaka asiswali Ijumaa (swala ya Idd inatosheleza) lakini sisi tutaswali Ijumaa". (Abu Daud).*

Kutokana na Hadithi hii ya mwisho, hii ni ruhusa tu na ni bora kuswali Iddi na Ijumaa kwani Mtume mwenyewe alifanya hivyo.

## 7. Swalatudh-Dhuhaa

Swala ya Dhuhaa ni sunnah inayoswaliwa kati ya kipindi cha baada ya jua kupanda juu kiasi cha mita tatu hivi na kabla ya jua kufikia katikati. Lakini ni bora kuswali katikati ya kipindi hicho.

Swala hii inaswaliwa kwa rakaa mbili mbili hadi zitimie nane, lakini kwa uchache unaweza kuswali rakaa mbili tu na pia unaweza kuswali zaidi ya rakaa nane.

Umuhimu wa swala ya Dhuhaa uko wazi. Kipindi kati ya swala ya Alfajir na Dhuhuri ni kirefu sana kiasi kwamba mja anaweza kusahau kumkumbuka na kumtaja Allah (s.w). Kama tunavyofahamu kumkumbuka Allah (s.w) kila wakati ndio ngao pekee ya kumzuia mja na mambo maovu na machafu. Hivyo Swalatudh-Dhuhaa kwa mtu mwenye wasaa katika kipindi hicho cha harakati nyingi za kutafuta riziki, itampa msukumo mpya wa kumkumbuka na kumuabudu Allah ipasavyo.

*Kutokana na hadith iliyopokelewa na Abu Daud na Ahmad, Buraidah (r.a) amesema kuwa Mtume (s.a.w) amesema: "Katika mwili wa binaadam kuna viungo (joints) 360 na binaadam ni lazima akitolee sadaka kila kiungo kimoja". Watu wakauliza:"Nani awezaye kufanya hivyo ewe Mjumbe wa Allah?"Mtume akawajibu: "Mtu anaweza kufanya hivyo kwa kuondosha kitu chenye madhara njiani. Na iwapo hatoweza, kufanya hivyo basi rakaa mbili za Dhuhaa zitamtosheleza".*

## 8. Swalatul-Istikharah

Istikharah kilugha ni kuomba jambo lolote zuri. Kwa hiyo swalatul-Istikharah ni swala ya kuomba uongozi wa Allah (s.w) juu ya uamuzi wa jambo.

*Jabir (r.a) amesimulia: Mtume (s.a.w) alikuwa akitufundisha kufanya Istikharah katika uamuzi wa mambo yetu yote kama alivyokuwa akitufundisha sura za Qur-an.Alikuwa akisema:"Mmoja wenu atakapokusudia kufanya jambo lolote, na aswali rakaa mbili mbali na swala za faradhi kisha baada ya swala hiyo asome dua ifuatayo:*

اللّهُمَّ إِنِّي أَسْتَخِيرُكَ
بِعِلْمِكَ وَأَسْتَقْدِرُكَ بِقُدْرَتِكَ
وَأَسْأَلُكَ مِنْ فَضْلِكَ الْعَظِيمِ

*Ewe Mwenyezi Mungu! Ninakuomba unijaalie yaliyo mazuri kutokana na ujuzi wako, uwezo wako na nguvu zako, hakika wewe ndiye mwenye nguvu, mimi sina, Wewe ndiye mjuzi wa mambo ya ghaibu (ya siri). Ewe Mwenyezi Mungu, ikiwa kutokana na ujuzi wako*

فَإِنَّكَ تَقْدِرُ وَلَا أَقْدِرُ وَتَعْلَمُ وَلَا أَعْلَمُ وَأَنْتَ عَلَّامُ الْغُيُوبِ.
اَللّٰهُمَّ إِنْ كُنْتَ تَعْلَمُ أَنَّ هٰذَا الْأَمْرَ خَيْرٌ لِي فِي دِينِي وَمَعَاشِي وَعَاقِبَةِ أَمْرِي أَوْ عَاجِلِ أَمْرِي وَآجِلِهِ فَاقْدُرْهُ لِي وَيَسِّرْهُ لِي ثُمَّ بَارِكْ لِي فِيهِ.

وَإِنْ كُنْتَ تَعْلَمُ أَنَّ هٰذَا الْأَمْرَ شَرٌّ لِي فِي دِينِي وَمَعَاشِي وَعَاقِبَةِ أَمْرِي أَوْ فِي عَاجِلِ أَمْرِي وَآجِلِهِ فَاصْرِفْهُ عَنِّي وَاصْرِفْنِي عَنْهُ وَاقْدُرْ لِيَ الْخَيْرَ حَيْثُ كَانَ ثُمَّ أَرْضِنِي بِهِ.

*jambo hili (litaje jambo lenyewe) ni zuri (jema) kwa imani (dini) yangu na kwa maisha (maslahi) yangu katika mwanzo wake na mwisho wake,basi nijaalie kulipata na nirahisishie (ulifanye liwe jepesi kwangu) na ulitilie baraka zako. Lakini, ikiwa kwa ujuzi wako jambo hili ni baya (au litakuwa baya) kwa imani (dini) yangu na maisha yangu katika mwanzo wake na mwisho wake, basi nakuomba uniepushe nalo na unijaalie kupata jingine lililo bora na unifanye niridhike nalo". (Bukhari).*

Swala hii pamoja na dua yake inamfundisha Muislamu kumtegemea Allah (s.w) katika kila jambo na kila hali. Mtu atakapofanikiwa katika hilo alililoomba hatatakabari kwani ana uhakika asilimia mia kuwa hakulipata kwa juhudi au uwezo wake bali ni Allah (s.w) aliyemuwezesha kulipata. Pia Muislamu atakapokosa kitu alichokihitajia, hatasononeka kwani ana uhakika asilimia mia kuwa kukosa kitu hicho ndio kheri kwake kuliko kukipata.

### 9. Swala ya Kukidhi Haja

Muislamu anatakiwa amtegemee Allah (s.w) katika kila hali. Kila anapokuwa na tatizo au anapohitajia jambo lolote, anatakiwa amuelekee Allah (s.w) na aombe msaada kutoka kwake.

*Abdur-Raham ibn Awfi (r.a) amesimulia kuwa Mtume (s.a.w) amesema: Yeyote atakayekuwa na haja ambayo anataka itoshelezwe na Allah (s.w) au na mwanaadamu na atawadhe inavyostahiki, kisha aswali (rakaa mbili) amhimidi Allah na kumtakia Mtume Rehma na amani kisha aseme:*

● لَا إِلٰهَ إِلَّا اللّٰهُ الْحَلِيمُ الْكَرِيمُ سُبْحَانَ اللّٰهِ رَبِّ الْعَرْشِ الْعَظِيمِ وَالْحَمْدُ لِلّٰهِ

*"Hapana Mola (apasaye kuabudiwa) ila Mwenyezi Mungu. Mwingi wa huruma, Mkarimu. Utukufu ni wa Allah, Mfalme wa Arshi Tukufu, Shukurani zote ni za Mwenyezi Mungu. Mola (Bwana) wa walimwengu.*

*Nakuomba unijaalie njia ya kupata rehma Zako na sababu ya kupata msamaha wako; Ninaomba hifadhi Yako kutokana na kila ovu. Usiniache na kosa (dhambi) lolote bila ya kunisamehe na (usiniache na) na wasi wasi wowote bila ya kuniondolea, na usiniache na haja yoyote yenye radhi Zako bila ya kunikidhia. Ewe Mwingi wa Rehma Mrehemevu". (Tirmidh, Ibn Majah).*

رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ اَسْئَلُكَ مُوْجِبَاتِ
رَحْمَتِكَ وَعَزَآئِمَ مَغْفِرَتِكَ
وَالْغَنِيْمَةَ مِنْ كُلِّ بِرٍّ وَالسَّلَامَةَ
مِنْ كُلِّ اِثْمٍ لَا تَدَعْ لِيْ
ذَنْبًا اِلَّا غَفَرْتَهُ وَلَا هَمًّا اِلَّا
فَرَّجْتَهُ وَلَا حَاجَةً هِيَ لَكَ
رِضًى اِلَّا قَضَيْتَهَا يَا اَرْحَمَ
الرَّاحِمِيْنَ.

## 10. Swalatut-Tawbah

Swalatut-Tawbah ni swala ya kutubia. Muislamu akiteleza na kumkosea Mola wake au binaadamu mwenzake au akidhulumu nafsi yake, hana budi kutubu upesi iwezekanavyo. Kutubu maana yake ni kujutia kosa ulilolifanya, kukoma moja kwa moja kufanya kosa hilo. kuahidi kwa dhati moyoni kutorudia kosa hilo na kuomba msamaha kwa Allah kama umemkosea Yeye moja kwa moja. Kama umemkosea binaadamu kwanza muombe msamaha yeye mwenyewe kama inawezekana, kisha muombe Mwenyezi Mungu msamaha. Kama haiwezekani kumuomba msamaha huyo uliyemkosea, muombe msamaha Mwenyezi Mungu.

Njia nzuri ya kutubia ni kuswali rakaa mbili kisha kuomba msamaha kwa Mwenyezi Mungu kama tunavyojifunza katika Hadithi ifuatayo:

> *Abu Bakar (r.a) amesimulia kuwa Mtume (s.a.w) amesema: Mtu yeyote akifanya dhambi, kisha akatawadha akaswali rakaa mbili, kisha akaomba msamaha kwa Allah (s.w) inatarajiwa kuwa Allah atamsamehe. Kisha Mtume (s.a.w) katika kusisitiza hayo akasoma aya zifuatazo:*

وَالَّذِينَ إِذَا فَعَلُوا فَاحِشَةً أَوْ ظَلَمُوا أَنفُسَهُمْ ذَكَرُوا اللَّهَ فَاسْتَغْفَرُوا
لِذُنُوبِهِمْ وَمَن يَغْفِرُ الذُّنُوبَ إِلَّا اللَّهُ وَلَمْ يُصِرُّوا عَلَىٰ مَا فَعَلُوا وَهُمْ
يَعْلَمُونَ ﴿١٣٥﴾

*“Na ambao wanapofanya uchafu au kudhulumu nafsi zao humkumbuka Mwenyezi Mungu na kumuomba msamaha kwa dhambi zao. Na nani anayeghufiria dhambi isipokuwa Mwenyezi Mungu? Na hawaendelei na (maovu) waliyoyafanya, hali wanajua (kuwa hayo ni maovu). (3:135-136)*

## 11. Swala ya Kupatwa kwa Jua na Mwezi

Swala ya kupatwa kwa mwezi au jua ni sunnah iliyokokotezwa ambayo huswaliwa katika jamaa. Jua au mwezi unapopatwa Waislamu wanatakiwa waitane na kuswali swala ya Suunah ya kupatwa jua au mwezi kama alivyokuwa akifanya Mtume wa Allah:

*Aisha (r.a) ameeleza kuwa jua lilitokea kupatwa wakati wa Mtume (s.a.w). Alisimama kuswali na alirefusha kisimamo (kiasi cha kumaliza kusoma Suratul-Baqara). Kisha alirukuu na kurefusha sana rukuu yake. Kisha aliinuka kutoka kwenye rukuu na akarefusha kisimamo lakini kilipungua kidogo kuliko kile cha kwanza. Kisha alirukuu tena na kurefusha rukuu lakini kupungua kidogo kuliko ile rukuu ya kwanza. Kisha alisujudu na kisha akasimama tena lakini kwa kitambo kilichopungua kidogo kuliko kisimamo kilichotangulia. Kisha alirukuu tena kwa kitambo kilichopungua kidogo kuliko kile cha rukuu iliyotangulia. Kisha aliinuka kutoka kwenye rukuu na kurefusha kisimamo lakini kupungua kidogo kisimamo kilichotangulia. Kisha alirukuu tena na kurefusha rukuu yake lakini kupungua kidogo kuliko ile iliyotangulia. Kisha alisujudu. Kisha ligeuka (aligeukia watu) na wakati huo jua lilikwisha kuwa jeupe na akawahutubia watu. Alimshukuru (alimhimidi) Allah na akasema: Jua na mwezi ni alama mbili za Allah (s.w). Havipatwi kutokana na kifo cha mtu yeyote, wala kutokana na kuzaliwa kwa mtu yeyote. Enyi Ummah wa Muhammad, hapana yeyote mwenye kupata ghadhabu kuliko Allah anavyomghadhibikia mja wake pindi anapozini. Enyi watu wa Muhammad, naapa kwa Allah kuwa kama mngelikuwa mnajua, mngelicheka kidogo na kulia sana”. (Muslim)*

Kutokana na Hadithi hii tunaona kuwa swala ya kupatwa jua na mwezi ina visimamo (au visomo) vinne, rukuu nne na sijda nne. Visimamo na rukuu hutofautiana urefu kama ilivyo oneshwa katika Hadithi.Imamu Shafii na Maimamu wengine wanashikilia kuwa swala ya kupatwa jua na mwezi haina budi kuswaliwa katika muundo huu ulioelezwa katika hadithi hii. Lakini Imamu Abu Daud, anashikilia kuwa swala ya kupatwa kwa jua na mwezi iswaliwe kama swala ya kawaida kwani kutokana na hadithi hiyo Mtume (s.a.w) aliwahi pia kuswali swala hiyo kwa kufuatia muundo wa swala za kawaida.

Kwa ujumla wanachuoni wengi wanasisisitiza kuwa pamoja na kwamba swala ya kupatwa kwa jua na mwezi inaweza kuswaliwa kwa kufuata muundo wa kawaida wa swala, ni vizuri zaidi kama swala hiyo itaswaliwa kwa kufuata muundo ulioelezwa katika Hadithi hii wa kuwa na visimamo (visomo) vinne, rukuu nne na sijda nne.

Lengo la swala hii ni kumkumbuka Allah(s.w) kwa kuzingatia alama zake. Hivyo ni vyema Imamu baada ya swala awawaidhi Waislamu kuwakumbusha wajibu wao kwa Allah(s.w) na kuwakumbusha marejeo yao ya akhera. Hivyo swala ya kupatwa jua (Swalatul-Kusuf) au swala ya kupatwa mwezi (swalatul-Khusuf) hufuatiwa na khutuba mbili kama ilivyo katika khutuba ya Idd. Katika swala hizi Imamu atasoma kwa sauti.

## 12. Swala ya Kuomba Mvua - (Swalatul Istisqaa)'

Istisqaa ina maana ya kuomba maji. Uislamu unatuhimiza kumuelekea Allah kwa msaada wakati wa matatizo na dhiki. Kwa hiyo panapokuwa na ukame Waislamu wanahimizwa kumuomba Allah(s.w)kwa unyenyekevu katika jamaa. Maombi haya yanajulikana kama "Swalatul Istisqaa". Kutokana na Hadithi mbali mbali maombi haya yanaweza kuombwa katika namna tatu zifuatazo:

(a) Kuomba Dua bila ya swala.

(b) Kuomba dua katika khutuba ya Ijumaa au mwisho wa swala za faradhi.

(c) Namna ya tatu ambayo ni muhimu sana ni ile ya kuswali rakaa mbili zinazofuatiwa na khutuba na kumalizia na Dua.

Maombi haya hapana budi yaombwe kwa unyenyekevu mkubwa ukiambatana na imani kamili juu ya uwezo wa Allah usio mipaka.

### Swalatul Istisqaa Inavyoswaliwa

Swala hii ni sunnah iliyokokotezwa wakati wa ukame na huswaliwa katika jamaa uwanjani kama inavyo swaliwa swala ya Idd. Kama swala ya Idd katika rakaa ya kwanza kuna takbira saba baada ya Takbira ya kuhirimia na kuna Takbira tano kabla ya kuanza Suratul Fatiha katika rakaa ya pili. Ni sunnah katika rakaa ya kwanza, baada ya Al-fatiha kusoma Surat-Qaf au Al-A'laa na katika rakaa ya pili kusoma baada ya Alfatiha. suratul-Qamar au Al-Ghashiyah. Imamu ni sharti awe kiongozi wa ngazi ya juu au naibu wake anayeshughulikia mambo ya Waislamu.

Swala hii hufuatiwa na khutuba mbili kama ilivyo katika khutuba

za Idd. Ni sunnah Imamu kuleta ***istighfaari*** mara tisa kabla hajaanza khutuba ya kwanza na ya pili. Istighfaari hii ni kusema

أَسْتَغْفِرُ للهِ الْعَظِيْمُ الَّذِي لاَ إِلَهَ إِلاَّ هُوَ الْحَيُّ الْقَيُّوْمُ الْمُدَبِّرُ كُلَّ شَيْءٍ وَ أَتُوْبُ إِلَيْهِ

***Astagh-firullahil-adhiimu alladhii laa ilaha illa huwal-hayyul-qayyuumu-almudabbiru kullu-shayin wa-atuubu ilaihi.***

*Ninamuomba maghfira Mwenyezi Mungu Mtukufu ambaye hapana Mola ila Yeye Mwenye uhai wa milele Msimamizi wa kila jambo na Kwake ninatubia.*

Ni sunnah wakati wa kuomba dua kugeuza mikono au kuelekeza mbinguni migongo ya viganja vya mikono . Tunafahamishwa hili katika Hadith za Mtume (s.a.w) zifuatazo kuwa:

*Abdullah bin Zaid Al—Ansari (r.a) amesimulia kuwa Mtume (s.a.w) alikwenda nje ya mji ili kuswali swalatul-Istisqaa.Alipotaka kuomba dua, alielekea Qibla na akageuza kilemba chake. (Muslim).*

*Anas bin Malik (r.a) amesimulia kuwa Mtume (s.a.w) katika kuomba dua ya mvua alielekeza juu migongo ya viganja vyake vya mikono. (Muslim).*

## Tathmini ya Swala Zetu

Tumeshafahamu lengo la swala na namna linavyopatikana. Lakini ukiichunguza jamii ya Waislamu wanao swali hivi leo, huoni lengo hili likifikiwa. Kwa maana nyingine Waislamu wengi tunaoswali swala tano kwa kila siku, mwenendo na tabia zetu katika maisha ya kila siku hazitofautiani na wale wasioswali.

Pamoja na kuswali kwetu tunapoteza wakati wetu katika mambo ya upuuzi, tunasema uwongo, tunasengenya, tunafitinisha watu, tunawadharau wengine, tunavunja ahadi tulizoweka, tunahini amana za watu, tunadhulumu haki za watu, tunachuma katika njia za haramu, tunawatii viongozi wetu kinyume na amri za Allah(s.w), tunafuata njia

nyingine za maisha kinyume na ile aliyoiridhia Allah (s.w), tunawatumikia wengine na kuwategemea kinyume na Allah (s.w) na tunatenda mengine mengi kinyume na ridhaa ya Allah (s.w).

Je, kama mwenendo wetu ndio huu katika kuendesha maisha yetu ya kila siku tunatofauti gani na wale wasio swali na tunajitofautishaje na makafiri na washirikina kiutendaji? Kama tabia na mwendo wetu katika kuendesha maisha yetu ya kila siku ni sawa na ule wa makafiri na washirikina tutasalimikaje na adhabu kali ya Allah (s.w) aliyowaandalia makafiri na washirikina? Je swala zetu hizi zisizotunufaisha kama ilivyo matarajio na zisizotufikisha kwenye lengo lililokusudiwa haiwi ni mzigo kwetu na usumbufu mtupu? Bila shaka, kwa kujiuliza maswali haya, wengi tunaoswali kwa nia njema kabisa, tutaona kuna haja kubwa ya kupata jibu sahihi la swali lifuatalo:

“Kwa nini swala zetu hazituzalii matunda yanayotarajiwa na kutufikisha katika lengo tarajiwa? Japo kila mmoja anaweza kujibu swali hili kwa jinsi anavyoona, mchango wetu katika kujibu swali hili ni kwamba wengi wanaoswali wana mapungufu yafuatayo:

### 1. Kutojua Lengo la Kusimamisha Swala

Kutojua lengo halisi la swala au kuipa swala lengo lingine lisilokuwa lile alililoliainisha Allah (s.w), ni sababu tosha ya kufanya mwenye kuswali asifikie lengo la swala na kukosa manufaa yanayoambatana nalo. Lengo la swala kama lilivyobainishwa katika Qur-an ni:

....إِنَّ ٱلصَّلَوٰةَ تَنْهَىٰ عَنِ ٱلْفَحْشَآءِ وَٱلْمُنكَرِ ۗ.... ﴿٤٥﴾

*“... Hakika swala humzuia mtu na maovu na mambo machafu...” (29:45)*

Kwa maana nyingine lengo la swala ni kumfanya Muislamu awe na mwenendo mzuri anaouridhia Allah (s.w) katika kuendesha maisha yake ya kila siku. Utendaji wowote, shughuli yoyote au tabia yoyote mtu atakayokuwa nayo kinyume na ridhaa ya Allah (s.w) itakuwa ni miongoni mwa maovu na mambo machafu. Wengi wetu wameelewa kuwa lengo la swala ni kupata ***Thawabu*** (ujira mwema kutoka kwa Allah). Ni kweli kabisa kuwa Allah (s.w) ameahidi kuwazawadia wale wote watakaoishi hapa ulimwenguni kulingana na ridhaa yake, lakini zawadi hii sio lengo bali ni matunda yanayopatikana baada ya lengo kufikiwa. Hali kadhalika lengo la swala si kupata thawabu bali ni kumwepusha mwenye kuswali na yale yote yenye kumuudhi Allah (s.w) na kumpa msukumo wa kuyafanya yale yote yenye kumridhisha Allah (s.w) ili kupata radhi yake

na kustahiki kupata ujira mwema (*Thawabu)* aliowaahidi waja wema.

Hatari ya kuchukulia kuwa kupata "Thawabu" ndio lengo la swala, ni kwamba mtu anaweza kuridhika na swala zake kuwa zimempatia "Thawabu" na akawa na tumaini la kupata "Pepo" na huku amezama katika maovu na mambo machafu katika kuendesha maisha yake ya kila siku.

**2. Kutohifadhi Swala**

Swala haitoi matunda yanayotarajiwa na kufikia lengo lililotarajiwa mpaka ihifadhiwe. *"Wamefuzu Waislamu ambao swala zao huzihifadhi" (23:1, 8).* Kuhifadhi swala ni kuzingatia na kuyatekeleza kwa ukamilifu masharti ya swala, na kutekeleza kwa ukamilifu nguzo zake.

Wengi tunaoswali hatutekelezi ipasavyo masharti na nguzo za swala ama kwa kutojua au kwa kupuuza. Ni makosa makubwa mno kufanya ibada bila ya kuwa na elimu yake. Miongoni mwa watu wanaochukiza mbele ya Allah (s.w) ni mtu kufanya ibada yoyote ile kwa ujinga.Swala yoyote iliyoswaliwa pasina kutimiza na kukamilisha masharti na nguzo zake haimfikishi mwenye kuswali katika lengo la swala bali humzidishia uovu na kumfanya astahiki kupata ghadhabu za Allah (s.w) na adhabu kali:

فَوَيْلٌ لِّلْمُصَلِّينَ ﴿٤﴾ الَّذِينَ هُمْ عَن صَلَاتِهِمْ سَاهُونَ ﴿٥﴾

*"Basi adhabu kali itawathubutikia wanao swali, ambao wanapuuza swala zao".*

Hivyo, ili tupate matunda ya swala zetu na tufikie lengo lililotarajiwa hatuna budi kuyafahamu vyema masharti ya swala na kuyatekeleza kwa ukamilifu na hatuna budi vile vile kuzijua nguzo za swala na kuzitekeleza kwa ukamilifu.

**3. Kutokuwa na khushui katika Swala**

Unyenyekevu(*khushui*) ndio roho ya swala. Swala iliyoswaliwa pasina unyenyekevu huwa si swala bali maiti ya swala. Ni dhahiri kwamba kama swala ya mtu itakuwa maiti, haitakuwa na uwezo wowote wa kumfikisha mwenye kuswali kwenye lengo lililotarajiwa.

Unyenyekevu katika swala hupatikana kwa kuwa na utulivu wa

mwili na mawazo na kuwa na mazingatio ya Allah (s.w). Mazingatio ya Allah katika swala ndio nguvu pekee inayompelekea mja kufikia lengo la swala:

... وَلَذِكْرُ ٱللَّهِ أَكْبَرُ ... ﴿٤٥﴾

*"... Kwa yakini kumbuko la Mwenyezi Mungu (lililomo ndani ya swala) ni jambo kubwa kabisa (la kumzuia mja na maovu na mambo machafu)...". (29:45)*

Ni swala ile tu iliyoswaliwa kwa unyenyekevu ndio inayoweza kumfikisha mwenye kuswali kwenye lengo la swala na kumfanya afaulu na kustahiki ujira mkubwa na pepo ya Firdaus kutoka kwa Allah (s.w):

قَدْ أَفْلَحَ ٱلْمُؤْمِنُونَ ﴿١﴾ ٱلَّذِينَ هُمْ فِى صَلَاتِهِمْ خَٰشِعُونَ ﴿٢﴾
أُو۟لَٰٓئِكَ هُمُ ٱلْوَٰرِثُونَ ﴿١٠﴾ ٱلَّذِينَ يَرِثُونَ ٱلْفِرْدَوْسَ هُمْ
فِيهَا خَٰلِدُونَ ﴿١١﴾

*Hakika wamefuzu Waislamu ambao huwa wanyenyekevu katika swala zao... Hao ndio warithi ambao watarithi Pepo wakae humo milele". (23:1-2, 10-11)*

Wengi tunaoswali hatuswali kwa unyenyekevu. Mara nyingi tunaswali huku mawazo yetu yamehama kwenye swala na yanajishughulisha na mambo mengine kabisa nje ya swala. Mara nyingi ndani ya swala ndimo tunamokumbuka mambo yetu mengi tuliyoyasahau.Hii yote huonyesha udhaifu tulionao katika kumzingatia Allah (s.w) katika swala zetu. Miongoni mwa sababu kubwa zinazotufanya tukose mazingatio katika swala zetu ni kutojua maana na undani wa yale tuyasemayo katika swala. Wengi wetu hatujui maana ya aya za Qur-an tunazozisoma, dhikri na tasbihi mbali mbali tunazozileta, maamkizi na dua mbali mbali tunazoziomba katika swala. Hali hii ya kutojua maana ya yale tuyasemayo katika swala inachangia kwa kiwango kikubwa kutupunguzia uwezo wa kumuelekea na kumnyenyekea Allah (s.w). Wengine tunajua maana ya yale tuyasemayo katika swala lakini hatuyazingatii bali tunayatamka kikasuku tu sawa na wale wasiofahamu maana yake.

Bila shaka tukisimamisha swala kwa kujua vyema lengo lake na

kwa nia ya kulifikia lengo hilo, tukajitahidi kuliendea lengo hilo kwa kutekeleza kwa ujuzi na kwa ukamilifu masharti yote na nguzo zote za swala, tukajitahidi kuyafahamu yale yote tuyasemayo katika kila hatua ya swala, na tukajitahidi kuyazingatia na kisha tukajitahidi kutuliza miili yetu na nyoyo zetu katika swala, tutalifikia lengo la swala na kupata matunda yatokanayo - Insha-a Allah(s.w)

رَبِّ ٱجْعَلْنِى مُقِيمَ ٱلصَّلَوٰةِ وَمِن ذُرِّيَّتِى ۚ رَبَّنَا وَتَقَبَّلْ دُعَآءِ

*Mola wangu! Nijaalie niwe msimamishaji swala na kizazi changu. Mola wetu na upokee maombi yangu mengine.*

## Swala ya maiti

### Mambo yanayostahiki kufanyiwa maiti ya Muislamu

Mambo yaliyo faradhi kufanyiwa maiti ya Muislamu ni manne yafuatayo:

(1) Kuoshwa.
(2) Kuvikwa sanda (kukafiniwa).
(3) Kuswaliwa.
(4) Kuzikwa.

Pamoja na haya manne kuna mambo mengine mengi yanayotakiwa afanyiwe Muislamu anayekaribia kufa na aliyekufa kama alivyotuelekeza Mtume (s.a.w). Hivyo, katika kitabu hiki tumeeleza mambo yote ya msingi yanayostahiki afanyiwe Muislamu pale anapokaribia kufa mpaka baada ya kuzikwa.

### Mambo muhimu anayofanyiwa Muislamu anayekaribia Kufa

Mauti ni jambo la lazima sana kumtokea mwanaadamu na viumbe vyote na huingia bila taarifa wakati wowote na mahali popote kama anavyotufahamisha Allah (s.w):

أَيْنَمَا تَكُونُوا۟ يُدْرِككُّمُ ٱلْمَوْتُ وَلَوْ كُنتُمْ فِى بُرُوجٍ مُّشَيَّدَةٍ ۗ

*Popote mlipo mauti yatakufikieni, na hata mkiwa katika ngome madhubuti...” (4:78).*

كُلُّ نَفْسٍ ذَآئِقَةُ ٱلْمَوْتِ ۗ وَإِنَّمَا تُوَفَّوْنَ أُجُورَكُمْ يَوْمَ ٱلْقِيَـٰمَةِ ۖ
فَمَن زُحْزِحَ عَنِ ٱلنَّارِ وَأُدْخِلَ ٱلْجَنَّةَ فَقَدْ فَازَ ۗ وَمَا ٱلْحَيَوٰةُ ٱلدُّنْيَآ إِلَّا
مَتَـٰعُ ٱلْغُرُورِ ﴿١٨٥﴾

*Kila nafsi itaonja mauti. Na bila shaka mtapewa ujira wenu kamili siku ya Kiyama. Na aliyewekwa mbali na moto na akaingizwa Peponi, basi amefuzu (amefaulu kweli kweli). Na maisha ya dunia (hii) si kitu ila ni starehe idanganyayo (watu). (3:185).*

Kutokana na ukweli huu ni jambo la busara mno kwa mwanaadamu mwenye akili timamu kujiandaa kukabili mauti wakati wowote na popote atakapokuwa. Ni kweli kuwa maisha ya ulimwengu yamejaa hadaa lakini hatuna budi kukumbuka kuwa maisha yote ni mtihani kwetu na Muumba wetu anatuchunga barabara na kudhibiti tuyatendayo katika kila pumzi ya maisha yetu. Kumbukumbu ya ukweli huu pamoja na kukikumbuka kifo katika kila sekunde ya maisha ndiyo nguvu pekee ya kumsukuma mja kwenye maisha ya wema anayoridhia Allah (s.w). Kifo ni tukio la lazima lisiloepukika kwa kila kiumbe. Hatuna budi kukifanya kifo kitu cha kawaida na kujiandaa kwacho badala ya kufanya zoezi la kukikimbia jambo ambalo ni muhali.

Mtu anapokaribia kufa na baada ya kufa huwa, pamoja na ujanja wake wote na vipaji vyake vyote alivyokuwa navyo, hajimudu kwa chochote na kwa hiyo anahitajia msaada wa kila jambo.

Hivyo Uislamu unatufundisha kuwa mtu anayekaribia kufa tumfanyie yafuatayo:

1. Kumuogesha, kumpigisha mswaki na kumpaka manukato iwapo kuna uwezekano.

2. Kumlaza kwa ubavu wa kulia na kumuelekeza Qibla kama kuna uwezekano. Kama hivi haiwezekani mgonjwa alazwe chali na uso wake unyanyuliwe kiasi cha kuelekea Qibla

3. Kumpa maji ya kunywa.

4. Kutamka kalima ya Laailaahaillallah bila ya kumuashiria kuwa naye atamke. Lengo la kumtamkia kalima hii ya Tawhiid ni kumkumbusha ili naye aweze kutamka kama ni mtu aliyeishi maisha yote kulingana na kalima hiyo. Kumtamkia kalima Muislamu anayekaribia kufa ni agizo la Mtume (s.a.w):

*Abu Said na Abu Hurairah (r.a)wamesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: "Wasomeeni watu wenu wanaokaribia kufa*:

*"Hapana mola ila Allah"* لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللهُ

Pia Mu'az bin Jabal amesimulia kuwa Mtume (s.a.w) amesema:

*Yule ambaye maneno yake ya mwisho yatakuwa: (Hapana mola ila Allah) ataingia Peponi. (Abu Daud).*

Kutokana na Hadithi hii haitakuwa rahisi kwa mtu wa motoni kutamka kalima hii bali ataitamka tu yule aliyeishi maisha yake yote kulingana na kalima hii. Kwa mtu mwema kuitamka kalima hii kunampa maliwazo kuwa amali yake njema imetakabaliwa. Kutamka huku si lazima kuwe kwa wazi. Kutamka kimoyo moyo tu kunatosha, japo ni vizuri kuibanisha kwa ulimi iwapo ipo fursa.

**Mambo Anayofanyiwa Mtu mara tu baada ya Kufa**

Baada ya kushuhudia kuwa ndugu yetu ameshakata roho vyema tuseme na kuzingatia maneno yafuatayo kama alivyotufahamisha Allah (s.w)

... إِنَّا لِلَّهِ وَإِنَّآ إِلَيْهِ رَاجِعُونَ ...

*"... Hakika sisi ni wa Allah na kwake tutarejea ..." (2:156).*

Maneno haya ni ya msingi sana katika hali hii ya kufiwa, kwani yanawaliwaza wafiwa na kuwaepusha na fadhaa zinazoweza kutokea juu ya kifo cha marehemu. Ukizingatia maneno ya aya hii utaona kuwa kwa vyovyote iwavyo, kurejea kwa Allah ni jambo lisilozuilika. Hivyo, chochote kile kitakachokuwa ndio sababu ya kifo cha marehemu kitakuwa ni sababu tu ya kifo hicho aliyoiweka Allah (s.w)

Baada ya maliwazo haya maiti ile yapasa kufanyiwa yafuatayo:

1. Kwa taratibu rudishia mdomo usibakie wazi kwa kufunga kidevu kwa kitambaa na kukizungushia kichwani.

2. Funga macho ya marehemu kwa taratibu na huku ukisoma:

> *"Kwa jina la Allah na kwa kufuata mila ya Mjumbe wa Allah. Ewe Mola wetu mrahisishie mambo yake ya sasa na msahilishie mambo yake baadaye. Na jaalia atakayokutana nayo yawe bora kuliko aliyoachana nayo".*

3. Lainisha viungo vya maiti kwa kukunja na kukunjua pole pole sehemu zote zenye viungo katika mikono na miguu. Kama patakuwa na ugumu wowote katika kumnyoosha viungo hivyo, maji ya moto au mafuta yanaweza kutumika ili kulainisha. Baada ya kulainisha viungo, miguu na mikono inyooshwe na alazwe huku uso ukielekea Qibla kwenye kitanda kisichokuwa na godoro.

4. Maiti avuliwe nguo zote alizokufa nazo kisha kumgubikwa kwa shuka kubwa, pia ni vyema afungwe kitambaa tumboni au kuwekewa kitu chenye uzito kidogo juu ya tumbo ili lisifutuke sana.

5. Marashi na ubani vitumike sana mahali alipo maiti ili kuzima harufu ya uvundo itokayo kwa maiti.Mwanaadamu ni msafi sana anapokuwa hai. Lakini muda mfupi tu baada ya kufa huanza kutoa harufu kali ya uozo.

**Kumuosha Maiti**

Kumuosha maiti ni Faradh Kifaya. Maiti hawezi kuswaliwa mpaka akoshwe kwanza kama vile ilivyo haramu kuswali bila ya kuwa twahara. Ni maiti ya Muislamu aliyekufa shahidi katika vita vya kupigania Uislamu tu ndiye anayezikwa hivyo hivyo na damu zake bila ya kuoshwa kama tunavyojifunza katika Hadith ifuatayo:

> *"Ibn Abbas (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah alipitisha amri juu ya watu waliokufa katika vita vya Uhud kuwa nguo zao za chuma na ngozi walizovalia zinaweza kuvuliwa bali wazikwe hivyo hivyo na damu pamoja na nguo zao nyingine za kawaida." (Abu Daud, Ibn Majah).*

Kabla ya kuanza kumuosha maiti hapana budi kuzingaqtia yafuatayo:

**1.** Maiti ya kiume ioshwe na wanaume na maiti ya kike ioshwe na wanawake. Watoto wadogo wanaweza kuoshwa na wanaume au wanawake.Pia ni Sunnah mke kumuosha mumewe na mume kumuosha mkewe.

**2.** Ni mtu mmoja tu anayeosha na mwingine/wengine wa kumpa msaada pale atakapohitajia.

**3.** Ni muhimu muoshaji ayafahamu masharti ya kuosha maiti ya Muislamu yafutayo:

(i) Muoshaji awe Muislamu.

(ii) Mahali pa kuoshea pawe faragha - panaweza kuwa bafuni, au sehemu ya ua uliojengwa maalumu kwa kazi hiyo au hata chumbani kama wafanyavyo watu wengi.

(iii) Maiti ioshwe huku imefunikwa gubi-gubi kwa nguo nyepesi inayoruhusu maji kupenyeza.

(iv) Muoshaji asiishike maiti bali aoshe akiwa amevaa *gloves*.

(v) Kuchunga yale masharti yote yanayopaswa yatekelezwe na mwenye kukoga josho la wajibu kama vile kuwa na maji safi ya kutosha, pasiwe na kizuizi cha kuzuia maji kupenyeza mwili wa maiti.

**4.** Ni muhimu muoshaji afahamu nguzo na Sunnah za kuosha maiti. Nguzo za kuosha ni mbili:

(i) Nia.

(ii) Kueneza maji mwili mzima wa maiti.

Ni sunnah kumuosha maiti mara tatu au zaidi ya hivyo. Lakini katika idadi ya witri kama tunavyojifunza katika hadithi ifuatayo:

*Ummu Atiyyah (r.a) amesimulia kuwa: Mtume wa Allah alitujia tulipokuwa tukimuosha (marehemu) binti yake (Zainab r.a). alisema: Muosheni mara tatu au mara tano au zaidi ya hapo kama mtaona hapana budi kufanya hivyo kwa maji ya mkunazi (lot tree) na wekeni kafuri (karafuu maiti) au kitu kama hicho kwenye maungio (joints). Mtakapo maliza niiteni. Kwa*

*hiyo baada ya kumaliza tulimwita. Alitupa shuka yake ya kiunoni na kutuambia: Mfunikeni nayo. Katika maelezo mengine, Mtume (s.a.w) alisema: Muosheni katika witri mara tatu, au mara tano, au mara saba na anzeni na upande wake wa kulia na viungo vya kutawadha. Akasema (Ummu Atiyah): Tulimuosha nywele zake mara tatu na kisha tukamlaza chali (kwa mgongo). (Bukhari na Muslim)*

## Namna ya Kuosha Maiti hatua kwa hatua

**1.** Maiti awekwe juu ya kitanda chenye tobo katikati la kupitishia uchafu utokao tumboni kama upo.

**2.** Lichimbwe shimo (ufuo) usawa wa tobo la kitanda, la kuhifadhi uchafu utakao toka kwa maiti. Iwapo hapana uwezekano wa kutengeneza ufuo, pawekwe kitu cha kukinga uchafu badala yake. Anaweza kuoshewa bafuni.

**3.** Maiti ifunikwe nguo moja kubwa, iliyo nyepesi kiasi cha kuruhusu maji kupita.

**4.** Maiti ikalishwe kitako juu ya hicho kitanda na makalio yake yawe sawa sawa na hilo tobo la kitanda na ufuo chini yake na iinamishwe kidogo nyuma.Kama ni maiti ya mtu mzima ni vyema msaidizi wa mwoshaji amuegemeze maiti kwa goti lake.

**5.** Mwoshaji apitishe mkono wake wa kushoto juu ya tumbo la maiti aliminyeminye kwa taratibu ili utoke uchafu uliomo humo ndani.

**6.** Amlaze chali na amminyeminye tumbo lake kama hapo awali.

**7.** Aikalishe tena kisha apitishe mkono wake wa kushoto chini, ukiwa umevalishwa gloves asafishe tupu mbili huku anajimiminia maji kwa mkono wa kulia mpaka atakate.

**8.** Muoshaji, baada ya hapo, azungurushe kitambaa kwenye kidole cha shahada cha mkono wa kushoto, akichovye majini, kisha amswakishe maiti vizuri meno ya juu na ya chini, kisha akitupe ufuoni.

**9**. Azungurushe kitambaa kingine kwenye kidole kidogo cha mkono wa kushoto, akichovye majini, kisha amsafishe kwacho tundu za pua, kisha akitupe ufuoni.

**10**. Achukue kijiti laini achokonoe kucha zake maiti, iwapo ni ndefu na chafu.

**11**. Akiwa pia amemkalisha, amtawadhishe maiti kwa kufuata utaratibu wa kawaida wa kutawadha. Lakini wakati wa kumwosha uso, amuinamishe mbele kidogo ili maji yasimwingie ndani.

12. Maiti akiwa katika hali hiyo hiyo ya kukaa, mwoshaji ataanza kumwosha kichwa huku akiwa amemuinamisha kwa mbele. Kama nywele ni nyingi zichanwe panapo uwezekano na zioshwe kwa sabuni. Kisha maji yamiminwe mpaka povu la sabuni liishe. Nywele na ndevu zichanwe vizuri na mwanamke mwenye nywele nyingi asukwe mikia. Nywele zitakazong'oka ziambatanishwe na sanda.
13. Baada ya kuoshwa kichwa, maiti alazwe kwa ubavu wa kushoto, kisha kuanza kumwosha ubavu wa kulia kwa kumiminia maji mbele na nyuma pamoja na kusugua kwa sabuni. Kisha kummiminia maji mengi mpaka povu liishe.
14. Kisha maiti atalazwa kwa ubavu wa kulia na kuoshwa ubavu wa kushoto kama ilivyofanyika kwa ubavu wa kulia.
15. Baada ya makosho haya mawili - la maji na sabuni na la kuondoa sabuni, pawe na kosho la tatu la maji yaliyowekwa karafuu maiti na marashi kidogo. Karafuu maiti inasaidia kulegeza maungio na kufanya mwili wa maiti usitepete.
16. Baada ya makosho haya matatu, mwoshaji anyooshe viungo vya maiti na kumlaza sawasawa kama alivyolazwa mara baada ya kufa, kisha achukue nguo kavu na kumfuta maiti kama mtu anavyojifuta kwa taulo baada ya kukoga. Kisha maiti awekwe juu ya mkeka mkavu na afunikwe nguo kubwa kavu tayari kwa kupambwa na kuvalishwa sanda.

## Namna ya Kumkafini Maiti

Kumkafini maiti au kumvalisha sanda ni Faradhi Kifaya. Nguo nzuri ya kutumia kwa ajili ya sanda ni nguo nyeupe ya pamba kama tunavyofahamishwa katika Hadithi ifuatayo:

*Ibn Abbas amesimulia kuwa Mtume wa Allah (s.a.w) amesema: Vaeni nguo nyeupe, kwa sababu hilo ni vazi lenu lililo bora kuliko yote, na wakafinini maiti wenu nguo (nyeupe). (Abu Daud, Tirmidh na Ibn Majah).*

Pia ni vyema nguo hiyo isiwe ya gharama kubwa na nguo iliyotumika ni bora zaidi kama tunavyofahamishwa katika Hadith ifuatayo:

*Ali (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: "Msigharamie sana nguo ya sanda, kwani inakwenda kuozeana (kaburini)". (Abu Daud).*

Hajj (mwenye kuhiji) akifa wakati wa Hija, akiwa bado kwenye “Ihram” (vazi rasmi la kuhijia - shuka mbili nyeupe zisizo shonwa), Ihram yake huwa ndio sanda na kichwa chake kubakia wazi bila ya kufunikwa kama tunavyofahamishwa katika Hadithi:

*Abdullah bin Abbas(r.a) amesimulia kuwa mtu mmoja alikuwa pamoja na Mtume (s.a.w) ngamia wake alimkanyaga, wakati akiwa anahiji mpaka akafa, Mtume wa Allah akasema:“Muosheni na maji na majani ya mkunazi na mumkafini kwa hayo mashuka yake mawili, msimpake manukato na msimfunike kichwa chake, na hakika siku ya Kiyama atafufuliwa akiitikia Labbaika. (Bukhari na Muslim).*

Ukubwa wa kitambaa cha sanda utategemea ukubwa wa maiti. Sanda ya mwanamume ina vipande vitatu vilivyo sawa sawa na sanda ya mwanamke ina vipande vitano.

**Sanda ya Mwanamume na Namna ya Kuivika**

Sanda ya mwanamume ina vipande (majamvi) vitatu. Utaratibu wa kutayarisha sanda na kukafini ni kama ifuatavyo:

1. Weka kipande cha kwanza juu ya mkeka au jamvi, kisha cha pili na cha tatu na kila kipande kifukizwe ubani na kupakwa marashi. Vipande vyote hivi vitatu vishikizwe na uzi katikati.

2. Pasua kamba katika pembe mbili za jamvi la kwanza, kamba moja kwa ajili ya kufungia kichwani na nyingine ya kufungia miguuni. Kamba nyingine ya kumfungia maiti katikati itatolewa kwenye jamvi la pili. Kamba nyingine tatu za kufungia juu ya mkeka zitatoka kwenye jamvi la pili na la tatu.

3. Maiti italazwa juu ya vipande vyote vitatu. Ichukuliwe pamba iwekwe manukato kisha iwekwe juu ya viungo vyote vya sijda - kipaji cha uso, viganja vya mikono, magotini na kwenye vidole vya miguu; pia pamba hiyo itumike kuzibia matundu yote mwilini - mdomo, pua, masikio na makalio.

4. Maiti itatatizwa na kipande cha kwanza mpaka kimuenee - kwa kuanza kutatiza kunjo la kushoto, kisha kunjo la kulia lije juu. Vipande viwili vilivyobaki vitatizwe kama hicho cha kwanza. Kisha zile kamba zitumike kufunga vitanzi kichwani, miguuni na tumboni ili sanda isije vuka na kumuacha maiti uchi. Katika hali hii maiti itakuwa tayari kwa kuswaliwa. Inaweza kuwekwa kwenye jeneza hivyo hivyo au inaweza kuzungushiwa mkeka kwanza ndio iwekwe kwenye jeneza.

**Sanda ya Mwanamke na Namna ya Kumvika**

Sanda ya mwanamke kawaida inavipande vitano. Vipande vikubwa viwili sawa na vile vya sanda ya mwanamume. Kipande cha tatu ni shuka au gagulo (*under skirt*), kipande cha nne ni kanzu na kipande cha tano ni ukaya au kipande cha nguo cha kufunikia kichwa na uso. Utaratibu wa kutayarisha sanda na kukafini ni kama ifuatavyo:

1. Vipande vikubwa viwili vitatandikwa kimoja hadi kingine kama inavyofanywa kwa sanda ya mwanamume.

2. Kikatwe kitambaa cha ukubwa wa shuka ya kawaida ya kufunga kiunoni. Kisha kipande hiki kiwekwe juu ya vipande viwili vikubwa katika sehemu ya chini atakapolazwa maiti ili shuka hii itatizwe kiunoni kama mtu anayefunga shuka ya kawaida.

3. Kisha ikatwe kanzu ambayo haishonwi vizuri, kwa kukunja kitambaa na kutoboa katikati ili iwe sehemu ya kuingiza kichwa wakati wa kuvalisha na kushikiza pembeni kwa uzi kufanya mfano wa kanzu kata mikono. Kanzu itatandikwa juu ya kipande kikubwa cha pili katika sehemu ya juu na sehemu ya chini itakuwa juu ya ile shuka (gagulo) baada ya kuwekwa manukato na kufukizwa ubani.

4. Kitambaa cha ukaya cha kutosha kufunika kichwa na uso kitaingizwa ndani ya shingo ya kanzu na kunyooshwa kwa juu. Baada ya hapo matayarisho ya sanda ya mwanamke yatakuwa yamekamilika.

5. Maiti ataanza kuvalishwa kanzu, kisha juu yake atafungwa shuka. Kisha atawekwa pamba yenye manukato viungo vyote vya sijda pamoja na sehemu zote za matundu kama inavyofanywa kwa maiti ya mwanamume. Baada ya hapo, maiti itatatizwa na vipande vikubwa viwili kimoja baada ya kingine, kila mara kunjo la kulia likiwa juu na itafungwa vile vile kwa kamba tatu - miguuni, tumboni na kichwani na kuwa tayari kuingizwa kwenye jeneza na kuswaliwa.

### Sanda ya Watoto

Sanda ya watoto wadogo, wa kike au wa kiume ni vipande vitatu tu kama ile ya wanaume wakubwa.

### Namna ya kumswalia Maiti

Swala ya maiti au swala ya jeneza ni faradhi kifaya. Ni faradhi kifaya kwa sababu ikifanywa na wachache au na mtu mmoja tu katika jamii inatosheleza na Waislamu wote wanasalimika na ghadhabu za Allah (s.w).

### Masharti ya Swala ya Maiti

Masharti ya swala ya maiti ni yale yale ya swala ya kawaida kwa wenye kumswalia maiti bali kwa maiti mwenyewe kuna masharti yafuatayo:

(i) Maiti awe Muislamu kwani Allah (s.w) amesema:

وَلَا تُصَلِّ عَلَىٰٓ أَحَدٍ مِّنْهُم مَّاتَ أَبَدًا

*"Wala usimswalie abadan mmoja wao (makafiri na wanafiki) yeyote akifa". (9:84)*

(ii) Maiti awe ameshaoshwa.

(iii) Maiti awekwe mbele ya wanaomswalia. Lakini pia inajuzu kumswalia maiti ambaye hayupo,swala ya ghaibu. Maiti zikiwa nyingi zitapangwa mbele za kiume zikiwa karibu na Imamu, kisha zitaswaliwa swala moja tu.

(iv) Maiti asiwe shahidi.Kwa mujibu wa Sunnah ya Mtume (s.a.w) watu waliokufa katika vita vya kupigania dini ya Allah (s.w) hawaoshwi wala kuswaliwa.Mtume (s.a.w) aliamuru Mashahidi katika vita vya Uhud wasioshwe wala wasiswaliwe. (Abu Daud).

## Nguzo za Swala ya Maiti

Nguzo za swala ya maiti ni tofauti kidogo na zile za swala ya kawaida. Tofauti na swala ya kawaida, swala ya maiti ina kusimama tu, hakuna rukuu, sijda wala vikao. Nguzo za swala ya maiti ni hizi zifuatazo:

1. Nia.
2. Takbira ya kuhirimia (Takbira ya kwanza)
3. Kusoma suratul fatiha
4. Kuleta takbira ya pili
5. Kumswalia Mtume(s.a.w) kama anavyoswaliwa katika swala ya kawaida
6. Kuleta takbira ya tatu.
7. Kumuombea dua maiti
   Kuleta takbira ya nne
8. Kutoa salaamu

## Sunnah za Swala ya Maiti

Sunnah za swala ya maiti ni hizi zifuatazo:

(i) Kusoma Audhubillah kabla ya Al-fatiha.
(ii) Kusema Amin baada ya Al-fatiha.
(iii) Kuyasema yote yanayosemwa katika swala hii kimya kimya, ila Imamu atatoa Takbira Nne naSalam kwa sauti.
(iv) Iswaliwe jamaa na safu ziwe witri; 1, 3, 5, 7, 9, n.k
(vi) Kuwaombea Waislamu wote dua pamoja na maiti.
(vii) Baada ya Takbira ya Nne na kabla ya Salaam kuomba dua ifuatayo:

اللَّهُمَّ لاَ تَحْرِمْنَا أَجْرَهُ , وَلاَتَفْتِنَا بَعْدَهُ

***"Allahumma laatahrimnaa ajrahu, walaataftinaa ba'adahu"***

*"Ewe Mwenyezi Mungu, usitunyime malipo yake na usitujaribu baada yake."*

(viii) Kutoa Salaam ya kwanza na ya pili kwa ukamilifu wake.
(ix) Imamu kusimama karibu na kichwa cha maiti ya kiume na kusisima karibu na kiuno (nyonga) ya maiti ya kike.

## Namna ya Kutekeleza Swala ya Maiti

Utaratibu wa kusimamisha swala ya maiti ni kama ifuatavyo:

1. Maiti iwekwe mbele.
2. Imamu asimame katikati ya mwili wa maiti kama maiti ni ya kike na asimame sawa na mabega kama maiti ni ya kiume.Iwapo maiti zinazoswaliwa ni zaidi ya mmoja zipangwe moja mbele ya nyingine .Maiti za kiume zikiwa karibu na Imamu.

3. Wanaomfuata Imamu wasimame kwenye mistari yenye idadi ya witri; 1, 3, 5, 7, n.k.



***Kielelezo:*** *Namna ambavyo swala ya maiti huswaliwa ikiwa katika safu za witri.*

4. Baada ya kusimama hivyo swala itaanza na kuendelea kama ifuatavyo:
   (i) Nia - nia ya kumswalia maiti iliyo mbele huwekwa moyoni (si lazima kutamka).
   (ii) Kisha nia hii huambatanishwa na Takbira ya kwanza - Takbira ya kawaida ya kuanzia swala - nayo ni kusema: ***Allahu Akbar***.
   (iii) Imamu na Maamuma watasoma Suratul Fatiha kimya kimya.
   (iv) Baada ya kuimaliza Suratul- Fatiha Imamu atasema tena ***Allahu Akbar*** na Maamuma watafuatisha hivyo hivyo - bila ya kuinua mikono.
   (v) Imamu na Maamuma watamswalia Mtume (s.a.w) kimya kimya kama ilivyo katika tahiyyatu ya mwisho ya swala ya kawaida.
   (vi) Baada ya kumswalia Mtume, Imamu atasema tena - ***Allahu Akbar*** na Maamuma watafuatisha hivyo hivyo kimya kimya bila ya kuinua mikono.
   (vii) Kisha kimya kimya maiti huombewa dua yoyote ile katika zile alizotufundisha Mtume (s.a.w). Moja kati ya dua hizo ni hii iliyosimuliwa na Abu Hurairah na kupokelewa na Maimamu wa hadith - Ahmad, Abu Daud, Timidh na Ibn Majah.

اللهمّ اغفرْلحَيِّنا وَميِّتنا وَشاهِدِنا وَغَائِبِنا وَذكَرِنا وأنْثَانا

اللهُمّ مَنْ أَحْيَيْتَهُ مِنَّا فَأَحْيِهِ عَلى الإِسْلاَمْ ،وَمَنْ تَوفَّيْتَهُ مِنَّا

فَتَوفَّهُ عَلى الاِيْمَان، اللهمّ لاَتَحْرِمْنَا أَجْرَهُ وَلاَتَفْتِنَا بَعْدَهُ

***Allaahumma gh-fir lihayyinaa wamayyitinaa washaahidinaa waghaaibinaa, wadhakirnaa waunthaanaa. Allaahumma man ahyaytahu minnaa fa-ahyihi 'alal Islam. Waman tawaffaytahuu minnaa fatawaffahu 'alal Imaani. Allaahumma laa tahrimnaa ajrahuu walaa taftinaa ba'adahuu.***

*Ewe Allah tusamehe sisi, na maiti wetu, na mashahidi wetu, na wanamume wetu, na wanawake wetu. Ewe Allah, yeyote yule miongoni mwetu utakayemuwezesha kuishi, mjaalie aishi Kiislamu; na yeyote yule miongoni mwetu utakaye mfisha mjaalie afe na Imani (ya Kiislamu). Ewe Allah, usitukatishe kupata ujira kutoka kwake na usitufitinishe baada yake"*

Au kwa kifupi kabisa tunaweza kumrehemu maiti kwa kusema:

اللَّهُمَّ اغْفِرْ لَهُ وَارْحَمْهُ

***Allaahummaghfir lahuu warhamhu***
*(Ewe Allah, Mghufirie na Umrehemu).*

(viii) Baada ya Dua hii Imamu atasema tena kwa mara ya nne - ***Allahu Akbar*** na Maamuma watafanya hivyo hivyo bila ya kuinua mikono.

(ix) Waombewe dua Waislamu wote (Dua hii si lazima kuileta). Dua ifuatayo inaweza kuombwa hapa:

رَبَّنَا ٱغْفِرْ لَنَا وَلِإِخْوَٰنِنَا ٱلَّذِينَ سَبَقُونَا بِٱلْإِيمَـٰنِ وَلَا تَجْعَلْ فِى

قُلُوبِنَا غِلًّا لِّلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ رَبَّنَآ إِنَّكَ رَءُوفٌ رَّحِيمٌ ﴿١٠﴾

*"... Mola wetu! Tusamehe sisi na ndugu zetu waliotutangulia (kufa) katika Imani (ya Kiislamu). Wala usijaalie katika nyoyo zetu uadui kuwafanyia Waislamu wenzetu. Mola wetu! Hakika wewe ni Mpole sana, mwenye Rehma mno". (59:10)*

(x) Baada ya dua hii itatolewa Salaam ya kumaliza swala na ni bora kuirefusha kidogo kuliko ile ya swala ya kawaida kwa kusema:

أَلسَّلامُ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَتُ اللهِ وَبَرَكَاتُهُ

*Amani iwe juu yenu na Rehma za Allah na Baraka zake.*

Swala ya maiti pia inaweza kuswaliwa kwa ghaib, yaani bila ya kuwa na jeneza mbele. Mtume (s.a.w) mara kadhaa katika maisha yake, aliongoza swala ya maiti wa mbali na karibu waliokwisha zikwa kama tunavyofahamishwa katika Hadith zifuatazo:

*Abu Hurairah (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah (s.a.w) alitoa habari za kifo cha Najashi (Mfalme wa Uhabeshi) kwa watu katika siku aliyokufa, akaenda nao katika sehemu ya kuswalia, akafanya mistari pamoja nao kisha akapiga takbira nne (yaani akaongoza swala ya Jeneza). (Bukhari na Muslim).*

*Ibn Abbas (r.a)amesimulia kuwa Mtume wa Allah alipita karibu na kaburi alimozikwa maiti usiku uliopita. Akauliza: Ni wakati gani alizikwa? Walijibu: Usiku uliopita. Akauliza: Kwa nini hamkunifahamisha? Walijibu: Tulizika katika giza la usiku. Kwa hiyo hatukupenda kukuamsha usingizini. Kisha alisimama na tukaunda mistari nyuma yake akaiswalia maiti ile. (Bukhari na Muslim).*

## Kusindikiza Jeneza

Baada ya maiti kuswaliwa jeneza litaongozwa kuelekea kaburini. Inatakiwa Waislamu walisindikize jeneza; wasiliweke mpaka likalishwe chini. Pia Mtume (s.a.w) ametuamrisha kusimama tutakapoona jeneza likipitishwa:

*Jabir (r.a) amesimulia: Wakati Jeneza lilipokuwa linapita, Mtume (s.a.w) alisimama nasi pia tukasimama pamoja naye. Tukauliza: Ewe Mtume wa Allah! Hakika huyo ni Myahudi. Akasema: "Hakika kifo ni tishio. Kwa hiyo wakati wote mtakapoona Jeneza likipita simameni".(Bukhari*

Maandamano ya mazishi yawe kimya kimya.Kumsindikiza maiti kwa muziki na vilio ni haramu.



**Kuzika**

Kuzika ni kitendo cha nne cha faradh tunacho lazimika kumfanyia ndugu yetu aliyetutangulia kufa. Japo ni faradhi kifaya, kila Muislamu anawajibika kushiriki katika mazishi kufanya hivyo kuna malipo makubwa mbele ya Allah (s.w) na yanapatikana mafunzo makubwa kwa mwenye kuzingatia kifo. Hadith ifuatayo inatukumbusha wajibu kwa ndugu zetu Waislamu:

*Ally (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: Muislamu kwa Muislamu mwingine anawajibika katika hali ya kawaida kumfanyia nduguye mambo sita:*

*(i) Atamsalimia atakapokutana naye.*
*(ii) Ataitikia wito wake atakapomkaribisha.*
*(iii) Atakapopiga chafya na kusema "**Al-hamdulillah**" atamuitikia (kwa kusema: **Rahmaka (ki) llaaahu**)*
*(iv) Atamuangalia atakapokuwa mgonjwa.*
*(v) Atafuata jeneza lake atakapokufa na*
*(vi) Atampendelea kile anachokipendelea yeye.*
*(Tirmidh).*

Pia Hadithi ifuatayo inatuonesha umuhimu wa kushiriki katika mazishi:

*Abu Hurairah (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: "Atakayefuata jeneza la Muislamu akiwa na imani na matarajio ya kupata malipo (kwa Allah) na hubakia na jeneza hiyo mpaka atakapoisualia maiti na kisha akamalizia mazishi yake, bila shaka atarudi na malipo Qirat (malipo makubwa), kila qirat ni sawa na mlima wa Uhud. Na yule atakayeiswalia na akaondoka kabla ya mazishi, bila shaka atarudi na*

*Qirat moja". (Bukhari na Muslim).*

Kinachosisitizwa katika Hadithi hii ni kwamba kushiriki katika mazishi ni jambo muhimu kwa Muislamu. Pia Mtume (s.a.w) amesisitiza kuwa mtu azikwe mapema iwezekanavyo kama Hadithi ifuatayo inavyotufahamisha:

*Huswayu bin Wahwal (r.a) amesimulia kuwa Talha bin Bara'a (r.a) aliugua. Hivyo Mtume (s.a.w) alikuja kumwona akasema:"Hakika simwoni Talha ila kifo kimeshampitia.Kwa hiyo nipeni amri juu yake (yaani niruhusuni nimswalie na kumzika) na fanyeni haraka si vizuri (si sawa) maiti ya Muislamu kungojeleshwa juu ya migongo ya watu wa familia yake". (Abu Daud).*



Mahali pa kuzikia ni kaburini. Kaburi linatakiwa liwe na upana na kina cha kutosha kiasi cha kutoweza kufukuliwa na mnyama au harufu kusikika. Ni Sunnah liwe refu kiasi cha kusimama mtu na kunyoosha mikono. Baada ya shimo la kaburi kukamilika, pachimbwe kishimo chenye urefu sawa na urefu wa maiti na upana, na kina chake kiwe na ukubwa kuienea maiti itakapolazwa kiubavu.Shimo hili dogo ndani ya shimo kubwa huitwa mwanandani. Kama ardhi ni ngumu sana, shimo la mwanandani linaweza kuchimbwa kwa kutoboa pembeni.

Utaratibu wa kuzika ni kama ifuatavyo:

1. Wateremke watu kaburini wenye idadi ya witri watatu, watano.
2. Jeneza liwekwe upande itakapokuwa miguu ya maiti.
3. Maiti atolewe kwa kutanguliza kichwa.
4. Maiti atakapoingizwa ndani ya kaburi, wapokeaji watamuweka magotini na kufungua kamba au vitanzi vyote vitatu vya miguuni, tumboni na kichwani. Pia watafunua shavu la kulia ili liguse ardhini wakati maiti itakapolazwa.



***Kielelezo:***
*Maiti ikipokelewa kaburini na kufunguliwa vitanzi.*

5. Maiti atalazwa kwa ubavu wa kulia katika mwanandani na kuelekezwa Qibla. Wakati wa kumlaza ni sunnah kusema maneno yaliyoelezwa katika Hadith iliyosimuliwa na Ibn Umar (r.a) kuwa Mtume (s.a.w) alipokuwa akizika alikuwa akisema:

بِسْمِ اللهِ وَبِ اللهِ وَ عَلَى مِلَّةِ رَسُوْلُ اللهِ

**Bismillahi wabillahi wa-'alaa millati Rasuulullahi**

*"Kwa jina la Allah na kwa uwezo wa Allah na kwa mujibu wa mwenendo wa Mtume wa Allah". (Ahmad, Tirmidh, Ibn Majah)*

6. Maiti apindwe kidogo miguuni na kichwani kwa kiasi ambacho uso na miguu iwe imegusa kuta za mwanandani.Kifua, tumbo na sehemu nyingine za katikati zibinuliwe nyuma kidogo.

7. Maiti awekewe mawe nyuma ya kichwa na nyuma ya miguu ili isije binuka na kukaa visivyo. Kisha ni sunnah kusoma aya za Qur-an kama iliyoelekezwa katika Hadith ifuatayo:

*Abdullah bin Umar (r.a) anasimulia kuwa amemskikia Mtume (s.a.w) akisema "wakati mmoja wenu atakapokufa, msimcheleweshe, bali mzikeni haraka haraka. Msomeeni aya 1-5 ya Sura ya pili au aya mbili za mwisho wa Suratul Baqara - 2:285-286)". (Baihaqi).*

kwa ubao, na kama patakuwa na sehemu zilizo wazi kiasi cha kuruhusu udongo kumfikia maiti zisiribwe kwa majani.

9. Kabla kaburi haijafunikwa, vitupiwe viganja vitatu vya udongo na katika kila tupio ni Sunnah kusema:

*Mara ya kwanza:*
***Minhaa khalaq-naakum*** مِنْهَا خَلَقْنَاكُمْ
*"Katika hii (ardhi) tumekuumbeni"*

*Mara ya Pili:*
***Wafiihaa nu'iidukum*** وَفِيهَا نُعِيدُكُمْ
*"Na humo tutakurudisheni"*

*Mara ya Tatu:* وَمِنْهَا نُخْرِجُكُمْ تَارَةً أُخْرَىٰ
***Waminhaa nukhrijukum taaratan-ukhrda***
*"Na kutoka humo tutakutoeni mara nyingine". (20:55)*

10. Kaburi lijazwe mchanga mpaka lijae na kisha liinuliwe kidogo kiasi cha shubiri moja.Iwekwe alama kichwani na miguuni au ipandwe miti mibichi katika pembe za kaburi ili ibakie kuwa alama za kaburi hilo. Pia ni vizuri kumimina maji juu ya kaburi ili kuufanya udongo ushikamane na usipeperushwe na upepo. Ni haramu kulijengea kaburi kwa namna yoyote ile, kukaa juu yake, kuwasha taa juu yake na kulielekea wakati wa kuswali kwa ushahidi wa Hadith zifuatazo:

*Jabir (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amekataza kuyajengea makaburi au kuyajengea nyumba juu yake au kukaa juu yake. (Muslim).*

*Abu Marsad al-ghafariyyi ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema:Msikae juu ya makaburi na wala msiswali kwa kuyaelekea". (Muslim).*

Baada ya kuzika Mtume(s.a.w) alikuwa akisimama baina ya kaburi na kaburi na kusema:

*Muombeeni msamaha ndugu yenu na mumuombee awe na kauli thabiti, kwani sasa anaulizwa.*

**Yaliyo muhimu kuyafanya baada ya mazishi** ni kuwashika wafiwa mikono na kuwausia kusubiri kwani kutokewa na msiba ni jambo la kawaida la maumbile na pia ni mtihani kwetu na watakaofaulu mtihani

huu ni wale watakao subiri ambao wanapopata msiba husema:

إِنَّا لِلَّهِ وَإِنَّآ إِلَيْهِ رَٰجِعُونَ ﴿١٥٦﴾

*"Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu na kwake yeye tutarejea". (2:155-156).*

## Zoezi la Pili

1. (a) Ni ipi tafauti iliyopo katika maana ya swala kilugha na kisheria

(b) Nukuu aya za Qur,an ambazo Allah(s.w) ametaja ndani yake vipimo vya kukubalika swala ya mja, na kufuzu.

(c) Hapana shaka kuwa kuswali kunatafautiana sana na kusimamisha swala, je ni kigezo kipi kilichobainishwa kwenye Qur,an kinachompambanua mja anayesimamisha swala na yule anayeswali?

2. (a) Lengo la kusimamisha swala ni kumzuilia mja na mambo maovu na machafu, eleza mambo ya msingi utakayozingatia kuyatekeleza kabla ya kuswali ili kufikia lengo hilo.

(b) Tumia ushahidi wa Qur,an na Hadithi kuonesha sababu zinazomfanya muislamu yeyote baleghe, asiwe na udhuru au dharura ya kuacha kusali swala ya faradhi kutokana na hali ya ukame,ugonjwa, safari au vita.

(c) Amri ya Allah kuwataka wanawake wa kiislamu wajisitiri, haiishii msikitini wakati wa kusali tu, bali kila penye watu wasiokuwa maharimu zao. Eleza ni kwanini, kwa kutumia ushahidi wa Qur,an na Hadithi za Mtume(s.a.w)

(d)( *"Swala ndio ufunguo wa peponi na ufunguo wa swala ni Twahara" (Mtume(s.a.w))*. mambo yepi ya kuzingatia na kutekeleza ili kuwa Twahara kwa ajili ya swala?

3. (a) Adhana ni wito wenye ujumbe mzito sana kwa Waislamu minghairi ya kengele, mbiu(ngoma) au tarumbeta. Kwa kuzingatia maneno ya adhana, thibitisha ukweli huu kwa kuorodhesha mafundisho yaliyomo ndani ya adhana.

(b) *(Swalini kama mlivyoniona nikiswali (Mtume(s.a.w))*
Eleza hatua kwa hatua namna Mtume alivyoswali.
(c) Orodhesha tafauti tatu baina ya ***Sijdatul-Tilawat*** na ***Sijidat-Sah-wi*** .
(d) Taja mafunzo makubwa mawili ya kiuongozi yanayopatikana katika ***Sijidat-Sah-wi*** wakati wa swala ya jamaa.

4. (a) Soma Qur,an {73:1-6}, {17:79}, {25:64}, {39:9}, {32:15-17}, {51:15-18}, na {3:16-17}. Kwa kuzingatia ujumbe wa aya hizi, eleza ni kwanini ni muhimu sana kwako kuswali Tahajjud, na kuwaelimisha Waislamu wengine wafanye hivyo?
(b) Bainisha tafauti na mfanano uliopo baina ya swala ya Jeneza na swala ya Id-lfitr.
(c) Orodhesha kwa mfuatano Sunnat Muakaddah zote zinazoambatana na swala tano za faradhi.

5. Allah(s.w) amesema kuwa: *"Popote mlipo mauti yatakufikieni, na hata mkiwa katika ngome madhubuti..." (4:78).*
(a) Mtu anayekaribia kufa anapaswa kufanyiwa mambo gani?
(b) Ni mambo gani ya faradhi ambayo Waislamu watapaswa kukufanyia wewe pindi utakapokuwa maiti leo au kesho?
(c) Onyesha kwa vitendo hatua kwa hatua, namna ya kuosha, kukafini, kuswalia na kuzika maiti ya muislamu.

6. *"..Na simamisha swala, Hakika swala humzuia (mtu na) maovu na mambo machafu..." (29:45)*
(a)Ainisha mafunzo au manufaa mengine matano wanayotakiwa kuyapata waislamu wanaosimamisha swala tano za faradhi kwa jamaa.
(b) Kuna baadhi ya Waislamu, pamoja na kutekeleza swala za faradhi na Sunnah, bado wamezama pamoja na wenye kuzama katika maovu na mambo machafu. Kwanini waislamu hawa wanakuwa hivyo?

****************************

## Sura ya Tatu

# ZAKAT NA SADAQAT

### Maana ya Zakat

**Kilugha**: Katika lugha ya Kiarabu neno "zakat" lina maana ya utakaso (*Purification*). Neno "Zakat" limetumika katika Qur'an kwa maana hii katika aya zifuatazo:

*"Bila shaka amefuzu aliyeitakasa (nafsi yake)" (91:9).* قَدْ أَفْلَحَ مَن زَكَّىٰهَا ﴿٩﴾

*"Hakika ameshafuzu aliyejitakasa (na mabaya)" (87:14).* قَدْ أَفْلَحَ مَن تَزَكَّىٰ ﴿١٤﴾

**Kisheria**: Katika sheria ya Kiislamu "Zakat" ni sehemu ya mali ya tajiri (2.5% au 1/40) anayoitoa kwa kutekeleza amri ya Allah (s.w) na kuwapa wanaostahiki, baada ya kupindukia mwaka au baada ya mavuno iwapo mali hiyo imefikia **Nisaab.** Nisaab ni kima cha chini cha mali ambacho mtu akiwa nacho au zaidi yake analazimika kutoa Zakat.

### Maana ya Sadaqa

**Kilugha:** Katika lugha ya Kiarabu neno "Sadaqa" linatokana na "Sidiq" lenye maana ya ukweli.

**Kisheria:** Katika sheria ya Kiislamu Sadaqat ni mali au huduma iinayotolewa au kupewa mtu yoyote anayehitajia kwa ihsani tu bila ya kutarajia malipo yoyote kutoka kwake. Maana ya "Sadaqat" inabainishwa vizuri katika Hadithi zifuatazo:

*1. Jabir na Hudhaifa (r.a) wameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: Kila kitendo kizuri ni Sadaqat". (Bukhari na Muslim).*

*2. Abu Hurairah (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: Katika kila kiungo cha mtu kuna Sadaqat. Kuna Sadaqat katika kila mtu. Kufanya uadilifu kati ya watu wawili ni sadaqat; kumsaidia mtu kupanda mnyama wake anayesafiri naye au kumsaidia mtu kutwika mzigo wake ni sadaqat; neno zuri ni sadaqat na kila hatua mtu anayotembea kwenda kwenye swala ni sadaqat na kuondoa kitu kibaya njiani ni sadaqat". (Bukhari na Muslim).*

**Msisitizo wa Utoaji wa Zakat na Swadaqat katika Uislamu**

1. Kutoa Zakat ni faradhi na nguzo ya tatu ya Uislamu. Amri ya kutoa Zakat ya vile Allah (s.w) alivyoturuzuku iko wazi katika Qur'an. Hebu turejee aya chache zifuatazo:

قُل لِّعِبَادِيَ ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ يُقِيمُواْ ٱلصَّلَوٰةَ وَيُنفِقُواْ مِمَّا رَزَقۡنَٰهُمۡ سِرّٗا
وَعَلَانِيَةٗ مِّن قَبۡلِ أَن يَأۡتِيَ يَوۡمٞ لَّا بَيۡعٞ فِيهِ وَلَا خِلَٰلٌ ﴿٣١﴾

*Waambieni waja wangu walioamini, wasimamishe Swala na watoe katika vile tulivyowaruzuku, kwa siri na kwa dhahiri, kabla haijafika siku isiyokuwa na (msaada unaopatikana kwa) kujikomboa wala urafiki (14:31).*

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓاْ أَنفِقُواْ مِمَّا رَزَقۡنَٰكُم مِّن قَبۡلِ أَن يَأۡتِيَ يَوۡمٞ لَّا بَيۡعٞ
فِيهِ وَلَا خُلَّةٞ وَلَا شَفَٰعَةٞۗ وَٱلۡكَٰفِرُونَ هُمُ ٱلظَّٰلِمُونَ ﴿٢٥٤﴾

*Enyi mlioamini! Toeni katika vile tulivyokupeni kabla haijafika siku ambayo hapatakuwa kujikomboa wala urafiki (wa kusaidiana) wala uombezi. Na waliokufuru ndio waliojidhulumu (kweli kweli). (2:254).*

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓاْ أَنفِقُواْ مِن طَيِّبَٰتِ مَا كَسَبۡتُمۡ وَمِمَّآ
أَخۡرَجۡنَا لَكُم مِّنَ ٱلۡأَرۡضِۖ

*"Enyi mllioamini! Toeni katika vile vizuri mlivyovichuma, na katika vile tulivyokutoleeni katika ardhi..." (2:267).*

2. Utoaji wa Zakat na Sadaqat ndio kitambulisho cha Uislamu na Ucha-Mungu wa mtu kama tunavyojifunza katika Qur-an:

ذَٰلِكَ ٱلۡكِتَٰبُ لَا رَيۡبَۛ فِيهِۛ هُدٗى لِّلۡمُتَّقِينَ ﴿٢﴾ ٱلَّذِينَ يُؤۡمِنُونَ بِٱلۡغَيۡبِ
وَيُقِيمُونَ ٱلصَّلَوٰةَ وَمِمَّا رَزَقۡنَٰهُمۡ يُنفِقُونَ ﴿٣﴾

*Hiki ni Kitabu kisichokuwa na shaka ndani yake, ni uwongozi kwa wamchao Mwenyezi Mungu. Ambao huyaamini yasiyoonekana (maadam yamesemwa na Mwenyezi Mungu na Mtume wake) na husimamisha Sala na hutoa katika yale tuliyowapa. (2:2-3).*

۞ لَّيْسَ ٱلْبِرَّ أَن تُوَلُّوا۟ وُجُوهَكُمْ قِبَلَ ٱلْمَشْرِقِ وَٱلْمَغْرِبِ
وَلَٰكِنَّ ٱلْبِرَّ مَنْ ءَامَنَ بِٱللَّهِ وَٱلْيَوْمِ ٱلْءَاخِرِ وَٱلْمَلَٰٓئِكَةِ وَٱلْكِتَٰبِ
وَٱلنَّبِيِّۦنَ وَءَاتَى ٱلْمَالَ عَلَىٰ حُبِّهِۦ ذَوِى ٱلْقُرْبَىٰ وَٱلْيَتَٰمَىٰ وَٱلْمَسَٰكِينَ
وَٱبْنَ ٱلسَّبِيلِ وَٱلسَّآئِلِينَ وَفِى ٱلرِّقَابِ وَأَقَامَ ٱلصَّلَوٰةَ وَءَاتَى ٱلزَّكَوٰةَ
وَٱلْمُوفُونَ بِعَهْدِهِمْ إِذَا عَٰهَدُوا۟ ۖ وَٱلصَّٰبِرِينَ فِى ٱلْبَأْسَآءِ وَٱلضَّرَّآءِ
وَحِينَ ٱلْبَأْسِ ۗ أُو۟لَٰٓئِكَ ٱلَّذِينَ صَدَقُوا۟ ۖ وَأُو۟لَٰٓئِكَ هُمُ ٱلْمُتَّقُونَ ﴿١٧٧﴾

*Sio wema (tu huo peke yake) kuwa mnaelekeza nyuso zenu upande wa Mashariki na Magharibi (katika kusali,. Yako na mema mengine). Bali wema (hasa) ni (wa wale) wanaomwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho na Malaika na Kitabu na Manabii, na wanawapa mali juu ya kuwa wanayapenda - jamaa na mayatima na maskini na wasafiri (walioharibikiwa) na waombao na katika (kuwakomboa) watumwa, na wakawa wanasimamisha sala na kutoa zaka, na watekelezao ahadi zao wanapoahidi, na wavumiliao katika shida na dhara na (katika) wakati wa vita; hao ndio waliosadikisha (Uislamu wao); na hao ndio wamchao Mungu. (2:177)*

Tunajifunza kutokana na aya hizi kuwa utoaji mali kwa ajili ya Allah ni miongoni mwa matendo yanayompelekea mtu kuwa Mcha-Mungu. Kwa ujumla Qur-an inapotaja sifa za waumini huwa ni pamoja na watoao Zakat. Kama tunavyojifunza katika aya ifuatayo:

وَٱلْمُؤْمِنُونَ وَٱلْمُؤْمِنَٰتُ بَعْضُهُمْ أَوْلِيَآءُ بَعْضٍ ۚ يَأْمُرُونَ بِٱلْمَعْرُوفِ
وَيَنْهَوْنَ عَنِ ٱلْمُنكَرِ وَيُقِيمُونَ ٱلصَّلَوٰةَ وَيُؤْتُونَ ٱلزَّكَوٰةَ وَيُطِيعُونَ ٱللَّهَ
وَرَسُولَهُۥٓ ۚ أُو۟لَٰٓئِكَ سَيَرْحَمُهُمُ ٱللَّهُ ۗ إِنَّ ٱللَّهَ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٧١﴾

*Na wanaoamini wanaume na wanaoamini wanawake, ni marafiki wao kwa wao. Huyaamrisha yaliyo mema na huyakataza yaliyo mabaya, na husimamisha sala na hutoa Zakat na humtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Hao ndio ambao Mwenyezi Mungu atawarehemu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu na Mwenye Hikima. (9:71).*

3. Utoaji mali kwa ajili ya Allah (s.w) ni miongoni mwa mambo makubwa ya kumpelekea mja kufuzu hapa duniani na huko akhera kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

قَدْ أَفْلَحَ ٱلْمُؤْمِنُونَ ﴿١﴾ ٱلَّذِينَ هُمْ فِى صَلَاتِهِمْ خَٰشِعُونَ ﴿٢﴾

وَٱلَّذِينَ هُمْ عَنِ ٱللَّغْوِ مُعْرِضُونَ ﴿٣﴾ وَٱلَّذِينَ هُمْ لِلزَّكَوٰةِ فَٰعِلُونَ ﴿٤﴾

*Hakika wamefuzu Waislamu. Ambao katika sala zao huwa ni wanyenyekevu. Na ambao hujiepusha na mambo ya upuuzi. Na ambao (nguzo ya) Zakat wanaitekeleza. (23:1-4).*

وَبَشِّرِ ٱلْمُخْبِتِينَ ﴿٣٤﴾ ٱلَّذِينَ إِذَا ذُكِرَ ٱللَّهُ وَجِلَتْ قُلُوبُهُمْ
وَٱلصَّٰبِرِينَ عَلَىٰ مَآ أَصَابَهُمْ وَٱلْمُقِيمِى ٱلصَّلَوٰةِ وَمِمَّا رَزَقْنَٰهُمْ
يُنفِقُونَ ﴿٣٥﴾

*"..Na wabashirie wanyenyekevu ambao anapotajwa Allah nyoyo zao hutetemeka na wanavumilia juu ya yale yanayowasibu na wanasimamisha swala na katika vile tulivyowapa wanatoa" (22:34-35).*

ٱلَّذِينَ يُنفِقُونَ أَمْوَٰلَهُم بِٱلَّيْلِ وَٱلنَّهَارِ سِرًّا وَعَلَانِيَةً فَلَهُمْ أَجْرُهُمْ
عِندَ رَبِّهِمْ وَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿٢٧٤﴾

*"Wale watoao mali zao usiku na mchana kwa siri na dhahiri, wana ujira wao kwa Mola wao, wala haitakuwa khofu juu yao wala hawatahuzunika". (2:274).*

4. Kutotoa mali kwa ajili ya Allah ikiwa ni pamoja na Zakat na Sadaqat ni jambo mojawapo kubwa litakalomfanya mja afeli katika maisha yake ya hapa duniani na ya huko akhera hata kama atajiita Muislamu na kutekeleza baadhi ya matendo mengine ya Kiislamu. Adhabu watakayoipata wale wenye kufanya ubakhili na kujizuilia wasitoe katika njia ya Allah (s.w) na huku wana uwezo, imewekwa bayana katika Qur'an na Hadithi. Hebu tuzingatie aya chache zifuatazo:

وَٱلَّذِينَ يَكۡنِزُونَ ٱلذَّهَبَ وَٱلۡفِضَّةَ وَلَا يُنفِقُونَهَا فِي سَبِيلِ
ٱللَّهِ فَبَشِّرۡهُم بِعَذَابٍ أَلِيمٖ ﴿٣٤﴾ يَوۡمَ يُحۡمَىٰ عَلَيۡهَا فِي نَارِ
جَهَنَّمَ فَتُكۡوَىٰ بِهَا جِبَاهُهُمۡ وَجُنُوبُهُمۡ وَظُهُورُهُمۡۖ هَٰذَا
مَا كَنَزۡتُمۡ لِأَنفُسِكُمۡ فَذُوقُواْ مَا كُنتُمۡ تَكۡنِزُونَ ﴿٣٥﴾

*"Na wale wakusanyao dhahabu na fedha wala hawazitoi katika njia ya Allah, wape habari ya adhabu iumizayo. Siku (mali yao) yatakapotiwa moto wa Jahannam na kwa hayo vikachomwa vipaji vya nyuso zao na mbavu na migongo yao(na huku wanaambiwa):"Haya ndiyo (yale mali) mliojilimbikizia nafsi zenu, basi onjeni yale mliyokuwa mkiyakusanya". (9:34-35).*

وَأَمَّا مَنۢ بَخِلَ وَٱسۡتَغۡنَىٰ ﴿٨﴾ وَكَذَّبَ بِٱلۡحُسۡنَىٰ ﴿٩﴾ فَسَنُيَسِّرُهُۥ لِلۡعُسۡرَىٰ

*Na afanyae ubakhili, asiwe na haja ya viumbe wenzake. Na akakadhibisha mambo mema (asiyafanye) tutamsahilishia njia ya kwendea Motoni (92:8-10).*

Hebu pia tuzingatie Hadithi inayotufahamisha juu ya adhabu itakayowafikia wale wanaoyafanyia ubakhili yale aliyowaruzuku Allah (s.w).

*Abu Hurairah (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: "Yule ambaye Allah (s.w) amempa mali lakini haitolei Zakat, mali yake itageuzwa kuwa nyoka mkubwa (mwenye sumu kali). Ataviringwa shingoni mwake katika siku ya Hisabu na kuanza kumuuma. Baadaye nyoka huyo atasema: "Mimi ni mali yako, mimi ni hazina yako iliyohifadhiwa". Kisha Mtume alisoma (aya ifuatayo): "Wala usiwaone wale ambao wamefanya*

*ubakhili katika yale aliyowapa Mwenyezi Mungu katika fadhila zake kuwa ni bora kwao. La, ni vibaya kwao. Watafungwa kongwa (madude ya kunasa shingoni) za yale waliyoyafanyia ubakhili- siku ya Kiyama. Na urithi wa mbingu na ardhi ni wa Mwenyezi Mungu. na Mwenyezi Mungu ana habari za mnayoyafanya" (3:180). (Bukhari).*

**Masharti ya Utoaji wa Zakat na Swadaqat**

Utoaji katika njia ya Allah (s.w) ni ibada ambayo hukamilika kwa kuzingatia masharti yafuatayo:

(1) Kutoa vilivyo halali
(2) Kutoa vilivyo vizuri
(3) Kutoa kwa kati na kati
(4) Kujiepusha na ria na kufuatilia kwa masimbulizi
(5) Kuwapa wanaostahiki.

**1. Kutoa vilivyo halali**

Sharti ya kwanza ya kutoa katika njia ya Allah (s.w) ni kutoa kilichochumwa au kilichopatikana kwa njia ya halali. Mali ya haramu ni najisi na ni sumu kwa nafsi zetu. Kumlisha mtu chakula cha haramu ni kama kumlisha sumu. Ukimlisha mtu mali ya haramu utakuwa umefanya makosa mawili mbele ya Allah (s.w), kwanza, umedhulumu mali uliyoipata kwa njia ya haramu na pili umemdhulumu mtu kwa kumlisha haramu. Kula chumo la haramu kumefananishwa na kula moto:

إِنَّ ٱلَّذِينَ يَأْكُلُونَ أَمْوَٰلَ ٱلْيَتَٰمَىٰ ظُلْمًا إِنَّمَا يَأْكُلُونَ فِى بُطُونِهِمْ
نَارًا ۖ وَسَيَصْلَوْنَ سَعِيرًا ﴿١٠﴾

*"Hakika wale wanaokula mali ya yatima kwa dhuluma, bila shaka wanakula moto matumboni mwao, na wataungua katika huo moto uwakao". (4:10).*

Aidha, Allah (s.w) hapokei mali itokanayo na uchumi haramu wala hapokei ibada ya mtu ambaye anaishi kutokana na chumo haramu kama tunavyojifunza katika Hadith zifuatazo:

*Abu Hurairah amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: Enyi watu Allah ni mzuri na kwa hiyo hakubali ila vilivyo vizuri tu.*

Na Allah ameamrisha waumini kama alivyowaamrisha Mitume wake kwa kuwaambia:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلرُّسُلُ كُلُوا۟ مِنَ ٱلطَّيِّبَٰتِ وَٱعْمَلُوا۟ صَٰلِحًا ۖ إِنِّى بِمَا تَعْمَلُونَ عَلِيمٌ

*Enyi Mitume! Kuleni vyakula vizuri na fanyeni mema, hakika mimi ni Mjuzi wa (yote) mnayoyatenda" (23:51).*

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا كُلُوا مِنْ طَيِّبَاتِ مَا رَزَقْنَاكُمْ

*Na Allah amesema: Enyi mlioamini! Kuleni vizuri tulivyokuruzukuni..." (2:172)*

*Kisha Mtume akaeleza juu ya mtu aliyesafiri safari ndefu mpaka nywele zake zikanyonyoka (kwa taabu na dhiki ya safari) na kufunikwa na vumbi. (Katika hali hii ya dhiki) akainua mikono yake mbinguni (na kuomba) Ee Allah! Ee Allah! ambapo chakula chake ni haramu, na kinywaji chake ni haramu na mavazi yake ni haramu, na siha yake ni haramu (imejengeka kwa chumo haramu), itawezekanaje sasa dua yake ikubaliwe? (Muslim).*

*Ibn Umar(r.a) ameeleza kuwa amesikia Mtume (s.a.w) akisema: Atakayenunua nguo kwa dirham kumi, ambapo dirhamu moja ni haram (imepatikana kwa njia ya haramu) Allah hatazikubali swala zake pindi atakapokuwa anasali na nguo hiyo" (Ahmad, Baihaq).*

**3. Kutoa vilivyo vizuri**

Tunapotoa kwa ajili ya Allah (s.w) hatuna budi kutoa vilivyo vizuri kama inavyosisitizwa katika aya zifuatazo:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا أَنْفِقُوا مِنْ طَيِّبَاتِ مَا كَسَبْتُمْ وَمِمَّا
أَخْرَجْنَا لَكُمْ مِنَ الْأَرْضِ ۖ وَلَا تَيَمَّمُوا الْخَبِيثَ مِنْهُ تُنْفِقُونَ وَلَسْتُمْ
بِآخِذِيهِ إِلَّا أَنْ تُغْمِضُوا فِيهِ ۚ وَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ غَنِيٌّ حَمِيدٌ ﴿٢٦٧﴾

*Enyi mlioamini! toeni katika vile vizuri mlivyovichuma, na katika vile tulivyokutoleeni katika ardhi. Wala msikusudie kutoa vilivyo vibaya, hali nyinyi wenyewe msingevipokea isipokuwa kwa kutoviangalia (Basi Mwenyezi Mungu atapokea kibaya)? Basi jueni kwamba Mwenyezi Mungu ni Mkwasi Asifiwaye. (2:267).*

لَنْ تَنَالُوا الْبِرَّ حَتَّىٰ تُنْفِقُوا مِمَّا تُحِبُّونَ ۚ وَمَا تُنْفِقُوا مِنْ شَيْءٍ
فَإِنَّ اللَّهَ بِهِ عَلِيمٌ ﴿٩٢﴾

*Hamtaweza kuufikia wema (khasa) mpaka mtoe katika vile mnavyovipenda na chochote mnachokitoa, basi hakika Mwenyezi Mungu anakijua (3:92).*

**4. Kutoa kwa kati na kati**

Muislamu anatakiwa atoe kiasi ambacho hakitamuathiri yeye pamoja na familia yake. Anatakiwa atoe kwa kipimo, atoe kila kilicho ziada ya matumizi muhimu ya maisha.Utoaji wa sadaqa hauna kiwango maalum wala nisaab, hivyo umeachwa huru ili tutoe kulingana na haja iliyopo huku tukizingatia maelekezo ya Allah (s.w) katika aya zifuatazo:

وَيَسْـَٔلُونَكَ مَاذَا يُنفِقُونَ قُلِ ٱلْعَفْوَ ۗ كَذَٰلِكَ
يُبَيِّنُ ٱللَّهُ لَكُمُ ٱلْـَٔايَٰتِ لَعَلَّكُمْ تَتَفَكَّرُونَ ﴿٢١٩﴾

*"... Na wanakuuliza watoe nini sema: 'Vilivyokuzidieni'. Namna hivi Mwenyezi Mungu anakubainishieni aya (Zake) mpate kufikiri". (2:219).*

وَلَا تَجْعَلْ يَدَكَ مَغْلُولَةً إِلَىٰ عُنُقِكَ وَلَا تَبْسُطْهَا
كُلَّ ٱلْبَسْطِ فَتَقْعُدَ مَلُومًا مَّحْسُورًا ﴿٢٩﴾

*Wala usifanye mkono wako kama uliofungwa shingoni mwako, wala usiukunjue ovyo ovyo, utakuwa ni mwenye kulaumiwa na kufilisika (ukiukunjua ovyo ovyo)" (17:29).*

**5. Kujiepusha na ria na kufuatilia kwa masimbulizi**

Kutoa kwa ria ni kutoa ili kujionyesha kwa watu na ili usifiwe. Pia tunakatazwa kufuatilia kile tulichokitoa kwa masimbulizi. Kusimbulia ni kwa mfano, kuwaambia watu wasiohusika kabisa, kuwa kila kitu alichonacho fulani ni mimi niliyempa.Allah (s.w) hapokei mali iliyotolewa kwa ria au iliyofuatiliwa kwa masimbulizi kama inavyobainika katika aya ifuatayo:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ لَا تُبْطِلُوا۟ صَدَقَٰتِكُم بِٱلْمَنِّ وَٱلْأَذَىٰ كَٱلَّذِى يُنفِقُ
مَالَهُۥ رِئَآءَ ٱلنَّاسِ وَلَا يُؤْمِنُ بِٱللَّهِ وَٱلْيَوْمِ ٱلْءَاخِرِ ۖ فَمَثَلُهُۥ كَمَثَلِ صَفْوَانٍ
عَلَيْهِ تُرَابٌ فَأَصَابَهُۥ وَابِلٌ فَتَرَكَهُۥ صَلْدًا ۖ لَّا يَقْدِرُونَ عَلَىٰ شَىْءٍ مِّمَّا

كَسَبُوا۟ ۗ وَٱللَّهُ لَا يَهْدِى ٱلْقَوْمَ ٱلْكَٰفِرِينَ ﴿٢٦٤﴾

*"Enyi mlioamini! Msiharibu sadaka zenu kwa masimbulizi na udhia; kama yule anayetoa mali yake kwa kuwaonyesha watu, wala hamwamini Mwenyezi Mungu wala siku ya mwisho. Basi hali yake ni kama hali ya jabali ambalo juu yake pana udongo kisha ikalifikia (jabali hili) mvua kubwa (ikasukuma udongo wote huo) na ikaliacha tupu. Basi hawatakuwa na uweza (wa kupata) chochote katika walivyovichuma; na Mwenyezi Mungu hawaongozi watu makafiri". (2:264).*

Ili kujiepusha na ria katika utoaji mali kwa ajili ya Allah (s.w) tunashauriwa katika Qur'an na Hadith kuwa ni vyema tutoe kwa siri kila iwezekanavyo hasa kwa Swadaqat na kuna malipo makubwa zaidi kwa wale wanaotoa kwa siri. Hebu turejee aya zifuatazo:

إِن تُبْدُوا۟ ٱلصَّدَقَٰتِ فَنِعِمَّا هِىَ ۖ وَإِن تُخْفُوهَا وَتُؤْتُوهَا ٱلْفُقَرَآءَ فَهُوَ خَيْرٌ
لَّكُمْ ۚ وَيُكَفِّرُ عَنكُم مِّن سَيِّـَٔاتِكُمْ ۗ وَٱللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرٌ ﴿٢٧١﴾

*Kama mkitoa Sadaqa kwa dhahiri ni vizuri; na mkitoa kwa siri na kuwapa mafakiri, basi ni ubora zaidi kwenu; na atakuondoleeni maovu yenu (mkifanya hivyo): na Mwenyezi Mungu anazo habari za (yote) mnayoyatenda. (2:271).*

ٱلَّذِينَ يُنفِقُونَ أَمْوَٰلَهُم بِٱلَّيْلِ وَٱلنَّهَارِ سِرًّا وَعَلَانِيَةً فَلَهُمْ أَجْرُهُمْ
عِندَ رَبِّهِمْ وَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿٢٧٤﴾

*Wale watowao mali zao usiku na mchana, kwa siri na dhahiri, wana ujira wao kwa Mola wao; wala haitakuwa khofu juu yao wala hawatahuzunika. (2:274).*

Pia Hadith ifuatayo inaonyesha ubora wa kutoa swadaqa kwa siri: *Abdullah bin Mas'ud (r.a) aliyesimulia Hadith hii ameeleza kuwa: "Kuna watu watatu ambao Allah anawapenda mtu anayeamka usiku kusoma Kitabu cha Allah, mtu anayetoa swadaqa kwa mkono wake wa kulia na kuuficha mkono wa kushoto (usiwe na habari); na mtu ambaye yuko katika kikosi vitani, akawa anawaendea maadui, japo wenzake wote wamekimbia" (Tirmidh).*

Kutokana na Hadith hii, tunaona umuhimu wa kutoa kwa siri. Kutoa kwa mkono wa kulia na mkono wa kushoto usiwe na habari ni kutoa kwa siri kwa kiasi ambacho, ikiwezekana, hata wale walio karibu sana nawe wasifahamu kuwa umetoa sadaqat kumpa fulani. Kutoa kwa siri humfanya mwenye kutoa aepukane na ria na humfanya mwenye kupokea ajisikie huru. Mtoaji Sadaqat akijificha asifahamike kabisa kwa mpokeaji ni vizuri zaidi.

### 6. Kuwapa wanaostahiki

Mtoaji wa Zakat na Sadaqat ni lazima awafahamu vyema wale wanaostahiki kupewa Zakat na Sadaqat. Tunahafamu kuwa Zakat na Sadaqat ni haki ya watu kupitia kwa matajiri. Hivyo, ni dhahiri kuwa kuchukua Zakat au Sadaqat na kumpa asiyestahiki ni kudhulumu haki za wale wanaostahiki. Kwa hiyo, Muislamu anaweza akatoa Zakat na Sadaqat na bado akastahiki ghadhabu za Allah (s.w.) badala ya kupata Radhi zake na malipo mema kutoka kwake, kwa kutoa mali yake na kuwapa wasiostahiki na kuwanyima haki zao wale wanaostahiki. Hii ni dhuluma iliyo wazi. Ili kuepukana na hatari hii hatuna budi kuwafahamu vyema wanaostahiki na wasiostahiki kupewa Zakat na Sadaqat.

۞ إِنَّمَا ٱلصَّدَقَٰتُ لِلْفُقَرَآءِ وَٱلْمَسَٰكِينِ وَٱلْعَٰمِلِينَ عَلَيْهَا وَٱلْمُؤَلَّفَةِ

قُلُوبُهُمْ وَفِى ٱلرِّقَابِ وَٱلْغَٰرِمِينَ وَفِى سَبِيلِ ٱللَّهِ وَٱبْنِ ٱلسَّبِيلِ ۖ فَرِيضَةً

مِّنَ ٱللَّهِ ۗ وَٱللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿٦٠﴾

*"Sadaqat hupewa (watu hawa): Mafakiri, Maskini, wanaozitumikia (wanaozikusanya na kuzigawanya) na wanaotiwa nguvu nyoyo zao (juu ya Uislamu),na katika kuwakomboa watumwa,na katika kuwasaidia wenye madeni, na katika njia ya Allah (s.w) na katika kuwapa wasafiri (walioharibikiwa). Ni faradhi inayotoka kwa Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi Mwenye hekima" (9:60).*

Japo aya hii imeanza na neno Swadaqat, mgawanyo ulioelezwa hapo umekusudiwa mgawanyo wa Zakat kutokana na msisitizo uliopo mwishoni mwa aya hii: *"Ni faradhi inayotoka kwa Mwenyezi Mungu"*. Tunafahamu kuwa Zakat ni faradh na Swadaqat ni wajibu au sunna iliyokokotezwa. Kama ilivyo katika aya hii Zakat inastahiki igawanywe katika mafungu manane yafuatayo:

**(a) Fukara**

Fukara ni kundi la wale wasiojiweza kabisa kumudu maisha yao bila ya msaada kutoka kwa wenziwao katika jamii. Hawa hupangiwa fungu la Zakat ili kuhakikisha kuwa wanapata mahitaji ya maisha yao ya kila siku ikiwa ni pamoja na chakula, mavazi, makazi na mahitajio mengine muhimu ya Mwanaadamu. Ni lazima Waislamu waunde utaratibu mzuri wa ugawaji wa Zakat ili pasiwe na yeyote katika hawa wasiojiweza kabisa anayekosa baadhi ya mahitajio muhimu ya maisha.

Ufukara unaotokana na maumbile au uzee ni wa kudumu au wa muda mrefu, lakini kuna fukara wengine wa muda mfupi ambao pia katika hali hiyo ya ufukara wanahitaji kusaidiwa kutokana na fungu la Zakat. Hawa ni pamoja na watu waliopatwa na ajali kama vile kuunguliwa nyumba na vyote vilivyokuwemo. Kwa ujumla Muislamu anapokabiliwa na matatizo ya wazi yaliyomtokea nje ya uwezo wake na akawa hana uwezo wa kupata kabisa mahitaji muhimu ya maisha yake na wale anaowaangalia, asaidiwe kwa fungu la Zakat mpaka hapo atakapopata tena uwezo wa kuyamudu maisha.

**(b) Masikini**

Kutokana na maelekezo ya Qur'an na Hadith, maskini ni wale ambao ukiwaangalia haraka haraka katika hali zao za nje bila ya kuwaangalia kwa undani, utawadhania kuwa wanao uwezo wa kujipatia mahitaji muhimu ya maisha kwa vile hawana kilema chochote kinachoonekana kwa nje na hawaombi (kama ni Waislamu kweli kweli). Lakini ukweli ni kwamba maskini hana uwezo wa kujitosheleza kwa mahitaji yake yote muhimu ya maisha bali ana uwezo wa kupata baadhi yake tu. Kwa mfano kama mahitaji yake muhimu ya maisha ni shilingi 1,000/= kwa siku,yeye ana uwezo wa kupata shilingi 400/= tu na inabidi aishi kwa dhiki bila ya shilingi 600/= zilizobakia. Katika Qur'an tunafahamishwa:

لِلْفُقَرَآءِ ٱلَّذِينَ أُحْصِرُوا۟ فِى سَبِيلِ ٱللَّهِ لَا يَسْتَطِيعُونَ ضَرْبًا فِى
ٱلْأَرْضِ يَحْسَبُهُمُ ٱلْجَاهِلُ أَغْنِيَآءَ مِنَ ٱلتَّعَفُّفِ تَعْرِفُهُم بِسِيمَٰهُمْ لَا
يَسْـَٔلُونَ ٱلنَّاسَ إِلْحَافًا ۗ وَمَا تُنفِقُوا۟ مِنْ خَيْرٍ فَإِنَّ ٱللَّهَ بِهِۦ عَلِيمٌ ﴿٢٧٣﴾

*(Wapewe hizo Sadaqat) Mafakiri waliozuiwa katika njia ya Mwenyezi Mungu, wasioweza kwenda huko na huko katika ardhi (kufanya kazi ya kutafuta riziki); asiyewajua hali zao anawadhania kuwa ni matajiri kwa sababu ya kujizuia kwao (na kuomba). Utawafahamu (kuwa wahitaji)*

*kwa alama zao (zinazooyesha ufakiri, lakini) hawawaombi watu wakafanya ung'ang'anizi. Na mali yoyote mnayoyatoa, basi kwa yakini Mwenyezi Mungu anayajua (atakulipeni) (2:273).*

Hivyo, kwa kuwa maskini si rahisi sana kumuona kwa kuwa hana alama ya nje kama fukara na wala hajitambulishi kwa kuomba, Waislamu wanatakiwa kujuana kwa hali zao na kila mmoja kuwa macho juu ya dhiki na huzuni za wengine ili kutoa msaada kila utakapohitajika. Kwani maskini hutambuliwa (hung'amuliwa) na wale wenye huruma na wanaojishughulisha na dhiki za Waislamu na wanaadamu wenziwao. Tumeamrishwa kuwasaidia wenzetu hawa ile asilimia sitini (60%) ya mahitajio yao muhimu ya maisha iliyobakia kwa kuwapa Zakat na Sadaqat.

### (c) Wanaozitumikia (Al-A'miliina A'laiha):

Wale wote watakaoshughulika katika ukusanyaji na ugawanyaji wa Zakat, ujira wao hutokana na hiyo hiyo Zakat. Kuwekwa fungu hili la Zakat ni ushahidi kuwa Zakat si ibada ya mtu binafsi au ibada ya matajiri tu bali ni ibada inayotakiwa itekelezwe na jamii yote kwa ujumla. Ni lazima jamii ya Waislamu iunde utaratibu wa ukusanyaji na ugawaji wa Zakat kama ilivyokuwa wakati wa Mtume Muhammad (s.a.w) na Makhalifa wake waongofu.

### (d) Wanaotiwa nguvu nyoyo zao juu ya Uislamu

Wanaohitaji kutiwa nguvu nyoyo zao ni wale Waislamu walioingia katika Uislamu katika siku za karibuni na kwa kiasi ambacho nyoyo zao hazijawa madhubuti katika Uislamu na huweza kuyumba wakati wowote wa dhiki. Haki ya kuwapa hawa Zakat iko wazi. Wakati mwingine kwa kuchukua uamuzi wa kuacha dini ya zamani na kujiunga na Uislamu huweza kumletea mtu matatizo ya kukosana na ndugu zake, marafiki zake na hata kukosa mali yake, matukio ambayo yatamuathiri sana katika maisha yake mapya. Kwa sababu hii Waislamu wanalazimika kumkaribisha mwenzao kwa kumtengea fungu maalum la Zakat na Sadaqat ili kumuonyesha udugu wa kweli wa Kiislamu na kumthibitishia moyoni mwake kuwa Uislamu ndio dini pekee inayomstahiki mwanaadamu. Tunao mfano mzuri kutoka kwa Mtume Muhammad (s.a.w). Katika vita vya Hunain Mtume (s.a.w) alitoa sehemu kubwa ya ngawira (vitu vilivyotekwa vitani) kuwapa maswahaba waliosilimu katika siku za karibuni. Ansar walipolalamika juu ya jambo hili, Mtume (s.a.w) alisema: "Watu hawa wameingia katika Uislamu sasa hivi baada ya kuacha kufru. Nataka nifariji mioyo yao".

Pia fungu hili linaweza kutumika katika kuwanunua maadui wa Waislamu ili wafute wazo la kupigana na Waislamu au katika kuwapa watu wanaoweza kuwashawishi maadui wa Waislamu wasipigane na Waislamu. Kitu muhimu mbele ya Uislamu na Waislamu ni amani, hivyo amani haina budi kutafutwa hata ikibidi kuinunua kwa namna hii kwa fungu la Zakat. Makhalifa wa Mtume walifanya hivi.

**(e) Kuwakomboa watumwa (Fir-riqaabu)**

Wakati Mtume (s.a.w) anahuisha Uislamu Uarabuni na duniani kote palikuwa na mtindo wa kijahili na ukandamizaji wa matajiri, watawala na wengine wenye uwezo wa kuwachukua watumwa kwa kuwanunua au kwa nguvu na kuwafanya watumwa wa kuwatumikia katika maisha yao yote bila ya malipo yoyote na bila ya uhuru. Uislamu unatufundisha kuwa wanaadamu wote wamezaliwa huru na hawapaswi kujidhalilisha kwa yeyote au kuutoa uhuru wao kwa yeyote asiyekuwa Allah (s.w), Aliye Bwana wao pekee . Hivyo Uislamu unalaani utumwa wa aina zote. Kufuatana na Hadithi ya Mtume (s.a.w), anayemfanya mwenziwe mtumwa, hata kama akijiita Muislamu mahali pake pa marejeo ni motoni. Mtume (s.a.w) ametoa onyo kali katika Hadithi ifuatayo:

> *Kuna watu wa aina tatu ambao mimi mwenyewe nitasimama kuwashitaki katika siku ya Hukumu; miongoni mwa hao ni yule anayemchukua mtu huru na kumfanya mtumwa na kumuuza... (Bukhari, Ibn Majah).*

Uislamu pamoja na kuukemea utumwa kiasi hicho, umewaamrisha Waislamu wawakomboe Waislamu wengine walio utumwani kwa kutoa kikomboleo kinachohitajika kutokana na Zakat na Sadaqat. Pia katika kundi hili ni pamoja na wafungwa wa kivita waliotekwa katika kupigania haki. Hawa nao watakombolewa kwa fungu hili la Zakat.

**(f)Kuwasaidia wadaiwa kulipa madeni yao**

Deni ni jambo linalochukuliwa kwa uzito mkubwa katika Uislamu. Inatakiwa Muislamu aingie katika deni inapokuwa hapana budi, na kamwe asithubutu kukopa wakati anao uwezo wa kuvumilia kuishi na hali ya upungufu wa mahitaji muhimu inayomkabili. Kukopa kwa ajili ya kutosheleza matamanio yasiyo ya muhimu katika maisha kumekatazwa. Dhambi kubwa inayofuatia madhambi makubwa ni kufa na deni kama tunavyofahamishwa katika hadithi ifuatayo:

> *Abu Musa ameeleza kutoka kwa Mtume (s.a.w) aliyesema: Hakika katika madhambi makubwa mtu atakayokwenda nayo mbele ya Allah baada*

*ya madhambi makubwa Allah aliyoyakataza ni mtu kufa na deni na ikawa hakuacha kitu cha kulipia deni hilo. (Ahmad, Abu Daud).*

Miongoni mwa dua za Mtume (s.a.w) ilikuwa hii ya kumuomba Allah (s.w) amkinge na madeni. Alikuwa akiomba:

*Ee Allah, Najikinga kwako kutokana na mtamanio (hamu na huzuni) kutokana na uzembe (ajizi na uvivu) kutokana na moyo mnyonge na ubakhili, kutokana na mzigo wa deni na kunyongeshwa na watu. (Bukhari na Muslim).*

Deni ni lazima lilipwe, ama hapa duniani au mbele ya Allah katika siku ya Hukumu. Kama mtu alikopa kwa shida ya wazi iliyomkabili na akashindwa kulipa katika wakati waliokubaliana na mdai, basi Waislamu wamsaidie kulipa deni hilo kwa fungu la Zakat na Sadaqat. Iwapo Waislamu hawatamlipia na akafa na deni hilo, basi Allah (s.w) atamlipia mwenyewe siku ya malipo.

### (g) Katika njia ya Allah (Fii-Sabilillah)

"*Katika njia ya Allah*" ni maneno yanayotumika kwa maana ya shughuli zote zinazofanywa kwa ajili ya kuhuisha Dini ya Allah na kusimamisha Ufalme wake hapa ulimwenguni. Kwa maana nyingine juhudi yoyote inayofanywa ili kuuwezesha Uislamu kusimama kama unavyostahiki inaingia katika uwanja huu wa *"Fii Sabilillah"*. Kwa hiyo aina zote za jihadi katika Uislamu - jihadi ya ulimi, jihadi ya kalamu na jihadi ya kitali (vita) zimo katika huu uwanja wa *"Fii Sabilillah"* na hasa fungu la Zakat limetengwa ili kuziendeleza kwa ufanisi jihadi hizi. Mtume (s.a.w) amesema kuwa hairuhusiwi kumpa Zakat mtu aliye tajiri lakini kama tajiri atataka msaada kwa ajili ya jihadi ni lazima apewe Zakat, kwani mtu mmoja hata akiwa tajiri inawezekana asiweze kutoa gharama zote zinazohitajika katika maandalizi ya jihadi. Tukumbuke kuwa kulingania na kupigania dini ya Allah si kazi ya watu maalum bali ni amri kwa kila Muislamu. Hivyo ikitokea Waislamu wako katika harakati za kusimamisha dini ya Allah au katika vita vya kuihami, wale wasioweza kujigharimia wenyewe katika harakati na mapambano hayo, wasaidiwe kwa mfuko wa Zakat.

### (h) Kuwasaidia wasafiri walioharibikiwa njiani (Ibnis Sabiil)

Msafiri aliyeharibikiwa njiani kwa kuibiwa, kupoteza mali yake, kupata ajali, kuishiwa na masurufu, (matumizi) n.k. Akawa hana uwezo wowote wa kupata mahitaji muhimu ya maisha, hata kama ni tajiri huko alikotoka,inabidi apewe fungu la Zakat ili aweze kuyamudu maisha mpaka afike mwisho wa safari yake. Fungu hili pamoja na mafungu mengine yote ya Zakat au mgawanyo wa Zakat kwa ujumla unatupa picha

kamili juu ya udugu wa Kiislamu.

### Wanaostahiki kupewa Sadaqat

Pamoja na Waislamu matajiri kuamrishwa watoe Zakat ili iweze kuinawirisha jamii kwa kufuata utaratibu huu, pia Sadaqat imewajibishwa kwa matajiri ili pamoja na kuwasaidia Waislamu katika mahitajio haya na mengine yasiyotajwa hapa, wawasaidie pia wanaadamu wenzi wao wasiokuwa Waislamu. Kama tulivyoona hapo awali tofauti iliyopo kati ya Zakat na Sadaqat ni kwamba Zakat hugawanywa katika mafungu haya manane yaliyotajwa hapo juu kwa Waislamu tu, ambapo Sadaqat hugawanywa kwa hata wasiokuwa Waislamu maadam wako katika dhiki inayohitaji msaada. Hebu pia tuzingatie aya zifuatazo juu ya watu wengine wanaostahiki kupewa Sadaqat pamoja na hao waliotajwa katika aya ya (9:60):

وَءَاتِ ذَا ٱلْقُرْبَىٰ حَقَّهُۥ وَٱلْمِسْكِينَ
وَٱبْنَ ٱلسَّبِيلِ وَلَا تُبَذِّرْ تَبْذِيرًا ﴿٢٦﴾

*Na umpe jamaa (yako) haki yake, na maskini na msafiri aliyeharibikiwa, wala usitawanye (mali yako) kwa ubadhirifu (17:26).*

۞ لَّيْسَ ٱلْبِرَّ أَن تُوَلُّوا۟ وُجُوهَكُمْ قِبَلَ ٱلْمَشْرِقِ وَٱلْمَغْرِبِ
وَلَـٰكِنَّ ٱلْبِرَّ مَنْ ءَامَنَ بِٱللَّهِ وَٱلْيَوْمِ ٱلْـَٔاخِرِ وَٱلْمَلَـٰٓئِكَةِ وَٱلْكِتَـٰبِ
وَٱلنَّبِيِّـۧنَ وَءَاتَى ٱلْمَالَ عَلَىٰ حُبِّهِۦ ذَوِى ٱلْقُرْبَىٰ وَٱلْيَتَـٰمَىٰ وَٱلْمَسَـٰكِينَ
وَٱبْنَ ٱلسَّبِيلِ وَٱلسَّآئِلِينَ وَفِى ٱلرِّقَابِ ... ﴿١٧٧﴾

*Sio wema (tu huo peke yake) kuwa mnaelekeza nyuso zenu upande wa Mashariki na Magharibi (katika kusali. Yako na mema mengine). Bali wema (hasa) ni (wa wale) wanaomwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho na Malaika na Kitabu na Manabii, na wanawapa mali juu ya kuwa wanayapenda - jamaa na mayatima na maskini na wasafiri (walioharibikiwa) na wawaombao na katika (kuwakomboa) watumwa..... (2:177).*

*Mwabuduni Mwenyezi Mungu wala msimshirikishe na chochote. Na*

۞ وَٱعْبُدُوا۟ ٱللَّهَ وَلَا تُشْرِكُوا۟ بِهِۦ شَيْـًٔا ۖ وَبِٱلْوَٰلِدَيْنِ إِحْسَـٰنًا وَبِذِى ٱلْقُرْبَىٰ
وَٱلْيَتَـٰمَىٰ وَٱلْمَسَـٰكِينِ وَٱلْجَارِ ذِى ٱلْقُرْبَىٰ وَٱلْجَارِ ٱلْجُنُبِ وَٱلصَّاحِبِ
بِٱلْجَنۢبِ وَٱبْنِ ٱلسَّبِيلِ وَمَا مَلَكَتْ أَيْمَـٰنُكُمْ ۗ إِنَّ ٱللَّهَ لَا يُحِبُّ مَن كَانَ
مُخْتَالًا فَخُورًا ﴿٣٦﴾

*wafanyieni ihsani wazazi wawili, na jamaa na mayatima na maskini na jirani walio karibu na jirani wa mbali, na rafiki wa walio ubavuni (mwenu) na msafiri aliyeharibikiwa, na wale iliyomiliki mikono yenu ya kulia (kuume). Bila shaka Mwenyezi Mungu hawapendi wenye kiburi wajivunao". (4:36).*

وَفِىٓ أَمْوَٰلِهِمْ حَقٌّ
لِّلسَّآئِلِ وَٱلْمَحْرُومِ ﴿١٩﴾

*Na katika mali zao ilikuwako haki ya kupewa maskini aombaye na ajizuiaye kuomba. (51:19).*

Tunajifunza kutokana na aya hizi kwamba mgawanyo wa Sadaqat ni kama ule ule za Zakat bali pamewekwa fungu la nyongeza la kuwapa jamaa haki yao. Linalosisitizwa na Uislamu ni kwamba kila mwenye uwezo lazima awaangalie jamaa zake kwanza wa karibu na mbali. Wala si Uislamu kuweka akiba kwa kipindi cha mwaka mzima huku jamaa zako wa karibu na hata wa mbali wamo katika dhiki na wanaishi bila ya kujitosheleza kwa mahitajio yao muhimu ya maisha.

Muislamu wa kweli kama ilivyoelezwa katika aya (2:177) ni yule anayetoa mali yake kwa moyo mkunjufu kuwapa jamaa zake wanaohitaji msaada, mayatima, maskini, wasafiri walioharibikiwa na wengineo wenye shida waombao na wasioomba. Baada ya kufanya hivyo kwa kipindi cha mwaka mzima, akiba ya mali iliyobaki ndiyo itakayohisabiwa na kutolewa Zakat na kugawanywa katika mafungu yaliyotajwa katika Qur'an (9:60). Kwa kufuata utaratibu huu wa kutoa Sadaqat kila inapohitajika na kuwapa wanaostahiki kupewa, utakuta kuwa kila mtu anao uwezo wa kutoa Sadaqat. Ni katika msingi huu Mtume (s.a.w) amesema:

*Kuna Sadaqat kwa kila Muislamu. Wakauliza: Kama hatapata cha kutoa je? Akajibu: Na afanye kazi kwa mikono yake miwili, kwa kufanya hivyo*

*atakuwa amejinufaisha mwenyewe na pia kitendo hicho ni Sadaqat. Wakauliza: Kama hawezi kufanya hivyo je? Alijibu: Basi na amsaidie (kihali) mhitaji na aliyedhikika. Wakauliza: Kama hakuweza kufanya hivyo je? Alijibu: Basi hana budi kuamrisha mema. Wakauliza: Kama hawezi kufanya hivyo je? Alijibu: Hana budi kujizuilia na maovu kwani hii hasa ni Sadaqat kwake. (Bukhari na Muslim).*

Hivyo kila Muislamu wa kweli anatakiwa apanie kutoa misaada ya hali na mali kwa jamaa na kila anayehitajia awe Muislamu au asiwe Muislamu. Kama Muislamu hana chochote cha kutoa basi aongee nao kwa wema na aonyeshe kuwa pamoja nao katika dhiki hiyo. Kufanya hivi huhesabiwa vile vile kuwa ni Sadaqat.

۞قَوْلٌ مَّعْرُوفٌ وَمَغْفِرَةٌ خَيْرٌ مِّن صَدَقَةٍ يَتْبَعُهَآ أَذًى ۗ وَٱللَّهُ غَنِىٌّ حَلِيمٌ ٢٦٣

*Kauli njema na kumsamehe (anayekukosea) ni bora kuliko Sadaqat inayofuatishwa na udhia. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mkwasi na Mpole kwa (viumbe vyake). (2:263).*

Katika aya hii tunafahamishwa kuwa kauli njema nayo ni Sadaqat na ni bora kuliko Sadaqat iliyotolewa kwa masimbulizi inayomdhalilisha mpokeaji na kumnyima uhuru wake. Pia si vyema kumpa mtu Sadaqat kisha umtake akurejeshee tena. Kutokana na kauli ya Mtume (s.a.w) Sadaqat hairejeshwi. Si vyema mwenye kupewa akaikataa kama ni mwenye kustahiki kupewa na si vyema kwa mtoaji atake arejeshewe tena baada ya kutoa. Kwani katika Hadith tunafahamishwa:

*Umar bin Khattab (r.a) ameeleza kuwa: Nilitoa farasi kwa ajili ya kupigania njia ya Allah, lakini yule aliyemchukua alimfanya akakondeana sana. Nilifikiria angeliuza kwa bei rahisi". Kisha nilimuuliza Mtume ambaye alisema: Usimnunue na usiirejeshe Sadaqat yako (kwako baada ya kuitoa) hata kama atairudisha kwako kwa bei ya dirhamu moja, kwa sababu anayerejesha Sadaqat baada ya kuitoa ni kama mbwa anayekula matapishi yake". Katika simulizi nyingine Mtume alisema: "Usichukue (usiirejeshe) Sadaqat baada ya kuitoa kwa sababu yule anayeirejesha Sadaqat baada ya kuitoa ni kama yule anayekula matapishi yake". (Bukhari na Muslim).*

**Mali inayojuzu kutolewa Zakat, Nisaab na kiwango cha Zakat**

Aina ya mali inayojuzu kutolewa Zakat imeelezwa kwa wazi katika

Qur-an na Hadith sahihi. Mali inayojuzu kutolewa Zakat ni ile iliyofikia au kuzidi kima maalum kiitwacho **Nisaab** na kubakia katika milki ya mwenye hiyo mali kwa kipindi chote cha mwaka mmoja. Kila aina ya mali ina nisaab yake, **Nisaab** ni kiwango cha mali kinachostahiki kitolewe Zakat. Aina ya mali inayojuzu kutolewa Zakat ni:

(i) Mazao yote ya shambani
(ii) Wanyama wafugwao kwa ajili ya chakula
(iii) Dhahabu (gold), fedha (silver), au fedha taslim (cash)
(iv) Vito (mapambo ya dhahabu na fedha)
(v) Madini na mali ya kuchimbuliwa chini ya ardhi au mali ya kuokota
(vi) Mali ya biashara

**(i) Mazao ya Shambani**

Mazao yote yanayolimwa shambani, yanastahiki kutolewa Zakat kutokana na amri ya Allah(s.w) katika aya zifuatazo:

يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓا۟ أَنفِقُوا۟
مِن طَيِّبَـٰتِ مَا كَسَبْتُمْ وَمِمَّآ
أَخْرَجْنَا لَكُم مِّنَ ٱلْأَرْضِ ۖ (٢٦٧)

*"Enyi mlioamini! Toeni katika vile vizuri mlivyovichuma, na katika vile tulivyokutoleeni katika ardhi..." (2:267)*

۞ وَهُوَ ٱلَّذِىٓ أَنشَأَ جَنَّـٰتٍ مَّعْرُوشَـٰتٍ وَغَيْرَ مَعْرُوشَـٰتٍ وَٱلنَّخْلَ
وَٱلزَّرْعَ مُخْتَلِفًا أُكُلُهُۥ وَٱلزَّيْتُونَ وَٱلرُّمَّانَ مُتَشَـٰبِهًا وَغَيْرَ
مُتَشَـٰبِهٍ ۚ كُلُوا۟ مِن ثَمَرِهِۦٓ إِذَآ أَثْمَرَ وَءَاتُوا۟ حَقَّهُۥ يَوْمَ حَصَادِهِۦ ۖ
وَلَا تُسْرِفُوٓا۟ ۚ إِنَّهُۥ لَا يُحِبُّ ٱلْمُسْرِفِينَ (١٤١)

*Naye (Mwenyezi Mungu) ndiye aliyeiumba miti inayoegemezwa (katika chanja katika kuota kwake), na isiyoegemezwa, na (akaumba) mitende na mimea yenye matunda mbali mbali, na (akaumba) mizaituni na mikomamanga inayofanana na isiyofanana. Kuleni matunda yake inapotoa matunda na toeni haki yake siku ya kuvunwa kwake (kwa kuwapa maskini na jamaa na majirani na wengineo). Wala msitumie kwa fujo, hakika Mwenyezi Mungu) hawapemndi watumiao fujo. (6:141).*

Aya hizi zinatuthibitishia kuwa mazao yote yatokayo shambani yakiwa ya chakula au ya biashara yanalazimu kutolewa Zakat. Haya ni pamoja na mazao yote ya aina ya mbegu, aina zote za matunda, mazao ya aina ya mizizi, mazao ya biashara kama vile katani, kahawa, pamba, chai, pareto, n.k. Pia kutokana na Hadithi ifuatayo hata asali inapaswa kutolewa Zakat:

*Abu Umar (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: "Juu (ya Zakat) ya asali: Kwa kila chupa kumi (za ngozi) chupa moja itolewe Zakat".*

## Nisaab ya mazao ya shambani

Nisaabu ya mazao ya shambani imeelezwa katika Hadithi ifuatayo:

*Abu Said al-Khudri (r.a) ameeleza kuwa Mtume (s.a.w) amesema: Hapana Zakat kwa mbegu au tende mpaka zifikie kiasi cha wasaq tano. (Nisai).*

Katika Hadith hii tunafahamishwa kuwa mazao ya shambani yanayostahiki kutolewa Zakat ni yale yaliyofikia 'wasaq' tano na hapana Zakat chini ya hapo. Katika kipimo tulichokizoea wasaq 1 = kilo 133.2, hivyo wasaq 5 = kilo (5 x 133.2) = kilo 666. Kwa hiyo mtu akiwa na mazao ya shambani yaliyofikia uzito wa kilo 666 itambidi atoe (Zakat) kiasi cha kilo 66.6 (nusu wasaq) na kama yamemwagiliwa maji atatoa kiasi cha kilo 33.3 (robo wasaq).

Kwa hiyo, mazao yote yanayopimwa kwenye pishi au kwenye kilo yapimwe na kutolewa Zakat iwapo yatakuwa yamefikia Nisaab. Jambo lingine muhimu katika utoaji wa Zakat ya mazao ya shambani ni kwamba si lazima utoe mazao yale yale bali unaweza ukayathamanisha kwa fedha taslim(cash) kulingana na bei ya zao hilo kwa wakati uliopo.

## Kiasi cha Zakat ya mazao ya shambani

Kima cha mazao kinachotakiwa kutolewa Zakat kimebainishwa katika Hadith ifuatayo:

*Abdullah bin Umar (r.a) ameeleza kutoka kwa Mtume (s.a.w) kuwa amesema: 'Kuna moja ya kumi (1/10) kutokana na mazao yaliyonyeshewa na mvua au maji ya chemchem (mto) au yaliyostawi kwenye ardhi yenye rutuba. Na kuna nusu ya moja ya kumi (1/20) kutokana na mazao yaliyonyweshwa kwa kutumia ngamia. (Bukhari).*

Katika Hadith hii tunafahamishwa kuwa kiasi cha kutoa kwa mazao ya shambani ni moja ya kumi (1/10) au (10%) ya mavuno yote, iwapo mazao hayo yalistawishwa kwa njia ya kawaida ya kutegemea mvua

au kunyweshelezwa kwa maji ya mto, au chemchem yanayotiririka yenyewe bila ya kutumia zana na nguvu ya kuyavutia. Kwa upande mwingine, iwapo mazao ya shambani yatastawishwa kwa kunyweshelezwa kwa gharama za mabomba, mashine, mikokoteni, kima cha Zakat kitapungua na kuwa moja ya ishirini (1/20) au (5%) ya mavuno yote.

*Atta bin 'Usaid (r.a) ameeleza kuwa Mtume (s.a.w) amesema: Katika Zakat ya Zabibu, zabibu zitapimwa kwa kipimo kile kile cha tende na Zakat yake italipwa baada ya kukaushwa kama Zakat ya tende inavyolipwa baada ya kukaushwa. (Tirmidh, Abu Daud).*

Hadith hii inatufahamisha kuwa Zakat itolewe baada ya kuvuna na kukausha kwa yale yanayowekeka yakiwa yamekauka. Vile vile ieleweke kuwa kutajwa tende na zazibu katika Hadithi hii na Hadithi nyingine mbali mbali haina maana kabisa kuwa tende na zabibu ndio matunda pekee yanayotolewa Zakat kama wengi wetu wanavyojaribu kuelewa, bali mazao haya yametajwa mara kwa mara katika Hadith mbali mbali kwa kuwa ndiyo yaliyokuwa katika mazingira ya Mtume Muhammad (s.a.w) na jamii ya Waislamu aliokuwa nao.Ukweli ni kuwa mazao yote yanayolimwa shambani yanastahiki kutolewa Zakat kwa ushahidi wa aya za Qur-an. Rejea Qur-an (6:141) na (2:267).

Muda wa kutoa Zakat ya mazao ya shambani ni mara tu baada ya mavuno. Hata kama utalima au kuvuna mara mbili au mara tatu zote. Ndio kusema Zakat ya mavuno haingoji kumalizika mwaka.

### (ii) Wanyama wafugwao kwa ajili ya chakula

Wanyama wafugwao wanaotolewa Zakat ni ngamia, ngo'ombe, mbuzi na kondoo. Farasi na Punda hawatolewi Zakat. Hadith zifuatazo zinatufahamisha juu ya Zakat ya wanyama:

*Ali bin Abii Talib (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: "Hapana Zakat kutoka kwa Farasi na Punda..." (Tirmidh, Abu Daud)*

*Sayydina Ali (r.a) vile vile ameeleza: "Ninaeleza kutoka kwa Mtume (s.a.w) aliyesema: "Lete moja ya nne ya ushuru, ikimaanisha kuwa kuna Dirham moja kwa kila Dirham arubaini na mtu haijuzu kwake Zakat mpaka awe na Dirham mia mbili (200). Kwa hiyo zinapokuwa Dirham 200 kuna Dirham tano za Zakat kinachozidi kitatolewa kulingana na hisabu hiyo (ya 1/40). Na kwa mbuzi kuna mbuzi mmoja katika kila arobaini mpaka ifikie idadi ya mbuzi 120, kama wakizidi kwa mmoja mpaka 200*

*watatolewa mbuzi majike wawili wa mwaka mmoja. Kama wakiwa zaidi ya hapo mpaka kufikia 300 mbuzi 3 wa mwaka mmoja; kama hakuna zaidi ya mbuzi 39 haina Zakat juu yake kutokana na mbuzi hao. Na kuhusu ng'ombe, kwa kila ng'ombe ng'ombe 30 kuna ndama mmoja wa mwaka mmoja na katika kila ng'ombe 40, kuna ndama mmoja wa miaka miwili, na hapana Zakat inayojuzu kutokana na ng'ombe waliotiwa kwenye kazi" (Abu Daud).*

**Nisaab na kiasi cha kila aina ya mnyama**

Wanyama waliotajwa watastahiki kutolewa Zakat baada yakuwa katika malisho na katika milki ya mfugaji kwa kipindi cha mwaka mmoja. Kwa hiyo kila mwaka wafugaji wanatakiwa wahesabu mifugo yao iliyopindukia mwaka na kutoa Zakat kama ilivyoeleza hadithi iliyotajwa hapo juu. Wanyama watolewao Zakat wawe wazima na wachanga wasio na kilema chochote. Watolewe wanyama walio wazuri zaidi tukikumbuka msisitizo wa Qur-an:

يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓاْ أَنفِقُواْ مِن طَيِّبَـٰتِ مَا كَسَبۡتُمۡ وَمِمَّآ
أَخۡرَجۡنَا لَكُم مِّنَ ٱلۡأَرۡضِۖ وَلَا تَيَمَّمُواْ ٱلۡخَبِيثَ مِنۡهُ تُنفِقُونَ وَلَسۡتُم
بِـَٔاخِذِيهِ إِلَّآ أَن تُغۡمِضُواْ فِيهِۚ وَٱعۡلَمُوٓاْ أَنَّ ٱللَّهَ غَنِيٌّ حَمِيدٌ ٢٦٧

*Enyi mlioamini! Toeni katika vizuri mlivyovichuma, na katika vile tulivyokutoleeni katika ardhi. Wala msikusudie kutoa vilivyo vibaya, hali nyinyi wenyewe msingevipokea isipokuwa kwa kuviangalia. Basi jueni ya kwamba Mwenyezi Mungu ni Mkwasi na Asifiwaye. (2:267).*

Hivyo, japo majike katika ng'ombe na mbuzi hayakusisitizwa katika Hadithi mbali mbali kama ilivyosisitizwa kwa upande wa ngamia, ni bora kutoa mbuzi jike au kondoo jike wa mwaka mmoja. Majike ni bora zaidi kuliko madume kwa kuwa yatazaa na kuongeza idadi ya mifugo. Kama katika kuthaminisha na fedha taslimu dume litakuwa na thamani zaidi kuliko jike na ikiwa mtoaji ametoa fedha taslimu badala ya wanyama, basi atoe thamani ya dume. Pia mifugo ya Zakat inaweza kuthamanishwa zitakapotolewa fedha taslim badala ya mifugo yenyewe. Lakini katika kufanya hivyo ni lazima liangaliwe lile litakalokuwa na maslahi bora kwa mpokeaji Zakat. Kama itakuwa ni bora kwa mpokeaji apokee mifugo badala ya kutoa thamani yake itakuwa sawa. Jambo muhimu linalosisitizwa hapa ni kwamba vinavyotolewa Zakat viwe vizuri

vinavyopendeka kwa mtoaji na mpokeaji.

**(iii) Dhahabu (gold), fedha (silver) na fedha taslimu (cash)**

Miongoni mwa vitu vinavyopendwa na wanaadam ni dhahabu na fedha. Ni vitu hivi walimwengu katika kipindi kirefu cha historia huvitumia kama kipimo cha thamani ya vitu mbali mbali, na ndio vimetumika kama kipimo cha utajiri. Kwa hiyo vimestahiki zaidi kutolewa Zakat:

*"... Na wale wakusanyao dhahabu na fedha wala hawazitoi katika njia ya Mwenyezi Mungu, wape habari ya adhabu iumizayo" (9:34).*

وَٱلَّذِينَ يَكۡنِزُونَ ٱلذَّهَبَ وَٱلۡفِضَّةَ وَلَا يُنفِقُونَهَا فِي سَبِيلِ ٱللَّهِ فَبَشِّرۡهُم بِعَذَابٍ أَلِيمٖ ﴿٣٤﴾

Aya hii inatuthibitishia kuwa kutoa katika njia ya Allah kutokana na dhahabu na fedha (silver) ni lazima kwa Muislamu. Pia fedha taslimu (Bank money or cash) ziko katika mkumbo huu.

**Nisaab ya dhahabu, fedha na fedha taslimu na viwango vya Zakat**

Nisaab ya dhahabu na fedha imeelezwa katika Hadith ifuatayo:

*Ali (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: Hapana Zakat kutoka kwa Farasi au Punda. Kwa hiyo chukua Zakat ya fedha (silver), dirham moja kwa kila dirham arobaini (1/40). Hapana Zakat kwa dirham 190. Zinapofika dirham 200, basi kuna dirham 5 za Zakat" (Tirmidh, Abu Daud).*

Kutokana na Hadith, kiwango cha Zakat ya dhahabu, fedha (silver) ni Dirham moja. Dirham ni fedha zilizotumika katika baadhi ya nchi za kiarabu tangu wakati wa Mtume Muhammad (s.a.w) hadi hivi sasa. Pia katika Hadith hii tunafahamishwa kuwa Nisaab ya fedha (silver) ambayo ni sawa na nisaab ya dhahabu na fedha taslim ni dirham 200. Tukitumia kipimo cha uzito Nisaab ya fedha ni gram 577.5 au tola 52.5. Nisaab ya dhahabu ni gramu 82.5 au tola 7.5. Muda wa kutoa Zakat ya fedha, dhahabu na fedha taslim ni baada ya kupindukia mwaka mmoja. Kwa hiyo dhahabu, fedha na fedha taslim zitakapowekwa akiba kwa kipindi cha mwaka mzima zikiwa zimefikia thamani ya dirham 200 au zaidi zitatolewa Zakat kwa kiwango cha 1/40 au 2.5%.

**(iv) Vito (mapambo )vya Dhahabu na Fedha**

Mapambo ya dhahabu na fedha yameharamishwa kwa Waislamu Wanaume. Wanawake wenye mapambo ambayo kiasi cha dhahabu au fedha kilichopo kwenye mapambo hayo kinafikia Nissab,wanalazimika kutoa Zakat kila mwaka unapopindukia.

*Zainab mke wa Abdullah(r.a) ameeleza: Mtume wa Allah alituhutubia na akasema: "Enyi jumuia (mkusanyiko wa) wa wanawake! Toeni Zakat hata kutoka kwenye mapambo yenu, kwa sababu katika wakazi wa motoni mtakuwa wengi zaidi katika siku ya Kiyama" (Tirmidh).*

*Amr bin Shuaib(r.a) amesimulia kutoka kwa baba yake na baba yake alisema kuwa wanawake wawili walikuja kwa Mtume (s.a.w) na bangili mbili za dhahabu wamevaa mikononi mwao Mtume aliwauliza "mmelipa Zakat yake" 'Hapana', walijibu. Kisha Mtume (s.a.w) akawauliza: 'Mngetaka kwamba Allah awavalishe bangili za moto?' 'Hapana' walijibu. Alisema (Mtume): "Basi lipeni Zakat yake" (Tirmidh).*

**(v) Mali yakuchimbuliwa chini ya ardhi au mali ya kuokota**

Mali iliyofukuliwa chini au madini hutolewa ushur au Zakat kiasi cha moja ya tano (1/5 au 20%) ya thamani ya mali hiyo kama tunavyofahamishwa katika Hadith.

*Abu Hurairah ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: "... Na kuna moja ya tano (1/5) inayolazimu kutolewa Zakat kutokana na mali iliyo chini ya ardhi". (Bukhari na Muslim).*

Hadith hii inatufahamisha kuwa mali yoyote iliyochimbuliwa chini ya ardhi ambayo haikuwa na mmiliki yoyote kabla ya hapo, itakuwa ni halali kwa aliyeigundua na kuichimbua lakini atalazimika kutoa ushuru au kiwango cha Zakat kiasi cha 1/5 au 20% ya mali hiyo. Hali kadhalika mali yoyote ya kuokota iliyokosa mwenyewe baada ya kutangazwa kwa muda mrefu wa kutosha unaokubalika katika sharia ya kiislamu inakuwa ni mali ya mwenye kuokota, na atalazimika kuitolea Zakat kiasi cha 1/5 au 20% ya mali hiyo. Mali ya kuchimbuliwa chini au mali ya kuokota haina Nisaab wala haina muda bali Zakat yake hutolewa pale pale inapopatikana.

**(vi) Mali ya Biashara**

Bidhaa za biashara pamoja na fedha taslimu zinatakiwa zihesabiwe na kutolewa Zakat baada ya mwaka kupindukia.

*Samura bin Jundab (r.a) ameeleza: Mtume wa Allah alikuwa akituelekeza tukusanye Zakat kutoka kwenye vile tulivyovihesabu kama bidhaa (za*

*biashara). (Abu Daud).*

Bidhaa za biashara zitatolewa Zakat kwa kuthamanishwa na fedha taslim kwa kiasi cha 1/40 au 2.5% ya mali yote ya bidhaa zote za biashara. Kwa hiyo mali ya biashara nisaab yake itakuwa sawa na nisaab ya fedha au dhahabu. Tofauti na dhahabu, fedha na fedha taslim ambazo hutolea Zakat baada ya kukaa kwa kipindi cha mwaka mmoja, bidhaa za biashara si lazima zikae kwa kipindi cha mwaka mmoja ndio ijuzu Zakat juu yake bali kila mwisho wa mwaka, mfanyabiashara atahesabu bidhaa zake zote anazozifanyia biashara na kuzitolea Zakat kwa kiwango cha 2.5%. Hapana Zakat juu ya vifaa vinavyotumika kwa matumizi ya nyumbani au vitendea kazi. Kwa mfano, nyumba za kufanyia kazi kama vile maduka, ofisi, na hoteli, mashine za kufanyia kazi, samani za nyumbani, ofisini dukani, hotelini, n.k. magari ya kusafiria na kusafirishia bidhaa, vyote hivi havistahiki kutolewa Zakat.

Kwa msisitizo zaidi Zakat inajuzu tu kwa mali inayotengenezwa kwa ajili ya kuuzwa au mali inayonunuliwa kwa ajili ya kuuzwa; kwa mfano magari yaliyonunuliwa au nyumba zilizotengenezwa kwa ajili ya kuuzwa zitatolewa Zakat kila mwisho wa mwaka.Jambo muhimu linalotakiwa lizingatiwe kabla ya kutoa Zakat ni madeni. Ni sharti madeni na haki nyingine zote za watu zitolewe ndio mali ihesabiwe kwa ajili ya Zakat. Kwa muhutasari mali inayojuzu kutolewa Zakat, nisaab yake, kiasi kinachotolewa na baada ya muda gani vinadhihirika katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali:** Mali inayojuzu kutolewa zakat, Nisaab, kiwango cha zakat na muda wa kutoa

| | Mali | Nisaab | Kiasi % | Kutoa |
|---|---|---|---|---|
| 1 | **Mazao ya shamba** | Wasaq 5 au kg 666 | (a) 1/2 Wasaq au kg 66.6 yaliyostawishwa kwa mvua<br>(b) 1/4 Wasaq au kg 33.3 yaliyomwagiliwa | Baada ya mavuno |
| 2 | **Wanyama wafugwao**<br>(a) Ngamia | Ngamia 5 | Mbuzi 1 | Baada ya mwaka |
| | (b) Ng'ombe | Ng'ombe 30 | Ndama mmoja wa mwaka 1 | |
| | (c) Mbuzi | Mbuzi 40 | Mbuzi 1 | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 2 | (d) Kondoo | Kondoo 40 | Kondoo 1 | Baada ya mwaka |
| | (e) Kondoo na mbuzi | Kondoo na mbuzi 40 | Mbuzi au kondoo 1 | |
| 3 | **Dhahabu & vito** | Gram 82.5 au tola 7.5 | 2.5% au 1/40 ya thamani yake | Baada ya mwaka |
| 4 | **Fedha & vito** | Gram 577 au tola 52 | 2.5% au 1/40 ya thamani yake | |
| 5 | **Fedha tasilimu** | Sawa na thamani ya dhahabu au fedha | 2.5% au 1/40 ya thamani yake | |
| 6 | **Mali ya Biashara** | Sawa na thamani ya dhahabu au fedha | 2.5% au 1/40 | |
| 7 | **Mali ya kuokota au kuchimbua chini** | Hazina Nisaab | 20% au 1/5 | Baada ya kukosa mwenyewe au mara tu baada ya kuchimbuliwa |

## Lengo la Zakat na jinsi Linavyofikiwa

Lengo la Zakat linawiana na neno "Zakat" lenye maana ya kutakasa au utakaso. Mali itolewayo Zakat inakusudiwa iwe kitakaso kama inavyobainishwa katika Qur-an:

خُذْ مِنْ أَمْوَٰلِهِمْ صَدَقَةً تُطَهِّرُهُمْ وَتُزَكِّيهِم بِهَا وَصَلِّ عَلَيْهِمْ ۖ إِنَّ صَلَوٰتَكَ

سَكَنٌ لَّهُمْ ۗ وَٱللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿١٠٣﴾

*"Chukua sadaqat katika mali zao uwatakase kwa ajili ya hizo na kuwataja kwa vizuri (mbele yangu) na uwaombee dua. Hakika kuwaombea kwako kutawapa utulivu. Na Mwenyezi Mungu ndiye asikiaye na ajuaye." (9:103)*

Pia imepokelewa kwa Ibn Abbas (r.a) kuwa Mtume (s.a.w) amesema:

*"Mwenyezi Mungu (s.w) hakuamrisha Zakat kwa sababu nyingine ila ni kuitakasa mali iliyotolewa".*

**Zakat huitakasa:**

(i) Mali ya mtoaji.

(ii) Nafsi ya mtoaji.
(iii) Nafsi ya mpokeaji.
(iv) Jamii ya Kiislamu kwa ujumla.

**(i) Zakat inavyotakasa mali ya mtoaji**

Zakat ni sehemu ndogo ya mali (1/40 au 2.5%) inayotolewa kutokana na mali anayomiliki Muislamu na kuwapa wanaohitajia miongoni mwa fukara, maskini, wasafiri walioharibikiwa na wengineo kama ilivyobainishwa katika Suratul-Tawba aya ya 60. Sehemu hii ya mali inayaotolewa Zakat ni haki ya wale wanaostahiki kupewa Zakat iliyopitishiwa mikononi mwa huyu mwenye mali kama amana tu kama inavyobainika katika Qur-an:

وَفِىٓ أَمْوَٰلِهِمْ حَقٌّ لِّلسَّآئِلِ وَٱلْمَحْرُومِ ﴿١٩﴾

*"Na katika mali zao ilikuwepo haki ya kupewa maskini aombaye na ajizuiaye kuomba". (51:19).*

**Mali iliyotolewa Zakat inatakasika kwa sababu:**

**Kwanza**, huepukana na haki za watu wanaostahiki kupewa zaka, hivyo mali yote huwa halali na safi. Ambapo kama mali haitatolewa Zakat itachanganyika na haki za watu.

**Pili**, Muislamu mwenye kutoa Zakat na sadaqat anafahamu vyema kuwa kutoa huko hakutasihi mbele ya Mwenyezi Mungu (s.w) iwapo chumo lake limepatikana katika njia za haramu. Hivyo Muislamu mwenye tabia ya kutoa Zakat na sadaqat atajitahidi kufuata njia za halali katika kuchuma kwake na kujipatia mali iliyo halali.

**(ii) Zakat na Sadaqat Inavyotakasa Nafsi ya Mtoaji**

"*Kutoa ni moyo si utajiri*". Msemo huu ni wa msingi sana. Maana hasa ya msemo huu ni kwamba si utajiri utakaomfanya mtu atoe mali yake kwa ajili ya Mwenyezi Mungu bali ni moyo wake utakaomlazimisha kutoa. Utowaji wa mali na kuwapa wengine kwa ajili ya kupata radhi ya Mwenyezi Mungu si jambo la dharura bali ni jambo la kudhamiria na kutenda kutokana na msukumo wa nafsi yenye yakini juu ya maisha ya Akhera.

Muislamu anapotoa mali yake kwa ajili ya Mwenyezi Mungu

kuwapa wanaostahiki kwa upande mmoja, Mwenyezi Mungu huitakasa nafsi yake na uchoyo, ubakhili, upupiaji mali, kuabudu mali, majivuno, kiburi, dhulma na maovu mengineyo yatokanayo na umilikaji mali. Kwa upande mwingine, mwenye kutoa mali yake kwa ajili ya Mwenyezi Mungu huivika nafsi yake pambo la huruma, ukarimu, upendo na uchungaji haki za wengine.

Pia utoaji wa zakat na sadaqat huwa ni sababu ya mja kufutiwa dhambi zake na kustahiki Pepo ya Mwenyezi Mungu kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ هَلۡ أَدُلُّكُمۡ عَلَىٰ تِجَٰرَةٖ تُنجِيكُم
مِّنۡ عَذَابٍ أَلِيمٖ ﴿١٠﴾ تُؤۡمِنُونَ بِٱللَّهِ وَرَسُولِهِۦ وَتُجَٰهِدُونَ فِي
سَبِيلِ ٱللَّهِ بِأَمۡوَٰلِكُمۡ وَأَنفُسِكُمۡۚ ذَٰلِكُمۡ خَيۡرٞ لَّكُمۡ إِن كُنتُمۡ تَعۡلَمُونَ
﴿١١﴾ يَغۡفِرۡ لَكُمۡ ذُنُوبَكُمۡ وَيُدۡخِلۡكُمۡ جَنَّٰتٖ تَجۡرِي مِن تَحۡتِهَا
ٱلۡأَنۡهَٰرُ وَمَسَٰكِنَ طَيِّبَةٗ فِي جَنَّٰتِ عَدۡنٖۚ ذَٰلِكَ ٱلۡفَوۡزُ ٱلۡعَظِيمُ ﴿١٢﴾

"*Enyi mlioamini! Je! Nikujulisheni biashara itakayokuokoeni na adhabu iumizayo?(Basi biashara yenyewe ni hii): Muaminini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na piganieni dini ya Mwenyezi Mungu kwa mali zenu na nafsi zenu, haya ni bora kwenu; ikiwa mnajua (kuwa ni bora, basi fanyeni).(Mkifanya hayo, atakusameheni dhambi zenu na atakuingizeni katika Mabustani yapitayo mito mbele yake na (atakupeni) maskani mazuri mazuri katika Bustani za milele: huku ndiko kufuzu kukubwa.(61:10-12)*

Katika Surat-Tawba, tunafahamishwa kuwa wale Waislamu waliozembea kuandamana na Mtume wa Mwenyezi Mungu katika msafara wa Tabuku kwa ajili ya kushughulishwa na mali, baada ya kutubia kwa Mola wao walitoa sadaqat ili kutakasa nafsi zao kama tunavyojifunza katika aya ya (9:102-103):

وَءَاخَرُونَ ٱعْتَرَفُوا۟ بِذُنُوبِهِمْ خَلَطُوا۟ عَمَلًا صَـٰلِحًا وَءَاخَرَ سَيِّئًا عَسَى
ٱللَّهُ أَن يَتُوبَ عَلَيْهِمْ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿١٠٢﴾ خُذْ مِنْ أَمْوَٰلِهِمْ صَدَقَةً
تُطَهِّرُهُمْ وَتُزَكِّيهِم بِهَا وَصَلِّ عَلَيْهِمْ ۖ إِنَّ صَلَوٰتَكَ سَكَنٌ لَّهُمْ ۗ وَٱللَّهُ سَمِيعٌ
عَلِيمٌ ﴿١٠٣﴾

*Na (wako) wengine wamekiri dhambi zao (wametubia kwa Mwenyezi Mungu wakapokelewa).Wamechanganya vitendo vizuri na vingine vibaya, Mwenyezi Mungu ni mwingi wa kusamehe na mwingi wa kurehemu. Chukua sadaqat katika mali zao (Ee Muhammad) uwatakase kwazo na kuwataja kwa vizuri (mbele yangu) na uwaombee dua...” (9:102-103).*

**(iii) Zakat inavyotakasa Nafsi ya Mpokeaji**

Kama mali ilivyo mtihani kwa tajiri ndivyo ilivyo mtihani kwa maskini au mwenye dhiki. Kwa tajiri mali ni mtihani kwa sababu anao uhuru wa kuitumia mali yake apendavyo ambapo ni amana tu kwake kutoka kwa Mola wake. Kwa maskini kukosa mali ni mtihani kwake kwa sababu anaweza kumdhania Mwenyezi Mungu (s.w) vibaya kuwa ni muonevu na mwenye kupendelea kati ya waja wake; wengine akawafanya matajiri na wengine akawafanya mskini. Pamoja na dhana hii mbaya juu ya Mwenyezi Mungu (s.w) maskini na mwenye dhiki huweza kujenga moyoni mwake tabia ya unyonge, udhalili, husuda, uadui, uhasama na tabia nyingine mbaya zinazosababishwa na ukosefu wa mali.

Utoaji wa Zakat na Sadaqat kwa wanaostahiki umewajibishwa kwa Waislamu wenye kumiliki mali ili pamoja na kuwatakasa wao wenyewe, iwatakase pia wapokeaji kutokana na husuda, chuki, uhasama, unyonge, na kadhalika, na badala yake kuwavisha nyoyoni mwao upendo, udugu, shukrani, uchangamfu, ushirikiano na maadili mengineyo yanayotokana na kukirimiwa mali kwa jina la Mwenyezi Mungu (s.w).

Pia mwenye kupokea Zakat au sadaqat daima atakumbuka kuwa Mwenyezi Mungu ndiye mwenye kuwaruzuku waja wake bila hesabu.

**(iv) Zakat na Sadaqat Inavyotakasa Jamii ya Waislamu**

Tumeshaona jinsi Zakat na Sadaqat zinavyotakasa nafsi za watoaji na wapokeaji ambao wote wako katika jamii moja. Fikiria jamii ambayo kwa upande mmoja matajiri wake hutoa haki za maskini na wale wote

wanaostahiki kupewa Zakat na Sadaqat huku wakiwahurumia na kuwakumbatia ndugu zao hao na kwa upande mwingine hao wanaoipokea zakat na Sadaqa, wanaipokea kwa moyo wa uchangamfu na upendo wakijua kuwa wamepokea tunu hiyo kutoka kwa Mola wao kupitia kwa ndugu zao waadilifu. Unafikiri jamii hii itakuwa na watu wenye mahusiano ya namna gani? Bila shaka jamii hii itakuwa ni jamii yenye kuishi kwa upendo na udugu na yenye kudumisha amani. Kila mmoja katika jamii atakuwa anapata mahitajio yake muhimu ya maisha. Jamii ya namna hii ni lazima iwe na maendeleo ya vitu na utu kwa sababu zifuatazo:

**Kwanza**, kila mmoja atakuwa na uwezo wa kimwili na wakisaikolojia wa kufanya kazi kwa juhudi zake zote. Inafahamika kuwa katika Uislamu uvivu na uzembe ni haramu. Hivyo kila aliyekuwa na dhiki ya muda mfupi baada ya kupewa Zakat na Sadaqat, atapata nguvu na uwezo wa kujikwamua katika dhiki yake hiyo, na baada ya muda mfupi naye atazalisha mali ya kutosha kutoa Zakat na Sadaqat. Hali hii huiwezesha jamii kufikia wakati ambao watu wasiojiweza watakuja kuwa wachache sana na sehemu kubwa ya zakat kupelekewa kwenye miradi ya maendeleo ya jamii kama vile ujenzi na uendeshaji wa shule na vyuo, hospitali, barabara, n.k.

**Pili**, uhusiano mzuri kati ya matajiri na wenye dhiki katika jamii unaojengwa kwa njia ya kusaidiana kwa Zakat na Sadaqat, huwafanya waislamu washikamane na kushirikiana ipasavyo katika kuusimamisha na kuuhami Uislamu jambo ambalo huwapelekea kupata radhi za Mwenyezi Mungu, baraka zake na upendo wake kama tunavyojifunza katika Qur-an:

إِنَّ ٱللَّهَ يُحِبُّ ٱلَّذِينَ يُقَـٰتِلُونَ فِى سَبِيلِهِۦ صَفًّا كَأَنَّهُم بُنْيَـٰنٌ مَّرْصُوصٌ

*"Kwa yakini Mwenyezi Mungu anawapenda wale wanaopigana katika njia yake, safusafu, (mkono mmoja); kama kwamba wao ni jengo lililokamatana barabara". (61:4).*

**Tatu**, uchumi wa halali ni miongoni mwa sharti za utoaji Zakat na Sadaqat. Hivyo katika jamii ambayo utoaji wa Zakat na Sadaqat umedumishwa, lazima pawe na uadilifu katika uchumi ambapo kila mtu hupata haki yake na kufaidika ipasavyo. Njia zote za uchumi haramu zikiepukwa katika jamii ni wazi kuwa udhalimu, wizi, ujambazi, kamari, riba, hongo na rushwa hutoweka na humuhamasisha kila mtu kuchuma kwa juhudi zake zote. Matokeo yake ni jamii kuendelea kiuchumi na kudumisha amani.

**Ukusanyaji na Ugawaji wa Zakat ni Suala la Jamii**

Mafanikio ya Zakat katika kuinua hadhi na uchumi wa jamii hayatapatikana iwapo utoaji na ugawaji wa Zakat utaendelea kubakia kuwa shughuli ya mtu binafsi.Tunafahamu vyema kuwa uchumi wa jamii haujengwi na mtu binafsi bali unajengwa kwa ushirikiano na kila mwana jamii. Hivyo, Zakat ikiwa sehemu kubwa na muhimu ya uchumi wa jamii ya Kiislamu, haina budi kukusanywa na kugawanywa na jamii. Kama Mtume (s.a.w) anavyosisitiza:

*"Nimeamrishwa nichukuwe zakat kutoka kwa matajiri miongoni mwenu na niigawanye kwa maskini (wanyonge) miongoni mwenu".*

Katika utekelezaji wa amri hii Mtume Muhammad (s.a.w) pia kama Rais au Mkuu wa dola ya Kiislamu aliwateua watu (Maamil) wa kwenda katika kila nyumba ya tajiri na kukusanya Zakat na kuziweka kwenye Hazina (Baitul-maali). Maamil waliwajibika pia kuigawa Zakat kwa wanaostahiki kutoka kwenye Baitul-maali.

Kwa ujumla ukusanyaji na ugawaji wa Zakat wakati wa Mtume (s.a.w) ulikuwa ni kazi ya Serikali na wenye kuishughulikia Zakat katika ukusanyaji na ugawanyaji wake walikuwa wakilipwa kutokana na Zakat hiyo. Rejea tena Qur-an:

۞ إِنَّمَا ٱلصَّدَقَٰتُ لِلْفُقَرَآءِ وَٱلْمَسَٰكِينِ وَٱلْعَٰمِلِينَ عَلَيْهَا وَٱلْمُؤَلَّفَةِ

قُلُوبُهُمْ وَفِى ٱلرِّقَابِ وَٱلْغَٰرِمِينَ وَفِى سَبِيلِ ٱللَّهِ وَٱبْنِ ٱلسَّبِيلِ ۖ فَرِيضَةً

مِّنَ ٱللَّهِ ۗ وَٱللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿٦٠﴾

*"Sadaqat (zaka) hupewa watu hawa:Mafakiri, na maskini na* ***wanaozitumikia*** *na wanaotiwa nguvu nyoyo zao juu ya Uislamu na katika kuwapa uungwana watumwa na katika kuwasaidia wenye deni na katika (kutengeneza) mambo aliyoamrisha Mwenyezi Mungu na katika (kupewa) wasafiri (waliohariblkiwa). Ni faradhi inayotoka kwa Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi (na) Mwenye hikima". (9:60)*

Kutokana na aya hii tunaona kuwa fungu la tatu la Zakat hutumika kama mshahara kwa Maamil wanaozitumikia katika kuzikusanya na kuzigawanya. Hii yote inathibitisha kuwa amri ya zakat ni lazima itekelezwe kijamii chini ya usimamizi wa dola au jumuiya ya Kiislamu. Hivi ndivyo Mtume (s.a.w) alivyoitekeleza pamoja na Makhalifa wake waongofu. Mafanikio yote yaliyopatikana katika kusimamisha na

kuimarisha Dola ya Kiislamu yalipatikana kutokana na utaratibu mzuri alioufuata Mtume (s.a.w) na Makhalifa wake waongofu katika kuinua uchumi wa jamii kwa Zakat na sadaqat na njia nyinginezo.

### Kwa nini Lengo la Zakat na Sadaqat Halijafikiwa katika Jamii yetu?

Tumejifunza kuwa jamii yenye kudumisha nguzo ya Zakat na kutilia mkazo suala la kutoa mali na huduma kwa ajili ya Mwenyezi Mungu ni jamii yenye kuendelea kiuchumi na yenye kuishi kwa furaha na amanai ya kweli ya kibinafsi na kijamii. Jamii ya Mtume (s.a.w) na ile ya Makhalifa waongofu ni mfano wa wazi ulio mbele yetu. Jamii yetu hivi leo, pamoja na mahimizo ya utoaji wa Zakat na Sadaqat katika majukwaa mbali mbali bado hatuyapati matunda ya Zakat katika jamii. Miongoni mwa sababu zinazowafanya Waislamu wasipate matunda yanayotarajiwa kutokana na utoaji wa Zakat na Sadaqat ni:

**(i) Wengi miongoni mwa Waislamu Hawatekelezi Nguzo ya Zakat**

Wengi miongoni mwa Waislamu wenye uwezo wa kutoa zakat hawaitekelezi nguzo ya zakat na hawajihimizi kutoa misaada midogo na mikubwa kwa wale wanaohitajia.

Kwa sababu ya kutotoa Zakat na Sadaqat kwa wale wenye uwezo miongoni mwa Waislamu, kumeipelekea jamii ya Waislamu kuwa duni na dhalili mbele aya Makafiri na Washirikina.

**(ii) Wengi Watoa Zakat na Sadaqat Hawatekelezi Masharti ya Utoaji**

Miongoni mwa matajiri wachache wanaojitahidi kutekeleza nguzo ya Zakat na utoaji mali kwa ajili ya kuwasaidia wanaohitajia, hawazingatii masharti ya utoaji.Baadhi ya matajiri hutoa mali zao kwa ria na hufuatilia kwa masimbulizi. Utoaji wa namna hii umefutiwa baraka na hauwezi kumnufaisha mwenye kutoa wala jamii. Ubaya wa kutoa mali au msaada wowote kwa ria na kwa masimbulizi umedhihirishwa wazi katika aya ifuatayo:

يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ لَا تُبْطِلُوا۟ صَدَقَـٰتِكُم بِٱلْمَنِّ وَٱلْأَذَىٰ كَٱلَّذِى يُنفِقُ
مَالَهُۥ رِئَآءَ ٱلنَّاسِ وَلَا يُؤْمِنُ بِٱللَّهِ وَٱلْيَوْمِ ٱلْـَٔاخِرِ ۖ فَمَثَلُهُۥ كَمَثَلِ صَفْوَانٍ
عَلَيْهِ تُرَابٌ فَأَصَابَهُۥ وَابِلٌ فَتَرَكَهُۥ صَلْدًا ۖ لَّا يَقْدِرُونَ عَلَىٰ شَىْءٍ مِّمَّا
كَسَبُوا۟ ۗ وَٱللَّهُ لَا يَهْدِى ٱلْقَوْمَ ٱلْكَـٰفِرِينَ ﴿٢٦٤﴾

*Enyi mlioamini! Msiharibu sadaka zenu kwa masimbulizi na udhia; kama yule anayetoa mali yake kwa kuwaonesha watu, wala hamwamini Mwenyezi Mungu wala siku ya mwisho. Basi hali yake ni kama hali ya jabali ambalo juu yake pana udongo, kisha ikalifikia (jabali hili) mvua kubwa (likasukuma udongo wote huo) na ikaliacha tupu. Basi hawatakuwa na uwezo (wa kupata) chochote katika walivyovichuma; na Mwenyezi Mungu hawaongozi watu makafiri". (2:264)*

Kuna baadhi ya miongoni mwa Waislamu matajiri wanaotoa Zakat bila ya kuzingatia wale wanaostahiki (Rejea Qur-an, 9:60). Badala yake huenda na kapu la fedha msikitini na kumgawia kila mtu atakayekuwa tayari kupokea. Ugawanyaji huu wa Zakat hupelekea kupewa wasiostahiki na kuwakosesha wanaostahiki na kuwabakisha katika dhiki yao. Utoaji wa namna hii huibakisha jamii ya Waislamu katika dhiki na katika uadui na uhasama. Kuna baadhi ya Waislamu pamoja na kutoa Zakat na Sadaqat, hawazingatii mipaka ya halali na haramu katika uchumi wao. Wengine huchuma kwa njia za haramu ambazo hazinufaishi jamii bali huiingiza jamii katika matatizo ya rushwa, riba, kamari, wizi, ujambazi na udhalimu wa kila namna.

**(iii) Zakat haikusanywi na Kugawanywa Kijamii**

Tumejifunza kuwa utoaji na ugawaji wa Zakat, ili unufaishe jamii hauna budi kusimamiwa na jamii. Lazima jamii ya Kiislamu iwe na watu maalum wanaopita kwa kila Muislamu mwenye uwezo wa kutoa zakat, na kuipokea Zakat yake kisha kuikabidhi kwa Mtunzaji wa Baitil-Mali (Mhazini), kisha kuigawa kwa wanaostahiki.

Sehemu kubwa ya jamii ya Waislamu hivi leo, haifuati utaratibu huu wa ukusanyaji na ugawaji wa Zakat na sadaqat bali kila mwenye kutoa Zakat huigawanya mwenyewe kwa wale wanaostahiki walio machoni mwake. Kuacha Zakat mikononi mwa watoaji binafsi, kuna hasara kubwa zifuatazo:

**Kwanza**; hapitiwi na mhimizo wa makusudi juu ya utoaji wa Zaka, kiasi kwamba wenye kustahiki kutoa Zakat hujisahau na hatimaye kuacha kutoa Zakat kabisa.

**Pili;** kwa kutokuwa na utaratibu wa ugawaji, sehemu kubwa ya Zakat hupewa wasiostahiki na wale wanaostahiki hubaki na dhiki yao.

************************************************

## Zoezi la tatu

1. (a) Katika sheria ya kiislamu, Zakat inatafautianaje na Sadaqat?
   (b) Kutoa Zakat na Sadaqat kumesisitizwa sana katika Qur,an na Sunnah; unadhani ni kwanini?

2. (a) Orodhesha mambo yanayopaswa kuzingatiwa katika utoaji wa Zakat na Sadaqat.
   (b) Katika jamii yetu, ni akina nani wanaostahiki kupewa Zakkat

3. (a) Ainisha vitu vinavyostahiki kutolewa Zakat katika vile wanadamu walivyoruzukiwa na Allah(s.w)
   (b) Eleza maana ya Nisaab kisha bainisha nisaabu ya kila kitolewacho Zakat na kima chake cha utolewaji.

4. (a) Bainisha lengo la kutoa Zakat na Sadaqat; thibitisha kwa ushahidi wa Qur,an.
   (b) Nukuu kwa tafsiri aya tano za Qur,an zinazodhihirisha kwa hoja tafauti kuwa kutoa Zakat si ukarimu wa matajiri kwa fukara na masikini, ila ni wajibu?

5. Eleza kwa muhtasari namna utoaji wa Zakat na Sadaqat unavyomnufaisha mtoaji, mpokeaji na jamii yake.

6. Allah anasema: *"Na simamisheni swala na toeni Zakat, na mkatieni Mwenyezi Mungu sehemu njema katika mali yenu. Na kheri yoyote mnayoitanguliza kwa ajili ya nafsi zenu mtaikuta kwa Mwenyezi Mungu imekuwa bora zaidi na ina thawabu kubwa sana (73:20)"*

   (a) Kwa kuzingatia ujumbe wa aya hii, bainisha mambo yaliyopo katika jamii yako yanayothibitisha kutekelezwa au kutotekelezwa ipasavyo kwa ibada ya Zakkat
   (b) Katika jamii ya Waislamu wa Tanzania kuna matajiri wengi lakini hatuipati taathira ya Zakat katika jamii yetu. Kwanini imekuwa hivyo?

***********************************

## Sura ya Nne
# SWAUMU

### Maana ya Swaumu (Funga)

**Kilugha**; neno “*Swaum*” lina maana ya kujizuilia kufanya jambo lolote la kawaida. Katika Qur-an tunafahamishwa kuwa Bibi Maryam baada ya kumzaa nabii Isa (a.s) alijizuilia (alikuwa katika Swaum ya) kutosema na mtu yoyote juu ya mtoto wake.

فَإِمَّا تَرَيِنَّ مِنَ ٱلۡبَشَرِ أَحَدٗا فَقُولِيٓ إِنِّي نَذَرۡتُ لِلرَّحۡمَٰنِ صَوۡمٗا
فَلَنۡ أُكَلِّمَ ٱلۡيَوۡمَ إِنسِيّٗا ﴿٢٦﴾

*“... Na kama ukimuona mtu yeyote (akauliza habari za mtoto huyu) sema: `Hakika mimi nimeweka nadhiri kwa Mwingi wa Rehema ya Swaum (kufunga), kwa hiyo leo sitasema na mtu’” (19:26).*

Katika **Sharia ya Kiislamu** kufunga (Swaum) ni kujizuilia kula, kunywa, kujamii, kuingiza kitu chochote katika matundu ya mwili na kujizuilia kumuasi Allah (s.w) kuanzia alfajiri ya kweli mpaka kuingia magharibi.

Lengo la Swaum katika Uislamu ni kumuwezesha mja awe mcha Mungu kwa kufuata maamrisho yote ya Allah (s.w) na kuacha makatazo yake yote. Hivyo, ili lengo hili litimie mfungaji pamoja na kujizuilia kula, kunywa, kujamii, hanabudi pia kujizuilia na kitendo chochote kitakachompelekea kuvunja amri ya Allah (s.w) na Mtume wake (s.a.w). Kwa maana nyingine, ili Swaum ya mfungaji iwe na maana na yenye kufikia lengo, mfungaji hana budi kukizuilia (kukifungisha) kila kiungo chake cha mwili - macho, ulimi, masikio, mikono na miguu pamoja na fikra na hisia zake -na matendo aliyoyakataza Allah (s.w.). Funga ya macho ni kujizuilia kutazama yale yote aliyoyakataza Allah (s.w), funga ya ulimi ni kujizuilia na mazungumzo yote aliyoyakataza Allah (s.w), kama vile kusengenya, kusema uwongo, kugombana n.k., funga ya masikio ni kujizuilia kusikiliza yale yote aliyoyaharamisha Allah (s.w); funga ya miguu ni kujizuilia kuendea yale yote aliyotukataza Allah (s.w); funga ya fikra na hisia, ni kujizuilia na fikra na dhana mbaya ambazo zinampelekea mja kuvunja amri na makatazo ya Allah (s.w). Ni katika maana hii Mtume (s.a.w) anasema katika Hadith zifuatazo:

*"Abu Hurairah (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: Yule ambaye haachi kusema uwongo na haachi kufanya vitendo viovu, Allah hana haja na kuona kuwa anaacha chakula chake na kinywaji chake - ( Allah (s.w) hana haja na funga yake). (Bukhari).*

*Abu Hurairah (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema; Ni wangapi wamefunga lakini hawana funga ila kukaa na kiu tu, ni wangapi wanaoswali usiku ambao hawana swala ila huambulia kupoteza usingizi tu. (Darimi).*

Hadith hizi zinatuthibitishia kuwa ufungaji usioambatana na kujizuilia na maovu na machafu, haumpatii mfungaji faida yoyote.

**Umuhimu wa Funga ya Ramadhani katika Uislamu**

Funga ya Ramadhani ni miongoni mwa nguzo za Uislamu na ni faradh kwa Waislamu kama inavyobainika katika aya ifuatayo:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ كُتِبَ عَلَيْكُمُ ٱلصِّيَامُ كَمَا كُتِبَ
عَلَى ٱلَّذِينَ مِن قَبْلِكُمْ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ ﴿١٨٣﴾

*Enyi Mlioamini! Mmelazimishwa kufunga (swaum) kama walivyolazimishwa waliokuwa kabla yenu ili mpate kumcha Mungu. (2:183).*

Kama ilivyo katika nguzo nyingine za Uislamu, mtu atakapoivunja makusudi nguzo hii hatabakia kuwa Muislamu japo atajiita Muislamu na watu wakaendelea kumuita hivyo. Katika Hadhith iliyopokelewa na Ibn Abbas (r.a), Mtume (s.a.w) amesema:

*"Kuna viungo vitatu vinavyomuunganisha Muislamu na dini ya Uislamu na yeyote yule atakayevunja kiungo kimoja katika hivi atakuwa amekana Uislamu na kuuawa kwake ni halali.Viungo hivi ni: Kushuhudia kuwa Hapana Mola ila Allah, kusimamisha Swala Tano na Kufunga Mwezi wa Ramadhani."*

Katika Hadith nyingine Abu Hurairah (r.a) amesimulia kuwa mtume (s.a.w) amesema:

*"Yeyote yule atakayeacha makusudi kufunga siku moja ya Mwezi wa Ramadhani, hawezi kuifidia siku hiyo hata akifunga kila siku katika umri wake wote (uliobakia)" (Abu-Daud).*

Funga ni ibada maalum iliyo muhimu sana katika kumuandaa mja kuwa mcha Mungu kwa kule kukata kwake matamanio ya kimwili. Kwa hivyo Allah (s.w) kwa ukarimu wake ameahidi malipo makubwa kwa wenye kutekeleza ibada hii, ili iwe motisha wa kuwawezesha kuitekeleza ibada hii kwa hima kubwa na kwa ukamilifu unaotakikana.

Ahadi ya Allah (s.w) ya malipo makubwa kwa wenye kufunga Ramadhani tunaipata katika Hadith kama ifuatavyo:

*Abu Hurairah (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: Mwenye kufunga Ramadhani akiwa na imani na akawa na matumaini ya kupata malipo kutoka kwa Allah dhambi zake zote zilizopita husamehewa; na mwenye kusimama kwa swala (Tarawehe) katika mwezi wa Ramadhani akiwa na imani na matumaini ya kupata malipo (kutoka kwa Allah), dhambi zake zote zilizopita zitasamehewa. (Bukhari na Muslim).*

*Pia Abu-Hurairah(r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: Kila amali njema anayoifanya mwanaadam italipwa mara kumi (Al-Qur'an 6:160) mpaka kufikia mara mia saba (Al-Qur'an 2:261). Allah (s.w) amesema: "Ila kufunga kwa sababu funga ni kwa ajili Yangu, na ni Mimi mwenyewe nitakayelipa. Mwenye kufunga anakata matamanio yake ya kimwili na anaacha chakula kwa ajili Yangu. Kwa mwenye kufunga kuna furaha mbili, furaha moja anaipata wakati wa kufuturu na nyingine wakati atakapokutana na Mola wake. Na hakika harufu ya mdomo wa mwenye kufunga ni bora mbele ya Allah (s.w) kuliko harufu ya miski. Na funga ni ngao. Kwa hiyo atakayefunga miongoni mwenu hataongea maneno ya upuuzi wala hatagombana. Kama itatokea achokozwe na yeyote, au mtu ataka kupigana naye, na aseme: "Nimefunga". (Bukhari na Muslim).*

*Abdullah bin Amr (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: "Funga na Qur'an vitamwombea mtu shufaa. Saum itasema: Ee Bwana (Rabb) nilimwachisha chakula na kujamii wakati wa mchana, kwahiyo nifanye niwe muombezi wake. Na Qur-an itasema: Nilimwachisha usingizi wakati wa usiku, kwa hiyo nifanye niwe muombezi wake. Kwa hiyo vyote vitamuombea shufaa." (Baihaqi).*

Vile vile Mtume (s.a.w.) katika kusisitiza umuhimu wa funga ya Ramadhani alitoa khutuba mwishoni mwa mwezi wa Shaabani kama ilivyonukuliwa katika Hadith ifuatayo:

*Salman al-Farisy (r.a) ameeleza: Mtume (s.a.w) alituwaidhi mwisho wa siku ya Shaabani akasema: Enyi watu! Hakika umekujieni mwezi*

*mtukufu, mwezi uliobarikiwa, mwezi ambao ndani yake kuna usiku ulio bora zaidi kuliko miezi elfu moja. Allah (s.w) amefaradhisha kufunga katika mwezi huu na kusimama (kwa swala ya tarawehe) katika mausiku yake ni Sunnah. Atakayetekeleza kitendo kizuri kisicho faradhi atapata ujira wa mtu aliyetekeleza kitendo cha faradhi katika miezi mingine na yule atakayetekeleza kitendo cha faradhi atapata ujira mara 70 wa ujira wa kitendo hicho katika miezi mingine. Na ni mwezi wa subira, na ilivyo, subira malipo yake ni Pepo. Na ni mwezi wa kuhurumiana na mwezi ambao mahitaji (mapato) ya Muumini huongezwa. Atakayetoa futari kwa mwenye kufunga katika mwezi huu kuna kusamehewa dhambi zake na kuwekwa huru na Moto, na atapata malipo sawa na ya yule aliyefunga bila ya yeye kupunguziwa chochote." Tukauliza: Ee Mtume wa Allah! Hakuna yeyote kati yetu mwenye uwezo wa kumfuturisha mtu aliyefunga. Alijibu Mtume: Allah atamlipa yule mwenye kumfuturisha aliyefunga kwa funda la maziwa, au tende moja au funda la maji. Na yule anayekidhi haja ya mtu Allah atamnywesha kutokana na Birika (Kawthar) langu na hatakuwa na kiu mpaka atakapoingia Peponi.Na (Ramadhani) ni mwezi ambao mwanzo wake kuna kurehemewa, katikati yake kuna kusamehewa na mwisho wake kuna kuachwa huru na Moto. Na yule atakayempunguzia kazi mtumwa (mtumishi) wake, Allah atamsamehe, na atamuacha huru na Moto.*

Hadith hizi zinatupa picha juu ya umuhimu wa funga ya Ramadhan kwamba funga ni ngao ya kumzuia Muumini na maovu yanayosababishwa na matashi ya kimwili na itakuwa ni sababu ya Muumini kuingia peponi na kuachwa huru na moto.

**Kwa nini Funga imefaradhishwa Mwezi wa Ramadhani**

Japo tumefahamishwa katika Qur-an kuwa, faradhi ya funga ni kwa umma zote hatufahamu umma zilizotangulia zilifaradhishiwa kufunga miezi gani au wakati gani wa mwaka. Umma huu umefaradhishiwa kufunga katika mwezi wa Ramadhani kwa sababu ndio mwezi ilipoanza kushuka Qur-an kama tunavyofahamishwa katika aya ifuatayo:

شَهْرُ رَمَضَانَ ٱلَّذِىٓ أُنزِلَ فِيهِ ٱلْقُرْءَانُ هُدًى لِّلنَّاسِ وَبَيِّنَٰتٍ مِّنَ ٱلْهُدَىٰ
وَٱلْفُرْقَانِ ۚ فَمَن شَهِدَ مِنكُمُ ٱلشَّهْرَ فَلْيَصُمْهُ ۖ ... (١٨٥)

*"(Mwezi huo mliofaradhishwa kufunga) ni mwezi wa Ramadhani ambao ndani yake imeshuka hii Qur-an ili iwe uongozi kwa watu na hoja zilizowazi*

*za uongozi na upambanuzi. Atakayeshuhudia mwezi huu miongoni mwenu na afunge ....” (2:185).*

Hivyo, Waislamu wameamrishwa kufunga katika mwezi wa Ramadhani ili pamoja na kutekeleza amri hii wafikie lengo lililokusudiwa, vile vle iwe ni kumbukumbu ya kushuka Qur-an, Mwongozo wa Allah (s.w) wa mwisho kwa wanaadamu. Ni kwa msingi huu kusoma Qur-an kwa wingi katika mwezi huu kumesisitizwa zaidi. Qur-an ilianza kumshukia Mtume (.s.a.w) alipokuwa Jabal-Hira, usiku wa manane katika usiku mmoja wa Mwezi wa Ramadhani. Usiku huo mtakatifu ni “Lailatul’qadri” (Usiku Wenye Cheo) kama tunavyojifunza katika Suratul-Qadr.

إِنَّآ أَنزَلْنَٰهُ فِى لَيْلَةِ ٱلْقَدْرِ ﴿١﴾ وَمَآ أَدْرَىٰكَ مَا لَيْلَةُ ٱلْقَدْرِ ﴿٢﴾ لَيْلَةُ ٱلْقَدْرِ
خَيْرٌ مِّنْ أَلْفِ شَهْرٍ ﴿٣﴾ تَنَزَّلُ ٱلْمَلَٰٓئِكَةُ وَٱلرُّوحُ فِيهَا بِإِذْنِ رَبِّهِم مِّن
كُلِّ أَمْرٍ ﴿٤﴾ سَلَٰمٌ هِىَ حَتَّىٰ مَطْلَعِ ٱلْفَجْرِ ﴿٥﴾

*Hakika Tumeiteremsha (Qur’an) katika usiku wa Laylatul Qadri. Na jambo gani litakalokujulisha ni nini huo usiku wa Laylatul Qadri? Huo usiku wa heshima ni bora kuliko miezi elfu. Huteremka Malaika na roho katika (usiku) huo kwa idhini ya Mola wao kwa kila jambo. Ni amani (usiku) huo mpaka mapambazuko ya alfajiri(97:1-5)*

**Kuonekana kwa mwezi wa Ramadhani**

Swaumu ya Ramadhani inaanza kwa kuona mwezi baada ya siku ya 29 Shaaban au 30 Shaaban kama tunavyofahamshwa katika hadithi zifuatazo:

*“Ibn Umar (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: Msifunge mpaka muuone mwezi umeandama na msiache kufunga mpaka muone mwezi (wa Shawwal) umeandama. Kama kuna mawingu (hukuuona) hesabu kamili (siku 30). Katika simulizi nyingine amesema: Mwezi una masiku 29, kwa hiyo usifunge mpaka uone mwezi umeandama kama kuna mawingu subiri na kamilisha idadi ya siku 30.”*
*(Bukhari na Muslim)*

Kutokana na Hadithi hii ni wazi kuwa watu hawaruhusiwi kufunga kwa kufuata kalenda. Inabidi juhudi za kuuangalia mwezi ziwepo kwa

umma wa Waislamu tangu mwanandamo wa Shaaban.

*"Abu Hurairah (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah ameagiza: Hesabu mwandamo wa Shaaban kwa ajili ya Ramadhani". (Tirmidh).*

**Kwanini kufuata mwandamo wa mwezi?**

Tunafunga kwa kuona mwezi kwa sababu ndivyo alivyotuamrisha Mtume wa Allah (s.w) kama tulivyojifunza kutokana na hadithi zilizonukuliwa hapo juu. Kumtii Mtume (s.a.w) ndio Uislamu. Rejea Qur-an katika aya zifuatazo:

قُلْ أَطِيعُوا۟ ٱللَّهَ وَٱلرَّسُولَ ۖ فَإِن تَوَلَّوْا۟ فَإِنَّ ٱللَّهَ لَا يُحِبُّ ٱلْكَٰفِرِينَ ﴿٣٢﴾

*"Sema: "Mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Na mkikengeuka (Allah atakuadhibuni) kwani Allah hawapendi makafiri." (3:32)*

وَمَآ ءَاتَىٰكُمُ ٱلرَّسُولُ فَخُذُوهُ وَمَا نَهَىٰكُمْ عَنْهُ فَٱنتَهُوا۟ ۚ

*"... Na anachokuleteeni Mtume, kipokeeni, na anachowakataza kiacheni..." (59:7).*

مَّن يُطِعِ ٱلرَّسُولَ فَقَدْ أَطَاعَ ٱللَّهَ ۖ

*"Anayemtii Mtume, kwa yakini amemtii Mwenyezi Mungu..." (4:80)*

Pia amri hii ina hekima yake. Mwaka unaohesabiwa kwa mwandamo wa mwezi una siku 354 kwani kwa wastani mwezi mmoja una siku 29½. Mwaka unaohesabiwa kwa kufuata jua, muda ambao dunia huchukua kulizunguka jua una siku 365, saa 5, dakika 48 na nukta 46. Kwa hiyo ukilinganisha mwaka wa hesabu ya mwezi na mwaka wa hesabu ya jua, utaona kuwa mwaka wa mwezi ni mfupi kwa siku10 hivi. Hivyo mwezi wa Ramadhani hurudi nyuma siku kumi katika kila mwaka ukilinganisha na mwaka wa jua. Hivyo basi, mtu yeyote atakayejaaliwa kufunga muda wa miaka 36 hatakuwa na siku au msimu katika mwaka ambao hakuufunga. Yaani atawahi kufunga siku zote za jua, za mvua, za upepo, za shwari, za kusi, za kaskazi na kadhalika. Kama ingelikuwa inafuatwa kalenda ya mwaka wa jua, wengine daima wangalifunga nyakati za joto tu, wengine nyakati za baridi tu, wengine nyakati za njaa tu, wengine nyakati za mavuno na kadhalika ilimuradi pasingalikuwa na mabadiliko.

### Ni lazima kila mfungaji aone mwezi?

Mwezi wa Ramadhani akiona mtu mmoja muadilifu inatosha na wengine waliobaki itawabidi wafunge. Hivi ndivyo alivyoamrisha Mtume (s.a.w) kama tunavyojifunza katika hadithi zifuatazo:

*"Ibn Abbas (r.a) ameeleza kuwa Mwarabu wa Jangwani alikuja kwa Mtume (s.a.w) akasema: Hakika nimeuona mwezi wa Ramadhani umeandama. Mtume (s.a.w) akamuuliza: Unashuhudia kuwa hapana Mola ila Allah? "Ndio" alijibu. Akamuuliza tena: Unashuhudia kuwa Muhammad ni Mtume wa Allah? Akajibu "Ndio". Akasema (Mtume): Ee Bilal! Watangazie watu kuwa hawana budi kufunga kesho". (Abu Daud, Tirmidh, Nisai, Ibn Majah).*

*"Ibn Omar (r.a) ameeleza: Watu waliuona mwezi. Kisha nikamfahamisha Mtume (s.a.w): Hakika nimeuona. Kwa hiyo alifunga na aliwaamrisha watu wafunge". (Abu Daud, Darimi).*

### Mwezi ukionekana sehemu moja, Waislamu wote ulimwenguni watalazimika kufunga?

Waislamu wote wanakubaliana kutokana na hadithi tulizozinukuu hapo juu, kuwa mtu mmoja au watu wachache wakishuhudia kuandama mwezi wa Ramadhani, Waislamu watalazimika kufunga. Pia waislamu wote wanakubaliana kuwa watu wa wili au zaidi wakishuhudia kuandama kwa mwezi wa Shawwal, Waislamu watalazimika kufuturu na kuswali Iddil-Fitr.

Hitilafu kati ya Waislamu juu ya swala la watu wachache kushuhudia kuandama mwezi wa Ramadhani au wa Shawwal ipo kwenye umbali, kwamba ni watu wa wapi wafunge watakaposikia habari za kuandama mwezi kutoka wapi? Juu ya suala hili Waislamu wamegawanyika katika makundi mawili yafuatayo:

**Kundi la kwanza** ni la wale wanaosema kuwa mwezi ukionekana katika mji mmoja au sehemu moja, basi Waislamu wengine popote walipo ulimwenguni watalazimika kufunga au kufungua. Haya pia ni maoni ya Imamu Hambali, Malik na Abu Hanifa. Hawa wamejiegemeza katika hadithi tulizozinukuu hapo juu.

**Kundi la pili** ni la wale wanaojiegemeza katika Hadithi ifuatayo:
*Kurayb (r.a) ameeleza kuwa Umm Fadhl, binti wa Harith alimtuma (mtoto wake) Fadhl Syria (Sham) kwa Muawiya. Fadhl aliwasili Syria na akatekeleza yale aliyotumwa na mama yake. Alipokuwa pale Syria mwezi*

*wa Ramadhani ulianza. (Amesema Fadhl): Niliuona mwezi wa Ramadhani ulipoandama siku ya Ijumaa. Kisha nilirudi Madina mwishoni mwa mwezi. "Abdullah bin Abbas (r.a) aliniuliza juu ya kuandama kwa mwezi wa Ramadhani na akasema: Mliuona lini? Nikajibu: Tuliuona usiku wa Ijumaa. Akaniuliza; Uliona wewe mwenyewe? Nikajibu; Ndio na watu pia waliuona na walifunga na Muawiya pia alifunga, ndipo akasema; lakini sisi tuliuona usiku wa Jumamosi. Kwa hiyo tutaendelea kufunga mpaka tukamilishe 30 au tuuone mwezi Shawwal baada ya 29 Ramadhani) Nikauliza; (Fadhili): kuonekana kwa Mwezi wa Muawiya hakukutosha? Akajibu; Hapana hivi ndivyo Mtume wa Allah (s.w) alivyotuamrisha". (Muslim).*

Kutokana na hadithi hii kama kuna masafa marefu kati ya mji ulipoonekana mwezi na mji watu walipopata taarifa juu ya kuonekana kwake haitajuzu kwao kufuata mwandamo huo, lakini endapo mji huo utakuwa umekaribiana basi watu waliopata taarifa ya kuandama mwezi kutoka mji wa karibu watawajibika kufunga au kufungua, mwanachuoni mashuhuri anayeshikilia rai hii ni Imamu Shafii.

Kutokana na hitilafu hizi, imetokea kuwa waislamu wote ulimwenguni hawaanzi kufunga Ramadhani siku moja na kuswali Iddil-Fitr na Iddil Hajj siku moja. Wale wanaoshikilia raia ya kwanza, wanaona kuwa si vyema umma mmoja wa Kiislamu kutofautiana katika matukio haya muhimu ambayo ni alama ya dini. Isitoshe kutokana na maendeleo ya sayansi, mawasiliano ulimwenguni hivi leo yamerahisika mno. Ulimwengu mzima unaweza kupata habari kwa muda wa dakika chache juu ya mwandamo wa mwezi katika mji mmoja.

Wale wanaoshikilia rai ya pili wanaoona kuwa si vyema kufunga au kufungua Ramadhani kwa kufuata habari ya kuandama kwa mwezi kutoka popote pale bila ya kujali masafa au machweo (matlai) kati ya mji huo na pale habari ya kuandamana mwezi ilipopokelewa. Kwani kijiografia sehemu mbali mbali za ulimwengu zinatofautiana sana. Kutokana na uchunguzi wa anga umepatikana ushahidi kuwa kuna kutofautiana katika kuona mwezi ambako katika mji mmoja kuna uwezekano mkubwa kabisa wa kuona mwezi endapo hapatakuwa na mawingu, katika mji mwingine ulio masafa ya mbali na matlai mengine, mwezi hauandami kabisa siku hiyo hata kama hapata kuwa na mawingu. Kwa hiyo hawa wenye mtazamo wa pili, pia kutokana na maendeleo hayo hayo ya kisayansi, wanaona kuwa hadithi zilizowaamrisha watu kufunga au kufungua kwa kupata habari ya kuandama mwezi kutoka kwa mtu mmoja au watu wachache, hazionyeshi kuwa wale walioleta habari za kuandama

mwezi walitoka masafa marefu na pale alipokuwa Mtume (s.a.w).

Kutokana na rai hizi mbili, ni vema Waislamu wasigombane kwa jambo hili. Kila mtu ana uhuru wa kufuata hoja iliyomtua zaidi. Hata hivyo, lingelikuwa jambo zuri kama wanachuoni wa kila jimbo lenye uhusiano mwema kama vile Afrika ya Mashariki, wangelijadiliana na kukubaliana juu ya msimamo mmoja.

## Nguzo za Funga

Nguzo za funga ni mbili: Kutia Nia na kujizuilia na kila chenye kufunguza tangu mwanzo wa alfajiri mpaka kuingia magharibi.Nia ni dhamira anayokuwa nayo mtu moyoni mwake kuwa atafunga. Nia ya funga ya faradhi inatakiwa iletwe kabla ya Alfajir, kwa mnasaba wa Hadith ifuatayo:

*Bibi Hafsah (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: ambaye hakunuia kufunga kabla ya alfajir, hana funga. (Tirmidh, Abu Daud, Nisai).*

Ama nia ya funga za sunnah, inaweza kuletwa mchana iwapo mtu hajala chochote tangu alfajir kama tunavyojifunza katika Hadith ifuatayo:

*Aisha, Mama wa Waumini (r.a) ameeleza: Mtume (s.a.w) alikuja kwangu siku moja akaniuliza: Una chochote (cha kula)? Nilijibu: Hakuna. Kisha akasema: "Basi nitafunga." Siku nyingine alikuja tena kwetu tukamuambia: Mtume wa Allah, tumeletewa zawadi ya Hais (aina ya chakula cha mchanganyiko wa Tende na Siagi). Kisha akasema: "Nionyeshe, nilifunga tangu asubuhi. Kisha alikula chakula kile." (Muslim).*

Katika Hadith hii tunajifunza mambo mawili. Kwanza tunajifunza kuwa mtu anaweza kunuia funga ya sunnah mchana kabla ya adhuhuri, iwapo atakuwa hajala chochote tangu alfajiri.

**Pili,** tunajifunza vile vile kutokana na Hadith hii kuwa mtu anaruhusiwa kuvunja funga ya sunnah pasi na sababu ya kisharia.

## Yanayobatilisha Funga

Mtu aliyefunga analazimika kujizuilia na vitendo mbalimbali ambavyo hubatilisha funga yake. Mfungaji akifanya moja wapo katika yafuatayo swaum yake itabatilika.

### (i) Kula na Kunywa

Ukila au ukinywa chochote kile kwa kudhamiria hata ikiwa ni dawa utakuwa umefungulia. Vile vile ukivuta sigara au chochote kile au ukivuta dawa ya mafua kwa pua utakuwa umefungua. Pia kupitisha chochote puani au masikioni kwa kudhamiria, hata ikiwa dawa utakuwa umefungua.

Ikumbukwe kuwa kujifunguza makusudi katika mwezi wa Ramadhani kwa kula na kunywa bila ya udhuru wowote wa kisharia ni kosa kubwa sana mbele ya Allah(s.w) kwa kiasi ambacho hata kama mtu atafunga umri wake wote hataweza kuilipia hiyo siku moja aliyojifunguza makusudi kama tunavyojifunza katika Hadith ifuatayo:

*Abu Hurairah(r.a) ameeleza kuwa Mtume (s.a.w) amesema: Yule anayefungua siku moja ya Ramadhani bila kuwa mgonjwa au kuwa na udhuru mwingine wa kisheria, hata akifunga maisha yake yote hataweza kuilipia funga hiyo. (Ahmad, Tirmidh, Abu Daud, Ibn Majah, Darimi).*

Hadith hii inatuasa tusifanyie mas-khara amri za Allah (s.w). Hivyo mtu akijifunguza makusudi ajue wazi kuwa amefanya kosa kubwa ambalo halitasameheka kwa kuilipia tu siku hiyo bali ni lazima pia arejee kwa Mola wake kwa toba ya kweli.

### (ii) Kujitapisha Makusudi

Mtu akijitapisha makusudi funga yake itavunjika kutokana na Hadith ifuatayo:

*Abu Hurairah(r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: Anayeshindwa kuzuia matapishi halipi. Lakini anayejitapisha makusudi, na alipe. (Tirmidh, Abu Daud, Ib Majah).*

Kutokana na Hadith hii kutapika kwa ugonjwa hakufunguzi.

### (iii) Kupatwa na Hedhi au Nifasi

Mwanamke akipatwa na hedhi au nifasi hata kama imempata nyakati za mwisho kabla ya jua kuchwa, atakuwa amefungua na atalazimika kuilipia siku hiyo baada ya Ramadhani.

### (iv) Kujitoa Manii Makusudi

Ukijitoa manii kwa mkono au kwa kubusiana na kukumbatiana

mume na mke, au kwa njia nyingine yoyote ile utakuwa umefungua.Kutokwa na manii kwa kuota au kwa njia nyingine isiyokuwa ya makusudi, hakufunguzi.

**(v) Kunuia Kula na hali umefunga**

Ukinuia kula hata kama hukula swaumu yako itakuwa imebatilika kwa kuwa utakuwa umevunja nguzo moja ya funga - nia.

**Yanayoharibu au Kupunguza Thamani ya Funga**

Yanayoharibu funga ya mtu au kupunguza thamani yake ni kujiingiza katika mazungumzo yaliyokatazwa kama vile kusengenya, kusema uwongo, kupiga porojo, n.k., na kujiingiza katika matendo maovu. Japo mtu mwenye kufanya matendo haya atajiona amefunga kwa vile atakuwa hajala, au hajanywa au hajafanya kitendo chochote katika vile vinavyobadtilisha funga atakuwa hana funga au hakupata malipo ya funga kwa ushahidi wa Hadith ifuatayo:

*Abu Hurairah(r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: "Yoyote yule ambaye hataacha mazungumzo mabaya na vitendo viovu, Allah (s.w) hana haja na kuacha kwake chakula chake na kinywaji chake (Allah (s.w) hatapokea funga yake). (Bukhari).*

Wakati mmoja Mtume (s.a.w) aliwaamuru watu wawili wafuturu (wavunje funga) kwa sababu walikuwa wanasengenya.

Wanachuoni wameshindwa kutoa uamuzi kuwa mtu akizungumza maneno maovu na machafu au akijiingiza katika matendo maovu, atakuwa amefungua kwa sababu ni vigumu kujua matendo ya ndani ya mtu. Hivyo, japo hapatakuwa na mtu yeyote atakayekuambia umefungua kwa kufanya vitendo viovu, wewe mwenyewe ujihesabu kuwa hukupata kitu kutokana na funga yako kama Mtume (s.a.w) anavyotufahamisha katika hadith ifuatayo:

*"Abu Hurairah (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: Ni watu wangapi wanaofunga, lakini hawana funga ila huambulia kiu tu ..." (Darimi).*

Mfungaji anatakiwa, ili funga yake iweze kutimia na kufikia lengo, ajiepushe na mambo yote maovu na machafu. hata akichokozwa na mtu, ajiepushe kugombana naye kwa kumwambia, "Nimefunga, nimefunga" kama anavyotushauri Mtume (s.a.w):

*Abu Hurairah (r.a) ameeleza kuwa Mtume (s.a.w) amesema: Wakati mmoja*

*wenu atakapoamka akiwa amefunga, asitumie au asitoe lugha chafu na asifanye matendo maovu. Na kama yeyote yule anamchokoza au anagombana naye, hana budi kusema: "Nimefunga, nimefunga."*

### Yasiyobatilisha funga

Kuna baadhi ya mambo ambayo mtu aliyefunga akiyafanya, anaweza kujiona kuwa amefungua lakini bado hajafungua. Miongoni mwa mambo haya ni:

### (i) Kula au Kunywa kwa Kusahau

Mtu akiwa amesahau kuwa amefunga akala au akanywa kiasi chochote, hata kiasi cha kushiba, bado atakuwa na swaumu kwa ushahidi wa Hadith zifuatazo:

*Abu hurairah(r.a) amesema kuwa Mtume (s.a.w) amesema: "Anayefungua Ramadhani kwa kusahau hatalipa wala hatatoa kafara" (Daral Qutni, Bayhaqi na Hakim).*

*Abu Hurairah ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: Yeyote yule atakayesahau akala au akanywa wakati amefunga, na amalizie funga yake kwa sababu Allah (s.w) amemlisha na kumnywesha". (Bukhari na Muslim).*

Hali kadhalika, kama mtu atalishwa au kunyweshwa au kufuturishwa kwa namna yoyote ile kwa kutezwa nguvu, saumu yake haitabatilika:

*Ibn Abbas (r.a) ameeleza kwamba Mtume (s.a.w) amesema: "Mwenyezi Mungu ameuondolea umati wangu (Jukumu la) kukosea, kusahau na waliotezwa nguvu." (Ibn Majah, Tabran na Hakim).*

### (ii) Kuoga wakati umefunga

Kuoga kwa kujimwagia maji au kujitumbukiza majini hakuharibu funga kwa maana imepokelewa kwamba Mtume (s.a.w) alikuwa akijimwagia maji kichwani kwa sababu ya kiu au joto, hali amefunga:

*Mmoja wa Maswahaba ameeleza: Hakika nimemuona Mtume (s.a.w) akiwa Arji (bonde moja kati ya Makka na Madina) akijimwagilia maji kichwani mwake akiwa amefunga kwa sababu ya kiu au joto. (Malik, Abu Daud).*

### (iii) Kutokwa na Manii

Mtu akitokwa na manii kwa kuota au kwa namna ambayo hakukusudia, atakuwa hajafungua.

### (iv) Kuamka na Janaba

Kuamka na janaba hakufunguzi kwani Mtume (s.a.w) wakati mwingine alikuwa anaamka na janaba na huku amefunga.

*Aysha (r.a) ameeleza kuwa alfajiri iliingia wakati Mtume (s.a.w) yuko katika janaba. Kisha alioga na kuendelea na swaumu. (Bukhari na Muslim).*

Hali kadhalika mwenye hedhi au nifasi, ambaye damu yake ilikoma kabla ya alfajiri, akiamka atafunga hata kama atakuwa hajaoga.

### (v) Kubusiana na kukumbatiana Mume na Mke

Mtu kumbusu na kumkumbatia mkewe au mumewe wakati amefunga haiharibu funga iwapo kuna haja ya kufanya hivyo alimradi tu waweze kujizuia wasiendelee zaidi ya hapo. Hivi ndivyo tunavyojifunza katika Hadithi ifuatayo:

*Aysha (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah alikuwa akimbusu na kumkumbatia wakati amefunga na alikuwa mwenye kumiliki matashi yake kuliko yeyote miongoni mwenu (Bukhari na Muslim).*

*Amehadithia baba wa Hisham kuwa: Aysha (r.a) amesema: "Mtume wa Allah alikuwa akiwabusu baadhi ya wake zake akiwa amefunga: na kisha akacheka. (Bukhari).*

Miongoni mwa Masahaba walioruhusu hili la mtu kumbusu na kukumbatia mkewe wakati amefunga ni Sayyidna Umar (r.a), Ibn Abbas (r.a.), Abu-Hurairah (r.a) na Bibi Aysha (r.a). Kwa maoni ya Imam Abu Hanifa na Shafii, kumbusu na kumkumbatia wakati mtu amefunga ni makruhu iwapo kutaamsha matamanio. Vinginevyo si makruhu, lakini ni bora kuacha iwapo hapana haja ya lazima kufanya hivyo.

### (vi) Kupiga Mswaki

Si vibaya kupiga mswaki wakati mtu amefunga kwani Mtume (s.a.w) alikuwa akipiga mswaki wakati amefunga kama tunavyofahamishwa katika Hadith zifuatazo:

*Amr bin Rabiyah (r.a) ameeleza: Nilimuona mtume (s.a.w) Mara nyingi nisizoweza kuhesabu akipiga mswaki akiwa amefunga.(Tirmidh na Abu Daud).*

*Amesimulia Abu Hurairah(r.a) kuwa Mtume (s.a.w) amesema: Si kwa kuwa ninahofia kuwa litakuwa jambo zito kwa ummati wangu, ningekuwa nimeshawaamrisha kutumia mswaki (kupiga mswaki) kila wakitawadha. (Bukhari).*

Hadith hii haikubagua mtu aliyefunga na asiyefunga. Bali tunapata fundisho kuwa kupiga mswaki ni kitendo kilichosisitizwa sana.

*Bibi Aysha (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: "Mswaki hutakasa mdomo na ni njia ya kutakia Radhi za Allah (s.w)." (Bukhari).*

**(vii) Kusukutua na kupandisha Maji Puani**

Wakati mtu anatawadha anaruhusiwa kusukutua na kupandisha maji puani lakini asifanye sana mpaka maji yakaingia ndani kwani hilo amelikataza Mtume (s.a.w) katika Hadith iliyopokelewa na Abu Daud, Tirmidh, Ibn Majah na Nasai.

**(viii) Kupaka Wanja na Dawa ya Machoni**

Kupaka wanja kunaruhusiwa kwa mtu aliyefunga Mtume (s.a.w) ameruhusu hilo katika Hadith ifuatayo:

*Anas(r.a) ameeleza kuwa mtu mmoja amekuja kwa Mtume (s.a.w) na akasema: "Ninaumwa macho. Ninaweza kupaka wanja wakati nimefunga? `Ndio' Alijibu Mtume (s.a.w)."*

Pia dawa ya macho iwe ya mafuta au ya maji inaruhusiwa kutumiwa wakati mtu amefunga kwa sababu hapana tundu la kuungana moja kwa moja na koo kama yalivyo matundu ya pua na masikio.

**(ix) Kumeza usichoweza kujizuia nacho**

Ukimeza vitu usivyoweza kujizuia kama vile mate, kohozi, vumbi la njiani, vumbi la unga, kumeza mdudu aliyeingia kwa ghafla hadi kooni, n.k. utakuwa hujafungua.

**(x) Kujipaka mafuta au manukato**

Kujipaka mafuta au manukato mwilini au nguoni, kunusa manukato, kujifukiza udi na ubani, n.k. hakuharibu funga.

**(xi) Kuumika au kutoa Damu**

Kuumika hakufunguzi kwani Mtume (s.a.w) amefanya hivyo wakati akiwa amefunga kama tunavyofahamishwa katika Hadith ifuatayo:

*Amehadithia Ibn Abbas (r.a) kwamba Mtume (s.a.w) aliumikwa akiwa katika "Ihram" na pia akiwa amefunga. (Bukhari).*

Hata hivyo, kama kuumika huko kutamfanya mtu awe dhaifu, basi itakuwa ni makruhu. Hali kadhalika mtu anaruhusiwa kutoa damu kwa ajili ya kuwasaidia wagonjwa (blood transfusion), akiwa amefunga.

**(xii) Kupiga Sindano**

Kupiga sindano ya dawa, iwe ya mshipa au chini ya ngozi, haifunguzi.

## Waislamu Wanaolazimika Kufunga Ramadhani

**(i) Wenye akili timamu**

Kila ibada katika Uislamu inamtaka mja awe hadhiri (conscious) wakati wa kuifanya. Hivyo mwendawazimu au punguani hatalazimika kufunga au kufanya ibada yoyote ile, hana thawabu mbele ya Allah (s.w) kwa jema atakalolifanya na hatapata dhambi kwa ovu atakalolifanya.

**(ii) Waliofikia Baleghe**

Kwa mtazamo wa Uislamu mtu huhesabiwa kuwa amekua kiakili na kuweza kutumia vizuri uhuru wake wa hiari anapofikia baleghe. Baleghe hufikiwa na mtoto wa kiume au wa kike anapokuwa na umri wa miaka 15 au kwa mtoto wa kiume kuota na kutokwa na manii na kwa mwanamke kuanza kupata hedhi hata kama hawajafikia umri wa miaka 15. Muislamu anapokuwa baleghe huhesabiwa kuwa ni mtu mzima mwenye kulazimika kutekeleza kila amri ya Uislamu, hivyo hesabu yake ya amali njema na mbaya huanza kuingizwa katika kitabu chake tangu wakati huo. Hivyo mtoto ambaye hajafikia baleghe halazimiki kufunga kama tunavyofahamishwa katika Hadith ifuatayo:

*Ali (r.a) ameeleza kwamba Mtume (s.a.w) amesema: "(Watu) watatu wameondolewa kalamu (hawaandikiwi dhambi) Mwenda wazimu mpaka arudiwe na akili, aliyelala mpaka aamke, na mtoto mpaka abaleghe." (Ahmad, Abu Daud, Tirmidh).*

Pamoja na kwamba watoto ambao hawajabaleghe hawalazimiki kufunga, wanatakiwa wazoeshwe kufanya hivyo tangu wangali wadogo. Walifanya hivyo masahaba wa Mtume (s.a.w) kama tunavyofahamishwa katika Hadith ifuatayo:

*Rubayyi bint Mu'awwidh (r.a) amesimulia kuwa Mtume (s.a.w) alimtuma mtu mmoja asubuhi siku ya Ashura, kwenda vijiji vya Answaar (na ujumbe huu): Aliyeamka na hali amefunga basi na akamilishe swaumu yake. na aliyeamka na hali amekula, basi na afunge sehemu iliyobaki ya siku*

*yake. Tukawa tunaifunga siku hiyo (ya Ashura) baada ya hapo, na kuwafungisha watoto wetu wadogo. Tukienda msikitini tulikuwa tukiwatengenezea vitu vya kuchezea vya sufi. Mmoja wao akililia chakula, tukimpa vitu hivyo (vya kuchezea) mpaka ufike wakati wa kufungua (kufuturu). (Bukhari na Muslim).*

Si katika ibada ya funga tu tunapotakiwa tuwazoweshe watoto wetu, bali katika kila ibada na kila mwenendo mwema. Katika Hadith nyingine Mtume (s.a.w) ametuagiza tuanze kuwazoesha watoto wetu kufanya hizi ibada maalum kama vile kuswali na kufunga wanapokuwa na umri wa miaka saba na wanapofikia umri wa miaka kumi tuwalazimishe kwa viboko endapo watazichenga ibada hizi.

**(iii) Wenye afya**

Wanaolazimika kufunga ni wale wenye afya nzuri. Wagonjwa wameruhusiwa kutofunga kama tunavyojifunza katika aya ifuatayo:

وَمَن كَانَ مَرِيضًا أَوْ عَلَىٰ سَفَرٍ فَعِدَّةٌ مِّنْ أَيَّامٍ أُخَرَ ... ﴿١٨٥﴾

*"... Na mwenye kuwa mgonjwa au safarini, basi (atimize hesabu) katika siku nyingine ..." (2:185).*

Mgonjwa akijiona hana afya ya kumuwezesha kufunga au kama anatakiwa kunywa dawa mchana, basi anaruhusiwa kutofunga. Lakini mgonjwa akijiona kuwa anaweza kufunga bila ya kuathirika anaruhusiwa kufunga. Hapa Muislamu amepewa uhuru wa kuamua kufunga au kutofunga kulingana na anavyojisikia yeye mwenyewe. Lakini iwapo Muislamu atafunga kwa kujikalifisha atakuwa amehalifu amri ya Allah (s.w), japo funga yake inaweza kukubalika. Allah (s.w) katika Qur-an anatuasa:

... وَلَا تَقْتُلُوٓا۟ أَنفُسَكُمْ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ كَانَ بِكُمْ رَحِيمًا ﴿٢٩﴾

*"...Wala msijiue, hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kukuhurumieni." (4:29).*

Pia baada ya Allah (s.w) kutoa ruhusa ya kutofunga wasafiri na wagonjwa, anaonyesha huruma zake kwa kutufahamisha:

... يُرِيدُ ٱللَّهُ بِكُمُ ٱلْيُسْرَ وَلَا يُرِيدُ بِكُمُ ٱلْعُسْرَ وَلِتُكْمِلُوا۟ ٱلْعِدَّةَ وَلِتُكَبِّرُوا۟ ٱللَّهَ عَلَىٰ مَا هَدَىٰكُمْ وَلَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿١٨٥﴾

*"... Mwenyezi Mungu anakutakieni yaliyo mepesi wala hakutakieni yaliyo mazito, na pia (anakutakieni) mtimize hisabu hiyo, na (anakutakieni) kumtukuza Mwenyezi Mungu kwa kuwa amekuongozeni, ili mpate kushukuru." (2:185).*

Mgonjwa atakayetumia ruhusa hii analazimika kulipa siku alizokula katika miezi mingine atakapokuwa mzima. Mama wajawazito au wale wanaonyonyesha, wakaona kuwa hawataweza kufunga kwa kuhofia afya zao na watoto wao, nao wanaruhusiwa kutofunga Ramadhani na wanalazimika kulipa siku walizokula katika miezi mingine. Wazee vikongwe na wagonjwa wale ambao hawategemei kupona kama vile wagonjwa wa kisukari, ambao hawawezi kufunga katika mwezi wowote ule, watatoa fidia kwa kuwalisha maskini kwa kutoa kibaba kimoja cha chakula kinachopendelewa na wakazi wa mji, au kutoa thamani yake kwa kila siku ya mwezi wa Ramadhani kama Qur-an inavyoelekeza:

... وَعَلَى ٱلَّذِينَ يُطِيقُونَهُۥ فِدْيَةٌ طَعَامُ مِسْكِينٍ ۖ ... ﴿١٨٤﴾

*"... Na wale wasioweza, watoe fidiya kwa kumlisha maskini ..." (2:184).*

### (iv) Wakazi wa Mji

Muislamu anayekutwa na Ramadhani akiwa ametulia katika mji ni lazima afunge.

... فَمَن شَهِدَ مِنكُمُ ٱلشَّهْرَ فَلْيَصُمْهُ ۖ ... ﴿١٨٥﴾

*"(... Atakayekuwa katika mji) atakapoushuhudia mwezi (wa Ramadhani) afunge ...." (2:185).*

Kwa upande mwingine msafiri ameruhusiwa kutofunga kama tunavyojifunza katika Qur-an:

وَمَن كَانَ مَرِيضًا أَوْ عَلَىٰ سَفَرٍ فَعِدَّةٌ مِّنْ أَيَّامٍ أُخَرَ ۗ ... ﴿١٨٥﴾

*"...Na mwenye kuwa mgonjwa au safarini, basi atimize hesabu (ya siku*

*alizoacha kufunga) katika siku nyingine ..." (2:185).*

Katika aya hii msafiri anaruhusiwa kutofunga akipenda. Pia anaweza kufunga akipenda. Uhuru wa kufunga au kutofunga uko kwa msafiri mwenyewe. Tunajifunza katika Hadith mbali mbali kuwa hawakuwa Maswahaba wote wakifunga walipokuwa safarini wala hawakuwa wote wanakula katika msafara huo huo mmoja. Hebu turejee Hadith zifuatazo:

*'Aysha (r.a) amesimulia kuwa Hamza bin 'Amr Al'Hisham (r.a) alimuuliza Mtume (s.a.w) juu ya funga katika safari: "Ewe Mtume wa Allah, mimi nina nguvu za kufunga katika safari. Je nina kosa (nikifunga)? "Akajibu (Mtume):'Hiyo ni ruhusa kutoka kwa Allah, atakayeichukua vema. Na anayependa kufunga hana kosa." (Muslim).*

Katika Hadith nyingine Sayyid al-Khudri (r.a) ameeleza:

*"Tuliungana na Mtume (s.a.w) katika vita vya Jihad, mwezi 16 Ramadhani. Miongoni mwetu walifunga na wengine hawakufunga. Aliyefunga hakumuona ana makosa yule asiyefunga na yule asiyefunga hakumtia makosani yule aliyefunga." (Muslim).*

Kama msafiri kutokana na mazoea yake kuhusu safari hiyo, hapana shida yoyote atakayoipata iwapo atafunga, basi ni vema afunge kwa kuzingatia ushauri wa Mtume (s.a.w) katika Hadith ifuatayo:

*"Salman bin Al-Musabbiq(r.a) amesimulia kuwa mtume wa Allah amesema: Yule ambaye atakuwa anasafiri na mnyama ambaye atamfikisha mahali ambapo atapata chakula cha kutosha, na afunge popote pale Ramadhani itakapomkuta" (Abu Daud).*

Hadithi hii haiondoi ruhusa ya kutofunga katika safari bali inamrahisishia msafiri kuchukua uamuzi wa kufunga pale ambapo ana usafiri wa uhakika utakaomwezesha kupata futari na daku. Lakini iwapo Muislamu ataanza safari yake akiwa amefunga, kisha katikati ya safari atapatwa na matatizo ni vema afungue kama tunavyojifunza katika Hadith zifuatazo:

*Anas (r.a) ameeleza: Tulikuwa na Mtume (s.a.w) safarini. Miongoni mwetu walifunga na miongoni mwetu hawakufunga. Tulitua mahali katika siku ya joto (jua kali). Wale waliofunga walianguka chini (hawakujijua) na wale ambao hawakufunga walibakia imara. Walikita mahema yao na kuwanywesha ngamia wao. Mtume (s.a.w) akasema:"Wale ambao hawakufunga wanatoka na thawabu leo zaidi kuliko wale waliofunga)."*

*(Bukhari na Muslim).*

*Jabir (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah alikuwa safarini. Aliona kundi la watu na mtu mmoja aliyelazwa kivulini.Akauliza: "Kuna nini?" Wakamjibu: "Mtu aliyefunga". Akasema (Mtume): "Kufunga katika safari si faradhi." (Bukhari na Muslim).*

Umbali gani wa safari Muislamu anaruhusiwa kutofunga? Hapana masafa maalum ya safari yaliyowekwa kama kipimo cha kufunga au kutofunga katika safari. Hili nalo limeachwa huru kwa msafiri mwenyewe kutegemeana na njia ya usafiri atakayoitumia. Safari yoyote ile ambayo mtu anaruhusiwa kupunguza swala, pia ameruhusiwa kutofunga.

Hali kadhalika, msafiri atakapokuwa ugenini anaruhusiwa kula kwa muda wa siku anazoruhusiwa kupungaza swala zake. Tunazidi kusisitiza kuwa uamuzi wa kufunga au kutofunga utategemea hali atakayoikuta msafiri huko ugenini. Iwapo atafika mahali ambapo anapata futari na daku yake pasina wasiwasi ni vyema afunge. Kama huko ugenini patakuwa na wasiwasi wa kupata mahitaji haya, basi ni vyema kutofunga mpaka anaporejea nyumbani. Jambo muhimu la kuzingatia ni kwamba, msafiri atalazimika kukamilisha siku alizokula katika miezi mingine.

### (v) Kwa Mwanamke, asiwe katika Hedhi wala Nifasi

Mwanamke aliye katika hedhi au nifasi ni haramu kwake kufunga, na analazimika kufunga siku alizoacha tofauti na swala kama tunavyojifunza katika Hadith ifuatayo:

*'Aysha (r.a) amesema: Tulikuwa tukipata hedhi wakati wa Mtume (s.a.w) tukaamrishwa kulipa saum wala hatukuamrishwa kulipa swala." (Bukhari na Muslim).*

## Hukumu ya Muislamu Aliyeacha Kufunga kwa Makusudi

Japo kadha ya Ramadhani inaruhusiwa kwa yule aliyeruhusiwa kutofunga kutokana na udhuru wa kisheria, kadha haitajuzu kwa mtu aliyeacha makusudi, kwani hata akifunga mwaka mzima hawezi kuilipia siku hiyo moja aliyoacha kufunga pasi na udhuru kwa ushahidi wa Hadith ifuatayo:

*Abu Hurairah (r.a) amesema kuwa Mtume (s.a.w) amesema: Mwenye kula siku moja ya Ramadhani bila ya ruhusa iliyotolewa na Mwenyezi Mungu, basi Swaum hiyo hailipiki hata akifunga mwaka mzima. (Abu, Daud, Ibn Majah na Tirmidh).*

Fundisho kubwa tunalolipata hapa ni kuwa kuacha makusudi kutekeleza amri ya Allah katika wakati wake uliowekwa ni jambo baya sana hata kama utatekeleza amri hiyo wakati mwingine. Ikumbukwe kuwa anachokiangalia Allah (s.w) si utekelezaji wa vitendo tu, bali huangalia na kumlipa mja kutokana na utii na unyenyekevu katika kufanya kitendo alicho kiamrisha.

### Kulipia Ramadhani

Mtu anapodaiwa siku alizo kula katika mchana wa mwezi wa Ramadhani,au siku ambazo swaumu yake ilibatilika, si lazima azilipe mara tu baada ya Ramadhani, japo ni bora mtu kumaliza deni lake haraka. Tunafahamishwa katika Hadith kuwa Bibi 'Aysha (r.a) alikuwa akilipia Ramadhani katika mwezi wa Shaaban:

*Aysha (r.a) ameeleza: "Nilikuwa na madeni ya swaumu ya Ramadhani. Sikuweza kulipa kadha ila katika mwezi wa Shaaban.*
*(Bukhari na Muslim).*

Hali kadhalika si lazima mtu kulipa mfululizo siku zote anazodaiwa, bali anaweza kuzilipa kidogo kidogo kutokana na Hadith ifuatayo:

*Ibn Umar (r.a) ameeleza kwamba Mtume (s.a.w) amesema juu ya kulipa Ramadhani: (Mtu) akitaka na afarikishe; na akitaka na afululize. (Daru Qutni).*

Kama mtu amechelewa kulipa siku anazodaiwa mpaka Ramadhani nyingine ikaingia, basi kwanza ataifunga hiyo Ramadhani iliyomuingilia. Baadaye ndipo alipe hiyo deni yake wala halipi fidia; iwe kuchelewa huko ni kwa udhuru ama si kwa udhuru. Lakini ni vizuri zaidi kulipa siku anazodaiwa kabla ya kuingia Ramadhani nyingine.

### Sunnah zinazoambatana na funga ya Ramadhani

Katika Mwezi wa Ramadhani kuna mambo kadhaa aliyoyafanya Mtume (s.a.w) na kutusisitiza nasi tuyafanye. Matendo haya ya Sunnah ambayo hurutubisha funga zetu na kutupelekea kufikia lengo la funga kwa ufanisi zaidi ni pamoja na:

#### (i) Kula na kuchelewesha Daku

Daku ni chakula kinacholiwa usiku wa manane kwa ajili ya kujiandaa kufunga siku inayofuatia. Kula daku ni sunnah iliyokokotezwa kama tunavyojifunza katika Hadith ifuatayo:

*Anas (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: ... Na kuleni na kunyweni mpaka ubainike kwenu weupe wa alfajir katika weusi wa usiku .. (2:187)*

### (ii) Kufuturu Mapema

Wakati wa kufuturu ni mara tu linapokuchwa jua kama tunavyofahamishwa katika Hadith:

*Umar (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: Usiku unapoingia na mchana ukitoweka, na jua likitua, mtu aliyefunga atafungua.(Bukhari na Muslim).*

Ni sunnah iliyokokotezwa kufanya haraka kufuturu mara tu linapokuchwa jua na kabla ya kuswali swala ya Magharibi kama tunavyojifunza katika Hadith zifuatazo:

*Sahl (r.a) amesimulia kwamba Mtume wa Allah amesema: Watu wataendelea kunawiri (kufanikiwa) pindi watakuwa wanaharakisha kufuturu. (Bukhari na Muslim).*

*Abu Hurairah (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: Allah (s.w) amesema: Mpendwa zaidi kwangu kati ya waja wangu ni yule ambaye mwepesi kuliko wote katika kufuturu. (Tirmidh).*

Pia ni Sunnah kufuturu kwa Tende au kwa maji kwani tunajifunza katika Hadith kuwa Mtume (s.a.w) alifanya hivyo na akatuagizia tufanye hivyo:

*Anas (r.a) ameeleza kuwa mtume (s.a.w) alikuwa akifungua kwa Tende mbivu kabla ya kuswali (Magharibi), kama hizi hazikuwepo alifungua kwa Tende kavu, na kama hizi hazikuwepo alikunywa mafunda machache ya maji. (Tirmidh na Abu Daud).*

*Salman bin Amir (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: "Mmoja wenu atakapokuwa anafuturu, na afuturu kwa Tende kwa sababu ni baraka, kama hakupata Tende, na afuturu kwa maji, kwa sababu yametakasika (ni twahara). (Ibn Majah).*

Vile vile ni sunnah wakati wa kufuturu kusoma dua ifuatayo:

اَللّٰهُمَّ لَكَ صُمْتُ وَعَلَى رِزْقِكَ اَفْطَرْتُ۔

***(Allahumma laka swumtu wa'alaariz-qika aftwar-tu)***

*"Ewe Mola! Nimefunga kwa ajili yako, na kwa riziki yako ninafuturu". (Abu Daud).*

Ni sunnah vile vile mtu kuzidisha dua anapokuwa katika swaumu kwani Mtume (s.a.w) amesema:

*"Watu watatu dua yao hairejeshwi - aliyefunga mpaka afungue. Imamu muadilifu na mtu aliyedhulumiwa." (Tirmidh).*

**(iii) Kuzidisha Ukarimu**

Pamoja na kuwa siku zote tumekokotezwa kuwakirimu na kuwasaidia wenzetu wenye shida mbalimbali, katika mwezi wa Ramadhani tunatakiwa tuzidishe. Mtume (s.a.w) alikuwa karimu zaidi katika mwezi wa Ramadhani, kuliko alivyokuwa katika miezi mingine kama tunavyojifunza katika Hadith ifuatayo:

*Amesimulia Ibn Abbas (r.a) kuwa Mtume (s.a.w) alikuwa ni mkarimu sana kuliko watu wote na alikuwa akizidisha ukarimu wake katika mwezi wa Ramadhani wakati ambao Jibril (a.s) alikuwa akimjia. Jibril (a.s) alikuwa akikutana naye kila usiku wa Ramadhani mpaka mwisho wa mwezi. Mtume (s.a.w) alikuwa akisoma Qur-an mbele ya Jibril, na Jibril alipokutana naye alikuwa mwema (mkarimu) zaidi kuliko upepo wa kusi (wa mvua) (Bukhari).*

Kufuturisha aliyefunga kumeahidiwa malipo makubwa kama tunavyojifunza katika hadith ifuatayo:

*Zaidi bin Khalid(r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: Atakayemfuturisha mtu aliyefunga, au atakayempa askari wa Allah zana za vita, kwake kuna malipo sawa na malipo ya mwenye kufunga au ya mpiganaji (bila wao kupunguziwa). (Baihaqi).*

**(iv) Kuzidisha kusoma Qur'an**

Kusoma Qur'an kumesisitizwa nyakati zote kwani Qur'an ndio mwongozo pekee wa maisha wanaotakiwa Waumini wa kweli waufuate hatua kwa hatua katika kila kipengele cha maisha yao ya kila siku. Lakini, katika mwezi wa Ramadhani, ambamo Qur-an imeanza kushuka, tumesisitizwa kuzidisha kusoma Qur'an katika swala na nje ya swala angalau tuumalize msahafu mzima katika mwezi huu. katika Hadith tumejifunza kuwa, Mtume (s.a.w) alikuwa akisoma Qur-an mbele ya Jibril kwa mwezi mzima.Kuhusu kushuka Qur-an katika mwezi wa Ramadhani tunafahamishwa katika aya ifuatayo:

شَهۡرُ رَمَضَانَ ٱلَّذِيٓ أُنزِلَ فِيهِ ٱلۡقُرۡءَانُ هُدٗى لِّلنَّاسِ وَبَيِّنَٰتٖ مِّنَ ٱلۡهُدَىٰ وَٱلۡفُرۡقَانِۚ . . . ١٨٥

*"Ni mwezi wa Ramadhani ambamo imeteremshwa Qur-an ili iwe uongozi kwa watu na hoja zilizo wazi za uongozi na upambanuzi .. (2:185).*

Ili Qur'an iwe mwongozo na kipambanuzi cha haki na batili, hatuna budi kuisoma kwa mazingatio na kwa hiyo ni muhimu kujua tafsiri ya yale tuyasomayo. Tukumbuke kuwa kusoma Qur'an bila ya mazingatio ni kama kuiangukia kwa uziwi na upofu, sifa ambayo waumini wa kweli wanatakiwa wajiepushe nayo. Kwani Allah (s.w) anatufahamisha kuwa miongoni mwa waja wake watakaofuzu ni pamoja:

وَٱلَّذِينَ إِذَا ذُكِّرُواْ بِـَٔايَٰتِ رَبِّهِمۡ لَمۡ يَخِرُّواْ عَلَيۡهَا صُمّٗا وَعُمۡيَانٗا ٧٣

*"Na wale ambao wanapokumbushwa aya za Mola wao hawaziangukii kwa uziwi na upofu" (25:73).*

### (v) Kusimamisha Swala ya Usiku ya Tarawehe

Swala ya Tarawehe ambayo tumeshajifunza habari zake, ni miongoni mwa Sunnah zilizokokotezwa katika mwezi wa Ramadhani.

### (vi) Kuutafuta usiku wa Lailatul-Qadr

Lailatul-Qadr au Usiku Wenye Cheo na Baraka ni usiku mmoja katika mwezi wa Ramadhani. Ni katika usiku huu Qur'an tukufu ilianza kushushwa kwa Mtume (s.a.w) kwa mara ya kwanza alipokuwa katika pango la mlima Hiraa (Jabal Hiraa). Aya za kwanza kumshukia Mtume (s.a.w) ni aya tano za mwanzo wa suratul-Alaq, sura ya 96 katika msahafu. Kuhusu kushuka Qur'an katika usiku huu tunafahamishwa katika Qur'an yenyewe:

إِنَّآ أَنزَلۡنَٰهُ فِي لَيۡلَةٖ مُّبَٰرَكَةٍۚ إِنَّا كُنَّا مُنذِرِينَ ٣

*"Kwa yakini Tumeteremsha (Qur-an) katika usiku uliobarikiwa. Bila shaka Sisi ni Waonyaji." (44:3).*

إِنَّآ أَنزَلْنَٰهُ فِى لَيْلَةِ ٱلْقَدْرِ ﴿١﴾

*"Hakika tumeiteremsha (Qur-an) katika Lailatul-Qadr (Usiku Wenye heshima kubwa)" (97:1).*

## Umuhimu wa usiku wa Lailatul Qadr

Umuhimu wa Usiku wa Lailatul Qadr umebainishwa wazi katika Qur-an kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

فِيهَا يُفْرَقُ كُلُّ أَمْرٍ حَكِيمٍ ﴿٤﴾ أَمْرًا مِّنْ عِندِنَآ ۚ إِنَّا كُنَّا مُرْسِلِينَ

*Katika (usiku) huu hubainishwa kila jambo la hikima. Ndiyo hukumu itokayo kwetu; kwa hakika sisi ni waletao (Mitume ili wawaongoe watu). (44:4-5).*

Katika Suratul-Qadr tunasoma

إِنَّآ أَنزَلْنَٰهُ فِى لَيْلَةِ ٱلْقَدْرِ ﴿١﴾ وَمَآ أَدْرَىٰكَ مَا لَيْلَةُ ٱلْقَدْرِ ﴿٢﴾ لَيْلَةُ ٱلْقَدْرِ
خَيْرٌ مِّنْ أَلْفِ شَهْرٍ ﴿٣﴾ تَنَزَّلُ ٱلْمَلَٰٓئِكَةُ وَٱلرُّوحُ فِيهَا بِإِذْنِ رَبِّهِم مِّن
كُلِّ أَمْرٍ ﴿٤﴾ سَلَٰمٌ هِىَ حَتَّىٰ مَطْلَعِ ٱلْفَجْرِ ﴿٥﴾

*"Hakika tumeiteremsha (Qur-an) katika Lailatul-Qadr (Usiku wenye heshima kubwa). Na ni jambo gani litakalo kujulisha ni nini huo usiku wa Lailatul-Qadr? Huo usiku (wa Lailatul-Qadr) ni bora kuliko miezi elfu. Huteremka Malaika na Roho (Jibril) katika usiku huo kwa idhini ya Mola wao kwa kila jambo. Ni amani usiku huo mpaka mapambazuko ya alfajir." (97:1-5).*

Tunajifunza katika aya hizi kuwa Allah (s.w) ameutukuza Usiku mmoja katika mwezi wa Ramadhani ili iwe kumbukumbu kwa Waumini wa umati huu wa Mtume Muhammad (s.a.w), ya kuletewa mwongozo pekee wa maisha yao kutoka kwa Mola wao. Mwongozo ambao huwa ni ponyo na rehma kwa Waumini na ambao hauwazidishii makafiri ila khasara:

وَنُنَزِّلُ مِنَ ٱلْقُرْءَانِ مَا هُوَ شِفَآءٌ وَرَحْمَةٌ لِّلْمُؤْمِنِينَ ۙ وَلَا يَزِيدُ

ٱلظَّٰلِمِينَ إِلَّا خَسَارًا ﴿٨٢﴾

*Na tumeteremsha katika Qur-an (hayo mafundisho yake) ambayo ni ponyo (poza la nyoyo) na rehema kwa wanaoamini. Wala hayawazidishii (mafundisho haya) madhalimu ila khasara" (17:82).*

Tunafahamishwa katika aya zilizomo katika Surat Qadr kuwa Allah (s.w) ameutukuza usiku huu zaidi ya miezi elfu moja au miaka 83 na miezi 4. Ina maana kuwa muumini akifanya amali njema katika usiku huu, thamani yake katika malipo na katika uwezo wa kumfikisha mja kwenye lengo la maisha yake itakuwa ni kubwa zaidi ya thamani ya amali hiyo iliyofanywa kwa miezi elfu moja. Umuhimu wa lailatul-Qadr pia unabainika katika Hadith ifuatayo:

*Amesimulia Abu Hurairah (r.a) kuwa Mtume (s.a.w) amesema: "Mwenye kufunga mwezi wa Ramadhani akiwa na Imani na akiwa na tegemeo la kupata malipo kutoka kwa Allah (s.w), basi dhambi zake zote zilizopita zitasamehewa. Na mwenye kusimama kwa swala katika usiku wa Qadr akiwa na imani na mategemeo ya kupata malipo kutoka kwa Allah, basi dhambi zake zote zilizotangulia zitasamehewa." (Bukhari).*

Ili kupata malipo na baraka ya usiku huu wa Lailatul-Qadr, Mtume (s.a.w) ametuhimiza sana kuupania huo usiku kwa kuzidisha ibada za usiku kwa kuswali, kusoma Qur-an, kumkumbuka Allah (s.w) kwa wingi na kuomba maghfira.

*Aysha (r.a) ameeleza: Niliuliza: "Ewe Mtume wa Allah! Nifahamishe niseme nini nitakapoudiriki usiku uliobarikiwa?" Akasema (Mtume s.a.w) sema; "Ee, Allah! Wewe ni Msamehevu Unayependa kusamehe, Basi (Nakuomba) Unisamehe". (Ahmad, Ibn Majah, Tirmidh).*

Usiku wa Lailatul-Qadr ni usiku uliofichwa na Allah (s.w). Yaani haijulikani siku maalum ya mwezi wa Ramadhani ambamo usiku huu hutokea. Kwa jitihada zetu tunaona hekima ya kufichwa usiku huu ni ili Waislamu wasiwe wavivu wa kufanya ibada katika mausiku yote ya mwezi wa Ramadhani na badala yake wakautegea usiku huo mmoja tu. Hata hivyo, kutokana na Hadith sahihi tunajifunza kuwa usiku huu hutegemewa zaidi kutokea katika kumi la mwisho la mwezi wa Ramadhani. Mtume (s.a.w) aliutafuta usiku huo katika kumi la mwisho kama tunavyojifunza katika Hadith ifuatayo:

*Abu Sayed al-Khudr(r.a) ameeleza kuwa Mtume (s.a.w) alikaa itiqaf katika siku kumi za kwanza za Ramadhani. Kisha akakaa tena itiqaf katika kumi la katikati la Ramadhani. Kisha aliinua kichwa chake akasema: "Hakika nilikaa Itiqaf katika siku kumi za mwanzo, niliutafuta usiku huu (wa Qadr). Kisha nilijiwa na kufahamishwa kuwa usiku huu hupatikana katika siku kumi za mwisho. Yule atakayekaa Itiqaf na mimi, basi na akae katika kumi la mwisho, kwa sababu nilionyeshwa kutokea kwake katika siku hizo lakini nilifanywa kusahau (siku gani hasa), japo niliuona mimi mwenyewe nikiwa (kwenye ndoto) nikiwa ninasujudu kwenye maji na matope. Basi utafuteni usiku huu katika siku kumi za mwisho na hasa mausiku ya witr ..." (Bukhari na Muslim).*

Hadith hii inatufahamisha kuwa mtume (s.a.w) alibainishiwa usiku huo kuwa katika kumi la mwisho la Ramadhani na akakokoteza watu wakae Itiqaf katika kumi hilo.Pia kutokana na Hadith hii mausiku yenye mategemeo zaidi katika hili kumi la mwisho ni zile za witr - usiku wa **21, 23, 25, 27, na 29.** Katika Hadith iliyosimuliwa na Zirri bin Hubaish (r.a) na kupokelewa na Muslim, usiku wa **27** umetiliwa mkazo zaidi. Lakini hasa alichosisitiza Mtume (s.a.w) sio kutegemea usiku mmoja tu kama vile usiku wa **27**, bali kujizatiti kwa kuzidisha ibada za usiku kwa kuswali, kusoma Qur-an, kumkumbuka Allah kwa wingi, kuomba maghfira na dua mbali mbali kwa mausiku yote ya kumi la mwisho la Ramadhani.Hivi ndivyo alivyofanya Mtume (s.a.w) kama tunavyojifunza katika Hadith zifuatazo:

*Aysha (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah alikuwa akijizatiti sana kufanya ibada katika mausiku ya kumi ya mwisho, kuliko ilivyokuwa kawaida yake katika wakati mwingine. (Muslim).*

*Aysha (r.a) ameeleza kuwa wakati usiku wa kumi la mwisho ulipoingia, Mtume (s.a.w) alikuwa akijifunga kibwebwe akikesha katika Ibada na akiamsha familia yake kwa swala. (Bukhari na Muslim).*

### Kukaa Itiqaf

Kukaa Itiqaf katika kumi la mwisho la Ramadhani ni sunna iliyokokotezwa. Ki-lugha "*Itqaf*" ina maana ya kukaa mahali. katika sheria ya Kiislamu "Itiqaf" ni kukaa msikitini kwa ajili tu ya kumkumbuka na kumtukuza Allah (s.w) na kufanya ibada maalum kama vile kuswali, kusoma Qur-an na kufanya amali yoyote njema ambayo inaruhusiwa kufanyika msikitini nje ya shughuli za kawaida za kutafuta rizki. Kwa hiyo mahali pa kukalia "Itiqaf" ni msikitini kama ilivyotajwa katika Qur-an:

...وَلَا تُبَٰشِرُوهُنَّ وَأَنتُمْ عَٰكِفُونَ فِى ٱلْمَسَٰجِدِ ۗ

*"... Wala msichanganyike nao, na hali mmekaa Itiqaf misikitini ...." (2:187).*

Misikiti inayokaliwa Itiqaf iwe ni ile inayoswaliwa jamaa na Ijumaa ili pasiwe na haja ya kutoka kwa swala za jamaa au kwa swala ya Ijumaa. Wanawake wanaruhusiwa kufanyia Itiqaf zao majumbani mwao katika sehemu zao za kusalia lakini baada ya kupata ruhusa kutoka kwa waume zao. Kwa muda wote mtu atapokuwa katika Itiqaf haruhusiwi kutokatoka msikitini ila kwa dharura kubwa sana kama vile kwenda haja au kwenda kula. Mtu akiwa katika Itiqaf hulazimika kujitenga na shughuli zote za kutafuta maslahi ya maisha na shughuli zote za kijamii kama vile kutembelea wagonjwa, kuhudhuria mazishi, na kadhalika. Mtu anapokuwa katika Itiqaf haruhusiwi kuchanganyika na mkewe.

...وَلَا تُبَٰشِرُوهُنَّ وَأَنتُمْ عَٰكِفُونَ فِى ٱلْمَسَٰجِدِ ۗ

*" ... Na wala msichanganyike nao na hali mnakaa Itiqaf msikitini. (2:187).*

Kwa ujumla katika muda huu wa kukaa Itiqaf, Mu'takif (Mwenye kukaa Itiqaf) anatakiwa ajihusishe tu na ibada maalum kama vile kuswali, kusoma Qur-an, kuleta tasbihi, tahmid, tahalili, takbir, istighfar na maombi mbali mbali.

Mu'takif anaruhusiwa kuja na matandiko yake msikitini na kuyaweka mahali pa uficho ambapo hayatawakarahisha watu wakati wa swala ya jamaa. Katika miezi mingine isiyokuwa Ramadhani mtu anaweza kukaa itiqaf kwa muda wowote ule, siku moja au masaa machache. Ni vyema mtu anapokuwa hana shughuli muhimu, anuie kukaa Itiqaf msikitini badala ya kujiingiza kwenye shughuli zisizo muhimu au shughuli za upuuzi zenye kumuingiza katika dhambi na kumpotezea muda ambao ni rasilimali pekee ya maisha yake. Katika mwezi wa Ramadhani Itiqaf imekokotezwa sana katika kumi la mwisho ili kumuwezesha Muumini kuudiriki usiku wa Lailatul-Qadr - akiwa katika hali ya kumkumbuka Allah (s.w). Mtume (s.a.w) alikuwa akikaa Itiqaf katika kumi hili la mwisho kama tunavyojifunza katika hadith zifuatazo:

*Amesimulia Abdullah bin Umar (r.a) kuwa Mtume (s.a.w) alikuwa akikaa Itiqaf katika siku kumi za mwisho za mwezi wa Ramadhani. (Bukhari na*

*Muslim).*

*Aysha (r.a.) amesimulia kuwa Mtume wa Allah alikuwa akikaa Itiqaf katika siku kumi za mwisho za Ramadhani mpaka alipotawafu (Allah alipo mchukua).Kisha wakeze waliendelea kukaa Itiqaf baada yake. (Bukhari na Muslim).*

## Zakatul-Fitri

Zakatul-Fitri ni zakat inayomlazimu kila Muislamu mwanamume na mwanamke,mdogo na mkubwa, ambayo hutolewa baada ya funga ya Ramadhani kabla ya kuswali swala ya Iddil-Fitri. Watoto, wanawake, wazee, na wengine wasio na uwezo wa kulipa zakatul-fitr watalipiwa na mawalii wao. Kwa mfano mume atamtolea mkewe na watoto ambao hawajaweza kujitegemea; pia atawatolea wazazi wake kama hawana uwezo wa kujilipia; vile vile baba atalazimika kuwalipia Zakatul-fitr wale wote wengine ambao ni Waislamu walio chini ya uangalizi wake. Mtoto mchanga aliyezaliwa dakika chache kabla ya kuandama mwezi wa Shawwal atatolewa Zakatul-Fitri.

## Umuhimu wa Zakatul Fitri

Zakatul Fitri ni faradhi iliyoambatanishwa na faradhi ya funga ya Ramadhani. Mtume (s.a.w) ameamrisha Zakatul-Fitri kutolewa na kila Muislamu mwanamume na kila Muislamu mwanamke na amebainisha wazi kuwa Swaumu ya mja haipokelewi endapo hajajitolea Zakatul Fitri na kuwatolea wote wale walio chini ya uangalizi wake. Msisitizo wa utoaji Zakatul-Fitr tunaupata katika Hadith ifuatayo:

*Ibn Umar (r.a) amesema kuwa Mtume wa Allah ameamrisha ulipaji wa Zakatul-fitr baada ya Ramadhan kwa kila Muislamu muungwana na mtumwa, mume na mke, (Mkubwa na mdogo) kwa (kila mtu) kutoa sai moja ya tende zilizokaushwa au sai moja ya shairi (Barley).(Bukhari na Muslim).*

## Nisaab ya Zakatul-Fitri

Zakatul Fitri inamlazimu yeyote yule mwenye kupata chakula cha kumtosha yeye mwenyewe na wale walio chini ya uangalizi wake kwa siku ya Idd na Usiku wake na akawa na ziada. Ziada hiyo ataitoa zakatul fitri kwa viwango vinavyostahiki.

## Kiwango cha Zakatul-Fitri

Kwa mujibu wa hadithi ya Ibn Umar (r.a) kiwango cha Zakatul-Fitri

kwa kila kichwa ni **Sa'i** moja ya chakula kinacholiwa kwa wingi katika sehemu husika. Kwa mfano chakula kinachopendelewa sana na watu wa mikoa ya pwani ya Tanzania ni **mchele** na kile kinachopendelewa sana na mikoa ya bara ni mahindi, uwele na mtama.

**Sa'i** iliyotumika wakati wa Mtume (s.a.w) imelinganishwa na pishi inayotumika katika mazingira ya Tanzania. **Pishi** moja ya vyakula hivyo vilivyotajwa ni sawa na kilo mbili na nusu (2.5kg). Pia inajuzu kuthaminisha pishi ya chakula husika na fedha taslimu. Kihalisia ni vizuri zaidi kutoa fedha taslimu ili kumuwezesha huyo anayepewa zakatul-fitri aweze kununua chakula husika pamoja na viungo mbali mbali vitakavyo kifanya chakula hicho kiwe kizuri na cha kuvutia kwa ajili ya kusherehekea Idd.

### Muda unaofaa kutolewa Zakatul-Fitri

Muda wa kutoa Zakatul fitri umebainishwa katika Hadith ifuatayo:

*Ibn Umar (r.a) ameeleza kuwa Mtume (s.a.w) aliwaamuru watu kuwa walipe zakatul fitri kabla ya swala (ya Iddil-Fitri) (Muslim).*

Kulipa Zakatul Fitri mapema kabla ya kuswali Idd au mapema zaidi ya hapo, kutawawezesha maskini na mafakiri kufurahia Idd pamoja na Waislamu wengine. Ikitokea sababu ya msingi, kama vile kusahau, mtu akachelewa kutoa Zakatul-fitri mpaka Idd ikaswaliwa, hana budi kuitoa baada ya swala. Lakini jambo la kuzingatia ni kwamba, amri ya kutoa Zakatul-fitri kabla ya swala imetolewa na Mtume (s.a.w), hivyo, mtu akiivunja amri hii makusudi au kwa uzembe ajue kuwa kutoa kwake huko hakutamnufaisha chochote.

### Watu wanaostahiki kupewa Zakatul-Fitri

Zakatul-Fitri si malipo ya maimamu wa Tarawehe kama wengi wanavyoichukulia bali ni chakula cha maskini na wale wote wasiojiweza kujipatia chakula pamoja na wale walio chini ya uangalizi wao kwa siku ya Idd na usiku wake ili nao wajisikie na wafurahie Idd pamoja na Waislamu wenzao wenye uwezo. Kama ilivyo katika Zakatul-Mal, akipewa Zakatul-Fitri asiyestahiki itakuwa ni kudhulumu haki ya wale wanaostahiki na mtoaji na mpokeaji wa zakatul-fitri hiyo watakuwa ni madhalimu.

Ili kuhakikisha kuwa katika jamii au katika mtaa wa Waislamu kila anayestahiki kupewa zakatul fitri amepata na kuzuia uwezekano wa mtu mmoja kulundikiwa zakatul-fitri kiasi kikubwa sana, na

mwingine kukosa au kupata kiasi kidogo sana kisichotosheleza mahitaji yake ya siku ya Iddi, ni vyema Waislamu wa mtaa mmoja au wa sehemu moja waikusanye Zakatul-Fitri kwa pamoja, na kisha waigawanye kwa wote wanaostahiki katika mtaa au sehemu hiyo wakizingatia mahitajio yao kulingana na majukumu ya kifamilia waliyo nayo.

### Iddil -Fitri

Iddil-Fitri ni siku kuu ya Kiislamu ya kusherehekea kumalizika kwa Mfungo wa Ramadhani. Mwezi wa Ramadhani ambao ndani yake imefaradhishwa funga ambayo imeambatanishwa na matendo mbali mbali ya sunnah, umekusudiwa uwe mwezi wa mafunzo na mazoezi ya kumfanya mja awe mchaji Mungu katika kiwango kinachostahiki kwa kipindi chote cha mwaka mzima. Iddil-Fitri ndicho kilele cha mafunzo haya ambapo Waislamu wanafurahia na kumshukuru Allah (s.w) kwa kumaliza salama mafunzo haya muhimu na wakati huo huo humuomba Allah (s.w) ayafanye mafunzo hayo yawe yenye kuwafikisha kwenye lengo lililokusudiwa. Hivyo, moja kwa moja inadhihiri kuwa Iddil-Fitri haisherehekewi kwa mavazi mazuri na kwa vyakula na vinywaji vizuri tu, bali kilele cha sherehe hii kinafikiwa kwa kuswali swala ya Iddil-Fitri na kumtukuza na kumuhimidi Allah (s.w) sana kwa Takbira.

### Swala ya Iddil-Fitri

Swala ya Idd mbili - Iddil-Fitri na Iddil-Hajj (kilele cha ibada ya Hija) ni sunnah zilizokokotezwa. Swala ya Idd inaswaliwa kwa rakaa mbili na kufuatiwa na Khutuba mbili kama zile zinazosomwa kabla ya swala ya Ijumaa. Swala ya idd ina Takbira 12,takbira 7 hutolewa katika rakaa ya kwanza kabla ya kusoma suratul-Faatiha na takbira 5 huletwa katika rakaa ya pili. vile vile kabla ya kusoma suratul-Faatiha.Mahali pa kuswalia Idd ni bora pawe uwanjani ili Waislamu wakusanyike pamoja kutoka sehemu mbali mbali za mji. Mtume (s.a.w) alikuwa akifanya hivyo. Ni sunnah kula chochote kabla ya kuswali Iddil-Fitri kama tunavyofahamishwa katika Hadith zifuatazo:

*Anas (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah hakwenda kuswali Iddil- Fitri mpaka alipokula Tende katika idadi ya witri. (Bukhari).*

*Buraydah (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah alikuwa hatoki kwa swala ya Iddil-Fitri mpaka awe amekula (Kitu) na hakuwa anakula katika siku ya kuchinja (Iddil-Hajj) mpaka aswali (Dirimi).*

Ni sunnah kuleta takbira mara kwa mara kuanzia pale mwezi wa Shawwal unapoandama mpaka baada ya swala ya Iddil-fitri. Takbira

yenyewe ni:

اللهُ أَكْبَرُ ،اللهُ أَكْبَرُ ،اللهُ أَكْبَرُ

لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللهُ اللهُ أَكْبَرُ اللهُ أَكْبَرُ ،وَ لِلَّهِ الْحَمْدُ

اللهُ أَكْبَرُ كَبِيرًا ،وَالْحَمْدُ لِلَّهِ كَثِيرًا ،وَسُبْحَانَ اللهِ بُكْرَةً وَأَصِيلاً

لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللهُ وَلاَ نَعْبُدُ إِلاَّ إِيَّاهُ مُخْلِصِيْنَ لَهُ الدِّيْنَ وَلَوْ كَرِهَ الْكَافِرُوْنَ

لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللهُ وَحْدَهُ ، صَدَقَ وَعْدَهُ ، وَنَصَرَ عَبْدَهُ ، وَأَعَزَّ جُنْدَهُ ، وَهَزَمَ الأَحْزَابَ وَحْدَهُ

لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللهُ ،اللهُ أَكْبَرُ اللهُ أَكْبَرُ ،وَ لِلَّهِ الْحَمْدُ

*Allahu Akbar, Allahu Akbar, Allahu Akbar*
*Laailaha illa Llahu Allahu Akbar*
*Allahu Akbar walillahil-hamdu*

*Allahu Akbaru kabiira walhamdulillaahi kathiyraa, wasubhaanallahi bukratan wa-aswiylaa.*

*Laailaahaillallahu walaa na'abudu illa iyyaahu mukhliswiyna lahudiyna walaukarihal-kaafiruun.*

*Laaillaha illallahu wahdahu, waswadaqa wa'adahu, wanaswara a'bdahu, wa-a'a-zza jundahu, wahazamal ahzaba wahda.*

*Laailaahaillallah Allahu Akbar, Allahu Akbar walillahil-Hamdu.*

***Allahumma swalli'alaa sayyidinaa Muhammad, wa'alaa aali sayyidnaa Muhammad, waa'laa asw-habi sayyidnaa Muhammad, wa'alaa answaari sayyidnaaaMuhammad,wa'ala azuwaji sayyidinaa Muhammad,wa'alaa dhurriyyati sayyidnaa Muhammad, wasalimutasliyman kathiyraa.***

**Tafsiri:**

*Allah Mkubwa, Allah Mkubwa, Allah Mkubwa hapana mola ila Allah Allah Mkubwa, Allah Mkubwa na shukurani zote ni za Allah. Allah Mkubwa aliyetukuka, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa wingi, na namtakasa asubuhi na jioni. Hapana Mola ila Allah. Wala hatumuabudu yeyote ila Yeye peke yake, tunamtakasa yeye na dini yake hata kama watachukia makafiri.Hapana mola ila Allah peke yake. Ameisadikisha (ameitimiza) ahadi yake na akamnusuru mja (Mtume s.a.w) wake, na akalitukuza jeshi lake, akalipa ushindi kundi lake. Hapana mola ila Allah. Allah Mkubwa. Ewe Allah, teremsha rehma zako juu ya Muhammad, na Maswahaba wake Muhammad, na waliomnusuru Muhammad, na Wakeze Muhammad, na kizazi chake Muhammad, na uwape salama na amani kwa wingi.*

## Yaliyo Sunnah kuyafanya Siku ya Idd

Ni sunnah siku ya Idd kukoga, kuvalia nguo nzuri kuliko zote ulizo nazo na kupaka uturi (manukato) kwa wanaume. Pia ni sunnah siku ya Idd kupika vyakula na kuandaa vinywaji vizuri zaidi kuliko siku za kawaida. kwa wafugaji na wale wenye wasaa, ni sunah kumchinja mnyama aliye bora zaidi kuliko wengine katika mifugo yake kama tunavyojifunza katika hadith ifuatayo:

*Amehadithia Hasan Asibbit (r.a) kuwa Mtume (s.a.w) ametuamrisha katika Idd mbili kuvaa vizuri zaidi kadri tuwezavyo, tupake uturi bora zaidi kuliko wote tulionao, na tuchinje wanyama wenye thamani zaidi kuliko wote tulionao. (Al-Hakim).*

Ni sunnah vile vile kuwakaribisha ndugu, marafiki, majirani, maskini, yatima na wengine wasiojiweza. Ni sunnah kuwatembelea ndugu, marafiki, majirani na wagonjwa. Ni sunnah vile vile kupeana zawadi.

## Tahadhari Katika Siku ya Idd

Waislamu hawana budi kukumbuka kuwa sherehe za Kiislamu,

makusudio yake na muundo wake, ni tofauti kabisa na sherehe zisizokuwa za Kiislamu. Sherehe za Kiislamu ni kilele cha kuonyesha shukrani zetu kwa Allah (s.w) kwa kutujaalia na kutuwezesha kutimiza wajibu wetu kwake katika kutekeleza ibada kubwa na nzito kama vile kufunga Ramadhani na kukamilisha Ibada ya Hija. Hivyo, sherehe hizi ni lazima ziambatane na kumshukuru, kumtukuza, kumtaja na kumkumbuka sana Allah (s.w).

Tunafahamu kuwa katika sherehe zisizokuwa za Kiislamu au zisizosherehekewa kwa mtazamo wa Kiislamu, ndio wakati ambao Allah (s.w) husahauliwa kuliko nyakati zote na ndio wakati ambao shetani hukumbukwa na kuadhimishwa kuliko nyakati zote. Kwa maana nyingine katika sherehe hizi watu hujiingiza kwa furaha na kicheko katika kumuasi Allah (s.w). Kutokana na uzoefu wetu sherehe hizi zimeambatana na ulevi, ngoma na mziki, mchanganyiko wa wanaume na wanawake, uzinifu na mengineyo kama haya.

Waislamu wanatahadharishwa sana wajiepushe na sherehe za namna hii, kwani zitawafanya wawe ni wenye kukufuru badala ya kuwa wenye kumshukuru Allah (s.w), kwa mafanikio hayo wanayo yasherehekea. Katika sherehe hizi za Idd Muislamu anatakiwa achukue hadhari kubwa katika kuchunga mipaka ya sherehe, kwani kumuasi Allah (s.w) katika siku ya Idd ni kosa kubwa sana mbele ya Allah kuliko kumuasi Allah (s.w) wakati mwingine, Mtume (s.a.w) amesema:

> *"Kumuasi Mwenyezi Mungu siku ya Idd ni sawa na kumuasi Mwenyezi Mungu siku ya Kiyama".*

## Funga za Kafara

Funga za kafara ni funga anazolazimika Muislamu kuzileta ili ziwe kitubio baada ya kutenda kosa fulani. Yaani funga hizi zimewekwa na sheria ya Kiislamu kama fidia au faini baada ya kutenda kosa na kutaka kutubia kwa Allah (s.w). Zifuatazo ni funga za kafara kama zilivyobanishwa katika Qur-an na Hadith:

(i) Kufunga miezi miwili mfululizo kwa Muislamu aliyemuua mtu kwa bahati mbaya na akakosa mali ya kulipia fidiya kama inavyobainishwa katika Qur-an:

وَمَا كَانَ لِمُؤْمِنٍ أَن يَقْتُلَ مُؤْمِنًا إِلَّا خَطَـًٔا ۚ وَمَن قَتَلَ مُؤْمِنًا خَطَـًٔا فَتَحْرِيرُ
رَقَبَةٍ مُّؤْمِنَةٍ وَدِيَةٌ مُّسَلَّمَةٌ إِلَىٰٓ أَهْلِهِۦٓ إِلَّآ أَن يَصَّدَّقُوا۟ ۚ فَإِن كَانَ مِن قَوْمٍ
عَدُوٍّ لَّكُمْ وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَتَحْرِيرُ رَقَبَةٍ مُّؤْمِنَةٍ ۖ وَإِن كَانَ مِن قَوْمٍۭ بَيْنَكُمْ
وَبَيْنَهُم مِّيثَـٰقٌ فَدِيَةٌ مُّسَلَّمَةٌ إِلَىٰٓ أَهْلِهِۦ وَتَحْرِيرُ رَقَبَةٍ مُّؤْمِنَةٍ ۖ فَمَن
لَّمْ يَجِدْ فَصِيَامُ شَهْرَيْنِ مُتَتَابِعَيْنِ تَوْبَةً مِّنَ ٱللَّهِ ۗ وَكَانَ ٱللَّهُ عَلِيمًا
حَكِيمًا ﴿٩٢﴾

*Na haiwi kwa Muislamu kumuua Muislamu (mwenziwe kusudi) ila kwa kukosea.Na mwenye kumuua Muislamu kwa kukosea basi ampe uungwana mtumwa aliye Muislamu, na pia atoe fidiya (Malipo) kuwapa warithi wake. Isipokuwa waache wenyewe kwa kufanya kuwa ni sadaqat (yao). Na aliyeuawa akiwa ni jamaa wa maadui zenu, hali yeye ni Muislam, basi ampe uungwana mtumwa aliye Muislamu (basi, hapana wa kupewa fidiya). Na kama (aliyeuawa) ni moja wa watu ambao kuna ahadi baina yenu na baina yao; basi warithi wake wapewe malipo na pia apewe uungwana mtumwa aliye Muislamu. Na asiyepata basi afunge miezi miwili mfululizo. Ndio kitubio kitokacho kwa Mwenyezi Mungu.Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi Mwenye Hekima. (4:92).*

Kufunga miezi miwili mfululizo kwa mtu atakayemsusa mkewe kwa kumfananisha na mama yake kwa kutamka: "Wewe kwangu mimi nakuona kama mgongo wa mama yangu." Maneno haya yalitamkwa na Sahaba wa Mtume (s.a.w) - Aus Ibn Samit (r.a), walipogombana na mkewe. Maneno haya kwa jamii ya Waarabu wakati ule wa Mtume (s.a.w) yalikuwa mabaya sana na yalikuwa ni ya kumdhalilisha mwanamke. Hivyo baada ya kufanyika kitendo hiki, mkewe huyu Sahaba alikwenda kwa Mtume (s.a.w) kushitakia; lakini Mtume (s.a.w) hakuweza kumpatia ufumbuzi wa tatizo lake. Mama huyu alizidi kusononeka sana huku akitarajia nusra ya Allah (s.w).Ni katika hali hii ya kusononeka huyu mama Allah (s.w) alishusha kwa Mtume wake aya zifuatazo:

*Mwenyezi Mungu amekwisha sikia usemi wa mwanamke yule anayejadiliana nawe sababu ya mumewe, na anashtaki mbele ya*

قَدْ سَمِعَ ٱللَّهُ قَوْلَ ٱلَّتِى تُجَـٰدِلُكَ فِى زَوْجِهَا وَتَشْتَكِىٓ إِلَى ٱللَّهِ وَٱللَّهُ
يَسْمَعُ تَحَاوُرَكُمَآ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ سَمِيعٌۢ بَصِيرٌ ﴿١﴾ ٱلَّذِينَ يُظَـٰهِرُونَ مِنكُم مِّن
نِّسَآئِهِم مَّا هُنَّ أُمَّهَـٰتِهِمْ ۖ إِنْ أُمَّهَـٰتُهُمْ إِلَّا ٱلَّـٰٓـِٔى وَلَدْنَهُمْ ۚ وَإِنَّهُمْ لَيَقُولُونَ
مُنكَرًا مِّنَ ٱلْقَوْلِ وَزُورًا ۚ وَإِنَّ ٱللَّهَ لَعَفُوٌّ غَفُورٌ ﴿٢﴾

*Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu; anayasikia majibizano yenu; hakika Mwenyezi Mungu ni mwenye kusikia mwenye kuona. Wale miongoni mwenu wawaitao wake zao mama zao,(kwa hivyo wakajiepusha nao wasiwaingilie wala wasiwape ruhusa kuolewa na mwanaume wengine), hao si mama zao. Hawakuwa mama zao ila wale waliowazaa.Wanasema neno baya na la uwongo.Na Mwenyezi Mungu ni mwenye msamaha, mwenye maghfira.(58:1-2).*

Baada ya kosa la huyu Sahaba kubainishwa katika aya hizi, aya zifuatazo zinatoa kitubio au adhabu ya kosa hili:

وَٱلَّذِينَ يُظَـٰهِرُونَ مِن نِّسَآئِهِمْ ثُمَّ يَعُودُونَ لِمَا قَالُوا۟ فَتَحْرِيرُ رَقَبَةٍ مِّن
قَبْلِ أَن يَتَمَآسَّا ۚ ذَٰلِكُمْ تُوعَظُونَ بِهِۦ ۚ وَٱللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرٌ ﴿٣﴾ فَمَن
لَّمْ يَجِدْ فَصِيَامُ شَهْرَيْنِ مُتَتَابِعَيْنِ مِن قَبْلِ أَن يَتَمَآسَّا ۖ فَمَن لَّمْ يَسْتَطِعْ
فَإِطْعَامُ سِتِّينَ مِسْكِينًا ۚ ذَٰلِكَ لِتُؤْمِنُوا۟ بِٱللَّهِ وَرَسُولِهِۦ ۚ وَتِلْكَ حُدُودُ
ٱللَّهِ ۗ وَلِلْكَـٰفِرِينَ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٤﴾

*Na wale wawaitao wake zao mama zao kisha wakarudia katika yale waliyoyasema (wakataka kuwarejea wake zao waendelee kuishi kama kawaida), basi wampe mtumwa huru kabla ya kugusana.Mnapewa maonyo kwa haya. Na Mwenyezi Mungu anajua (yote) mnayoyatenda. Na asiye pata (mtumwa) basi afunge saumu ya miezi miwili mfululizo kabla ya kugusana; na asiyeweza basi awalishe maskini sitini.*

*(Mmeambiwa haya ili mumuamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na hiyo ni mipaka ya Mwenyezi Mungu,na kwa makafiri iko adhabu iumizayo. (58:3-4).*

(iii) Kufunga siku tatu mfululizo kama kafara ya kuvunja kiapo kama tunavyoamrishwa katika aya ifuatayo:

لَا يُؤَاخِذُكُمُ ٱللَّهُ بِٱللَّغْوِ فِيٓ أَيْمَٰنِكُمْ وَلَٰكِن يُؤَاخِذُكُم
بِمَا عَقَّدتُّمُ ٱلْأَيْمَٰنَ ۖ فَكَفَّٰرَتُهُۥٓ إِطْعَامُ عَشَرَةِ مَسَٰكِينَ مِنْ
أَوْسَطِ مَا تُطْعِمُونَ أَهْلِيكُمْ أَوْ كِسْوَتُهُمْ أَوْ تَحْرِيرُ رَقَبَةٍ ۖ فَمَن لَّمْ
يَجِدْ فَصِيَامُ ثَلَٰثَةِ أَيَّامٍ ۚ ذَٰلِكَ كَفَّٰرَةُ أَيْمَٰنِكُمْ إِذَا حَلَفْتُمْ ۚ
وَٱحْفَظُوٓا۟ أَيْمَٰنَكُمْ ۚ كَذَٰلِكَ يُبَيِّنُ ٱللَّهُ لَكُمْ ءَايَٰتِهِۦ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ

*"Mwenyezi Mungu hatakuteseni kwa viapo vyenu vya upuuzi, lakini atakukamateni kwa viapo mlivyo viapa kwa nia mlioifunga bara bara. Basi kafara yake ni kuwalisha maskini kumi kwa chakula cha katikati mnacho walisha watu wa majumbani mwenu, au kuwavisha, au kumpa uungwana mtumwa. Lakini asiyeweza kupata hayo, basi afunge siku tatu. Hii ndiyo kafara ya viapo vyenu mnapoapa. Na vilindeni viapo vyenu (msiape kisha msitimize). Namna hivi Mwenyezi Mungu anakubainisheni aya zake ili mpate kushukuru" (5:89).*

(iv)Kufunga miezi miwili mfululizo kama kitubio cha kufanya tendo la ndoa kati ya mume na mkewe makusudi katika mchana wa mwezi wa Ramadhani.

(v)Mtu aliyehirimia Hijja au Umra haruhusiwi kuwinda na endapo atavunja amri hii ya kutowinda kitubio au kafara yake ni kufunga kama inavyobainishwa katika aya ifuatayo

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ لَا تَقْتُلُواْ ٱلصَّيْدَ وَأَنتُمْ حُرُمٌۚ وَمَن قَتَلَهُۥ مِنكُم
مُّتَعَمِّدًا فَجَزَآءٌ مِّثْلُ مَا قَتَلَ مِنَ ٱلنَّعَمِ يَحْكُمُ بِهِۦ ذَوَا عَدْلٍ مِّنكُمْ هَدْيًۢا
بَٰلِغَ ٱلْكَعْبَةِ أَوْ كَفَّٰرَةٌ طَعَامُ مَسَٰكِينَ أَوْ عَدْلُ ذَٰلِكَ صِيَامًا لِّيَذُوقَ وَبَالَ
أَمْرِهِۦۗ ... ﴿٩٥﴾

*"Enyi mliomini! Msiue mawindo na hali (ya kuwa) mumo katika Hija au Umra. Na miongoni mwenu atakayemuua kwa kusudi, basi malipo yake yatakuwa kwa (kuchinja) kilicho sawa na alichokiua,katika wanyama wanaofugwa,kama watakavyohukumu waadilifu wawili miongoni mwenu mnyama huyo apelekwe iliko Ka'aba, au badala ya hayo ni kufunga, ili aonje ubaya wa jambo lake hili ... (5:95).*

Muda wa kufunga utategemeana na thamani ya mnyama ambaye angalimchinja katika hesabu ya vibaba vya chakula.

(vi)Kama mwenye kuhiji au kufanya Umra atavunja miiko ya Ihram au iwapo atashindwa kutekeleza baadhi ya matendo ya Hijja, atalazimika kufunga kama inavyobainishwa katika aya ifuatayo:

وَأَتِمُّواْ ٱلْحَجَّ وَٱلْعُمْرَةَ لِلَّهِۚ فَإِنْ أُحْصِرْتُمْ فَمَا ٱسْتَيْسَرَ مِنَ ٱلْهَدْيِۖ
وَلَا تَحْلِقُواْ رُءُوسَكُمْ حَتَّىٰ يَبْلُغَ ٱلْهَدْيُ مَحِلَّهُۥۚ فَمَن كَانَ مِنكُم
مَّرِيضًا أَوْ بِهِۦٓ أَذًى مِّن رَّأْسِهِۦ فَفِدْيَةٌ مِّن صِيَامٍ أَوْ صَدَقَةٍ أَوْ نُسُكٍۚ

*Na timizeni Hija na Umra kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Na kama mkizuiwa, basi (chinjeni) wanyama walio wepesi kupatikana (nao ni mbuzi). Wala msinyoe vichwa vyenu mpaka wanyama hao wafike machinjioni mwao. Na atakayekuwa mgonjwa katika nyinyi au ana vya kumuudhi kichwani mwake (akafanya yaliyokatazwa kama vile kunyoa), basi atoe fidia kwa kufunga au kutoa sadaqat au kuchinja wanyama ..... (2:196).*

## Funga za Sunnah

Funga za Sunnah tutakazoziorodhesha hapa ni zile alizozitekeleza Mtume (s.a.w) na kuzikokoteza. Umuhimu wa kutekeleza funga za Sunnah ni sawa na umuhimu wa kutekeleza Swala za Sunnah na Ibada nyinginezo alizoziagiza na kuzitekeleza Mtume (s.a.w) mbali na zile Ibada za faradh. Tunawajibika kutekeleza hizi Ibada za Sunnah kwa sababu zifuatazo:

(1) Tunawajibika kumtii Mtume kwa kufuata yale aliyotuagiza na kuacha yale aliyotukataza na tunawajibika pia kumfanya kiigizo chetu.

(2) Ibada za Sunnah zinakamilisha zile Ibada za faradh zilizotekelezwa kwa upungufu kutokana na udhaifu wa kibinaadamu. Hivyo zinamuwezesha Muumini kufikia kwa uhakika lengo la kila ibada maalum -Shahada, Swala, Zakat, Swaumu, n.k.

Ni Karaha Kufunga Mwezi Mzima isipokuwa katika Ramadhani tu .

Mtume (s.a.w), mbali na Mwezi wa Ramadhani, hakuonekana kufunga mwezi mzima mfululizo; bali katika mwezi wa Shaabani alionekana akifunga siku nyingi zaidi kuliko katika miezi mingine yote kwa kuwa ndio wa kujiandaa kuupokea mwezi mtukufu wa Ramadhani. Pia Mtume (s.a.w) hakuonekana kuacha kufunga kabisa katika mwezi wowote ule kama tunavyojifunza katika Hadith ifuatayo:

*Aysha (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah alikuwa akifunga (katika mwezi wa Shaabani) mfululizo mpaka tuseme hatafungua tena na aliacha kufunga mfululizo mpaka tuseme hatafunga tena; na sikumuona Mtume wa Allah akifunga mwezi mzima ila mwezi wa Ramadhani na sikumuona akifunga katika mwezi mwingine zaidi kuliko alivyokuwa akifunga katika mwezi wa Shaabani" (Muslim).*

### (i) Kufunga siku tatu katika mwezi

Mtume (s.a.w) ametukataza kufunga mfululizo na badala yake tufunge siku tatu kwa mwezi kwani kufanya hivyo mtu hupata ujira wa kufunga mwezi mmoja (jema moja hulipwa mara 10) kama inavyobainishwa katika Hadith ifuatayo:

*Abdullah bin Amr bin al-Aas(r.a) amehadithia kuwa Mtume wa Allah alifahamishwa kuwa (Al-Aas) alikuwa akisimama katika swala usiku kucha na alikuwa anafunga kila siku katika maisha yake, ndipo Mtume wa Allah (s.a.w) akasema: "Ni wewe uliyesema haya?" Nikamjibu: Ee Mjumbe wa Allah ni mimi niliyesema hayo. Ndipo Mtume (s.a.w) akasema: "Huna uwezo wa kutosha kufanya hivyo. Funga na kufungua, lala na usimame kwa swala (usiku), na funga siku tatu katika mwezi: kwani*

*kila jema huzidishwa mara kumi, na huku ni kama kufunga maisha yote." Nikasema (Al-Aas): Mjumbe wa Allah, nina uwezo wa kufanya zaidi ya hivi. Ndipo (Mtume) akasema: Funga siku moja na ufungue siku mbili zinazofuata.Nikasema: Mjumbe wa Allah nina uwezo wa kufanya zaidi ya hivyo. Mtume (s.a.w) akasema: Funga siku moja na ufungue siku inayofuata. Hiyo inajulikana kama funga ya Daud (a.s) na hiyo ni funga bora kuliko zote. Nikasema: Nina uwezo wa kufanya zaidi ya hivi. Hapa Mtume (s.a.w) akasema: "Hakuna nyingine iliyo bora kuliko hii." Abdullah bin Amr (r.a) anasema: "Ningali kubali zile siku tatu (za kufunga katika mwezi) kama alivyonishauri Mtume wa Allah (s.a.w), zingalikuwa na thamani kwangu zaidi kuliko familia yangu na mali yangu." (Muslim).*

Kutokana na Hadith hii, kufunga siku tatu katika kila mwezi pamoja na funga ya Ramadhani kunatosha kumpa mja mazoezi ya kumbakisha katika lengo la maisha yake na pia kumbakisha katika afya au siha ya kumuwezesha kutekeleza vizuri majukumu yake kwa jamii. Hata mtu mwenye uwezo wa kiafya kwa kiasi ambacho swaumu haiathiri majukumu yake kwa wengine, bado mtu haruhusiwi kufunga mfululizo. Mwisho wa wingi wa ufungaji ni ule wa funga ya Daud (a.s) kama ilivyobainishwa katika hadith hii. Hizi siku tatu katika mwezi si lazima zifungwe mfululizo na hapana siku maalum kama tunavyojifunza katika Hadith ifuatayo:

*Muazat bint Adyyah (r.a) ameeleza kuwa alimuuliza Aysha (r.a): "Je, Mtume (s.a.w) alikuwa na tabia ya kufunga siku tatu katika kila mwezi?" Ndio, alijibu (Aysha). Nilimuuliza: "Ni siku gani za mwezi alizokuwa anafunga?" Akasema: "Hakuwa anajali ni siku gani ya mwezi afunge." (Muslim).*

Hata hivyo, kuzifunga mfululizo ni bora kwani Mtume (s.a.w) alikuwa akifanya hivyo kama tunavyojifunza katika Hadith zifuatazo:

*"Abdullah bin Mas'ud (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah alikuwa akifunga siku tatu za mwanzo za kila mwezi ...." (Tirmidh, Nisai, Abu Daud).*

*Aysha (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah aliwahi kufunga Jumamosi, Jumapili na Jumatatu katika mwezi mmoja na Jumanne, Jumatano na Alhamisi katika mwezi uliofuatia. (Tirmidh).*

Katika kufunga hizi siku tatu katika mwezi ni Sunnah kuzifunga siku za mbalamwezi kali - mwezi 13, 14, na 15 kama tunavyojifunza

katika Hadith ifuatayo:

*Abu Dharr(r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema; "Ee Abu Dharr! Ukifunga siku tatu katika mwezi funga mwezi 13, 14, na 15". (Tirmidh, Nisai).*

### (ii) Funga za Jumatatu na Alhamisi

Ni Sunnah kufunga siku ya Jumatatu na Alhamisi kama tunavyojifunza katika Hadith zifuatazo:

*Abu Hurairah(r.a) ameeleza kuwa Mtume (s.a.w) alikuwa akifunga siku ya Jumatatu na Alhamisi. Akaulizwa:"Ee Mtume wa Allah! Unafunga siku ya Jumatatu na Alhamisi? Akajibu: "Siku ya Jumatatu na Alhamisi Allah (s.w) humsamehe kila Muislamu ila wawili waliosusiana, Anasema Allah (s.w): "Waache mpaka wapatane" (Ahmad, Ibn Majah).*

*Abu Hurairah (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: "Amali zinawasilishwa siku ya Jumatatu na Alhamisi: Kwa hiyo ninapenda amali zangu ziwasilishwe wakati nimefunga". (Tirmidh).*

*Abu Qatadah(r.a) ameeleza kuwa Mtume (s.a.w) aliulizwa juu ya funga ya Jumatatu: Mtume alijibu: "Nilizaliwa siku hiyo na nilianza kushushiwa wahay (Qur-an) siku hiyo." (Muslim).*

Hadith hii inatufahamisha wazi kuwa Mtume (s.a.w) alisherehekea siku ya kuzaliwa kwa kufunga kila Jumatatu badala ya kusoma Maulid mara moja kwa mwaka.

### (iii) Kufunga siku sita katika Mwezi wa Shawwal

Kufunga siku sita katika mwezi wa Shawwal (Mfungo Mosi) ni sunnah iliyokokotezwa kama tunavyojifunza katika Hadith ifuatayo:

*Abu Ayyub Al-Answaar (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: "Atakayefunga Ramadhani kisha akafuatisha na funga ya siku sita katika mwezi wa Shawwal atakuwa kama amefunga mwaka mzima." (Muslim).*

Ilivyo ni kwamba, Allah (s.w), kwa huruma yake ameahidi kuwalipa waja wake wema mara kumi kwa kila jema watakalolifanya kwa ajili yake. Hivyo malipo ya kufunga siku 30 za mwezi wa Ramadhani ni sawa na malipo ya mwenye kufunga siku 300 (30 x 10) na malipo ya kufunga siku 6 za Shawwal ni sawa na mtu aliyefunga siku 60 (6 x 10). Mwaka mmoja una siku 360 (mwaka wa muandamo). Kwa hiyo utaona wazi kuwa mtu akifunga Ramadhani na kufuatisha siku sita za Shawwal

malipo yake mbele ya Allah (s.w) ni sawa na mtu aliyefunga mwaka mzima.

Je, hizi siku sita ni lazima zifungwe mfululizo kuanzia mwezi 2 Shawwal au mtu anaweza kufunga wakati wowote katika mwezi huu na bila kufululiza? Hili ni swali wanalojiuliza wengi. Wanavyuoni wametofautiana katika kujibu swali hili. Kwa mfano, Imamu Shafii, anaona kuwa ni vyema kufunga mfululizo kuanzia, mwezi wa pili Shawwal.

Kwa upande mwingine Imamu Abu Hanifa anaona ni vyema kutozifunga mfululizo na kuzifunga wakati wowote katika mwezi huu wa Shawwal ili watu wasije kuichukulia kuwa kufunga mfululizo ni lazima na bila ya kufanya hivyo ibada hiyo haikamiliki.

### (iv) Funga ya Arafa

Arafa ni siku ya mwezi 9 Dhul-Hajj siku ambayo mahujaji husimama katika uwanja wa Arafa. Ni sunnah kwa Waislamu wengine kufunga ili kujihusisha kiroho na kisimamo cha Arafa. Katika Hadith iliyosimuliwa na Abu Qatadah (r.a) Mtume (s.a.w) amesema:

> *"Funga katika siku ya Arafa hufuta dhambi (ndogo) za mwaka uliopita na mwaka ujao na funga ya Ashura inafuta dhambi za mwaka uliopita". (Muslim).*

Kwa Mahujaji ni vyema kutofunga katika siku ya Arafa. Mtume (s.a.w) hakufunga siku ya Arafa wakati alipohiji. Pia ni Sunnah kufunga katika kumi la mwanzo la mwezi wa Dhul-Hijjah (yaani kuanzia mwezi 1-9 Dhul-Hijjah. Tunajifunza hili katika Hadith ifuatayo:

> *Hafsah (r.a) ameeleza kuwa kuna mambo manne ambayo Mtume (s.a.w) hakuyaacha kuyafanya - Kufunga siku ya Ashura, kufunga siku 10 za Dhul-Hijjah, kufunga siku tatu kila mwezi na kuswali rakaa mbili ya swala ya Alfajir (Nisai).*

### (v) Funga ya Ashura

Siku ya Ashura ni siku ya mwezi 10 Muharram (mfungo nne) Mtume (s.a.w) kabla ya kufaradhishwa Ramadhani alianza kuwaamrisha Waislamu kufunga siku ya Ashura. Siku ya Ashura ndio siku ambayo Nabii Musa (a.s) na Banii Israil waliokolewa na Allah (s.w) kutokana na udhalimu wa Firaun na utawala wake kama tunavyojifunza katika Hadith ifuatayo:

*"Ibn Abbas (r.a.) ameeleza kuwa, Mtume (s.a.w.) alipofika Madina aliwakuta Mayahudi wamefunga siku ya Ashura. Ndipo Mtume (s.a.w.) akawauliza: "Ni siku gani hii ambayo mnafunga?" Walijibu: "Hii ni siku kubwa (siku kuu) ambayo Allah (s.w.) alimuokoa Musa (a.s.) na watu wake na kumzamisha Fir'aun na watu wake. Musa (a.s.) akawa anafunga katika siku hii kama njia ya kuonyesha shukrani zake kwa Allah (s.w.) na sisi tunafanya hivyo vile vile". Kisha Mtume wa Allah akasema: "sisi tuwakweli zaidi na tuko karibu zaidi na Musa (a.s.) kuliko nyinyi. Hivyo Mtume (s.a.w.) alifunga siku hiyo na akawaamrisha Waislamu wafunge". (Bukhari na Muslim)*

Umuhimu wa kufunga siku ya Ashura unabainika katika Hadith ifuatayo:

*"Abu Hurairah (r.a.) ameeleza kuwa Mtume wa Allah (s.a.w.) amesema: "Funga bora kuliko zote baada ya Ramadhani ni funga ya mwezi wa Allah - Muharram, na swala bora kuliko zote baada ya swala za faradhi ni swala ya usiku (Tahajjud)". (Muslim)*

**(vi) Funga katika mwezi wa Shaaban**

Katika Hadith tuliyoinukuu mwanzoni, tumejifunza kuwa Mtume (s.a.w) alikuwa akifunga kwa wingi katika mwezi wa Shaaban kuliko katika miezi mingine yote mbali na Ramadhan. Alipoulizwa kwa nini alipendelea kufunga sana katika mwezi huu, alijibu kuwa alikuwa akijiandaa kwa funga ya Ramadhani.

Pia tunajifunza katika hadith ifuatayo kuwa kufunga katikati ya mwezi wa Shaaban ni sunnah iliyokokotezwa:

*Imraan bin Husain(r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah (s.a.w) alimuuliza mtu mmoja:"Ulifunga funga yoyote katikati ya mwezi huu (Shaaban)?" Akajibu: Hapana". Ndipo Mtume wa Allah akamwambia: "Funga siku mbili (badala ya moja) baada ya kumaliza Ramadhani."*

## Nia katika Funga za Sunnah

Katika funga ya Ramadhani, kutokana na hadith iliyosimuliwa na Hafsah (r.a), funga haisihi endapo mtu hatatia nia ya kufunga usiku kabla ya Alfajir kuingia. Lakini katika funga za Sunnah mtu anaweza kunuia swaum mchana kabla ya kuingia adhuhuri, endapo atakuwa hajala chochote tangu alfajir, kama inavyobainika katika Hadithi ifuatayo:

*Aysha (r.a) ameeleza kuwa siku moja Mtume wa Allah (s.a.w) aliniuliza: "Aysha, una chochote (cha kula)?" Nikasema: "Mjumbe wa Allah, hatuna chochote". Ndipo akasema: "Nimefunga". (Muslim).*

## Uhuru wa kuvunja Funga ya Sunnah

Mtu aliyefunga sunnah ana uhuru kamili wa kufungua katikati endapo ataona ni vyema kwake kufanya hivyo. Tunajifunza hili katika Hadith zifuatazo:

*Aysha (r.a) ameeleza: Mtume wa Allah alikuja kwangu akasema: "Una chochote cha kula?" Nikajibu: "Hapana." Kisha akasema: "Basi, nitafunga". Kisha siku nyingine alitujia tukamwambia: Mtume wa Allah, tumeletewa zawadi ya Hais (aina ya chakula). Ndipo akasema: "Nionyeshe, nilikuwa nimefunga tangu alfajir, kisha alikula." (Muslim).*

*Ummi Hani (r.a) ameeleza kuwa katika siku ya kutekwa Makka Fatma (r.a) alikaa kushotoni mwa Mtume na Ummi Hani alikuwa kuliani kwake. Kisha Walidah (r.a) alileta kikombe cha maji, alichukua akanywa, kisha Ummi Hani naye alichukua na kunywa. Akasema: Ee Mtume wa Allah, nilifunga na sasa nimefungua. akamuuliza: Ulikuwa unalipa? Akajibu: 'Hapana' Akasema Mtume (s.w.): "Haidhuru iwapo ilikuwa ni funga ya sunnah. Mtu anayefunga funga ya sunnah ana uhuru kamili. Akipenda atafunga na akipenda ataacha." (Abu Daud, Tirmidh, Ahmad).*

## Aliyefunga Sunnah akikaribishwa aseme: "Nimefunga"

*Mtu aliyefunga akikaribishwa chakula aseme 'nimefunga' kama tunavyofahamishwa katika Hadith ifuatayo:*
*Abu Hurairah (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah (s.a.w) amesema:"Kama mmoja wenu atakaribishwa chakula akiwa amefunga sema: "Nimefunga":. (Muslim).*

Si vibaya mtu asiyefunga kula mbele ya yule aliyefunga, bali mfungaji hupata ujira kwa kule kuamua kwake kuendelea kufunga pamoja na kuwaona wengine wakila mbele yake. Tunajifunza katika Hadith zifuatazo:

*Ummi Umrah bin Ka'ab (r.a) amesimulia: Mtume (s.a.w) alimtembelea na akamuandalia chakula, Mtume akamwambia kula. Akasema: "Nimefunga." Ndipo Mtume (s.a.w) akasema: "Wakati kitu kinapoliwa mbele ya mtu aliyefunga, malaika wanamrehemu mpaka wamalize kula" (Ahmad).*

*Buraidah (r.a) amesimulia kuwa Bilal alikuja kwa Mtume (s.a.w) akamkuta anafungua kinywa. Mtume wa Allah akamkaribisha Bilal akamwambia: "Kifungua kinywa, Ee Bilal." Bilal akasema: Nimefunga. Ee! Mtume wa Allah.' Kisha Mtume wa Allah akasema: "Tunakula riziki yetu na riziki*

*ya Bilal ya hali ya juu. Riziki ya hali ya juu kuliko zote ni Pepo.Unafahamu Ee Bilal kwamba mifupa ya mtu aliyefunga inamtukuza Allah na Malaika wanamuombea msamaha kwa muda wote ambao watu wanakula karibu yake?" (Baihaqi).*

**Funga za Sunnah na utekelezaji wa majukumu**

Endapo kufunga sunnah kutamfanya mtu ashindwe kutekeleza majukumu yake kwa wengine katika jamii, ni vyema kutofunga. Katika Hadith tunafahamishwa kuwa wakeze Mtume (s.a.w) walikuwa aghlabu hawafungi mbali ya Ramadhani na Shaabani kwa kuhofia kushindwa kutekeleza wajibu wao kwa Mtume (s.a.w). Katika mwezi wa Shaaban Mtume (s.a.w) alikuwa akifunga sana kuliko miezi mingine:

*Aysha (r.a) ameeleza: Kama mmoja wetu aliacha siku katika Ramadhani (kwa udhuru wa sheria) katika maisha ya Mtume (s.a.w) hakuweza kuzilipa alipokuwa na Mtume wa Allah mpaka Shaaban inaingia." (Muslim).*

Hadith hii inasisitiza kuwa kwa kuchelea kutoweza kutekeleza wajibu wao kwa Mtume wa Allah, wakeze Mtume(s.a.w) hawakuthubutu kufunga walipokuwa na Mtume. Mwanamke haruhusiwi kufunga sunnah mpaka aridhiwe na mume wake.

## Siku Zilizoharamishwa Kufunga Sunnah

**(i) Siku kuu za Iddil-Fitri na Iddil-Hajj**

Imeharamishwa kufunga katika siku hizi kama tunavyojifunza katika Hadith ifuatayo:

*Abu Sayyid al-Khudri (r.a) ameeleza kwamba Mtume (s.a.w) amesema: Hakuna funga katika siku mbili - siku ya (Iddil) Fitr na siku ya (Idd ya) kuchinja." (Bukhari na Muslim).*

**(ii) Siku za Tashriq**

Siku za Tashriq ni mwezi 11 hadi 13 Dhul-Hijjah. Ni haram kufunga katika siku hizi kama tunavyojifunza katika Hadith ifuatayo:

*Ibn Al-Hazali(r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: "Siku za Tashriqu ni siku za kula na kunywa na kumkumbuka Allah (s.w) (kwa Takbira). (Muslim).*

**(iii) Siku ya Shaka**

Siku ya Shaka ni siku moja kabla ya Ramadhani. Yaani mwezi 30 Shaabani ambapo inawezekana ikawa ni siku ya kufunga. Mtume (s.a.w) amekataza kufunga sunnah katika siku hii ya mashaka ila kwa yule

mwenye ada ya kufunga. Kwa mfano mtu mwenye ada ya kufunga Jumatatu ameruhusiwa kufunga endapo siku hiyo itaangukia Jumatatu. Hadith ifuatayo inabainisha makatazo haya:

*Abu Hurairah (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: "Usifunge siku moja au mbili kabla ya Ramadhani ila kwa mtu yule mwenye ada ya kufunga funga fulani (k.m. funga ya Alhamisi), yeye anaruhusiwa kufunga" (Muslim).*

Inatakiwa siku moja au mbili kabla ya Ramadhani tusifunge ili tuweze kuukabili tukiwa na nguvu mpya na ili tutofautishe funga ya Ramadhani na funga za Sunnah.

**(iv) Siku ya Ijumaa**

Mtume (s.a.w) amekataza funga ya Sunnah katika siku ya Ijumaa tu, lakini kama mtu ana tabia ya kufunga sunnah, ikatokea siku ya Ijumaa ni miongoni mwa siku anazofunga, basi hapana ubaya. Tunajifunza haya katika Hadith zifuatazo:

*Abu Hurairah (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: "Na asifunge siku ya Ijumaa yeyote miongoni mwenu; ila tu akiwa ameanza kufunga kabla yake au ameendelea kufunga baada yake". (Muslim).*

*Abu Hurairah (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: "Usiuchopoe usiku kabla ya Ijumaa ukafanya usiku pekee kwa kusimama kwa swala na usiichague siku ya Ijumaa pekee kati ya siku za wiki kuwa ndio siku ya kufunga, ila kama mmoja wenu ana tabia ya kufunga sunnah na ikatokea siku ya Ijumaa imeangukia katika tarehe anayopaswa kufunga." (Muslim).*

## Lengo la Funga

Lengo la funga limebainishwa katika Qur-an pale ilipotolewa amri ya kufunga:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ كُتِبَ عَلَيْكُمُ ٱلصِّيَامُ كَمَا كُتِبَ

عَلَى ٱلَّذِينَ مِن قَبْلِكُمْ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ ﴿١٨٣﴾

*"Enyi mlioamini! Mmeamrishwa kufunga kama walivyoamrishwa waliokuwa kabla yenu ili mpate kumcha Mungu". (2:183)*

Hapa tunabainishwiwa kuwa lengo la kufunga ni kuwafanya Waumini kuwa wacha-Mungu. Neno ***“Taqwa”*** ambalo linatafsiriwa kuwa ni “***Uchamungu***” lina maana pana zaidi. ***“Taqwa”*** ni hali ya kuhofu ghadhabu za Mwenyezi Mungu (s.w) ambayo humfanya mja ajiepushe mbali na yale yote yanayomghadhibisha Mwenyezi Mungu (s.w) na ayaendee mbio kwa unyenyekevu na kwa jitihada kubwa yale yote aliyoamrisha Mwenyezi Mungu (s.w) na yale yote anayoyaridhia. Maana ya ‘Taqwa’ inabainishwa vyema na Hadith ifuatayo:

> *Siku moja Umar (r.a) alimuuliza Ubbay bin Ka’b (r.a) amueleweshe maana hasa ya Taqwa. Ubbay (r.a) alijibu: “Amir Muuminin, umewahi kupita njia ya kichaka chenye miba?” Umar (r.a) akajibu:“Naam, nimepita mara nyingi” Kisha Ubbay (r.a) akamuuliza ni hadhari gani uliyoichukua wakati ukipita huko? “Nilishikilia na kukusanya pamoja nguo zangu na kutembea kwa uangalifu katika kupita njia hiyo”, alisema Umar (r.a) ili sehemu yoyote ya nguo zangu isije shikwa na miba hiyo”. Kutokana na jibu hili, Ubbay (r.a) alisema: “Hii hasa ndio maana ya “**Taqwa**”.*

Kutokana na mfano huu mtu mwenye ***“Taqwa”*** au Muttaq ni yule mwenye shauku na jitihada kubwa kuepukana na kila aina ya mwiba (uovu) katika kila hatua na kila kipengele cha maisha yake yote na wakati huo huo huwa na shauku na jitihada kubwa ya kuyakimbilia mema katika kila hatua ya maisha yake ili kupata radhi za Mwenyezi Mungu (s.w). Muttaq ni mtu mwenye cheo na hadhi kubwa sana mbele ya Mwenyezi Mungu (s.w) kama tunavyofahamishwa katika Qur-an:

... إِنَّ أَكْرَمَكُمْ عِندَ ٱللَّهِ أَتْقَىٰكُمْ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ عَلِيمٌ خَبِيرٌ ﴿١٣﴾

> *“... Hakika aheshimiwaye sana miongoni mwenu mbele ya Mwenyezi Mungu ni yule aliye Muttaq (amchaye Mwenyezi Mungu zaidi) katika nyinyi. Kwa yakini Mwenyezi Mungu ni Mjuzi Mwenye khabari ya mambo yote. (49:13).*

Hiki ni cheo kikubwa sana ambacho hakina mfano wake katika vyeo vya hapa ulimwenguni. Cheo hiki hakipatikani kwa kuomba kura au kwa hongo, bali kinapatikana kwa kujizatiti kujiepusha na makatazo yote ya Mwenyezi Mungu (s.w) na kujitahidi kutenda mema na kutekeleza maamrisho yote ya Mwenyezi Mungu (s.w) kwa matarajio ya kupata Radhi ya Mwenyezi Mungu (s.w).

### Funga inavyomuandaa mtu kuwa mcha-Mungu.

Tumedhihirishiwa katika Qur-an kuwa lengo la kufaradhishwa kufunga ni kuwafanya waumini wawe wacha Mungu (Muttaq). Yaani kuwawezesha waumini kutekeleza maamrisho yote ya Allah (s.w) kama inavyostahiki kwa matarajio ya kupata radhi zake, na kuwawezesha waumini kuepukana kwa unyenyekevu na kwa moyo mkunjufu na yale yote yanayokwenda kinyume na radhi za Allah (s.w) kwa kuhofia ghadhabu zake. Sasa ni vipi funga ya Ramadhani na funga nyingine za Sunnah humfikisha mja kwenye lengo hili? Swali hili litajibiwa vyema kwa kuiangalia sura ya funga yenyewe. Funga humtayarisha muumini kufikia lengo lililokusudiwa kama ifuatavyo:

**(i) Funga humzidishia mja imani na uadilifu**

Funga ni ibada iliyofichikana. Ni siri ya aliyefunga na Allah (s.w) tu. Ibada nyingine kama kusimamisha swala, kutoa zaka na sadaka na kuhiji hubainika kwa wengine pindi mtu anapozitekeleza. Lakini ibada ya funga si rahisi kuonekana utekelezaji wake kwa wengine. Mtu anaweza akala, akanywa au akafanya kwa siri kitendo chochote kinachofunguza na bado akadai kuwa amefunga na akajikausha midomo yake kiasi cha kuufanya ulimwengu uamini kuwa amefungal Pamoja na hivyo, Muislamu huamua kufunga kwa kujizuilia na vyote vinavyofunguza ambavyo angalikuwa na uwezo wa kuvitumia kwa siri bila ya kuonekana na mtu yeyote. Na wakati mwingine hushikwa na kiu ya kumkausha koo na akawa na uwezo wa kupata maji baridi na kuyanywa na hata kuyatamani. Labda tungejiuliza; ni nguvu gani iliyomfanya mtu ajizuie na kula na kunywa tangu alfajiri mpaka magharibi wakati ana uwezo wa kula na kunywa bila hata ya kusimamiwa na yeyote? Tukijua kuwa huyu mfungaji hakufanya hivyo ili kupunguza uzito au hayuko katika mgomo wa kula, bila shaka atakuwa amefunga kwa ajili ya kutekeleza amri ya Allah (s.w) na kutaraji kupata radhi yake na kupata malipo makubwa aliyomuahidi. Ni usiri huu uliopo katika funga unayoifanya ibada hii iahidiwe malipo makubwa kuliko ibada nyingine kama tunavyofahamishwa katika hadithi ifuatayo:

> *"Abu Hurairah (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: "Kila amali njema anayoifanya mwanaadamu italipwa mara kumi mpaka mara mia saba". Kisha Allah (s.w) amesema: "Ila kwa Funga kwa sababu funga ni kwa ajili yangu na ni mimi mwenyewe ndiye nitakayeilipa. Anajizuia kutosheleza matashi yake ya kimwili na kuacha chakula chake kwa ajili yangu…" (Bukhari na Muslim).*

Ni dhahiri kwamba mja atakapotekeleza amri hii ya kufunga Ramadhani kwa unyenyekevu kwa kutaraji kupata radhi ya Allah (s.w)

na kuepukana na ghadhabu zake, itamzidishia mja imani juu ya Allah (s.w) na malipo ya Akhera kwa maana nyingine kufunga kwa ajili ya Allah humzoesha mja kuwa muadilifu katika utekelezaji wake wa kila siku. Kile kilichomfanya asizime njaa yake na chakula alichokuwa nacho ambacho angaliweza kula kwa siri bila ya kufahamika kwa yeyote, Kile kilichomfanya asikate kiu yake kwa maji baridi ambayo anayo chumbani mwake, na kile kilichomfanya ajizuie kufanya vitendo mbalimbali vinavyofuturisha ambavyo ana uwezo wa kuvifanya kwa siri asifahamike kwa mtu yeyote, ndicho kile kile kitakachomfanya mja huyu awe muadilifu katika kutekeleza wajibu wake katika maisha yake ya kila siku. Mja huyu atakumbuka daima kuwa Allah (s.w) ni mjuzi wa kila kitu na hapana siri inayofichikana kwake. Kwa hiyo katika kutekeleza wajibu wake hatahitajia kusimamiwa na mnyapara au polisi, bali atatenda wajibu wake ipasavyo hata akiwa peke yake porini au nyikani.

**(ii) Funga humzidishia mja nidhamu na utii kwa Allah (s.w)**

Ukiichunguza funga ilivyo, utadhihirikiwa kuwa, haikuamrishwa ili kuwa mateso kwa waja wa Allah (s.w), bali imekusudiwa iwe zoezi maalum la kuwafanya waja wawe wacha Mungu kwa kutii kwa unyenyekevu maamrisho yote ya Allah (s.w) na kuacha kwa unyenyekevu vile vile, makatazo au makemeo yote ya Allah (s.w).

**Kwanza**, zoezi hili linadhihirika pale mja anapoharamishiwa katika mchana wa Ramadhani kuanzia alfajiri mpaka magharibi kula, kunywa na vinginevyo alivyohalalishiwa kuvitumia katika maisha yake yote. Kwani tumeagizwa katika Qur-an:

يَـٰٓأَيُّهَا ٱلنَّاسُ كُلُوا۟ مِمَّا فِى ٱلْأَرْضِ حَلَـٰلًا طَيِّبًا وَلَا تَتَّبِعُوا۟ خُطُوَٰتِ
ٱلشَّيْطَـٰنِ ۚ إِنَّهُۥ لَكُمْ عَدُوٌّ مُّبِينٌ ﴿١٦٨﴾

*"Enyi watu! Kuleni vilivyo katika ardhi halali na vizuri, wala msifuate nyayo za shetani (mkala visivyo halali). Bila shaka yeye kwenu ni adui dhahiri". (2:168).*

يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ كُلُوا۟ مِن طَيِّبَـٰتِ مَا رَزَقْنَـٰكُمْ وَٱشْكُرُوا۟ لِلَّهِ إِن
كُنتُمْ إِيَّاهُ تَعْبُدُونَ ﴿١٧٢﴾

*"Enyi mlioamini! Kuleni vizuri tulivyokuruzukuni, na mumshukuru Mwenyezi Mungu, ikiwa mnamwabudu Yeye peke yake". (2:172).*

Tunajifunza kuwa katika aya hizi na aya nyingine za Qur-an Allah (s.w) ametubainishia vilivyo halali kwetu kuvila na ametupa ruhusa ya kuvitumia maridhawa alimuradi tusivile kwa fujo au tusifanye israfu (ubadhirifu). Lakini katika mwezi wa Ramadhani vitu hivi ameviharamisha mchana kutwa kuanzia alfajiri mpaka magharibi ili kuukuza na kuudumisha utii wetu kwake. Ni kwamba, mja atakayemtii Allah (s.w) akafunga kwa kujizuia na vilivyokuwa halali siku zote na vinavyoendelea kuwa halali baada ya magharibi kuingia na kabla ya alfajiri, kwa vyovyote vile baada ya Ramadhani, haitakuwa rahisi kwake kula vilivyoharamishwa kwake siku zote.

**Pili** zoezi hili la utii kwa Allah (s.w) pia linapatikana katika kujizuilia kusema na kutenda maovu wakati mtu amefunga. Kama tunavyorejea katika Hadithi:

> *"Abu Hurairah (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah (s.a.w) amesema: "Asiyeacha kusema uwongo na kufanya vitendo viovu, Allah (s.w) si muhitaji wa kuona anaacha chakula chake na kinywaji chake (i.e. Allah (s.w) hana haja na funga yake)". (Bukhari)*

Hivyo, mja anapofunga kwa ajili ya Allah (s.w) pamoja na kujizuilia kula na kunywa vilivyo halali kwake, anajitahidi mwisho wa kujitahidi kwake kujizuilia kusema na kufanya mambo maovu na machafu kwa kuchelea kukosa malipo ya funga yake na kuambulia kiu na njaa. Kwa hiyo, funga pamoja na kukuza utii wa mja katika kujiepusha na chumo la haramu au riziki haramu, humzoesha pia mja kujiepusha na mambo yote maovu na machafu.

**Tatu**, pia katika funga tunapata zoezi la kumtii Allah (s.w) kwa kule kutekeleza kwa ukamilifu masharti na nguzo za funga. Hatufungi Ramadhani mpaka uonekane mwezi au mwezi wa Shaaban utimie siku 30, na hatufungui Ramadhani mpaka mwezi wa Shawwal uandame au Ramadhani ikamilishe siku 30. Tunajizuilia kula, kunywa, kujimai na kufanya vyote vinavyofunga kwa wakati maalum, kuanzia alfajiri mpaka magharibi. Ili kuona kuwa kufunga si mateso bali ni mazoezi tu ya kukuza utii wetu kwa Allah (s.w), ni vyema turejee msisitizo wa Mtume (s.a.w) juu ya kula daku na kuichelewesha na juu ya kufuturu mapema mara tu linapotua jua. Tunapata msisitizo wa kuharakisha kufuturu katika Hadithi nyingi, ifuatayo ikiwa miongoni mwa hizo:

> *"Abu Hurairah (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah (s.w) amesema: Allah (s.w) amesema: "Walio bora kuliko wote mbele yangu miongoni mwa*

*waja wangu ni wale wanaoharakisha kufuturu". (Tirmidh).*

Msisitizo wa kula daku na kuichelewesha tunaupata katika Hadithi ifuatayo:

*"Anas (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah (s.w) amesema: "Kula daku kabla ya alfajiri kwa sababu daku ina baraka". (Bukhari na Muslim).*

Pia tunafahamishwa kuwa Mtume (s.a.w) aliwazoesha masahaba kuchelewesha daku kama tunavyojifunza katika Hadithi zifuatazo:

*Amesimulia Aysha (r.a): "Bilal alikuwa akitoa adhana usiku, kwa hiyo Mtume wa Allah (s.w) akasema: 'Endeleeni kula mpaka Ibn Um Makhtuum aadhini. Kwani haadhini mpaka alfajiri iwe imeshaingia". (Bukhari).*

*Anas (r.a) amesimulia: Zaid bin Thabit (r.a) amesema: "Tulikula daku pamoja na Mtume (s.a.w). Kisha akasimama kwa swala. "Nikauliza; Nikitambo gani kati ya (kumaliza kula) daku na adhana (ya alfajiri?" Alijibu: "Kitambo cha kutosha kusoma aya 50 za Qur-an". (Bukhari).*

Bila shaka katika Hadithi hizi tumepata msisitizo wa kuwahisha futari, kula daku na kuichelewesha. Hekima yake ni kufupisha muda wa kufunga na kuibakisha miili yetu na afya. Tunalolipata hapa kwenye kuwahi kufuturu na kula daku na kuichelewesha ni zoezi kubwa la utii kwa Allah (s.w). Hebu mfikirie mja huyu anayeitekeleza Sunnah hii ya Mtume (s.a.w) ya kuwahi kufuturu mara tu baada ya kuchwa jua. Bila shaka mja huyu atacha shughuli zake na mapema kidogo na kujitayarisha kwa swala ya magharibi, akiwa na tende au maji karibu naye ili mara tu jua linapotua afuturu pale pale. Je, huoni hali hii hukuza nidhamu ya mja na utii wake kwa Allah (s.w) na Mtume wake kama kengele ya kuingia darasani inavyokuza nidhamu na utii wa mwanafunzi kwa mwalimu wake wa somo au wa darasa? Tofauti tu iliyopo ni kwamba ambapo nidhamu na utii wa mwanafunzi unapatikana kwa kuogopa adhabu ya mwalimu wake wa darasa au somo, nidhamu na utii kwa mwenye kufunga hupatikana kwa kumuogopa Allah (s.w).

Hali kadhalika kula daku na kuichelewesha nako hukuza nidhamu na utii wa mfungaji kwa Allah (s.w). Hebu mfikirie mtu anayekatisha usingizi wake usiku wa manene au karibu na alfajiri ili ale daku jambo ambalo si la kawaida kabisa katika miezi mingine. Mfikirie vile vile yule anayekula daku katika saa za mwisho mwisho kabisa huku akiwa na saa mkononi akikazana kula chakula chake haraka kabla ya muadhini wa Alfajir. Bila shaka utaona kuwa kitendo hiki cha kuamka kula daku na kuichelewesha, kikifanywa kwa ajili ya kufuata Sunnah

ya Mtume (s.a.w) na hata kama mtu atakunywa angalau maji tu au kipande kimoja cha tende, kitakuza nidhamu na utii wa mfungaji kwa Allah na Mtume wake (s.a.w).

**Nne**, pia katika funga ya Ramadhani kuna Sunnah nyingi zilizoambatanishwa kama vile kusimama usiku katika swala ya Tarawehe, kuzidisha kusoma Qur-an, kukaa Itiqaf katika kumi la mwisho na kutafuta siku ya Lailatul Qadr kwa kuzidisha ibada za usiku ili kuzidisha au kukuza ucha-Mungu wa mfungaji. Ni maratajio ya kila mwenye kufunga Ramadhani kwa ajili ya Allah (s.w) na akajitahidi kutekeleza kwa ukamilifu masharti yote, nguzo zote na sunnah za funga pamoja na kutekeleza funga zilizoambatanishwa na mwezi wa Ramadhani, kuwa baada ya Ramadhani atakuwa na nidhamu na utii wa hali ya juu kwa Allah (s.w) na Mtume wake (s.a.w) katika kutekeleza maamrisho na hukumu zote za Allah (s.w) katika kuendesha maisha yake ya kila siku.

### (iii) Funga humzoesha mja kumiliki matashi ya Unyama wake

'Funga pia inatupa zoezi la kuumiliki unyama wetu. Tumeshaona kuwa japo mwanaadamu ana mwili kama wanyama na ana matashi ya kinyama kama vile kula, kunywa, kujamii, kupumzika, kulala na kadhalika, si mnyama bali ni mtu ambaye umbile lake ni mchanganyiko wa **mwili** ambao asili yake ni udongo na **roho** ambayo hutoka kwa Allah (s.w). Ambapo mwili humng'ang'aniza mwanaadamu kurudi chini katika ardhi ili kujipatia maslahi ya kinyama yatokayo ardhini. Roho humnyanyua mwanaadamu juu ili kukidhi mahitaji ya kiutu au mahitaji ya kimaadili yapatikanayo kutoka kwa Allah (s.w). Ilivyo ni kwamba, iwapo matashi ya kimwili yatamtawala mwanaadamu, basi mwanadamu hapa ulimwenguni ataishi kama mnyama au hali duni zaidi kuliko ile ya mnyama japo atakuwa analala ndani ya nyumba, analala kitandani na anakula vyakaula vizuri vilivyopikwa vizuri na kuandaliwa vizuri. Kwa upande mwingine iwapo maadili ya kiroho ndiyo yatakayomtawala mwanaadamu, basi mwanaadamu ataishi kama Khalifa wa Allah (s.w) hapa ulimwenguni na hadhi yake mbele ya Allah (s.w) itakuwa ya juu kuliko ile ya malaika. Ni vyema vile vile tufahamu kuwa mwanaadamu ana uhuru kamili wa kuamua ama kujishusha hadhi yake kuwa chini kuliko walio chini au kuipandisha hadhi yake kuwa juu kuliko ile ya malaika. Mwanaadamu atakapoamua kuyafanya matashi ya unyama wake kuwa ndio Mungu wake na kuyaabudu na kuyanyenyekea basi hadhi yake hapa duniani itakuwa chini kuliko ile ya wanayama. Rejea Qur-an:

أَرَءَيْتَ مَنِ ٱتَّخَذَ إِلَـٰهَهُۥ هَوَىٰهُ أَفَأَنتَ تَكُونُ عَلَيْهِ وَكِيلًا ﴿٤٣﴾ أَمْ

تَحْسَبُ أَنَّ أَكْثَرَهُمْ يَسْمَعُونَ أَوْ يَعْقِلُونَ إِنْ هُمْ إِلَّا كَالْأَنْعَامِ بَلْ هُمْ أَضَلُّ سَبِيلًا ﴿٤٤﴾

*"Je, umemuona yule aliyefanya matamanio yake kuwa mungu wake? Basi je utaweza kuwa mlinzi wake, au je, unafikiri ya kwamba wengi katika wao wanasikia au wanafahamu? Hawakuwa hao ila ni kama wanyama, bali wao wamepotea zaidi njia." (25:43-44)*

Na mwanaadamu atakapomfanya Allah (s.w) kuwa ndiye Mola wake, akamtii kwa unyenyekevu yeye pekee, basi hadhi yake itakuwa ni ile ya ukhalifa (ya mtawala wa ulimwengu kwa niaba ya Allah (s.w)) yenye daraja kuliko hadhi ya malaika. Rejea Qur-an (2:30-34)

Muumini anapofunga huyakandamiza matashi ya unyama wake kama vile kula, kunywa, kujamii na kadhalika kwa ajili tu ya kumtii Allah (s.w). Kitendo cha mja kuamua kwa hiari yake kuacha kula, na huku ana njaa, kuacha kunywa na huku ana kiu na kuacha kutumia vitu mbali mbali na huku anavihitajia, huudunisha unyama wake na kuuweka chini ya utawala wa maadili ya kiroho yanayotoka kwa Allah (s.w). Ni vyema tukumbuke kuwa katika sheria ya kawaida ya maumbile, kuwa kila mwili unapokuwa dhaifu ndivyo matashi na matamanio ya kimwili (kinyama) yanavyopungua au kuwa dhaifu. Kwa mfano mtu mwenye matamanio makubwa ya kujamii ameshauriwa afunge. Pia vijana wasiopata uwezo wa kuoa wameshauriwa wafunge ili wakate matamanio yao yatakayoweza kuwapelekea kuzini. Hebu turejee ushauri huu katika hadithi ifuatayo:

*"Amesimulia Alqama (r.a): "Nilipokuwa ninatembea pamoja na Abdullah (r.a) alisema: Tulikuwa pamoja na Mtume (s.a.w) akasema: "Yule mwenye uwezo wa kuoa na aoe kwa sababu itamsaidia kujizuilia kuangalia wanawake (kwa matamanio) na itamsaidia kuhifadhi tupu yake kutoiendea zinaa, na yule asiyemudu kuoa anashauriwa afunge kwani funga itapunguza nguvu". (Bukhari)*

Allah (s.w) ndiye aliyetuumba na matashi ya kimwili tuliyonayo. Hivyo ni yeye pekee anayefahamu ni namna gani tutayamiliki matashi yetu ili pamoja na kuyatosheleza tubakie na utu wetu. Basi ametuwekea funga kama njia ya kumiliki matashi ya unyama wetu.

Mja aliyefunga mwezi wa Ramadhani kwa ajili ya Allah na kwa

kuzingatia masharti na nguzo za funga, anatarajiwa awe na uwezo wa kukandamiza matashi ya unyama wake pale yanapompelekea kuchupa mipaka ya Allah (s.w). Muislamu mwenye kufunga Ramadhani vilivyo, hatarajiwi kabisa kutosheleza matashi yake kinyume na utaratibu aliouweka Allah (s.w).

**(iv) Funga humzoesha mja kuwahurumia wanaadamu wenzake**

Funga pia inatoa mafunzo ya huruma. Kwa fukara au masikini kushinda njaa na kula mara moja kwa siku si jambo kubwa wala ajabu sana. Lakini kwa tajiri ambaye anavyo vyakula vingi na vizuri vilivyomzunguka na ambaye ana wasaa wa kuvila, kushinda njaa na kiu ni ajabu kubwa na jambo zito kwake. Hivyo tajiri anayefunga kwa ajili ya Allah atapata wasaa wa kuona hali ya njaa wanayokuwanayo mafakiri, masikini. Mayatima, wasafiri walioharibikiwa kwa sababu ya kukosa uwezo wa kujipatia chakula. Mafunzo haya aliyoyapata katika funga yatampa msukumo wa kuwahurumia fukara, masikini, mayatima, wasafiri walioharibikiwa na wengine waliokumbwa na njaa na kuwalisha chakula kwa kutaraji malipo kutoka kwa Allah (s.w) tu.

Vile vile kuzidisha kutoa sadaqa katika mwezi wa Ramadhani na kuwafuturisha waliofunga ni miongoni mwa sunnah zilizokokotezwa. Kama tulivyojifunza katika hadithi ya Ibn Abbas(r.a), Mtume (s.a.w) alikuwa mpole na mkarimu sana katika mwezi wa Ramadhani kuliko kawaida yake katika miezi mingine. Hapakuwa na muombaji yeyote aliyekuja kwake akarudi mikono mitupu kutoka mlangoni kwake.

> Pia *Ibn Abbas (r.a) ameeleza kuwa mwezi wa Ramadhani ulipoingia alikuwa akiwaacha huru watumwa - mateka wa vita - na alikuwa akitoa sadaqa kwa kila muombaji (Baihaqi).*

Mfungaji tajiri akijitahidi kutekeleza Sunnah hizi katika mwezi mzima wa Ramadhani, atapata zoezi la kumwezesha kuwahurumia watu wengine na kuwalisha masikini kwa kadri ya uwezo wake katika miezi kumi na moja ya mwaka inayofuatia Ramadhani.

Halikadhalika utoaji wa Zakatul-fitri hutupa zoezi hilo hilo la kuwahurumia wengine, kwamba mtu akipata kiasi cha chakula kinachotosha kwa siku moja pamoja na wale walio chini ya uangalizi wake, anawajibika kutoa ziada iliyobakia kwa jirani yake ambaye hana kabisa. Zoezi hili ni muhimu sana kwani hatutakuwa waumini endapo tutashiba na ilihali majirani zetu wanalala njaa. Ibn Abbas (r.a) amesimulia:

*"Nimemsikia Mtume wa Allah akisema: "Si muumini yule ambaye anashiba na ili hali jirani yake pembeni analala njaa." (Baihaqi).*

Hata kufunga kwenyewe bila ya kuambatanisha na utoaji wa sadaqa na zakatul fitr, kunamlainisha tajiri na kuwa mpole kwa wengine na kuwa mnyenyekevu kwa Mola Karim. Ilivyo ni kwamba katika kawaida ya maisha mtu mnyonge na dhaifu daima hujidhalilisha mbele ya matajiri na wenye uwezo. Kwa upande mwingine matajiri na wenye uwezo hutakabari na hujiona bora zaidi kuliko wanyonge. Tajiri na mwenye uwezo anapofunga njaa na kiu humfanya awe mnyonge na dhaifu, na hujiona yeye bora chochote, bali aliye bora kuliko wote ni Allah (s.w) pekee. Kwa hiyo, tajiri mwenye nguvu na mwenye hadhi katika jamii, atakapofunga kwa ajili ya Allah (s.w) atapata zoezi la kumzuia na takaburi juu ya wanyonge na atapata zoezi la kuwahurumia wengine. Funga huwakumbusha matajiri, wenye wadhifa na wenye nguvu mawaidha ya aya ifuatayo:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلنَّاسُ إِنَّا خَلَقۡنَٰكُم مِّن ذَكَرٖ وَأُنثَىٰ وَجَعَلۡنَٰكُمۡ شُعُوبٗا وَقَبَآئِلَ
لِتَعَارَفُوٓاْۚ إِنَّ أَكۡرَمَكُمۡ عِندَ ٱللَّهِ أَتۡقَىٰكُمۡۚ إِنَّ ٱللَّهَ عَلِيمٌ خَبِيرٞ ١٣

*"Enyi watu! Kwa hakika tumekuumbeni (nyote) kwa (yule) mwanaume (mmoja) Adam na (yule yule) mwanamke (mmoja Hawwa). Na tumekufanyeni mataifa na makabila (mbali mbali) ili mjuane (tu basi). Hakika aheshimiwaye sana miongoni mwenu mbele ya Mwenyezi Mungu ni yule aliye Mcha Mungu zaidi katika nyinyi. Kwa yakini Mwenyezi Mungu ni Mjuzi mwenye habari za mambo yote. (49:13)*

### (v) Funga humpatia mfungaji siha

*Mtume (s.a.w) amesema: "Fungeni mtakuwa na afya". (Tabrani).*

Imethibitika katika utafiti wa madaktari kuwa kufunga ni matibabu ya baadhi ya maradhi na kwamba funga ni kinga ya baadhi ya maradhi.

**Kwanza**, mwili wa mwanaadamu unahitaji mapumziko baada ya kufanya kazi kwa muda mrefu. Baada ya mapumziko, mtu hupata nguvu mpya wakati anaporejea kazini na ufanyaji wake unakuwa na ufanisi zaidi. Hali kadhalika matumbo yetu yanahitaji mapumziko kidogo kwa mwaka kwa muda tunaofunga, ili yaweze kuifanya kazi yake kwa ufanisi

zaidi na kuupatia mwili afya inayostahiki Madaktari wengi katika sehemu mbali mbali huwashauri wagonjwa wa baadhi ya magonjwa ya kudumu kujiepusha na baadhi ya vyakula, kujizuia kulal kula ovyo, na kupunguza kula ili kujilinda na magonjwa yanayotokana na kula kula ovyo au kula lma kwa mara vyakula mchanganyiko.

**Pili**, imegunduliwa katika utafiti kuwa tumboni kuna aina Fulani ya dawa (acidities) ambazo hutokea kutokana na njaa na kiu, ambazo huua vijidudu vya magonjwa ya aina mbali mbali. Takwimu zinaonyesha kuwa magonjwa mengi yanayotokana na usagaji wa chakula, hayapatikani kwa wingi kwa watu wenye kawaida ya kufunga mwezi mmoja kila mwaka.

**Tatu**, binaadamu anapokula chakula mwili hutumia kiasi tu cha chakula kinachohitajika kwa wakati ule. Ziada yoyote ya chakula hubadilishwa kutoka hali yake ya kawaida na kuwa katika hali ambayo kitafaa kutunzwa na kuwekwa akiba kwa matumizi ya baadaye. Hali hii ya mwili ya kuweka akiba huendelea siku hadi siku. Lakini mwili wa binaadamu unakikomo cha uwezo wa kutunza chakula hiki cha akiba. Kama miaka kwa miaka akiba zitazidi kurundikana tu bila kutumiwa, akiba ya zamani huharibika na kuwa sumu kwa mwili.

Mfungaji wa Ramadhani hawezi kudhuriwa na akiba hizi za chakula mwilini mwake, kwani akiba zote zilizotunzwa mwilini kwa miezi kumi na moja hutumika katika mwezi mmoja wa Ramadhani. Hii ni kwa sababu katika masaa 12 hadi 14 ya kufunga, ambapo mfungaji hali wala hanywi, mahitaji ya mwili ya chakula hutoshelezwa na ile akiba. Tukumbuke kuwa aliyetuumba ni Allah (s.w) na ndiye aliyetuamrisha kufunga mwezi mmoja kwa mwaka katika masaa hayo ya kufunga. Hivyo kiasi hicho cha funga katika mwaka kinatosha kusafisha akiba ya chakula cha mwaka ambayo ikiendelea kubakia itadhuru miili yetu kwa njia moja au nyingine.

Umuhimu wa siha hauna budi kuzingatiwa ipasavyo. Ni kwamba kipando cha kuifikisha roho kwenye lengo lake ni mwili. Mwili ukiwa hauna afya nzuri, basi roho yenyewe haitaweza kuusimamisha ufalme wa Allah (s.w) hapa ulimwenguni. Ni katika msingi huu Mtume (s.a.w) amesema: "Waumini wote ni bora mbele ya Allah (s.w), lakini aliyebora ziadi miongoni mwenu ni yule mwenye siha nzuri".

Umma wa Waislamu katika mwezi wa Ramadhani huzidisha kufanya wema na kuamrisha wengine kufanya hivyo, pia hujitahidi

kuacha maovu na kukataza maovu, hujitahidi kusaidiana na kuhurumiana na kuufanya ulimwengu kuwa na furaha na amani zaidi. Mwenendo huu wa Waislamu kuamrisha mema na kukataza maovu, kuhurumiana na kupendana ndio mwenendo wanaotakiwa wawe nao Waislamu ili waweze kuwa Makhalifa wa Allah (s.w) hapa ulimwenguni.

### Kwa nini Lengo la Funga halifikiwi na Wafungaji Wengi?

Amri ya kufunga imeambatanishwa na lengo lake. Lengo la funga ni kuwafanya wafungaji wawe wacha-Mungu. Lakini maswali ya kujiuliza: Ni kweli watu wanafunga vile ipasavyo? Je, watu wengi hawaanzi kufunga kwa vunja jungu ambapo baadhi ya Waislamu wanaotarajia kufunga Ramadhani humuasi Mola wao tani yao siku ya mwezi 29 au 30 Shaabani? Je, baada ya kufuturu baadhi ya Wafungaji hawajiingizi kwenye laghwi - kucheza karata, bao, mabishano, uvutaji sigara, mazungumzo ya upuuzi, na kadhalika - mpaka utakapoingia wakati wa daku? Je, siku ya Iddil-Fitri baadhi ya waliofunga hawajiingizi katika kumuasi Mwenyezi Mungu (s.w) katika kiwango cha hali ya juu kwa kujihusisha na ulevi, uzinifu, kamari na ngoma za kila aina?

Ni wazi kuwa Waislamu wanaofanya matendo haya mara tu baada ya kufuturu au mara tu baada ya kumaliza mwezi wa Ramadhani hawakupata matunda yatokanayo na swaumu na hawakufikia lengo lililokusudiwa. Labda tujiulize tena: Inakuwaje kwa Muislamu aliyefunga kwa nia safi, akose matunda yatokanayo na funga na ashindwe kufikia lengo la funga linalotazamiwa? Hii inatokea kwa sababu Waislamu wengi wafungao wana mapungufu yafuatayo:

### (i) Lengo la Funga Halijulikani kwa Wengi

Lengo la kufunga kama lilivyobainishwa katika Qur-an ni kutufikisha katika ucha-Mungu katika maisha yetu yote. Uchaji Mungu hupatikana kwa kufuata kwa unyenyekevu maamrisho yote ya Mwenyezi Mungu (s.w) na kuacha kwa unyenyekevu vile vile makatazo yote ya Mwenyezi Mungu (s.w) kwa kutarajia kupata Radhi Yake na kuepukana na ghadhabu zake. Wengi wa wafungaji hawafahamu lengo la funga. Wengi wanadhania wakishinda na njaa na kiu ndio watakuwa wamemaliza kufunga kana kwamba Mwenyezi Mungu (s.w) ametoa amri hii ya kufunga ili afurahie kuona waja wake wanavyohangaika kwa njaa na kiu! Mwenyezi Mungu (s.w) ameepukana na udhaifu huo. Yeye Mwenyezi Mungu (s.w) hahitaji lolote kutoka kwa waja wake bali ni waja wanaohitajia msaada kutoka kwake kama tunavyojifunza katika Qur-an:

وَمَا خَلَقْتُ ٱلْجِنَّ وَٱلْإِنسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ ﴿٥٦﴾ مَآ أُرِيدُ مِنْهُم مِّن رِّزْقٍ وَمَآ
أُرِيدُ أَن يُطْعِمُونِ ﴿٥٧﴾ إِنَّ ٱللَّهَ هُوَ ٱلرَّزَّاقُ ذُو ٱلْقُوَّةِ ٱلْمَتِينُ ﴿٥٨﴾

*"Sikuwaumba Majini na Watu ila wapate kuniabudu. Sitaki kwao riziki wala sitaki wanilishe.Kwa yakini Mwenyezi Mungu ndiye Mtoaji wa riziki, Mwenye nguvu madhubuti". (51:56-58)*

Kwa hiyo Waumini wa kweli wanaofunga hawana budi kufahamu vyema kuwa swaumu si kujiingiza kwenye mateso au si mgomo wa kula na kunywa ili kumfurahisha Mwenyezi Mungu (s.w) bali ni neema ya Mwenyezi Mungu (s.w) aliyotuletea ili ituwezeshe kuishi maisha ya utu yatakayotuletea furaha na amani ya kweli hapa ulimwenguni.

Wafungaji wengine wamelielewa lengo la funga kuwa ni kuwapatia thawabu tu, kiasi kwamba anaposhinda na njaa na kiu kuridhika kuwa ameshapata thawabu bila ya kujali kuwa swaumu imemfikisha au haijamfikisha kwenye uchaji Mungu katika maisha yake ya kila siku. Hatuna budi kukumbuka kuwa thawabu au "ujira wa matendo mema" kutoka kwa Mwenyezi Mungu, ni siri ya Mwenyezi Mungu (s.w). Hatuna namna yoyote ya kujua kuwa kitendo tulicho kifanya kimetupatia thawabu au la.

Tunaloweza kuhakikisha ni matunda tunayotarajiwa kuyapata kutokana na amali njema tulizoamrishwa kuzitenda. Kwa mfano tutakuwa na tumaini kuwa tumepata thawabu kutokana na funga zetu endapo, funga zetu zitatufikisha kwenye lengo la kumcha Mwenyezi Mungu (s.w) katika kila kipengele cha maisha yetu ya kila siku. Lakini kama baada ya kufuturu usiku tutajihusisha tena na kumuasi Mwenyezi Mungu(s.w) au kama baada ya funga ya Ramadhani tutaendelea kufuata mwenendo wa maisha kinyume na ule anaoridhia Mwenyezi Mungu (s.w) na Mtume wake (s.a.w), tujue kuwa hatukupata chochote kutokana na funga zetu bali tumeambulia njaa na kiu.

### (ii) Kutofahamika mahusiano baina ya funga na lengo la maisha

Kutofahamika kwa maana halisi ya Ibada kwa Waislamu wengi imekuwa ni kikwazo kikubwa cha kuzifanya ibada zetu kama vile kusimamisha swala, Zaka, Swaumu na Hija, zisitufikishe kwenye lengo lililokusudiwa. ***'Ibada***' ni neno la Kiarabu ambalo hutokana na neno ***'Abd'*** lenye maana ya mtumwa. Kwa hiyo, katika Uislamu kufanya ibada ni kumtumikia Mwenyezi Mungu (s.w) kwa utii na unyenyekevu wa hali ya juu. Kutofahamika vyema maana halisi ya Ibada kumechangia sehemu kubwa ya kutofahamika lengo halisi la maisha ya mwanaadamu hapa ulimwenguni. Kama tunavyorejea katika Qur-an:

وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ ﴿٥٦﴾

*"Sikuwaumba majini na watu ila wapate Kuniabudu". (51:56).*

Kwa maana nyingine mwanaadamu anayetarajiwa aishi kwa kumtii Mwenyezi Mungu (s.w) kwa unyenyekevu katika kuendesha kila kipengele cha maisha yake yote hapa ulimwenguni.

Lakini mwanaadamu ameumbwa na matashi ya kimwili na amepewa uhuru wa kuamua; anaweza kukidhi matashi yake kwa kumuasi Mwenyezi Mungu (s.w) kwa kuruka mipaka aliyomuwekea. Matashi haya na uhuru huu aliopewa mwanaadamu, humfanya mwanaadamu awe katika mtihani mkubwa katika maisha yake ya hapa ulimwenguni. Ama ayasalimishe matashi yake kwa Mwenyezi Mungu (s.w) kwa kumtii kwa unyenyekevu katika kufuata maamrisho yake na kuacha makatazo yake, afaulu mtihani au ayafanye matashi yake mungu kwa kuyatii na kuyanyenyekea kinyume na kumtii na kumnyenyekea Mwenyezi Mungu (s.w) afeli mtihani.

**(iii) Miiko ya Funga haifuatwi vilivyo**

Kila mfungaji hana budi kufahamu vyema masharti na nguzo za swaumu. Ibada yoyote haikamiliki mpaka itekelezwe kwa kufuata masharti na nguzo zote za Ibadah hiyo na pawe na kumkumbuka Mwenyezi Mungu (s.w) katika kipindi chote cha kuitekeleza. Wengi wa wafungaji hawatekelezi vilivyo miiko ya funga na kwahiyo funga zao zimeshindwa kuwapatia matunda yanayotarajiwa. Hatuna budi kufahamu kuwa Miiko ya Kufunga haiishii kwenye kujizuilia kula, kunywa na kujamii tu bali ni pamoja na kujizuilia na maovu yote aliyoyakemea Mwenyezi Mungu (s.w) na Mtume wake. Rejea Hadithi ifuatayo:

> *Abu Hurairah (r.a) amesimulia kuwa Mtume (s.a.w) amesema: "Yule ambaye hataacha lugha mbaya na matendo mabaya, Mwenyezi Mungu (s.w) hana haja ya kuona kule kuacha kwake chakula na kinywaji chake (Mwenyezi Mungu (s.w) hakubali funga yake)" (Bukhari).*

Ni wangapi wanaofunga huku wanasengenya wengine, wanasema uwongo, wanafitinisha na kugombanisha watu na huku futari yao na daku inapatikana kwa njia za haramu? Ni wangapi wanaofunga ambao hufanya maovu mengine kuliko haya? Ni wazi kwamba funga zao haziwapatii faida yoyote mbali na kushinda njaa na kiu.

## Zoezi la Nne

1.(a) Fafanua maana mbili za swaumu kwa mujibu wa mwongozo wa Qur,an.
(b) Ibada ya funga si mateso ila ni neema kwa waislamu, thibitisha.

2. (a) Nukuu aya ya Qur,an inayobainisha kuwa swaumu ya Ramadhani ni ukumbusho na dira inayotuelekeza kufuata mwongozo wa Allah(s.w.) katika maisha ya kila siku.
(b) "Si Waislamu wote wanaolazimika kufunga katika mwezi wa Ramadhani" Fafanua kauli hii.

3. Bainisha:
(a) Nguzo za funga pamoja na Sunnah zake.
(b) Mambo yasiyobatilisha swaumu ya mfungaji.

4.
(a) "*Amesimulia Abu Hurairah (r.a) kuwa Mtume (s.a.w) amesema: "Mwenye kufunga mwezi wa Ramadhani akiwa na imani na akiwa na tegemeo la kupata malipo kutoka kwa Allah (s.w), basi dhambi zake zote zilizopita zitasamehewa. Na mwenye kusimama kwa swala katika usiku wa Qadr akiwa na imani na mategemeo ya kupata malipo kutoka kwa Allah, basi dhambi zake zote zilizotangulia zitasamehewa." (Bukhari).*

Kwa kuzingatia Hadithi, Waislamu wanapaswa wafanyaje ili kuudiriki usiku huu mtukufu katika mwezi wa Ramadhani kama alivyofanya Mtume Muhammad(s.a.w) na Maswahaba zake?

(b) Bainisha tafauti zilizopo kati ya Zakatul-fitr na Zakkatul-maali.

5. (a) Ni mambo yepi anayotakiwa kufanya Muislamu katika kilele cha kukamilisha funga ya Ramadhani?
(b) Bainisha siku ambazo hairuhusiwi Muislamu kufunga.

6. (a) Kwa kurejea mafundisho ya Qur,an na Sunnah chambua kwa muhtasari aina za funga.
(b) Unafikiri kwanini lengo la funga halifikiwi na wengi wanaofunga?

*************************

## Sura ya Tano

# HIJA NA ’UMRA

## Maana ya Hija na ’Umra

Katika lugha ya Kiarabu neno “**Hajj**” lina maana ya kuzuru au kutembelea mahali kwa lengo maalum. Katika Sharia ya Kiislamu, “**Kuhiji**” ni kuizuru Ka’aba - Nyumba takatifu ya Allah (s.w) - katika mwezi na siku maalum, kwa kuzingatia masharti na kutekeleza matendo yote yanayo ikamilisha ibada ya Hija kama ilivyoelekezwa katika Qur’an na Sunnah. Hija ni faradh kwa kila Muislamu ‘Mukallaf’ mwenye uwezo wa kiafya na mali mara moja katika umri wake.

Neno “***Umrah***” lina maana ya kutembelea. Katika sharia ya Kiislamu, kufanya `*Umrah*” ni kutembelea nyumba takatifu ya Ka’abah katika mwezi wowote na siku yoyote katika mwaka, kwa kuzingatia masharti na kutekeleza kwa ukamilifu matendo ya `Umrah ambayo ni Kutia nia katika vituo maalum (*Miqat*), kuwa katika Ihram, kutufu, kusa’i na kupunguza au kunyoa nywele. Ibada ya **‘Umrah** ina matendo machache zaidi kuliko ibada ya Hijja hivyo imeitwa “Hijja ndogo”. Ibadah ya ‘Umrah ni Sunnah iliyokokotezwa.

### Umuhimu na nafasi ya Ibada ya Hija katika Uislamu

Hija ni nguzo ya tano ya Uislamu iliyofaradhishwa kwa waumini kama tunavyojifunza katika aya ifuatayo:

... وَلِلَّهِ عَلَى ٱلنَّاسِ حِجُّ ٱلْبَيْتِ مَنِ ٱسْتَطَاعَ إِلَيْهِ سَبِيلًا ۚ وَمَن كَفَرَ
فَإِنَّ ٱللَّهَ غَنِىٌّ عَنِ ٱلْعَٰلَمِينَ ﴿٩٧﴾

*“... Na Mwenyezi Mungu amewawajibishia watu wafanye Hija katika Nyumba hiyo (Al-Ka’aba), yule awezaye kufunga safari kwenda huko. Na atakayekanusha (asiende na hali ya kuwa ana uwezo) basi Mwenyezi Mungu si muhitaji anayewahitajia walimwengu”(3:97).*

Pia katika Hadith iliyosimuliwa na Abu Hurairah (r.a), Mtume (s.a.w) alitoa khutuba akasema:

*“Enyi watu! Hija imeamrishwa kwenu, basi Hijini”. Mtu mmoja akauliza: “Ee Mtume wa Allah! ni kila mwaka? Mtume (s.a.w) alinyamaza mpaka*

*yule mtu akarudia kuuliza swali hilo mara tatu. Kisha Mtume akasema:"kama ningalisema 'ndio', ingalikuwa faradhi kuhiji kila mwaka na pangalikuwa hakuna hiari " (Muslim).*

Hija imefaradhishwa kwa Waislamu wenye uwezo wa kusafiri na kugharimia safari na masurufu, mara moja katika maisha yao. Mwenye uwezo wa kuhiji, akaacha makusudi kuhiji si Muislamu japo ataendelea kujiita Muislamu na watu wataendelea kumuita hivyo, kwani Allah (s.w) anasema

وَمَن كَفَرَ فَإِنَّ ٱللَّهَ غَنِيٌّ عَنِ ٱلْعَٰلَمِينَ ﴿٩٧﴾

*"...Na atakayekanusha (asiende na hali ana uwezo) basi Mwenyezi Mungu si muhitaji, kuwahitajia walimwengu" (3:97).*

Maneno haya ya Allah (s.w) ni makemeo makubwa sana kwa wanaopuuzia Ibada hii. Allah (s.w) hana haja na Uislamu wao, na matendo yao mema waliyofanya yataruka patupu kwani Allah (s.w) hana haja nayo. Katika kuonyesha ubaya wa kukanusha amri hii ya Hija, Mtume (s.a.w) anasema katika Hadith iliyosimuliwa na Ali (r.a) kuwa:

*Yeyote atakayekuwa na uwezo wa kuhiji katika Nyumba ya Allah, lakini asifanye hivyo akifa atakuwa hana tofauti na Myahudi au Mkristo na hiyo ni kwa sababu Allah (s.w) amesema:*

...وَلِلَّهِ عَلَى ٱلنَّاسِ حِجُّ ٱلْبَيْتِ مَنِ ٱسْتَطَاعَ إِلَيْهِ سَبِيلًا ... ﴿٩٧﴾

*"... Na Mwenyezi Mungu amewaamrisha watu wafanye Hija katika Nyumba hiyo, yule awezaye kufunga safari kwenda huko ..." (3:97) (Tirmidh).*

Ni katika msingi huu Mtume (s.a.w) ameamuru katika Hadith aliyosimulia Ibn Abbas(r.a):

*"Yeyote anayehusika kuhiji, na aharakishe". (Abu Daud, Darimi).*

Hivyo basi mtu akifikia baleghe na akawa na afya njema na uwezo wa kugharimia safari ya Hija, Ibada hiyo itakuwa faradhi kwake na kama hataitekeleza wakati huo na ikawa uwezo huo umemuishia baada ya Hija hiyo, basi afahamu vyema kuwa atahesabiwa kuwa kavunja faradhi ya Hija. Kwa hivyo kila Muislamu anapopata uwezo wa kuhiji, hana budi

kuhiji wakati huo huo.

Hija na Umrah ni Ibada za hali ya juu zenye kuahidiwa malipo makubwa mbele ya Allah (s.w) kama tunavyojifunza katika hadith zifuatazo:

*Abu Hurairah (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: "Atakayefunga safari ya Hija kwa ajili ya Allah bila kuongea maneno maovu na kufanya vitendo viovu, atarudi (akiwa huru na dhambi) kama siku ile aliyozaliwa na mama yake." (Bukhari na Muslim).*

*Abu Hurairah (r.a) amesimulia tena kuwa Mtume wa Allah kasema: "Umra moja ni kifutio cha dhambi zilizofanywa katika kipindi kati ya Umra hii na Umra inayofuatia na Haji iliyokamilika haina malipo mengine isipokuwa Pepo." (Bukhari na Muslim)*

**Wanaowajibika kuhiji**

...وَلِلَّهِ عَلَى ٱلنَّاسِ حِجُّ ٱلْبَيْتِ مَنِ ٱسْتَطَاعَ إِلَيْهِ سَبِيلًا... ﴿٩٧﴾

*"...Na Mwenyezi Mungu anawaamrisha watu kufanya Hija katika nyumba hiyo (Al-Ka'aba) yule awezaye kufunga safari kwenda huko ..." (3:97).*

**(a) Waliobaleghe**

Watoto wa kiume na wa kike ambao hawajabaleghe au hawajafikia umri wa kubaleghe (miaka 15), hawawajibiki kwa Hija hata kama wana uwezo wa kwenda huko. Hata hivyo watoto wanaruhusiwa kuhiji kama tunavyofahamishwa katika Hadith zifuatazo:

*Ibn Abbas(r.a) ameeleza kuwa katika safari ya Hija ya kuaga, mwanamke mmoja alimleta mtoto wake mbele ya Mtume na akauliza kama naye anaruhusiwa kuhiji. Mtume (s.a.w) alijibu: "Ndio na pia utapata malipo yake." (Bukhari).*

*Jabir (r.a) amehadithia:" Tuliongozana na Mtume (s.a.w) katika msafara wa Hija na tulikuwa pamoja na wanawake na watoto. Tuliitikia - "Labbayka" kwa niaba ya watoto na tulitupa mawe kwenye minara( kwa niaba yao)". (Ahmad, Ibn Majah).*

Kutokana na Hadith hizi watoto pia wanaruhusiwa kuhiji, na vile vitendo wasivyoweza kuvitekeleza vifanywe kwa niaba yao na wazazi au

walezi wao. Kama mzazi au mlezi itabidi ambebe mtoto kwa ajili ya kutekeleza ibada ya tawafu na sa'i, ni lazima anuie kuwa anamfanyia mtoto na haitachanganywa na tawafu na sa'i yake. Hivyo itabidi atufu na kusai tena kwa niaba yake mwenyewe. Ieleweke kuwa Hija ya mtoto haimvui mtu kwenye wajibu wa kuhiji atakapofikia baleghe. Hivyo mtu atakapofikia baleghe atalazimika kuhiji tena iwapo atakuwa na uwezo wa kufanya hivyo.

**(b) Wenye Akili Timamu**

Mtu aliyepungukiwa au aliyevurugikiwa na akili kama vile kichaa, punguani, taahira, n.k. hawajibiki kwa amrisho lolote lile la Uislamu na hesabu yake ni kama ile ya mtoto ambaye hajafikia baleghe, kwani Mtume (s.a.w) amesema:"Kalamu (ya kuandika amali njema au mbaya ya mja) inasimamishwa kwa watu watatu - mtu aliye lala mpaka aamke, mtoto mpaka afikie baleghe, na kichaa (mgonjwa wa akili) mpaka apone."

**(c) Waungwana**

Wafungwa au watumwa hawawajibiki kwa Hija mpaka watakapokuwa huru.

**(d) Wenye Uwezo**

Wanaowajibika kuhiji ni wale wenye uwezo wa afya, na nauli ya kuwawezesha kufunga safari ya Makka ya kwenda na kurudi, pamoja na matumizi (masurufu) ya safari nzima na matumizi ya kuwaachia familia yake nyumbani. Si vyema mtu kuzunguka huku na huko kuomba omba kwa ajili ya Hija. Halikadhalika si vyema mtu kufunga safari ya Hija na huku hana masurufu ya kumtosha kiasi cha kumpelekea kuwa aanze kuombaomba ili aweze kumaliza safari. Pia si vema mtu kuwaacha ahali zake pasina matumizi ya kawaida katika kipindi chote atakapokuwa safarini na kuwaacha katika hali itakayowapelekea kuwa ombaomba. Kwa ujumla kuombaomba katika Uislam ni haramu. Kwa nini kujikalifisha nafsi na hali faradhi ya Hija ni kwa wale tu wenye uwezo kama isemavyo Qur'an

...وَلِلَّهِ عَلَى ٱلنَّاسِ حِجُّ ٱلْبَيْتِ مَنِ ٱسْتَطَاعَ إِلَيْهِ سَبِيلًا... ﴿٩٧﴾

*"... .Na Mwenyezi Mungu amewajibisha wafanye Hija katika Nyumba hiyo (al-Ka'aba) kwa yule awezaye kufunga safari kwenda huko. (3:97).*

Aidha Allah (s.w) anatuhimiza kuchukua masurufu ya kutosha

katika aya ifuatayo:

وَتَزَوَّدُوا۟ فَإِنَّ خَيْرَ ٱلزَّادِ ٱلتَّقْوَىٰ ۚ وَٱتَّقُونِ يَـٰٓأُو۟لِى ٱلْأَلْبَـٰبِ ﴿١٩٧﴾

*"...Na chukueni masurufu (ya kutumia njiani, msiombe) Na hakika masurufu bora ni yale yanayomfanya mtu asiombe. Na nicheni Mimi enye wenyi akili" (2:197).*

Ni dhahiri kuwa endapo mtu hana masurufu ya kumtosha yeye mwenyewe kutumia njiani,na ya kumtosha kuwabakishia kitu cha kuwatosha ahali zake, hawajibiki kwa Hija hata kama ana nauli ya kwenda na kurudi. Kama mtu ana uwezo wa mali lakini hana uwezo wa afya kwa sababu ya ugonjwa au uzee, hatawajibika kwa Hija. Mgonjwa atawajibika tena atakapopona endapo atakuwa bado ana uwezo wa kimali. Wazee na wenye magonjwa ya kudumu, kama wana mali ya kutosha kuhiji watawapa ndugu zao Waislamu wakahiji kwa niaba yao, kama tunavyojifunza katika Hadith ifuatayo:

*Imesimuliwa na Fazal bin Abbas (r.a) kuwa mwanamke mmoja kutoka katika kabila la Banu Khasham alimuuliza Mtume (s.a.w): "Allah (s.w) amefaradhisha Hija kwa watu wote, lakini baba yangu ni mzee sana kwa kiasi kwamba hawezi kufunga safari hii ya Hija Je, ninaweza kuhiji kwa niaba yake?" Mtume (s.w) alimpa ruhusa ya kufanya hivyo. Hii ilitokea katika Hija ya kuaga. (Bukhari na Muslim).*

Ni muhimu kwa wenye kuhiji kwa niaba ya wengine, wawe wenyewe wameshahiji kwa mnasaba wa Hadith ifuatayo:

*Abdullah bin Abbas(r.a) ameeleza kuwa katika Hija ya kuaga, Mtume (s.a.w) alimsikia mtu mmoja akiitikia "Labbayka" kwa niaba ya Shubruma. Alimuuliza yule mtu kuwa yeye mwenyewe keshahiji. Alipopata jibu kuwa haja hiji, Mtume (s.a.w) alimuamuru kufanya Hija yake kwanza na ndio baadaye afanye Hija kwa niaba ya Shubruma. (Abu Daud).*

Mwenye kuhiji kwa niaba ya mwingine atapata malipo ya Hija sawa na yule aliyefanya Hija kwa niaba yake ambaye ndiye aliyetoa gharama zote za Hija. Pia inajuzu kufanya Hija kwa niaba ya ndugu Muislamu aliyefariki huku akiwa na uwezo na nia ya kuhiji kama tunavyojifunza katika Hadith ifuatayo:

*Amehadithia Abdullah bin Abbas (r.a) kuwa mwanamke mmoja aliuliza: "Mama yangu alinuia kuhiji lakini alifariki kabla ya Kuhiji. Je, naweza kuhiji kwa niaba yake? Alijibu Mtume (s.a.w)" unaweza, hasa. Jaalia*

*kuwa mama yako alikuwa na deni, je isingelikuwa umeshamlipia deni hilo? Hali kadhalika hili ni deni la Allah (s.w) juu yako na Allah (s.w) ana haki zaidi na deni lake kuliko mwingine yeyote"(Bukhari).*

Kutokana na Hadith hii Muislamu yeyote aliyekufa na deni la Hija, yaani aliyekuwa na mali na uwezo wa kumuwezesha kuhiji lakini akafa bila ya kuhiji, itabidi warithi wake, kabla ya kugawanya urithi watenge fungu la kutosha kuhiji kwani hili ni deni kwa Allah (s.w). Kisha warithi watamteau miongoni mwao au Muislamu yeyote kwenda kufanya Hija kwa niaba ya marehemu kwa kutumia fungu hilo.

**(e) Wasiowekewa kizuizi njiani**

Iwapo njia wanayosafiria kwenda Hija itakuwa imewekewa kizuizi au imefungwa kwa karantini (Quarantine), kwa usalama au kwa sababu nyingine yoyote, basi Waislamu wa sehemu hiyo hawatalazimika kwa Hija mwaka huo.

**(f) Wanawake waongozane na Maharim**

Hija imeamrishwa kwa Waislamu wanaume na wanawake wenye sifa zote hizo zilizotajwa hapo juu (a)-(e), lakini pia mwanamke hatawajibika kwa Hija mpaka apate wa kuongozana naye, awe mume wake au maharimu wake kama tunavyojifunza katika Hadith zifuatazo:

*Abu Sayyid Khudhr (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: "Ni haramu kwa mwanamke mwenye kumuamini Allah na siku ya Mwisho kuchukua safari ya siku moja au zaidi bila ya kuandamana na baba yake au kaka yake au mume wake au mtoto wake wa kiume au maharimu wake wengine" (Bukhari).*

*Imesimuliwa kuwa Sahaba mmoja alieleza kuwa mke wake ameenda kuhiji, na yeye mwenyewe alijiandikisha kwa vita fulani vya Jihadi. Mtume (s.a.w) alimuamuru asiende kwenye vita na badala yake aende kuhiji. (Bukhari).*

Mwanamke ambaye Hija imemuwajibikia na ambaye anaongozana na maharimu wake, hana budi kumtaka ruhusa mumewe. Kama mumewe atamnyima ruhusa, itabidi aende tu kwani mume hana haki ya kumkataza mkewe kutekeleza maamrisho ya Allah (s.w) bali anaweza kumkatalia kufanya kitendo cha Naafilah(Sunnah).

*Amesimulia Abdullah bin Umar(r.a) kuwa wakati mmoja mwanamke tajiri alikataliwa kwenda safari ya Hija ya nyongeza. Shauri hili lilipofikishwa kwa Mtume (s.a.w) Mtume (s.a.w) alikubaliana na uamuzi wa yule mumewe. (Dar Qutni).*

Kwa ujumla matendo yote ya Naafilah (Sunnah) wanawake watafanya kwa kutaka ruhusa kwa waume zao. Muislamu atakapokamilika kwa sifa zote hizi, (a)-(f) hana budi kuharakisha kukamilisha ibada hii ya Hija, ili baada ya muda asije akapungukiwa na baadhi ya sifa hizi na kushindwa kutekeleza ibada hii. Tukumbuke kuwa tukijicheleweshа kufanya Hija kwa uzembe tu baada ya kuwa na uwezo tutakuwa mas-uul (wenye kuulizwa) mbele ya Allah (s.w), endapo tutaondokewa na uwezo wa kuhiji baada ya muda kupita. Daima mwanadamu hajui yanayokuja mbele yake. Mtu anaweza kufilisika au kupatwa na ugonjwa wa kudumu au kufa wakati wowote.Hivyo, daima Muislamu anatakiwa aharakie kutekeleza maamrisho ya Allah (s.w). Ni katika msingi huu Mtume (s.a.w) anatuusia:

*"Yeyote anayekusudia kuhiji na aharakishe". (Abu Daud, Darimi).*

**Muda wa Hijja**

Ibada ya Hija hufanywa katika muda maalum wa mwaka kama inavyosisitizwa katika Qur-an:

ٱلْحَجُّ أَشْهُرٌ مَّعْلُومَٰتٌ ۚ ... ﴿١٩٧﴾

*"Hija ni miezi maalum..." (2:197).*

Miezi iliyowekwa kwa ajili ya Muislamu kunuia kuizuru Ka'ba kwa ajili ya Hija ni mwezi wa Shawwal, mwezi wa Dhul-Qaadah (mfungo pili) na siku kumi za mwanzo za mwezi wa Dhul-Hijah. Wakati wowote katika miezi hii mtu anaweza kwenda Makka kwa ajili ya Hija, lakini hataweza kufanya matendo ya Hija mpaka uanzie mwezi wa Dhul-Hija. Siku za Hija ni kuanzia tarehe 8 Dhul-Hija mpaka tarehe 13 Dhul-Hija.

**Mwenendo wa mwenye kunuia Hija au 'Umra**

Mwenye kunuia kuhiji katika miezi hiyo iliyotajwa, analazimika ajipambe na tabia nzuri.Ajizuilie na maneno na matendo machafu na maovu. Ajitahidi kuishi na watu kwa wema, awatake radhi kwa yale yote mabaya aliyowatendea na azidishe kuwatendea wema.Allah (s.w) anatuagiza:

... فَمَن فَرَضَ فِيهِنَّ ٱلْحَجَّ فَلَا رَفَثَ وَلَا فُسُوقَ وَلَا جِدَالَ فِى
ٱلْحَجِّ ۗ وَمَا تَفْعَلُوا۟ مِنْ خَيْرٍ يَعْلَمْهُ ٱللَّهُ ۗ ... ﴿١٩٧﴾

*... Na anayekusudia kufanya Hija katika miezi hiyo, basi asiseme maneno machafu wala asifanye vitendo vichafu wala asibishane katika hiyo Hija.*

*Na kheri yoyote mnayoifanya Mwenyezi Mungu huijua ....” (2:197).*

Mwenye kuhiji au kufanya ‘Umra anatakiwa ajipambe na tabia hiyo njema kwa kipindi chote atakapokuwa safarini. Yafuatayo ni mambo muhimu anayotakiwa ayazingatie mtu anapokuwa katika safari ya Hija au Umra.

(i) Ajiepushe na maneno maovu na machafu, pia ajiepushe na vitendo viovu na vichafu.

(ii) Azidishe kusoma Qur’an na Kuswali swala za faradhi kwa jamaa, kuswali swala za sunnah, kuomba msamaha na kutubu kikweli kweli kwa Mola wake.

(iii) Ajitahidi kuwa mwema na mpole kwa wasafiri wenzake, kuongea nao vizuri, kuwapa msaada wanaohitajia, kuwasamehe kwa kosa lolote watakalomfanyia, kujizuia na hasira na kuvumilia maudhi mengi yanayotokana na wasafiri wenzake au wenyeji wa sehemu za Hija.

(iv) Ajitahidi kuchanganyika na wasafiri wenzake kutoka sehemu mbalimbali, ajitahidi kujihusisha kwenye mikutano na mazungumzo ya kheri na kujaribu kubadilishana mawazo na wenzake kutoka sehemu mbalimbali ambao wanaelewana lugha, juu ya usimamishaji Uislamu ulimwenguni.

(v) Ajitahidi kuinamisha macho yake katika makundi yenye mchanganyiko wa wanawake na wanaume na kila itakapowezekana ajiepushe kuwa katika mchanganyiko wa wanaume na wanawake.

## Vituo vya kunuia Hija

Miongoni mwa mambo muhimu kwa wenye kuhiji au kufanya ‘Umra ni kufahamu vituo ambapo watanuia kuanza kuhiji rasmi na kuvalia vazi la Ihram. Vituo hivi huitwa ***Miiqaat***. ***Miiqaat*** ni vituo maalum vilivyowekwa katika njia za sehemu mbali mbali za kuingilia sehemu takatifu (Haram) ya Makka ambapo mahujaji wakifika humo huvua nguo zao za kawaida na kuvalia vazi rasmi la Ihram na kunuia rasmi kuanza ibada ya Hija au ‘Umra. Vituo vya kunuia Hijja alivyoviweka Mtume (s.a.w) kwa watu wa kutoka kila upande ni hivi vifuatavyo:

(i) **Zul-Hulaifa**: - ni kituo cha watu wanaotoka sehemu za Madina. Kituo hiki kiko umbali wa kilometa 450 kutoka Makka. Hivi sasa kituo hiki kinajulikana kwa jina la Bir-’Ali.

(ii) **Juhfah**: Kituo hiki kiko umbali wa Kilometa 187 Kaskazini-Magharibi ya Makka. Ni kituo cha watu wanaotoka sehemu za Misr, Sham (Syria), n.k. Hivi sasa kituo hiki kinajulikana kwa jina la **Rabigh.**

(iii) **Qurnul Manazil**: - Kituo hiki kiko umbali wa Kilometa 94 mashariki ya Makka na ni kituo cha watu kutoka mji wa Najd. Kituo hiki hivi sasa kinajulikana kwa jina la **Sail.**

(iv) **Yalamlam**: Kituo hiki kiko umbali wa kilometa 54 kusini magharibi ya Makka: Ni kituo cha watu kutoka Yemen na sehemu nyingine za kusini kama vile Afrika ya Mashariki, Afrika ya Kusini, n.k.

(v) **Makka**: Wakazi wa Makka watavalia Ihram na kunuia Hija au 'Umra humo humo majumbani mwao. Vile vile wakazi wa vituo vingine, vilivyotajwa hapo juu, watanuia Hija au 'Umra na kuvalia Ihram humo humo majumbani mwao. Vituo hivi vitano vimebainishwa katika Hadith ifuatayo:

*Amesimulia Ibn Abbas (r.a) kuwa Mtume wa Allah ameweka Dhul-Hulaifa kama Miiqaat ya watu wa Madina; Al-Juhfa kwa watu wa Sham (Syria); Qarn ul-Manaazil kwa watu wa Najd; na Yalamlam kwa watu wa Yemen. Kwa hiyo hivi ni vituo (Mawaaqiit) kwa wale wote wanaoishi katika vituo hivi na wale wanaopitia katika vituo hivi kwa nia ya Kuhiji au kufanya 'Umra na yeyote anayeishi katika sehemu hizi atavalia Ihram nyumbani kwake, hali kadhalika wakazi wa Makka wanaweza kuvalia Ihram humo humo Makka. (Bukhari).*

(vi) **Dhaaru-Irq**: Kituo hiki kipo umbali wa kilomita 94 kaskazini-mashariki ya Makka. Ni kituo cha watu wa Iraq, Iran, n.k. Kituo hiki hakikuwekwa na Mtume (s.a.w) bali kiliwekwa na 'Umar bin Khattaab (r.a) alipokuwa Khalifa kama tunavyofahamishwa katika Hadith ifuatayo:

*Amesimulia Ibn Umar (r.a): Wakati miji hii miwili (Basra na Kufa) ilipotekwa, watu walikwenda kwa 'Umar (r.a) na kusema: Ee Amir wa Waumini, Mtume (s.a.w) ameweka Qarn kama Miiqaat ya watu wa Najd, lakini iko kinyume kabisa na njia yetu na ni vigumu sana kwetu kupitia hapo. Akasema, (Umar), fanyeni kituo (miiqaat) chenu katika sehemu iliyo kinyume na Qarn ambayo iko katika njia yenu ya kawaida. kwa hiyo aliiweka Dhaaru-irq kama Miiqaat. (Bukhari)*

(vii) **Jiddah**: Miiqaat ya Wasafiri wa ndege. Kama ilivyosisitizwa katika Hadith watu kutoka sehemu mbali mbali wanalazimika kuvalia Ihram na kunuia Hija au 'Umra katika vituo vilivyowekwa endapo watapitia humo. Ilivyo ni kwamba vituo vyote hivi vilivyotajwa katika Hadith hizi vinapitiwa na wasafiri wa gari au wanyama. Wasafiri wengi wanaotoka nchi za mbali husafiri kwa ndege mpaka Jiddah na hapo ndipo wanapovalia Ihram na kunuia Hija au 'Umra. Jiddah iko kilomita 72 kutoka Makka.

## Ihram

Mwenye kunuia Hija au 'Umra katika Miiqaat anakuwa katika hali ya kuchunga masharti kadhaa mpaka akamilishe matendo kadhaa ya Hija au 'Umra. Hali hii ya kuchunga masharti hujulikana kwa jina la "*Ihram*".

Wanaume wanapokuwa katika Ihram hulazimika kuvaa vazi rasmi la Ihram.Vazi la Ihram kwa wanaume ni kuvaa shuka mbili nyeupe zisizo shonwa.Shuka moja hufungwa kiunoni na mkanda huweza kutumika ili kuhakikisha isivuke. Shuka la pili huvaliwa lubega kwa kufunika bega la kulia na kuacha wazi bega la kushoto. Katika hali ya Ihram, ni haram kwa mwanamume kuvaa nguo nyingine yoyote, ni haramu kufunika kichwa, ni haram kuvaa soksi au kuvaa viatu vinavyofunika miguu.

Wanawake hawana vazi rasmi la Ihram. Akiwa katika Ihram Hajat analazimika kama kawaida kujifunika mwili wake wote isipokuwa uso na viganja vya mikono na atavalia ushungi. Hijab yaweza kuwa ya rangi yoyote isiyovutia kama kawaida ya vazi la mwanamke wa Kiislamu lakini vazi jeupe ni bora. Mwanamke akiwa katika Ihram ni haramu kufunika uso au kuvaa soksi za mikononi*(gloves)*. Pia wanawake katika Ihram hawaruhusiwi kuvaa soksi wala kuvaa viatu vinavyofunika miguu.

## Yaliyoharamishwa kwa Mwenye kuwa katika Ihram

(i) Kujimai (kufanya tendo la ndoa) au kubusu au kukumbatiana au kufanya vitendo vingine vya kimapenzi kati ya mume na mke ambavyo vitawaletea fikra za kufanya tendo la ndoa.

(ii) Kusema maneno maovu na machafu kama vile kusengenya,kugombana, kugombanisha, kusema uwongo, kubishana, n.k.

(iii) Kutenda maovu na machafu.

- فَمَن فَرَضَ فِيهِنَّ ٱلْحَجَّ فَلَا رَفَثَ وَلَا فُسُوقَ وَلَا جِدَالَ فِى ٱلْحَجِّ

*Na anayekusudia kufanya Hija katika (miezi) hiyo basi asiseme maneno machafu wala asifanye vitendo vichafu wala asibishane katika hiyo Hija ... (2:197).*

(iv) Kunyoa au kung'oa nywele, kukata kucha au kukata au kupunguza sehemu yoyote ya mwili ila kwa matibabu kama vile kuumika, kutolewa damu kwa ajili ya matibabu na mengineyo.
(vi) Kuoa au kufanya mipango ya ndoa au hata kupeleka posa.
(vii) Kujipaka manukato
(viii) Kuvaa nguo ya rangi yenye kuvutia
(ix) Kwa wanaume kuvaa nguo iliyoshonwa, na kufunika kichwa.
(x) Kwa wanawake kufunika uso na kufunika viganja vya mikono kwa kuvaa glovu (gloves).
(xi) Kuvaa viatu vinavyofunika miguu na kuvaa soksi.
(xii) Kuwinda au kusaidia kuwinda angalau kwa kuonyesha mnyama anayewindwa.
(xiii) Kula nyama iliyowindwa au iliyopatikana kwa msaada wa mtu aliyekuwa katika Ihram.
(xiv) Kula mayai ya ndege waliopatikana kwa kuwindwa.

**Kafara kwa mwenye kuvunja masharti ya Ihram**

Allah (s.w) kwa Urehemevu wake, ametoa nafuu kwa wale watakaovunja masharti ya Ihram kwa kutoa fidia isipokuwa kwa kosa la jimai.Tunafahamishwa katika Qur-an:

فَمَن كَانَ مِنكُم مَّرِيضًا أَوْ بِهِۦٓ أَذًى مِّن رَّأْسِهِۦ فَفِدْيَةٌ مِّن صِيَامٍ أَوْ صَدَقَةٍ أَوْ نُسُكٍ

*"... Na atakayekuwa mgonjwa katika nyinyi au ana vya kumuudhi kichwani mwake (akafanya yaliyokatazwa, kama vile kunyoa), basi atoe fidia kwa kufunga au (kwa kutoa) sadaqat au kuchinja mnyama ..." (2:196)*

Katika Hadith tunafahamishwa:
*Ka'ab bin Ajra (r.a) ameeleza: "Nilipokuwa katika (hali ya) Ihram kwa ajili ya 'Umra nilisumbuliwa sana na chawa kichwani mwangu. Mtume*

*wa Allah (s.a.w) akaniambia ninyoe kisha nifunge siku tatu au nichinje mbuzi wa sadaqat au niwalishe maskini sita. (Bukhari, Muslim, Abu Daud).*

Kwa hiyo kwa Muharim atakayevunja sharti lolote la Ihram atalazimika kutoa kafara kwa ama (i) kufunga siku 3 au (ii) kumchinja mbuzi na kuitoa nyama yake sadaqat au (iii) kulisha maskini sita.

Kumwingilia mke ni kosa lisilosameheka kwa kutoa kafara bali hubatilisha Hija au 'Umra moja kwa moja. Ama kwa mume aliyefanya mapenzi na mkewe kwa kubusiana na kumkumbatia bila ya kufanya kitendo cha ndoa, atatoa kafara ya ngamia (au thamani yake) kama atatokwa na manii na kama hatatokwa na manii, atatoa kafara ya mbuzi.

Kafara kwa mwenye kuwinda au kuonyesha windo akiwa katika Ihram ni mbuzi iwapo mnyama huyo ana ukubwa wa mbuzi, au mdogo zaidi kuliko hivyo; vinginevyo atatoa kafara ya mnyama aliye sawa na huyo aliyemuwinda au atatoa thamani yake anunue vibaba vya chakula kinacholiwa sana katika sehemu hiyo, na kumlisha kila maskini kwa vibaba vitakavyopatikana. Hivi ndivyo tunavyoagizwa katika Qur-an:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ لَا تَقْتُلُواْ ٱلصَّيْدَ وَأَنتُمْ حُرُمٌۚ وَمَن قَتَلَهُۥ مِنكُم
مُّتَعَمِّدًا فَجَزَآءٌ مِّثْلُ مَا قَتَلَ مِنَ ٱلنَّعَمِ يَحْكُمُ بِهِۦ ذَوَا عَدْلٍ مِّنكُمْ هَدْيًۢا
بَٰلِغَ ٱلْكَعْبَةِ أَوْ كَفَّٰرَةٌ طَعَامُ مَسَٰكِينَ أَوْ عَدْلُ ذَٰلِكَ صِيَامًا لِّيَذُوقَ وَبَالَ
أَمْرِهِۦۗ عَفَا ٱللَّهُ عَمَّا سَلَفَۚ وَمَنْ عَادَ فَيَنتَقِمُ ٱللَّهُ مِنْهُۗ وَٱللَّهُ عَزِيزٌ ذُو ٱنتِقَامٍ

*Enyi mlioamini! Msiue mawindo na hali ya kuwa mmo katika Hija au 'Umra. Na miongoni mwenu atakayemuua makusudi basi malipo yake yatakuwa kwa (kuchinja) kilicho sawa na alichokiua katika wanyama wanaofugwa kama watavyohukumu waadilifu wawili miongoni mwenu.Mnyama huyo apelekwe ilipo Ka'aba (akachinjwe na kutolewa sadaqat huko) au badala ya hayo ni kufunga, ili aonje ubaya wa jambo lake (hili). Mwenyezi Mungu ameyafuta yaliyopita; lakini atakayefanya tena Mwenyezi Mungu atamuadhibu. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye Nguvu na Mwenye kuadhibu. (5:95).*

### Aina za Hija

Kuna aina tatu za Hija ambazo kila mwenye kuhiji ana uhuru wa kuchagua mojawapo kulingana na uwezo wake wa kukidhi masharti ya kila aina. Aina hizi ni (i) Ifraad, (ii) Qiran na (iii) Tamattu kama zinavyoelezewa katika hadith ifuatayo:

*Amesimulia Aysha (r.a): "Tulitoka na Mtume wa Allah (s.a.w) (kwenda Makka) katika Hija ya Mtume ya kuaga. Miongoni mwetu tulivaa Ihram kwa nia ya kufanya `Umra tu (al-Tamattu) wengine kwa Hija na `Umra pamoja (al-Qiran) na kwa wengine kwa Hija tu (al-Ifraad). Mtume wa Allah (s.a.w) alivaa Ihram kwa nia ya Hija tu. Kwa hiyo kwa yule aliye vaa Ihram kwa Hija tu au kwa Hija na `Umra pamoja, hakutoka katika Ihram mpaka siku ya kuchinja (kutoa muhanga yaani siku ya mwezi 10 Dhul-Hija). (Bukhari).*

(i) **Ifraad**: Ni aina ya Hija ambapo, "Hajj" anavaa Ihram kwa nia ya kufanya Hija tu bila ya "Umra" na ataanza kuitikia mwito wa Allah (s.a.w ) kwa:(*Labbaika lhajji* ) yaani "Nimeitika kwa Hija." Hajj hatavua Ihram yake mpaka amalize matendo yote ya Hija yanayomlazimu kuwa katika Ihram. Haji huruhusiwa kuvua Ihram na kutoka kwenye masharti yake baada ya kutupa mawe kwenye mnara na kunyoa au kupunguza nywele siku ya mwezi 10 Dhul-Hija. Kwa yule aliyechagua aina hii ya Hija halazimiki kuchinja siku ya mwezi 10 Dhul-Hija.

(ii) **Qiran**: Ni aina ya Hija ambapo Haji huvaa Ihram kwa nia ya kufanya Hija na 'Umra pamoja na katika talbiya ataanza kutikia mwito wa Allah kwa: (*labbaika lhajji wa Umra*) - yaani "Nimeitika kwa Hija na 'Umra'.Hajj katika aina hii ya Hija hatavua Ihram mpaka baada ya kuchinja na kufanya Tawaful-Ifadha (tawafu ya nguzo) siku ya mwezi 10 Dhul-Hija.

*Aina hii ya Hija inafanywa na wale wanaokuja Makka na wanyama. Katika Hija yake ya kuaga, baada ya kumaliza ibada ya 'Umra, Mtume (s.a.w) aliwaamrisha watu wote wavue Ihram ila kwa wale waliokuja na wanyama.*

(iii) **Tamattu**: Katika aina hii ya Hija, Haji anapofika katika Miiqaat yake huvaa Ihram kwa nia ya kufanya ‘Umra tu na ataitikia mwito wa (*Labbaika liumra*) - yaani “Naitikia kwa ‘Umra’. Baada ya kumaliza ‘Umra atanyoa au kupunguza nywele na kuvua Ihram na kuwa huru na miiko yote ya Ihram. Atavaa tena Ihram kwa nia ya Hija mnamo mwezi 8 Dhul-Hija, na atabakia na Ihram mpaka amalize Hija ya mwezi 10 Dhul-Hija kama ilivyo katika aina nyingine za Hija. Haji analazimika kuchinja siku ya mwezi 10 Dhul-hija.

Katika aina hizi tatu za Hija, At-Tamattu ndio aina bora zaidi na yenye nafuu kubwa kwa wale wanaotoka mbali wasioweza kuja na wanyama, ama kwa wakazi wa Makka au majirani wa Makka ambao wana uwezo wa kwenda na wanyama, Hija iliyo bora kwao ni hii ya Al-Qiran. Lakini wenye kuhiji Hija ya Tamattu wanalazimika kununua mnyama na kumchinja siku ya mwezi 10 Dhul-Hija kama tunavyofahamishwa katika Qur’an:

فَإِذَآ أَمِنتُمۡ فَمَن تَمَتَّعَ بِٱلۡعُمۡرَةِ إِلَى ٱلۡحَجِّ فَمَا ٱسۡتَيۡسَرَ مِنَ ٱلۡهَدۡيِۚ
فَمَن لَّمۡ يَجِدۡ فَصِيَامُ ثَلَٰثَةِ أَيَّامٖ فِي ٱلۡحَجِّ وَسَبۡعَةٍ إِذَا رَجَعۡتُمۡۗ
تِلۡكَ عَشَرَةٞ كَامِلَةٞۗ ذَٰلِكَ لِمَن لَّمۡ يَكُنۡ أَهۡلُهُۥ حَاضِرِي ٱلۡمَسۡجِدِ ٱلۡحَرَامِۚ
وَٱتَّقُواْ ٱللَّهَ وَٱعۡلَمُوٓاْ أَنَّ ٱللَّهَ شَدِيدُ ٱلۡعِقَابِ ١٩٦

*“... Na mtakapokuwa kwenye salama, basi mwenye kujistarehesha kwa kufanya `Umra kisha ndio akahiji, basi achinje mnyama aliyesahilika (mbuzi au kondoo).Na asiyepata, afunge siku tatu katika Hija na siku saba atakaporudi (kwake); hizi ni kumi kamili. Hayo ni kwa ajili ya yule ambaye watu wake hawako karibu na msikiti Mtakatifu wa Makka. Na mcheni Mwenyezi Mungu na jueni ya kuwa Mwenyezi Mungu ni Mkali wa kuadhibu.” (2:196).*

## Matendo ya Hija na ‘’Umra

### 1.Ihram na Nia ya Hija au ‘Umra

Matendo ya Hija au ‘Umra huanza rasmi kwa kuvalia vazi la Ihram. Kama tulivyoona Ihram huvaliwa nyumbani au katika vituo maalum -

Mawaaqiit - vilivyowekwa na Mtume (s.a.w) kabla ya kuingia kwenye uwanja Mtakatifu wa Makka. Wakazi wa Makka huvalia Ihram nyumbani kwao.

Utaratibu unaofuatwa ni kwamba Hajj, kabla ya kuvaa Ihram, ni sunna kunyoa nywele za makwapani na sehemu nyingine za mwili, kupunguza nywele za kichwani, kunyoa ndevu na kukata kucha. Kisha ni sunnah kukoga, kutawadha na kupaka manukato ndipo uvalie Ihram. Ni vyema kuvaa Ihram wakati wa swala mojawapo ya faradhi. Mtume (s.a.w) katika Hija ya kuaga alivaa Ihram wakati wa swala ya Adhuhuri.

Kabla ya kutia nia ya aina ya Hija au 'Umra, Haji ataswali rakaa mbili za sunnah, kisha mara tu baada ya kutoa salaam atanuia aina ya Hija anayokusudia kuifanya, na ataitikia wito wa Allah (s.w) kulingana na nia yake.Kama nia yake ni ya kufanya 'Umra (At-Tamattu) ataitika:

اللّٰهُمَّ لَبَّيْكَ الْعُمْرَةَ

*Ee Allah nakutikia kwa 'Umra.*

***Allahumma labbaikal 'Umrata***

Kama nia yake ni ya kufanya Hija na 'Umra (Al-Qiran) ataitika:

اللّٰهُمَّ لَبَّيْكَ الْحجَّ وَعُمْرَةَ

*Ee Mola. Naitika kwa Hija na 'Umra.*

***Allahumma labbaikal hajji wa Umrata***

Kama nia yake ni ya kufanya Hija tu (Al-Ifraad) ataitikia:

اللّٰهُمَّ لَبَّيْكَ الْحجَّ

*Ee Mola, Naitika kwa Hija*

***Allahumma labbaikal hajji***

**2. Talbiya**

Talbiya ni maneno ya kuitikia wito wa Allah (s.w) pale alipomuamrisha Nabii Ibrahim (a.s) kuwaita watu kwa Hija:

وَأَذِّن فِى ٱلنَّاسِ بِٱلْحَجِّ يَأْتُوكَ رِجَالًا وَعَلَىٰ كُلِّ ضَامِرٍ يَأْتِينَ مِن كُلِّ فَجٍّ عَمِيقٍ ﴿٢٧﴾ لِّيَشْهَدُوا۟ مَنَـٰفِعَ لَهُمْ وَيَذْكُرُوا۟ ٱسْمَ ٱللَّهِ فِىٓ أَيَّامٍ مَّعْلُومَـٰتٍ

*"Na (tukamwambia Ibrahim): Utangaze kwa watu habari za Hija, watakujia*

*(wengine) kwa miguu na (wengine) juu ya kila mnyama aliyokonda (kwa uchovu wa safari ndefu). Ili washuhudie manufaa yao na kulitaja jina la Mwenyezi Mungu katika siku zinazojulikana ...” (22:27-28).*

Maneno ya kuitikia wito huu wa Allah, yaani maneno ya Talbiya, kama yalivyo katika hadith iliyosimuliwa na Abdullah bin Umar (r.a) ni haya yafuatayo:

لَبَّيْكَ اللَّهُمَّ لَبَّيْكَ، لَبَّيْكَ لاَ شَرِيكَ لَكَ لَبَّيْكَ، إِنَّ الْحَمْدَ وَالنِّعْمَةَ لَكَ وَالْمُلْكَ، لاَ شَرِيكَ لَكَ.

***“Labbayka Allaahumma labbayka. Labbayka laashariika laka labbayka. Innal-hamda wanni-i-mata laka wal-mulku; laashariika laka”.***

**Tafsiri:**

*“Naitika wito wako Ee Allah, Naitika. Naitika, Ewe Usiye na mshirika, Naitika. Hakika sifa zote njema na neema zote ni zako na Ufalme ni Wako, Ewe Usiye na mshirika (Bukhari na Muslim).*

Wanaume wataitika kwa sauti ya juu na wanawake wataitika kwa sauti ndogo. Kwa wale walionuia kwa Hija tu au Hija na ‘Umra, Talbiya huanza mara baada ya kuvaa Ihram na kunuia, mpaka watakapotupa jiwe la kwanza katika mnara mkubwa -”*Jamaratul’ Aqaba*” siku ya mwezi 10 Dhul-Hija.

Talbiya ya ‘Umra huanzia kwenye Miiqaat baada ya kuvaa Ihram na kutia nia ya ‘Umra mpaka kwenye Nyumba Takatifu ya Ka’aba. Kwa wale walionuia Hija ya “Tamattu”, wataanza Talbiya tena baada ya kuvalia Ihram kwa nia ya Hija siku ya mwezi 8 Dhul-Hija, na wataendelea mpaka wakati watakapoanza kutupa jiwe la kwanza kulenga mnara mkubwa siku ya mwezi 10 Dhul-Hija.

Wakati wa kwenda Makka Talbiya itarudiwa tena na tena. Isomwe kila baada ya swala ya faradh, kila Haji au Hajjat anapopanda na kuteremka katika kipando au chombo anachosafiria, kila akipanda na akiteremka mlima na kila anapokutana na msafara mwingine.Mtume (s.a.w) alifanya hivyo pamoja na maswahaba wake alioongozana nao katika Hija ya kuaga. Kila alipotaka Waislamu wasome talbiya aliwaamrisha kwa kusema “**Takbiir**”.Kisha Masahaba wake na yeye mwenyewe walianza kusoma Talbiya kwa nguvu.

## 3. Tawaf

Kutufu ni kitendo cha kuizunguka Ka'aba mara saba kuanzia kwenye Jiwe Jeusi (Hajaratil-aswad). Wakati wa kuzunguka Ka'aba inakuwa upande wa kushoto, yaani mzunguko ni kinyume na ule wa saa (anti-clockwise). Kutufu ndio Ibadah ya kwanza anayoifanya mwenye kuhiji au kufanya 'Umra mara tu baada ya kuizuru Ka'aba na kubusu Jiwe Jeusi.

### Masharti ya Tawaf

Mwenye kutufu hana budi kuwa twahara. Yaani awe ameepukana na najisi na aina zote za hadath - asiwe na janaba, hedhi wala nifasi na awe na udhu.

Kwa wanawake wenye hedhi wanaruhusiwa kuingia katika Ihram na kufanya vitendo vyote vya Hija isipokuwa kutufu kama tunavyofahamishwa katika hadith ifuatavyo:

> *Amesimulia Aisha (r.a): Nilikuwa katika hedhi nilipoingia Makka, kwa hiyo sikuweza kutufu wala kusali. Kisha nilimfahamisha Mtume wa Allah, akaniambia, 'fanya vitendo vyote vya Hija kama wengine lakini usitufu mpaka uwe twahara.: (Bukhari).*

### Namna ya Kutufu

Kama kawaida ya kila ibada, mwenye kutufu atatia nia ya kutufu na ataanza tawafu kwa kulibusu Jiwe Jeusi kisha atasema: "*Bismillaah Allaahu Akbar*". Kama, kutokana na msongamano wa watu haitawezekana kulibusu ***"Jiwe Jeusi"***, basi inatosha kwa kuligusa kwa mkono au kwa fimbo kisha kuubusu mkono au fimbo na kusema: "*Bismillaah Allahu Akbar*". Kama vile vile itashindikana kuligusa jiwe jeusi kwa mkono au kwa fimbo, basi itatosha kuashiria kwa mbali kwa mkono au fimbo bila kubusu mkono au fimbo hiyo, kisha utasema: *"Bismillaah Allaahu Akbar"*. Hivi sasa kuna alama ya mstari mweupe uliochorwa ili kuwawezesha wale wanaozunguka mbali na ***Jiwe Jeusi*** kujua kuwa wamefika usawa na Jiwe Jeusi ili waashirie (*Angalia kielelezo A na B uk. 297-8*).

Wakati wa kuzunguka Ka'aba itakuwa upande wa kushoto na kuzunguka karibu na kuta za Ka'aba ni bora zaidi iwapo kuna uwezekano. Pembe nne za Ka'aba zimepewa majina. Pembe ya Mashariki ni hii yenye "Jiwe Jeusi" inaitwa Ar-Ruknul-aswad, ambapo mzunguko huanza baada ya kulibusu Jiwe Jeusi. Pembe inayofuatia wakati wa kuzunguka huitwa Ruknul-Iraaq, hii ni pembe ya Kaskazini, inayofuatia hii ni Ruknu-Sham, hii ni pembe ya Magharibi na inayofuatia ni Ruknul-Yaman, hii ni pembe



Kielelezo: A. Picha ya Ka'aba

ya kusini, kisha mzunguko hukamilika kwa kurejea tena kwenye pembe ya "Jiwe Jeusi." Pamoja na kumkumbuka Allah (s.w) na kumtaja wakati wote wa kutufu, bado mwenye kutufu anaruhusiwa kuongea itakapotokea haja ya kufanya hivyo kama tunavyojifunza katika Hadith ifuatayo:



*Ibn Abbas (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: "Kutufu katika Nyumba (Tukufu) ni kama mtu aliyeko kwenye swala isipokuwa mtu anaweza kuongea wakati wa kutufu. Kwa hiyo yeyote atakayeongea katika Tawaf hana budi kuongea maneno mazuri." (Tirmidh, Nisai, Darimi).*




kielelezo: B. Eneo la Ka'aba

Kwa wanaume ni sunnah kukimbia matiti (jogging or trotting) katika safari tatu za mwanzo, na kisha kumalizia safari nne zilizobakia kwa kutembea kawaida. Wanawake watatembea kama kawaida kwa mizunguko yote saba.Baada ya mzunguko wa saba, Haji au Hajjat ataendelea mbele mpaka pale aliposimama Nabii Ibrahim (a.s) wakati akiinua kuta za Ka'aba. Sehemu hii inaitwa "Maqamu Ibrahim" ambapo alama ya unyayo wa Nabii Ibrahim (a.s) huonekana. Katika Qur'an tunakumbushwa juu ya alama hii.

إِنَّ أَوَّلَ بَيْتٍ وُضِعَ لِلنَّاسِ لَلَّذِي بِبَكَّةَ مُبَارَكًا وَهُدًى لِّلْعَالَمِينَ ﴿٩٦﴾ فِيهِ
آيَاتٌ بَيِّنَاتٌ مَّقَامُ إِبْرَاهِيمَ ۖ • • • ﴿٩٧﴾

*Kwa yakini Nyumba ya kwanza iliyowekwa kwa ajili ya watu ni ile iliyoko Makka, yenye baraka na uwongozi kwa ajili ya walimwengu wote. Humo mna ishara zilizo wazi (za kuonyesha utukufu wake na ukongwe wake. Miongoni mwa hizo ni) mahali alipokuwa akisimama Ibrahim, ..." (3:96-97).*

Haji atakapofika "Maqamu Ibrahim" ataswali rakaa mbili kwa kutekeleza amri ya Allah (s.w).

وَإِذْ جَعَلْنَا الْبَيْتَ مَثَابَةً لِّلنَّاسِ وَأَمْنًا وَاتَّخِذُوا مِن مَّقَامِ إِبْرَاهِيمَ مُصَلًّى ۖ

*"... Na mahali alipokuwa akisimama Ibrahim pafanyeni pawe pa kuswalia ..." (2:125).*

Mtume (s.a.w) katika Hija ya kuaga alipofika hapa Maqamu Ibrahim alisoma kipande hiki cha aya kisha aliswali rakaa mbili. Katika rakaa ya kwanza alisoma: Suratul Kaafiruun na katika rakaa ya pili alisoma Suratul Ikhlas.

Kama kutokana na msongamano wa watu hapatakuwa na uwezekano wa kuswali karibu na sehemu hii, basi Hajj au Hajjat ataswalia sehemu yoyote katika usawa wa eneo hili la Maqamu Ibrahim.

### Tawaf ya Mgonjwa au Mkongwe

Mgonjwa au mkongwe asiyeweza kutembea mwenyewe anaruhusiwa kutufu juu ya kipando kama vile mnyama au anaweza kubebwa katika machela au juu ya gari la kusukuma. Mtume (s.a.w) aliwahi kutufu juu ya mnyama alipokuwa ameumia mguu kama tunavyofahamishwa katika Hadithi ifuatayo:

*Amesimulia Ibn Abbas (r.a) kuwa Mtume wa Allah alitufu akiwa juu ya ngamia (wakati huo Mtume (s.a.w) alikuwa ameumia). Kila alipofika kwenye pembe ya Jiwe Jeusi aliiashiria kwa kitu mkononi mwake na kusema: "Allaahu Akbar" (Bukhari).*

Vile vile katika Hadith ifuatayo tunafahamishwa kuwa mtu anaweza kutufu akiwa amebebwa mgongoni:

*Amesimulia Ummu Salama (r.a): "Nilimfahamisha Mtume wa Allah juu ya maradhi yangu". Alisema: "Tufu ukiwa umepanda juu ya migongo ya watu (ukiwa umebebwa) ..." (Bukhari).*

### Hukumu ya aliyekatisha Tawafu

Je, mtu akitokewa na dharura ikabidi akatishe tawafu kabla ya kumaliza mara zote saba, itabidi akirudi aanze upya? Kwa mfano mtu anaweza kutenguka udhu katikati ya tawafu ikabidi akatishe tawafu ili akatie udhu ndio arejee tena kutufu.Au, panaweza kukimiwa kwa swala ya faradh ikabidi akatishe tawafu ili ajiunge na jamaa kwa swala. Je, itabidi kuanza tawaf upya atakaporudi baada ya kutia udhu au baada ya kumaliza kuswali swala ya jamaa? Jibu la swali hili linajibiwa na Hadith ifuatayo:

*'Atta (r.a) amesema: "Kama mtu anatufu na pakakimiwa kwa ajili ya swala na swala ikaanza au kusukumwa na kutolewa nje ya sehemu" alimokuwa, hana budi kurudi na kuanzia pale alipoachia (na kumalizia safari zilizobakia)".*

Hadithi hii pia imesimuliwa na Ibn Umar (r.a) na Abdur-Rahman

bin Abuu Bakr (Bukhari).

## Aina za Tawaf

### (i) Tawaful-Quduum

Tawaf hii ni ile inayofanywa mara tu baada ya kuingia Makka kwa 'Umra au kwa Hija. Katika tawaf hii Haji (mwanamume) atafunika bega lake la kushoto na kuacha wazi bega la kulia. Kitendo hiki kinaitwa "Iztibaa." Pia katika tawaf hii wanaume watakwenda matiti katika mizunguko mitatu ya kwanza. Kitendo hiki cha kukimbia matiti kinaitwa "Ramal". Mizunguko minne iliyobakia itamaliziwa kwa kutembea kwa hatua fupi za kawaida.

### (ii) Tawaful-Ifadha (Tawaf ya Nguzo)

Tawaf hii ni miongoni mwa matendo ya nguzo za Hija na hufanywa siku ya mwezi 10 Dhul-Hija baada ya kukamilisha ibada za Rami (kutupa mawe kwenye mnara mkubwa - *Jamaratul-Aqaba*), Nahar (kuchinja mnyama) na Halqa (kunyoa kichwa). *"Iztibaa" na "Ramal*" hazipo katika tawaf hii. Tawaf hii wakati mwingine inaitwa "*Tawafuz `Ziyaara*."

### (iii) Tawaful-Widaa

Tawaf hii ya kuaga hufanywa wakati Haji akiwa tayari kuondoka Makka kurejea makwao. Hiki ni kitendo cha mwisho cha ibada ya Hija.

## 4. Kusa'i

Kusai ni kitendo cha kutembea mara saba baina ya vilima viwili - Saffaa na Marwa vilivyo karibu na Ka'aba. Mtume (s.a.w) alipoukaribia mlima wa Saffaa, alisoma:

۞ إِنَّ ٱلصَّفَا وَٱلْمَرْوَةَ مِن شَعَآئِرِ ٱللَّهِ ۖ

*"Hakika Saffaa na Marwa ni katika alama za (kuwepo) Allah (s.w) ...." (2:158).*

Kisha Mtume (s.a.w) alipanda kilima cha Saffaa kiasi cha kuweza kuiona Ka'aba, akiwa ameielekea Ka'aba (Qibla) na akiwa ameinua mikono yake juu akasema:

لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللهُ واللهُ أَكْبَرُ

*Hapana mola ila Allah. Allah ni Mkubwa.*

Kisha Mtume (s.a.w) alisoma mara tatu:

● لا إله إلا الله وحده
لا شريك له له الملك
وله الحمد وهو على كل
شيء قدير لا إله إلا الله
وحده أنجز وعده ونصر
عبده وهزم الأحزاب
وحده

*"Hapana mola ila Allah. Allah ni mmoja asiye na mshirika. Yeye ndiye Mmiliki (Mfalme) wa kila kitu, sifa zote amestahiki Yeye na ni Muweza wa juu ya kila kitu. Hapana mola ila Allah pekee ambaye ni Mtekelezaji wa Ahadi Yake, ambaye aliwanusuru waja wake na kuwatoa maadui wake". (Abu Daud).*

Kisha baada ya kusoma hivi mara tatu Mtume (s.a.w) alishuka mlimani na kuelekea kilima cha pili - Marwa. Alipofika bondeni alikimbia matiti mpaka alipoanza kupandisha kilima cha Marwa ndio akatembea kama kawaida. Alipofika juu ya kilima cha Marwa kiasi cha kuweza kuiona Ka'aba alielekea huko na kurudia kusoma na kuleta dua kama ile aliyoileta katika kilima cha Saffa. Mtume (s.a.w) alikwenda baina ya Saffa na Marwa mara saba, akirudia Dhikiri au maneno hayo hapo juu kila alipofika katika kila kilima. Alimalizia safari yake ya saba katika kilima cha Marwa.

Wale wanaofanya aina ya Hijja ya "at-Tamattu" au walionuia kufanya Umra tu, wakimaliza safari ya saba hupunguza nywele (au kuchopoa nywele kidogo) na kuvua Ihram au huwa huru na masharti ya Ihram. Ama wale walionuia Hijja tu (Al-Ifraad) au Hijja na Umra (al-Qiran) wataendelea kubakia na Ihram zao na kuendelea na Talbiya mpaka mwezi 10 Dhul Hija baada ya kutupa mawe kwenye mnara mkubwa.Na hapa ndipo unapoonekana urahisi wa Hija ya aina ya at-Tamattu.Mtume (s.a.w) aliwaamuru wale wote ambao hawakuja na wanyama wavue Ihram mpaka mwezi 8 Dhul-Hija wakati ibada ya Hija itakapoanza rasmi, ndio wavae tena Ihram na kuanza talbiya. Katika hadith ifuatayo tunafahamishwa:

*Mtume (s.a.w) alipofika al-Marwa kwa mara ya mwisho, alitangaza: "Kama ningelijua kabla, kama nilivyo kuja jua baadaye kuhusu dini yangu, nisingalikuja na wanyama wa muhanga (Haady) na nikafanya Umra tu. Kwa hiyo yeyote yule miongoni mwenu ambaye hakuja na mnyama anaweza kuvua Ihram na kuifanya hii Umra (Ambayo huisha baada ya Sai.)" Suraqa bin Jushum (r.a) aliinuka na akauliza: "Ee Mtume wa Allah, hii ni kwa mwaka huu tu au ni kwa nyakati zote"? Mtume wa Allah*

*alifumbanisha vidole vyake na akasema: "Umra imeoanishwa na Hijja daima (muda wote) mpaka siku ya mwisho (Muslim).*

Baada ya Sai,Haji au Hajjat atakaa Makka mpaka siku ya Tarwiya - mwezi 8 Dhul-Hija.

### 5. Siku ya Tarwiyya

Mwezi 8 Dhul Hija imeitwa siku ya Tarwiyyah kwa sababu siku hii, Mahujaji wanaandaa mali kwa ajili ya safari ya siku zinazofuatia mpaka mwezi 13 Dhul-Hija. Siku ya mwezi 8 Dhul -Hija, wenye kuhiji Hija ya aina At-Tamattu, watavalia tena Ihram wakiwa hapo hapo Makka kwa nia ya Hija, na wataanza tena Talbiya na kujiunga na Mahujaji wenzi wao kwa safari ya Mina. Mtume (s.a.w) hakufanya Tawaf kabla ya kuondoka kwenda Mina. Muda wa kwenda Mina uwe ni kabla ya swala ya Adhuhuri. Mtume (s.a.w) aliswalia Mina swala ya Adhuhuri, Asr, Magharibi na Ishaa na aliswali kwa Qasr yaani kwa kuswali kwa rakaa mbili swala zote za rakaa nne kwa nyakati zake. Hapana shughuli maalum ya kufanya hapa Mina katika siku hii, bali Haji anatakiwa azidishe kuleta Talbiyyah na hasa kila swala ya faradhi. Mahujaji watalala Mina, wataswali swala ya Al-fajir humo humo, na baada ya jua kuchomoza wataanza safari ya kuelekea uwanja wa Arafa huku wakileta Talbiyyah.

### 6. Siku ya Arafa (mwezi 9, Dhul-Haji)

Arafa ni bonde lililozungukwa na vilima pande tatu. Kufika katika bonde hili siku ya 9 Dhul-Hija kabla ya jua kuchwa ni kitendo cha nguzo za Hija. Hatakuwa na Hija yule ambaye hatadiriki kufika katika uwanja huu angalau muda mfupi kabla kuchwa kwa jua. Ama kwa yule aliyezuiliwa njiani au aliyekuwa na kipingamizi cha msingi, akashindwa kufika Arafa kabla ya kuchwa jua la siku ya mwezi 9 Dhul-Hija, basi Hija yake itakamilika iwapo atadiriki kufika katika uwanja wa Arafa kabla ya alfajir ya siku ya kuchinja - mwezi 10 Dhul-Hija kwa ushahidi wa Hadith ifuatayo:

*Mtume (s.a.w) amesema: "Yeyote aliyediriki swala yetu hii - swala ya Al-fajir ya siku ya kuchinja - na akawa nasi mpaka tukachinja na akawa amesimama Arafa, mchana au usiku, amekamilisha Hija yake".*

Pia Mtume (s.a.w) amesema:

*Hapana Hija bila ya Arafa. Yule atakaye kuja kwenye siku ya al-Jam (siku ya kulala Muz-dalifa), kabla ya Al-fajri ya siku ya kuchinja, atakuwa amekamilisha matendo muhimu ya Hija.*

Amri ya kusimama Arafa imebainishwa katika Qur-an katika aya ifuatayo:

ثُمَّ أَفِيضُوا۟ مِنْ حَيْثُ أَفَاضَ ٱلنَّاسُ وَٱسْتَغْفِرُوا۟ ٱللَّهَ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ

*Kisha miminikeni kutoka mahali wamiminikapo watu wote, (napo ni Arafaat) na ombeni samahani kwa Mwenyezi Mungu, Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe na Mwingi wa kurehemu" (2:199).*

Shughuli kubwa ya kufanya katika uwanja wa Arafa ni kumkumbuka Allah (s.w) na kukumbuka siku ya kukutana naye siku ya Kiyama. Jua lilipopinduka, yaani ilipoingia Adhuhuri, Mtume (s.a.w) alitoa khutuba iliyofafanua na kuwakumbusha Waislamu mambo mbali mbali katika hukumu za Kiislamu. Khutuba hii haikuwa na kikao cha katikati kama khutuba za Ijumaa na Idd. Baada ya khutuba, Bilal (r.a) aliadhini kwa ajili ya swala. Mtume (s.a.w) aliongoza swala na akaswali Adhuhuri pamoja na Al-asr kwa rakaa mbili mbili. Baada ya rakaa mbili za Adhuhuri, Mtume (s.a.w) alitoa salamu na hapo hapo Bilal alisimama na kutoa Iqama kwa swala ya al-Asr. Baada ya swala Mtume (s.a.w) alisimama katika kitako cha mlima uitwao "Jabalur-Rahman" (Mlima wa Rehma), akiwa ameelekea Qibla aliinua mikono yake mpaka kwenye usawa wa kifua kuomba dua (mbali mbali) kwa unyenyekevu kamili mpaka kuchwa kwa jua. Akasema Mtume (s.a.w), kuwa kuomba dua ni kitendo cha msingi katika siku ya Arafa. Tunajifunza katika Hadith ifuatayo:

*Amr bin Shuayb(r.a) amesimulia kutoka kwa baba yake, naye aliyepokea kutoka kwa babu yake kuwa Mtume (s.a.w) amesema: "Dua iliyo bora kuliko zote ni dua iliyoombwa siku ya Arafa, na maneno yaliyo bora zaidi niliyosema na waliyosema Mitume wengine kabla yangu ni :-*

● لَا إِلٰهَ إِلَّا اللهُ وَحْدَهُ
لَا شَرِيكَ لَهُ لَهُ الْمُلْكُ
وَلَهُ الْحَمْدُ وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ
شَيْءٍ قَدِيرٌ

*"Hapana Mola ila Allah, aliye Mmoja siye na Mshirika. Yeye ni Mfalme na Msifiwa pekee na Yeye ni Muweza juu ya kila kitu". (Tirmidh, Malik).*

## 7. Kulala Muzdalifa

Muzdalifa ni kitongoji kilichoko kati ya Arafa na Mina. Baada ya jua kuchwa Mtume (s.a.w) na Waislamu waliongozana nao katika Hija ya kuaga, waliondoka Arafa na kuelekea Muzdalifa kwa kufuata njia tofauti na ile waliyoijia kutoka Mina.

Wakati wa kwenda Muzdalifa, Mtume (s.a.w) amewaamrisha Waislamu waende kimya kimya katika mwendo wa utulivu bila ya makelele na vishindo.Mtume (s.a.w) na Waislamu alioongozana nao waliswali al-Magharibi pamoja na al-Ishai kwa Qasr walipofika Muzdalifa. Mtume (s.a.w) na Waislamu walilala Muzdalifa mpaka Alfajir, bali Mtume (s.a.w) aliwaruhusu watu dhaifu pamoja na wanawake na watoto waondoke kwenda Mina usiku wa manane baada ya mwezi kutua ili waende pole pole na kuepukana na msongamano wa watu wakati wa kutupa mawe. Lakini aliwaamuru wasianze kutupa mawe mpaka jua lichomoze. Baada ya swala ya Al-fajir, Mtume (s.a.w) alipanda ngamia na kuelekea sehemu takatifu iitwayo "*Mash-arul-Haram*". Ilivyo ni kwamba bonde lote la Muzdalifa linaitwa kwa jina hili lakini sehemu hasa ambayo Mtume (s.a.w) alisimama katika hija ya Kuaga ni pale ulipo Msikiti wa Muzdalifa hivi sasa. Mtume (s.a.w) alipofika hapa "Mash-arul Haram" alielekea Qibla, akatoa Takbira na kumuomba Allah (s.w).Haya ndio maagizo ya Allah (s.w) kama tunavyosoma:

... فَإِذَآ أَفَضْتُم مِّنْ عَرَفَـٰتٍ فَٱذْكُرُوا۟ ٱللَّهَ عِندَ ٱلْمَشْعَرِ
ٱلْحَرَامِ ۖ وَٱذْكُرُوهُ كَمَا هَدَىٰكُمْ وَإِن كُنتُم مِّن قَبْلِهِۦ لَمِنَ ٱلضَّآلِّينَ ﴿١٩٨﴾

*".Na mtakaporudi kutoka Arafaat mtajeni Mwenyezi Mungu kwenye Mash-arul Haram. Namkumbukeni kama alivyokuongozeni. Na hakika zamani mlikuwa miongoni mwa waliopotea" (2:198).*

Jambo muhimu la kukumbuka ni kwamba si lazima kila Haji asimame sehemu ya Msikiti, bali sehemu yoyote atakayosimama wakati huu wa kumtukuza Allah (s.w) kwa Takbira na kuomba dua, itafaa ili mradi tu aelekee Qibla. Kwani kama tulivyoona katika hadith, Mtume (s.a.w) amesema:

*"Ninasimama hapa lakini bonde lote la Muz-dalifa ni mahali pakukaa na kusimama" (Muslim).*

Baada ya jua kuchomoza, Mtume (s.a.w) na mahujaji wengine walianza safari ya kuelelekea Mina. Walipofika kwenye bonde la Muhassir (mahali walipouawa watu wenye jeshi la tembo), Mtume (s.a.w) aliwaamuru watu wapite haraka haraka. Wakati wakielekea Mina Mtume (s.a.w) alimtuma Fadhl bin Abbas (r.a) amuokotee vijiwe saba na akawaamuru watu wengine waokote vijiwe saba. Mahali popote pale njiani kuelekea Mina isipokuwa kwenye bonde la Muhassir mtu anaweza kuokota vijiwe saba kwa ajili ya ibada ya kutupa mawe kwenye mnara mkubwa (Jamaratul Aqaba). Mtume (s.a.w) alikuwa akiitikia Labbayka (Talbiya) kuanzia Muzdalifa mpaka alipofika Mina na kuanza kutupa jiwe la kwanza kwenye mnara mkubwa kama tunavyojifunza katika hadith ifuatayo:

> *Amesimulia Ibn Abbas (r.a): Mtume (s.a.w) alimpandisha Al-Fadhl katika kipando chake na akawa nyuma yake, na Fadhl ameeleza kuwa Mtume (s.a.w) aliendelea mfululizo kuleta Talbiya mpaka alipofanya Ramy katika Jamrat (Jamratul Aqaba). (Bukhari).*

## 8. Siku ya Kuchinja (10 Dhul-Hija)

Mwezi 10 Dhul-Hija, siku ya kuchinja na siku ya Idd ni siku yenye shughuli nyingi kwa mwenye kuhiji. Siku hii Haji analazimika kutekeleza matendo manne ya nguzo za Hija kwa utaratibu ufuatao:

(i) Kutupa mawe kwenye Mnara Mkubwa - Jamaratul Aqaba
(ii) Kuchinja mnyama kwa wenye kuhiji Hija za Al-tamatta na Al-Qiran.
(iii) Kunyoa kichwa
(iv) Kutufu tawaful ifadha (Tawaf ya nguzo).

Huu ndio utaratibu alioufuata Mtume (s.a.w) katika Hijja ya kuaga, lakini endapo kwa sababu moja au nyingine Haji hakuweza kufuata utaratibu huu, hapatakuwa na ubaya wowote. Kwa mujibu wa Hadith kadhaa jambo muhimu ni kutekeleza vitendo vyote vinne katika siku hiyo hiyo ya 10 Dhul Hija.

## 9. Siku za Tashriq (Ayyamut Tashriq)

Siku za Tashriq ni siku za mwezi 11, 12 na 13 Dhul Hija. Katika siku hizi Hajj hubakia Mina kwa madhumunni ya kumkumbuka na kumtukuza sana Allah (s.w) na kutupa mawe kwa kulenga minara yote mitatu - Mnara wa kwanza, Mnara wa kati na Mnara Mkubwa. Kila mnara hulengwa vijiwe saba kwa kila siku. Haji akitupa kila kijiwe husema: ALLAHU AKBAR. kipindi kinachojuzu kutupa mawe ni baada ya kuingia Adhuhur mpaka kuchwa jua.

۞وَٱذۡكُرُواْ ٱللَّهَ فِيٓ أَيَّامٖ مَّعۡدُودَٰتٖۚ فَمَن تَعَجَّلَ فِي يَوۡمَيۡنِ فَلَآ إِثۡمَ عَلَيۡهِ وَمَن تَأَخَّرَ فَلَآ إِثۡمَ عَلَيۡهِۖ لِمَنِ ٱتَّقَىٰۗ وَٱتَّقُواْ ٱللَّهَ وَٱعۡلَمُوٓاْ أَنَّكُمۡ إِلَيۡهِ تُحۡشَرُونَ ٢٠٣

*Na mtajeni Mwenyezi Mungu katika zile ziku zinazohisabiwa. Lakini afanyaye haraka katika siku mbili (akarejea) basi si dhambi juu yake, na mwenye kukawia pia si dhambi juu yake kwa mwenye kumcha Mwenyezi Mungu. Na mcheni Mwenyezi Mungu na jueni kwamba nyinyi mtakusanywa kwake. (2:203).*

Katika aya hii tunajifunza kuwa endapo Haji atakuwa na haraka ya kurejea nyumbani basi anaruhusiwa kuondoka siku moja kabla, yaani anaweza kuondoka mwezi 12 Dhul Hija baada ya kulenga mawe katika minara mitatu.

Khutuba katika siku za Tashriq ni jambo muhimu. Mtume (s.a.w) katika siku hizi za Tashriq alitoa khutuba za kuwakumbusha Waislamu mambo mbali mbali ya msingi juu ya Uislamu.

## 10 Tawaful Widaa (Tawaf ya Kuaga)

Baada ya Haji kukaa Mina siku tatu za Tashriq au siku mbili kama atakuwa na haraka ya kuondoka, atarejea Makka na kufanya Tawaful Widaa (Tawafu ya Kuaga). Tawaf hii hufanywa baada ya Haji kuwa tayari kuondoka na ni tendo la wajibu lakini si nguzo. Tawaf hii kama ilivyokuwa Tawaful ifadha haina ***"Ramal"*** wala ***"Iztibaa"***. Baada ya Tawaf hii hapana Sai. Kwa wale waliofanya Hija ya aina ya Ifraad (walionuia Hijja tu), baada ya kurejea Makka kutoka Mina wanaweza kuvaa Ihram tena na kunuia 'Umra. Baada ya kufanya 'Umra ndio watafanya Tawaful Wadaa iwapo watakuwa tayari kuondoka.

Kama tunavyojifunza katika Hadith, wanawake wenye hedhi, iwapo watakuwa wamekamilisha matendo yote ya nguzo za Hija, wanaruhusiwa kuondoka bila ya kufanya Tawaful-Wadaa.

## Kubatilika kwa Hija

Hija itabatilika iwapo Haji ataacha kutekeleza moja wapo ya matendo yafuatayo:

(i) Ihram au nia ya Hija na kuwa katika hali ya Ihram ikiwa ni pamoja na vazi lake kwa wanaume na kuchunga masharti ya Ihram. Mtu akivunja masharti ya Ihram Hija haibatiliki lakini analazimika kufidia kwa kuchinja mnyama au kulisha maskini au kufunga. Ila kufanya tendo la ndoa ndani ya Ihram hubatilisha Hija kabisa.

(ii) Sa'i kati ya Safaa na Marwa.

(iii) Kuhudhuria katika uwanja wa Arafat siku ya mwezi 9 Dhul- Hija kati ya kuchomoza jua la mwezi 9 dhul-Hija na alfajir ya mwezi10 Dhul-Hija.

(iv) Tawaful Ifadha (Tawafu ya Nguzo).

## Lengo la Hija

Kama tulivyojifunza katika masomo yaliyopita, lengo la ujumla la kuamrishwa kusimamisha nguzo tano za Uislamu, Shahada, kusimamisha Swala, Kutoa Zaka, Kufunga Ramadhani na Kuhiji Makka - ni kumuandaa mja aweze kuishi kulingana na lengo la kuumbwa kwake na kuletwa hapa duniani. Lengo la kuumbwa mwanaadamu limebainishwa katika Qur-an kuwa ni kumwabudu Allah(s.w.) katika kila kipengele cha maisha yake (Rejea Qur'an 51:56).

Ibada ya Hijja ni kilele au ni Chuo Kikuu cha kukamilisha maandalizi ya kumfikisha Muumini katika lengo la kumuabudu Mwenyezi Mungu (s.w) katika kila kipengele cha maisha na kumuwezesha Muumini kuisimamisha dini ya Mwenyezi Mungu (s.w) kuwa juu ya dini zote.

### Namna Hija inavyomuandaa Muumini kuwa Khalifa wa Allah katika jamii

Katika sehemu hii tutaangalia falsafa ya kila kitendo cha Ibada ya Hija kuanzia maandalizi ya safari mpaka mwisho wa safari na kuonesha namna ya kila kitendo cha Hijja kinavyomuandaa mja kuwa mcha-Mungu aliyetayari kuipigania Dini ya Mwenyezi Mungu (s.w) kwa hali na mali.

## Maandalizi ya Safari ya Hija

Maandalizi ya Hija hayaanzii kwenye miezi ya Hija, bali huanzia mbali katika umri wa mtu. Tunafahamu kuwa utekelezaji wa Ibada ya Hija unahitaji kuwa na uwezo wa kifedha (kimali). Hivyo Muislamu wa kweli katika kuchuma na kutumia mali yake, hana budi kuzingatia suala la nguzo ya Zaka na nguzo ya Hija. Muislamu atakapoweka mbele yake wazo la kutoa Zaka na Kuhiji, daima atachunga mipaka ya Mwenyezi Mungu (s.w) katika kuchuma kwake, kwani anafahamu wazi kuwa mali

iliyochumwa kwa njia za haramu haifai kutolea Zaka au Kuhijia. Hebu tuzingatie hadithi ifuatayo:

> *Ibn Umar amesimulia kuwa Mtume (s.a.w) amesema: Swala haikubaliwi bila ya Twahara, wala Sadaqa haikubaliwi kama inatolewa kutokana na mali iliyochumwa kwa njia za haramu. (Muslim).*

Halikadhalika, kutokana na hadithi hii, Hija haitasihi endapo mtu atahiji kwa kutumia mali iliyopatikana kwa njia za haramu. Hivyo, fikra ya kuhiji, humzoesha Muumini kuchunga mipaka ya Mwenyezi Mungu katika uchumi.

Pia fikra ya Hija humzoesha Muumini kutumia mali yake kwenye mambo muhimu tu ili kumuwezesha kuweka akiba kwa ajili ya Hija. Yaani fikra ya kutekeleza nguzo hii, humuepusha na ubadhirifu au utumiaji bila ya haja na bila ya ratiba.

Mtu anayekusudia kuhiji azidishe kutenda wema. Ajizatiti katika kusimamisha swala tano, kutoa Zaka, kufunga Ramadhani, kuwahurumia wanyonge kwa kuwapa misaada wanayohitajia na kusuhubiana vizuri na watu wote kwa ujumla. Amuombe msamaha kila aliyemkosea na amsamehe kila aliyemkosea. Pia mwenye kunuia Hija anatakiwa ajitahidi kujiepusha na maovu na azidishe kuomba msamaha kwa Mwenyezi Mungu (s.w) kwa yote aliyokosea kwa kujua au kutojua na yaliyowazi au yaliyofichikana. Katika Qur-an Mwenyezi Mungu (s.w) anaagiza kwa wanaokusudia kuhiji:

... فَمَن فَرَضَ فِيهِنَّ ٱلْحَجَّ فَلَا رَفَثَ وَلَا فُسُوقَ وَلَا جِدَالَ فِى ٱلْحَجِّ ۗ وَمَا تَفْعَلُوا۟ مِنْ خَيْرٍ يَعْلَمْهُ ٱللَّهُ ۗ ... ﴿١٩٧﴾

> *"Na anayekusudia kufanya Hija katika miezi hiyo, basi asiseme maneno machafu, wala asifanye vitendo vichafu wala asibishane katika hiyo Hija. Na kheri yoyote mnayoifanya Mwenyezi Mungu anajua..." (2:197)*

Utaona mtu mwenye fikra ya kutekeleza ibada ya Hija daima atakuwa mwangalifu katika mwenendo wake wa kila siku. Atajitahidi kutekeleza maamrisho yote ya Mwenyezi Mungu (s.w) na kujiepusha na makatazo yake yote atajitahidi kuwatendea wema wanaadamu wenzake na kila mara atakuwa mwenye kujiandaa kuitika mwito wa Mola wake (Labbayka), kama vile mtu anayejiandaa kukutana na Mola wake kwa

kifo, muda mfupi ujao.

### Safari ya Hija

Mtu aliyeisafia nia yake kwa ajili ya Hija na kwa ajili tu ya kutaraji Radhi za Mola wake, hupata zoezi kubwa kutokana na safari ya Hija la kumfanya awe tayari kujitoa muhanga kwa mali yake, nafsi yake na wapenzi wake kwa ajili ya Mwenyezi Mungu (s.w).

Tujuavyo, gharama ya safari ya Hija, ikiwa ni pamoja na usafiri, matumizi ya chakula, malazi, mnyama wa kuchinja, na kadhalika ni kubwa sana. Kwa mfano mwaka 1420/1999 gharama za Hija kwa Tanzania kwa wastani ilikuwa Shs. 700, 000/-. Kwa tajiri kiasi hiki cha fedha kitaonekana si kikubwa sana, lakini ukizingatia kuwa hatarajii kupata malipo yoyote ya kidunia kutokana na fedha hiyo ila Radhi ya Mwenyezi Mungu (s.w) bado hali ya kujitoa muhanga inapatikana. Kwa mtu wa kawaida ambaye amepata gharama ya safari ya Hija kwa kulimbikiza kidogo kidogo kwa umri wake wote wa uchumi Tsh. 700,000/- ni kiasi kikubwa sana kwake ambacho humpa zoezi kubwa sana la kuwa tayari kutoa mali yake wakati wowote na kiasi chochote kwa ajili ya kuihuisha na kuisimamisha Dini ya Mwenyezi Mungu (s.w).

Mtu anapoaga kwenda Hija anakuwa tayari kwa moyo mkunjufu kuwaacha ahali zake, jamaa zake, rafiki zake na wapenzi wake wote ili akaitikie wito wa Mwenyezi Mungu (s.w). Kitendo hicho cha Haji kuwa tayari kuachana na wapenzi wake, kwa ajili ya safari ya Hija, humpa zoezi kubwa la kuwa tayari kumpenda Mwenyezi Mungu na Mtume wake kuliko chochote kingine. Hili ni zoezi muhimu sana kwa Muislamu kwani mtu hawezi kufuzu mbele ya Mwenyezi Mungu (s.w) mpaka kwanza aweze kumpenda Mwenyezi Mungu (s.w) na Mtume wake kuliko anavyoipenda nafsi yake na yoyote yule aliyempenzi kwake na kuliko anavyokipenda chochote kile chenye thamani kwake. Hebu tuzingatie usia wa Mwenyezi Mungu (s.w) ufuata

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ لَا تَتَّخِذُوٓا۟ ءَابَآءَكُمْ وَإِخْوَٰنَكُمْ أَوْلِيَآءَ إِنِ ٱسْتَحَبُّوا۟
ٱلْكُفْرَ عَلَى ٱلْإِيمَٰنِ ۚ وَمَن يَتَوَلَّهُم مِّنكُمْ فَأُو۟لَٰٓئِكَ هُمُ ٱلظَّٰلِمُونَ ﴿٢٣﴾ قُلْ
إِن كَانَ ءَابَآؤُكُمْ وَأَبْنَآؤُكُمْ وَإِخْوَٰنُكُمْ وَأَزْوَٰجُكُمْ وَعَشِيرَتُكُمْ وَأَمْوَٰلٌ

ٱقْتَرَفْتُمُوهَا وَتِجَٰرَةٌ تَخْشَوْنَ كَسَادَهَا وَمَسَٰكِنُ تَرْضَوْنَهَآ أَحَبَّ

إِلَيْكُم مِّنَ ٱللَّهِ وَرَسُولِهِۦ وَجِهَادٍ فِى سَبِيلِهِۦ

فَتَرَبَّصُوا۟ حَتَّىٰ يَأْتِىَ ٱللَّهُ بِأَمْرِهِۦ ۗ وَٱللَّهُ لَا يَهْدِى ٱلْقَوْمَ ٱلْفَٰسِقِينَ ﴿٢٤﴾

*Enyi mlioamini! Msiwafanye baba zenu na ndugu zenu kuwa vipenzi vyenu ikiwa wanastahabu (wanapenda) ukafiri kuliko Uislamu. Na katika nyinyi atakayewafanya hao kuwa ndio vipenzi vyake, basi hao ndio madhalimu (wa nafsi zao). Sema: Kama baba zenu na wana wenu na ndugu zenu na wake zenu na mali mlizochuma na biashara mnazoogopa kuharibikiwa, na majumba mnayoyapenda, (ikiwa vitu hivi) ni vipenzi zaidi kwenu kuliko Mwenyezi Mungu na Mtume wake na kupigania dini yake, basi ngojeni mpaka Mwenyezi Mungu alete amri yake; na Mwenyezi Mungu hawaongozi watu maasi. (9:23-24)*

Kwa wastani safari ya Hija ni ngumu sana kwa watu wa kawaida (wasio wakuu wa Dola wanaopata mapokezi ya serikali ya Kifalme). Ugumu wa safari ya Hija unapatikana katika safari yenyewe, mabadiliko ya hali ya hewa, mkusanyiko wa watu wengi sana (milioni moja na zaidi) kwa wakati mmoja katika sehemu ndogo takatifu, msongamano katika kutekeleza baadhi ya nguzo za Hija kama vile kutufu, kusai na kutupa mawe katika minara mitatu. Kila mwaka watu hufa katika minara mitatu. Kila mwaka watu hufa katika sehemu hizi za msongamano. Ukimuuliza mtu yeyote wa kawaida aliyewahi kuhiji atakuhadithia zaidi juu ya uzito wa safari ya Hija. Ugumu huu wa safari ya Hija humpa Muislamu mazoezi ya kuitoa nafsi yake muhanga kwa kuwa yu tayari kukabiliana na magumu yote, hata ikibidi kufa kwa ajili ya kutekeleza amri ya Mwenyezi Mungu (s.w). Kwa maana nyingine safari ya Hija inatupa funzo la kuwa tayari kupigania dini ya Mwenyezi Mungu (s.w) kwa nafsi zenu. Mtume (s.a.w) amelinganisha safari ya Hija na Jihad:

*Aysha (r.a) amehadithia: "Niliuliza: "Ee Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.w)! Kunajihadi kwa wanawake?" "Ndio" alijibu Mtume, 'Kwao kuna jihadi isiyo ya kupigana' - Hajj na Umra'. (Ibn Majah).*

Katika hadithi nyingine iliyosimuliwa pia na Aysha (r.a) Mtume (s.a.w) amesema:

*"Jihad bora kwa (wanawake) ni Hajj Mabruur (Hajj yenye kukubaliwa)".*

*(Bukhari)*

Pia tunajifunza kutokana na Sunnah ya Mtume (s.a.w) kuwa Haji anayekufa katika vazi la Ihram, huzikwa na Ihram yake kama shahidi anavyozikwa na vazi lake la vita:

> *Ibn Abbas (r.a) ameeleza kuwa mtu mmoja akiwa katika vazi la Ihram (katika hali ya Ihram) alianguka juu ya ngamia, akavunjika shingo na akafa. Mtume (s.a.w) alipofahamishwa habari hii aliamuru: "Muosheni kwa maji yaliyochanganywa na karafuuu maiti (leaves of the lot tree) na mumkafini kwa vipande viwili vya Ihram na msimfunike kichwa chake kwani Mwenyezi Mungu (s.w) atamfufua siku ya Kiyama akitamka Talbiya (akiitika Labbaya...)".*

Katika hadithi nyingine, Hijja na Jihad vimelinganishwa kama ifuatavyo:

> *Amesimulia Abuu Hurairah (r.a) kuwa mtume (s.a.w) aliulizwa: Ni kitendo gani kilichobora kuliko vyote? Akajibu: "Kumuamini Mwenyezi Mungu (s.w) na Mtume wake". Akauliza tena: Ni amali gani inayofuatia kwa uzuri? Akasema: "Kufanya Jihad katika njia ya Mwenyezi Mungu (s.w)". Akaulizwa tena: Ni amali gani inayofuatia hii? Alijibu: "Kufanya Hija yenye kukubaliwa (Hajj Mabruur)". (Bukhari).*

Hadithi zote hizi zinatupa fundisho kuwa safari ya Hija inatoa mafunzo ya Jihad kwa waumini.

**Ihram**:

Tumejifunza kuwa Ihram ni vazi rasmi kwa ajili ya Hija na Umra na pia Ihram ni hali anayokuwa nayo mwenye kuhiji au kufanya Umra ambapo analazimika kuchunga mambo mbali mbali. Ihram kama vazi ni zoezi kubwa sana la kuwakumbusha waumini kwa vitendo juu ya usawa wa binaadamu. Bila shaka ubaguzi wowote, hali ya tajiri na maskini, mfalme na raia, afisa na mtumishi, mweusi na mweupe nakadhalika, wanaume wote huvalia vazi la aina moja ambalo ni shuka ya kufunga kiunoni na nyingine ya kuteremsha lubega, kuacha wazi kichwa na kuvalia makubazi (malapa) au viatu vya wazi (sandles) bila ya soksi. Wakati wote Mahujaji wanapokuwa katika vazi hili wanathibitisha kwa matendo ujumbe wa Mwenyezi Mungu (s.w) ufuatao:

*Enyi watu! Kwa hakika tumekuumbeni (nyote) kwa (yule) mwanamume*

يَٰٓأَيُّهَا ٱلنَّاسُ إِنَّا خَلَقْنَٰكُم مِّن ذَكَرٍ وَأُنثَىٰ وَجَعَلْنَٰكُمْ شُعُوبًا وَقَبَآئِلَ

لِتَعَارَفُوٓا۟ ۚ إِنَّ أَكْرَمَكُمْ عِندَ ٱللَّهِ أَتْقَىٰكُمْ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ عَلِيمٌ خَبِيرٌ ﴿١٣﴾

*(mmoja, Adam) na yule mwanamke (mmoja Hawwa). Na tumekufanyeni mataifa na makabila (mbali mbali) ili mjuane (tu basi, sio kubaguana). Hakika aheshimiwaye sana miongoni mwenu mbele ya Mwenyezi Mungu ni yule amchaye Mwenyezi Mungu zaidi katika nyinyi. Kwa yakini Mwenyezi Mungu ni Mjuzi, Mwenye habari (za mambo yote). (49:13)*

Katika kuchunga masharti mbali mbali anapokuwa katika hali ya Ihram Haji hupata mazoezi ya hali ya juu ya utii kwa Mwenyezi Mungu (s.w). Tumejifunza kuwa Hajj anapokuwa katika hali ya Ihram, Haji hukatazwa kufanya matendo ya kuchana nywele na kunyoa. Je, mtu aliyejizatiti katika kuchunga masharti haya madogo madogo kwa ajili ya Mwenyezi Mungu (s.w) kwa muda wote anapokuwa katika ihram, itakuwa vigumu kwake kujiepusha na makatazo yote ya Mwenyezi Mungu (s.w) katika kuendesha maisha yake ya kila siku baada ya Hija? Isitoshe Hajj, aweza kuvunja mojawapo ya masharti haya bila ya yoyote kumbaini lakini bado hafanyi hivyo. Ikitokea kwa bahati mbaya kavunja sharti mojawapo, bila ya kushitakiwa na mtu yoyote yeye mwenyewe hujihukumu na kujiadhibu kwa kutoa fidia (faini) kwa kuchinja mnyama na kutoa sadaqa au kwa kutoa chakula kuwalisha maskini au kufunga. Je, huoni kuwa kuchunga masharti ya ihram pia humzoesha Hajj kuwa muadilifu na mcha-Mungu mwenye kuchunga mipaka ya Mwenyezi Mungu (s.w) pasi na usimamizi wowote katika kuendesha maisha yake ya kila siku?

Kwa hiyo, tunajifunza kuwa, ambapo vazi la Ihram linampa Haji mazoezi ya kudumisha usawa kati ya wanaadamu na kukata mzizi wa ubaguzi wa aina yoyote na majivuno, uchungaji wa masharti ya ihram, unampa Haji zoezi la kumtii Mwenyezi Mungu (s.w) kwa uadilifu katika kuacha makatazo yake na kufuata maamrisho yake katika kuendesha maisha yake ya kila siku.

**Talbiya**

Talbiya ni kuitikia wito wa Mwenyezi Mungu (s.w) kwa maneno yafuatayo:

لَبَّيْكَ اللَّهُمَّ لَبَّيْكَ، لَبَّيْكَ لاَ شَرِيْكَ لَكَ لَبَّيْكَ، إِنَّ الْحَمْدَ وَالنِّعْمَةَ لَكَ وَالْمُلْكُ، لاَ شَرِيْكَ لَكَ.

***Labbayka Allaahumma Labbayka. Labbayka laashariika laka labbayka. Innal-hamda wanni-imata laka wal-mulku; laashariika laka.***

*"Naitika wito wako Ee Mwenyezi Mungu, Naitika. Naitika, ewe usiye na*

*Mshirika, Naitika. Hakika sifa zote njema na neema zote ni Zako na Ufalme ni wako, Ewe Usiye na mshirika." (Bukhari na Muslim).*

Kutekeleza nguzo ya Haji ni kuitika wito wa Mwenyezi Mungu (s.w) ambaye alimuamrisha Nabii Ibrahim (a.s), mwanzilishi wa Ibada ya Hija, kuwaita watu wote ulimwenguni waje kuhiji Makka katika nyumba takatifu, Al-Ka'aba. Mwito huu umedhihirishwa katika aya ifuatayo:

*"Na (Tukamwambia Ibrahim), utangaze kwa watu habari za Hijja,*

وَأَذِّن فِى ٱلنَّاسِ بِٱلْحَجِّ يَأْتُوكَ رِجَالًا وَعَلَىٰ كُلِّ ضَامِرٍ يَأْتِينَ مِن كُلِّ فَجٍّ

*watakujia (wengine) kwa miguu na (wengine) juu ya kila mnyama aliyekonda, wakija kutoka katika kila njia ya mbali. (22:27)*

عَمِيقٍ ﴿٢٧﴾

Talbiya, inampa haji zoezi la kumuitika Mwenyezi Mungu (s.w) katika maamrisho yake yote. Je, mtu anayejitoa muhanga kwa kumuitikia Mwenyezi Mungu (s.w) kwa kufunga safari nzito ya Hija, atashindwa baada ya kurejea nyumbani, kumuitikia Mwenyezi Mungu (s.w) katika miito mingine iliyo miepesi zaidi kama vile mwito wa kusimamisha swala tano, kutoa Zaka, kufunga Ramadhani na miito ya kiutekelezaji katika maisha ya kila siku.

Talbiya ambayo makundi kwa makundi ya Waislamu huitamka pamoja wakiwa na vazi la sare (Ihram) wakati wakiwa katika msafara wa kutekeleza Ibada ya Hija, huwahamasisha Waislamu na kuwakumbusha kuwa wao ni askari wa Mwenyezi Mungu (s.w) ambao ni tishio la maadui wa Mwenyezi Mungu ulimwenguni kote kutokana na umoja na mshikamano wao uliojengwa katika msingi thabiti ya kumuamini na kumwitikia Mwenyezi Mungu (s.w) pekee. Historia inatuthibitishia jinsi Waislamu walivyokuwa tishio kwa washirikina wakati Waislamu walipofunga safari ya Umra, mwaka wa 6 A.H. na kuzuiliwa kuingia Makka na Makuraysh waliojizatiti kwa vita. Bila ya silaha, Waislamu kwa umoja wao na uthabiti wao katika kumuitikia Mwenyezi Mungu (s.w) na Mtume wake walichukuwa ahadi mbele ya Mtume (s.a.w) kupambana na washirikina hawa kama tunavyojifunza katika aya ifuatayo:

*Hakika Mwenyezi Mungu amekuwa radhi na Waislamu walipofungamana*

۞ لَّقَدْ رَضِىَ ٱللَّهُ عَنِ ٱلْمُؤْمِنِينَ إِذْ يُبَايِعُونَكَ تَحْتَ ٱلشَّجَرَةِ فَعَلِمَ مَا فِى

قُلُوبِهِمْ فَأَنزَلَ ٱلسَّكِينَةَ عَلَيْهِمْ وَأَثَـٰبَهُمْ فَتْحًا قَرِيبًا ﴿١٨﴾

*nawe chini ya mti; na anajua yaliyomo nyoyoni mwao. Basi akateremsha utulivu juu yao, na akawapa kushinda kwa zama za karibu. (48:18).*

Washirikina wa Makka, pamoja na silaha zao, waliogopa kupigana na Waislamu ambao hawakuwa na silaha na badala yake wakawekeana mkataba wa amani - mkataba wa Hudaybiyyah. Miaka miwili baada ya Hudaybiyyah, mwaka wa 8 Hijiria. Waislamu elfu kumi waliiteka Makka kwa Tahalili na Takbir bila ya kutumia silaha. Umoja wa jeshi hili la Waislamu, uliodumishwa na kalima ya "*Laailaaha illallahu allaahu Akbar*" ulikuwa ni tishio kwa washirikina wa Makka ambao walijifungia ndani kwa khofu na kuwawezesha Waislamu kuikomboa Makka na Ka'aba kwa amani bila ya kumwaga hata tone la damu katika mji Mtakatifu.

**Tawaf**

Haji anapoingia Makka huendelea na Talbiya mpaka atakapofika kwenye Jiwe Jeusi na kulibusu au kuliashiria tayari kuanza tawaf. Tawaf ni ibada ya kuizunguka Ka'aba mara saba. Kila mzunguko huanza kwenye Jiwe Jeusi kwa kulibusu, au kuligusa kwa fimbo au kuliashiria. Jiwe Jeusi ndio jiwe la msingi la nyumba takatifu ya Al-Ka'aba.Kuna mafunzo mengi yanayopatikana katika tawaf.

**Kwanza**, kule kuishuhudia Ka'aba na mazingira yake, hasa sehemu ile iitwayo "Maqamu Ibrahim", mahali aliposimama Nabii Ibrahim wakati wa kuinua kuta za Ka'aba, humpelekea Haji kuwa na yakini zaidi juu ya kuwepo Mwenyezi Mungu (s.w). Kwa maana nyingine Muislamu aliyeitikia wito wa Hija kwa ajili ya Mwenyezi Mungu (s.w), kuwemo katika mazingira ya Ka'aba huzikurubisha fikra zake kwa Mwenyezi Mungu (s.w) kuliko anapokuwa katika sehemu nyingine yoyote katika ardhi. Mwenyezi Mungu (s.w) anabainisha hili katika Qur-an:

إِنَّ أَوَّلَ بَيْتٍ وُضِعَ لِلنَّاسِ لَلَّذِي بِبَكَّةَ مُبَارَكًا وَهُدًى لِّلْعَٰلَمِينَ ﴿٩٦﴾ فِيهِ
ءَايَٰتٌۢ بَيِّنَٰتٌ مَّقَامُ إِبْرَٰهِيمَ ۖ وَمَن دَخَلَهُۥ كَانَ ءَامِنًا ۗ ... ﴿٩٧﴾

*Ka yakini Nyumba ya kwanza iliyowekwa kwa ajili ya watu (kufanya ibada) ni ile iliyoko Makka, yenye baraka na uwongozi kwa ajili ya walimwengu wote. Humo mna ishara zilizo wazi (za kuonyesha utukufu wake na ukongwe wake. Miongoni mwa hizi ni) mahali alipokuwa akisimama Ibrahim, na anayekuwa katika sehemu hiyo huwa katika amani..." (3:96-97)*

**Pili**, kitendo cha kutufu, endapo kitafanywa kwa kumzingatia Mwenyezi Mungu (s.w) kwa undani kama mazingira yenyewe yanavyoruhusu, humpa Haji zoezi kubwa la kumdhukuru na kumtukuza Mwenyezi Mungu (s.w) katika kiwango cha juu kabisa kama kile cha Malaika. Tunafahamishwa katika Hadithi kuwa Ka'aba ni nakala halisi ya Baitil-Ma'amuur, nyumba tukufu ya Mwenyezi Mungu (s.w) iliyopo Mbinguni ambayo daima kuna makundi ya Malaika yanayomdhukuru Mwenyezi Mungu (s.w) mpaka siku ya Kiyama. Hivyo Mahujaji wakitufu kwa kumzingatia Mwenyezi Mungu (s.w) na wakasimama kwa swala katika Maqamu Ibrahim baada ya Tawaf, hufanya kitendo kile kile wanachokifanya Malaika katika mbingu ya saba.

**Tatu**, kitendo cha kubusu Jiwe Jeusi kila mutawaf anapoanza mzunguko, ni kitendo cha kuchukua ahadi upya kwa Mwenyezi Mungu (s.w) kuwa atamuabudu ipasavyo na hatamshirikisha na yeyote au chochote katika maisha yake yote. Kuhusu ahadi hii, imebainishwa katika hadithi iliyosimuliwa na ibn Abbas kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema: "Jiwe Jeusi ni mkono wa kuume wa Mwenyezi Mungu hapa ardhini, kwa mkono huo anapeana mkono waja wake, kama ambavyo mtu anavyopeana mkono ndugu yake.

**Nne**, Ibada ya Tawaf, ambayo Waislamu kutoka sehemu mbali mbali za dunia, wenye rangi na lugha tofauti huifanya kwa pamoja bega kwa bega, wanaume na wanawake, matajiri na masikini, wafalme na raia, weusi na weupe, wenye nguvu na dhaifu, bila ya ubaguzi wa aina yoyote, inatoa zoezi kubwa la kuwawezesha Waislamu kudumisha udugu na umoja wa Waislamu na usawa wa binaadamu.

Funzo hili la udugu, umoja na usawa linalopatikana katika ibada ya Tawaf, linadhihiri katika matendo mengine ya Hija ambapo Waislamu huyafanya kwa pamoja kama vile tendo la Sai, Kusimama Arafa na Kutupwa mawe katika Minara mitatu. Tunajifunza kutokana na matendo haya ya Hija kuwa, udugu, umoja na usawa halisi na wa kweli kati ya wanaadamu haupatikani mahali popote au kwa njia yoyote ila chini ya bendera ya "*Laailaaha illaallaahu Muhammaadar-rasuulullaah*" kwa kumuabudu Mwenyezi Mungu (s.w) ipasavyo kwa pamoja na kushirikiana bega kwa bega kusimamisha ufalme wake hapa ulimwenguni.

### Sa'i

Sai ni ibada ya kutembea mara saba kati ya vilima viwili - Safa na Marwa, vilivyo karibu na Ka'aba - ambapo kuna kukimbia matiti kwa wanaume katika sehemu ya bondeni.

Kitendo hiki cha Sai kinawawezesha Waislamu, Kumtii Mwenyezi Mungu (s.w) kwa kuwa tayari kutekeleza kila wanaloamrishwa.

**Pili**, kukimbia matiti (jogging) kunawapa Waislamu wanaume mazoezi na kuwakumbusha kuwa kupigana kwa uhodari na ushujaa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu (s.w) kumelazimishwa juu yao, kama kulivyolazimishwa juu yao kusimamisha swala, kutoa Zaka, kufunga Ramadhani na Kuhiji. Rejea Qur-an

كُتِبَ عَلَيْكُمُ ٱلْقِتَالُ وَهُوَ كُرْهٌ لَّكُمْ ۖ وَعَسَىٰٓ أَن تَكْرَهُوا۟ شَيْـًٔا
وَهُوَ خَيْرٌ لَّكُمْ ۖ وَعَسَىٰٓ أَن تُحِبُّوا۟ شَيْـًٔا وَهُوَ شَرٌّ لَّكُمْ ۗ وَٱللَّهُ يَعْلَمُ
وَأَنتُمْ لَا تَعْلَمُونَ ﴿٢١٦﴾

*Mmelazimishwa kupigana vita (kwa ajili ya dini ya Mwenyezi Mungu). Nalo ni jambo zito kwenu. Lakini huenda mkachukia kitu, nacho ni kheri kwenu. Na huenda mkapenda kitu nacho ni shari kwenu. Na Mwenyezi Mungu ndiye anayejua (lakini) nyinyi hamjui. (2:216)*

**Tatu**, ibada ya Sai inawazoesha Waislamu kuwa tayari kuhangaika kwa namna yeyote ile kwa ajili ya Mwenyezi Mungu (s.w). Ili tulipate funzo hili vizuri, ni vyema tujikumbushe historia ya nabii Ibrahim (a.s), mwanzilishi wa Hija. Nabii Ibrahim (a.s) kama historia yake inavyosimuliwa katika Qur-an (Rejea juzuu ya tatu), alipewa na Mola wake amri nyingi na nzito, ambazo, kutokana na utiifu wake wa hali ya juu kwa Mola wake, alizitekeleza zote kwa moyo mkunjufu. Miongoni mwa amri hii ni ile ya kumwacha mkewe Hajrah na mtoto wake mchanga (Ismail) ambaye alikuwa ni mtoto pekee aliyekuwa naye, katika bonde kavu la Makka lisilokaliwa na mkazi yeyote na bila ya kuwaachia chochote, isipokuwa ulinzi wa Mwenyezi Mungu (s.w). Tukio hili la Nabii Ibrahim (a.s) kuwaacha ahli zake Makka pasi na msaada wowote limerejewa katika Qur-an:

رَّبَّنَآ إِنِّىٓ أَسْكَنتُ مِن ذُرِّيَّتِى بِوَادٍ غَيْرِ ذِى زَرْعٍ عِندَ بَيْتِكَ ٱلْمُحَرَّمِ
رَبَّنَا لِيُقِيمُوا۟ ٱلصَّلَوٰةَ فَٱجْعَلْ أَفْـِٔدَةً مِّنَ ٱلنَّاسِ تَهْوِىٓ إِلَيْهِمْ وَٱرْزُقْهُم مِّنَ
ٱلثَّمَرَٰتِ لَعَلَّهُمْ يَشْكُرُونَ ﴿٣٧﴾

*“Mola wetu! Hakika mimi nimewaweka (nimewakalisha) baadhi ya kizazi changu (mwanangu Ismail na mama yake Hajrah) katika bonde (hili la Makka) lisilokuwa na mimea yoyote; katika nyumba yako takatifu (Al-Ka’aba). Mola wetu! Wajaalie wasimamishe swala. Na ujaalie nyoyo za watu zielekee kwao (wapende kuja kukaa hapa ili pawe mji) na uwaruzuku matunda ili wapate kukushukuru”. (14;37)*

Bibi Hajra aliyakinisha kuwa Nabii Ibrahim (a.s) hakuwaacha pale kwa kuwatupa tu ila ni katika kutekeleza amri ya Mwenyezi Mungu (s.w) alibakia pale na mtoto wake kwa ridhaa au kwa kauli ya Muumini: “*Nimesikia na Nimetii*”. Baada ya Nabii Ibrahim (a.s) kutoweka, bibi Hajra na mtoto wake, pamoja na upweke waliokuwa nao, walishikwa na kiu kali, lakini hapakuwa na dalili yoyote ya kupata maji katika eneo lile. Alimwacha mtoto wake karibu na Ka’aba na akakimbilia kwenye kilima cha Safa kuwa pengine atapata mpita njia (msafiri) amsaidie maji kwa ajili ya mtoto wake na yeye mwenyewe. Alipoona katika kilima cha Safa hakufanikiwa kumuona mpita njia yoyote, alikimbilia kwa shauku kilima cha pili cha Marwa, ambapo pia hakufanikiwa kumuona mtu yoyote. Aliendelea kukimbia huku na huko katikati ya vilima hivi viwili mara saba bila ya mafanikio yoyote. Katika kilele cha mahangaiko na mwisho wa jitihada za kibinaadamu Mwenyezi Mungu (s.w) alijaalia chem.-chem hii pamoja na kukidhi haja ya bibi Hajra na mtoto wake, aliwavutia watu kufanya makazi katika sehemu ile na ikawa ndio jibu la Dua aliyoiomba nabii Ibrahim (a.s) wakati alipowaacha pale. (Rejea Qur-an 14:37). Chem chem, hiyo ambayo inajulikana kwa jina la Zam-zam, haijakauka tangia wakati huo na mpaka siku ya mwisho.

Haji, endapo ataiweka mbele yake historia hii wakati wa kusai, atapata zoezi kubwa litakalomuwezesha kuwa tayari kujitoa muhanga kwa nafsi yake na kwa nafsi ya wapenzi wake kwa ajili ya Mwenyezi Mungu (s.w).

Funzo analolipata Haji, wakati wa kunywa maji ya Zam-zam, endapo atakumbuka historia ya chanzo chake, ni kwamba Mwenyezi Mungu (s.w) hawatupi waja wake wema wala hakusudii kuwatesa kwa kuwapa maamrisho mengi na magumu, bali anawapa mazoezi yatakayowawezesha kuwa wacha-Mungu na kubakia katika hadhi yao ya ukhalifa wa Mwenyezi Mungu (s.w) hapa ulimwenguni.

### Kupiga kambi Mina, Mwezi 8 Dhul-Hija

Mwezi 8 Dhul-Hajj, ya Tarwiya, Mahujaji wanapiga kambi Mina, ambapo wanashinda na kulala humo. Kitendo hiki huwazoesha Waislamu kuwa askari wa Mwenyezi Mungu (s.w) ambao daima watakuwa tayari kuacha majumba yao na starehe za kimji na kutoka kupigania dini ya Mwenyezi Mungu (s.w).

Kuzidisha kuleta talbiya humo kambini, kunatukumbusha kuwa mwanajeshi wa Kiislamu tofauti na wanajeshi wengine, anapokuwa vitani hafanyi ufisadi na ufasiqi, bali hubakia katika kumkumbuka Mwenyezi Mungu (s.w) na kuchunga mipaka yake ipasavyo.

### Kusimama Arafa, Mwezi 9 Dhul-Hajj

Haji wote wanalazimika kukusanyika pamoja katika uwanja wa Arafa siku ya mwezi 9 Dhul-Hajj wakiwa wamevalia ihram. Shughuli kubwa zinazofanywa katika uwanja huu, pamoja na kumdhukuru Mwenyezi Mungu kwa wingi, ni kusikiliza khutba inayotolewa na kiongozi wa Hija wakati wa Adhuhuri na kuomba dua na maghfira baada ya swala ya Adhuhuri (ambayo huchanganywa na Asr) mpaka kutua kwa jua.

Zoezi hili la kusimama Arafa linawakumbusha Waislamu mkutano mkuu wa siku ya Kiyama ambapo atayeonekana bora na muheshimiwa mbele ya Mwenyezi Mungu (s.w) ni yule amchaye Allah (s.w) ipasavyo na akasimamisha au kujitahidi kusimamisha ufalme wa Mwenyezi Mungu (s.w) hapa ulimwenguni. Kwa maana nyingine siku hiyo, tofauti kati ya wanaadamu katika misingi ya taifa, lugha, rangi, hali na hadhi, haitakuwa na maana yoyote. Khutuba inayotolewa na Kiongozi wa Hija, ni katika kuwakumbusha Waislamu kukumbuka mkutano huo wa Siku ya Malipo ambamo walimwengu wote wa mwanzo na wa mwisho watahudhurishwa mbele ya Mola wao wakiongozwa na Mitume wao ili wakalipwe kulingana na walivyowajibika kwa Mola wao hapa ulimwenguni.

### Kupiga Kambi Muzdalifa

Kitendo cha kulala Muzdalifa na kuamka asubuhi kuelekea Mina kwenye Mnara mkubwa na mawe saba mkononi, kinafanana sana na zoezi la askari wapiganaji waliojiandaa usiku kuwashambulia maadui asubuhi na mapema. Kwa hiyo Haji anapokuwa Muzdalifa na hasa wakati wa kuokota mawe kwa ajili ya kazi ya kesho yake - hana budi kukumbuka kuwa yeye ni askari wa Mwenyezi Mungu (s.w) anayetakiwa daima awe tayari kupambana na maadui wa dini Yake.

Kitendo cha kuomba dua au Kumuomba Mwenyezi Mungu (s.w) na kumtukuza kwa utukufu wake katika mash-arul-haram, kinamkumbusha kila mpiganaji katika jeshi la Mwenyezi Mungu (s.w) kuwa ushindi katika vita vya kupigania Dini ya Mwenyezi Mungu (s.w) haupatikani kwa kutegemea ubora wa silaha na uhodari wa wapiganaji tu, bali ni lazima pawe na kumtegemea Mwenyezi Mungu (s.w) na kumtii ipasavyo.

### Kutupa Mawe Mina

Ibada ya kutupa mawe Mina, Minara Mitatu ambayo inamuwakilisha Shetani, hufanyika mwezi 10 Dhul-Hajj na siku tatu za tashriq zinazofuatia.

Zoezi hili la kutupa mawe, humkumbusha Muislamu wajibu wake wa kupambana na maadui wote wa Mwenyezi Mungu (s.w) watakaosimama kumzuilia kusimamisha Dini ya Mwenyezi Mungu (s.w) katika maisha ya kila siku. Aidha, zoezi hili ni kumbukumbu ya kitendo alichokifanya Nabii Ibrahim (a.s) alipokuwa akimfukuza Shetani alipokuwa akimfuata na kumlaghai ili amuasi Mola wake katika kutekeleza amri ya kumchinja mwanawe Ismail (a.s).

Waislamu hatuna budi kufahamu kuwa Dini ya Mwenyezi Mungu (s.w) ina maadui wengi sana na wa aina mbali mbali wanaotumia mbinu mbali mbali za kuihujumu na kuifanya isiwemo au iwe chini ya dini zao. Ni jukumu la Waislamu kuwafahamu maadui wa Dini yao, kufahamu mbinu na silaha wanazotumia maadui hao katika kuuhujumu Uislamu na kuwa tayari kupambana nao vikali kwa mali na nafsi.

### Kuchinja Mnyama

Zoezi la kuchinja mnyama siku ya mwezi 10 Dhul-Hajj ni zoezi la utii kwa Mwenyezi Mungu (s.w) kama inavyobainishwa katika aya ifuatayo:

... لُحُومُهَا وَلَا دِمَآؤُهَا وَلَـٰكِن يَنَالُهُ ٱلتَّقْوَىٰ مِنكُمْ ۚ كَذَٰلِكَ
سَخَّرَهَا لَكُمْ لِتُكَبِّرُوا۟ ٱللَّهَ عَلَىٰ مَا هَدَىٰكُمْ ۗ وَبَشِّرِ ٱلْمُحْسِنِينَ ﴿٣٧﴾

*"... Nyama zao (wanyama hao wanaochinjwa) hazimfikii Mwenyezi Mungu (wala damu zao, lakini unamfikia Mwenyezi Mungu utii wenu (Kwake). Namna hivi tumewatiisha kwenu, ili mumtukuze Mwenyezi Mungu kwa sababu ya huku kukuongozeni. Na wape habari njema wafanyao mema". (22:37)*

Wote wawili, Ibrahim (a.s) na mtoto wa Ismail (a.s) aliwatangazia ushindi na kumfanya Ibrahim (a.s) kuwa kiongozi wa wacha-Mungu ulimwenguni kote na mila yake kuifanya mila ya walimwengu wote.

Kutokana na kisa hiki, tunajifunza kuwa Muislamu wa kweli anatakiwa amfanye Mwenyezi Mungu mpenzi wa moyo wake kuliko kipenzi kingine chochote kile. Na katika kufaulu na kustahiki malipo mema pamoja na nusra ya Mwenyezi Mungu (s.w) kurehemu kutokana na magumu mbali mbali kama alivyomnusuru Ismail kutokana na kisu kikali kilichokuwa tayari kukata juu ya koo lake. Mafanikio haya kwa Nabii Ibrahim (a.s) na mwanawe yanadhihirishwa katika aya zifuatazo:

فَلَمَّآ أَسْلَمَا وَتَلَّهُۥ لِلْجَبِينِ ﴿١٠٣﴾ وَنَـٰدَيْنَـٰهُ أَن يَـٰٓإِبْرَٰهِيمُ
قَدْ صَدَّقْتَ ٱلرُّءْيَآ ۚ إِنَّا كَذَٰلِكَ نَجْزِى ٱلْمُحْسِنِينَ ﴿١٠٤﴾ إِنَّ
هَـٰذَا لَهُوَ ٱلْبَلَـٰٓؤُا۟ ٱلْمُبِينُ ﴿١٠٥﴾ وَفَدَيْنَـٰهُ بِذِبْحٍ عَظِيمٍ ﴿١٠٦﴾ وَتَرَكْنَا
عَلَيْهِ فِى ٱلْـَٔاخِرِينَ ﴿١٠٧﴾ سَلَـٰمٌ عَلَىٰٓ إِبْرَٰهِيمَ ﴿١٠٨﴾ كَذَٰلِكَ
نَجْزِى ٱلْمُحْسِنِينَ ﴿١٠٩﴾ إِنَّهُۥ مِنْ عِبَادِنَا ٱلْمُؤْمِنِينَ ﴿١١٠﴾

*"Basi wote wawili walipojisalimisha (kwa Mwenyezi Mungu) na akamlaza kifudi fudi (amchinje), pale pale tulimuita: "Ewe Ibrahim, umesadikisha ndoto!" Kwa yakini hivi ndivyo tunavyowalipa watendao mema. Bila shaka (jambo) hili ni jaribio lililodhahiri. Basi tukamkomboa kwa mnyama wa kuchinjwa mtukufu. Na tukamwachia (sifa nzuri) kwa watu wote waliokuja baadaye. Amani kwa Ibrahim. Hivi ndivyo tuwalipavyo watenda wema. Bila shaka yeye alikuwa miongoni mwa waja wetu walioamini (kweli kweli)" (37:103-111)*

Endapo Muislamu ataitekeleza ibada hii ya kuchinja mnyama, huku kumbukumbu ya kisa hiki cha Nabii Ibrahim cha kumchinja mwanawe amekiweka mbele yake, bila shaka zoezi hili litamuandaa kuwa tayari kujitoa muhanga nafsi yake na nafsi ya kila kipenzi chake kwa ajili ya kusimamisha Dini ya Mwenyezi Mungu hapa ulimwenguni.

## Kupiga kambi Mina mwezi 11 - 13 Dhul-Hijja

Siku za Tashriq ndio kilele cha ibada ya Hijja ambapo askari wa Mwenyezi Mungu (s.w) hupumzika kambini kwao baada ya mazoezi makali ya kijeshi waliyoyaanza tangu mwezi 8, Dhul-Hajj, ambayo endapo watakuwa wameyafanya kwa mazingatio makubwa yanayostahili yatawawezesha kuwa wapiganaji hodari wa Mwenyezi Mungu katika kusimamisha dini yake na ufalme wake hapa ulimwenguni. Pamoja na mapumziko haya, askari hawa wa Mwenyezi Mungu (s.w) hawawi kama askari wa majeshi ya kilimwengu ambao katika sherehe zao hujizamisha katika ufasiqi kama vile ulevi, uzinifu, uporaji wa mali za raia, n.k., bali wao wanaendelea kumkumbuka na kumtukuza Mwenyezi Mungu (s.w) kwa Takbira, Swala, Dua na Stighfari na kila baada ya jua kupindukia hujitokeza kwa mazoezi ya shabaha katika kuilenga kwa mawe ile minara mitatu ambayo imesimamishwa pale kuwakilisha maadui wote wa Dini ya Mwenyezi Mungu (s.w).

## Kuaga Ka'aba

Baada ya siku tatu (siku za Tashriq) za sherehe za kufunga ibada ya Hijja Mahujaji hujiandaa kurejea makwao. Baada ya kuwa tayari kuondoka, huenda kwenye Ka'aba na kufanya Tawaf ya kuaga.

Katika kufanya zoezi hili la Tawaf ya kuaga, Haji akiwa anazingatia mafunzo aliyoyapata katika zoezi zima la ibada ya Hija, ambayo yamelengwa kuwaandaa Waislamu kuwa Makhalifa wa Mwenyezi Mungu (s.w) hapa ulimwenguni kwa ufalme wa Mwenyezi Mungu (s.w) hapa ardhini na kuporomosha falme nyingine zote kwa silaha ya udugu na umoja na kujitoa muhanga kwa mali na nafsi, ataaga kwa kutoa ahadi tena kwa Mwenyezi Mungu (s.w) kuwa kuanzia pale atayaingiza mafunzo aliyoyapata katika matendo na atahakikisha kuwa hafi isipokuwa ametekeleza wajibu wake katika kusimamisha Dini ya Mwenyezi Mungu. Si katika kumaliza ibada maalum kwa kutoa ahadi kwa Mwenyezi Mungu (s.w) kuwa atayaingiza mafunzo aliyoyapata katika ibada hiyo katika matendo kwa kutumia juhudi zake zote kwa ushirikiano wa kidugu na Waislamu wenzake. Kila Muislamu anapomaliza swala ya faradhi, anapokamilisha ibada ya Zaka na ibada ya funga, anatakiwa atoe ahadi hii ya kuaga kwa Mwenyezi Mungu (s.w) kwani hana uhakika kuwa ataweza kufikia ibada nyingine kama hiyo kabla hajarejea kwa Mola wake. Ni katika mtazamo huu Mwenyezi Mungu (s.w) anatutanabahisha:

يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ ٱتَّقُوا۟ ٱللَّهَ حَقَّ تُقَاتِهِۦ وَلَا تَمُوتُنَّ إِلَّا وَأَنتُم مُّسْلِمُونَ

*"Enyi mlioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu kama ipasavyo kumcha; wala msife isipokuwa mmekwisha kuwa Waislamu kamili". (3:102)*

## Yanayopelekea Lengo la Hijja Kutofikiwa

Tumeona namna Ibada ya Hijja inavyowatayarisha na kuwazoesha Waislamu kuwa Makhalifa wa Mwenyezi Mungu (s.w) hapa ulimwenguni. Kwa maana nyingine inatarajiwa kuwa Waislamu wakitekeleza ibada ya Hijja vilivyo kila mwaka, wataweza kuwa Makhalifa katika ulimwengu na kuisimamisha dini ya Mwenyezi Mungu (s.w) kuwa juu ya dini zote japo makafiri na washirikina watachukia. Mwenyezi Mungu (s.w) anaahidi katika aya mbali mbali za Qur-an kuwa Waislamu wakiamua kusimamisha Dini yake hapa ulimwenguni atawawezesha kuisimamisha. Hebu turejee aya chache zifuatazo:

وَعَدَ ٱللَّهُ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ مِنكُمْ وَعَمِلُوا۟ ٱلصَّٰلِحَٰتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِى
ٱلْأَرْضِ كَمَا ٱسْتَخْلَفَ ٱلَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ ٱلَّذِى
ٱرْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّنۢ بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ يَعْبُدُونَنِى لَا يُشْرِكُونَ بِى
شَيْـًٔا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُو۟لَٰٓئِكَ هُمُ ٱلْفَٰسِقُونَ ﴿٥٥﴾

*Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na kufanya vitendo vizuri, kuwa atawafanya makhalifa katika ardhi kama alivyowafanya makhalifa wale waliokuwako kabla yao, na kwa yakini atawasimamishia dini yao aliyowapendelea, na atawabadilishia amani baada ya khofu yao.Wale watakaokufuru baada ya hayo, basi hao ndio wavunjao amri zetu. (24:55).*

يُرِيدُونَ لِيُطْفِـُٔوا۟ نُورَ ٱللَّهِ بِأَفْوَٰهِهِمْ وَٱللَّهُ مُتِمُّ نُورِهِۦ
وَلَوْ كَرِهَ ٱلْكَٰفِرُونَ ﴿٨﴾ هُوَ ٱلَّذِىٓ أَرْسَلَ رَسُولَهُۥ بِٱلْهُدَىٰ
وَدِينِ ٱلْحَقِّ لِيُظْهِرَهُۥ عَلَى ٱلدِّينِ كُلِّهِۦ وَلَوْ كَرِهَ ٱلْمُشْرِكُونَ ﴿٩﴾

*Wanataka kuzima nuru ya Mwenyezi Mungu (Uislamu) kwa vinywa vyao,*

*na Mwenyezi Mungu atakamilisha Nuru yake ijapokuwa makafiri watachukia. Yeye ndiye aliyemtuma Mtume wake kwa uongofu na kwa dini ya Haki ili kuifanya ishinde dini zote, ijapokuwa watachukia Washirikina. (61:8-9)*

Lakini pamoja na ahadi hii na pamoja Waislamu kumininika Makka kwa mamilioni kila mwaka kwa Ibada ya Hija, hatuoni Uislamu kusimama katika jamii ya waislamu ulimwenguni. Miongoni mwa sababu zinazofanya Hija zetu zisitufikishe kwenye lengo lililokusudiwa ni hizi zifuatazo:

### (i) Kuhiji kwa Chumo la Haramu

Wengi wahijio wanahiji kwa fedha waliyoichuma kwa njia za haramu. Ilivyo ni kwamba ibada yoyote itakayofanywa kutokana na chumo haramu haitapokelewa mbele ya Mwenyezi Mungu (s.w). Hili amelidhihirisha Mtume (s.a.w) kwa uwazi kama tunavyojifunza katika Hadithi zifuatazo:

*Ibn Umar(r.a) amesimulia kuwa Mtume (s.a.w) amesema:"Swala haikubaliwi bila ya Tahara wala Sadaqat haikubaliwi kama imetokana na mali iliyochumwa kwa njia za haramu". (Muslim).*

Mtume (s.a.w) amesema:

*"Kama mtu atanunua nguo kwa dirham 10, na ikawa dirham moja katika hizo 10 zimepatikana kwa njia ya haramu haitakubaliwa swala yake yoyote ile pindi atakapokuwa anaswali na nguo hiyo".*

Hadithi hizi zatosha kutuhakikishia kuwa iwapo chumo letu linapatikana kwa njia za haramu, tusahau kabisa kuvuna matunda ya ibada ya Hijja yanayotarajiwa tuyapate.Je, uchumi wetu haukujengwa katika msingi ya riba? Je miongoni mwetu hatupokei rushwa na kuwa tayari kufisidi haki za wengine au kuhujumu uchumi wa Umma? Je, wengi wetu sio waajiriwa katika miradi ya kuzalisha riba kama vile mabenki na mashirika ya bima? Ni vipi sasa tunatarajia kupata matunda ya ibada zetu na ili hali kipato chetu kimetokana na njia hizi haramu? Bila shaka chumo haramu latosha kuwa sababu kubwa inayoifanya ibada ya Hijja inayotekelezwa kila mwaka na mamilioni ya Waislamu isiweze kuwafikisha Waislamu katika kuutawala ulimwengu kama Makhalifa wa Mwenyezi Mungu (s.w) na kuifanya Dini yake kuwa juu ya dini zote pamoja na mbinu na juhudi za Makafiri na Washirikina dhidi ya Uislamu.

Hivyo, ili Waislamu tuweze kupata matunda ya Ibada hii kuu ya Hijja pamoja na ibada nyingine zote, hatuna budi kuusafisha uchumi wa jamii. Lakini tukumbuke kuwa kuusafisha uchumi wa jamii si lele mama, bali inahitajia kuifuma jamii upya kwa kuwaelimisha 'Waislamu kwausahihi juu ya uislamu kama mfumo kamili wa maisha.

**(ii) Kutochunga Miiko ya Hijja**

Hijja kama ibada nyingine ina miiko yake ambayo kama haitachungwa vilivyo, mafunzo yanayokusudiwa kutokana na Hijja hayapatikani. Masharti ya Hijja yametolewa kwa muhtasari na aya ifuatayo:

فَمَن فَرَضَ فِيهِنَّ ٱلْحَجَّ فَلَا رَفَثَ وَلَا فُسُوقَ وَلَا جِدَالَ فِى ٱلْحَجِّ ۗ

*"... Na anayekusudia kufanya Hija katika miezi hiyo, basi asiseme maneno machafu wala asifanye vitendo vichafu, wala asibishane katika hiyo Hija..." (2:197).*

Tunalojifunza katika aya hii ni kwamba, mtu anayekusudia kuhiji ni lazima ajitahidi kuwa mcha-Mungu ambaye hujiepusha kwa moyo mkunjufu na yale yote aliyoyakataza Mwenyezi Mungu (s.w), ambaye hujitahidi kwa jitihada zake zote kufuata inavyostahiki na kwa unyenyekevu maamrisho yote ya Mwenyezi Mungu (s.w), ambaye anajitahidi kwa jitihada zake zote kuwafanyia wema wanaadamu wenzake na ambaye ametubia kwa Mola wake kwa makosa yake na anawaomba msamaha wanaadamu wenzake aliowakosea. Pia tunafahamishwa katika aya hii kuwa, Hajji au Hajjat anatakiwa abakie katika hali hii ya Ucha-Mungu katika safari yote ya Hijja ikiwa ni pamoja na kuchunga kwa ukamilifu miiko ya Ihram.

Wengi wetu wanaohiji hawachungi miiko ya Hijja. Tabia za wengi wanaokwenda kuhiji haina tofauti kabisa na tabia za makafiri na washirikina. Ni mara ngapi tunawaona watu wanaojiita waislamu na wanaokusudia kuhiji lakini hawasimamishi swala, hawatoi Zakat na hawawahurumii Waislamu wenzao hata wale waliokaribu nao na walio majirani zao?Je, hatujaona Waislamu wanaojiandaa kuhiji na huku wanadhulumu haki za watu, wanashirikiana na makafiri na Washirikina katika kuupiga vita Uislamu, wanagombanisha na kuwafitinisha watu na hata waislamu wenzao na wanashiriki katika maovu mbali mbali ikiwa ni pamoja na uchumi haramu. Kama tunashuhudia kuwa huu ndio mwenendo wa wengi wanaohiji na kurudi na majina ya Al-Hajj, vipi tunaitarajia Hijja iwafanye watu hawa Makhalifa wa Mwenyezi Mungu (s.w) hapa ulimwenguni?

Ili Hija zetu zituzalie matunda yanayotarajiwa, hatuna budi kuchunga miiko ya Hijja kwa kujipamba na mwenendo wa Kiislamu tangu katika maandalizi ya Ibada ya Hijja mpaka mwisho wake.

**(iii) Kutotekeleza Nguzo za Hija Vilivyo**

Ibada ya Hija kama ibada nyingine imejengwa na nguzo zinazoipa sura yake halisi. Endapo nguzo moja katika nguzo za Hijja haitatekelezwa vilivyo, ima kwa kukusudia au kwa kutojua, ibada ya Hijja haitasihi. Kutosihi au kutokubaliwa Ibada ya Hijja mbele ya Mwenyezi Mungu (s.w) ni sababu tosha ya kufanya ibada ya Hija isiweze kumtayarisha mja kuwa Khalifa wa Mwenyezi Mungu (s.w) hapa ulimwenguni.

Ukweli ni kwamba, wengi wanaokwenda kuhiji kila mwaka hawajui masharti na nguzo za ibada ya Hijja kwa kiasi kwamba wanaitekeleza ibada hiyo visivyo na wanavunja miiko ya Ihram bila ya kujitambua. Wengi wa wanaohiji hutosheka tu na kupata tikiti ya usafiri na gharama nyingine za safari. Kujielimisha juu ya namna ya utekelezaji wa Ibada ya Hijja haimo kabisa katika ratiba ya matayarisho ya safari ya Hija. Je, kama wengi wetu tunaitekeleza ibada ya Hijja ovyo ovyo kwa kutokuwa na ujuzi unaostahiki juu ya ibada hiyo, tunatarajiaje kupata matunda ya Hijja sawa na wale walioitekeleza vilivyo? Si kwa ibadah ya Hijja tu, bali ibada yoyote itakayofanywa kwa ujinga,hatuna budi kufahamu vema kuwa haitampatiamfanyaji matunda yaliyokusudiwa. Hivyo ili Waislamu wapate matunda ya Hijja zao, hawana budi kujitahidi kujielimisha juu ya ibada ya Hijja kama wanavyojitahidi kutafuta gharama za safari ya Hijja.

**(iv) Kutojulikana kwa Lengo la Hijja**

Kwa muhtasari tumeona kuwa lengo la Hija ni kuwatayarisha na kuwazoesha Waislamu kuwa Makhalifa wa Allah (s.w) hapa ulimwenguni kwa kusimamisha na kuipigania Dini ya mwenyezi Mungu (s.w) bega kwa bega mpaka iwe juu ya dini zote japo watachukia makafiri na washirikina.

Je, ni wangapi wanaohiji wakiwa na lengo hili akilini mwao? Ukweli ni kwamba wengi wanaohiji hawana habari hata juu ya lengo la ujumla la maisha yao hapa ulimwenguni.

*******************************************************

## Zoezi la Tano

1. (a) Eleza maana ya Hijja
   (i) Kilugha (ii) Kisheria

   (b) Ni zipi tafauti za msingi baina ya Hija na 'Umra?

2. (a) Taja sifa ambazo Muislamu akiwanazo kwa ukamilifu wake, humwajibikia kufanya ibada ya Hijja
   (b) Ni mwenendo upi anaotakiwa kushikamana nao Muislamu aliyekusudia kuhiji?

3. (a) Kwanini ibada ya Hijja ni muhimu kwa kila Muislamu mwenye sifa na uwezo?
   (b) Ni miezi ipi ambayo Muislamu anaweza kunuia kufanya ibada ya Hijja?

4. (a) Bainisha vituo vya kunuia Hijja vinavyotumiwa na mahujaji toka pande zote za dunia.
   (b) Taja tarehe rasmi za kuanza na kumaliza Ibada ya Hijja.

5. (a) "Ihram" ni nini?
   (b) Ni yepi masharti ya Ihramu?

6. (a) Toa maelezo kwa muhtasari juu ya:
   (i ) Ifraad (ii) Qiran (iii) Tamattu
   (b) Eleza kwa kifupi kafara impasayo Hajji anapovunja moja ya masharti ya Hija kwa dharura au makusudi.

7. (a) Toa ufafanuzi mfupi juu ya aina za Tawaf zifuatazo:
   (i) Tawaful-Quduum (ii) Tawafil-Ifadha (iii) Tawaful-Widaa.
   (b) Lengo la safari ya ibada ya Hijja si kwenda kutambika au kutalii, bali humuandaa Muislamu aweze kuhuisha Uislamu na kuulinda kwa mali na nafsi yake. Thibitisha ukweli wa hili kwa kurejea Ibada ya Hijja tokea maandalizi yake, vitendo vya Hijja pamoja na masharti yake.

8. (a) Bainisha mafunzo ya kuhuisha na kuulinda Uislamu yanayopatikana katika vitendo vifuatavyo vya Hijja :
   (i) Kusitisha kazi, kuacha familia, na kufunga safari kwenda Makkah.
   (ii) Kumpiga shetani kwa mawe katika minara mitatu (rami)
   (iii) Kupiga kambi Minna.
   (iv) Kusa'i
   (v) Kuchinja mnyama
   (b) Hivi sasa jamii ya Kiislamu ina hazina kubwa ya Waislamu waliopata fursa ya kuhiji(Ma-Alhaji); lakini hainufaiki na matunda yanayotokana nalengo zima la ibada ya Hijja. Kwanini?

*********************